

Mafundisho juu ya Biblia

AGANO JIPYA

WAROMA – WAKOLOSAYI

**Maelezo ya
Maandiko Matakatifu
kwa Waamini**

Mwandishi : William MacDonald



Mtengenezaji wa Maneno ya Mbele: Arthur Farstad

Everyday Publications Inc.
Port Colborne, ON L3K 6A6
Canada

Traduit de l'anglais
par G. I. Harlow, 2015
avec collaboration de M. et J. Wolcott

Copyright © 2016
par Everyday Publications, Inc.
310 Killaly Street West
Port Colborne, ON L3K 6A6
Canada

ISBN 978-0-88873-159-3

Imprimé aux Etats-Unis d'Amérique

Fahirisi

Majina ya Vitabu vya Agano Jipyा	4
Utangulizi wa Mwandishi	5
Namna gani kitabu hiki kiliandikwa	5
MLANGO KWA AGANO JIPYA	6
Waroma	9
Wapagano Wasiosikia Habari Njema	18
Mafundisho juu ya Zambi	27
Mafundisho juu ya Enzi ya Mungu na Madaraka ya Watu	58
1 Wakorinto	95
2 Wakorinto	169
Wagalatia	225
Mafundisho juu ya Sheria	254
Waefeso	259
Mafundisho juu ya Mchaguo wa Mungo	264
Wafilipi	317
Wakolosayi	347
Mafundisho juu ya Upatanisho	358
Mafundisho juu ya Nyumba ya Wakristo	377

Majina ya Vitabu vya Biblia

VITABU VYA AGANO JIPYA		Jina	Ufupisho
Jina	Ufupisho	Hesabu	Hes.
Matayo	Mt.	Kumbukumbu la Torati	Tor.
Marko	Mk.	Yosua	Yos.
Luka	Lk.	Waamuzi	Amu.
Yoane	Yn.	Ruta	Rut.
Matendo	Mdo.	1 Samweli	1 Sam.
Waroma	Rom.	2 Samweli	2 Sam.
1 Wakorinto	1 Kor.	1 Wafalme	1 Fal.
2 Wakorinto	2 Kor.	2 Wafalme	2 Fal.
Wagalatia	Gal.	1 Mambo ya Siku	1 Sik.
Waefeso	Efe.	2 Mambo ya Siku	2 Sik.
Wafilipi	Flp.	Ezra	Ezr.
Wakolosayi	Kol.	Nehemia	Neh.
1 Watesalonika	1 Tes.	Esiteri	Est.
2 Watesalonika	2 Tes.	Yobu	Yob.
1 Timoteo	1 Tim.	Zaburi	Zab.
2 Timoteo	2 Tim.	Mezali	Mez.
Tito	Tit.	Mhubiri	Mhu.
Filemono	Flm.	Wimbo wa Solomon	Wim.
Waembrania	Ebr.	Isaya	Isa.
Yakobo	Yak.	Yeremia	Yer.
1 Petro	1 Pet.	Maombolezo	Omb.
2 Petro	2 Pet.	Ezekieli	Eze.
1 Yoane	1 Yn.	Danieli	Dan.
2 Yoane	2 Yn.	Hosea	Hos.
3 Yoane	3 Yn.	Yoeli	Yoe.
Yuda	Yud.	Amosi	Amo.
Ufunuo	Ufu.	Obadia	Oba.
		Yona	Yon.
		Mika	Mik.
		Nahumu	Nah.
		Habakuki	Hab.
		Zefania	Zef.
Mwanzo	Mwa.	Hagai	Hag.
Kutoka	Kut.	Zekaria	Zek.
Walawi	Law.	Malaki	Mal.

VITABU VYA AGANO LA KALE

Jina	Ufupisho
Mwanzo	Mwa.
Kutoka	Kut.
Walawi	Law.

UTANGULIZI WA MWANDISHI

Kusudi la Kitabu hiki cha *Mafundisho juu ya Biblia kwa Waamini* ni kusaidia Mkristo kujifunza Biblia na kuendelea kujuana na Maandiko Matakatifu. Lakini hakuna kitabu cha Mafundisho kinachoweza kukomboa faida ya Biblia yenye. Kinaweza kueleza tu maana yake na kusaidia msomaji kufahamu maneno anayosoma yehe mwenyewe ndani ya Maandiko Matakatifu. Ninaamini kabisa ya kwamba Mkristo ye yote anayedumu kusoma na kujifunza Neno la Mungu anaweza kugeuka “mfanya kazi asiemeona haya, akifasiri vema neno la kweli” (2 Tim. 2:15).

Lakini kujua tu maneno ya Biblia hakutoshi. Ni lazima kwa msomaji kutii mafundisho yake ndani ya maisha yake ya kila siku. Kwa sababu hii mwandishi wa kitabu hiki cha Mafundisho anajaribu sana kuonyesha namna gani msomaji anaweza kuwa *mtendaji* wa Neno la Mungu, si *msikiaji* tu.

Msomaji akisoma kitabu hiki cha Mafundisho peke yake, pasipo Biblia, kitabu hiki hakitamsaidia, lakini kitageuka mtego kwake. Kitakuwa na faida tu kama kikiongeza hamu yake kutafuta Maandiko yehe mwenyewe na kutii maagizo ya Bwana.

Ninaomba Roho Mtakatifu, aliyeongoza kuandika kwa Biblia, afungue na kutia nuru nia ya msomaji wakati anapojoitoa kwa neno hili zuri zaidi – kujua Mungu kwa njia ya Neno lake.

Namna gani kitabu hiki kiliandikwa

Vitabu vingi vimeandikwa kueleza maana ya Biblia kwa njia mbalimbali, na kwa makusudi mbalimbali. Vingine vinaieleza kila neno moja moja, na vingine vinaieleza sura kwa sura.

Maelezo ya vitabu vingine hayapatani na maana ya kweli ya Neno la Mungu.

Ndani ya kitabu hiki cha “**MAFUNDISHO YA BIBLIA**” kusudi la mwandishi William MacDonald ni

1. kueleza maana ya Biblia wazivazi, hata maneno yale yaliyo ngumu kufahamu.
2. kuongoza msomaji kujuana na kupendana na Bwana Yesu Kristo sana, na kugeuka *mfuata na mtumishi* wake mwaminifu.

Unaweza kutumika na kitabu hiki kwa njia mbalimbali.

1. Unaweza *kusoma nusu nusu* ya mafundisho ndani ya sura mbalimbali na kuonja utamu wake bila kufuata utaratibu fulani.
2. Labda wakati unaposoma Neno la Mungu, unakuta *mashairi magumu* ambayo yanakushinda kabisa kufahamu. Maelezo ndani ya kitabu hiki yatakusaidia sana.
3. *Elimu ya dini* – labda unataka kujua mafundisho ya Biblia juu ya neno fulani, kama sabato, ubatizo, haki ya Mungu. Ndani ya Tafsiri kwa ukurasa 3 utsaona mafundisho juu ya maneno 17 ya namna hii.
4. *Kitabu fulani katika Biblia* – Labda watu wa kanisa lako, au katika Ecole du dimanche wamechagua kujifunza barua moja ya Agano Jipyamamoja. Utapata faida kubwa kwa roho yako na kuweza kusaidia watu wengine vilevile kama ukijifunza kila juma mbele ya kusanyiko lenu mafundisho yanayopatikana ndani ya kitabu hiki.
5. *Kitabu kizima* – Kwa mwisho ingepasa kila Mkristo kusoma Biblia nzima. Utakutana na mashairi magumu mara kwa mara, lakini kitabu hiki cha Mafundisho kitakusaidia sana kuyafahamu.

MLANGO KWA AGANO JIPYA

“Maandiko haya ya Agano Jipyä yana faida kubwa kupita ufhamu wetu, kwa maneno ya historia, na roho. Kristo wa Unabii wa Agano la Kale anageuka Kristo wa Historia ndani ya vitabu vya Habari Njema; Kristo wa Uzoevu wa Maisha ndani ya Barua za Agano Jipyä; na Kristo ndani ya Utukufu ndani ya Ufunuo.”

I. Jina la “Agano Jipyä”

Mbele ya kujiingiza kabisa ndani ya kujifunza habari za kitabu hiki, ni vizuri tuwaze kwanza juu ya maneno mengine ya Kitabu hiki Kitakatifu tunachoita “Agano Jipyä.”

Kweli kitabu hiki ni mapatano, ndiyo *agano* la Mungu na watu wake.

Kinaitwa Agano *Jipyä* kuonyesha kwamba ni namna nyininge na Agano la Kale, ndilo Agano la zamani.

Mungu aliongoza kuandika Maagano mbili yote, na kwa sababu hii yana faida kwa Wakristo wote. Lakini hatushangai kuona kwamba mwamini wa Kristo anageuka kupita kwa sehemu ile ya Biblia inayopasha zaidi juu ya Bwana na kamisa lake, na inayofundisha namna gani anataka wanafunzi wake kuishi.

Augustine alionyesha vizuri ya kwamba Agano Jipyä lilifichwa ndani ya Agano la Zamani; Agano la Zamani linafunuliwa ndani ya Agano Jipyä.

II. Kanuni ya Agano Jipyä

Neno hili *kanuni* ni tafsiri ya *kanon* kwa Kiyunani. Ni kama kipimo cha maneno. Kanuni ya Agano Jipyä ndiyo mku-sanyo wa vitabu vilivyoandikwa kwa maongezi ya Mungu. Tunaweza kujua kama inafaa kwa vitabu *hivi tu* kuwa ndani ya kanuni, au kwamba inapassa vitabu *hivi* vyote 27 kuwa sehemu yake? Kulikuwa na maneno mengine yaliyo-

andikwa na Wakristo kwa wakati ule (hata maandiko ya mafundisho ya uwongo). Namna gani tunaweza kujua kwamba maandiko yale 27 yanafaa kuwa ndani ya kanuni?

Tunasikia mara nyangi ya kwamba kuna baraza ya kanisa karibu na 400 A.D. waliokusanya majina ya vitabu ndani ya kanuni. Lakini vitabu hivi vilikuwa *sehemu ya kanuni* mara moja nyuma ya kuandikwa. Wanafunzi wenye kuogopa Mungu na wenye ufhamu walitambua maandiko matakatifu mara moja, kama Petro alivyotambua maandiko ya Paulo (2 Pet. 3:15, 16). Lakini hawakupatana juu ya vitabu vingine (Yuda, 2 na 3 Yoane, kwa mfano) kwa wakati.

Kwa kawaida, kama kitabu kiliandikwa na mtume, kama Matayo, Petro, Yoane, au Paulo, au mmoja wa wale walitumika pamoja na mitume, hakuna shaka ya kwamba kilikuwa sehemu ya kanuni.

Baraza walitambua kanuni yetu waliyakinisha maneno yaliyokwisha *kukubaliwa* na watu kwa miaka mingi sana. Baraza hawakukusanya orodha ya *vitabu vilivyoandikwa na maongozi ya Mungu*, lakini waliandika orodha ya *majina ya vitabu vilivyoandikwa kwa maongozi ya Mungu*.

III. Waandishi

Mwandishi wa Agano Jipyä ni Mungu Roho Mtakatifu. Ni ye ye aliyeongoza

Matayo, Marko, Luka, Yoane, Paulo, Yakobo, Petro, na mwandishi wa Waebrania tusiyejua jina lake. Lakini liliandikwa na watu hawa vilevile. Haifai kusema kwamba kwa sehemu liliandikwa na watu, na kwa sehemu na Mungu. Njia nzuri zaidi kueleza neno hili ni kusema ni maandiko ya Mungu na watu pamoja kwa saa moja. Roho Mtakatifu alizuiza waandishi wa binadamu kuandika maneno yasiyo kweli. Hivi maandiko yao ya kwanza yalikuwa bila makosa wala upungufu.

Kwa kutusaidia kufahamu neno hili, tunaweza kusawanisha Neno (Biblia ilioandikwa na Mungu pamoja na watu), na Neno Hai – ndiye Bwana wetu Yesu Kristo. Yeye si mtu kwa sehemu, na Mungu kwa sehemu. Yeye ni Mungu mkamilifu, pamoja na mtu mkamilifu. Kwa sababu ya uungu wake haikuwezekana kwaye kuanguka au kufanya zambi hata kidogo.

IV. Tarehe

Karibu miaka elfu moja ilihitajiwa kuandika Agano la Kale (karibu 1400–400 av. J.C.). Agano Jipyä liliandikwa ndani ya muda wa miaka 50 tu (50–100 A.D.)

Namna vitabu vinavyofuatana katika Agano Jipyä ni vizuri sana kwa kanisa kwa kila wakati. Vinaanza na habari za maisha ya Kristo, vinaendelea na habari za kanisa, na mafundisho kwa kanisa, na mwishoni vinafunua habari za kuja za kanisa, na za dunia. Lakini vitabu hivi havikuandikwa kwa utaratibu huu. Vili-

andikwa kwa wakati vilipohitajiwa. Tunafikiri vitabu nya kwanza viliandikwa kwa makanisa yaliyosimamishwa kwanza, ndizo Barua ya Yakobo, kwa Wagalatia, na kwa Watesalonika, na viliandikwa karibu na mwaks 96 A.D.

Vitabu nya Habari Njema vilifuata, kwanza Matayo, au labda Marko, nyuma yake Luka, kisha Yoane. Kitabu cha mwisho ni Ufunuo, karibu na mwisho wa miaka mia moja ya kwanza A.D.

V. Muhtasari

Vitabu nya Agano Jipyä vinaweza kujumlishwa hivi:

Vitabu nya historia

Vitabu vine nya Habari Njema

Matendo

Vitabu nya Barua

Barua za Paulo

Barua nyingine

Kitabu cha mwisho

Ufunuo

Mkristo anayefahamu mafundisho ya vitabu hivi vizuri “ametengenezwa kabisa kwa kila tendo jema” (2 Tim. 3:17).

Tunaomba kitabu hiki kiweze ku-saidia waamini wengi kuwa watumishi wa faida kubwa kwa Bwana.

VI. Lugha

Agano Jipyä liliandikwa kwa namna ya Kiyunani ambayo Wayunani walitumika nayo kila siku. Kiliitwa *koine* vilevile. Kwa njia ya majeshi ya Alesandro, mfalme mkubwa, watu wa inchi nyingi nyingine walisema lugha hii.

BARUA YA PAULO MTUME KWA WAROMA

Utangulizi

Msingi wa Dini ya Wakristo

I. Nafasi ya pekee katika Kanuni

Waroma ni ndefu kupita zote za barua za Paulo. Kitabu cha Matendo kiliwisha na habari za Paulo akifika kwa Roma, hivi ni akili njema kwa sehemu ya Barua za Agano Jipyka kuanza na barua hii ya mtume Paulo kwa kanisa la Roma. Aliiandika mbele ya kufikia mji ule ye ye mwenyewe. Kitabu hiki kina mafundisho makubwa na mengi ya dini (théologie) kupita vitabu vyote vingine vya Agano Jipyka.

Katika miaka inayopita kitabu hiki kiligusa roho za watu wa kujulikana kupita vitabu vyote vingine vya Biblia. Augustin aliokolewa wakati aliposoma Rom. 13:13-14 (A.D. 380). Matengenezo ya Kanisa la kiingereza yalianza wakati Luther (mwalimu mwengine wa kujulikana) alipofahamu maana ya haki ya Mungu, na ya kwamba “mwenye haki ataishi kwa imani” (1517).

John Wesley alifahamu kwamba nyuma ya kupokea wokovu haitawezekana kwaye kupotea kamwe wakati aliposikia utangulizi wa mafundisho ya Luther juu ya neno hili (1738). John Calvin aliandika ya kwamba “Mtu aki-fahamu barua hii anapata njia kufahamu Biblia nzima.”

II. Mwandishi

Hata walimu wa uwongo na wajuzi wenyewe roho ya kukana wanakubali kwamba mwandishi wa barua kwa

Waroma alikuwa mtume kwa Mataifa, ndiye Paulo. Marcion, ndiye mwalimu wa uwongo, alikuwa mtu wa kwanza aliyetaja jina la Paulo kama mwandishi wa kitabu hiki. Wakristo wengine wa kweli wa zamani (ndio Clement wa Roma, Ignatius, Justin Martyr, Polycarp, Hippolytus, na Irenaeus) walitaja sehemu za barua hii.

Namna barua hii ilivyoandikwa inatuaminisha vilevile ya kwamba iliandikwa na Paulo. Mashairi kama 1:1; 15:15-20 na mengine yanasema wazi kwamba iliandikwa na Paulo. Neno ambalo linatuaminisha zaidi kwamba Paulo alikuwa mwandishi wake ni ya kwamba alitaja tena na tena habari toka Matendo, kama makusanyo ya mali ku-saidia waamini wenyewe hitaji, habari za Gayo, Erasto, na shauri la mwandishi kufikia Roma. Tertio alikuwa karani yake (16:22).

III. Tarehe

Barua kwa Waroma iliandikwa nyuma ya 1 na 2 Wakorinto kwani sadaka kwa watakatifu iliyotajwa ndani ya barua zile ilikuwa tayari sasa kupelekwa kwa Yerusalem kusaida watakatifu masikini. Mwandishi alitaja Kenkurea, bandari ya Korinto. Neno hili, pamoa na habari nyingine vilevile zinafikirisha wenyewe elimu kwamba Paulo alikuwa kwa Korinto saa ya kuandika barua kwa Waroma. Alikuwa kwa mji ule kwa

miezi mitatu tu (kwa mwisho wa safari yake ya tatu ya kuhubiri) mbele ya kufukuzwa kwa sababu ya mashauri ya adui kumzuru, hivi ni kama aliandika barua hii kwa muda ule mfupi, karibu 56 A.D.

IV. Msingi na Jambo Kubwa

Habari Njema ilifikia Roma namna gani? Hatujui kabisa, lakini kulikuwa na Wayuda toka Roma kwa Yerusalem siku ya Pentekote (ona Mdo. 2:10) nao walirudi na Habari Njema, karibu na 30 A.D.

Paulo hakuwa kwa Roma bado yeye mwenyewe wakati alipoandika barua hii toka Korinto nyuma ya muda wa miaka karibu 26, lakini alijua wengine wa Wakristo wa Roma, kama tunavyoona ndani ya sura 16. Wakristo wa wakati ule walikuwa watu wa safari, labda kwa sababu ya mateso waliyopata, au kwa sababu ya kutangaza Habari Njema, au kwa sababu ya kazi yao ya kila siku. Wakristo hawa katika Roma walikuwa Wayuda na Mataifa mbele.

Mwishoni Paulo alifikia Roma yeye mwenyewe, lakini si kwa njia aliokusudi. Alifika kama mfungwa kwa sababu aliamini Kristo Yesu.

Barua hii kwa Waroma ni andiko linalokubaliwa na wenye elimu kuwa bora sana. Inaelezea wasioamini kwamba wao ni wenye zambi, na njia Mungu aliyatayarisha kwa wokovu wao. Waamini wa sasa wanajifunza umoja wao na Kristo na ya kwamba wanaweza kushinda kwa njia ya uwezo wa Roho Mtakatifu. Waamini wa kukomea wanafurahi sana juu ya kweli nyingi mbalimbali zinazopatikana ndani ya barua hii, juu ya mafundisho ya dini ya Wakristo, unabii, na mwenendo.

Njia nzuri sana kufahamu barua hii kwa Waroma ni kama maongezi ya Paulo na mtu mwingine (hatujui jina lake) anayeshindana na mafundisho

yake. Wakati Paulo anapoeleza Haberi Njema, ni kama mtu huyu anabishana naye tena na tena. Mtume anajibu mabishano yake yote moja moja. Mwishoni Paulo amemaliza kujibu maulizo na mabishano yote ya watu juu ya Habari Njema ya neema ya Mungu. Maulizo ya mwenye kubishana naye si wazi kila mara, lakini ni yote juu ya Habari Njema ya wokovu kwa njia ya kuamini Kristo, bila kazi za sheria.

Tutawaza juu ya Waroma kwa njia ya maulizo kumi na moja:

- 1) Neno kubwa la barua hii ni nini? (1:9, 15, 16)
- 2) Habari Njema ni nini? (1:1-17)
- 3) Watu wanahitaji Habari Njema kwa sababu gani? (1:18 – 3:20)
- 4) Namna gani wenye zambi wanaweza kuhesabiwa haki na Mungu mtakatifu kwa njia ya Habari Njema? (3:21 – 31)
- 5) Habari Njema inapatana na mandiko ya Agano la Kale? (4:1-25)
- 6) Faida ya kuhesabiwa haki ni nini kwa maisha ya mwamini? (5:1-21)
- 7) Mafundisho ya wokovu kwa njia ya neema yanakubali, au hata kutia mtu hamu kutenda zambi? (6:1-23)
- 8) Uhusiano wa Mkristo na sheria ni nini? (7:1-25)
- 9) Nini inawezesha Mkristo kuwa na mwenendo mtakatifu? (8:1-39)
- 10) Mungu amevunja ahadi zake kwa watu wake wa dunia, ndio Wayuda, kwa njia ya kuahidi wokovu kwa Wayuda na Mataifa vilevile? (9:1 – 11:36)
- 11) Namna gani ingepasa wale walohesabiwa haki kwa njia ya imani kutenda ndani ya maisha yao ya kila siku? (12:1 – 16:27).

Kuwaza juu ya maulizo haya kumi na moja na majibu yao kutatusaidia kujuana na barua hii kubwa. Bila shaka jibu la ulizo

la kwanza, “Neno kubwa la barua hii ni nini?” ni “Habari Njema.” Paulo alianza mara moja kuandika juu yake. Aliitaja mara ine ndani ya mashairi kumi na sita ya kwanza (mash. 1, 9, 15, 16).

Habari hizi zinatufikisha kwa ulizo la pili, “Habari Njema ni nini?” Ndani ya mashairi 1-17 mtume alitupasha maneno makubwa sita juu ya Habari Njema: (1)

Inatoka kwa Mungu (sh. 1); (2) Iliahi-diwa ndani ya unabii wa maandiko ya Agano la Kale (sh. 2); (3) Ni habari nzuri juu ya Mwana wa Mungu, Bwana Yesu Kristo (sh. 3); (4) Ni uwezo wa Mungu kuleta wokovu (sh. 16); (5) Ni kwa watu wote, Mataifa na Wayuda vilevile (sh. 16); (6) Ni kwa njia ya imani peke yake (sh. 17). Tuangalie mashairi haya karibu kupita sasa.

HABARI YALIYOMO

- | | |
|--------------------------------------------------|----------------|
| 1. MAFUNDISHO: HABARI NJEMA YA MUNGU | (SURA 1 – 8) |
| A. Mlango kwa Habari Njema | (1:1-15) |
| B. Habari Njema ni nini? | (1:16, 17) |
| C. Watu wote wanahitaji Habari Njema | (1:18 – 3:20) |
| D. Msingi na maelezo ya Habari Njema | (3:21-31) |
| E. Mapatano ya Habari Njema na Agano la Kale | (Sura 4) |
| F. Faida ya Habari Njema | (5:1-11) |
| G. Kazi ya Kristo inashinda zambi ya Adamu | (5:12-21) |
| H. Maisha matakatifu kwa sababu ya Habari Njema | (Sura 6) |
| I. Nafasi ya Sheria ndani ya mwenendo wa mwamini | (Sura 7) |
| J. Roho Mtakatifu ni Uwezo kwa maisha matakatifu | (Sura 8) |
| 2. HABARI NJEMA NA ISRAELI | (SURA 9 – 11) |
| A. Israeli kwa wakati wa zamani | (Sura 9) |
| B. Israeli kwa wakati wa sasa | (Sura 10) |
| C. Israeli kwa wakati wa kuja | (Sura 11) |
| 3. KAZI YA HABARI NJEMANDANI YA MAISHA YA WATU | (SURA 12 – 16) |
| A. Kujitoa mzima kwa Mungu | (12:1, 2) |
| B. Utumishi kwa njia ya zawadi za Roho | (12:3-8) |
| C. Katikati ya watu | (12:9-21) |
| D. Na serikali | (13:1-7) |
| E. Kwa wakati wa kuja | (13:8-14) |
| F. Pamoja na waamini wengine | (14:1 – 15:13) |
| G. Mashauri ya Paulo | (15:14-33) |
| H. Sifa ya Paulo kwa kazi ya watu wengine | (Sura 16) |

Maelezo

1. MAFUNDISHO:

HABARI NJEMA YA MUNGU (Sura 1 – 8)

A. Mlango kwa Habari Njema (1:1-15)

1:1 Paulo alijiita mtumwa wa Yesu Kristo, (aliyenunuliwa), aliyeitwa kuwa **mtume** (katika njia ya kwenda Damasiki), na **aliyewekwa mbali** kuhubiri **Habari Njema** kwa Mataifa (ona Mdo. 9:15; 13:2). Sisi vilevile tumenunuliwa na damu ya damani ya Kristo, tumeitwa kushuhudia uwezo wake kuokoa, na kurtangaza Habari Njema pahali po pote tunapokwenda.

1:2 Paulo hakutaka wasomaji wake Wayuda kufikiri Habari Njema ni neno jipya kabisa na namna nyininge kabisa na dini yao, hivi alipasha kwamba **manabii waliiahidi** waziwazi ndani ya maandiko ya Agano la Kale (Tor. 18:15; Isa. 7:14; Hab. 2:4) na kwa njia ya mifano (kama safina ya Noa, nyoka ya shaba, na utarabitu wa zabihu).

1:3 Habari Njema ni habari za **Mwana wa Mungu, Yesu Kristo Bwana wetu**, aliye mzao wa Daudi kwa **namna ya mwili** (maana kwa umtu wake). Maneno haya **kwa namna ya mwili** yanatufahamisha kwamba hakuwa mtu tu, kama tunavyoona ndani ya shairi 4.

1:4 Bwana Yesu alionyeshwa kuwa **Mwana wa Mungu kwa uwezo**. Roho Mtakatifu, aliyeitwa hapa **Roho ya utakatifu**, alionyesha Yesu kwa wakati wa ubatizo wake na kwa njia ya maajabu aliyoitenda. Maajabu ya uwezo ambayo Mwokozi alitenda kwa uwezo wa Roho Mtakatifu yalimshuhudia kuwa Mwana wa Mungu. Wakati tunaposoma kwamba **alionyeshwa kuwa Mwana wa Mungu kwa uwezo ... kwa ufufuko katika wafu**, tunakumbuka ufufuko wake mwenyewe, lakini tunasoma “ufufuko wa

wafu,” hivi labda mtume alifikiri vilevile juu ya wakati Kristo alipofufua binti ya Yairo, mwana wa mjane wa Naina, na Lazaro. Lakini bila shaka maneno haya ni zaidi juu ya ufufuko wa Bwana mwenyewe.

Wakati tunaposema kwamba Yesu ni **Mwana wa Mungu**, maana yake ni ya kama yeye ni Mwana wa namna nyininge. Mungu ana wana wengi. Waamini wote ni wana wake (Gal. 4:5-7). Hata malaika waliiitia wana (Yobu 1:6; 2:1). Lakini Yesu ni Mwana wa Mungu *bila kifani*. Wakati Bwana Yesu aliposema juu ya Mungu kama Baba yake, Wayuda walifahamu kwamba alisema yeye ni sawasawa na Mungu (Yn. 5:18).

1:5 Paulo **alipokea neema na utume katika** Yesu Kristo Bwana wetu (ndicho kibali asichostahili kupokea ambacho kili-mwokoa). Wakati Paulo alipoandika **tulipokea neema na utume**, bila shaka alijifikiri mwenyewe tu. Neno ambalo linatufikirisha hivi ni namna alivyotaja **utume** wake kwa utii wa imani katikati ya **mataifa**. Hakutaja mitume wengine. Paulo aliagizwa kuita watu wa mataifa yote kwa utii kwa imani, maana yake kutii Habari Njema kwa njia ya kutubu na kuamini Bwana Yesu Kristo (Mdo. 20:21). Kusudi la tangazo hili duniani pote lilikuwa kwa sababu ya jina lake, kumpendeza na kumtukuza.

1:6 Paulo aliheshimu wale waliopokea Habari Njema na jina zuri sana, ndilo **waitwa wa Yesu Kristo**. Neno hili linaonyesha kwamba alikuwa Mungu aliyeanza kuwavuta kwake kwa wokovu.

1:7 Barua hii iliandikwa kwa waamini **wote katika Roma**, si kwa kanisa moja tu (kama barua nyininge). Sura ya mwisho ya barua hii inataja majina ya waamini toka makanisa kupita moja, na salamu hii ni kwa waamini hawa wote.

Wapenzi wa Mungu walioitwa

kuwa watakatifu. Haya ni majina mawili matamu sana ya wote waliokombolewa kweli na damu ya damani ya Kristo. Wanapendwa na Mungu kupita watu wengine, na kuitwa vilevile kuwekwa mbali kwa Mungu toka maneno ya dunia, ndiyo maana ya neno hili **watakatifu**.

Ni desturi ya Paulo kusalimu watu na **neema na salama**. **Neema** (*charis*) ni Kiyunani, na **salama** (*shalom*) ni salamu ya Wayuda. Salama hii ina maana sana hapa kwa sababu kwa hotuba ya Paulo inaonyesha kwamba waamini Wayuda na Mataifa ni moja sasa ndani ya Kristo.

Neema inayotajwa hapa si neema inayookoa watu (wasomaji wa barua hii ya Paulo walikuwa wameokolewa mbele), lakini **neema** ambayo inaleta Wakristo uwezo kwa maisha na utumishi wao. **Salama** hii si zaidi salama na Mungu (wasomaji walikuwa na salama ile kwa sababu walikuwa wamehesabiwa haki kwa njia ya imani), lakini **salama** ya Mungu inayoweza kutawala ndani ya roho zao hata wakati walipokaa katikati ya makelele ya watu. **Neema na salama** zimetoka **kwa Mungu Baba yetu na Bwana Yesu Kristo**. Habari hizi zinaonyesha wazi kwamba Mwana na Baba ni sawasawa. Kama Yesu akiwa mtu tu, ingekuwa upumbavu kusema juu yake akitoa **neema na salama** pamoja na Baba.

1:8 Kama ikiwezekana, mtume alianza barua zake na sifa kwa mambo mazuri yo yote ndani ya maisha ya wasomaji wake. (Hii ndiyo desturi nzuri kwa sisi kuiga!) Hapa anashukuru Mungu katika Yesu Kristo, Mpatanishi, kwa sababu **imani** ya Wakristo katika Roma ilitangazwa **katika dunia nzima**. Watu walisema juu ya ushuhuda wa Wakristo pahali pote katika ufalme wa Roma iliyokuwa kama **dunia nzima** kwa watu waliokaa karibu na Bahari ya Méditerranée kwa wakati ule.

1:9 Kwa sababu Wakristo wa Roma waliacha nuru yao kungaa mbele ya watu,

Paulo aliwaombea **bila kuacha**. Alisema Mungu ni **mshuhuda** wa **maombi** haya kwa sababu hakuna mtu aliyeweza kujua neno hili. Lakini **Mungu** alijua – ndiye Mungu ambaye mtume alitumikia **kwa roho yake katika Habari Njema ya Mwana wake**. Paulo alitumikia Mungu kwa **roho yake**. Hakufuata kawaida ya kuchokeza ya kusema tena na tena maombi ambayo alijifunza kwa nia. Utumishi wake ulisimama kwa sababu ya maombi yake ya roho ya kuwaka. Alitumikia Bwana na kutaka kwake, na alijitoa mzima kwa utumishi huu kwa sababu ya mapendo yake makubwa kwa Bwana Yesu, na kwa sababu ya bidii ya moyo wake kutangaza Habari Njema juu ya Mwana wa Mungu.

1:10 Pamoja na kushukuru Mungu kwa watakatifu wa Roma, aliomba vilevile aweze kuwafikia nyuma ya muda fupi, kama safari hii ikiwa kwa **mapenzi ya Mungu**.

1:11 Mtume alitaka sana sana kusaidia watakatifu kwa Roma kusudi waweze **kusimamishwa imara** katika imani. Hakukusudi kuwapa zawadi nyininge ya roho kwa njia ya kuwawekea mikono wake (kama alivyofanya kwa Timoteo katika 2 Tim. 1:6). Alitaka kusatisha **roho** zao nguvu kwa njia ya mafundisho toka Neno la Mungu.

1:12 Anaendelea kueleza kwamba **watabarikiana**. **Imani yao itasaidia** roho yake, nao watasaidiwa na imani ya Paulo. “Chuma kinanoa chuma; ndivyo mtu anavyonoa uso wa rafiki yake” (Mez. 27:17). Ona unyenyekevu na neema ya Paulo – hakufikiri yeeye ni mkubwa kupita waamini wengine asiyehitaji kusaidiwa.

1:13 **Alifanya shauri** mara nydingi kufikia Roma, **lakini** labda alizuiwza na mahitaji ya kazi ya Mungu pahali pengine. Au alizuiwza na Roho Mtakatifu, au na Shetani. Alitaka **kuwa na matunda** katika Mataifa ya Roma **kama katika Mataifa mengine**. Hapa anasema juu ya

matunda kwamba anasema hapa juu ya mbolewa kweli na damu ya damani ya Kristo. Wanapendwa na Mungu kupita watu wengine, na kuitwa vilevile kuwekwa mbali kwa Mungu toka maneno ya dunia, ndiyo maana ya neno hili watakatifu.

Ni desturi ya Paulo kusalimu watu na neema na salama. Neema (charis) ni Kiyunani, na salama (shalom) ni salama ya Wayuda. Salama hii ina maana sana hapa kwa sababu kwa hotuba ya Paulo inaonyesha kwamba waamini Wayuda na Mataifa ni moja sasa ndani ya Kristo.

Neema inayotajwa hapa si neema inayookoa watu (wasomaji wa Paulo waliokuwa wameokolewa mbele), lakini neema ambayo inaleta Wakristo uwezo kwa maisha na utumishi wao. Salama hii si zaidi salama na Mungu (wasomaji waliokuwa na salama ile kwa sababu waliokuwa wamehesabiwa haki kwa njia ya imani), lakini salama ya Mungu inayoweza kutawala rohoni mwao hata wakati walipokaa katikati ya makelele ya watu. Neema na salama zimetoka kwa Mungu Baba yetu na Bwana Yesu Kristo. Habari hizi zinaonyesha wazi kwamba Mwana na Baba ni sawasawa. ni sawasawa. Kama Yesu akiwa mtu tu, ingekuwa upumbavu kusema juu yake akitoa neema na salama pamoa na Baba.

1:8 Kama ikiwezekana, mtume alianza barua zake na sifa kwa mambo mazuri yo yote ndani ya maisha ya wasomaji wake. (Hii ndiyo desturi nzuri kwa sisi kuiga!) Hapa anashukuru Mungu katika Yesu Kristo, Mpatanishi, kwa sababu imani ya Wakristo katika Roma ilitangazwa katika dunia nzima. Watu walisema juu ya ushuhuda wa Wakristo pahali pote katika ufalme wa Roma, ili yokuwa kama dunia nzima kwa watu waliokaa karibu na Bahari ya Méditerranée kwa wakati ule.

1:9 Kwa sababu Wakristo wa Roma waliacha nuru yao kungaa mbele ya watu, Paulo aliwaombea bila kuacha. Alisema

Mungu ni mshuhuda wa maombi haya kwa sababu hakuna mtu aliyeweza kujua neno hili. Lakini Mungu alijua – ndiye Mungu ambaye mtume alitumikia kwa roho yake katika Habari Njema ya Mwana wake. Paulo alitumikia Mungu kwa roho yake. Hakufuata kawaida ya kuchokeza ya kusema tena na tena maombi ambayo alijifunza kwa nia. Utumishi wake ulisimama kwa sababu ya maombi yake ya roho ya kuwaka. Alitumikia Bwana na kutaka kwake, na alijitoa mzima kwa utumishi huu kwa sababu ya mapendo yake makubwa kwa Bwana Yesu, na kwa sababu ya bidii ya moyo wake kutangaza habari njema juu ya Mwana wa Mungu.

1:10 Pamoja na kushukuru Mungu kwa watakatifu wa Roma, aliomba vilevile aweze kuwafikia nyuma ya muda fupi, kama safari hii ikiwa kwa mapenzi ya Mungu.

1:11 Mtume alitaka sana sana ku-saidia watakatifu kwa Roma kusudi waweze kusimamishwa imara katika imani. Hakukusudi kuwapa zawadi nyininge ya roho kwa njia ya kuwawekea mikono wake (kama alivyofanya kwa Timoteo katika 2 Tim. 1:6). Alitaka ku-patisha roho zao nguvu kwa njia ya ma-fundisho toka Neno la Mungu.

1:12 Anaendelea kueleza kwamba watabarikiana. Imani yao itasaidia roho yake, nao watasaidiwa na imani ya Paulo. “Chuma kinanoa chuma; ndivyo mtu anavyonoa uso wa rafiki yake” (Mez. 27:17). Ona unyenyekevu na neema ya Paulo – hakufikiri ye ye ni mkubwa kupita kusaidiwa na watakatifu wengine.

1:13 **Alifanya shauri** mara nyingi kufikia Waroma, **lakini** alizuiwza na mahitaji ya kazi ya Mungu pahali pengine. Labda alizuiwza na Roho Mtakatifu, au labda na Shetani. Alitaka **kuwa na matunda** katika Mataifa ya Roma **kama katika Mataifa mengine**. Mash. 14 na 15 yanaonyesha kwamba anasema hapa juu ya **matunda** ya Habari

matunda kwa njia ya Habari Njema. Ndani ya mash. 11 na 12 aliweka roho kwa Wakristo katika Roma kupatishwa nguvu katika imani yao. Katika shairi 13 hamu yake ilikuwa zaidi kupata watu kwa Kristo katika mji mkubwa wa ufalme wa Roma.

1:14 Mtu ye yote aliyepokea Kristo ana majibu kwa mahitaji makubwa zaidi ya dunia hii. Anajua namna gani mtu anaweza kuponyeshwa toka ugonjwa wa zambi, namna gani anaweza kuепuka hofu kubwa ya milele ya Gehena, na namna gani anaweza kukaa kwa milele na furaha pamoja na Mungu. Akijua maneno haya yote ana deni kubwa kushiriki Habari Njema na watu namna namna – **washenzi** na watu wenyewe elimu kwa kipimo mbalimbali, **wenye akili na wajinga**. Neno hili lilikuwa mzigo mku'bwa kwa roho ya Paulo na alisema, “**Mimi ni mdeni.**”

1:15 Kwa kulipa deni hii, alikuwa tayari **kuhubiri Habari Njema** kwa watu waliokaa **katika Roma** na uwezo wote aliopokea toka Mungu. Mahubiri haya hayakuwa kwa waamini katika Roma, kwani wao walikwisha kupokea Habari Njema, lakini alikuwa tayari kuhubiri kwa watu wa mataifa ambayo hawakuokolewa bado.

B. Habari Njema ni nini? (1:16, 17)

1:16 Paulo **hakuwa na haya** kufikisha Habari Njema kwa Roma. Hata kama habari hizi zilikuwa kikwazo kwa Wayuda na upumbavu kwa mafikiri ya Wayunani, Paulo alijua ni **uwezo wa Mungu hata wokovu** – namna kwa uwezo wake Mungu anaokoa kila mtu ambaye anaamini Mwana wake, wa Wayuda na wa Wayunani vilevile.

Kwa Myuda kwanza, na kwa Myunani vilevile – neno hili lilitimizwa ndani ya muda wa Matendo. Sasa tungali na deni kuhubiri Habari Njema kwa watu wa zamani wa Mungu, ndio Wayuda, lakini hatuagizwi kuhubiri Habari Njema kwa

mbele ya kuihubiri kwa Mataifa. Habari ya Mungu kwa Wayuda na Mataifa ni sawasawa kwa wakati wa sasa. Ni kwa watu wote.

1:17 Hii ni mara ya kwanza tunayoona neno hili **haki**, hivi tuwaze kwanza kama maana yake ni nini. Neno hili linatumiwa kwa njia mbalimbali ndani ya Agano Jipy, lakini tutafikiri juu ya njia tatu tu.

Kwanza, linatumiwa juu ya Mungu, na namna matendo yake yote ni haki na yanapatana na maneno yote ya tabia yake. Wakati tunaposema Mungu ni mwenye haki, tunasema kwamba hakuna ubaya, uwongo, au udanganyifu ndani yake.

La pili, haki ya Mungu inaweza kusema juu ya namna Mungu anavyohesabia haki wazalimu na wenyewe zambi. Anaweza kufanya hivi pamoja na kuwa mwenye haki kwa sababu Yesu, Mkombozi asiyе na zambi alitimiza yote yaliyohitajiwa na haki ya Mungu.

Mwishoni, haki ya Mungu inasema vilevile juu ya hali timilifu ambayo Mungu anapatia wote wanaoamini Mwana wake (2 Kor. 5:21). Watu wasio na haki wanatendewa sawasawa wao ni wenyewe haki kwa sababu Mungu anawona ndani ya utimilifu wa Kristo. Wana-hesabiwa haki.

Maana gani ni maana ya shairi 17? Zingeweza kuwa maana tatu zote, lakini ni kama haki ya Mungu inasema zaidi juu ya namna anavyohesabia haki wenyewe zambi ambao wanamwamini.

Haki ya Mungu inafunuliwa ndani ya Habari Njema. Kwanza Habari Njema inatujulisha kwamba haki ya Mungu inalazimisha kwa zambi kuazibiwa na ya kwamba azabu ya zambi ni mauti ya milele. Lakini tunasikia ya kwamba mapendo ya Mungu yaliweka tayari neno ambalo haki la Mungu iliagiza. Alituma Mwana wake kufa kama Mkombozi kwa wenyewe zambi na kulipa deni nzima ya zambi zao. Haki yake ilitimizwa kabisa, na sasa Mungu anaweza kuponyesha na

haki wote wanaopokea kazi ya Kristo kwa ajili yao.

Haki ya Mungu **inafunuliwa, toka imani hata imani**. Maana ya maneno haya inaweza kuwa: (1) toka uaminifu wa Mungu hata imani yetu; (2) toka kipimo kimoja cha imani hata kipimo kingine; au (3) toka mwanzo wa imani hata mwisho. Tunafikiri maana ya tatu ni maana yake hapa. Mungu hahesabii watu haki kwa sababu ya kazi yao, au kuwapa haki wale wanaojaribu kustahili kuipokea. Inafunuliwa kwa njia ya imani tu. Neno hili linapatana na amri ya Mungu katika Hab. 2:4, “**Mwenye haki ataishi kwa imani yake.**” Maana ya maneno haya ingeweza kuwa vilevile “Wale wanaohesabiwa haki kwa imani wataishi.”

Ndani ya mashairi 17 ya kwanza ya Waroma Paulo amejulisha wasomaji jambo kubwa la barua hii, na kutaja kwa ufupi maneno yake makubwa. Aliendelea sasa kujibu ulizo kubwa la tatu: “Watu wanahitaji Habari Njema kwa sababu gani?” Kwa sababu bila Habari Njema wanapotea. Lakini ulizo hili linazaa maulizo mane mengine: (1) Wapagano wasiosikia Habari Njema kamwe wanapotea? (1:18-32); (2) Wapagano wanaofikiri wanatembea vizuri wakiwa Wayuda au Mataifa, wanapotea? (2:1-16); (3) Watu wa zamani wa Mungu, ndio Wayuda, wamepotea? (2:17 – 3:8); (4) Watu wote wamepotea? (3:9-20).

C. Watu wote wanahitaji

Habari Njema (1:18 – 3:20)

1:18 Hapa tunaona kwa sababu gani watu wanahitaji Habari Njema. Ni kwa sababu bila Habari Njema wanapotea, na kwa sababu **kasirani ya Mungu imefunuliwa kutoka mbingu juu ya uasi wa watu, na uovu wa watu wanaofunga kweli** kwa njia ya maisha yao ya uzalimu. Lakini gazabu ya Mungu **inafunuliwa** namna gani? Mungu anawacha katika tamaa za miyo yao wafuate

uchafu (sh. 24), kwa tamaa za aibu (1:26), na kwa akili zao zisizofaa (sh. 28). Na wakati na wakati anaonyesha uchungu wake mkubwa waziwazi katikati ya watu, kwa mfano kwa njia ya garika (Mwanzo 7; uharibifu wa Sodomo na Gomora (Mwa. 19); na azabu ya Kora, Datani, na Abiramu (Hes. 16:32).

1:19 Ulizo lingine ndilo: “Wapagano wasiosikia Habari Njema kamwe wanapotea?” Paulo anaonyesha kwamba wanapotea kweli, si kwa sababu ya ukosefu wa kujua maneno mengine, lakini **kwa sababu** wanakataa maneno yale ya Mungu **wanayokwisha kujua**, ndiyo maneno Mungu anayokwisha kuwafunulia kwa njia ya kuyaumba. Hakuacha watu bila ufunuo juu yake mwenyewe.

1:20 Maneno mawili ya Mungu **yasiyoonekana tangu kuumbwa kwa ulimwengu** yanaonekana wazi kwa watu wote, ndiyo **uwezo wake wa milele na uungu** wake. Uungu wake unatufkirisha hapa juu ya tabia yake kama Mungu.

Mawazo ya mwandishi ni wazi: Dunia hii iliyoumbwa ilihitaji Mwumba mwenye shauri la namna gani kuiumba. Mtu akiangalia jua, mwezi na nyota anajua kwamba kuna Mungu.

Jibu la ulizo juu ya wapagano ndilo hili: **Hawana uzuru.** Mungu amejifunua kwao ndani ya vitu alivyoumba, lakini hawakukubali ufunuo huu. Hivi watu hawahukumiwi kwa sababu ya kukataa Mwokozi ambaye hawakusikia habari zake, lakini kwa sababu hawakubali na kutii maneno ambayo iliwasapa kujua juu ya Mungu.

1:21 Hata kama walijua Mungu kwa njia ya vitu alivyoumba, **hawaku-mtukuza kama Mungu**, wala kumshukuru kwa vyote alivyonenda. Walijitoa kwa mafundisho **yasiyo na faida** na kufikirifikiri juu ya miungu mingine. Kwa sababu hii hawakuweza kufikiri tena vizuri na ufahamu wao ulitiwa giza.

1:22 Kwa kipimo walicho jivuna juu ya maneno waliyofikiri walijua, wali-zidi kuwa wajinga na wapumbavu. Maneno haya mawili yana onekana kila mara ndani ya maisha ya watu wanaokataa kujuana na Mungu – pamoja na kuwa wenyewe kiburi sana wanageuka wajinga kabisa.

1:23 Kwa sababu hawakukubali **Mungu asiyé na uharibifu** walishuka kushikamana na upumbavu na upotovu wa kuabudu sanamu.

Watu wana roho inayohitaji kuwa na kitu wanachowenza kuabudu. Wakati walipokataa kuabudu Mungu aliye hai, walijifanyia miungu yao wenyewe toka miti na mawe kwa sura ya **mtu, na ya ndege, na nyama, na vitu vya kutambaa**. Tukumbuke kwamba mtu anageuka kufanana na kitu anachoabudu. Kwa kipimo anachoacha kuabudu Mungu mtakatifu, mwenendo wake una-haribika vilevile. Kama mungu wake ni nyoka, anafikiri anawenza kufanya neno lo lote analotaka. Kumbuka vilevile kwamba ni desturi kwa mwabudaji kuji-hesbu kuwa chini kupita kitu ana-choabudu. Hivi mtu aliyeumbwa kwa mfano na sura ya Mungu anajihesbu kuwa chini kupita nyoka!

Wakati mtu anapoabudu sanamu anaabudu mashetani. Paulo alisema waziwazi kwamba vitu Mataifa wavyotoa wanavitolea mashetani, wala si kwa Mungu (1 Kor. 10:20).

1:24 Tunasoma mara tatu kwamba **Mungu aliachá** watu. Aliwaacha **kwa uchafu** (1:24), kwa tamaa za aibu (1:26), na wafuate akili zao zisizofaa (1:28). Hivi tunafahamu kwamba gazabu ya Mungu iligusa mtu mzima.

Kwa sababu ya tamaa ovu za miyo yao, Mungu aliwaacha kwa tamaa za aibu – uzini, uasherati, uchafu, ukahaba, vivi hivi. Watu waliweka roho juu ya maneno haya tu, **wakaharibiana heshima ya miili yao**.

1:25 Mungu aliwaacha hivi kwa sababu kwanza wao walikuwa wame-acha **kweli** juu yake na kuikomboa na **uwongo** wa sanamu. Sanamu ni uwo-ngo, sura isiyo sura ya haki ya Mungu. Mwabudaji sanamu anaabudu mfano wa **kiúmbe**, na kwa njia hii anatukana na kuaibisha **Mwumba** anayestahili kupo-keea heshima na utukufu kwa milele, si matukano.

1:26 Kwa sababu hii **Mungu ali-acha** watu kwa tamaa za aibu, **wa-nawake** wakilala na wanawake kufanya zambi, bila haya.

1:27 **Wanaume** vilevile waligeuka na kutenda zambi na wanaume wengine, ndilo tendo lililo mbali na kusudi la Mungu. Waliacha utaratibu wa ndoa uliosimamishwa na Mungu, **wakawa-kiana tamaa kwa wanaume wengine**, wanaume wakilala na wanaume. Lakini zambi hii ilizaa matunda mabaya miilini na rohoni mwao na walipata ndani yao wenyewe malipo yaliyofaa kwa upotevu wao.

Kwa wakati wa sasa watu wengine wanasema kwamba tamaa hii kwa wanaume wengine ni ugonjwa. Kuna wengine wanaosema desturi hii ya wa-naume kulala na wanaume wengine ni mwenendo unaokubaliwa. Lazima Wa-kristo wakae na ange na kukataa mawazo haya ya zambi ya watu wa dunia, na waongozwe na Neno la Mungu. Ndani ya Agano la Kale azabu kwa zambi hii ilikuwa mauti (Law. 18:29; 20:13). Ndani ya Agano Jipyu tu-naona kwamba watendaji zambi hii wanastahili kufa (Rom. 1:32). Biblia inaonyesha kwamba zambi hii ndiyo zambi mbaya sana, na kwa sababu hii Mungu aliharibu miji ya Sodomo na Gomora kabisa (Mwa. 19:4-25).

Lakini hata watendaji zambi mbaya hii, kama wenyewe zambi wote wengine wanawenza kusamehewa kama wakitubu na kuamini Bwana Yesu Kristo. Wa-kristo walioanguka na kutenda zambi hii

mbaya sana wanaweza kupokea usamehe na kurudishwa karibu na Bwana kwa njia ya toba na kuiacha. Wote walio tayari kutii Neno la Mungu wanaweza kufunguliwa kabisa toka utumwa wa zambi hii. Ni vizuri Wakristo wengine wafungane pamoja nao na kuwasaidia na Neno la Mungu.

Ni kama zambi hii ni jaribu kubwa zaidi kwa watu wengine. Hatuwezi kushangaa juu ya neno hili kwa sababu wenyе zambi wanaweza kutenda maovu namna zote. Jaribu lenyewe si zambi; lakini ni zambi kukubali kufanya neno tunalojaribiwa kufanya. Roho Mtakatifu ni tayari kutuwezesha kushinda majoribu kabisa (1 Kor. 10:13). Maisha ya Wakristo wengine katika Korinto yalihakikisha kwamba si lazima kwa zambi hii mbaya kufunga na kutawala mtu daima (1 Kor. 6:9-11).

1:28 Kwa sababu watu wanakataa kuwa na Mungu katika ufahamu wao kama Mwumba na Mwokozi, **Mungu aliwaacha wafuate akili zao zisizofaa** na kutenda uovu namna namna. Shairi hili linatusaidia kufahamu kwamba watu **hawataki kujua Mungu**. Ndiyo, wana-taka kukaa bila Mungu kwani wanajua kwamba kuna Mungu, inawapasa kumnyenyekea.

1:29 Basi tunaona hapa zambi namna namna zinazotenga watu na Mungu. Ona ya kwamba hawatendi zambi hizi mara moja moja tu lakini *wamejaa* zambi zisizofaa hata kidogo kwa watu, ndizo **uzalimu, ubaya, tamaa na uovu; wamejaa hasidi, uuaji na ugomvi**, wenyе **kusengenya**;

1:30 wenyе kusingizia; wenyе kuchukia Mungu, wenyе jeuri na kujivuna; wenyе kutunga maneno mabaya, wasiotii wazazi wao,

1:31 bila ufahamu, wenyе kuvunja mapatano, wasiopenda jamaa zao wala kuwasamehe na kuwa na rehemea.

1:32 Watu wanaofanya zambi zina-

zotajwa ndani ya mashairi 24, 26, 27 na 29-31 wanafahamu rohoni mwao kwa-mba maneno haya ni mabaya, na ya kwamba wao wenyewe **wanastahili kufa**. Hata wakijua hii ndiyo hukumu ya Mungu, wanakaa kufanya maneno haya na kushiriki na watu wengine ambaو wanayatenda.

WAPAGANO WASIOSIKIA HABARI NJEMA

Tuone jibu la Mungu kwa ulizo hili: “Wapagano wasiosikia Habari Njema wanapotea?” Wapagano wanahukumiwa kwa sababu hawatii maneno wanayo-kwisha kujua juu ya Mungu kwa njia ya vitu alivyoumba, lakini wanaabudu sanamu na kujitoa kutenda uovu namna namna.

Basi labda kuna mpagano anayetii maneno yote anayojuu juu ya Mungu na anayeteketeza sanamu zake zote. Mtu huyu anaokolewa?

Waamini wa kweli wana mawazo mbalimbali juu ya neno hili.

Wengine wanaamini kama kweli mpagano akitii maneno yote anayojuu juu ya Mungu kwa njia ya vitu alivyoumba, Mungu atatumua kwake mtu ambaye atamtangazia Habari Njema, kama alivyofanya na Kornelio. Korne-lilio alitaka kujua Mungu. Maombi yake na sadaka zake zimefika juu kama ukumbusho mbele ya Mungu (Mdo. 10:4). Halafu Mungu alituma Petro kumjulisha namna gani aliweza kuokolewa (Mdo. 11:14).

Kuna watu wengine wanaofikiri kama mtu akitegemea Mungu wa kweli aliye hai namna alivyojifunua ndani ya vitu alivyoumba, lakini mtu huyu aki-kufa mbele ya kusikia Habari Njema, Mungu atamwokoa kwa sababu ya kazi ya Kristo kwa Kalvari. Hata kama mtu huyu hakujua habari za kazi ya Kristo, Mungu anamhesabia faida ya kazi ile wakati anapoamini Mungu kwa sababu

ya maneno anayojua juu yake. Watu wanaosimamia elezo hili wanasema kwamba Mungu aliokoa watu kwa njia hii mbele ya kufa kwa Kristo kwa Kalvari, na namna anavyoookoa hata sasa wenye upungufu wa akili, na watoto wadogo vilevile wanaokufa mbele ya kuweza kujuua na kufahamu Habari Njema.

Elezo la kwanza linasimamishwa na habari zilizotokea ndani ya maisha ya Kornelio. Hakuna neno ndani ya Mandiko kusimamisha elezo la pili kwa muda nyuma ya mauti na ufufuko wa Kristo (muda wa sasa), nalo linapungusa vilevile bidii ya watu kwa kazi ya kuitangaza Habari Njema. ♦♦♦

Paulo ameonyesha kwamba wapagano wanapotea na wanahitaji Habari Njema. Sasa ndani ya sura 2 ya barua yake kwa Waroma anasema juu ya namna nyiningine ya watu.

2:1 Watu hawa ndio wale wanaoona wapagano kama watu bure na wanaofikiri wao wenyewe ni wazuri kupita kwa namna wanavyoishi na kujifunza, vivi hivi. Wanahukumu wapagano kwa sabbu ya matendo yao maovu sana, lakini wanafanya maneno namna hii wao wenyewe. Ni nyepesi kwa wasioamini kuona zambi ndani ya watu wengine bila kuziona ndani ya maisha yao wenyewe. Ni kama matendo maovu sana ndani ya maisha ya watu wengine yanakubaliwa ndani ya maisha yao wenyewe. Lakini kwa njia ya kuweza **kuhukumu** zambi ndani ya maisha ya watu wengine wanavyesha kwamba wanafahamu maneno gani ni mazuri na maneno gani ni zambi. Akijua kwamba ni zambi kwa mtu kuiba mke wa mtu mwengine, anajua vilevile kwamba ni zambi kwa ye ye mwenyewe kuiba mke wa mtu mwengine. Hivi kama akihukumu zambi fulani ndani ya maisha ya mtu mwengine hana uzuru wakati anapokubali zambi hii ndani ya maisha yake mwenyewe.

Namna ya zambi za wenyewe malezi mema na zile za wapagano ni karibu sawasawa. Labda mwenye elimu anataka kusema hakufanya zambi namna zote wapagano wanazofanya; inampasa kukumbuka kwamba:

1. angeweza kuzifanya zote.
2. akiasi agizo moja tu anayaasi yote (Yak. 2:10).
3. amekosa kwa njia ya *kuwaza* juu ya zambi fulani bila kuzitenda. Neno hili linakatazwa vilevile ndani ya Biblia. Yesu alifundisha kwamba mtu akitazama mwanamke kwa kumtamani anakwisha kuzini naye moyoni mwake (Mt. 5:28).

2:2 Wale wanaowaza mwenendo wao ni safi kupita mwenendo wa watu wengine wanahitaji kujifunza juu ya **hukumu ya Mungu**. Ndani ya mashairi 2-16 mtume aliwfundisha juu ya neno hili. Neno la kwanza ndilo ya kwamba **hukumu ya Mungu ni ya kweli**. Inasi-mama juu ya kweli nzima juu ya neno fulani, si juu ya ushuhuda wa watu juu ya mambo wanayosema yaliyotokea.

2:3 Neno la pili ni ya kwamba *hakuna njia* kwa wale kuepuka **hukumu ya Mungu** wanaofanya wao wenyewe zambi ambazo **wanashitaki** watu wengine juu yao.

Hakuna njia kuepuka hukumu ya Mungu ila kwa njia ya *kutubu na kupoakea usamehe*.

2:4 Mara nyiningine hukumu ya Mungu inachelewa. Neno hili linaonyesha **wema na saburi na uvumilivu** wake. Maana ya **wema** wake ndiyo ya kwamba ana mapendo kwa wenyewe zambi, hata kama hapendi zambi zao. Maana ya **saburi** ndiyo ya kwamba anazuiza kwanza azabu kwa uovu na uasi wa watu. **Uvumilivu** unaonekana kwa namna anavyojizuiza hata wakati watu wanapokaa kumkasirisha.

Wema wa Mungu unaonekana kwa namna anavyolinda na kuchunga watu na kusudi la kuwaongoza kutubu. Hataki

“mtu mmoja kupotea, lakini wote wafike kutubu” (2 Pet. 3:9).

Toba ndiyo kwa mtu kugeuka kabisa, na kuachana na zambi zake. Si kugeuka kwa njia ya akili na mawazo yake tu, lakini kwa roho na damiri, na matendo.¹

2:5 Neno la ine tunalojifunza juu ya hukumu ya Mungu ni ya kwamba ni *kipimo mbalimbali kupatana na ukubwa wa hatia* ya mtu. Paulo anaandika juu ya watu wenye roho ngumu bila toba ambao wanajivimbishia hukumu, namna mtu anavyojivimbishia **hazina** ya zahabu na feza. Lakini wakati mwishoni **gazabu** ya Mungu itakapofunuliwa kwa **hukumu** ya kiti cha ufalme kikubwa cheupe (Ufu. 20:11-15) **hukumu ya Mungu** itaonekana kuwa **haki** kabisa, *bila upendeleo wo wote*.

2:6 Ndani ya mashairi yanayofuata Paulo anatukumbusha kwamba **hukumu ya Mungu** itakuwa kwa **kadiri ya matendo** ya mtu. Labda mtu angeweza kutegemea wema wake, au kabilia au taifa lake. Labda anakumbuka kwamba wengine wa wazazi wake walikuwa watu wa Mungu kabisa. Lakini atuhukumiwa kwa kadiri ya *mwenendo ya matendo yake mwenyewe*.

Kama tukisoma mashairi 6-11 peke yao, labda tungeweza kufikiri ya kuwa yanafundisha kwamba wokovu unapatikana kwa njia ya matendo. Ni kama yanaonyesha kwamba watu wanaweza kupata uzima wa milele kwa njia ya kutenda mema.

Lakini maana hii haiwezi kuwa maana ya kweli ya mashairi haya. Haipatani na mafundisho mengine ya Biblia kwamba wokovu unapatikana kwa njia ya imani tu bila kazi njema. Mwalimu mmoja, jina lake Chafer, alionyesha kwamba mashairi karibu 150 ndani ya Agano Jipyä yanafundisha ya kuwa wokovu unapatikana kwa njia ya kuamini, ndiyo imani tu.²

Basi maana ya mashairi haya ni nini? Lazima tufahamu kwamba mtu hawezi

kufanya kazi njema mbele ya kuzaliwa tena. Wakati watu walipouliza Bwana Yesu, “Tufanye nini, tupate kufanya kazi za Mungu?” Bwana alijibu, “Hii ndiyo kazi ya Mungu, mumwamini yeye aliyetumwa naye” (Yn. 6:28, 29). Hivi kazi njema ya kwanza mtu anayoweza kutenda ni kuamini Bwana Yesu Kristo. Tusingahau kamwe kwamba *mtu hawezi kupata wokovu kwa njia ya kufanya matendo mema*. Hivi wasioamini waki-hukumiwa kwa kadiri ya kazi zao njema, kazi hizi wanazofikiri ni kazi za haki zitaonekana kuwa vitambaa nya kuperasukapasuka nya taka (Isa. 64:6). Watahukumiwa kwa sababu hawakumini Yesu kuwa Bwana wao (Yn. 3:18). Zaidi ya ile, wataazibwa kwa kadiri ya kazi zao (Lk. 12:47, 48).

Hukumu ya *waamini* kwa kadiri ya kazi zao itakuwa namna gani? Kazi njema zote walizofanya mbele ya kukoleta zilikuwa na zambi. Lakini damu ya Kristo ilizizima zote. Sasa Mungu mwenyewe haoni neno baya ambalo linawastahilisha kuhukumiwa kwa Gehena. Wakati wanapokwisha kupa-wokovu wanaanza kutenda kazi njema – labda si nzuri kwa macho ya watu wa dunia, lakini kwa macho ya Mungu ni kazi njema. Kazi hizi ni matunda ya wokovu. Hawazifanyi kupa-wokovu lakini kwa sababu wanakwisha kuokolewa. Kwa kiti cha hukumu cha Kristo kazi hizi zitapimwa, na waamini watapokea zawabu kwa kadiri ya uaminifu wa utumishi wao.

Lakini tukae kukumbuka kwamba mashairi haya si juu ya maneno ya waamini. Ni juu ya wasioamini tu.

2:7 Wakati Paulo alipoeleza kwamba hukumu itakuwa kwa kadiri ya matendo, alisema Mungu atawapa **uzima wa milele watu wale ambao kwa matendo mazuri wanatafuta utukufu na heshima na kutokuharibika**. Maana yake *haiko* ya kwamba watu hawa wanapata wokovu kwa njia ya **kuende-**

lea kwa saburi katika matendo mema. Hakuna mtu anayeweza kuishi maisha namna hii kwa nguvu yake mwenyewe. Inawezekana kwa uwezo wa Mungu tu, hivi inawezekana kwa watu wale tu wanaokwisha kuokolewa kwa neema na imani. Kwa njia ya kutafuta **utukufu, heshima, na kutokuharibika** wanaonyesha kwamba wanakwisha kuzaliwa tena. Maneno yote ya maisha yao yanaonyesha kwamba wanakwisha kupata uzima mpya.

Anatafuta **utukufu** wa mbingu; **heshima** inayotoka kwa Mungu tu (Yn. 5:44); **kutokuharibika** ndiyo namna ya mwili unaokwisha kufufuliwa toka mauti (1 Kor. 15:53-54); uriti wa mbingu, usioharibika, usio na uchafu wala usiopunguka (1 Pet. 1:4).

Mungu atawapa **uzima wa milele** wote ambao wanaonyesha kwa njia hizi kwamba wameokolewa. **Uzima wa milele** unaonyeshwa kuwa namna mbali mbali katika Agano Jipy. Mtu anaupokea dakika ile ile anapozaliwa tena (Yn. 5:24). Tutakuwa na uzima wa milele wakati tutakapopokea miili yetu ya utukufu (hapa na kwa Rom. 6:22). Ni zawadi ambayo tunapokea kwa njia ya imani, lakini mara nyingine tunasoma juu yake kama zawabu kwa maisha maaminifu (Mk. 10:30). Waamini wote watakuwa na **uzima wa milele**, lakini watu wengine wataweza kuufurahia kupita wengine. Si uzima unaoendelea kwa milele tu; ni namna ya **uzima, uzima** tele ambao Mwokozi aliahidi kutupa sisi ndani ya Yoane 10:10. Ni **maisha** ya Kristo mwenyewe (Kol. 1:27).

2:8 Lakini wale wenye fitina, na wasiotii kweli, lakini wanatii uzalimu, watapata kasirani na gazabu. Hawatii kweli; hawakupokea Habari Njema kamwe. Walichagua kutawaliwa na uzalimu. Maisha yao ya magomvi, fitina na uasi yanaonyesha wazi kwamba hawakuzaliwa tena.

2:9 Sasa mtume alionyesha tena hukumu ya Mungu kwa namna mbili ya watumishi na kazi, lakini mara hii aliandika juu ya waovu kwanza.

Kila mtu **anayetenda uovu** atahukumiwa na **mateso na taabu**. Kazi hizi mbovu zinaonyesha wazi kutokuamini kwa mwenye kuzitenda, na kwamba anakosa heshima kwa Bwana.

Maneno haya, kwa **Myuda kwanza; na Myunani vilevile**, yanaonyesha kwamba *hukumu ya Mungu itakuwa kwa kadiri ya mapendeleo au nuru* mtu alizopokea. Wayuda walikuwa **wa kwanza** kupokea mapendeleo ya Mungu kama watu wachaguliwa wa Mungu duniani; hivi wamepewa kazi au daraka kubwa kupita. Tutasema juu ya neno hili tena ndani ya mashairi 12-16.

2:10 Myuda au Myunani vilevile **anayetenda mema** atapata **utukufu, heshima, na salama**. Lakini tuisahau kamwe ya kwamba hakuna mtu anayeweza kutenda yaliyo mema kwa macho ya Mungu bila kuamini Bwana Yesu Kristo kwanza.

Maana ya **kwa Myuda kwanza, na kwa Myunani vilevile** si kuonyesha upendeleo, kwa sababu shairi linalifuata linaonyesha wazi kwamba hukumu ya Mungu ni bila upendeleo. Hivi maneno haya yanaonyesha kwamba Habari Njema ilihubiriwa kwanza kwa Wayuda, Rom. 1:16, na waamini wa kwanza walikuwa Wayuda.

2:11 Kweli nyingine ndiyo hii: hukumu ya Mungu ni *bila upendeleo*. Mara nyingi waamuzi wa dunia wana upendeleo kwa watu wanaoonekana vizuri, walio na mali na heshima, **lakini Mungu** hana upendeleo hata kidogo. Haweki roho juu ya kabila, au heshima wakati anapohukumu mtu.

2:12 Mashairi 12-16 yanaongeza juu ya mafundisho ya shairi 9, ya kwamba hukumu ya Mungu ni kwa kadiri ya nuru, ndiyo maneno mtu anayokwisha kujua. Tunaona watu wa

namna mbili: wale wasiojua sheria (Mataifa), na wale wanaotawaliwa na sheria (Wayuda). Kunabaki namna moja ya watu, ndio wale walio ndani ya kanisa la Mungu (ona 1 Kor. 10:32 linaloonyesha kwamba kuna namna hizi tatu za watu duniani).

Wale waliokosa pasipo sheria watapotea pasipo sheria. Biblia haisemi kwamba “*watahukumiwa pasipo sheria*” lakini **watapotea pasipo sheria.** Watahukumiwa kwa kadiri ya maneno ambayo Bwana aliwafunulia; **watapotea** kama wasipotii maneno haya waliofunuliwa.

Wote waliokosa wakiwa na sheria watahukumiwa kwa sheria, na kama waliasi sheria, watapotea vilevile. Ni lazima kutii sheria kwa kila neno.

2:13 Haitoshi kujua sheria. Ni lazima kuitii katika kila neno na kwa kila saa. Hakuna mtu anayehesabiwa haki kwa njia ya kujua tu maagizo ya sheria. Kuna njia moja tu kuhesabiwa haki kwa njia ya sheria, ndio kuitii kabisa kabisa, kila agizo. Lakini watu wote ni wenye zambi, hivi neno hili linashinda wadamu.

Agano Jipyä linafundisha waziwazi ya kwamba haiwezekani kwa mtu ku-hesabiwa haki kwa njia ya kushika sheria (ona Matendo 13:39; Rom. 3:20; Gal. 2:16, 21; 3:11). Mungu hakukusudi kamwe kwa mtu kuokolewa kwa njia ya sheria. Hata mtu akiweza kushika sheria kuanza sasa katika kila neno, hawezi ku-hesabiwa haki kwa njia hii kwani Mungu angemhukumu juu ya maneno aliyofanya mbele vilevile. Hivi tukisoma ndani ya shairi 13 kwamba wale **wanaotenda sheria watahesabiwa haki**, inatupasa kufahamu kwamba ni lazima kutii sheria katika kila neno tangu siku ya kuzaliwa, kwa kuweza ku-hesabiwa haki. Lakini hakuna mtu anayeweza kufanya hivi.

2:14 Ndani ya mashairi 14 na 15

tunarudi tena kwa mwanzo wa shairi 12 pahali tuliposoma kwamba wote waliokosa pasipo sheria wanapotea pasipo sheria. Sasa Paulo anaeleza kwamba Mataifa hawakupewa sheria, lakini wanajua hata hivi maneno gani ni mema na maneno gani ni mabaya. Wanajua hata bila sheria kwamba ni zambi kusema uwongo, kuiba, kuzini, na kuua mtu. Agizo la pekee wasilojua bila sheria ni agizo kushika sabato, ndio kawaida ya dini.

Hivi **mataifa wasio na sheria ... wamekuwa sheria kwa nafsi zao.** Wanafahamu ndani ya roho yao wenyewe mambo gani ni mema au mabaya.

2:15 Wanaonyesha **kazi ya sheria iliyoandikwa ndani ya miyo yao.** Si *sheria yenye* inayoandikwa ndani ya miyo yao, lakini **kazi ya sheria.** Kazi ambayo Mungu alikusudi sheria kufanya ndani ya maisha ya Waisraeli ili-onekana kwa sehemu ndani ya maisha ya mataifa hawa. Kwa mfano wanajua kwamba ni vzuri kuheshimu wazazi wao. Neno hili linaonyesha **kazi ya sheria imeandikwa katika miyo yao.** Wanajua vilevile kwamba maneno mengine ni mabaya. **Zamiri yao** inawafahamisha maneno haya. Mawazo yao yanawafahamisha saa zote kama matendo yao ni mema au mabaya, na **kuwashitaki** juu ya yale yaliyo mabaya.

2:16 Shairi hili linaendelea na ma-fundisho ya shairi 12. Linaonyesha *wakati gani* watu bila sheria na wale wanaotawaliwa na sheria watakapo-hukumiwa. Na linafundisha kweli moja ya mwisho juu ya hukumu ya Mungu: **zambi watu wanazotenda kwa siri zitahukumiwa vilevile**, si *zambi zile zinazoonekana wazi tu mbele ya watu*. Zambi zilizotendwa kwa siri zita-funuliwa wazi kwa Hukumu kwa Kiti Kikubwa Cheupe. Mwamuzi kwa wakati ule atakuwa **Yesu Kristo**, kwani Baba amempa Yeye hukumu yote (Yn. 5:22). Paulo aliongeza, **sawasawa na**

Habari Njema yangu, maana yake: “kama inavyofundisha na Habari Njema yangu.” **Habari Njema yangu** ndiyo Habari Njema Paulo aliyo-fundisha, iliyokuwa sawasawa na ile iliyohubiriwa na mitume wengine.

2:17 Halafu ilipasa mtume kufundiha juu ya watu wa namna ya tatu, hivi aliliza: *Basi Wayuda waliopewa sheria, wanapotea vilevile?* Jibu kwa ulizo hili ni wazi, “Ndijo, wanapotea vilevile.”

Bila shaka Wayuda wengi walifikiri kwamba hawatahukumiwa na Mungu. Walifikiri Mungu hatatuma **Myuda** kwa Gehena kamwe. Moto wa Gehena ulikuwa kwa Mataifa tu. Hivi ilikuwa lazima kwa Paulo kuonyesha kwamba labda kwa mambo mengine Mataifa ni karibu na Mungu kupita Wayuda.

Kwanza alitaja maneno Myuda aliyo-fikiri ni mazuri sana na yatampa ukubali na Mungu. Alitwa **Myuda**, hivi alikuwa mmoja wa taifa chaguliwa la Mungu duniani. Alitegemea **sheria**, lakini kusudi la sheria halikuwa kamwe kuleta raha, lakini kuamsha damiri ya mtu na kumfahamisha kwamba yeze ni mwenye zambi. Myuda alifurahi **ndani ya Mungu**, Mungu wa pekee wa kweli aliyefanya agano na taifa la Israeli tu.

2:18 Alijua **mapenzi** ya Mungu yaliyofunuliwa ndani ya Maandiko. Alikubali maneno yaliyo **mazuri sana** kwa sababu **sheria** ilimfahamisha yaliyo mema au mabaya.

2:19 Alijisifu akifikiri yeze ni **kiongozi** cha wale walio **wapofu** kwa maneno ya roho, **nuru** kwa watu walio katika **giza** la ujinga.

2:20 Alifikiri aliweza kufundisha **wajinga**, na kuwa mwalmu wa **watoto wadogo**, kwa sababu **sheria** ilikuwa imemjulisha **akili** na **kweli**.

2:21 Lakini maneno haya ambayo Myuda alijisifu juu yao hayakugeza maisha yake kamwe. Yalikuwa kiburi tu ya taifa na dini na hekima bila kuacha

maneno haya kugeuza mwenendo kupatana nao. Alifundisha watu wengine bila kujifundisha mwenyewe. Alihubiri kwamba kuiba ni zambi, lakini alikuwa mwizi yeze mwenyewe.

2:22 Alikataza watu **kuzini**, lakini alizini yeze mwenyewe. Ni kweli kwamba alichukia sanamu, lakini hakuo-gopa kuiba sanamu **katika mahekalu** ya wapagano.

2:23 Alijisifu ndani ya **sheria**, lakini alizarau **Mungu** kwa njia ya **kuvunja** maagizo yake matakatifu.

2:24 Matendo haya ya Wayuda yasiyopatana na mahubiri yao yalifanyiza **Mataifa** kutukana jina la Mungu. Ni desturi ya watu kupima Mungu kwa maneno wale wanaojiita wafuata wake wanafanya. Ilikuwa hivi kwa wakati wa Isaya (Isa. 52:5) na ni vivyo hivyo sasa. Ingetupasa sisi sote kujiuliza kama maneno gani ndani ya maisha yetu yanafikirisha watu juu ya Kristo.

2:25 Pamoja na sheria, Wayuda walijisifu juu ya kawaida ya **tohara**, ndiyo kukata kidogo ngovi ya wanaume Wayuda. Mungu alisimamisha kawaida hii kuwa alama ya agano lake na Abrahamu (Mwa. 17:9-14). Ilikuwa alama kuonyesha kwamba Wayuda walitengwa na watu wa dunia na kuwekwa mbali kwa Mungu. Kwa wakati wa nyuma Wayuda walijisifu sana juu ya kuhaririwa kwao hata waliita Mataifa “ku-tokutahiriwa.”

Hapa Paulo alifunganisha **tohara** pamoja na **Sheria** ya Musa. Alionyesha kwamba ilikuwa na maana tu kama yule aliyetahiriwa alitii Mungu ndani ya maisha yake ya kila siku tu. Mungu hafurahii kawaida ya matendo ya kuonekana ya dini tu kama matendo haya si matunda ya utakatifu rohoni. Hivi Myuda mtahiriwa anayeasi sheria ni kama mtu asiyetahiriwa.

2:26 Hivi, Mtaifa akitii maagizo ya **sheria**, **kutokutahiriwa kwake** kunakubaliwa na Mungu kupita tohara ya

Myuda anayeasi sheria. Roho ya Mtaifa huyu imetahiriwa – hili ndilo neno la faida zaidi.

2:27 Matendo mema ya Mtaifa yanahukumu Myuda aliye na **maandiko** na **tohara**, lakini asiyetii **sheria**, wala kuishi maisha yanayofaa kwa mtu aliyetahiriwa, mtu aliyetakaswa na kuwekwa mbali kwa Mungu.

2:28 Kwa mafikiri ya Mungu **Myuda** wa kweli si mtu mwenye damu ya Abrahamu mwilini mwake tu, au aliyetahiriwa tu. Inawezekana kwa mtu kuwa na damu ya Abrahamu, na alama ya tohara, pamoja na kuwa mtu mwovu kabisa. Bwana haweki roho juu ya maneno ya kuonekana kwa macho ya taifa au dini. Anataka kuona mtu mwenye roho safi na ya haki.

2:29 Myuda wa kweli si mzao wa Abrahamu tu, lakini mwenye kupendeza Mungu kwa mwenendo vilevile. Mashairi haya hayafundishi kwamba waamini wote ni Wayuda, au kwamba kanisa ni Israeli la Mungu. Paulo alisema juu ya watoto wa Wayuda, na ya kwamba kuwa na wazazi Wayuda na kuhiriwa hakutoshi. Lazima maneno haya yaonekane kwa njia ya mwenendo ya roho na usafi.

Tohara ya kweli ni ya **moyo** – si kukata mwili tu. Ni kwa mtu kujitenga kabisa na tabia ya zamani isiyozaliwa tena.

Wayuda wanaotahiriwa kwa mwili, na kwa moyo vilevile hawatapokea **sifa** toka watu, lakini **toka Mungu**.

3:1 Ndani ya mashairi 1-8 ya sura 3 Paulo anakaa kufundisha juu ya hatia ya Wayuda. Hapa mbishi Myuda mmoja anaanza kuuliza mtume:

MBISHI: Kama maneno yote amayo ulisema ndani ya 2:17-29 ni kweli, **Myuda anapita** watu wengine namna gani, na **tohara ina faida gani**?

3:2 PAULO: Wayuda ni wenye mapendeleo mengi. Faida kubwa zaidi ndiyo ya kwamba walipewa **maneno ya**

Mungu. Wayuda walipewa kazi ya kuandika na kulinda Maandiko ya Agano la Kale, lakini wengi wa Wa-israeli hawakuweka roho juu ya neno hili kubwa. Zaidi yao walikosa imani.

3:3 MBISHI: Ndiyo, ni kweli kwamba Wayuda wengine hawakuamini. Kwa sababu hii Mungu hatatimiza ahadi zake? Mungu alichagua Israeli na alifanya maagano nao. **Ukosefu wa imani** wa wengine unaweza kusukuma **Mungu** kuvunja maagano haya?

3:4 PAULO: Sivyo, hata kidogo! Watu wakiuliza kama nani akisema haki, au Mungu, au watu, kumbuka kwamba **Mungu** ni mwenye haki, na **kila mtu** ni **mwongo**. Haya ndiyo masemo ya Daudi katika Zaburi 51:4, “Ujulikane kuwa mwenye haki wakati unaposema, na kuwa safi wakati unapotoa hukumu.” Zambi zetu zinasaidia kuhakikisha tu kweli ya masemo ya Mungu.

3:5 MBISHI: Basi, kama ni hivi, kwa sababu gani Mungu anatuhukumu? Kama **uzalimu wetu** ukisaidia **haki ya Mungu** kungaa na utukufu zaidi, namna gani **Mungu** anaweza kutuhukumu na **gazabu**? (Paulo anaonyesha hapa kwamba anasema namna watu wanavyosema.)

3:6 PAULO: Ulizo namna hii halistahili jibu. Kama ingaliwezekana kwa Mungu kuwa mzalimu kwa neno lo lote, namna gani atawea **kuhukumu ulimwengu**? Lakini sisi sote tunakubali kwamba *atahukumu ulimwengu*.

3:7 MBISHI: Basi zambi yangu ikitukuza Mungu, kama **kweli** yake ikizidi kwa sababu ya **uwongo** wangu, kama Mungu akitumika na gazabu ya mtu kujitkuza mwenyewe, namna gani ananiesabu kuwa **mwenye zambi**?

3:8 Kwa nini isingalikuwa akili njema kusema –

PAULO: Uniruhusu kusema kwanza neno moja: Kuna watu **wengine** wanosema kwamba sisi Wakristo tunasema maneno namna hii, lakini ni masingizio.

MBISHI: Kwa nini isingalikuwa akili njema kusema, “**Tufanye mabaya ili mema yapate kuja?**”

PAULO: Kuna jibu moja tu kwa watu wanaosema maneno namna hii: Wana-stahili kupokea **hukumu** wanayopata.

(Ulizo hili la mwisho linakosa akili, lakini ni neno watu wanaloiliza tena na tena juu ya Habari Njema ya neema ya Mungu. Wanasema: “Kama watu waki-weza kupata wokovu kwa njia ya kuamini Kristo tu, watu wangeendelea kutenda zambi. Neema ya Mungu ikiwa kubwa kupita zambi za watu, kwa ki-pimo mtu anachotenda zambi, neema ya Mungu inakaa kuzidi.” Paulo atajibu ulizo hili ndani ya sura 6.)

3:9 MBISHI: Hivi unasema kwamba **sisi** Wayuda ni **wema kupita** Mataifa wale wenye zambi? Jibu la ulizo hili ni: Sivyo. Wayuda si wazuri kupita watu wengine. Wote ni wenye zambi.

Paulo ameonyesha kwamba wapagano wanapotea; Wayuda na Mataifa ambaa wanajisifu juu ya mwenendo wao wa haki wanapotea; Wayuda wana-potea. Sasa anauliza kwamba *watu wote wanapotea*.

Jibu la ulizo hili ni, “Ndiyo, tume-kwisha kuonyesha kwamba watu **wote pia ni chini ya uwezo wa zambi.**” Wayuda si namna nyingine na Mataifa.

3:10 Neno hili linahakikishwa ndani ya Agano la Kale. Tunaona kwanza ya kwamba wote wanaozaliwa na watu wa dunia ni wenye zambi (3:10-13). Halafu tunaona kwamba zambi imegusa viungo vyote wa mtu (3:13-18). Tunaweza kujumlisha habari hizi na masemo ya Zaburi 14:1, “**Hakuna mmoja anayetenda mema.**”

3:11 “Hakuna mwenye kutafuta Mungu” (Zab. 14:2). Hakuna mwenye zambi angalichagua kutafuta Mungu. Ni Roho Mtakatifu tu anayeamsha hamu kwa Mungu ndani ya roho za watu wengine.

3:12 “Wote wametoka kwa njia,

wote wamekuwa pasipo faida; **hakuna mwenye kufanya mema, hata mmoja**” (Zab 14:3).

3:13 “Koo lao ni **kaburi wazi**; kwa ndimi zao wamedanganya” (Zab. 5:9). “Sumu ya nyoka ni chini ya midomo yao” (Zab. 140:3).

3:14 Vinywa vyao **vimejaa laana** na uchungu” (Zab. 10:7).

3:15 **Miguu yao ina mbio** kumwa-naga damu” (Isa. 59:7).

3:16 “Kuharibu **na taabu** ni katika njia zao” (Isa. 59:7).

3:17 “Na njia ya **salama hawaku-ijua**” (Isa. 59:8).

3:18 “Hawana woga kwa **Mungu** mbele ya macho yao” (Zab. 36:1).

Haya ndiyo maneno Mungu anayo-na ndani ya taifa la wanadamu. Anaona uzalimu (3:10); ujinga na roho ya kujitawala mwenyewe bila kutafuta Mungu (3:11). Anaona vilevile kwamba wameacha njia na kuwa pasipo faida wala wema (3:12). Koo lao linaoza, ulimi wao ni mdanganyifu, midomo yao ina sumu ya nyoka (3:13); vinywa vyao vinajaa matukano (3:14); miguu yao inataka kutenda uuaji (3:15); wanaacha taabu na uharibifu njiani nyuma yao (3:16); hawajui namna gani kupatana na salama (3:17); na hawana heshima kwa Mungu (3:18). Maneno haya yanaonyesha kwamba zambi imegusa wanadamu wote, na kila sehemu ya maisha yao. Ndiyo, zambi hizi zote hazitendwi na kila mtu, lakini kila mtu *angweza kuzi-tenda zote*.

Paulo angaliweza kutaja zambi nyingi nyingine kama angalitaka, kama uzini, ulevi, uchungu, uharibifu, wongo, kutamani, vivi hivi. Hatuhitaji maneno mengine kuhakikisha upotovu wa wanadamu.

3:19 Wakati Mungu alipotolea taifa la Israeli sheria, alitumika na Israeli kama mfano wa wanadamu. Lakini taifa la Israeli lilishindwa, ndio mfano wa ku-shindwa kwa wanadamu wote. Ni sa-

wasawa mwangalizi wa maji anayepima maji nusu ya kisima na kuona kama haya yamechafuwa. Halafu anasema maji yote ya kisima kile yamechafuwa.

Hivi Paulo alieleza kwamba **sheria** inasema na wale **walio chini ya sheria** – ndio watu wa Israeli – kusudi **kila kinywa kifungwe**, cha *Wayuda na Mataifa*, na **ulimwengu wote** uwe chini ya **hukumu ya Mungu**.

3:20 Hakuna mtu anayeweza **kuhe-sabiwa haki** kwa njia ya kushika sheria. Halikuwa kusudi la sheria kuhesabia watu haki, lakini **kuwafahamisha zambi** zao. Kusudi lake halikuwa kuonyesha *njia ya wokovu*, lakini kusaidia watu kujuua kama **zambi ni nini**.

Hatuwezi kujuua kama mstari ukujnjama kama hatuwezi kuusawanisha na mstari wa kunyoloka. Sheria ni kama mstari unaonyoloka. Wakati watu wanapojisawanisha nayo wanafahamu kwamba maisha yao yanapotoka.

Tunaweza kuangalia uso wetu ndani ya kioo, kuona kama ukiwa na uchafu, lakini kazi ya kioo si kunawa uso mchafu.

Sheria ina faida kutufahamisha kwamba sisi ni wenye zambi, lakini haiwezi kutuokoa toka zambi.

D. Msingi na maelezo ya Habari Njema (3:21-31)

3:21 Sasa Paulo atajibu ulizo kubwa la barua kwa Waroma: *Namna gani wenye zambi wanaweza kuhesabiwa haki na Mungu Mtakatifu?*

Anaanza kusema kwamba **haki ya Mungu** imeonyeshwa **pasipo sheria**. Ni kusema kwamba shauri **limefunuliwa** kwa njia yake Mungu anaweza kuokoa wenye zambi, wazalimu, pamoja na kuteenda haki yeye mwenyewe, na bila kulaazimisha watu kushika sheria. Mungu ni mtakatifu, na kwa sababu hii hawezi kukubali zambi, wala kuziachilia na kuziona bure. Ni lazima kwake kuziazibu. Na azabu kwa zambi ni mauti.

Lakini Mungu anapenda mwenye zambi na anataka kumwokoa. Ni neno gumu kabisa. Kwa sababu ya haki ya Mungu ni sharti kwa mwenye zambi kufa, lakini kwa sababu ya mapendo yake Mungu anataka sana kwa mwenye zambi kukaa na furaha kwa milele. Habari Njema inaonyesha namna gani Mungu anaweza kuokoa wenye zambi, bila kuacha kuwa mwenye haki yeye mwenyewe.

Shauri hili **lilishuhudiwa na sheria na manabii**. Lilionyeshwa kwa njia ya mifano ya utaratibu wa kuabudu na zabihu zilizolazimisha damu kumwangika kufanya upatanisho kwa zambi. Na manabii wa Agano la Kale walitabiri wazi juu yake (ona Isa. 51:5, 6, 8; 56:1; Dan. 9:24).

3:22 Shairi 21 lilitujulisha kwamba watu *hawawezi* kupata wokovu huu wa haki kwa njia ya kushika sheria. Sasa mtume anatujulisha namna gani watu wanaweza kuupata – **kwa njia ya imani katika Yesu Kristo**. Imani hii inategemea kabisa Mwokozi wa pekee toka zambi, ndiye tumaini la peke la watu kuweza kufikia mbingu. Msingi wa wokovu ni ufunuo wa Kristo na kazi yake unaoyulikana ndani ya Biblia.

Imani haikosi akili. Inataka ushuhuda wa hakika. Ushuhuda huu unapatikana ndani ya Neno la Mungu lililo pasipo kosa. Imani inapatana na akili ya mtu. Hakuna neno la akili kupita kwa kiumbe kuamini Mwumba wake!

Imani si kazi inayostahilisha mtu kupata wokovu. Mtu hawezi kujivuma kwa sababu ya kuamini Bwana; angalikuwa mjinga kama *asipoamini*. Hatujaribu kujipatia wokovu kwa njia ya imani. Imani ni kupokea na asante wokovu amba Mungu anataka kutoa kama zawadi bila bei.

Halafu Paulo anaendelea kusema kwamba wokovu huu ni **kwa wote na juu ya wote wanaoamini**. Maana ya **kwa wote** ni ya kwamba ni tayari kwa watu wote na unatosha kwa watu wote.

Lakini ni **juu ya** watu wale tu wanaoamini, ndio wale wanaopokea Bwana Yesu na imani. Usamehe ni tayari kwa watu wote, lakini kwa usamehe huu kufanya kazi ndani ya maisha ya mtu, ni lazima aupokee yeche mwenyewe.

Paulo alisema wokovu ni tayari kwa watu wote, Mataifa na Wayuda vile, kwa sababu **hakuna tofauti**. Wayuda hawabarikiwi kupita Mataifa.

3:23 Watu wote wamefanya zambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu, na habari njema ni tayari kwa watu wote vilevile. Kila mtu **amefanya zambi** ndani ya Adamu. Wakati Adamu alipofanya zambi, alitenda kama mju-mbe wa wazao wake wote. Lakini watu si wenye zambi kwa sababu ya tabia yao tu; wao ni wenye *kutenda* zambi vile vile. Wao wenyewe **wanapungukiwa na utukufu wa Mungu**.

MAFUNDISHO JUU YA ZAMBI

Zambi ni wazo, neno, au tendo lisilofikia utakatifu na ukamilifu bora wa Mungu.

Zambi ni uasi (1 Yn. 3:4), ni mtu aki-asi na kushindana na mapenzi ya Mungu. Ni zambi kwa mtu kutenda mabaya, lakini zaidi ya ile, ni kukosa kufanya neno analojua ni jema (Yak. 4:17). Kila tendo lisilotoka katika imani ni zambi (Rom. 14:23). Hivi ni vibaya kwa mtu kutenda lo lote ambalo ana shaka juu yake. Anafanya zambi kama akilitenda bila kuwa na damiri safi.

“Yote yasiyo ya haki ni zambi” (1 Yn. 5:17). Fikiri la upumbavu ni zambi (Mez. 24:9). Zambi inaanza ndani ya nia yetu. Tukikaa kuwaza juu ya neno fulani kwamba labda lingekuwa vizuri kilitenda, nyuma kidogo tunalitenda, na mwisho wake ni mauti. Mara nyingi zambi inaonekana kwanza kama neno la kupendeza, lakini nyuma ya kuitenda inageuka neno la kuchukiza sana.

Mara nyingine Paulo anaonyesha tofauti ya zambi moja, na zambi nyingi.

Zambi nyingi ndizo maneno mabaya tuliyofanya. Zambi (moja) inasema juu ya tabia yetu ovu – namna tulivyo. Ubaya wa namna tulivyo unapita mbali ubaya la neno lo lote tulilotenda. Lakini Kristo alikufa kwa tabia yetu mbovu vilevile, pamoja na matendo yetu maovu. Mungu anasamehe zambi zetu, lakini hatusomi kamwe ndani ya Biblia juu ya Mungu akisamehe zambi yetu. Kwa pahali pa kuisamehe, *anaihukumu* katika mwili (Rom. 8:3).

Zambi ni mbali na makosa vilevile. Ni kosa kufanya kitu kilichokatazwa na sheria yo yote. Kwa mfano, kuiba ni zambi. Ni kosa vilevile wakati kuna agizo kutukataza kuiba. “Pasipo sheria kosa hapana” (Rom. 4:15).

Paulo ameonyesha kwamba watu wote wamefanya zambi na wanakaa kupungukiwa na utukufu wa Mungu. Sasa anaendelea kuonyesha matengenezo ya neno hili. ♦

3:24 Watu wanahesabiwa haki kwa bure kwa neema yake. Habari Njema inatujulisha namna gani Mungu ana-hesabia wenye zambi haki kama zawadi, na kwa njia ya upendeleo wasiostahili kupokea. Basi wakati tunaposema juu ya tendo la ku-hesabia haki, maana yake nini?

Maana ya *ku-hesabia haki* ni kutangaza kuwa haki. Kwa mfano, Mungu anatangaza mwenye zambi kuwa haki wakati mwenye zambi huyu anapoamini Bwana Yesu Kristo. Tunaona maneno haya mbili zaidi na maana hii ndani ya Agano Jipyta.

Lakini mtu anaweza ku-hesabia Mungu kuwa na haki (ona Luka 7:29) kwa njia ya kuamini na kutii neno la Mungu. Ni kusema kwamba anatangaza Mungu kuwa haki ndani ya maneno yote Mungu anayosema na kufanya.

Na mtu anaweza kuji-hesabia mwenyewe haki, maana yake anaweza kuji-weka mwenyewe haki (ona Luka 10:29).

Akifanya hivi anajidanganya mwenyeewe.

Maana ya kuhesabia haki haiko *kufanyiza* mtu kuwa haki. Hatuwezi *kufanyiza* Mungu kuwa haki kwani yeye ni haki. Lakini tunaweza *kutangaza* kwamba yeye ni mwenye haki. Mungu *hafanyizi* mwamini kuwa haki na bila zambi, lakini anamhesabia haki. Mwalimu mmoja, ndiye A.T. Pierson, ali-sema, "Wakati Mungu anapohesabia wenyewe zambi haki, anawaita kuwa wenyewe haki wakati wasipokuwa na haki – hawahesabii zambi wakati walipo na zambi, na anawahesabia haki wakati wasipokuwa na haki."³

Watu wengi wanapenda kusema kwamba kuhesabiwa haki ni kama *nisipofanya zambi kamwe*. Lakini elezo hili halitoshi. Wakati Mungu anapohesabia mwenye zambi aliye mwamini haki, hamwondolei hatia yake tu, lakini anamvalisha na haki yake mwenyeewe, na kumtengeneza kuweza kwenda mbinguni. Wakati mtu anapohesabiwa haki, haandolewi hatia yake tu, lakini zaidi ya ile anakubaliwa na Mungu kama mwenye haki kabisa.

Mungu anaweza kutangaza waovu, wenyewe zambi, kuwa wenyewe haki kwa sababu Bwana Yesu amelipa bei nzima ya deni ya zambi zao kwa njia ya mauti yake na ufufuko wake. Wakati wenyewe zambi wanapopokea Kristo na imani, wanahesabiwa haki.

Wakati Yakobo anapofundisha kwamba mtu anahesabiwa haki kwa matendo yake (Yak. 2:24), maana ya masemo yake haiko kwamba tunaokolewa kwa sababu ya kutenda mema, au kwa njia ya imani pamoa na matendo mema, lakini tunaokolewa kwa namna ya imani inayozaa matendo mema.

Sharti tufahamu kwamba kuhesabia haki ni neno linalofanywa ndani ya nia ya Mungu. Si neno mwamini analoona moyoni mwake. Anajua ni neno lililofanyikana kwa sababu Biblia inasema

kwamba limefanyikana. C.I. Scofield alisesema: "Kuhesabia haki ni tendo la Mungu. Kwa njia ya tendo hili anahesabia haki wote wanaoamini Yesu. Ni neno linalotukia ndani ya nia ya Mungu, si ndani ya tabia ya mwamini."

Ndani ya Waroma 3:24 mtume Paulo anafundisha kwamba **tunahesabiwa haki bure**. Si kitu tunachowenza kupata kwa njia ya kutumika kazi, au kukinunua. Ni kitu Mungu anachotaka sisi kupokea kama zawadi.

Halafu tunajifunza kwamba **tunahesabiwa haki ... kwa neema** ya Mungu. Ni kusema kwamba sisi wenyewe hatustahili kuhesabiwa haki. Ni neno tusilo-jitafutia, wala kulinunua.

Vizuri tueleze kwanza kwamba kuna namna sita za kuhesabiwa haki ndani ya Agano Jipy.

Tunahesabiwa haki kwa njia ya neema, ya imani, ya damu, ya uwezo, ya Mungu, na kwa njia ya kazi; lakini maneno haya yote yanapatana.

Tunahesabiwa haki kwa neema – maana hatustahili kuhesabiwa haki.

Tunahesabiwa haki kwa njia ya imani (Rom. 5:1) – maana yake inatupasa kuamini Bwana Yesu Kristo kwa kuhesabiwa haki.

Tunahesabiwa haki kwa damu (Rom. 5:9) – ndiyo bei Mwokozi aliyolipa ili tuweze kuhesdabiwa haki.

Tunahesabiwa haki kwa uwezo (Rom. 4:24, 25) – ndio uwezo uliofufua Bwana Yesu toka wafu.

Tunahesabiwa haki na Mungu (Rom. 8:33) – ni yeye ambaye anatuhesabu kuwa haki.

Tunahesabiwa haki na kazi (Yak. 2:24) – maana yake si kazi tunayofanya tuweze kujipatia haki, lakini kazi zina-zoonyesha kwamba tumekwisha kuhesabiwa haki.

Tukirudi tena kwa Waroma 3:24, tunasoma kwamba tunahesabiwa haki **kwa njia ya ukombozi ulio katika**

Kristo Yesu. Maana ya ukombozi ni kulipa bei kununua kitu tena, mara ya pili. Bwana Yesu alitununua tena toka utumwa wa zambi. Bei ya ukombozi ilikuwa damu yake ya damani iliyohitajiwa kutosha kwa Mungu mwenye haki na mtakatifu. Hatusomi pahali po pote ndani ya Maandiko Matakatifu kwamba bei hii ililipwa kwa Mungu, au kwa Shetani. Ilikuwa mapatano ya nia yaliyokuwa msingi wa haki yaliyowezesha Mungu kuokoa waovu.

3:25 Mungu aliweka Yesu Kristo awe **upatanisho**. **Upatanisho** ni njia kwa haki kutimizwa, kwa hasira ya Mungu kugeuzwa mbali, na kuwezesha Mungu kutenda na rehema kwa sababu ya zabihu iliyokubaliwa.

Tunasoma mara tatu ndani ya Agano Jipyu juu ya Kristo kama **upatanisho**. Hapa ndani ya Waroma 3:25 tunajifunza ya kwamba wale wanaoamini Kristo wanapokea rehema kwa sababu ya damu aliywawaga. Ndani ya 1 Yoane 2:2 tunasoma juu ya Kristo kama kipatanisho kwa zambi zetu, na kwa zambi za ulimwengu wote. Kazi yake inatosha kuokoa ulimwengu mzima, lakini ina faida kwa watu wale tu ambao wanamwamini. Na mwishoni, ndani ya 1 Yoane 4:10, Mungu alionyesha mapendo yake kwa njia ya kutuma Mwana wake kuwa kipatanisho kwa zambi zetu.

Ombi la mtoza kodi ndani ya Luka 18:13 linaweza kutafsiriwa hivi: "Mungu, uwe kipatanisho kwa mimi mwenye zambi." Alikuwa akiomba Mungu kumrehemu na kutokumlazimisha kulipa azabu kwa hatia yake.

Neno hili **upatanisho** ni ndani ya Waebrania 2:17 vilevile: "Kwa hivyo ilimpasa kufananishwa na ndugu zake katika maneno yote, apate kuwa kuhani mkubwa mwenye rehema na mwanminifu *katika mambo ya* Mungu kusudi afanye upatanisho kwa zambi za watu." Hapa maana ya "afanye upatanisho" ni kuondosha kwa njia ya kulipa azabu.

Katika Agano la Kale neno lenye maana sawa na *upatanisho ni kiti cha rehema*. Kiti cha rehema kilikuwa kifuniko cha sanduku ya agano. Siku ya Upatanisho kuhani mkubwa alinyuniza damu ya nyama ya zabihu juu ya kiti cha rehema. Kwa njia hii makosa ya kuhani mkubwa na ya watu yalilipwa au kufunikwa.

Wakati Kristo alipofanya upatanisho kwa zambi zetu, *hakuzifunika* tu, lakini *aliziondoshaka bista*.

Halafu Paulo anatuambia ndani ya 3:25 ya kwamba **Mungu amekwisha kuweka Kristo awe upatanisho kwa njia ya imani katika damu yake**. Hatuagizwi kuamini damu yake, lakini *Kristo mwenyewe*. Ni Kristo Yesu tu aliyefufiliwa toka mauti na aliye hai anayeweza kuokoa. Yeye ndiye upatanisho. Kwa njia ya **kumwamini** tunapata faida ya **upatanisho. Damu yake** ilikuwa bei yake.

Kazi Kristo aliyyotimiza inatangaza **haki** ya Mungu kuachilia **zambi** zilizofanywa zamani, mbele ya kufa kwa Kristo. Kuanza na Adamu kufika Kristo, Mungu aliokoa watu wale ambao wanaamini maneno ambayo Mungu aliwafunua kwa wakati ule. Kwa mfano, Abrahamu aliamini Mungu; ikamhe-sabiwa kwa haki (Mwa. 15:16). Lakini Mungu aliweza kufanya neno hili na haki? Mwingine asiye na zambi haku-uawa bado kwa pahali pa wenyewe zambi. Damu ya Zabihu mkamilifu ilikuwa hai-yamwangika bado. Kwa ufupi, Kristo hakufa na kulipa deni ya zambi iliyohitajiwa na Mungu mwenye haki. Halafu Mungu aliweza kuokoa wenyewe zambi walioamini namna gani kwa wakati wa Agano la Kale?

Hata Kristo asipokufa bado, Mungu alijua kwamba *atakufa* kwa wakati wa kuja, na aliokoa watu kwa sababu ya kazi Kristo atakayofanya. Watakatifu katika Agano la Kale hawakujua habari za Kalvari, lakini *Mungu alizijua*, na ali-

wahesabia faida ya kazi ya Kristo wakati walipoamini Mungu. Waliokolewa kwa sababu ya bei itakayolipwa kwa wakati wa kuja. Wao walitazama mbele kwa Kalvari; sisi tunatazama nyuma kwa tukio hili kubwa.

Hii ndiyo maana ya maneno ya Paulo ya kwamba upatanisho wa Kristo una-tangaza **haki ya Mungu kwa sababu ya kuachilia zambi zilizofanya za-mani**. Watu wengine wanaanguka wakati wa-napofikiri Paulo alisema juu ya zambi mtu alizofanya mbele ya kuokolewa. Mawazo namna hii yangetufikirisha kwamba kazi ya Kristo ilitosha k w a usamehe wa zambi zile tu, lakini ya kama nyuma ya kuzaliwa tena ni kazi ya mtu mwenyewe kuepuka zambi. Sivyo. Paulo alifundisha juu ya upole wa Mungu aliyeachilia zambi za watu wale waliookolewa mbele ya mauti ya Kristo msalabani. Tungeweza kuwaza kwamba Mungu hakuweka roho juu ya zambi zile. Lakini Paulo hakufikiri hivi. Bwana alijua kwamba Kristo atalipa kwa zambi zile zote. Akijua neno hili aliokoa watu.

Hivi muda wa Agano la Kale ulikuwa wakati wa **uvumilivu** wa Mungu. Aliengoja kwa miaka 4000 au zaidi mbele ya kuhukumu zambi. Halafu kwa wakati wa kutimia alituma Mwana wake kubeba hukumu ya zambi hizi. Wakati Bwana Yesu alipochukua yeye mwenyewe zambi zetu, Mungu alimwangia Mwana wake mpandwa gazabu yake kali sana, gazabu haki, na takatifu.

3:26 Sasa mauti ya Kristo inata-nangaza **haki** ya Mungu. Mungu ni **mwenye haki** kwa sababu aliamuru zambi ziazibiwe na malipo kamili. Na anaweza kuhesabia wazalimu haki bila kukubali zambi zao, na bila kuhatarisha haki yake mwenyewe, kwa sababu Mwingine aliye mkamiliu kabisa amekufa na kufufuliwa.

3:27 Basi wapi tena njia ya kujisifu? Kumefungwa inje. Hakuna njia

kwa mtu kujisifu kwa sababu ya matendo. Ni kwa njia ya sheria ya imani peke yake. Mtu aliyesabwa haki anaweza kusema, “nilifanya zambi zote; lakini Yesu aliniokoa kabisa.” Mtu yule hafikiri kwamba angaliweza kujisaidia mwenyewe, au kujioskwa mwenyewe. Alipokea Kristo tu kuwa Mwokozi wake.

3:28 Hivi hakuna njia kujisifu, na Paulo anasema tena kwamba **mtu ana-hesabwa haki kwa imani pasipo ma-tendo ya sheria**.

3:29 Mungu ni Mungu wa Wayuda tu? Sivyo; yeye ni Mungu wa Mataifa vilevile. Bwana Yesu Kristo hakufa kwa taifa moja tu, lakini kwa ulimwengu mzima wa wenye zambi. Anataka kuleta wokovu bila bei kwa mtu ye yote anayefika kwake, kila Myuda na kila Mtaifa.

3:30 Hakuna Miungu miwili – mmo-ja kwa Wayuda na mwininge kwa Mataifa. Kuna **Mungu mmoja** tu, na kuna njia moja tu kwa watu wa dunia nzima kupata wokovu. Anahesabia **haki waamini waliotahiriwa, na wasiotahi-riwa anawahesabia haki kwa njia ile vilevile**.

3:31 Kuna ulizo moja lingine. Wakati tunaposema watu wanaokolewa kwa njia ya imani, si kwa njia ya kushika sheria, ni kusema kwamba sheria haina faida, na ingetupasa kuiacha? Haina kazi tena kwa sababu ya Habari Njema? **Ha-pana, hata kidogo.** Habari Njema inasi-mamisha **sheria**. Namna gani?

Ni lazima kutii sheria ndani ya kila neno. Ni lazima kwa mtu anayeasi sheria kuazibwa. Azabu yenyewe ni MAUTI. Kama mwenye kuasi sheria akipata azabu hii atapotea kwa milele. Habari Njema inaonyesha kwamba Kristo alikuwa kupokea azabu kwa sheria ambayo watu waliasi. Hakuindea kama kitu bure. Alibeba azabu nzima kwa zambi zile zote. Sasa mtu ye yote aliyeasi sheria anaweza kujua

kwamba Kristo alibeba azabu ambayo ye ye alistahili kupata. Hivi Habari Njema iliyoko kwa imani inasimamia sheria kwa njia ya kuamuru na nguvu kwa maagizo yote ya sheria kutimizwa.

E. Mapatano ya Habari Njema na Agano la Kale (Sura 4)

Ulizo la tano ambalo Paulo anajibu ndilo hili: *Mafundisho ya Habari Njema na ya Agano la Kale yanapatana?* Wayuda wangetaka sana kusikia jibu la ulizo hili. Hivi mtume anaonyesha sasa kwamba Habari Njema katika Agano Jipya na katika Agano la Kale yanapatana kabisa. Tangu zamani watu wamehesabiwa haki kwa njia ya imani.

4:1 Kuhakikisha neno hili Paulo alitaja wawili wa watu wakubwa zaidi wa historia ya Israeli: Abrahamu na Daudi. Mungu alifanya maagano na watu hawa wawili. Mmoja wao aliishi mia za miaka mbele ya kutolewa kwa sheria. Mtu wa pili aliishi miaka mingi nyuma ya kutolewa kwa sheria.

Tuwaze kwanza juu ya **Abrahamu**. Wayuda wote waliweza kumwita mzazi wao. Abrahamu alipata nini **kwa njia ya mwili?** Aliona nini juu ya namna gani mtu anahesabiwa haki?

4:2 Kama Abrahamu angalihesabiwa haki kwa ajili ya matendo, angaliweza kujisifu akifikiri alijipatia haki mbele ya Mungu. Lakini neno hili haliwezekani hata kidodo. Hakuna mtu atakayeweza kujisifu mbele ya Mungu kamwe (Efe. 2:9). Hakuna neno ndani ya Maandiko linaloonyesha kwamba Abrahamu aliweza kujisifu juu ya kuhe-sabiwa haki kwa njia ya matendo yake.

Labda mtu mwingine atauliza, “Hatusomi ndani ya Yak. 2:21 kwamba Abrahamu alihesabiwa haki kwa njia ya matendo?” Ndiyo, tunasoma hivi, lakini maana yake hapa ni namna nyingine. Abrahamu alihesabiwa haki kwa njia ya imani kwa Mwa. 15:6 wakati alipoamini ahadi ya Mungu kwamba atakuwa na

wazao wengi sana kupita hesabu. Halafu nyuma ya miaka makumi tatu alihe-sabiwa haki kwa njia matendo wakati alipoanza kutoa Isaka kuwa zabihu ya kuteketezwa kwa Mungu (Mwa. 22). Tendo hili la kutii agizo la Mungu lilionyesha wazi kwamba alikuwa ame-hesabiwa haki kwa njia ya imani.

4:3 Maandiko yanasema nini juu ya kuhe-sabiwa haki kwa Abrahamu? “Akaamini Bwana; akamhesabia kwa haki” (Mwa. 15:6). Mungu alijifunua kwa Abrahamu na kumwahidi kwamba atakuwa na wazao wengi kupita hesabu. Abrahamu aliamini Bwana, na Mungu alimhesabia **haki**. Ni kusema Abrahamu alihesabiwa haki kwa njia ya imani. Matendo hayakutajwa hata kidogo.

4:4 Shairi hili linatufikisha kwa moja la masemo bora zaidi ndani ya Biblia linaloonyesha tofauti ya matendo na imani ndani ya njia ya wokovu.

Waza juu ya habari hizi: wakati mtu anapofanya kazi ya mshahara na anapopokea mali yake kwa mwisho wa kutumika kwa juma moja, anastahili kupokea **mshahara** huu. Alifanya kazi kuupokea. Hainami mbele ya bwana wake wa kazi na kumshukuru kwa wema wake na kusema hastahili kupokea mali hii. Sivyo! Anaweka mali yake ndani ya mfuko wa vazi lake na anakwenda kwake akifikiri kwamba ame-pokea malipo kwa saa na kazi yake.

Lakini kuhe-sabiwa haki ni namna nyingine kabisa.

4:5 Tunashangaa kusoma kwamba mtu anayehesabiwa haki ndiye asiyefanya kazi. Anakataa kwamba ange-weza kujipokea wokovu kwa njia ya kutumika kazi. Anakana kwamba ana mema au unastahili. Anakubali kwamba kazi zake njema zaidi zote hazitoshi kwa haki ya Mungu.

Lakini mtu anayehesabiwa haki **anamwamini yeye anayehesabia haki** watu *wasioogopa Mungu*. Anaamini neno la Bwana na anamtegemea. Hili si

tendo la kujipatia sifa njema. Mwenye ustahili na sifa njema ni *Yule ambaye anamwamini*.

Ona ya kwamba **anamwamini yeye anayehesabia haki yule asiyegopa Mungu**. Hasemi kwamba alijaribu sana kutenda mema, na kwamba watu wengine ni waovu kupita yeye. Sivyo. Anakaribia Mungu kama mwenye zambi na hatia, na anasihi Mungu kumrehemu.

Mwisho wake nini? **Imani yake inahesabiwa** kwake **kuwa haki**. Kwa sababu anafikia Mungu na imani, si na matendo mema, Mungu anamhesabia **haki**. Kwa sababu ya ustahili wa Mwokozi aliyefufuliwa, Mungu anavika mwenye zambi na **haki**. Kwa njia hii anamstahilisha kukaa mbinguni. Sasa Mungu anampokea na kumwona ndani ya Kristo.

Hivi tunaona kwamba ni waovu wanaohesabiwa haki, si watu wema. Wanahesabiwa haki kwa sababu ya neema – si kama mshahara kwa kazi yao. Wanahesabiwa haki kwa sababu ya imani – si kwa sababu ya kazi njema.

4:6 Halafu Paulo anaendelea na ma-fundisho haya kwa njia ya kusema juu ya **Daudi**. Maneno haya “Kama ... vilevile” kwa mwanzo wa shairi 6 yanaonyesha kwamba habari tulizosoma juu ya maisha ya Abrahamu ni kweli ndani ya maisha ya Daudi vilevile. Daudi, aliyeitwa vilevile “mwimbaji mtamu wa Israeli”, alionyesha heri ya mwenye zambi ambaye Mungu anahe-sabia haki **pasipo matendo**. Daudi hakusema hivi yeye mwenyewe, lakini Paulo alitambua neno hili kwa njia ya Zab. 32:1,2 aliyotaja ndani ya 4:7 na 8:

4:7 Heri waliosamehewa makosa yao, na zambi zao zimefunkwa;

4:8 Heri mtu yule, ambaye Bwana hamhesabii zambi kwake.

Paulo alifahamu nini kwa njia ya

mashairi haya? Aliona kwanza kwamba Daudi hakusema hata neno moja juu ya kufanya kazi; watu wanaohesabia kwa sababu ya neema ya Mungu, si kwa njia ya kazi zao wenyewe. Neno la pili alifahamu ni kama Mungu **hahesabii mtu zambi**, sharti mtu huyu ni mwenye haki yeye mwenyewe, na anaweza kusimama mbele ya Mungu. Na neno la tatu Paulo aliloona ni kwamba Mungu anahesabia wazalimu haki. Daudi alikuwa amezini, na aliua mtu, lakini mashairi haya yanaonyesha kwamba alijuana na utamu wa usamehe mtimilifu wa Mungu.

4:9 Lakini labda Wayuda wengine walikaa kufikiri kwamba watu wachaguliwa wa Mungu tu waliweza kuhe-sabiwa haki, ndio watu waliotahiriwa. Hivi mtume alitaja maisha ya **Abra-hamu** tena kuonyesha kwamba neno hili si kweli. Aliuliza, “Haki hii ni kwa waamini Wayuda tu, au kwa waamini Mataifa vilevile?” Tungeweza kufikiri kwamba ni kwa Wayuda tu kwani mtume alitaja habari za Abrahamu.

4:10 Halafu Paulo aliendelea na kutaja habari ambazo watu wengi wasingalifikiri mbele. Alionyesha kwamba Abrahamu alihesabiwa haki (Mwa. 15:6) mbele ya **kutahiriwa** (Mwa. 17:24). Tungeweza kuuliza kama baba ya taifa la Israeli aliweza kuhe-sabiwa haki mbele ya kutahiriwa, kwa nini watu wengine wasiotahiriwa hawawezi kuhe-sabiwa haki? Abrahamu alihesabiwa haki wakati alipokuwa kama Mtaifa, na neno hili lilifungua njia kwa watu wa Mataifa kuhe-sabiwa haki vilevile bila kutahiriwa.

4:11 Hivi Abrahamu hakuhe-sabiwa haki **kwa sababu alitahiriwa**. Tohara ilikuwa **alamu** ya kuonekana mwilini kwamba alikuwa amehesabiwa haki kwa imani. Ilikuwa alama ya kuonekana tu ya agano la Mungu na watu wa Israeli, lakini ndani ya shairi 11 inaonyesha vilevile haki aliyohe-sabia Abrahamu kwa njia ya imani.

Tohara haikuwa alama tu. Ilikuwa mhuri vilevile – **mhuri wa ile haki ya imani aliyokuwa nayo mbele ya kutahiriwa**. Alama inaonyesha kwamba kitu fulani kinakuwa. Mhuri unahakikisha kwamba kitu hiki ni kitu cha hakika na kweli. Tohara iliyakinisha kwa Abrahamu ya kwamba Mungu alimtendea kama mwenye haki kwa sababu ya imani.

Tohara ilikuwa **mhuri wa haki ya imani** ya Abrahamu. Labda maana yake ndio ya kwamba **imanı** yake ilikuwa haki, au kwamba alipokea haki kwa njia ya **imanı**. Tunafikiri maana ya pili ni maana ya kweli. **Tohara** ilikuwa **mhuri wa haki** iliyoqua sehemu ya **imanı** yake ambayo alipokea kwa njia ya **imanı**.

Kwa sababu Abrahamu alihesabiwa haki mbele ya kutahiriwa, **anaweza kuwa baba** ya watu wengine **wasiotahiriwa** – ndio waamini wa Mataifa. Wanaweza kuhesabiwa haki namna Abrahamu alivyohesabiwa – kwa imani.

Abrahamu aliipta **baba** ya waamini wa Mataifa, lakini hakuwa baba yao kwa njia ya mwili. Waamini hawa waliokuwa watoto wake kwa sababu waliiga imani yake. Hawakuwa watoto wake kwa njia ya kuzaliwa, lakini kwa sababu Abrahamu alikuwa mfano kwao, nao walifuata nyayo za imani yake. Mashairi haya hayafundishi kwamba waamini wa Mataifa wanageuka Israeli ya Mungu. Israeli ya Mungu ndio Wayuda wanopokea Yesu, Masiya, kuwa Bwana na Mwokozi wao.

4:12 Abrahamu alipokea alama ya **tohara** kwa sababu nyingine vilevile. Alitahiriwa ili aweze kuwa **baba ya** Wayuda wale wasiotahiriwa tu, **lakini wa wale** walifuata **imanı** yake vilevile, ndio namna ya **imanı ambayo alikuwa nayo mbele ya kutahiriwa**.

Wazao wa Abrahamu si sawasawa na watoto wa Abrahamu. Yesu alisema na Wafarisayo, “Ninajua ya kama ninyi ni

uzao wa Abrahamu” (Yn. 8:37). Lakini aliendelea na kusema, “Kama mungekuwa watoto wa Abrahamu, mungefanya kazi za Abrahamu” (Yn. 8:39). Hivi kwa Rom. 4:12 Paulo anaonyesha wazi kwamba kutahiriwa mwilini si neno kubwa zaidi. Lazima wale wanaotahiriwa wawe na **imanı** ndani ya Mungu aliye hai vilevile. Israeli ya kweli ndio **wale waliotahiriwa** na kuamini Bwana Yesu Kristo.

Kwa kujumlisha, kulikuwa na wakati Abrahamu alipokuwa na **imanı mbele ya kutahiriwa**, na kwa wakati mwininge alikuwa na imani na alitahiriwa vilevile. Hivi Paulo alitambua kwamba watu wa Mataifa walio waamini, na Wayuda wenye imani vilevile wanaweza kuita Abrahamu baba yao na kujiita wenywewe watoto wake.

4:13 Halafu ilipasa mtume kujibu masemo ya watu wengine kwamba watu walibarikiwa kwa njia ya sheria. Hivi Mataifa wasiokuwa na sheria walilaaniwa (ona Yn. 7:49).

Wakati Mungu alipoahidi **Abrahamu** na **uzao wake** kwamba atakuwa **mriti wa ulimwengu**, hakusema ahadi hii itatimizwa kama wakitii maagizo fulani. (Miaka 430 ilipita mbele ya kutolewa kwa sheria – Gal. 3:17). Ilikuwa **ahadi** ya neema isiyolazimisha watu kutilimiza maneno fulani. Inapasa kupokea ahadi hii kwa **imanı** – imani kwa njia yake tunapokea **haki** ya Mungu kwa wakati wa sasa.

Maana ya semo hili **mriti wa ulimwengu** ni ya kwamba atakuwa baba ya Mataifa na Wayuda wanaoamini vilevile (4:11, 12), ya kwamba atakuwa baba ya mataifa mengi (4:17, 18), si ya taifa la Wayuda tu. Ahadi hii itatimizwa kabisa wakati Bwana Yesu, mzazo wa Abrahamu, atakapotawala juu ya ulimwengu mzima kama Mfalme wa wafalme na Bwana wa wabwana.

4:14 Imani imekuwa bure, na **ahadi inafanyizwa bure** kama watu

wanaotaka kubarikiwa na Mungu, na kuhesabiwa haki, wakiweza kupokea baraka hii kwa njia ya kutii sheria. Imani ni namna nyingine kabisa na sheria: wenye imani *wanaamini*, lakini wenye kushika sheria *wanatenda*. Ahadi inge-kuwa bure kwa sababu hakuna mtu anayeweza kutii maagizo yote ya sheria.

4:15 Sheria inaleta kasirani ya Mungu, si baraka yake. Inahukumu watu wale ambaio hawatii maagizo yake yote saa zote. Hivi kwa sababu hakuna mtu anayeweza kufanya hivi watu wote waliotawaliwa na sheria wanahukumiwa kufa.

Haiwezekani kutawaliwa na sheria bila kulaaniwa.

Lakini **pasipo sheria makosa hanpana**. Maana ya makosa ndiyo kuasi sheria fulani. Paulo hasemi kwamba pahali **sheria** isipokuwa, hakuna *zambi*. Mtu anaweza kufanya neno haya hata kama sheria kukataza tendo hili ikikosa. Lakini tendo hili linageuka kosa wakati linapokatazwa waziwazi.

Wayuda walifikiri walikuwa wame-riti baraka kwa sababu walipewa sheria, lakini waliriti **makosa** tu. Mungu alitoa sheria kuonyesha kwamba zambi ndiyo **makosa**, na kuonyesha ubaya mkubwa wa zambi. Halikuwa kusudi lake kamwe kwa sheria kuwa njia ya wokovu kwa wakosaji wenye zambi!

4:16 Kwa sababu sheria inaleta kasirani ya Mungu na haihesabii watu haki, Mungu alifanya shauri kuokoa watu kwa **neema** kwa njia ya **imani**. Ataleta uzima wa milele kama zawadi kwa wenye zambi wasiostahili, lakini ambaio wanaipokea kwa njia ya imani.

Kwa njia hii ahadi ya uzima ni **imara kwa wazao wote**. Tunataka kutaja maneno mawili sasa – imara, na wote. Kwanza, Mungu alitaka **ahadi** kuwa *imara*. Kama mtu akihesabiwa haki kwa sababu ya kazi zake za kutii sheria, asingaliweza kujua kamwe kama hesabu za

kazi zake njema ingalitosha, au kama alifanya namna ya kazi zilizohitajiwa. Hakuna mtu anayejaribu kuhesabiwa haki kwa njia ya *kutumika kazi* anayeweza kukaa na matumaini na salamu kama kazi zake zilitosha. Lakini wakati Mungu anapotoa wokovu kama zawadi kwa mtu kupokea kwa njia ya kuamini, mtu yule anaweza kujua kabisa kwamba aliokolewa kwa sababu neno la Mungu linasema hivi.

Neno la pili ndilo hili: Mungu anataka ahadi kuwa **imara kwa wazao wote** – si kwa Wayuda tu, walipewa **sheria**, lakini kwa Mataifa **vilevile** walioamini Bwana namna **Abrahamu** alivyoamini. **Abrahamu ni baba yetu sisi sote** – ndio Wayuda na Mataifa **wote** wanaoamini.

4:17 Kwa kuimarisha kwamba Abrahamu ni baba ya waamini wote, Paulo alitaja nusu ya Mwanzo 17:5: “**Nimekuweka baba ya mataifa mengi**.” Mungu alichagua Israeli kuwa watu wake, lakini halikuwa kusudi kwa taifa hili *peke yake* kubarikiwa na neema na rehema yake. Na akili sana mtume alitaja mashairi mengi toka Agano la Kale kuonyesha kwamba tangu zamani Mungu alikusudi kupokea wenye imani, si neno kama wao ni watu wa kabilan gani.

Maneno “**mbele yake aliyeamini**” yanaendelea na maneno ya 4:16: “... Abrahamu: aliye baba yetu sisi sote.” Ni kusema kwamba Abrahamu ni baba yetu sisi sote kwa macho yake (Mungu) Abrahamu aliamini **Mungu anayewapa wafu uzima, na** anayesema juu ya **vitu visivyokuwa** kama vimekuwa. Mashairi yanayofuata yanatusaidia kufahamu habari hizi juu ya Mungu. **Mungu anawapa wafu uzima** – ndio Abrahamu na Sara, maana hata kama walikuwa kwanza hai, hawakuwa na watoto, na kwa sababu ya uzee hawakuweza kuzaa watoto (ona Mwa. 49:19). Mungu anaita **vitu visivyokuwa kama vimekuwa** – ndio wazao wao kupita hesabu ndani ya mataifa mengi (ona 4:18).

4:18 Paulo alikuwa amesema na nguvu kwamba Abrahamu alipokea ahadi hii kwa njia ya imani, si kwa njia ya sheria, kusudi ahadi iwe kwa neema, na kwa wazao wote. Halafu Paulo aliendelea kusema kwamba Abrahamu aliamini Mungu wa ufufuko. Mungu alikuwa ameahidi kwamba wazao wa Abrahamu watakuwa wengi sana, kupita hesabu, kama nyota na mchanga. Hakuna taraja kwa watu wa dunia kwamba ahadi ya neno hili litawezekana, lakini Abrahamu **aliamini kwa taraja** kwamba **atakuwa baba ya mataifa mengi**, ndilo neno Mungu alilohahidi katika Mwa. 15:5: "**Ndivyo utakavyokuwa uzao wako.**"

4:19 Wakati Mungu alipompa Abrahamu ahadi hii mara ya kwanza kwamba atakuwa na wazao wengi, Abrahamu alikuwa na miaka makumi saba tu (Mwa. 12:2-4). Kwa wakati ule ilizewekana kwa Abrahamu kuwa na mtoto, naye alizaa Isimaeli nyuma yake (Mwa. 16:1-11). Lakini ndani ya shairi 19 Paulo alisema juu ya wakati Mungu alipomtolea ahadi hii mara ya pili. Kwa saa ile Abrahamu alikuwa karibu na miaka 100 (Mwa. 17:15-21). Haikuwezekana tena kwa yeye na Sara kuzaa mtoto isipokuwa kwa uwezo wa ajabu wa Mungu. Lakini Mungu alimtolea ahadi mbele kwamba atazaa mwana, na Abrahamu aliamini ahadi ya Mungu.

Yeye asiyekuwa **zaifu katika imani, hakufikiri hali ya mwili wake**, ya kama **umekwisha kufa, na hali ya kufa ya tumbo lake Sara**. Kwa watu wa dunia, tumaini halikuwa kwamba wataweza kuzaa mtoto, lakini Abrahamu alikuwa na imani.

4:20 Hakuona shaka kwa **ahadi** ya Mungu, kama itatimizwa kweli. **Aliamini** ahadi ya Mungu, akijua kwamba Mungu hawesi kusema uwongo. Akiwa mwenye imani ya nguvu, **alimpa Mungu utukufu**, na kumheshimu kuwa mwenye kutimiza ahadi yake isiyowezekana kwa watu wa binadamu.

4:21 Abrahamu *hakujua* namna gani Mungu atatimiza ahadi yake, lakini hakusumbuka juu ya neno hili. Alijua na kutumaini kabisa kwamba Mungu **aliweza** kufanya **maneno yale aliyoahidi**. Ndiyo, Abrahamu alikuwa na imani kubwa. Lakini alitenda na akili vilevile kwa sababu neno la Mungu ni imara kupita vitu vyote ulimwenguni, na haikuwa hatari kwa Abrahamu kulihamini!

4:22 Mungu alipendezwa kukuta mtu ambaye aliamini neno lake na kulitegemea. Neno hili linampendeza kila mara, na kwa sababu hii alihesabia Abrahamu **haki**. Aliweza kusimama sasa na haki mbele ya Mungu, bila zambi na hatia. Alikuwa ameponyeshwa toka hukumu, na alihesabiwa haki na Mungu mtakatifu kwa njia ya imani.

4:23 Habari hizi za namna Abrahamu alihesabiwa haki kwa njia ya imani **hazikuandikwa kwa ajili yake tu**. Ndiyo, ziliandikwa kwa ajili yake, kuhakikisha daima kwamba zambi zake zilisamehewa na alikuwa mkamilifu sasa mbele ya Mungu.

4:24 **Lakini ziliandikwa kwa ajili yetu vilevile**. Tunahesabiwa haki vilevile wakati **tunapoamini** Mungu, **aliyefufua Yesu Bwana wetu toka wafu**. Kuna tofauti moja tu: Abrahamu aliamini kwamba Mungu *atawapa* wafu uzima (maana, mwili wake zaifu, na tumbo la uzazi tasa la Sara). Sisi tunaa mini kwamba Mungu amewapa wafu uzima kwa njia ya kufufua Bwana Yesu Kristo. C.H. MacIntosh aliandika:

Abrahamu aliitwa kuamini ahadi, lakini sisi tunaweza kuamini neno linalokwisha kutimizwa. Abrahamu aliitwa kutazamia neno litakalofanywa; sisi tunaangalia nyuma kwa neno linalokwisha kufanywa, ndilo ukombozi unaokwisha kutimizwa. Neno hili linashuhudiwa na Mwokozi wetu aliyefufuliwa toka wafu, anayetukuzwa na kukaa kwa mkono wa kuume wa mwenye enzi mbinguni.⁴

4:25 Bwana Yesu **alitolewa kwa**

ajili ya makosa yetu, na kufufuliwa ili tuhesabiwe haki. Hakutolewa **kwa ajili ya makosa yetu** tu, lakini ili kuyaondoa. **Alifufuliwa ili tuhesabiwe haki** – maana yake, tumehesabiwa haki. **Kwanza** alitengeneza maneno **ya makosa** yetu. Kisha tunajua hakika kwamba **tunahesabiwa haki** kwa sababu ya ufufuko wa Kristo. Neno hili halinngaliwezekana kama Kristo angalibaki kaburini. Lakini kwa sababu alifufuka tunajua kwamba kazi yake kutupatia wokovu imekwisha, alilipa bei ya zambi zetu, na Mungu anapendezwa sana na kazi ya upatanisho ya Mwokozi.

F. Matunda ya Habari Njema (5:1-11)

Mtume aliendelea na mafundisho yake juu ya kuhesabiwa haki kwa njia ya kuuliza kama *faida ya kuhesabiwa haki ni nini ndani ya maisha ya mwamini?* Anataja baraka kubwa saba kila mwamini alizo nazo. Anazipokea kwa njia ya Kristo. Yeye ndiye Mpata-nishi katikati ya Mungu na watu, na za-wadi zote za Mungu zinatufikia kwa njia yake.

5:1 Baraka kubwa ya kwanza za watu wanaokwisha **kuhesabiwa haki kwa njia ya imani ni salama kwa Mungu kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo.** Hatushindani na Mungu tena. Vita imekwisha. Kwa njia ya kazi ya Kristo maneno yote yaliyo uadui katikati ya nafsi zetu na Mungu ziliondolewa. Hatuko adui za Mungu tena, lakini tumegeuzwa kuwa rafiki zake kwa njia ya ajabu ya neema.

5:2 Tumepata njia vilevile kufikia pahali pa baraka zaidi pa wenyewe kukubaliwa na Mungu. Tunakubaliwa na kupokewa ndani ya Yesu Mpandwa, na tuko karibu na tunapendwa na Mungu Baba kwa kipimo anachopenda Mwana Mpandwa wake mwenyewe. Mungu Baba anatukaribisha kama wana, si kama wageni. **Neema hii**, au ukubali

wetu mbele ya Mungu ni kamilifu, usioweza kubadilika, kama ule wa Kristo mwenyewe, kwa sababu sisi ni ndani yake.

Zaidi ya ile, tunafurahi katika **tumaini la utukufu wa Mungu.** Maana ya neno hili ni ya kwamba tunatazamia na furaha wakati tutakapotazama utukufu wa Mungu, na pamoja na ile sisi wenyewe tutaonyeshwa katika utukufu (ona Yn. 17:22; Kol. 3:4). Hatuwezi kufahamu maana nzima ya tumaini hili tungali hapa duniani, na tutashangaa juu yake kwa milele.

5:3 Baraka ya ine ni tunda la ku-hesabiwa haki: **tunafurahi katika mateso vilevile**, si katika maumivu ya wakati wa sasa tu, lakini kwa sababu ya matunda ya mateso haya kwa wakati wa kuja (ona Ebr. 12:11). Ndiyo, Mkristo anaweza kukaa na furaha hata wakati wa mateso. Neno lililo mbalimbali kabisa na furaha si mateso, lakini ni zambi. Tunda moja la mateso ndani ya maisha ya Mkristo ni **saburi**. Tusingaliweza kuendeleza **saburi** ndani ya maisha yetu bila mateso.

5:4 Paulo anaendelea kueleza kwamba **saburi** inazaa **uvumilivu**. Mungu anapendezwa wakati anapoona kwamba tunavumilia mateso yetu na kumwomba yeye kutimiza makusudi yake kwa njia yao. Ukubali wake unatujaza na tumaini. Tunajua kwamba Mungu anatumika ndani ya maisha yetu na kuongeza uvumilivu wetu. Neno hili linatujaza na **tumaini** ya kwamba yeye aliyeanza kazi njema ndani yetu ataitimiza (Flp. 1:6).

5:5 Tumaini halipatizi haya. Tukiwa na tumaini kwamba tutapata kitu fulani, lakini nyuma tunasikia kwamba hatutakipata kamwe, tumaini letu linapatizwa haya. Lakini tumaini letu la wokovu halitapatizwa haya kamwe. Tunawenza kujuu neno hili namna gani? **Kwa sababu mapendo ya Mungu yamemimiwa ndani ya miyo yetu.** Labda maana ya **mapendo ya Mungu**

ni mapendo yetu kwa Mungu au mapendo yake kwa sisi. Ndani ya shairi hili ni mapendo yake kwa sisi, kwa sababu ndani ya mashairi 6-20 tunasoma juu ya maneno mengine yanayohakikisha kabisaa mapendo ya Mungu kwa sisi. **Roho Mtakatifu tuliyepewa** mara moja wakati tulipoamini, anajaza miyo yetu na mapendo ya milele ya Mungu, nayo yanahakikisha kwa roho zetu kwamba atatufikisha kwetu mbinguni na salama. Wakati unapokwisha kupokea Roho Mtakatifu utafahamu kwamba Mungu anakupenda *wewe*.

5:6 Ndani ya mashairi 6-20 Paulo anaendela kuonyesha kwamba Mungu ambaye alitupenda wakati tulipokuwa adui zake wazalimu, anatulinda hata kupita sasa wakati tulipo mali yake. Neno hili linatufikisha kwa tunda la tano la kuhakikishwa kwetu, ndilo ya kwamba *ndani ya Kristo tunakaa salama kwa milele*. Mtume alieleza kweli hii kwa njia ya kusema juu ya maneno matano yaliyo “zaidi sana”:

“zaidi sana” tunaokolewa toka gazabu (5:9).

“zaidi sana” tunaokolewa kwa uzima nyuma ya ufufuko wake (5:10).

“zaidi ya” zawadi ya neema (Rom. 5:15).

“zaidi ya” utawala wa mwamini katika uzima kwa neema ya kuzidi (Rom. 5:17).

“zaidi ya neema ya kuzidi” (5:20)

Ndani ya mashairi 6, 7, na 8 Paulo alionyesha kwamba **tulikuwa pasipo nguvu** na wenye zambi wakati **Kristo alipotukufia**. Ndani ya mashairi 9 na 10 alionyesha kwamba sasa **tumehesabiwa haki** kwa damu ya Kristo, na tunapatanishwa kwa mauti yake. Anionyesha kwamba bila shaka Mwokozi atatuokoa toka gazabu, na kutulinda kwa uzima wake.

Kwanza tunakumbushwa kwamba tulikuwa zaifu, hatukuweza kujisaidia

wenyewe, **bila nguvu**, na hatukuweza kujiokoa. Lakini kwa saa iliyochaguliwa mbele, Bwana Yesu Kristo alifikia dunia na alikufia watu. Hakukufia watu wema (labda watu wengine wamefikiri hivi, lakini alikufia watu **wasiogopa Mungu**. Hatuna neno lo lote kutustahilisha kwa Mungu, lakini Kristo alitukufia hata hivi.

5:7 Watu wa dunia hawakujuana na tendo la mapendo namna hii mbele. Watu wa dunia wanapenda uzima wao na wasingali kuupoteza kwa mtu mwiningine asiyestahili. Kwa mfano, asingalikufa kwa ajili ya mwuaji, mzini, au mtu wa jeuri. Ndiyo, na roho ya kutokekubali inawezekana kwa mtu **kufa kwa ajili ya mtu wa haki**. na labda hata kwa mtu “**mwema**”, maana mtu anayependa watu wengine.

5:8 Mapendo ya Mungu ni namna nyingine kabisa na mapendo ya watu wa dunia, si mapendo namna ya ulimwengu. Alionyesha **mapendo yake** ya ajabu **kwa sisi** kwa njia ya kutuma Mwana wake mpendwa **kufa kwa ajili yetu wakati tulipokuwa tungali wenye zambi**. Hakuna elezo kwa mapendo ya ajabu namna hii ila kutaka kwa Mungu mwenye enzi. Hakuna neno jema ndani yetu ambayo linastahili mapendo namna hii.

5:9 Sasa hatuhesabiwi kuwa wenye hatia na zambi tena. Kwa sababu ya bei kubwa sana ya **damu** ambayo Mwokozi alimwanga kwa Kalvari Mungu anatuhesabu kuwa wenye haki. Alikuwa amelipa bei kubwa kwa kutuhesabia haki wakati tulipokuwa wenye zambi. Zaidi sana atatuokoa **katika gazabu** kwa Kristo. Nyuma ya kulipa bei kubwa namna hii kutupatanisha naye, atatuacha kupotea nyuma?

Maana ya **katika gazabu** ni “toka gazabu”. Hatutakutana na gazabu ya Mungu tena sasa, na hata milele.

5:10 Tukiwaza tena juu ya namna

tulivyokuwa mbele, na namna tulivyyo sasa, tukumbuke kwamba **wakati tulipokuwa adui tulipatanishwa na Mungu kwa kufa kwa Mwana wake.** Tulikuwa na uadui kwa Bwana wala hatukuhuzunishwa juu ya hali hii, na hatukufikiri kwamba tulihitaji kupatanishwa naye. Fikiri kwanza: tulikuwa **adui za Mungu!**

Lakini mawazo ya Mungu yalikuwa namna nyingine, na alitenda kwa neema safi. Mauti ya Kristo kwa ajili yetu iliondoshia sababu ya uadui wetu na Mungu – maana, zambi zetu. Kwa njia ya kuamini Kristo **tumepatanishwa na Mungu.**

Mungu alilipa bei kubwa sana kwa kutupatanisha naye. Atatuacha kupotea tena? **Tulipatanishwa na Mungu kwa kufa kwa Mwana wake**, ndio mfano wa uzaifu kabisa; zaidi sana atatulinda hata mwisho kwa njia ya maisha ya sasa ya Kristo kwa mkono wa kuume wa Mungu, ndiyo maisha ya uwezo usio na mpaka. Kama **mauti** yake yalikuwa na uwezo mkubwa sana kutuokoa, zaidi sana anaweza kutulinda katika **uzima wake!**

5:11 Na sasa tunafikia tunda la sita la kuhesabiwa haki: **tunafurahi katika Mungu katika Bwana wetu Yesu Kristo.** Hatufurahi ndani ya zawadi zake tu, lakini ndani ya Yule ambaye anatutolea zawadi hizi. Mbele ya kuokolewa tulijifurahisha na maneno ya dunia. Sasa **tunafurahi zaidi** wakati **tunapomkumbuka** yeye, na tunakaa na huzuni tu saa **tunapomsasau.** Nini ilitugeuza hivi? Ni kazi ya **Bwana Yesu Kristo.** Tunapokea furaha hii **kwa yeye** tu, pamoja na baraka zetu nyingine zote.

Tunaona tunda la saba ndani ya maneno haya: **kwa yeye tumepata upatanisho.** Kwa njia ya upatanisho Mungu na watu wanakaa na salama na upatano tena kwa sababu ya zabihu ya Mwokozi msalabani. Zambi ilikuwa imeleta ma-

gawanyiko na uadui katikati ya Mungu na watu. Kwa njia ya kuondosha zambi, iliyokuwa imetenga Mungu na watu, Bwana Yesu alirudisha waamini tena kwa ushirika na Mungu. Si *Mungu* aliyehtaji kupatanishwa. Ni *mtu* anayehitaji kupatanishwa kwa sababu alikuwa adui ya Mungu.

G. Kazi ya Kristo inashinda zambi ya Adamu (5:12-21)

5:12 Baki la sura hii linafunga mwanzo wa sehemu ya kwanza ya barua hii na sura 6-8. Linasema tena juu ya hukumu kwa njia ya Adamu na kuhesabiwa haki kwa njia ya Kristo, na kuonyesha kwamba baraka za kazi ya Kristo ni nyingi kupita taabu na hasara za kazi ya Adamu. Mashairi haya yanapita toka mafundisho juu ya kuhesabiwa haki na kutufikisha kwa mafundisho juu ya utakaso, na toka mattendo ya zambi na kufundisha juu ya tabia ya zambi.

Ndani ya mashairi haya tunaona Adamu kama mkubwa wa watu wote wa muumbo wa zamani. Kristo ni Mkubwa wa watu wote wa muumbo mpya. Wakubwa hawa wawili walitenda kwa ajili ya watu waliokuwa chini yao.

Kwa sababu ya **zambi** ya Adamu, **mauti** yaliingia duniani na yamegeuka mwisho wa watu **duniani.** Ndani ya Adamu watu **wote** walikosa. Kila mtu ametenda zambi vilevile, lakini hapa Paulo alionyesha kwamba Adamu alifanya zambi kama **mkubwa wa uumbo wa kwanza**, na kwa sababu hii wazao wake wote **wametenda zambi** ndani yake.

Labda mtu mwininge anasema alikuwa Hawa aliyetenda zambi ya kwanza. Hakuwa Adamu. Ni kweli, lakini Adamu alipewa *ukuu* kwa sababu aliumbwaa kwanza. Hivi tunamwona hapa akitenda kwa ajili ya wazao wake wote.

Mtume Paulo alisema **kufa kulikuja**

juu ya watu wote, ndiko **kufa** kwa *mwili*, lakini zambi ya Adamu ilileta mauti ya roho vilevile. (Mash. 13 na 14 yanaonyesha kwamba alisema juu ya mauti ya mwili.).

Mashairi haya yanaamsha maulizo ndani ya nia zetu. Ilikuwa haki kwa wazao wa Adamu kuhesabiwa wenye zambi kwa sababu ya zambi ya Adamu? Mungu anahukumu watu kwa sababu walizaliwa wenye zambi, au kwa zambi walizotenda? Watu wakizaliwa na tabia ya zambi, na kama wakitenda zambi kwa sababu walizaliwa wenye zambi, namna gani Mungu anaweza kufanya hivi?

Wenye kujifunza Biblia sana wame-shindana na maulizo haya, na mambo mengi mengine namna hii, na kuyaeleza kwa njia mbalimbali. Lakini kuna mambo mengine yaliyo hakika.

Kwanza, Biblia inafundisha kwamba watu wote ni wenye zambi, kwa njia ya kuzaliwa, na kwa njia ya matendo yao. Kila mtu anayezaliwa na mtu wa dunia anariti zambi ya Adamu, na anachagua kufanya zambi.

Tunajua vilevile kwamba mshahara wa zambi ni mauti – mauti ya mwili, na kutengwa na Mungu kwa milele.

Lakini hakuna mtu anayelazimishwa kuazibiwa kwa zambi kama asipochagua kufanya hivi. Hili ni neno kubwa sana. Mungu alilipa bei kubwa wakati alipotuma Mwana wake kufa kwa pahali pa wenye zambi. Sasa mwenye zambi anaweza kupokea wokovu kama zawadi kwa njia ya kuamini Bwana Yesu Kristo.

Mtu anahukumiwa kwa njia tatu: *Ana tabia ya zambi*, zambi ya Adamu *inahesabiwa* kwake, naye ni *mwenye zambi kwa njia ya matendo yake*. Lakini ye ye ni mwenye hatia kubwa zaidi kama akikataa njia Mungu aliyotayarisha kwa wokovu wake (Yn. 3:18, 19, 36).

Halafu watu wengine wanauliza, “Basi watu wasiosikia Habari Njema kamwe wanahukumiwa vilevile?” Kuna

jibu, kwa sehemu, ndani ya sura 1, lakini tunajua vilevile kwamba Mwamuzi wa dunia nzima atatenda yaliyo haki kila mara (Mwanzo 18:25). Atahukumu watu kwa haki tu. Maneno mengine yanatu-fazaisha sisi kwa sababu ya akili yetu ndogo, lakini maneno haya hayamfazaishi yeye kamwe. Hakuna mtu ataka-yeweza kubishana naye kusema haku-hukumu kwa haki.

5:13 Sasa Paulo ataonyesha ya kuwa zambi ya Adamu iligeuza taifa zima la wanadamu. Alionyesha kwamba **zambi ilikuwa ulimwenguni** katika muda toka Adamu kufika wakati wa kutolewa kwa **sheria** kwa mlima Sinai. Kwa muda ule sheria ya Mungu haikufunuliwa wazi. Mungu alisema na Adamu nini ilimpasa kufanya, na mia za miaka nyuma amri kumi ziliandikwa na kufunua sheria ya Mungu wazi. Kufika wakati ule watu hawakupewa kawaida kwa maisha yao toka Mungu. Ndiyo, watu walifanya *zambi* kwa wakati ule, lakini **makosa** hayakuwa kwa sababu zambi hizi hazikuasi maagizo fulani. **Zambi hai-hesabiwi wakati sheria isipokuwa.**

5:14 Lakini watu wote **walikufa** kwa wakati ule vilevile ila mmoja, ndiye Enoka. Watu hawa hawakufa kwa sababu ya kuasi agizo fulani la Mungu, kama Adamu. Basi walikufa kwa sababu gani? Walikufa ndani ya Adamu. Haifai kwa sisi kufikiri neno hili si haki, lakini tukumbuke kwamba hatusomi juu ya wokovu hapa. Wote wanaokolewa kwa milele. Lakini miili yao ilikufa hata hivi kwa sababu ya zambi ya mkubwa wao, ndiye Adamu. Adamu ni **mfano wake ataka-yeuka**, ndiye Bwana Yesu Kristo. Ndani ya mashairi yatakayofuata Paulo ataonyesha tofauti ya wakubwa hawa wawili. Ataonyesha kwamba ndani ya Kristo wanadamu walipokea baraka nyingi kupita zile baba yao Adamu ali-zopoteza.

5:15 Kwanza anaonyesha kwa njia gani **kosa** la Adamu ni mbalimbali na **zawadi isiyo na bei** ya Kristo. Kwa sababu ya mtu wa kwanza wengi walikufa, ndio wazao wa Adamu. Tunafikiri mauti hii ilikuwa kwa mwili na kwa roho vilevile.

Zawadi ya neema ilizidi kwa watu **wengi zaidi**. Zawadi hii inaonyesha **neema kubwa sana ya Mungu** kwa wenyе zambi. **Iliwezekana kwa njia ya neema ya mtu mmoja**, Yesu Kristo. Ilikuwa neema ya ajabu kwa yeche kufa kwa viumbe vyake waasi. Kwa sababu ya zabihu yake, ndiyo kufa kwake, **watu wengi** wanaweza kupokea zawadi ya uzima wa milele.

Tunasoma mara mbili juu ya watu **wengi** namna mbili ndani ya shairi hili. “**Wengi walikufa**” ndio wote waliokufa kwa sababu ya kosa la Adamu. Halafu kwa mwisho wa shairi hili tunasoma juu ya watu **wengi** tena, lakini ni watu walio geuka viumbe vipyta ndani ya Kristo, mkubwa wa muumbo mpya. Zawadi ya Mungu **ilizidi** kwao, nao ni waamini wa kweli. Rehema kubwa ya Mungu ni tayari kwa watu wote, lakini wale tu wanaoamini Mwokozi wanajitwalia neema yake.

5:16 Zambi ya Adamu ni namna nyingine na **zawadi** ya Kristo kwa njia moyo nyingine. **Zambi ile moja** ya Adamu ililetä hukumu na azabu. **Zawadi** ya Kristo ililetä usamehe kwa makosa **mengi**, si kwa kosa moja tu, na ililetä kuhesabiwa haki. Paulo anaonyesha tofauti ya upotetu mkubwa, ndilo tunda la zambi moja, mwisho wake **azabu**, na wokovu mkubwa toka zambi nyingi, ndio **kuhesabiwa haki**.

5:17 **Kwa njia ya kosa la mtu mmoja, kufa kulitawala** kama mtawala mkali. Lakini kwa njia ya **zawadi ya haki**, ndiyo zawadi ya neema kubwa sana, waamini wote **wanatawala katika uzima kwa yule mmoja**, Yesu Kristo.

Ni neema kubwa sana! Hatuokolewi toka utawala wa mauti tu, lakini tunatawala kama wafalme, tukiishi na furaha sasa duniani, na kwa milele. Tunafahamu baraka hii kubwa? Tunaiishi sasa kama wana wa jamaa ya mfalme wa mbingu, au tunajifurahisha na uchafu wa dunia hii?

5:18 **Kosa** la Adamu lililetä **hukumu** ya azabu kwa watu wote, lakini **tendo la haki** la Kristo lililetä **haki yenye uzima** kwa watu wote. Tendo hili **la haki** halikuwa maisha ya Mwokozi hapa duniani wala kushika kwa sheria, lakini mauti yake kwa msalaba wa Kalvari kwa pahali pa wenyе zambi. Ni tendo hili lililoletea watu **haki yenye uzima** – ndio **uzima** kwa njia ya kuhesabiwa haki – unaotelwa kwa **watu wote**.

Tunasoma juu ya watu **wote** namna mbili ndani ya shairi hili, lakini ni watu namna mbalimbli. Mara ya kwanza ni watu **wote** walio katika Adamu. Mara ya pili ni **wote** walio ndani ya Kristo. Maneno tuliyosoma ndani ya shairi 17 yanatufahamisha neno hili, ndiyo “wao *wanaopokea* neema ya kuzidi na zawadi ya haki” *Ni lazima kwa watu kupokea zawadi hii kwa imani*. Wale tu wanaoamini Bwana wanapokea **haki yenye uzima**.

5:19 **Kwa sababu** Adamu aliasi agizo la Mungu, **watu wengi walilingizwa katika hali ya zambi**. Vivyo hivyo kwa sababu Kristo **alitii Baba**, wengi ambao wanamwamini wameingizwa katika **hali ya haki**. Kwa sababu ya kutii kwake Kristo alikufa msalabani kubeba azabu ya zambi zetu.

Kuna watu wengine wanaoanguka wakati wanapajaribu kutumika na mashairi haya kuhakikisha kwamba mwishoni watu wote wataokolewa. Mashairi haya yanaonyesha wazi kwamba zambi ya Adamu inagusa watu wote walio “ndani yake”, na tendo la

haki la Kristo linasaidia watu wale tu walio “ndani yake.”

5:20 Bila shaka masemo haya ya Paulo yalishitusha Wayuda kwa sababu walifikiri msingi wa dini yao ilikuwa sheria. Sasa waliskia kwamba zambi na wokovu ni ndani ya Adamu na Kristo. Ikiwa hivi, labda waliuliza kama sheria ilitolewa kwa sababu gani. **Sheria ili-ningia, ili zambi iwe kubwa sana.** Sheria haikuzaa zambi, lakini ilifunua zambi kuwa kukosea Mungu. Haikuokoa watu toka zambi zao, lakini ilifunua ubaya wake wote.

Lakini neema ya Mungu ni kubwa kupita zambi zote za watu. **Pahali zambi ilipozidi, neema** ya Mungu **ilizidi zaidi sana** kwa Kalvari!

5:21 Sasa utawala wa zambi ulioleta mauti kwa watu wote umekwisha, na neema inatawala kwa njia ya haki na kuleta uzima kwa njia ya Yesu Kriso, Bwana wetu. Azabu ya kuasi sheria imelipwa, na sasa Mungu mtakatifu anaweza kuleta uzima wa milele kwa wote wanaofika wakiomba wokovu kwa sababu ya ustahili **wa Kristo** aliyebeba azabu hii kwa pahali pao.

Labda mashairi haya yanajibu kwa sehemu ulizo la watu tangu zamani, “Kwa sababu gani Mungu aliacha zambi kuingia duniani?” Mungu ametukuzwa kupita, na watu wamebarikiwa kwa sababu ya zabihu ya Kristo kupita wangalibarikiwa kama zambi isipoingia dunia. Tunabarikiwa ndani ya Kristo kupita tungalibarikiwa ndani ya Adamu kama Adamu asipofanya zambi. Kama Adamu asipofanya zambi kamwe, angalifurahi kukaa kuishi duniani katika Shamba la Edene. Lakini asingalikuwa na tumaini kugeuka mtoto mkombolewa wa Mungu, mriti wa Mungu, au mriti pamoja na Kristo. Hangalipewa ahadi kuwa na kao mbinguni au kuwa pamoja na Kristo na sawasawa naye kwa milele. Tunapoeaka baraka hizi kwa sababu ya kazi ya ukombozi ya **Yesu Kristo Bwana wetu** tu.

H. Maisha matakatifu kwa sababu ya Habari Njema (Sura 6)

Kwa mwisho wa sura 5 Paulo ali-sema kwamba neema ilizidi sana kupita zambi. Masemo haya yanaamsha ulizo lingine ndani ya nia zetu. Ni ulizo kubwa. *Mafundisho ya Habari Njema (ndiyo wokovu kwa sababu ya neema kwa njia ya imani) yanakubali kwa watu kuendelea ndani ya zambi?*

Hapana, hata kidogo. Tunapata jibu kwa ulizo hili ndani ya sura 6-8. Hapa ndani ya sura 6 maneno matatu yanatusaidia kupata jibu kwa ulizo hili kubwa: *kufahamu na kujua* (mash. 3, 6), *kujihesabu* (sh. 11), na *kujitoa* (sh. 13).

Itatusaidia kufahamu mawazo ya Paulo ndani ya sura hii kama tukijua tofauti ya mahali pa mwamini, na kazi yake. Mahali pa mwamini ni ndani ya Kristo. Kazi yake ni namna alivyo, au namna inavyompasa kutenda ndani ya maisha yake ya kila siku. Kwa sababu ya neema ya Mungu mahali yetu ni kamilifu kabisa kwa sababu tuko *ndani ya Kristo*. Ingepasa maisha na matendo yetu kupatana na mahali yetu. Hayapatana katika kila njia kufika tutakapoona Mwokozi mbinguni, lakini ingetupasa kubadilishwa kupita na kupita kufanana na mfano wake wa utukufu.

Paulo anaonyesha kwanza ya kwamba tumefanywa mamoja na Kristo katika kufa na ufufuko, kisha anatuonya kukumbuka kweli hii kubwa ndani ya mwenendo na matendo yetu.

6:1 Myuda mbishi mmoja ana ulizo ambalo anafikiri mtume hataweza kujibu. Kama habari ya neema ya Mungu ikifundisha kwamba kwa njia ya zambi za watu neema ya Mungu ikionekana zaidi, neno hili halifundishi kwamba ingetupasa **sisi kuendelea ndani ya zambi ili neema** izidi sana?

Watu wa wakati wa sasa wanasema hivi: “Unasema watu wanaokolewa kwa neema kwa njia ya imani, bila sheria.

Lakini kama ikipasa mtu kuamini tu kwa kuokolewa, halafu anaweza kuendelea ndani ya maisha ya zambi.” Watu wanaosema hivi hawafikiri kwamba neema inatosha kuamsha hamu ndani ya roho za watu kuishi maisha matakatifu. Wanafikiri inapasa watu kutii sheria vilevile.

Kuna majibu mane ndani ya sura 6 kwa ulizo hili, **Tudumu katika zambi?**

1. *Huwezi*, kwa sababu umeungwa na Kristo (mash. 1-11).

2. *Hulazimishwi* kufanya hivi, kwa sababu neema imevunja utawala wa zambi (mash. 12-14).

3. *Haifai hata kidogo*, kwa sababu ukidumu katika zambi, zambi itageuka bwana wako tena (mash. 15-19).

4. *Usifanye hivi!* Mwisho wa kudumu katika zambi utakuwa uharibifu.

6:2 Jibu la kwanza la Paulo ni kwamba hatuwezi kuendelea kutenda zambi kwa sababu **tulikufia zambi**. Wakati Yesu alipokufa, alikufa kama Mjumbe wetu. Hakutukufia tu, maana *hakufa tu kwa pahali petu*. Alikufa kama *Mjumbe* wetu, maana yake *kama sisi*. Hivi, wakati Yesu alipokufa, sisi tulikuwa. Kwa njia ya kufa kwake alimaliza maneno ya zambi kabisa, na kwa watu wote. Mungu anaona watu wote walio ndani ya Kristo kama watu waliokwisha kufa kwa maneno ya zambi.

Maana ya neno hili haiko kwamba mwamini hana zambi. Ni kusema kumba amefanywa mamoa na Kristo ndani ya mauti yake, na maana yote ya mauti hii.

6:3 Neno kubwa la kwanza ndani ya mafundisho ya Paulo ni **FAHAMU**. Anaanza kusema juu ya ubatizo kuonyeshi kwamba haifai kwa waamini kuendelea kutenda zambi. Lakini Paulo alikuwa akisema juu ya ubatizo gani?

Wakati mtu anapookolewa, **anabatizwa katika Yesu Kristo**. Ni kusema anafanywa mamoa na Kristo katika

kufa kwake na ufufuko wake. Ubatizo huu ni mbali na ubatizo katika (au ubatizo wa) Roho unaotokea kwa saa ile vilevile. Ubatizo katika Roho unaingiza mwamini ndani ya mwili wa Kristo (1 Kor. 12:13); si ubatizo **katika** mauti. Mungu anahesabu mwamini aliyebatizwa **katika Kristo** kuwa mtu aliye-kufa pamoja na Kristo na kufufuliwa pamoja naye.

Wakati Paulo anaposema juu ya ubatizo hapa anafikiri juu ya kufanywa mamoa na Kristo, na vilevile juu ya mfano wake kwa njia ya ubatizo katika maji. Lakini kuanza sasa ni kama anawaza kupita na kupita juu ya ubatizo katika maji, na anakumbusha wasomaji wake kwamba “walizikwa” na “kupandwa pamoja” katika “mfano” wa mauti ya Kristo.

Hatusomi kamwe ndani ya Agano Jipyä juu ya mwamini asiyebatizwa. Linafundisha kwamba watu wanaookolewa wanapokea ubatizo mara moja. Kwa sababu hii Bwana wetu aliweza kusema juu ya imani na ubatizo pamoja: “Anayearmini na kubatizwa ataokolewa” (Mk. 16:16). Si lazima kwa mtu kubatizwa kwa kupata wokovu, lakini ubatizo ni alama mbele ya watu kwamba amegeuka Mkristo.

6:4 **Ubatizo** ndani ya maji ni mfano wa ubatizo katika Kristo. Ni mfano wa mwamini akiingizwa kabisa ndani ya giza la mauti (ndani ya Bwana Yesu), na ni mfano wa mtu mpya ndani ya Kristo akifufuka na kutembea katika uzima mpya. Ni kama mwamini anazika mtu wake wa zamani wakati anapobatizwa. Saa anapoingizwa ndani ya maji, anasema, “Namna nilivyokuwa kama mwana mwenye zambi wa Adamu imekufa kwa msalaba.” Na wakati anapotoka maji, anasema: “Mwenye kuishi sasa si mimi, lakini Kristo ni hai ndani yangu” (ona Gal. 2:20).

Conybeare and Howson wanasema kwamba “kwa kufahamu maana ya

mashairi haya inatupasa kukumbuka kwamba mtu alibatizwa kwa njia ya kuingiza mwili mzima ndani ya maji.”

Halafu mtume anaendelea kusema kwamba kwa sababu ya ufufuko wa Kristo tunaweza **kutembea katika upya wa uzima**. Anasema kwamba **Kristo alifufuka toka wafu kwa njia ya ufufuko wa Baba**. Ni kusema ili-kuwa lazima kwa Mungu, kwa sababu ya utimilifu wake –wema, na mapendo, na haki yake, vivi hivi –kufufua Bwana Yesu. Mwokozi alikuwa bora zaidi, na Mungu, akiwa mwenye sifa njema, hakuweza kumwacha kaburini. Basi Mungu alimfufua kweli, na kwa sababu sisi tunafungamanishwa na Kristo katika ufufuko wake, **sisi tunaweza, na ingetupasa kutembea katika upya wa uzima**.

6:5 Kama tulivyoungwa pamoja na Kristo **katika mfano wa kufa kwake, bila shaka tutakuwa katika mfano wa utukufu wake** vilevile. Maneno haya **katika mfano wa kufa kwake** yanasema juu ya mwamini akifunikwa na maji ya ubatizo. Karibu miaka 2,000 imepita tangu mwamini alipoungwa na Kristo katika kufa kwake, lakini ubatizo ni mfano wa neno hili lililotokea zamani.

Hatingii ndani ya maji tu, lakini tunatoka ndani ya maji vilevile, ndio **mfano wa ufufuko wake**. **Kama tulivyoungwa** pamoja na Kristo **katika mfano wa kufa kwake** (kuingizwa ndani ya maji), vivyo hivyo **tutaungwa naye katika mfano wa ufufuko wake** (kunyanyuliwa toka maji). Hata kama tukisoma **tutaungwa**, neno hili halisemi hapa juu ya wakati wa kuja tu. Hodge anasema:

Shairi hili si juu ya maneno yatakyotokea kwa wakati wa kuja, lakini linaonyesha kwamba neno fulani likitokea, neno lingine litatokea vilevile.⁵

6:6 Kwa njia ya kubatizwa tunakiri kwamba **mtu wetu wa zamani alisuli-**

bishwa pamoja na Kristo. Mtu wetu wa zamani ndio namna tulivyokuwa kama watoto wa Adamu, mbele ya kuzaliwa tena, ndizo desturi zetu zote za zamani, na tamaa yetu. Wakati tulipo-zaliwa tena tuliondoshwa mtu wa zamani, na tulivaa mtu mpya, kama kuondosha mavazi machafu, na kuvaa mavazi bila kipako kwa pahali pao (Kol. 3:9, 10).

Maana ya kusulibishwa kwa **mtu wa zamani** kwa Kalvari ni ya kwamba mwili wa zambi hauna kazi tena. **Mwili wa zambi** si mwili tunaoona na macho. Ni zambi rohoni mwetu inayoonyesha kuwa sultani mzalimu, anayetawala mtu. Mwili huu wa zambi **unaharibiwa** na hauna uwezo kututawala tena, **tusiwe watumwa wa zambi** tena.

6:7 Kwa sababu ye ye aliyekufa amekwisha **kuhesabiwa haki toka zambi**. Kama mfano, waza juu ya mtu aliyehukumiwa kufa kwa sababu aliu polisi. Mara moja nyuma ya kufa kwake **anahesabiwa haki toka zambi**, maana yake amelipa azabu kwa zambi ile. Hatahukumiwa tena juu ya zambi hii.

Sisi tumekufa pamoja na Kristo juu ya msalaba wa Kalvari. Azabu kwa zambi zetu ililipwa, na zaidi ya ile, hatuko watumwa wa zambi tena.

6:8 Mauti yetu **pamoja na Kristo** ni sehemu moja ya kweli kubwa sana. Sehemu ya pili ndiyo ya kwamba **tutaishi pamoja naye vilevile**. Tulikufa kwa zambi; tutaishi kwa haki. Utawala wa zambi juu yetu umeharibiwa, na tunashiriki ndani ya uzima wa ufufuko wa Kristo hata sasa. Na tutashiriki ndani ya uzima wake kwa milele. Jina lake lisifiwe!

6:9 Msingi wa tumaini letu ndio kujua kwamba Kristo amefufuka na hatakufa tena kamwe. **Kufa hakumtawali tena**. Ndiyo, kufa kulintawala kwa siku tatu, mchana na usiku, lakini utawala ule ulipita kwa milele. Kristo hawezি kufa tena kamwe!

6:10 Wakati Bwana Yesu **alipokufa, alikufia zambi mara moja.** Alikufa kwa mishahara yake na azabu yake. Alimaliza maneno haya yote pia na hakuna hitaji kwa kazi hii kufanywa tena kamwe. Sasa **anaishi kwa Mungu.** Ndiyo, aliihi kwa Mungu tangu milele. Lakini sasa anaishi kwa Mungu na udugu mpya, kama Mfufufiliwa, na kwa pahali zambi haiwezi kuingia kamwe.

Mbele ya kuendelea na baki la sura hii, tufikiri tena juu ya mashairi haya kumi ya kwanza. Yanasema zaidi juu ya **utakaso** – namna Mungu anavyotaka sisi kuishi maisha matakatifu. Tuliona mbele kwamba tumekufa pamoja na Kristo na kufufufiliwa pamoja naye tena. Ubatizo ndio mfano wa neno hili. Maisha yetu kama wanaume na wana-wake, wazao wa Adamu, yalikwisha wakati tulipokufa pamoja na Kristo. Hukumu ya Mungu kwa mtu wa zamani haikuwa kumtengeneza tena, lakini kufa kwake. Hukumu hii ilitimizwa wakati tulipokufa pamoja na Kristo. Sasa tumefufufiliwa pamoja na Kristo tuweze kuishi maisha mapya. Hatuko watumwa wa zambi tena, kwani zambi haiwezi kuangusha mfu. Tuko huru sasa kuishi kwa Mungu.

6:11 Paulo ameonyesha *hali* yetu mbele ya Mungu. Anaendelea sasa kuonyesha *namna gani inapasa kweli hii kuonekana* ndani ya maisha yetu. Inatupasa **kujihesabu** kuwa **wafu kwa zambi, lakini walio hai kwa Mungu katika Kristo Yesu Bwana wetu.**

Maana ya kuhesabu ni kukubali kwamba maneno Mungu anayosema ni kweli, na kuishi kama mfu kwa maneno ya zambi, lakini mtu mpya, mtu aliye hai kwa Mungu.

Tunajihesabu kuwa **wafu kwa zambi** wakati tunapajaribiwa kufanya zambi, kama tukitenda kama mfu, maana yake hatufanyi kitu chenyewe. Siku moja mwanamke mmoja alifuata Augustin, Mkristo wa kujulikana ali-

yezini naye mbele. Wakati Augustin alipomwona aligeuka na kutembea mbio kuondoka karibu naye. Mwanamke alilalamika nyuma yake, “Augustin, ni mimi, ni mimi.” Augustin alikwenda hata mbio kupita na alijibu, “Ndiyo, ninajua, lakini si mimi sasa!”⁶ Maana ya jibu lake ndiyo ya kwamba **amekufa kwa zambi** na alikuwa **hai kwa Mungu.** Mfu hazini, wala kusema uwongo, wala kudanganya, kusingizia, wala zambi yo yote nyngine.

Sasa tuko **hai kwa Mungu katika Kristo Yesu.** Ni kusema tunaitwa kuishi maisha ya utakatifu, kuabudu, maombi, utumishi, na kuzaa matunda.

6:12 Tuliona ndani ya 6:6 ya kwamba mtu wetu wa zamani alisulibishwa ili tusiwe watumwa wa zambi tena. **Haifai tuache zambi kutawala ndani ya miili** yetu ya **kufa**, na kutii tamaa zake. Mauti yalimaliza utawala wa zambi kwa Kalvari. Sasa inatupasa kutaka neno hili kufanyikana ndani ya maisha yetu. Mungu tu anaweza kutufanyiza kuwa watakatifu, lakini hatafanya hivi bila ukubali wetu.

6:13 Neno kubwa la tatu ndani ya sura hii ni **KUTOA.** Haifai kwa sisi **kutoa viungo vya miili yetu kutenda zambi**, kama silaha za uzalimu. Sharti tuvitoe **kwa Mungu** aweze kutumika navyo kutenda **yaliyo haki.** Tumefufufiliwa toka mauti na, kama tunavyo-kumbushwa ndani ya 6:4, na inatupasa kutembea katika upya wa uzima.

6:14 Ndani ya shairi hili tunaona sababu nyngine ambayo **haifai kwa zambi kututawala** sisi waamini. Sababu ya kwanza ilikuwa ya kwamba mtu wetu wa zamani alisulibishwa pamoja na Kristo (6:6). Sababu ya pili ni ya kwamba sisi **si chini ya sheria, lakini chini ya neema.**

Ndiyo, zambi inatawala mtu aliye chini ya sheria. Kwa nini? Kwa sababu sheria inamwagiza nini ambayo inampasa kufanya, lakini haimwezeshi

kufanya maneno haya. Na sheria inamsha ndani ya mtu wa zamani hamu kufanya maneno ambayo ilimkataza.

Zambi haina uwezo juu ya mtu aliye chini ya neema. Mwamini amekufa kwa zambi. Amepokea Roho Mtakatifu kukaa ndani yake, naye anampa uwezo kuishi katika utakatifu. Mapendo yake kwa Mwokozi wake yanamsukuma kuishi hivi, si woga ya kwamba atazibiwa.

6:15 Watu wengine wanaogopa **neema** kwa sababu wanafikiri neema inawapa ruhusa kutenda zambi. Paulo anaonyesha wazi kwamba haya ndiyo mafundisho ya uwongo. Tumefunguliwa toka utawala wa sheria, lakini hatuko bila sheria. Kwa sababu ya **neema** tuko huru kutumikia Bwana, si kumkosea.

Katika 6:1 tulisoma, “Tudumu katika zambi?” Hapa ndani ya shairi 15 tunauliza, “**Tufanye zambi** nusu tu?” Jibu kwa maulizo haya mawili ni, “**Hapana, hata kidogo!**” Mungu hawezi kukubali zambi yo yote hata kidogo.

6:16 Ni wazi ya kwamba wakati tunaponyenyeka mtu fulani kama bwana wetu, tunageuka mtumwa wa mtu yule. Hivi, tukijitoa kufanya zambi, tunageuka **watumwa** wa zambi, na mwisho wa maisha yetu ni **kufa** kwa milele. Lakini tukichagua kutii Mungu, tutaishi maisha matakatifu. Watumwa wa zambi wanafungwa na hatia, woga, na taabu, lakini watumishi wa Mungu ni huru kufanya maneno ambayo tabia yao mpya inapenda. Basi kwa nini tutakuwa watumwa kama tukiweza kuwa huru?

6:17 “Mungu ashukuriwe, kwa maana ninyi mulikuwa watumwa wa zambi, mumetii kwa miyo yenu namna ya mafundisho ya Kristo muliyopewa.” Wakristo wa Roma walikuwa wamejitoa kutii na roho moja habari njema ya neema, pamoja na **mafundisho** yote ya Paulo ndani ya barua hii.

6:18 Walipokea kweli ya kwamba

waliwekwa huru toka zambi, na **wali-geuka watumwa wa haki**. Maana ya kuwekwa **huru toka zambi** hapa haiko ya kwamba hawakuwa na tabia ya zambi tena, na ya kwamba hawakute-nda zambi. Maana ya maneno haya ni kwamba hawakutawaliwa na zambi tena.

6:19 Ndani ya shairi 18 mtume alisema juu ya watumwa wa haki, lakini alijua kwamba wenyewe mwendo wa haki hawako watumwa. Kutembea katika haki si utumwa. Paulo alikuwa akijaribu kueleza kweli na masemo watu waliyoweza kufahamu. Watendaji zambi ni watumwa wa zambi, lakini wale wanafunguliwa na Mwana wa Mungu ni huru kabisa (Yn. 8:34, 36).

Paulo alitumika na mifano ya **watumwa** na bwana kusaidia wasomaji wake kufahamu kweli hizi vizuri. Mbele ya kuokolewa kwao waamini walikuwa wametoa miili yao kama **watumwa wa uchafu** na uovu namna yo yote. Sasa iliwapasa kutoa miili hii kama **watumwa wa haki** ili maisha yao yawe matakatifu.

6:20 **Wakati** walipokuwa **watu-mwa wa zambi**, walijuana na uhuru wa namna moja tu, ndio uhuru mbali na **haki**. Ilikuwa taabu kabisa kufungwa na uovu wa kila namna, na kuwa **huru** mbali na haki yote!

6:21 Paulo anawaita (na sisi vile-vile) kuwaza juu ya matunda ya maisha yao mbele ya kuokolewa. **Walikuwa na haya sasa** juu ya matunda ya matendo yale.

Mwisho wa maneno haya ni kufa. A.T. Pierson aliandika ya kwamba kila zambi inatuongoza ndani ya njia ya mauti, na kama tukidumu kuifanya, mwisho na tunda lake ni mauti.

6:22 Hali ya mtu inageuka kabisa wakati anapookolewa. Amewekwa **hu-ru toka** utawala wa **zambi**, naye ni tayari kugeuka mtumwa wa **Mungu**. Anaishi maisha matakatifu sasa, na

mwisho wake utakuwa **uzima wa milele**. Mwamini ana **uzima** wa milele sasa vilevile, lakini shairi hili linasema juu ya uzima tele, pamoja na ufufuko mtukufu wa mwili.

Halafu Paulo anajumlisha tofauti ya maneno haya:

Bwana wawili – **zambi** na **Mungu**.
Njia mbili – **mshahara** na **zawadi**.
Matokeo mawili – **mauti** na **uzima wa milele**.

Ona ya kwamba uzima wa milele ni katika **Kristo Yesu Bwana wetu**. Watu wote walio **ndani ya Kristo** wana **uzima wa milele!**

I. Sheria na mwenendo wa mwamini (Sura 7)

Mtume alijua kwamba watu watauliza kama *sheria ina kazi gani ndani ya maisha ya Mkristo*. Labda Paulo alifikiri zaidi juu ya waamini Wayuda wakati alipojibu ulizo hili, kwa sababu sheria ilitolewa kwa Israeli, lakini jibu hili ni kwa waamini Mataifa vilevile wanaotaka, kwa upumbavu, kutawaliwa na sheria tena, nyuma ya kuhesababiwa haki.

Ndani ya sura 6 tuliona ya kwamba kufa kulimaliza utumwa wa tabia ya zambi ndani ya maisha ya mtoto wa Mungu. Sasa tutaona kwamba kufa kunamaliza utawala wa sheria ndani ya maisha ya watu waliotawaliwa nayo mbele.

7:1 Shairi hili linakumbusha wasomaji habari za 6:14: “Ninyi si chini ya sheria, lakini chini ya neema.” Ingewapasa kujua kwamba wao si chini ya sheria, na ya kuwa **sheria inatawala mtu** angali **yeye** ni hai tu. Paulo alikuwa akisema na watu waliojuana na kawaida ya sheria, na iliwapasa kujua kwamba **sheria** haiagizi mfu neno.

7:2 Paulo alitoa mfano wa neno hili kwa njia ya kuonyesha kwamba kwa **njia ya sheria** ya ndoa **mwanamke** anafungwa kwa mume wake **angali mume anapokuwa hai**. Lakini **wakati** mume

anapokufa, mwanamke **anafunguliwa** toka **sheria** ile.

7:3 Kama mwanamke akioa mtu mwingine wakati mume wake ni hai, anatenda uzini. Lakini **kama** mume wake amekufa, mwanamke ni huru kuoa tena. Si kosa kwa yeye kufanya hivi.

7:4 Ndani ya elezo hili, *wala* mume *wala* mke ni mfano wa sheria. Lin-aonyesha tu ya kwamba mauti yanavunja ufungu wa ndoa. Vivyo hivyo wakati mwamini anapokufa pamoja na Kristo, amri ya sheria juu yake imevunjwa.

Ona ya kwamba Paulo *hasemi* kwamba sheria imekufa. Sheria ingali na kazi ya kusadikisha watu zambi zao. Tukumbuke vilevile ya kwamba wakati Paulo aliposema hapa *tuzae*, alifikiri watu waliokuwa Wayuda mbele ya kuamini Kristo.

Tumefanywa **wafu kwa sheria, kwa njia ya mwili wa Kristo**, ndio **mwili** aliota hata kufa msalabani. Hatufungwi **na sheria** tena; tunafungwa sasa na Kristo mfufulawi. Mauti yamevunja ndoa moja, na tumeputa kuwa mali ya mwingine. Kwa sababu tuko huru **toka sheria** sasa tunaweza **kuzaa matunda kwa Mungu**.

7:5 Tunakumbushwa namna ya **matunda tuliozaa wakati tulipokuwa katika mwili**, lakini si mwili wa mnofu na mifupa. **Katika mwili** hapa ni hali yetu mbele ya Mungu wakati tusipo-okolewa bado. Tulijitegemea wenyewe na maneno tuliyoweza kufanya kupata ukubali mbele ya Mungu. **Katika mwili** ni mbalimbali kabisa na kuwa “katika Kristo.”

Mbele ya kuokolewa tulitawaliwa na **tamaa za zambi zilizowakishwa kwa njia ya sheria**. Sheria haikuzianzisha, lakini kwa njia ya kuzitaja, na halafu kuzikataza, iliamsha hamu kubwa ndani yetu kuzifanya!

Tamaa hizi za zambi zilionekana kwa njia ya viungo vyta miili yetu, na wakati

tunaposhindwa na majaribu, tunazaa matunda ya sumu, mwisho wao **kufa**. Mtume Paulo aliita matunda haya mate-ndo ya mwili: ndio “uasherati, uchafu, uzini, kuabudu sanamu, ulozi, uadui, ugomvi, uwivu, hasira, fitina, faraka, uzushi, husuda, uuaji wa mtu, ulevi, ulafi” (Gal. 5:19-21).

7:6 Moja la maneno mazuri sana yanayotokea wakati tunapookolewa ndilo hili: **tunafunguliwa kwa sheria** kwa sababu tulikufa pamoja na Kristo. Kwa sababu Kristo alikufa kwa pahali petu, sisi **tulikufa** pamoja naye. Kwa njia ya mauti yake alitimiza maagizo yote ya sheria na kulipa azabu yake nzima. Hivi sisi tumefunguliwa kwa sheria na laana yake. Mwokozi wetu anakwisha kulipa yote, na Mungu hataki malipo mara mbili.

Sisi ni huru sasa **tutumikie kwa hali mpya ya Roho, si katika hali ya zmani, ya andiko**. Tunatumikia Bwana kwa sababu tunampenda, si kwa sababu ya woga. Sisi ni huru sasa kumtumikia. Hatulazimishwi kutii kila agizo dogo la utaratibu wa sheria, lakini tunaweza kujitoa na furaha kutukuza Mungu na kuwa na baraka kwa watu wengine.

7:7 Labda maneno haya yanatufikirisha kwamba Paulo aliwaza sheria si nzuri. Alikuwa amesema waamini ni wafu kwa zambi na kwa sheria, na masemo haya yaliweza kufikirisha watu kwamba sheria ni mbaya. Lakini neno hili si kweli hata kidogo.

Ndani ya 7:7-13 aliendelea kuonyeshi kazi kubwa ya sheria ndani ya maisha yake mwenyewe wakati asipozaliwa tena bado. Alisema kwa nguvu kwamba sheria haina zambi, lakini *inafunua zambi ndani ya mtu*. Ni sheria ambayo ilimsadikisha uovu mkubwa wa moyo wake. Wakati alipokaa kusawaniشا matendo yake na yale ya watu wengine, alifikiri mwenendo wake ulikuwa mzuri. Lakini wakati alipofahamu maagizo magumu ya sheria,

alifahamu hatia yake na hakuweza kusema neno.

Amri ya kumi ilimfunulia zambi kupita amri nyingine. Amri ile iliagiza: **Usitamani**. Kutamani ni zambi ya nia. Labda Paulo hakutenda zambi mbaya zaidi za mwili, lakini alifahamu sasa kwamba mawazo yake yalikuwa maovu. Alifahamu kwamba *mawazo* maovu ni zambi vilevile, si *matendo* maovu tu. Labda mwenendo wake ulikuwa bila hatia, lakini mawazo ya moyo wake yalikuwa maovu kabisa.

7:8 Zambi, ikipata nafasi kwa njia ya amri, ilifanya ndani yangu kila namna ya tamaa. Wakati sheria inapokataza kila namna ya **tamaa mbaya**, tabia mbovu ya zambi ya mtu inawakishwa, na mtu anataka kufanya maneno haya maovu hata kupita mbele. Kwa mfano, ni kama sheria inasema, “Usiwaze juu ya matendo ya tamaa za mwili.” Sheria inatukataza kushinda na mawazo juu ya matendo machafu na maovu. Ni huzuni kwa sababu sheria haitutolei uwezo kushinda tamaa hii. Hivi watu waliotawaliwa na sheria wanaingiza hata kupita ndani ya zambi na uovu kwa njia ya mawazo yao. Wanaanza kufahamu ya kwamba watu wakikatazwa kufanya neno fulani, tabia yao ya zamani inataka kufanya zambi hii hata kupita mbele. “Maji ya kuiba ni matamu, na mkate unaokuliwa kwa siri unapendeza” (Mez. 9:17).

Kwa maana **pasipo sheria zambi imekufa**. Tabia yetu ya zambi ni kama imbwa inayolala usingizi. Wakati sheria inapokuja na kukataza neno fulani, imbwa inaanika na kuruka kufanya neno lililokatazwa.

7:9 Mbele ya kusibitishwa na sheria hatia ya kosa, Paulo alikuwa **hai**, maana ni kama tabia yake ya zambi ililala usingizi, na yeze mwenyewe haku-fahamu uovu mkubwa moyoni mwake.

Lakini wakati sheria ilipokuja – na uwezo kabisa kumsibitisha hatia ya kosa

– tabia yake ya zambi iliwaka kabisa. Kwa kipimo alichojaribu kuitii, kwa kipimo kile alishindwa. Tumaini lake kujipatia wokovu yeye mwenyewe **lilikufa**. Alikuwa **mfu** asiyefikiri tena juu ya uzuri wake mwenyewe, na ya kwamba atawenza kuhesabiwa haki kwa njia ya kutii sheria.

7:10 Aliona kwamba **amri inayoleta uzima**, kwake **ilileta kufa**. Lakini alifikiri maana ya **kuleta uzima** ilikuwa nini? Tunafikiri inatukumbusha Walawi 18:5, pahali Mungu alipoagiza, “Mutashika amri zangu na hukumu zangu, mtu akizifanya, ataishi kwa sababu yao; mimi ni BWANA.” Sheria iliahidi kuleta uzima kwa watu ambao waliitii. Kwa mfano, mtoto akitii agizo la mama kukaa mbali na imbwa mkali, atapona na kuishi; mtoto anayeasi agizo lake na anayejaribu kucheza na imbwa mkali, ataumizwa na kuuawa.

7:11 Paulo alisema tena kwamba haifai kushitaki sheria. Ilikuwa zambi iliyopanga moyoni mwake ambayo ilimsukuma kuasi agizo la sheria. Ilikuwa zambi ambayo ilimdanganya kuwaza kwamba neno hili liliokatazwa na amri halikuwa baya sana, lakini litamfurahisha, na ya kwamba hatapata matata kwa sababu ya kuitenda. Ni kama alifikiri Mungu alimwima maneno ambayo yaliweza kumfurahisha na kumsaidia. Hivi ni kama zambi **ilimwua**, maana yake iliua tumaini yake kustahili au kuweza kujipatia wokovu.

7:12 Lakini **torati ni takatifu, na kila amri ni takatifu, na ya haki, na njema**. Haifai tufikiri kamwe kwamba torati ni mbaya kwa njia yo yote. Ni Mungu ambaye alitoa, hivi inaonyesha mapenzi yake kwa watu wake. Lakini ilikuwa zaifu kwa sababu ilitolewa kwa watu wenye zambi. Walihitaji torati kuwajulisha zambi zao, lakini zaidi ya ile walihitaji Mwokozi kuwaokoa toka azabu na uwezo wa zambi.

7:13 Ille iliyo njema ni torati, kama

tulivyoona wazi ndani ya shairi 12. Halafu Paulo anauliza, “Torati **ilikuwa kwangu kufa?**” Maana ya ulizo lake ni kama torati ilimhukumu yeye, (na sisi sote) kufa?” Jibu la ulizo hili ni “Hapani, hata kidogo!” Ni **zambi**. Torati haikuanza zambi, lakini inaonyesha uovu mkubwa wa zambi. “Kwa njia ya sheria zambi *inajulikana*” (Rom. 3:20b). Na zaidi ya ile, tabia ya zambi ya mtu inafanya nini wakati torati takatifu ya Mungu inapoikataza kufanya neno fulani? Tunajua jibu la ulizo hili. Labda tulikuwa na hamu rohoni kufanya neno fulani, lakini saa tunapokatazwa kufanya neno hili, hamu kufanya neno hili inaongezeka sana, hata kuwaka rohoni mweti! Hivi **zambi kwa njia ya amri**, inazidi kuwa **mbaya kabisa**.

Labda msomaji atafikiri ya kwamba maneno Paulo aliyosema hapa hayapatani na masemo yake katika 7:10. Ndani ya shairi lile alisema amri ilileta kufa. Hapa ndani ya shairi 13 alikana kwamba amri ilikuwa kufa kwake. Elezo la masemo haya mawili ndilo hili: Torati peke yake haiwezi kugeuza tabia ya zamani ya mtu kuwa nzuri kupita, na haifanyizi kuilazimisha zambi. Inafunua na kuonyesha zambi tu.

Hili ndilo neno linalotokea: Tabia ya zamani ya mwenye zambi inataka kufanya neno lo lote linalokatazwa. Basi inatumika na torati kuamsha tamaa inayolala ndani ya maisha ya mwenye zambi. Hata mtu akijaribu sana kushinda tamaa hii, inazidi kuongezeka, na mwishoni tumaini la mtu kuweza kuishinda inakwisha kabisa. Hivi zambi inatumika na torati kuua tumaini yake yote kwamba atawenza kushinda zambi yeye mwenye. Anafahamu kupita mbele zambi na uovu mkubwa sana wa tabia yake ya zamani.

7:14 Kufika saa hii Paulo alipasha habari za neno la kuogopesha sana lililotokea ndani ya maisha yake wakati kwa njia ya kazi ya torati ali-

pofahamu hatia kubwa ya zambi yake.

Sasa aligeuka na kusema juu ya maneno yaliyotokea tangu alipozaliwa tena. Alikuta tabia zake mbili ziki-pigana, na ya kwamba hakuwa na uwezo kwa nguvu yake mwenyewe kushinda na kufunguliwa toka uwezo wa zambi rohoni mwake. Alikubali kwamba **torati ni ya roho** – maana ni takatifu, na ilitengenezwa kwa faida ya watu. Lakini anafahamu kwamba yeche ni mtu **wa mwili** kwa sababu hakushinda uwezo wa zambi rohoni mwake. **Aliuzwa chini ya zambi**. Ni kama aliuzwa kuwa mtumwa wa zambi, na zambi ilikuwa bwana wake.

7:15 Sasa mtume anapasha habari za mwamini asiyejuana bado na habari za kusibitishwa pamoja na Kristo katika kufa na ufufuko. Tabia mbili za mtu huyu zinapiga vita. Ni kama mtu anayepanda mlima Sinai akitatifu utakatifu. Hili ndilo elezo la Harry Foster:

Mtu huyu anajaribu kuwa mtakatifu kwa nguvu yake mwenyewe. Anapima sana kutii “amri takatifu na za haki na njema” za Mungu. Anakuta kwamba kwa kipimo anachojaribu kutenda yaliyo mema, hali yake imageuka kuwa mbaya. Anashindwa kabisa, kwa sababu tabia ya zambi ya mtu inakosa uwezo kushinda zambi na kuishi maisha matakatifu.⁷

Ona ya kwamba ndani ya mashairi 9-25 ya sura hii mwandishi aliandika juu yake mwenyewe mara nyingi sana. Alijifikiri mwenyewe tu, akijaribu kushinda kwa nguvu yake, lakini neno hili haliwezekani.

Ni huzuni kuona kwamba zaidi ya waongozi Wakristo wa wakati wa sasa wanajaribu kusaidia watu kwa njia ya kujifikirisha, lakini neno hili linaongeza taabu ya watu hawa. Inapasa watu kujua kwamba walikufa pamoja na Kristo, na wamefufuliwa. Halafu kwa pahali pa

kujaribu kugeuza tabia ya zamani kuwa nzuri wataitupa kwa kaburi la Yesu.

Wakati Paulo alipoandika juu ya tabia zake mbili, alisema, **sijui ninalofanya**. Alifanya maneno asiyotaka kufanya, na kutenda yale aliychukia.

7:16 Kwa njia ya kufanya maneno ambayo alifahamu ni mabaya, alikubali kwamba sheria ni **njema**.

7:17 Na alifahamu kwamba si mtu mpya aliyekuwa ameamini Kristo aliye mwenye hatia, lakini tabia yake mbovu ya zambi iliyo ndani yake. Haifai kwetu kutoa uzuru kwa zambi tunazofanya na kusema ni **zambi** inayokaa ndani yetu. Sisi wenyewe tutahukumiwa juu ya maneno tunayofanya. Paulo anaonyesha tu pahali matendo yetu yanapotoka, si kutoa uzuru kwa matendo haya.

7:18 Haiwezekani kwa sisi kuendelea ndani ya mwenendo mtakatifu kufika saa tunapojifunza, kama Paulo, ya kwamba **ndani yangu, maana, ndani ya mwili wangu, halikai neno njema**. Maana ya **mwili** hapa ni tabia mbaya na mbovu inayokaa ndani ya kila mwamini. Ni msingi wa kila tendo baya la mtu.

Wakati tunapofahamu neno hili, tutaacha kuhuzunishwa wakati tusipokuta mema yo yote ndani ya tabia ya zamani. Na tutaacha kuwaza juu ya hali ya roho yetu wenyewe isiyoweza kuttushindisha. Mkristo mtakatifu mmoja aliyeishi zamani, jina lake Robert Murray McCheyne alisema kila mara tunapoitazama wenyewe, inatupasa kutazama Kristo mara kumi.

Paulo anaendeleda kuonyesha huzuni yake kwa sababu tabia yake ya mwili haikuweza kumsaidia. Ilimshinda kuteenda yaliyo mema ambayo alitaka kufanya. Kwa nini? Kwa sababu alitaka kufanya hivi kwa nguvu yake mwenyewe.

7:19 Hivi tabia zake mbili zinakaa kushindana. Anafahamu kwamba hawezi kufanya **lile jema** analopenda, lakini anafanya **lile baya** asilopenda.

Maneno haya hayapatani hata kidogo.

7:20 Ni kama alisema ndani ya shairi hili kwamba “**Mimi** (tabia yangu ya zamani) **nikifanya** (ndiyo tabia yangu mpya) neno nisilotaka **kufanya**, **si mimi tena ambaye ninalifanya**, **lakini ile zambi inayokaa** ndani **yangu.**” Vizuri tufahamu kwamba Paulo hatoi uzuru kwa matendo yake. Anasema tu kwamba hakufunguliwa toka uwezo wa zambi rohoni mwake, na ya kwamba si tabia mpya ambayo inamsukuma kufanya zambi.

7:21 Anakuta **sheria** nyingine ndani yake, na hata akijaribu sana sana kutenda mema, anashindwa kila mara. Wakati anapotaka kufanya yaliyo haki, anatenda zambi tu.

7:22 Tabia yake mpya inafurahia **sheria ya Mungu.** Anajua sheria ni takatifu, na ya kwamba inafunua mapenzi ya Mungu. Anataka kufanya mapenzi ya Mungu.

7:23 Lakini anakuta vita ndani ya maisha yake, inayopigana na tabia mpya, na kumfanya mfungwa **wa zambi** inayokaa ndani yake.

7:24 Halafu Paulo anaugua na huzuni kubwa. Ni kama maiti imefungwa kwa mgongo wake. **Mwili** huu wa kufa ndio tabia yake ya zamani, ya kuoza. Katika taabu yake kubwa anakiri kwamba hawezi kufanya neno lo lote kujifungua mwenyewe toka utumwa huu wa haya na kuchukiza. Lazima apate kusaidia toka uwezo mwingine.

7:25 Tunaweza kufahamu mashukuru ya shairi 25 kwa njia mbili. Labda maana yake ni “**Ninashukuru Mungu** kwa wokovu wake kwa njia ya Yesu Kristo, Bwana wetu,” au labda Paulo anashukuru Mungu kwa sababu **kwa njia ya Bwana Yesu** yeye si mtu wa taabu tena kama ndani ya shairi 24.

Baki la shairi hili linajumlisha vita ya tabia mbili mbele ya wokovu. **Kwa akili** mpya, ndiyo tabia mpya, mwamini anatumikia **sheria ya Mungu**, **lakini kwa**

mwili (tabia ya zamani) **sheria ya zambi.** Ndani ya sura inayofuata tutapata elezo la njia ya uhuru huu.

J. Roho Mtakatifu ni Uwezo kwa maisha matakatifu (Sura 8)

Sura 8 inaendelea na mafundisho juu ya maisha matakatifu. Ndani ya sura 6 Paulo alijibu ulizo, “Mafundisho ya Habari Njema (ya kwamba tunaweza kupata wokovu kwa njia ya imani peke yake) inaruhusu, na hata kusibitisha watu kuendelea ndani ya zambi?” Ndani ya sura 7 alijibu ulizo ya kama “Habari Njema inaagiza Wakristo kushika sheria ili waweze kuishi maisha matakatifu?” Sasa anaendelea kujibu ulizo hili: **Namma gani Mkristo atawezeshwa kuishi maisha matakatifu?**

Tunaona mara moja ya kwamba sasa hatusomi tena juu ya maneno yetu na majaribu yetu kama ndani ya sura 7. Kuanza sasa Roho Mtakatifu anaonekana zaidi. Neno hili litatusaidia kufahamu mafundisho ya sura hii. Hatuwezi kushinda kwa nguvu yetu wenyewe, lakini kwa njia ya Roho Mtakatifu anayekaa ndani yetu. A. J. Gordon anaonyesha kwamba Roho Mtakatifu anatusaidia kwa njia saba: uhuru katika utumishi wetu kwa Bwana (sh. 2); nguvu kwa utumishi huu (sh. 11); kushinda zambi (sh. 13); maongozi ndani ya utumishi (sh. 14); ushuhuda kwamba tulifanywa wana wa Mungu (sh. 16); kusaidiwa katika utumishi (sh. 26); kusaidiwa katika maombi (sh. 26).

8:1 Kwa mwisho wa sura 7 mtume hakuwa na tumaini la kushinda tena, lakini kwa mwanzo wa sura 8 alitoa kilio cha kushinda kabisa: **Sasa, basi hakuna hukumu ya azabu juu yao walio katika Yesu Kristo!** Tunaweza kufahamu neno hili kwa njia mbili:

Kwanza, Mungu **hatuhukumu** kwa zambi kwa sababu sisi ni ndani ya Kristo. Tulikuwa na hukumu mbele

wakati tulipokuwa ndani ya Adamu. Lakini sasa sisi ni ndani ya Kristo, na tuko huru toka hukumu kama Yeye. Hivi tunaweza kuita na roho ya kushinda:

Ondosha Mwokozi wangu kwanza,
Toka heshima ya Mungu;
Hakikisha kwamba Yesu alifanya
hata zambi moja,
Kisha tangaza kwamba mimi si safi.

– W. N. Tomkins

Au labda maana yake ni kwamba hatuhitaji kujihukumu kwa sababu inatushinda kutii amri zote za sheria kwa nguvu yetu wenye, kama Paulo ali-voonyesha ndani ya sura 7. Shairi 2 linaonyesha kwa sababu gani **hakuna hukumu** ya azabu.

8:2 Sheria ya Roho ya **uzima ulio katika Yesu Kristo imetufanya huru kwa sheria ya zambi na kufa**. Sheria hizi mbili hazipatani. Roho Mtakatifu anampa mwamini uwezo kuishi maisha matakatifu, lakini zambi rohoni mwa mtu inamkokota chini hata mauti. Roho Mtakatifu anatolea mwamini uzima wa ufufuko wa Bwana Yesu, na kumfungua **toka sheria ya zambi na kufa**.

8:3 Ilishinda sheria kuwezesha watu kutii amri zake takatifu, lakini neno hili liliwezekana kwa njia ya neema. Namna gani?

Sheria haikuweza kuzaa maisha matakatifu ndani ya watu kwani **ili-kuwa zaifu sababu ya mwili**, ndiyo tabia ovu ya watu. Walikuwa wenye zambi na walikosa nguvu kuitii. Lakini Mungu alisaidia kwa njia ya **kutuma Mwana wake mwenyewe katika mfano wa mwili ulio wa zambi**. Ona ya kwamba Bwana Yesu hakuja katika mwili wa zambi, lakini **katika “mfano wa” mwili ulio wa zambi**. Hakufanya zambi (1 Pet. 2:22). Hakujua zambi (2 Kor. 5:21), na zambi haikuwa ndani yake (1 Yn. 3:5). Lakini kwa njia ya kuja duniani na mwili wa mtu, alifanana na watu wenye zambi. Akiwa zabihu kwa

zambi, Kristo **alihukumu zambi katika mwili**. Hakufa kwa zambi sisi tunazofanya tu (1 Pet. 3:18) lakini kwa tabia yetu ya zambi. Ni kusema alikuwa kwa sababu *sisi ni wenye zambi*, na kwa *zambi tulizotenda*. Kwa njia ya kufanya hivi, **alihukumu zambi katika mwili**. Hatusomi kamwe kwamba kuna usamehe kwa tabia yetu ya zambi; **ime-hukumiwa**; lakini kuna usamehe kwa zambi *tulizotenda*.

8:4 Sasa **haki ya sheria inatimizwa ndani yetu, tusiotembea kufuata maneno ya mwili, lakini kufuata maneno ya Roho**. Wakati tunapoacha Roho Mtakatifu kutawala maisha yetu, anatuwezesha kupenda Mungu na marani yetu. Hili ndilo agizo la sheria.

Ndani ya mashairi haya mane mtume alijumlisha mafundisho yake ndani ya 5:12 kufika 7:25. Ndani ya 5:12-21 alisema juu ya ujumbe wa kutawala wa Adamu, na wa Kristo. Ndani ya 8:1 alionyesha kwamba hukumu tuliyoriti wakati tulipokuwa ndani ya Adamu imeondoshwa sasa kwa sababu sisi ni ndani ya Kristo. Ndani ya sura 6 na 7 alisema juu ya neno gumu sana, ndilo zambi. Sasa anafanya tangazo la furaha, la kushinda ya kuwa sheria ya Roho ya uzima ndani ya Kristo Yesu imetufungua toka sheria ya zambi na mauti. Ndani ya sura 7 alifundisha juu ya maneno yote ya sheria. Sasa tunajifunza ya kwamba maagizo ya sheria yanatimizwa ndani ya maisha ya mtu anayetawaliwa na Roho.

8:5 **Wale wanaofuata maneno ya mwili** – ndio wasiozaliwa tena – wanafikiri **maneno ya mwili**. Wanafanya maneno ambayo mwili unawsukuma kufanya. Wanishi kupendeza hamu ya tabia ya zambi. Wanabe-mbeleza miili yao ambayo itageuka mavumbi tena nyuma ya miaka michache.

Lakini wale wanaofuata maneno ya Roho – ndio waamini wa kweli –

wanaachana na maneno yale na wanaishi kwa maneno yanayokaa kwa milele. Wanaweka saa na roho zao juu ya neno la Mungu, maombi, kuabudu, na kazi kwa Mungu.

8:6 Maana **nia ya mwili** – ndiyo ya tabia ya zambi – **ni mauti**. Haileti furaha kwa wakati wa sasa, wala kwa wakati wa mwisho. Inaleta mauti tu, kama dawa nyingi kupita kipimo cha sumu.

Lakini **nia ya Roho ni uzima na salama**. Roho ya Mungu ndiye amana ya uzima wa salama na Mungu, uzima wa utulivu.

8:7 Nia ya mwili ni mauti, kwa sababu **ni uadui juu ya Mungu**. Mweenye zambi ni mwasi wa Mungu ndani ya matendo yake. Kusulibishwa kwa Bwana Yesu Kristo kunaonyesha neno hili wazi zaidi. Nia ya mwili **haitii sheria ya Mungu**. Inataka kufanya mapenzi yake mwenyewe, si mapenzi ya Mungu. Inataka kujitawala yenye, si kunye-nyekea utawala wake. Haiwezi kutii sheria ya Mungu. *Haitaki* kuitii, na *inakosa uwezo* kuitii vilevile. Nia ya mwili imekufa kwa maneno ya Mungu.

8:8 Hivi hatushangai kusoma kwamba **wale walio wa mwili hawawezi kupendeza Mungu**. Waza juu ya neno hili! Hakuna neno ambalo msiyeamini anaweza kufanya **kupendeza Mungu** – hakuna kazi njema, hakuna matendo ya dini wala zabihu, - hakuna neno lo lote. Lazima akubali kwanza kwamba yeche ni mwenye zambi, na kuamini Kristo. Nyuma ya kufanya hivi atakubaliwa na Mungu, na ataweza kumpendeza.

8:9 Wakati mtu anapozaliwa tena, yeche **si kwa mwili lakini kwa Roho**. Anaishi ndani ya mahali nyingine. Kama samaki anavyoishi ndani ya maji, na mtu anavyoishi ndani ya hewa, vivyo hivyo mwamini anaishi ndani ya Roho. Haishi ndani ya Roho tu, lakini Roho anaishi ndani yake. Kama Roho ya Kristo asipokaa ndani yake, mtu huyu si

mtu wa Kristo. **Roho ya Kristo** ndiye Roho Mtakatifu.

8:10 Kwa njia ya kazi ya Roho Mtakatifu **Kristo** anakaa **ndani** ya mwamini. Tunakumbuka kwamba miili yetu ilikuwa kwa pahali pa mauti **kwa sababu ya zambi**. Ni ajabu kubwa kufikiri kwamba Bwana wa uzima na utukufu anakaa ndani ya miili hii. Labda mtu mwingine atasema kwamba hawayakufa bado. Ni kweli, lakini mauti inafanya kazi ndani yao hata sasa, na mwishoni watakuwa, isipokuwa Bwana atarudi kwanza.

Roho ni namna nyingine na mwili. **Ni hai kwa sababu ya haki**. Mbele mwili ulikuwa mfu kwa maneno ya Mungu, lakini sasa umepokea uzima kwa njia ya kazi ya haki ya Bwana Yesu Kristo katika mauti na utukufu wake, na kwa sababu tumehesabiwa haki ya Mungu.

8:11 Lakini hatuhitaji kuogopeshwa wakati tunapokumbuka ya kuwa miili yetu itakufa siku nyingine. **Roho Mtakatifu** anakaa ndani ya miili yetu. Neno hili ni kama amana au ahadi ya kwamba **namna alivyofufua Kristo katika wafu**, vivyo hivyo **ataleta uzima** kwa **miili yetu iliyo katika hali ya kufa**. Hili litakuwa tendo la mwisho la ukombozi wetu – wakati miili yetu itakapotukuzwa kuwa kama mwili wa utukufu wa Mwokozi wetu.

8:12 Wakati tunaposawanisha mwili na Roho, tunafahamu kwamba hatuna deni karibu na mwili, na hatulazimishwi kuishi **kufuata mambo ya mwili**. Mwili ule mwovu sana wa zamani haukutusaidia kamwe. Kama Kristo asipotuokoa, **mwili ungalitukokota** chini kabisa katika moto wa kuwaka sana wa Gehena. Kwa nini tutafikiri tuna deni karibu na adui namna hii?

8:13 Wale **wanaoishi kufuata mambo ya mwili watakuwa**, si miili yao ya **sasa tu**, lakini kwa milele. Mtu

anayeishi kufuata mambo ya mwili hakuokolewa. Neno hili linaonyeshwa wazi ndani ya 8:4, 5. Lakini kwa sababu gani Paulo anaandika neno hili kwa Wakristo? Linaonyesha kwamba labda wengine watapotea nyuma? Sivyo, lakini mara nyingi mtume anaongeza maonyo namna hii ndani ya barua zake kusudi wasomaji wake waweweze kupima roho zao. Alijua kwamba katikati ya makusanyiko yote ya Wakristo, labda kuna watu wengine wasiookolewa kwanza.

Baki la shairi hili linaonyesha maneno yaliyo kweli ndani ya maisha ya waamini wa haki. Wakiwezeshwa na **Roho Mtakatifu wanaaua matendo ya mwili.** Wanafurahia uzima wa milele sasa, na watafurahia tele kwa wakati watakapoondokea dunia hii.

8:14 Neno lingine Paulo analosema juu ya waamini wa kweli ni ya kwamba **wanaongozwa na Roho ya Mungu.** Hafikiri hapa juu ya maongozi ya kushangaza ya Mungu ndani ya waamini wa kujulikana. Anasema hapa juu ya neno lililo kweli kwa **wana wote wa Mungu**, ya kwamba wao wote **wanaongozwa na Roho ya Mungu.** Hasemi juu ya kipimo walichojoitoa kunyenyeka maongozi ya Roho ya Mungu, lakini juu ya neno lililotokea saa walipookolewa.

Kuwa wana wa Mungu ni kupokewa ndani ya jamaa ya Mungu, pamoja na mapendeleo na madaraka yote ya wana wa kukomea. Mwamini wa sasa hahitaji kungoja muda fulani mbele ya kupokea uriti wake wa roho; ni uriti wake mara moja wakati anapoamin. Ni vivyo hi-vivo kwa wanaume na wanawake, vijana na watoto wote walio waamini.

8:15 Wale wanaotawaliwa na sheria ni kama watoto, wanaoagizwa kama watumishi, na wanaoogopa kuazibiwa kama wasipotii. Lakini wakati mtu anapozaliwa tena, hazaliwi kuwa mtumishi.

Haingizwi ndani ya nyumba ya Mungu kama mtumwa. Anapokea **roho ya kufanywa wana**, maana anaingizwa ndani ya jamaa ya Mungu kama mwana mzima. Na tabia ya roho anaita Mungu “**Aba Baba.**” **Aba** kwa kiaramaik ni jina la moyo na ukaribu kwa baba, na linatukumbusha ya kwamba Mungu, aliye juu sana, ni karibu sana nasi vilevile.

Labda maneno haya **Roho ya kufanywa wana** yanasesma juu ya Roho Mtakatifu kama yule anayefahamisha na kukumbusha mwamini kwamba ni he-shima kubwa kwaye kuwa mwana. Au labda yanaonyesha kwamba kufanywa mwana ni namna nyingine kabisa na **roho ya utumwa.**

Tunasoma juu ya **kufanywa wana** kwa njia malimbali tatu ndani ya Waroma. Hapa ndani ya shairi 15 ni ya kwamba Roho Mtakatifu anafahamisha mwamini rohoni mwake kwamba amefanywa mwana. Ndani ya Waroma 8:23 tunatazamia wakati mwili wa mwamini utakapokombolewa au kutukuzwa. Ndani ya 8:4 mawazo yetu yanarudishwa nyuma kwa wakati Mungu alipoonyesha Israeli kuwa mwana wake (Kut. 4:22).

Ndani ya Wagalatia 4:5 na Waefeso 1:5, kufanywa wana ni kuweka waamini wote kuwa wana wenye mapendeleo na madaraka ya wana. Kila mwamini ni mtoto wa Mungu, na anazaliwa ndani ya jamaa yenye Mungu aliye Baba. Lakini kila mwamini ni mwana vilevile ndiye na mwenye mapendeleo na madaraka yote ya mwanamume wa kukomea.

Kwa dunia yetu ya sasa maana ya **kufanywa wana** ni kwa mtu kukamata mtoto wa wazazi wengine na kumfanyiza kuwa mwana wake mwenyewe. Ndani ya Agano Jipy, hii si maana yake kamwe.

8:16 Mwamini wa sasa anafahamu rohoni mwake kwamba yeche ni mwana

wa Mungu. **Roho** Mtakatifu anamfahamisha neno hili. **Roho mwenyewe ana-shuhudu pamoja na roho** ya mwamini kwamba yeye ni mtoto wa Mungu. Anafanya hivi zaidi kwa njia ya Neno la Mungu. Wakati Mkristo anaposoma Biblia, Roho Mtakatifu anayakinisha kwake kweli ya kwamba yeye ni mtoto wa Mungu sasa kwa sababu aliamini Mwokozi.

8:17 Wale walio ndani ya jamaa ya Mungu wanabarikiwa na mapendeleo makubwa kupita ufahamu wetu. **Watoto** wote wa Mungu ni **wariti wa Mungu**. Maana yake hapa ni ya kwamba mwishoni mrifi anariti mali ya Baba yake. Yote na vyote vivilivo vyta Baba ni vyetu. Hatukupokea na kufurahi navyo vyote kwa wakati wa sasa, lakini hakuna kitu kinachoweza kuzuiza neno hili kutimizwa kwa wakati wa kuja. **Na** sisi ni **wariti pamoja na Kristo**. Wakati atakaporudi kutawala ulimwengu mzima, sisi tutashiriki naye mali yote ya Baba.

Halafu Paulo aliongeza maneno haya: **kama tukiteswa pamoja naye, ili tutukuzwe pamoja naye vilevile**. Hase-mi mateso haya ni neno la sharti kwa sisi kupata wokovu. Na haandiki juu ya jamii bora kabisa ya washindaji waliovumilia maumivu makubwa sana. Kwa mafikiri yake Wakristo wote wanateswa pamoja, nao wote **wanatukuzwa** pamoja na Kristo. Maana ya **kama** hapa ni “kwa sababu.” Ndiyo, watu hawa-teswi wote kwa kipimo kimoja kwa ajili ya Kristo, na kwa sababu hii watapokea zawabu na **utukufu** kwa kipimo mbalimbali. Lakini watu wote wanaopokea Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wanahe-sabiwa kuwa adui na watu wa dunia, pamoja na kulaumiwa na kupatishwa haya.

8:18 Haya kubwa zaidi tunayoweza kuvumilia duniani kwa ajili ya Kristo itakuwa kama kitu kidogo sana wakati atakapotuheshimu mbele ya majeshi ya

mbingu. Hata maumivu makubwa kupita kipimo ya wale wanaokufa kwa sababu ya imani yao yatakuwa madogo kama kuumizwa na sindano tu wakati Mwokozi atakapoweka taji juu ya vichwa vyao. Ndani ya barua nyingine Paulo anasawanisha taabu yetu ya wakati wa sasa na mateso mapesi yaliyo kwa dakika tu, lakini anasema juu ya utukufu ulio wa milele na unaozidi mwingi sana (2 Kor. 4:17). Wakati ana-poandika juu ya utukufu utakaokuja, ni kama inamshinda kupata maneno mazuri ya kutosha. Kama sisi tungetambua uzuri wa **utukufu** utakaofunuliwa kwetu, tungehesabu **mateso** tunayopata wakati wa sasa kama kitu kidogo sana tu!

8:19 Halafu sasa Paulo anasema juu ya viumbe vyote vikitazamia na hamu sana wakati wa ufunuo wa wana wa Mungu. Neno hili litatokea wakati Bwana Yesu atakapotokea kutawala, na sisi tutarudi pamoja naye.

Sisi ni **wana wa Mungu** hata kwa wakati wa sasa, lakini watu wa dunia hawatutambui wala kutufurahia kuwa wana wa Mungu. Hata hivi watu wa dunia wanatazamia wakati mzuri kupita, lakini muda huu hautakuwa kufika wakati Mfalme atakaporudi pamoja na watakatifu wake wote. “Viumbe vyote vinangojea na hamu kubwa kuona wana wa Mungu wakifunuliwa wazi” (JBP)

8:20 Wakati Adamu alipofanya zambi, zambi hii haikugusa wanadamu tu, lakini viumbe vyote, vivilivo hai, na vile visivyo na uzima. Udongo unalaaniwa. Nyama vingi vinakufa mauti ya ukali. Ndege na nyama, na samaki na nyoka vilevile vinateeswa na ugonjwa. Matunda ya zambi ya mtu wa kwanza yameenea ndani ya ulimwengu mzima.

Hivi, kama Paulo anavyoeleza, **viumbe vyote viliwekwa chini ya ubatili**, mazuizo na machafuko, **si** kwa sababu ya kutaka kwao, lakini kwa

agizo la Mungu, kwa sababu ya kuasi kwa mtu wa kwanza.

Labda maneno mawili ya mwisho ya shairi 20, **katika tumaini**, yanafungana na shairi 21 vilevile: “kwa tumaini kwa kuwa viumbe vitawekwa huru.”

8:21 Habari za zamani za kuumbwa kwa vitu vyote zinatukumbusha hali ya baraka shambani mwa Edeni. Ni huzuni kwa sababu maangamizi makubwa yali-fuata, ndiyo tunda la kuingia kwa zambi duniani. Lakini tangu zamani watu wanakaa na tumaini kwamba siku nyingine dunia itageuka tena kwa hali ya baraka ya mbele. Wanakaa kutazamia wakati **viumbe vitakapofunguliwa toka utumwa wa kuharibika**, na wataingia muda wa uhuru saa tutakapofunuliwa katika utukufu kama **watoto** wa Mungu.

8:22 Tunaishi ndani ya dunia inayojaa na huzuni, na kuugua na mateso. **Viumbe vyote vinaugua**, na kusikia maumivu kama mwanamke saa ya kuzaa mtoto. Tunaona alama ya mauti juu ya kila kitu kilicho hai.

8:23 Waamini hawaepuki maneno haya vilevile. Hata **wakiwa na malimbuko ya Roho**, yanayohakikisha kwamba watawekwa huru toka maumivu haya kwa wakati wa kuja, wanakaa **kuugua** na hamu kungojea kufika kwa siku ile ya utukufu. **Roho** Mtakatifu mwenyewe ni **malimbuko**. Mkono una-ojazwa na mbegu za ngano inayokomea, ni kama arabuni ya mavuno mazima yatakayofuata, vivyo hivyo Roho Mtakatifu ni arabuni au ahadi kwamba tutapokea uriti mzima.

Yeye ni arabuni ya kwamba **tutafanywa wana**, ili kuleta **ukombozi wa mwili** (Efe. 1:14). Tumefanywa wana hata sasa, maana yake tumepekewa ndani ya jamaa ya Mungu kama wana. Lakini neno hili litatimia kabisa wakati tutakapopokea miili yetu ya utukufu, “**ukombozi wa mwili wetu**.” Roho na nafsi zetu zimekwisha kukombolewa, na

miili yetu itakombolewa kwa wakati Kristo atakapokuja kwa Kanisa (1 Tes. 4:13-18).

8:24 **Tuliokolewa** na hali hii ya **taraja**. Hatukupokea faida nzima ya wokovu wetu mara moja wakati tulipokolewa. Tangu mwanzo tulitazamia wakati tutakapofunguliwa toka zambi, mateso, ugonjwa, na mauti. Kama tungalipokea baraka hizi, tusingalikaa kutumaini kuzipokea. Tunatumainia tu maneno ya wakati wa kuja.

8:25 Ahadi ya Mungu ndiyo msingi wa taraja yetu kwamba tutaokolewa toka ukaribu wa zambi na matunda yake mabaya yote. Hivi ni kama tunakwisha kuokolewa hata sasa toka mabaya yale, na **tunangoja na uvumilivu** kutimizwa kwa maneno haya.

8:26 Kama taraja hii ya utukufu inavyotutegemeza, vivyo hivyo **Roho** anatutegemeza ndani ya **enzaifu wetu** vilevile. Mara nyingi tunafazaika juu ya maombi yetu. **Hatuju kuomba** namna inavyotupasa kuomba. Tunaomba na ujinga, na tukijifikiri wenye tu. Lakini Roho Mtakatifu anatufikia tena katika uzaifu wetu, **akituombea kwa kuugua kusikoweza kusemwa**. Ndani ya shairi hili si sisi lakini Roho anayegua, hata kama sisi tunaugua vilevile.

Maneno haya ni siri tusiyoweza kuona, pahali Mkubwa mmoja na nguvu kubwa nyingine ni wenye kufanya kazi kwa ajili yetu. Inatushinda kabisa kufahamu maneno haya, lakini tunasaidiwa rohoni wakati tunapokumbuka kwamba labda mara nyingine kuugua kwetu ni ombi la roho lenye uwezo zaidi.

8:27 Basi Mungu **anayetafuta mioyo ya watu**, anaweza kujua vilevile **nia ya Roho**, hata kama ni kwa njia ya kuugua. Neno kubwa ndilo hili: maombi ya Roho Mtakatifu kwa sisi ni **namna Mungu anavyopenda**. Na kwa sababu hii ni kwa baraka yetu tu. Tutaona ndani

ya shairi 28 kwamba neno hili linaleza maneno mengi ambayo yanatufazaisha.

8:28 Mungu anafanyiza maneno **yote kutumika kazi pamoja kupatia mema wale ambao wanampenda, walioitwa kwa kusudi lake.** Mara nyingine ni nguvu kwa sisi kuamini neno hili. Wakati tunapopata huzuni kubwa ya kuvunja roho, uchungu, mazuizo, na mauti ya wapenzi wetu, tunafazaika kama faida ya maneno haya ni nini. Tunapata jibu kwa ulizo hili ndani ya shairi 29: Kusudi la neno lo lote ambalo Mungu anaruhusu kutupata ni kutufananisha na sura ya Mwana wake. Wakati tunapofahamu neno hili, hatufazaiki tena. Maisha yetu hayataliwi na bahati, lakini na Bwana wetu wa ajabu, Bwana wetu mwenyewe, asiyeweza kuanguka kwa sababu yeze ni mwenye mapendo na hekima kubwa.

8:29 Sasa Paulo anaonyesha makusudi matukufu ya Mungu kwa kuleta wana wengi kwa utukufu.

Kwanza, Mungu **alitujua mbele**, tangu milele. Hakutujua na akili ya kichwa tu. Ndiyo, alijua *kila mtu* atakayezaliwa duniani. Lakini wale ambao alijua tangu zamani, aliwaweka tangu zamani, **wafananishwe na sura ya Mwana** wake. Hivi hakuna neno linaloweza kuzuiza kujuu huku kamwe. Haitoshi kusema tu kwamba Mungu **alijua mbele** wale watakaotubu na kuamini. Ni kwa sababu alijua neno hili, watu wale watatubu na kuamini siku nyingine.

Kuwaza ya kwamba wenyе zambi watageuzwa siku nyingine kwa ajabu ya neema, kufanana na sura ya Kristo, ni moja ya kweli za kutushangaza zaidi za ufunuo wa Mungu. Hatutakuwa na tabia ya Mungu kamwe, wala kuwa na uso utakaofanana na ule wa Kristo, lakini tutakuwa na *sifa njema* kama yeye, bila zambi hata kidogo, na tutakuwa na miili ya utukufu kama mwili wake.

Kwa siku ile ya utukufu **Yeye atakuwa Mzaliwa wa kwanza katikati ya ndugu wengi.** Hatakuwa sawasawa nao, lakini atakuwa Mwenye heshima kubwa zaidi katikati ya ndugu zake waume na wake.

8:30 Kila mtu **aliyewekwa** tangu zamani **anaitwa** vilevile kwa wakati wa sasa. Hasikii tu Habari Njema, lakini anaitikia vilevile. Hivi ni mwito unaozaa tunda. Watu wote wanaitwa, ndio mwito wa Mungu wenyе sababu vilevile, lakini watu wachache tu wanaitika. Huu ndio mwito wa Mungu unozaa tunda, ndilo wokovu.

Wote wanaoitika **wanahesabiwa hakiki** kabisa na Mungu. Wanavalishwa na haki ya Mungu kwa sababu ya ustahili wa Kristo, na kwa sababu hii wanafaa kuwa mbele ya Bwana.

Wale **wanaohesabiwa haki wanatukuzwa** vilevile. Hatutukuzwi kwanza sasa, lakini ni neno litakalotokea bila shaka, hivi Mungu anawenza kusema juu yake kama neno ambalo linakwisha kutokea hata sasa!

Hili ni moja la mashairi katika Agano Jipyа yanayofundisha wazi zaidi ya kwamba mwamini hawezi kupotea kwa milele. Mungu alijua milioni za watu na **kuwaweka**, na kila mmoja wa milioni hawa **ataitwa, kuhesabiwa haki**, na **kutukuzwa**. Hakuna mmoja atakayepotea! (Sawanisha na “wote” katika Yoane 6:37.)

8:31 Wakati tunapowaza juu ya sehemu hizi zote za wokovu wetu, tunafahamu neno moja wazi kabisa! **Mungu akiwa upande wetu**, maana ameweza sisi kwa yeye mwenyewe, **hakuna mtu** anayeweza **kutushinda**.⁸ Kama Mungu Mwenyezi akitusimamia, hakuna uwezo mdogo kupita yeye utawenza kushinda shauri lake.

8:32 Yeye asiyearchilia Mwana wake, lakini alimtoa kwa ajili yetu yote. Masemo ya ajabu kabisa! Hata tukiyasoma tena na tena, tusiache uzuri wao

kuacha kamwe kutujaza na roho ya kuabudu. Wakati dunia hii ya wapotevu ilipohitaji kuokolewa na Mwingine badala yao asiyekuwa na zambi, Mungu mkubwa wa ulimwengu hakuzuiza Yule aliye hazina kubwa zaidi ya roho yake, lakini alimtoa kwa mauti ya haya na hasara kwa ajili yetu.

Na kwa sababu Mungu amekwisha kututolea zawadi hii kubwa zaidi, kuna zawadi nyingine yo yote, iliyo ndogo kupita, ambayo atakataa kututolea? Akikwisha kulipa bei kubwa zaidi, atasita kulipa kwa kitu kidogo kupita? Akikwisha kufanya maneno haya yote kwa wokovu wetu, attuacha kupotea siku nyingine? **Namna gani atakosa kututolea vitu vyote pamoja naye?**

Mackintosh alisema, “Mwenye kuto-kuamini atasema, ‘Namna gani atawenza?’ Mwenye imani atauliza, ‘Nini itamzuiza asifanye hivi?’”

8:33 Maulizo hayakwishi bado. Kuna washitaki wengine wa mwenye zambi aliyekwisha kuhesabiwa haki? Hakuna! Haiwezekani kuwa na **wenye kushitaki** kwani Mungu anakwisha kuhesabia haki wachaguliwa wake.

Inatusaidia kufahamu mashairi 32-34 vizuri kupita kama tukiingiza maneno haya “Hakuna, kwa sababu...” mbele ya kila jibu. Hivi tungesoma, **Ni nani atakayeshitaki wachaguliwa wa Mungu? Hakuna, kwa sababu Mungu anawahesabia haki.**

8:34 Ulizo lingine: Ni nani anayehukumu? *Hakuna, kwa sababu Kristo aliyekufa*, ndiyo zaidi, amefufuka, naye yuko **kwa mkono wa kuume wa Mungu**, akituombea. Kama Bwana Yesu, aliyewekewa hukumu yote, asipohukumu mshitakiwa, hakuna mwiningine anayeweza kuwa na sababu ya haki kumhukumu.

8:35 Sasa tunafikia ulizo kubwa la mwisho: Kuna mtu ye yote anayeweza kutenga wale waliohesabiwa haki, na

mapendo ya Kristo? Wapelelezi wanatafuta pahali pote maneno yanayoweza kuwatenga naye, lakini wana-shindwa. **Mateso** yo yote, au **taabu** chungu sana ya mwili au roho, au **ufukuzo** unaleta maumivu makali, na hata mauti kwa wenye mawazo me-ningine, au **njaa** inayoleta kukonda na kuacha mifupa mitupu tu, au **utupu**, au **hatari** ya mauti, au **upanga** unaoweza kuua, unaweza kuwatenga.

8:36 Kama ingaliwezekana kwa maneno haya kutenga mwamini na mapendo ya Kristo, kama neno hili lingalitokea zamani, kwa sababu mai-sha ya Mkristo ni mauti hata wakati alipo kwanza na uzima. Haya yalikuwa mawazo ya mwandishi wa zaburi wakati aliposema, **tunauawa mchana wote**, na tunahesabiwa kuwa **kondoo za kuchinjwa** (Zab. 44:22).

8:37 Maneno haya magumu haya-tutengi hata kidogo na mapendo ya Kristo, lakini yanatukokota karibu kupita naye. Sisi si **wenye kushinda** tu, lakini **wenye kushinda zaidi**. Hatushindi tu ndani ya vita hii, lakini kwa njia ya kushinda, tunaleta utukufu kwa Mungu, baraka kwa watu, na mema kwa sisi wenyeewe. Tunageuze adui zetu kuwa watumwa.

Lakini maneno haya hayafanyikani kwa njia ya nguvu yetu wenyeewe, **lakini kwa njia ya mwenye kutupenda**. Uwezo wa Kristo tu unaweza kuleta utamu toka uchungu, nguvu toka uzaifu, kushinda toka msiba, na baraka toka huzuni kubwa ya kuvunja moyo.

8:38 Mtume anakaa kutafuta ndani ya ulimwengu mzima kama kuna neno lo lote ambalo linaweza kututenga na mapendo ya Mungu, lakini hakuna. Wala **mauti**, wala **uzima**, wala **malaika**, wala **mamlaka**, wala **wenye uwezo**, wala **maneno ya sasa**, wala **maneno yatakayokuja** yanayoamsha woga ndani ya roho zetu,

8:39 wala **yaliyo juu**, wala **yaliyo**

chini, kama vile maneno ya siri. Paulo hakutaka kukosa kutaja kitu cho chote ambacho kingewenza kututenga na mapendo ya Mungu, hivi aliongeza kusema: **wala kiumbe cho chote kingine**. Alikuwa ametafuta sana, lakini ilimshinda kupata kitu cho chote kinachowenza **kututenga na mapendo ya Mungu yaliyo ndani ya Kristo Yesu Bwana wetu**.

Hatushangai kwa sababu watu waliouawa kwa sababu ya imani yao walikufa wakiimba mashairi haya ya kushinda, na waamini waliokuwa wakiteswa sana kwa sababu ya imani yao walikaa kutolea Mungu sifa kubwa!

2. HABARI NJEMA NA ISRAELI (Sura 9–11)

A. Israeli kwa wakati wa zamani (Sura 9)

Ndani ya sura 9-11 Paulo anajibu Myuda asiyekubali mafundisho haya ya Paulo, na anayeuliza: *Kama Habari Njema ikiahidi wokovu kwa Mataifa pamoja na Wayuda, Mungu amevunja ahadi zake kwa watu wake wa dunia, ndio Wayuda?* Jibu la Paulo juu ya Israeli kwa wakati wa zamani ni ndani ya sura 9, juu ya Israeli kwa wakati wa sasa ni ndani ya sura 10, na juu ya Israeli kwa wakati wa kuja ni ndani ya sura 11.

Ndani ya sura hizi tatu kuna mafundisho makubwa juu ya enzi ya Mungu, na kazi yenye madaraka mengi ya watu. Waroma 9 ni moja ya sura zenye mafundisho juu ya mchaguo wa enzi wa Mungu. Ndani ya sura 10 tunaona kweli kubwa nyingine, ndiyo madaraka ya mtu.

MAFUNDISHO JUU YA ENZI YA MUNGU NA MADARAKA YA WATU

Wakati tunaposema Mungu ni mwenye enzi, ni kusema ya kwamba anatawala ulimwengu, na anafanya

maneno yo yote anayotaka. Lakini tunajua ya kwamba hatafanya kitu kilicho kibaya kamwe, wala neno lisilo haki. Hivi wakati tunaposema kwamba Mungu ni mwenye enzi, ni kukubali kwaye kuwa Mungu. Haifai tuogope kweli hii au kutoa uzuru juu yake. Ni kweli nzuri muno na inatusukuma kuabudu.

Mungu mwenye enzi amechagua watu fulani kuwa watu wake. Lakini pamoja na ile Biblia inafundisha kwamba mchaguo wa Mungu unafundisha madaraka ya watu. Ni kweli ya kwamba Mungu anachagua watu kupokea wokovu, lakini ni lazima kwa mtu kuchagua wokovu ye ye mwenye. Maneno haya, “Wote amba Baba ananipa watakuja kwangu” yanaonyesha kusudi la Mungu, “naye anayekuja kwangu sitamtupa inje kabisa” (Yn. 6:37). Tunafurahi, kwa sababu Mungu alituchagua sisi waamini ndani ya Kristo, mbele ya kuwekwa misingi ya ulimwengu (Efe. 1:4). Lakini tunaamini vilevile ya kwamba ye ye anayetaka anaweza kutwaa maji ya uzima bure (Ufu. 22:17). Mhubiri D. L. Moody alieleza kweli hizi hivi: Wakati tunapokaribia mlango wa wokovu, tunaona maandiko upande wa juu yanayosema, “Mtu ye yote anayetaka kuja aje.” Halafu wakati tunapo-ingia mlango, tunaangalia nyuma na kusoma, “Wachaguliwa kwa kujua kwa Mungu tangu zamani” kwa upande wa juu wa mlango.

Kweli hii ya uchaguzi wa Mwenyezi Mungu ni kwa jamaa ya wale wanaoamini tu, ndio wale wanaokwisha kuingia.

Namna gani Mungu anaweza kuchagua watu fulani kuwa watu wake, na vilevile kuita watu wote pahali pote kupata wokovu? Namna gani tunaweza kupatanisha kweli hizi mbili? Hatuwezi. Kwa nia zetu za umtu zinashindana. Lakini Biblia inafundisha kweli hizi

mbili, hivi ingetupasa kuziamini, na kukumbuka kwamba mashaka haya ni tunda la nia zetu sisi watu, si katika nia ya Mungu.

Watu wengine wamejaribu kupatanisha uchaguzi wa Mungu na madaraka ya watu kwa njia ya kusema Mungu alijua mbele nani atakayeamin Mwokozi, na ya kwamba ni watu hawa amba alichagua kuokolewa. Wanasi-mamisha mawazo haya juu ya Waroma 8:29 (“wale amba aliwajua tangu zamani aliwaweka tangu zamani”) na 1 Petro 1:2 (“aliviyotangulia kuwajua ninyi”). Lakini Mungu hakujua tu mbele watu gani wataamini Mwokozi, lakini *aliamuru* mbele ya kwamba wataamini kwa njia ya kukokota watu wengine karibu naye.

Hata kama Mungu anachagua watu wengine kuokolewa, hachagui kamwe watu wengine kulaaniwa. Biblia inafundisha uchaguzi, lakini haifundishi laana kamwe. Lakini labda watu wengine watauliza, “Kama Mungu akichagua watu wengine kubarikiwa, ni kusema kwamba anachagua wengine kuharibiwa?” Sivyo! Mataifa yote ya dunia wamekuwa chini ya hukumu ya uharibifu kwa sababu ya zambi zao wenyewe, si kwa sababu ya amri isiyo sheria wala shauri la Mungu. Kama Mungu angaliacha watu wote kwenda Gehena – na ingekuwa haki kwaye kufanya hivi – watu wangalipata hukumu waliyostahili kupokea. Ulizo kubwa ndilo hili: Ni haki na ruhusa ya Bwana mwenye enzi kujishusha na kuchagua watu wachache, amba wanganiluhukiwa, kuwa bibi arusi kwa Mwana wake? Jibu la ulizo hili ni Ndiyo. Watu wakipotea, ni kwa sababu ya zambi na maasi yao; kama watu wakiokolewa, ni kwa sababu ya neema ya enzi ya Mungu ambayo inawaokoa.

Ingepasa mtu anayeokolewa kukaa kustaajabu juu ya uchaguzi wa enzi ya

Mungu. Mwamini anaona watu wenye wengine wenyewe tabia na nafsi na nia nzuri kupita zake, na anauliza, “Kwa sababu gani Mungu alinichagua mimi?”

Haifai wasioamini kutegemea kweli ya uchaguzi kama uzuru kwa kutokumini kwao wenyewe. Haifai waseme, “Sina kitu ninachowea kufanya kupata wokovu kama sikuchaguliwa.” Kuna njia moja tu kwa watu kujuu kama walichaguliwa, ndiyo kutubu zambi zao na kupokea Bwana Yesu Kristo kuwa Mwokozi wao (1 Tes. 1:4-7).

Wala haifai waamini kutaja kweli hii ya uchaguzi kama uzuru kwa sababu ya kukosa kujitoa kwa kazi ya kuhubiri Habari Njema. Haifai tuseme, “Kama walichagiliwa na Mungu, wataokolewa bila mahubiri yangu.” Mungu tu anajua wanani ni wachaguliwa. Sisi watu tunaagizwa kuhubiri Habari Njema kwa dunia nzima, kwa sababu Mungu anataka kuwapa watu wote njia kupokea wokovu. Watu wanakataa kupokea Habari Njema kwa sababu ya ugumu wa roho zao, si kwa sababu Mungu hakuita na roho ya kweli watu wote kuokolewa.

Inatupasa kuepuka hatari mbili kwa maneno haya. Hatari ya kwanza ni kuamini sehemu moja tu ya kweli hii, ndiyo kuamini uchaguzi wa mwenyezi Mungu, na kukataa kwamba ni lazima kwa mtu kuchagua au kukataa wokovu. Hatari ya pili ni kusimamia kweli moja kupita nytingine. Biblia inatufundisha kuamini uchaguzi wa mwenyezi Mungu, na kuamini vilevile kwamba mtu ni mwenye daraka, anayepaswa kuchagua wokovu yeeye mwenyeewe. ♦

Sasa turudi kwa Waroma 9 na kusoma mafundisho ya mtume mpandwa Paulo juu ya maneno haya.

9:1 Wakati Paulo alipokaa kufundisha kwamba wokovu ni kwa Mataifa vilevile, si kwa Wayuda tu, ilionekana kwa Wayuda kwamba alikuwa haini, na hakushika tena dini yake, ndiyo dini ya

Wayuda. Hivi alionyesha na kiapo mapendo yake makubwa kwa Wayuda. Alisema **kweli**, hakusema **uwongo**. **Zamiri** yake, pamoja na upatano wa **Roho Mtakatifu**, ilishuhudia kwamba alisema kweli.

9:2 Alifikiri kwanza juu ya mwito wa utukufu wa Israeli, lakini sasa walikataliwa na Mungu kwa sababu walikuwa wakikataa Masiya. Mafikiri haya yalijaza **roho** yake na **huzuni kubwa na uchungu usiokoma**.

9:3 Aliweza **kuomba** yeze mwenye **akatazwe** na kutengwa na Kristo, kama kwa njia ya kuondolewa wokovu wake mwenye, ndugu zake Wayuda wangeweza kuokolewa. Ndaani ya masemo haya tunaona mapendo makubwa zaidi – mapendo yanayosukuma mtu kutoa uzima wake mwenye kwa ajili ya rafiki zake (Yn. 15:13). Na tunaona mzigo mzito sana rohoni mwa mwamini Myuda kwa **ndugu zake kwa namna ya mwili**, waweze kuokolewa vilevile. Tunakumbushwa ombi la Musa kwa watu wake: “Lakini sasa, kama ukitaka kusamehe zambi zao - ; na kama sivyo, uniondoshe, ninakusihi, katika kitabu chako ulichoandika” (Kut. 32:32).

9:4 Pamoja na Paulo kutoa machozi kwa sababu ya watu wake, anakumbuka vilevile mapendeleo yote waliyopokea. Walikuwa **Waisraeli**, kama wana wa watu wachaguliwa wa zamani wa Mungu.

Mungu *aliweka* taifa lile kama mwana (Kutoka 4:22), na aliponyesha watu wake toka Misri (Hos. 11:1). Alikuwa baba kwa Israeli (Tor. 14:1), na Efuraimu alikuwa mzaliwa wake wa kwanza (Yer. 31:9). (Hapa *Efuraimu* ni jina lingine kwa taifa la Israeli.)

Shekina, ndilo wingu la **utukufu**, lilikuwa mfano kuonyesha kwamba Mungu alikuwa katikati yao, akiwongoza na kuwalinda.

Mungu alifanya **maagano** na Israeli, si na Mataifa. Kwa mfano, alifanya na Israeli Agano la Palestina, lilioahidi kwamba inchi toka Mto wa Misri kufika Mto Furati itakuwa inchi yao (Mwa. 15:18). Na kwa wakati wa kuja atasibitisha nao Agano Jipy, ikiahidi kwamba taifa la Israeli litendelea bila mwisho, watatibu na kuokolewa na kubarikiwa kwa wakati wa kuja (Yer. 31:31-40).

Israeli walikuwa taifa la pekee waliotolewa **sheria**.

Walipewa kawaida za dini na maongozi ya **utumishi wa Mungu** katika hema na hekalu, na kwa maneno ya ukuhani.

Zaidi ya maagano yaliyotajwa mbele, Mungu alitoa **ahadi** nyingi kwa Israeli, kuwalinda, kuwakalisha na salama na usitawi.

9:5 Ni taratibu kwa Wayuda kuhe-sabu wazee wakubwa wenye heshima kuwa wao – ndio Abrahamu, Isaka, Yakobo, na wana kumi na wawili wa Yakobo. Watu hawa walikuwa baba za taifa lao. Nao walikuwa wenye mapendeleo makubwa zaidi – Masiya ni Mwisraeli, kwa maneno ya uzazi duniani, hata kama yeze ni Mwenye enzi wa ulimwengu, **Mungu Mbarekiwa kwa milele**. Shairi hili linaponyesha wazi uungu na utu wa Mwokozi.

9:6 Mtume alijibu sasa ulizo ku-bwa moja linalofazaisha watu. Kama Mungu alitolea ahadi kwa Israeli kama watu wake wachaguliwa, neno hili linapatana namna gani na kukataliwa kwao kwa wakati wa sasa, na Mataifa wakibarikiwa kwa pahali pao? Paulo anaonyesha ya kuwa neno hili halionyeshi kwamba Mungu alivunja ahadi yake. Aliendelea kuonyesha kwamba tangu zamani msingi wa uchaguzi wa Mungu ulikuwa ahadi, si uzazi wa mwili. Si kila Mwisraeli

anayeriti ahadi hizi. Ndani ya taifa la **Israeli** Mungu ana baki walio waamini wa kweli.

9:7 Si **wote** waliozaliwa na Abrahamu ni **watoto** wa Abrahamu. Kwa mfano, Isimaeli alikuwa **mzao wa Abrahamu**, lakini hakuwa mriti wa ahadi. “**Katika Isaka wazao wako wataitwa**” (Mwa. 21:12). Kama tulivyoonyesha ndani ya mafundisho juu ya 4:12, Bwana Yesu alionyesha tofauti hii vilevile wakati aliposemezana na Wayuda wasioamini katika Yoane 8:33-39. Walisema naye, “Tuko wazao wa Abrahamu...” (sh. 33). Yesu alikubali semo hili, akasema, “Ninawajua ninyi kama wazao wa Abrahamu” (sh. 37). Lakini wakati waliposema, “Abrahamu ni baba yetu,” Bwana alijibu, “Kama mungalikuwa watoto wa Abrahamu, mungalifanya kazi za Abrahamu” (sh. 39). Ni kusema, walikuwa wazao wa Abrahamu, lakini hawakuwa na imani ya Abrahamu, hivi hawakuwa watoto wake kwa roho.

9:8 Neno kubwa si uzazi wa mwili. Israeli la kweli ndilo Wayuda waliochaguliwa na Mungu. Mungu aliwapa **ahadi** fulani ambayo iliwaonyesha kuwa **watoto** wake. Habari za Isaka na Yakobo zinaonyesha uchaguzi huu wa Mungu mwenye enzi.

9:9 Mungu alitokea kwa Abrahamu na aliahidi kwamba atarudi kwa **wakati** fulani, na kwamba **Sara atakuwa na mwana**. Mwana yule alikuwa Isaka. Alikuwa kweli mtoto wa **ahadi**, aliyezaliwa namna nyingine na viumbe wa ulimwengu.

9:10 Habari za Yakobo zinaonyesha uchaguzi wa enzi vilevile. **Isaka** na **Rebeka** walikuwa wazazi wake. Lakini **Rebeka** alikuwa na watoto *wawili* tumboni mwake, si mmoja tu.

9:11 Kulikuwa na tangazo **mbele** ya **kuzaliwa kwa watoto**. Tangazo hili halikuwa juu ya kazi za faida za kila

mtoto kwani hawakuzaliwa bado. Lili-kuwa tangazo la maneno Mungu aliyo-chagua, juu ya maneno yeye aliyotaka, si juu ya nia au maarifa yao. Maana ya **kusudi la Mungu kuchagua** ni ya kwamba anachagua yeye mwenyewe kugawa baraka zake namna yeye mwenye enzi anavyotaka.

Shairi hili linahakikisha kwamba Mungu hakuchagua Yakobo kwa sababu alijua mbele maneno ambayo Yakobo atafanya. Imeandikwa wazi “**si** kwa sababu ya **matendo!**”

9:12 Mungu alikusudi ya kwamba **mkubwa atatumikia mdogo**. Esau atakuwa chini ya Yakobo. Yakobo alichaguliwa kupokea *utukufu na mapeendeleo ya dunia*. Esau alikuwa mzaliwa wa kwanza wa mapacha hawa, na ingalimpasa yeye kupokea heshima hii. Lakini Mungu alichagua kwa Yakobo kuipokea.

9:13 Kuonyesha hata wazi kupita enzi ya Mungu kuchagua, Paulo alitaja Malaki 1:1, 2: “**Nimependa Yakobo, lakini nilichukia Esau.**” Hapa Mungu anasema juu ya mataifa mawili, Israeli na Edomu. **Yakobo** alikuwa mkubwa wa Israeli, na **Esau** alikuwa mkubwa wa Edomu. Mungu alichagua kutolea taifa la Israeli Masiya na ufalme wa Masiya. Taifa la Edomu halikupokea ahadi namna hii. Inchi yao ilikuwa milima, na uriti wao ulikuwa ukiwa pahali mbweha za jangwa walipokaa (Mal. 1:3; ona vilevile Yer. 49:17, 18; Ezek. 35:7-9).

Malaki 1:2,3 yanaonyesha zaidi namna Mungu alivyotendea mataifa, lakini yanaonyesha haki yake kuchagua watu mmoja mmoja vilevile.

Mungu alikuwa ameagiza kwamba **mkubwa atatumikia mdogo**. Agizo hili linatusaidia kufahamu masemo yake, **nikapenda Yakobo, lakini nikachukia** Esau. Uchaguzi wake kwa Yakobo yalionyesha mapendo yake kwaye. Hakusema hivi juu ya Esau, na tuki-

sawanisha neno hili na masemo yake juu ya Yakobo, lilionyesha kwamba alichukia Esau. Mungu hakuchukia Esau na uchungu mkali, lakini hakumpenda kwa kipimo alichopenda Yakobo, na kwa sababu hii alichagua Yakobo.

Mashairi haya ni juu ya *baraka za dunia*, si juu ya uzima wa milele. Maana ya Mungu akichukia Esau haiko ya kwamba Waedomu mmoja mmoja *hawezzi* kuokolewa, kama vile maana ya mapendo yake kwa Yakobo haiko kwamba Wayuda mmoja mmoja *hahitaji* kuokolewa. (Ona ya kwamba Esau alipokea baraka za dunia vile-vile – ona masemo yake mwenyewe katika Mwanzo 33:9.)

9:14 Paulo hakushangaa kwa sababu watu hawakufurahi juu ya mafundisho yake juu ya uchaguzi wa Mungu. Hata sasa watu wanasema Mungu hatendi na haki. Wanasema kama akichagua watu fulani, ni kusema analaani watu wote wengine. Wanafikiri kama Mungu alichagua maneno haya yote mbele, watu hawawezi kufanya kitu juu yao, na si haki kwa Mungu kuhukumu watu.

Paulo alikataa na nguvu kwamba Mungu alikuwa, na alitenda na **uzalimu**. Hakubembeleza washitaki wake na masemo ya kupunguza enzi ya Mungu, la-kini alisema mafundisho yake tena hata na nguvu kupita mbele.

9:15 Alitaja kwanza maneno ya Mungu kwa Musa, “**Nitamrehemu ye ye ambaye nitamrehemu, na nitamhurumia ye ye ambaye nitamhurumia**” (ona Kut. 33:19). Nani anaweza kusema kwamba Mungu Mjuu sana, Bwana wa mbingu na dunia, hana ruhusa kuonyesha **rehemna huruma?**

Watu wote wanahukumiwa kwa sababu ya zambi na kutokuamini kwao. Kama wangaliachwa kufanya mapenzi yao wenyewe wangalipotea *wote*. Mungu anaita watu wote kupokea wokovu.

Zaidi ya ile anachagua wengine wa watu hawa wahukumiwa aweze kuwaonyeshea neema hata kubwa kupita. Lakini hata kama akifanya hivi, hachagui wengine kuhukumiwa. Wamekwisha kuhukumiwa kwa sababu wao ni wenye zambi tangu kuzaliwa kwao na wamekataa Habari Njema. Wale wanaochaguliwa na Mungu wanaweza kumshukuru kwa neema yake. Wale wanaopotea wanaweza kujishitaki wenyewe tu.

9:16 Kwa kujumlisha maneno haya, ni **Mungu wa rehema** anayeo-ngoza mwisho wa watu au mataifa, si nguvu ya kutaka au bidii yao.

Wakati Paulo anaposema **si katika uwezo wa mwenye kutaka**, hakutaka kusema kwamba mtu hahitaji yeye mwenyewe kuchagua kuokolewa. Mwito wa Habari Njema ni kwa kila mtu, kama tunavyosoma ndani ya Ufunuo 22:17: “na yeye anayetaka atwae maji ya uzima bure.” Ndani ya Yoane 5:40 Yesu alionyesha kwamba Wayuda wasioamini hawakutaka kuja kwake. Wakati Paulo anaposema, **wala mwenye kupiga mbio**, hakukana kwamba inatupasa kufanya nguvu kuingia katika mlango mwembamba (Luka 13:24). Lazima tuwe na roho ya kutaka na bidii vilevile. Maneno haya ni maneno makubwa, lakini neno kubwa zaidi ndilo hili: wokovu unatoka kwa Bwana. Morgan anasema:

Hata tukitaka sana, na kukimbia na nguvu yetu yote, maneno haya hayawezi kutupatia wokovu tunahitaji, wala kutuwezesha kufurahishwa na baraka zake ... Sisi wenyewe hatutataka wokovu, na hatutajaribu kupokea. Maneno yote ya wokovu wa watu yanaanza na Mungu.⁹

9:17 Hatuoni enzi ya Mungu kwa njia ya kurehemu watu wengine tu, lakini kwa njia ya kufanya wengine wagumu. **Farao** ni mfano wa neno hili.

Hakuna habari hapa ya kwamba mfalme Mmisri alihukumiwa tangu siku ya kuzaliwa kwake. Hili ndilo neno lililotokea: Wakati Farao alipokwisha kupata nguvu alikuwa mtu mwovu, mkali, na mkaidi sana. Hata kama alionya na nguvu tena na tena, alikaa kufanyiza moyo wake mgumu. Mungu angaliweza kumharibu mara moja, lakini hakufanya hivi. Alimwacha kuishi ili aweze kuonyesha **uwezo** wake kwa njia yake, na ili kwa njia ya Farao jina la Mungu liweze kujulikana pahali pote duniani.

9:18 Farao alifanyiza moyo wake mwenyewe mgumu *tena na tena*, na kila mara aliyofanya hivi Mungu alimhukumu kwa njia ya *kuongeza* ugumu wa moyo wake. Jua linaloyeyusha barafu, linafanyiza udongo nguvu. Jua lile linaloondosha rangi ndani ya nguo linafanyiza rangi ya ngozi ya mtu kuwa nyeusi kupita. Mungu yule aliye mwenye rehema kwa wenyewe mioyo ya kuvunjika anafanyiza ngumu roho za wale wasiotubu. Hakuna neema kwa mtu yule anayekataa kupokea neema ya Mungu.

Ni ruhusa ya Mungu kuonyesha **rehema** kwa mtu ye yote ambaye anataka kumrehemu, na kufanya mgumu mtu ye yote ambaye anataka. Lakini ye ye ni Mungu, na kwa sababu hii hatendi kamwe bila haki.

9:19 Masemo ya nguvu ya Paulo ya kwamba Mungu anaweza kufanya neno lo lote analotaka yalamsha manunguniko ndani ya roho za watu. Walisema kama ni hivi, **haifai kwa Mungu kulaumu** mtu kwa sababu hakuna mtu **aliyeshindana na kusudi** lake. Washitaki walifikiri kwamba watu hawawezi kufanya wala kusema neno kugeuza namna ya mwisho wa uzima wao.

9:20 Mtume anahamakia kwanza kiburi cha mtu ye yote aliye na

ukaramisu kushitaki Mwumba wake. **Mtu wa dunia**, mwenye zambi, ujinga na uzaifu, hawezi kubishana na **Mungu** juu ya akili au haki ya maneno ana-yofanya.

9:21 Halafu Paulo alisema juu ya **mfinyanzi na udongo** kama mfano wa enzi ya Mungu. Siku moja **mfinyanzi** anaingia kiwanda chake na anaona fungu la udongo bila umbo. Anakamata fungu hili na kuliweka juu ya gurudumu lake na kuufanyiza kuwa chombo kizuri. Hana ruhusa kufanya hivi?

Mfinyanzi ndiye Mungu. **Udongo** ni watu wa dunia, wenyewe zambi, wapotevu. Kama mfinyanzi angaliwaacha ndani ya hali yao, wangalitumwa wote kwa Gehena. Angalitenda kwa haki kama angaliwaacha kufanya kutaka wao. Lakini hakufanya hivi. Kwa sababu ye ye ni mwenye enzi, alichagua wenyewe zambi wachache, aliwaokoa kwa neema yake, na kuwageuza kwa mfano wa Mwana wake. Ana ruhusa kufanya hivi? Kumbuka kwamba hachagui watu wengine kwenda Gehena. Walikwisha kuhukumiwa kwa sababu ya ukaidi na kutokuamini kwao.

Mungu ana **uwezo** na amri kufanyiza nusu ya udongo ule kuwa **chombo cha heshima**, na nusu nyingine kuwa chombo **pasipo heshima**. Watu wote hawakustahili, hivi Mungu anaweza kutoa baraka zake pahali po pote anapotaka au kukataa kuzitoa wakati wo wote anapotaka. Barnes aliandika, “Wakati wote wasipostahili, wanaweza kuomba neno moja tu, ndilo asitendee mtu ye yote na uzalimu.”¹⁰

9:22 Paulo anaonyesha **Mungu**, mfinyanzi mkubwa, kama mwenye shindano rohoni. Anataka kuonyesha **gazabu** na **uwezo** wake kwa njia ya kuazibu zambi, lakini anataka kuwa na saburi nyingi vilevile kwa **vyombo** **nya gazabu vilivyofanywa tayari kwa kuanjamia**. Tunaona kwanza ukali wa

haki wa Mungu, na nyuma tunaona **uvumilivu** wake wa rehema. Mungu angalitenda kwa haki kama angaliazibu waovu mara moja, lakini kwa pahali ya kufanya hivi aliaonyeshea saburi nyingi. Nani atamshitaki juu ya neno hili?

Angalia vizuri semo hili: **vyombo vyazabu vilivyofanywa tayari kwa kuangamia.** Vyombo vyazabu ndio wale waliostahili **gazabu** ya Mungu kwa sababu ya zambi zao. Walifanywa tayari kwa kuangamia kwa sababu ya zambi zao na maasi yao wenyewe, si kwa njia ya amri isiyo ya sheria ya Mungu.

9:23 Nani atasema kwamba haifai Mungu **kujulisha mali ya utukufu wake** kwa watu amba o anataka kuteendea rehema – watu **ambao aliwachagua tangu zamani** wapate utukufu? Masemo ya C. R. Erdman yana maana mazuri sana. Alisema:

Mungu mwenye enzi hahukumu kama mwe watu amba o walipaswa kuokolewa, lakini anaokoa watu amba wanastahili kupotea.¹¹

Mungu hatayarishi vyombo vyazabu waangamizwe, lakini anatayari sha **vyombo vyazabu rehema vimate utukufu.**

9:24 Paulo anaeleza kwamba vyombo vyazabu rehema ndivyo sisi Wakristo amba o Mungu **aliita** toka Wayuda na Mataifa. Elezo hili ni msingi wa nyingi za habari tutakazosoma – ya kwamba taifa la Wayuda, ila baki dogo, waliwekwa kando, na **Mataifa** waliitwa kupokea baraka.

9:25 Mtume anataja mashairi mawili toka Hosea kuonyesha kwamba haifai Wayuda kushangaa juu ya mwito wa Mataifa. Shairi la kwanza ni Hosea 2:23: “**Nitawaita wale watu wangu, wasiokuwa watu wangu, na nitamwita mpenzi asiyekuwa mpenzi wangu.**” Katika Hosea shairi hili linasema juu ya Israeli, si juu ya

Mataifa. Linatazamia wakati Waisraeli watakaporudishwa kama watu wa Mungu na kama wapenzi wake. Lakini Paulo analitaja hapa katika Waroma kusema juu ya mwito wa Mataifa. Ilikuwa vizuri kwa Paulo kufanya hivi? Ndiyo. Roho Mtakatifu aliyeandikisha Hosea maneno haya kwanza ana ruhusa kuyatafsiri au kuyatumia kwa njia nyingine kwa wakati wa nyuma.

9:26 Shairi la pili ni Hosea 1:10: **Na itakuwa pahali pale walipoambiwa: “Ninyi si watu wangu, kule wataitwa wana wa Mungu aliye hai.**” Hapa tena, katika Agano la Kale, shairi hili si juu ya Mataifa, lakini juu ya Israeli wakati watakaporudi karibu na Mungu. Maneno haya yanaonyesha kwamba wakati Roho Mtakatifu anapotaja ndani ya Agano Jipy Mashairi toka Agano la Kale, anaweza kutumika nayo namna anavyotaka.

9:27 Ndani ya 9:27-29 tunasoma kwamba taifa zima la Israeli ila baki watakataliwa. **Isaya** alitabiri kwamba wachache tu wa **Waisraeli wataokolewa**, hata kama hesabu ya watu wa Israeli itaongezeka sana (Isa. 10:22).

9:28 Wakati Isaya aliposema, “**ata maliza neno lake na kulikata kwa haki: kwa maana Bwana atafanya neno fupi juu ya dunia**” (Isa. 10:23), alikuwa akisema juu ya Wababeli wakiingia Palestina, na juu ya kuhamishwa kwa Israeli toka inchi yao. **Kazi** hii ilikuwa hukumu ya Mungu. Wakati Paulo alipotaja maneno haya, alisema kwamba maneno haya yaliyopata Israeli zamani yaliweza kuwapata tena, hata kwa wakati wa Paulo.

9:29 **Kama Isaya alivyotangulia kusema** (ndani ya sehemu ya mbele nabii wake): **Kama Bwana** wa majeshi ya mbingu **asingalituachia** wachache na uzima, kama Waisraeli wangaliaribiwa wote **kama Sodomo na Gomora** (Isa. 1:9).

9:30 Halafu Paulo anauliza kama mwisho wa maneno haya ni nini kwa wakati wa sasa, ndio muda wa Kanisa? Neno la kwanza ni habari za **Mataifa, wasiofuata haki**, lakini waliotenda uovu. Hawakufuata haki ambayo wao walifikiri inatosha, lakini walipata **haki** iliyio ya **imani** ndani ya Bwana Yesu Kristo. Si Mataifa yote waliohesabiwa haki, lakini wale tu walioamini Kristo.

9:31 Lakini **Israeli**, waliojaribu ku-hesabiwa haki kwa njia ya kushika sheria, hawakukuta kamwe **sheria** ambayo iliwavezesha kupata **haki**.

9:32 Kwa nini? Kwa sababu walikataa kuamini kwamba kwa njia ya **kuamini** Kristo tu watu wanaweza kuhesabiwa haki, **lakini** walikaa na roho ya ukaidi kujipatia wenyewe haki kwa njia ya matendo ya kuwastahilisha. **Walijikwaa** juu ya **jiwe la kukwaza**, ndiye Bwana Yesu Kristo.

9:33 Hili ndilo neno Bwana alilotangaza mbele kwa njia ya Isaya. Kuja kwa Masiya kwa Yerusalem kutagusa watu kwa njia mbalimbali mbili. Kwa watu wengine atakuwa **jiwe la kukwaza na mwamba wa kuangusha** (Isa. 8:14). Lakini watu wengine watamwamini na hawatakuwa na sababu ya kupata **haya**, uchungu, wala chukizo (Isa. 28:16).

B. Israeli kwa wakati wa sasa

(Sura 10)

10:1 Wayuda wasioamini walichukizwa na mafundisho ya Paulo. Walifikiri ye ye ni haini na adui ya Israeli. Lakini wakati alipoandikia **ndugu** zake Wakristo aliwaambia kwa hakika ya kwamba neno ambalo liliweza kumfurahisha zaidi lilikuwa wokovu wa Waisraeli. Aliomba **Mungu** na bidii **kwa ajili ya Israel waweze kuokolewa**.

10:2 Hakuwahukumu na kusema kwamba hawakuamini Mungu. Sivyo. Aliwashuhudia na kusema **wana uwivu kwa Mungu**. Walionyesha neno hili

wazi kwa namna walivyotimiza na bidii kawaida ya kuabudu ya dini ya Wayuda, na hawakuvumilia mafundisho yo yote mengine. Lakini **uwivu** peke yake haukutosha. Sharti uwe pamoja na kweli. Uwivu peke yake unaweza kuzaa maumivu.

10:3 Walikuwa wameanguka kwa njia ile. **Hawakujua haki ya Mungu**, walikuwa **wajinga** ya kwamba Mungu anahesabia watu **haki** kwa njia ya imani, si kwa sababu ya matendo mema. Walijaribu kusimamisha **haki yao wenyewe** kwa njia ya kushika sheria. Walijaribu kupendeza Mungu kwa njia ya mwenendo, na matendo mema yao wenyewe. Walidumu kukataa kunyenyekea njia ya Mungu kuhesabia haki wenye zambi waovu wanaoamini Mwana wake.

10:4 Kama wangali amini **Kristo** kama wangalifahamu kwamba ye ye ndiye **mwisho wa sheria** kwa maneno ya haki. Kusudi la sheria ni kufunua zambi, kusadikisha wavunja sheria zambi zao, na kuwahukumu. Haiwezi kamwe kuwalettea haki. Azabu kwa kuvunja sheria ni mauti. Kristo alilipa azabu ya sheria ambayo watu walivunja. Wakati mwenye zambi anapopokea Bwana Yesu kuwa Mwokozi wake, sheria haina neno naye tena. Amekufa kwa sheria kwa njia ya Mkombozi wake. Hahitaji kujaribu tena kujipatia haki kwa njia ya kuishika.

10:5 Ndani ya maandiko ya Agano la Kale tunaweza kuona tofauti ya maneno ya sheria na maneno ya imani. Kwa mfano, katika Walawi 18:5, **Musa anaandika** kwamba mtu anayepata **haki** inayotoka kwa sheria **ataishi** kwa njia ya kufanya maneno yanayoagizwa kwa sheria.

Basi tunajua kwamba neno hili haliwezekani kwa mwenye zambi. Linasema tu ya kwamba mtu akiweza kutii sheria katika kila neno na kwa kila saa, hatahukumiwa kufa. Lakini sheria ilitolewa kwa watu waliokuwa wenye

zambi na waliokwisha kuhukumiwa kufa. Hata kama wakiweza kutii sheria ndani ya kila neno kuanza siku ile, watapotea, kwa sababu Mungu anataka malipo kwa zambi walizofanya mbele vilevile. Hakuna njia wala tumaini kwa watu kupata haki kwa njia ya kutii sheria.

10:6 Kuonyesha kwamba imani ni namna nyingine na sheria, Paulo alitaya sehemu ya Torati 30:12, 13, “Si mbinguni, hata useme: Nani atapanda mbinguni kwa ajili yetu ayalete kwetu na kutuambia tuyasikie, tupate kuyafanya?”

Wala si ngambo ya bahari, hata useme, “Nani atavuka bahari kwa ajili yetu, ayalete kwetu na kutuambia tuyasikie tupate kuyafanya?”

Ona ya kwamba ndani ya Torati mashairi haya hayasemi juu ya imani na Habari Njema hata kidogo. Yanasema juu ya sheria, zaidi juu ya agizo la kugeuka “kwa Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote na kwa roho yako yote” (Tor. 30:10b). Mungu anasema kwamba sheria haikufichwa. Haikuwa mbali, wala neno lisilonendeka. Mtu hahitaji kupanda **mbinguni**, wala kuvuka bahari kuipata. Ni karibu, ikingoja kwa mtu kuitii.

Lakini Mtume Paulo anatumika na mashairi haya kufundisha juu ya Habari Njema. Anasema kwamba mweenye **imani** hahitaji kupanda **mbinguni kuleta Kristo chini**. Neno hili lisngaliwezekana, na vilevile *lisngalihitajiwa*, kwa sababu Kristo alikuwa ameshuka duniani kufanyika mtu!

10:7 Wakati mtume anapotaja Torati 30:13, kwa pahali pa kusema, “Nani atavuka bahari”, ananasema, **nani atakayeshuka kwa kuzimu**. Alitaka watu kujuu kwamba Habari Njema haiagizi watu kushuka kaburini kuleta Kristo juu kutoka kwa wafu. Neno hili lisngaliwezekana, na vilevile *lisngalihitajiwa* kwa sababu Kristo alikuwa amefufuka. Ona ya kwamba

ndani ya 10:6,7 kuna mafundisho mawili ya dini juu ya Kristo yaliyo magumu zaidi kwa Myuda kukubali, ndiyo ya kwamba Kristo alifanyika mtu, na ya kwamba alifufuka. Lakini sharti Myuda akubali mafundisho haya kwa kupata wokovu. Tutayaona tena ndani ya 10:9, 10.

10:8 Habari Njema inasema nini basi kama haiwaambii watu kufanya maneno yasiyowezekana kwao kufanya, au kufanya neno linalokwisha kufanywa na Bwana?

Paulo anatumika tena na shairi toka Torati 30 kuonyesha kwamba habari njema ni **karibu**, tunaweza kuifahamu, na ni nyepesi kuipokea; tunaweza kusemezana juu yake (**katika kinywa chako**), na ni nyepesi kufahamu na nia (**katika moyo wako**) (Tor. 30:14). Ni habari njema ya wokovu kwa njia ya imani iliyohubiriwa na Paulo na mitume wengine.

10:9 Hapa tunaona kwa ufupi ya kwamba: 1. Lazima upokee kweli hii ya kuwa Kristo alifanyika mtu, ya kwamba Mtoto mchanga ndani ya sanduku ya kulisha nyama kwa Betelehemu ni Bwana wa uzima na utukufu, ya kwamba **Yesu** wa Agano Jipyä ni **Bwana** (Yehova) wa Agano la Kale.

2. Inakupasa kuamini ya kwamba alifufuka. **Mungu alimfufua toka wafu** kuhakikisha ya kwamba Kristo alitimiza kazi iliyohitajiwa kwa wokovu wetu, na ya kwamba Mungu alikubali kazi hii. Maana ya kuamini **moyoni** ni kuamini na akili, roho, na kutaka kwako.

Hivi **unakiri kwa kinywa chako ya kuwa Yesu ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua toka wafu**. Ni kupokea kwa wewe mwenyewe Bwana Yesu Kristo na kazi aliyofanya. Hii ndiyo imani inayookoa mtu.

Mara nyingi watu wanaauliza kama ikiwezekana kwa mtu kuokolewa kwa

njia ya kupokea Bwana Yesu Kristo kama Mwokozi bila kukiri kwamba yeye ni Bwana wake vilevile. Hakuna mafundisho ndani ya Biblia kuruhusu mtu kuamini Yesu na nia yake tu bila kuwa tayari kumfanyiza Bwana wa maisha yake mazima. Lakini watu wanaofundisha kwamba wale tu wanaonyenyekea Yesu kama Bwana wanaweza kupokea wokovu, wanapaswa kuuliza: "Kwa kipimo gani inatupasa kumkiri kuwa Bwana wetu?" Wakristo wachache tu wangesema kwamba wamejitoa kabisa kwake kwa maneno yote. Wakati tunapohubiri Habari Njema, lazima tufundishe kwamba *mtu anahitaji kuwa na imani tu kwa kuhesabiwa haki*. Lakini sharti tukae kukumbusha wenyе zambi na watakatifu vilevile ya kwamba Yesu Kristo *ni* Bwana (Yehova-Mungu), na inatupasa kumkiri kuwa Bwana ndani ya maisha yetu.

10:10 Paulo anaendelea kueleza kwamba **kwa moyo mtu anaamini hata kupata haki**. Si neno la ukubali na akili tu, lakini na roho yake nzima. Wakati mtu anapofanya hivi, anahesabiwa haki mara moja.

Halafu **kwa kinywa anakiri hata kupata wokovu**; maana yake mwamini anakiri mbele ya watu wengine kwamba amepokea wokovu. Kukiri mbele ya watu wengine *si neno la sharti* ambalo inapasa mtu kufanya kwa kupata wokovu, lakini linaonyeshya neno linalokwisha kutoke. Wakati mtu anapoamini neno fulani kabisa, anataka kuwaambia watu wengine juu yake. Hivi wakati mtu anapozaliwa tena kweli, itamshinda kuficha habari hizi. Hivi anashuhudia Kristo mbele ya watu wengine.

Maneno haya mawili yanafungana pamoja. Hivi Kelly alisema, "Kama mtu hakiri Kristo kuwa Bwana, hatuwezi kusema kwamba ameokolewa,

kwani Bwana wetu alisema, 'Yeye anayeamin na kubatizwa ataokolewa.'"¹² Na Denny alisema,

"Mtu akiamini moyoni na kuhe-sabiwa haki, na akikiri neno hili kupata wokovu, si maneno mballimali mawili, lakini sehemu mbili za neno moja."¹³

Watu wameuliza kwa sababu gani ndani ya 10:9 tunasoma juu ya kukiri kwanza, na ndani ya 10:10 juu ya kuamini kwanza, kisha juu ya kukiri. Si nguvu kujibu ulizo hili. Ndani ya shairi 9 tunasoma zaidi juu ya kuzaliwa kwa Yesu na mwili wa mtu, na nyuma yake juu ya ufufuko wake. Kuzaliwa kwake ni kwanza – Yesu ni Bwana. Kisha ufufuko wake – Mungu alimfufua toka wafu. Ndani ya shairi 10 tunasoma zaidi juu ya namna maneno yanavyofuatana wakati mwenye zambi anapokwisha kuokolewa. **Anaamini kwanza, kisha anatoa ushuhuda** mbele ya watu kwamba amepokea wokovu.

10:11 Halafu mtume alitaja Isaya 28:16 kusema na nguvu kwamba **mtu gani ambaye anamwamini, hatapata haya**. Labda watu waliogopa watapata haya kama wakikiri Kristo mbele ya wasioamini, lakini neno hili si kweli. Tukimkiri hapa *duniani*, yeye atatukiri *mbinguni*. Bila shaka tumaini letu litatimilizwa.

Maneno haya **mtu gani** yanafungana na maneno yatakayofuata – ya kwamba wokovu mtukufu wa Mungu ni kwa watu wote, Mataifa na Wayuda vilevile.

10:12 Waroma 3:23 lilitufundisha kwamba hitaji la Wayuda na Mataifa kwa wokovu ni sawasawa, kwani wao wote ni wenyе zambi. Sasa tunajifunza kwamba wokovu ni tayari kwa Wayuda na Mataifa vilevile. Mungu wetu hana tofauti, naye ni Bwana wa wote. Yeye ni **mwenye utajiri kwa watu wote ambao wanamwitia**.

10:13 Yoeli 2:23 linahakikisha na maneno machache kwamba Habari Njema ni kwa watu wote: “**Kila mtu anayeitia jina la Bwana ataokolewa.**” **Jina la Bwana** ni badala ya **Bwana** mwenyewe.

10:14 Lakini ni lazima kwa Habari Njema hii kutangazwa kwa watu wote. Habari za wokovu zina faida gani kwa Wayuda na Mataifa kama hawazisikii? Maulizo matatu yanayofuata yanayonyesha tena njia kwa Wayuda na Mataifa kupata wokovu. Mtume analuliza, **Namna gani wataitia ... wataamini ... watasikia bila mhubiri?** Labda maneno haya ni wazi kupita kufahamu kama tukiyapindua:

Mungu anatuma watumishi wake.
Wanahubiri habari njema za wokovu.

Wenye zambi wanaskia ya kama Mungu anataka kuwapa uzima ndani ya Kristo.

Wengine wa wasikiaji wanaamini habari hizi.

Wale wanaoamini wanaitia jina la Bwana.

Wale ambao wanamwitia wanaoko-kolewa.

Paulo anasimamia hapa kwa sababu gani anahubiri habari njema kwa Mataifa, ndilo neno Wayuda wasio-amini walifikiri ni baya muno.

10:15 Mungu ndiye anayetuma wahubiri. Sisi ndio wale **wanaotumwa**. Tuna **miguu mizuri**, kama Isaya alivyoandika juu yake **aliyehubiri habari za furaha ya maneno mazuri** (Isa. 52:7)? Isaya aliandika juu ya **miguu mizuri Yake** - ndiye Masiya. Hapa ndani ya Waroma “yake” inageuka “**yao**.” Miaka zaidi ya 1900 imepita tangu *Yeye* alikuja na **miguu mizuri**. Sasa ni mapendeleo na kazi yetu kufikia na **miguu mizuri** dunia hii ya wapotevu walio karibu kufa.

10:16 Lakini huzuni kubwa wa

Paulo ambayo haikumwacha kamwe ilikuwa ya kwamba **si watu wote wa Israeli waliosikiliza habari njema**. Isaya alikuwa ametabiri neno hili wakati alipouliza, “**Bwana, nani aliyesikia habari zetu?**” (Isa. 53:1). Jibu kwa ulizo hili ndilo: Si watu wingi. Wakati habari za kuja mara ya kwanza kwa Masiya zilipotangazwa, watu wa-chache tu walizipokea vizuri.

10:17 Wakati Paulo alipotaja shairi hili toka unabii wa Isaya, alionyesha kwamba habari watu walizosikia zili-amsha imani ndani ya roho zao, na ya kwamba habari hizi zinakuja kwa njia ya **neno** juu ya Masiya. Hivi alisema **imani inakuja kwa kusikia, na kusikia kwa Neno la Mungu**. Imani inafikia watu wakati wanaposikiliza mahubiri yetu juu ya Bwana Yesu Kristo. Msingi wa mahubiri haya ndio **neno la Mungu** lililoandikwa.

Lakini kusikiliza tu na masikio hakutoshi. Sharti mtu asikilize na roho na nia zilizo tayari kusikiliza kweli ya Mungu. Kama akifanya hivi, atatabmbua kwamba ni neno la kweli. Halafu ataliamini. Lakini ni wazi ya kwamba **kusikia** ndani ya shairi hili si kusikia na masikio tu. Labda mtu anaweza kupokea neno kwa njia ya *kusoma*, au kwa njia yo yote nytingine.

10:18 Halafu Paulo aliuliza kama Habari Njema haikuhubiriwa kwa watu wote? Ndiyo, Wayuda na Mataifa wali-kuwa **wamesikia** mahubiri ya Habari Njema. Alitaja sehemu ya Zaburi 19:4 kuhakikisha neno hili, akasema,

**“Sauti yao imetoka, ikaenea kaitika dunia yote,
Na maneno yao hata mwisho wa dunia.”**

Lakini neno ambalo linatufazaisha ni ya kwamba habari hizi toka Zaburi 19 hazikuandikwa juu ya Habari Njema. Ziliandikwa juu ya ushuhuda wa jua, mwezi, na nyota kwa utukufu wa

Mungu. Lakini kama tulivyoona mbele, Paulo alitumika nazo na kusema kwamba ni kweli juu ya matangazo ya Habari Njema duniani pote kwa wakati ye ye ali poishi. Mara nyingi Roho Mtakatifu aliongoza mtume kutaja mashairi toka Agano la Kale na kutumika nayo kufundisha maneno mengine kabisa. Roho Mtakatifu aliyeongoza kuandika maneno haya kwanza, ana ruhusa kutumika nayo kufundisha maneno mengine.

10:19 Taifa la **Israeli** wasingalishangaa juu ya mwito wa Mataifa, kwa sababu zaidi ya Wayuda walikataa Habari Njema. Unabii ndani ya Maandiko yao wenyewe uliwajulisha habari zitaka-zotoke. Kwa mfano Mungu aliaonya mbele kwamba **atatia** Israeli **wivu** kwa njia ya watu wasiokuwa taifa (ndio Mataifa), na kukasirisha Israeli na **taifa waliokosa ufhamu**, waabudayi sanamu (Tor. 32:21).

10:20 Na ukaramisu hata kupita, **Isaya** alitaja masemo ya Bwana kwamba **alipatikana** na Mataifa ambao hawakumtafuta, na **ambao hawaku-uliza** juu yake (Isa. 65:1). Zaidi ya Mataifa hawakujaribu kujuu Mungu. Walikuwa wapagano na walifurahi na dini zao. Lakini hata hivi wengi wao **walitikia** Habari Njema saa walipo-sikia. Ndiyo, waliitikia kupita Wayuda.

10:21 Akifikiri juu ya Mataifa wakisongana na Yehova, Isaya anaonyesha Bwana kama mwenye kusimama mchana mzima akinyosha mikono kwa Israeli, lakini walikuwa waasi na wenyewe ubishi.

C. Israeli kwa wakati wa kuja (Sura 11)

11:1 Basi nini itapata Israeli kwa wakati wa kuja? Watu wengine wanafundisha kwamba Mungu hana maneno na Israeli tena, na ya kwamba kanisa ni sasa Israeli la Mungu, na ahadi zote zilizotolewa kwa Israeli

zitatimizwa kwa kanisa.¹⁴ Waroma 11 ni moja ya sura za Biblia zinazonyesha kwamba mafundisho haya si kweli hata kidogo.

Maana ya ulizo la Paulo ni, “**Mungu amesukumia mbali watu wake kabisa?** Kila Mwisraeli mmoja mmoja ametupwa?” **Hapana, hata kidogo!** Hata kama Mungu **alisukumia mbali watu wake**, kama tunavyosoma kwa 11:15, maana yake haiko kwamba aliwakataa *wote*. Paulo ye ye mwenye-we alihakikisha kwamba si watu wote waliokataliwa. Yeye mwenye-we ali-kuwa **Mwisraeli, mmoja wa wazao wa Abrahamu, mtu wa kabila la Benyamina**. Maneno haya yote yali-hakikisha kwamba alikuwa Myuda safi.

11:2 Hivi tunafahamu kwamba maa-na ya sehemu ya kwanza ya shairi hili ni, “**Mungu hakusukumia mbali kabisa watu wake ambao aliwajua tangu zamani.**” Habari namna hii zilitokea kwa wakati wa **Elia** vilevile. Zaidi ya taifa la Israeli walikuwa wameacha kufuata Mungu na waliabudu sanamu. Hali yao ilikuwa mbaya sana hata Elia hakuwaombea lakin aliwashitaki mbe-le ya Mungu.

11:3 Alikumbusha **Bwana** namna watu walivyonyamazisha sauti za **manabii** kwa njia ya kuwaua. Walikuwa **wamebomoa mazabahu** za Mungu. Ilionekana kama ye ye alikuwa nabii mwaminifu wa pekee wa Mungu, na ya kwamba hata **uzima** wake ulikuwa katika hatari ya mauti.

11:4 Lakini mambo yote hayakuwa mabaya na bila tumaini, kama Elia ali-vyoogopa. Mungu alikumbusha nabii kwamba alikuwa amejiwekea watu elfu saba waliokataa na bidii kufu-ngana na taifa lao kuabudu Bali.

11:5 Kama kwa wakati ule, ni vi-vyo hivyo leo. Mungu hajiaachii bila ushuhuda kamwe. Anabaki siku zote na **baki** la watu waaminifu ambao alicha-gua ye ye mwenye-we kwa **neema** yake.

11:6 Mungu hachagui baki hili kwa sababu ya **kazi** yao, lakini kwa sababu ya uchaguzi wa **enzi** wa **neema** yake. Neema na kazi ni mbalimbali kabisa. Haiwezekani kufanya kazi kwa kupokea zawadi. Zawadi haina bei. Huwezi kuinunua. Ni kitu ambacho mtu hastahili kuipokea. Ni asante kwa sababu msingi wa uchaguzi wa Mungu ulikuwa **neema**, si **kazi**. Isipokuwa hivi, hakuna mtu angaliweza kuchaguliwa.

11:7 Ikiwa hivi, **Israeli** hawakupokea haki, kwa sababu walijaribu kuipata kwa njia ya kazi yao wenyewe, si kwa njia ya kazi ambayo Kristo ametimiza. Baki lililochaguliwa na Mungu walipokea haki kwa sababu waliyamini Kristo. Taifa lao walihukumiwa na upofu wa roho. Kwa sababu walikataa kupokea Kristo, kutaka na uwezo wao kumpokea zilikaa kupunguka.

11:8 Neno hili lilitabiriwa wazi ndani ya Agano la Kale (Isa. 29:10; Tor. 29:4). **Mungu** aliacha **roho ya usingizi** kuwapata na hawakutambua maneno ya roho tena. Walikuwa wamekataa kuona Bwana Yesu kama Masiya na Mwokozi, na sasa hawakuweza kumwona tena. Walikuwa wamekataa kusikia kusihu kwa Mungu, na sasa walitiwa uziwi wa roho. Hukumu hii ya kuogofya inaendelea **mpaka leo**.

11:9 **Daudi** vilevile alitabiri kwa mba Mungu atahukumu Israeli. Ndani ya Zaburi 69:22, 23 aliandika juu ya Mwokozi mkataliwa akiita Mungu kugeuza **meza yao** kuwa **tanzi na mtego**. **Meza** inasema hapa juu ya mapendeleo na baraka zote ambazo ziliwafikia kwa njia ya Kristo. Ingalipasa maneno haya kuwa baraka, lakini yaligeuzwa laana.

11:10 Ndani ya zaburi hii, Mwokozi mteswa aliitia Mungu kuacha **macho yao kutiwa giza**, na miili yao kuinamishwa kama miili ya wenye

kutumika kazi ya nguvu, au ya wazee.

11:11 Halafu Paulo ana ulizo lingine: **Wamejikwaa waanguke kabisa?** Maana yake, *kwa milele?* Wali-jikwaa waanguke bila kusimamishwa tena kamwe? Mtume anakataa wazo hili na nguvu. Shauri la Mungu ni kuwarudisha. Kusudi lake ni ya kwamba kwa sababu ya kuanguka kwao, **wokovu** uweze **kufikia Mataifa**, na Israeli watiwe wivu. Kusudi la **wivu** hili lilikuwa, mwishoni, kuwarudisha kwa Mungu.

Paulo hakukana kwamba Waisraeli walianguka. Ndani ya shairi hili ana-sema wazi: **kwa sababu ya kuanguka kwao ... wokovu umefikia Mataifa**. Na ndani ya shairi 12 alisema – “kama ikiwa *kuanguka* kwao kulikuwa mali ya dunia.” Lakini anakana na nguvu kabisa kwamba Mungu hana maneno na Israeli tena kamwe.

11:12 Kwa sababu Israeli walikataa Habari Njema, taifa lenyewe liliachwa, na Habari Njema ilihubiriwa **kwa Mataifa**. Kwa njia hii **kuanguka** kwa Wayuda kulikuwa **mali kwa dunia**. Neno lililokuwa hasara kwa Wayuda lilikuwa faida kwa Mataifa.

Lakini kama neno hili ni kweli, **zaidi sana** kurudishwa kwa Israeli karibu na Mungu kutakuwa baraka nyingi sana kwa dunia nzima! Wakati taifa la Israeli litakaporudi karibu na Bwana kwa mwisho wa Mateso Makubwa, litakuwa baraka kwa Mataifa.

11:13 Ndani ya shairi hili mtume alisema na **Mataifa** (11:13-24). Watu wengine wanafikiri kwamba anasema na Mataifa Wakristo katika Roma, lakini mashairi haya yanaonyesha kwamba alikuwa akisema na Mataifa yote. Hakusema juu ya kanisa la Mungu na hatukai katika hatari ya kucatiliwa mbali (11:22), ndilo neno lisilopatana na mafundisho ya Biblia.

Paulo alikuwa **mtume kwa Mataifa**, hivi ilikuwa nyepesi kwaye

kusema wazi nao. Alikuwa akitimiza **utumishi** wake kwa njia hii.

11:14 Alijaribu kwa kila **njia kuamsha wivu ndani ya wale** walikuwa watu wa kabilia lake, ili kwa njia hii Mungu aweze kutumika naye **kuokoa wengine**. Alijua, na sisi tunajua, kwamba ye ye mwenyewe hakuweza kuokoa mtu ye yote. Lakini Mungu wa wokovu anajifanya mamaja na watumishi wake hata anawaruhusu kusema kwamba wao wanafanya maneno ye ye tu anayoweza kufanya.

11:15 Shairi hili linafundisha tena habari za 11:12, lakini na masemo mengine kidogo. Wakati taifa la Israeli lilipowekwa kando kama watu wachaguliwa wa Mungu duniani, Mataifa walipokewa na Mungu kwa pahali pale pa mapendeleo, na kupatanishwa. Wakati Israeli litakaporudishwa kwa Mungu kwa wakati wa utawala wa Kristo kwa miaka elfu moja, ni kama kutakuwa na matengenezo na ufufuko.

Habari za Yona ni mfano wa maneno haya. Yona alikuwa mfano wa taifa la Israeli. Saa Yona alipotupwa toka merikebu wakati wa tufani, watu wote wa Mataifa ndani ya merikebu waliokolewa na kupona. Lakini wakati Yona aliporudi karibu na Mungu na kuhubiri kwa Ninawe, Mataifa waliojaza mji huu waliokolewa. Hivi ni kama wakati Mungu alipoweka Israeli kando kwa wakati, Habari Njema ili-hubiriwa kwa Mataifa wachache, lakini wakati Israeli watakaporudi karibu na Mungu, makundi makubwa ya Mataifa watakokolewa na kuingizwa katika ufalme wa Mungu.

11:16 Sasa Paulo anataja mifano mingine miwili. Wa kwanza ni **mali-mbuko na fungu**. Mfano wa pili ni **shina na matawi**. **Malimbuko na fungu** yanasema juu ya unga uliotayarishwa kwa kuokwa. Hayasemi juu ya matunda. Ndani ya Hesabu 15:19-21 tunasoma juu ya fungu la unga

lililotolewa kwa Bwana kama sadaka ya kunyanyuliwa. Kama fungu hili la unga likiwekwa kwa Bwana, ni vivyo hivyo na unga yote inayotayarishwa toka fungu hili.

Abrahamu ndiye mfano wa **mali-mbuko**. Alikuwa **mtakatifu**, maana aliwekwa mbali kwa Mungu. Neno hili likiwa kweli juu ya Abrahamu, ni kweli juu ya wazao wake wachaguliwa vilevile. Wamewekwa kwa pahali pa mapendeleo mbele ya Mungu.

Mfano wa pili ni **shina na matawi**. **Kama shina** likiwekwa kwa Mungu, ni **vivyo hivyo na matawi**. Abrahamu ndiye **shina**, maana yake Mungu alimweka mbali kuanza chama mpya, mbali na Mataifa. Abrahamu akiwekwa mbali, ni vivyo hivyo na wazao wake.

11:17 Mtume Paulo anaendelea kusema juu ya mfano wa **shina na matawi**.

Matawi yaliyokatwa ni mfano wa sehemu wasioamini ya makabila kumi na mawili ya Israeli. Kwa sababu walikataa Masiya waliondoshwa kwa pahali pao pa upendeleo kama watu wachaguliwa wa Mungu. Lakini **nusu tu ya matawi** yaliondoshwa. Baki la taifa (Paulo alikuwa mmoja wao) walikuwa wamepokea Bwana.

Mzeituni wa pori ni mfano wa Mataifa yote pamoja, kama taifa moja. **Waliingizwa** ndani ya mzeituni.

Walishiriki na shina na unono wa **mzeituni**. Mataifa walishiriki katika pahali ya upendeleo ambapo Waisraeli walipewa mbele. Baki la Israeli wanaoamini wanakaa kushiriki ndani ya pahali pale pamoja nao hata sasa.

Sharti tufahamu kwamba ndani ya mfano huu wa **mzeituni**, shina lake si *Israeli*, lakini jamii ya mapendeleo ya Mungu kwa mia za miaka.

Inatupasa kufahamu vilevile kwamba mtawi wa **mzeituni wa mwitu si kanisa**, lakini Mataifa yote pamoja.

Paulo alikuwa ameonyesha mbele kwamba haiwezekani kwa waamini kuondoshwa katika upendeleo wa Mungu (Rom. 8:38, 39).

Wakati tunaposema juu ya “shina la upendeleo” tangu mia za miaka, maana yake nini? Mungu alikusudia kwa watu fulani kukaa karibu zaidi naye. Watawekwa mbali na baki la dunia, na kubarikiwa na mapendeleo mengine. Kwa kila tarehe Mungu atakuwa na watu wengine watakaokuwa karibu zaidi naye.

Taifa la Israeli walikuwa wa kwanza ndani ya shina hili la upendeleo. Walikuwa watu ambao Mungu alichagua zamani kuwa watu wake hapa duniani. Kwa sababu walikataa Masiya, **mengine ya matawi haya yаликатва**, na kwa sababu hii walipoteza pahali pao pa “mwana mpendwa.” Mataifa **waliingizwa** ndani ya mzeituni na kushiriki pamoja na waamini Wayuda **ndani ya unono wake**. Shina linalrudisha mawazo yetu kwa Abrahamu, mwanzo wa shina la upendeleo. **Unono** wa mzeituni unasema juu ya mavuno makubwa ya zeituni na mafuta yao. Hapa **unono** unasema juu ya mapendeleo ya kukaa ndani ya **mzeituni**.

11:18 Lakini haifai Mataifa **куjisifu** na kufikiri wao wanastahili kupita Wayuda. Si Mataifa walioanza shina la upendeleo, lakini ni kwa sababu ya shina la upendeleo walikubaliwa ndani yake.

11:19 Paulo alijua mbele kwamba mtaifa ambaye alizungumuza naye **atasema**, “Matawi **Wayuda walikatwa ili mimi** na Mataifa wengine tuweze **kuingizwa**.”

11:20 Mtume alikubali kwamba masemo haya ni kweli kwa sehemu. Matawi Wayuda **walikatwa** na Mataifa waliingizwa. Lilitokea kwa sababu ya

kutokuamini kwa Wayuda, si kwa sababu Mataifa walistahili kupita Wayuda. Mataifa waliingizwa, kama taifa, kwani walismama kwa sababu ya imani yao. Semo hili **unasimama kwa sababu ya imani yako**, linatufikirisha kwamba Paulo alisema juu ya waamini wa kweli. Labda hii si maana yake kabisa. Mataifa walismama kwa njia moja tu, ndiyo walionekana kuwa na **imani** kupita Wayuda. Hivi Yesu ali-sema na akida Mtaifa, “Sikuona imani kubwa namna hii, hata katika Israeli” (Lk. 7:9). Na kwa wakati wa nyuma Paulo alisema kwa Wayuda katika Roma, “Basi ijulikane kwenu ya kuwa wokovu huu wa Mungu ulipelekwa kwa Mataifa, nao watasikia” (Mdo. 28:28). Ona semo hili, “nao watasikia.” Hata wakati wa sasa Mataifa ni tayari kupita Wayuda kupokea Habari Njema. **Kusimama** ni mbalimbali na *kuanguka*. Taifa la Israeli walikuwa wameanguka toka pahali pao pa upendeleo. Mataifa walikuwa wameingizwa ndani ya pahali pale.

Lakini mtu anayefikiri anasimama akae na ange asianguke. Mataifa wasijisifu, **lakini** wakae na **woga**.

11:21 Kama Mungu **hakuachia** matawi ya asili ndani ya shina la upendeleo, hakuna sababu kufikiri kwamba **ataachia** matawi ya mzeituni wa mwitu kama wakienda mbali naye.

11:22 Hivi mfano wa mzeituni unaonyesha maneno mawili yaliyo mbalimbali kabisa katika tabia ya Mungu – **wema wake**, na **ukali wake**. **Ukali** wake ulionekana kwa njia ya kuondosha Israeli toka pahali pao pa taifa pendelewa. **Wema** wake ulionekana wakati alipogeuka kwa Mataifa na Habari Njema (ona Mdo. 13:46; 18:6). Lakini hata **wema** huu kwa Mataifa ungegeuka, nao wataondoshwa kama

wasipokaa kupokea Habari Njema na roho tayari kama wakati Mwokozi alipohubiri saa alipokuwa duniani (Mt. 8:10; Lk. 7:9).

Tukae kukumbuka kwamba Paulo hasemi juu ya kanisa au juu ya waamini mmoja mmoja. Anasema juu ya Mataifa. Hakuna neno linaloweza kutenga Mwili wa Kristo toka Kichwa chake kamwe, na hakuna neno linaloweza kutenga mwamini toka mapendo ya Mungu, lakini inawezekana kwa Mataifa kuondoshwa toka pahali pao pa upendeleo pa wakati wa sasa.

11:23 Wala si lazima kwa Israeli kukatwa daima toka pahali pa upendeleo. **Kama** taifa hili wakiacha **kutokuamini** kwao, hakuna neno linaloweza kuzuiza Mungu asiwarudishe kwa pahali pao pa upendeleo pa mbele.

11:24 Ingekuwa nyepesi kwa Mungu kurudisha Israeli kuwa watu wake wenyewe upendeleo kupita kuweka Mataifa kwa pahali pale. Waisraeli walikuwa matawi ya kwanza ndani ya mti mpendelewa wa Mungu, hivi waliitwa **matawi ya asili**. Matawi ya Mataifa yalitoka kwa mzeituni wa **asili** wa pori. Kuingiza **tawi la mzeituni wa pori** ndani ya mzeituni uliopandwa ni mbali na hali ya asili. Kuingiza matawi ya kwanza ndani ya mzeituni wa mbele uliopandwa ni neno jepesi.

11:25 Sasa Paulo anafunua ya kwamba taifa la Israeli litarudishwa kweli kwa wakati wa kuja. Habari hizi zilikuwa **siri** mbele – ndiyo kweli watu wasiyoweza kujua kufika wakati ule. Paulo anaifunua sasa kusudi waamini Mataifa wasijione kuwa **wenye akili**, na kuzarau Wayuda. Hizi ndizi habari za **siri hii**:

Sehemu ya Israeli wasioamini tu **walipatwa na upofu**, si taifa zima.

Watacaa na upofu huu kwa wakati tu, mpaka **utimilifu wa Mataifa** ume-fika. **Utimilifu wa Mataifa** ndio

wakati mwamini wa mwisho atakapowingia kanisa, na wakati Mwili mzima wa Kristo utakapopelekwa mbinguni. **Utimilifu wa Mataifa** ni mbali na nyakati za Mataifa (Luka 21:24). **Utimilifu wa Mataifa** na kupelekwa kwa Kanisa mbinguni ni kwa saa moja. “*Nyakati za Mataifa*” ni muda mzima wakati Mataifa walipotawala Wayuda, kuanza na wakati Wayuda walipohamishwa na kufungwa na Wababeli (2 Mam. 36:1-21), na kufika wakati Kristo atakaporudia dunia kutawala.

11:26 Upofu wa sehemu wa Israeli ambaa walihukumiwa nao mbele, utaondolewa wakati kanisa litakapolelekwa mbinguni, lakini Waisraeli wote hawataokolewa mara moja. Wayuda wengine wataokolewa kwa wakati wa Mateso, lakini baki wachaguliwa zima hawataokolewa kufika wakati Kristo atakaporudia dunia kama Mfalme wa wafalme na Bwana wa wabwana.

Paulo alisema **Israeli wote wataokolewa**, maana yake **Israeli wote wenye imani**. Sehemu ya taifa wasioamini wataharibiwa wakati Kristo atakapokuja mara ya pili (Zek. 13:8, 9). Wale tu wanaosema “Abarikiwe Yeye anayekuja kwa jina la Bwana” wataachiliwa waweze kuingia ufalme.

Isaya alisema juu ya habari hizi wakati aliposema juu ya Mkombozi akikuja kwa **Sayuni** na kugeuza uovu toka Yakobo (Isa. 59:20). Ona ya kwamba hasemi juu ya Kristo akikuja kwa Betelehemu, lakini juu ya kuja kwake kwa Sayuni – maana kuja kwake mara ya pili.

11:27 Ni saa ile ile tunayosoma juu yake kwa Isaya 27:9 na Yeremia 31: 33,34, wakati Mungu atakapoondoa zambi zao kwa wakati wa **Agano** Jipy.

11:28 Hivi tunaweza kusema **juu ya Habari Njema, Israeli wamekuwa adui kwa ajili yenu. Wamekuwa adui kwa sababu waliwekwa mbali, walitengwa na**

upendeleo wa Mungu, ili Habari Njema iweze kufikia Mataifa.

Lakini kwa maneno ya habari za uchaguzi wamekuwa wapenzi kwa sababu za baba zao, ndio Abrahamu, Isaka, na Yakobo.

11:29 Wanapendwa hata sasa kwa sababu **zawadi** na **mwito** wa Mungu hazina majuto. Mungu haondoshi tena zawadi zake alizotoa mbele. Hageuzi kamwe ahadi bila masharti aliyotoa mbele. Aliwapa Waisraeli mapendeleo yanayotajwa katika 9:4,5. Aliita Israeli kuwa watu wake duniani (Isa. 48:12), mbali na mataifa yote mengine. Hakuna neno linaloweza kugeuza makusudi yake.

11:30 Zamani Mataifa **walikuwa** wakali na **waasi**, lakini wakati Israeli walipokataa Masiya, na Habari Njema ya wokovu, Mungu aligeuka kwa Mataifa na rehema.

11:31 Maneno yanayofanana na habari hizi yatatokea kwa wakati wa kuja vilevile. Wakati **rehema** ya Mungu kwa **Mataifa** itakapoamsha wivu ndani ya roho za Israeli, **rehema** itafuata uasi wao. Watu wengine wanafundisha kwamba rehema ya Mataifa kwa Wayuda itarudisha Wayuda karibu na Mungu, lakini tunajua neno hili si kweli. Taifa la Israeli litarudishwa karibu na Mungu wakati Bwana Yesu atakapokuja mara ya pili.

11:32 Wakati unaposoma shairi hili kwanza, labda utafikiri Mungu ali-hukumu Wayuda na Mataifa vilevile bila sheria kwa sababu ya kutokuamini kwoo, na ya kwamba hawakuweza kufanya kitu kugeuza hukumu hii. Mawazo haya si kweli. Wao wenyewe walikataa kuamini. Maana ya shairi hili ni hivi: Mungu aliona kwamba Wayuda na Mataifa wote walikuwa waasi, hivi aliwafunga wote katika hili hii ya kuasi, kusudi wasiwe na njia kujifungua toka hali hii ila kwa njia yeeye aliyochagua.

Kuasi kwao kulifungua njia kwa Mungu **kurehemu wote**, Wayuda na Mataifa vilevile. Lakini shairi hili halisemi kwamba watu wote watapokea wokovu. Mungu ameonyeshea Mataifa rehema, na atakuwa na rehema kwa Wayuda vilevile, lakini si watu wote wataokolewa. Mafundisho haya ya **rehema** ni juu ya mataifa mazima, si juu ya watu mmoja mmoja. George Williams anasema:

Mungu alijaribu Waebrania na Mataifa, nao wote walishindwa. Mungu akionyesha wazi kwamba havakustahili mapendeleo yake, aliwafunga katika hali ya kutokuamini ili, kwa sababu ya utajiri wa neema yake ambao hatuwezi kutambua, atawarehemu wote.¹⁵

11:33 Wimbo huu wa sifa kwa Mungu unatukumbusha maajabu yake yote yaliyofunuliwa ndani ya barua hii nzima kufika sura hii. Paulo ameeleza njia ya ajabu Mungu aliyotayarisha kwa wazalimu wenye zambi kuweza kupata wokovu bila yeeye mwenyewe kupoteza haki yake mwenyewe. Alionyesha namna kazi ya Kristo ilitokuza Mungu na kubariki watu kupita baraka ambao Adamu aliyopoteza kwa njia ya zambi yake. Alieleza namna neema inawezesha watu kuishi maisha matakatifu, ndilo neno lisilowezekana kwa sheria. Alionyesha shauri la Mungu tangu mwanzo kufika hata utukufu wa mwisho. Alieleza mafundisho ya uchaguzi wa enzi wa Mungu, na daraka ya watu. Na alionyesha haki na utaratibu wa namna Mungu aliyotendea Israeli na Mataifa. Mwisho unaofaa kabisa kwa mambo haya yote ni wimbo wa sifa na kuabudu.

Tazameni namna ya utajiri wa akili na maarifa ya Mungu!

Utajiri wa Mungu! Yeye ni mwenye tajiri ya rehema, mapendo, neema, uaminifu, uwezo, na wema.

Akili ya Mungu! **Akili** yake haina

mpaka, inatuishinda kuifahamu, haiwezekani kuisawanisha na akili nyingine yo yote, wala kuishinda.

Maarifa ya Mungu! Arthur W. Pink aliandika, “Mungu anajua maneno yote. Anajua maneno yote yanayowezekana; maneno yote kwa wakati wa sasa; maneno yote yanayotokea leo, viumbe vyote, maneno yote ya mbele, ya wakati wa sasa, na ya kuja.¹⁶

Hukumu zake **hazivumbulikani**: watu wa dunia hawawezi kuyafahamu. **Njia** zake, maana namna alivyotengeneza umbo la dunia, habari za maneno yaliyotokea (historia), ukombozi, na kuongoza mambo yote, yanashinda ufahamu wetu, sisi watu.

11:34 Hakuna kiumbe anayeweza **kujua nia ya Bwana**, ila sehemu Bwana anayochagua kufunua. Na hata sehemu hii nusu tunaona kama ndani ya kioo tu, si wazi kabisa (1 Kor. 13:12). Hakuna mtu anayeweza kutolea Mungu shauri. Hahitaji shauri letu, na shauri letu lisinalikuwa na faida kwaye (ona Isa. 40:13).

11:35 Hakuna mtu ambaye alifanyiza Mungu kuwa na deni kwake (ona Yobu 41:11). Tungeweza kumpa zawa-di gani ambayo ingelazimisha Mungu wa milele kutulipa?

11:36 Mwenyezi hahitaji kitu. Me-ma yote yanatoka kwake. Ni yeye anayetegemeza ulimwengu, na vyote vilumbwa kwa yeye. Kusudi la kila kitu ni **kumtukuza**.

Utukufu uwe kwake kwa milele.

3. KAZI YA HABARI NJEMA NDANI YA MAISHA YA WATU (Sura 12 – 16)

Ndani ya baki la barua kwa Waroma tunapata jibu kwa ulizo hili: *Inapasa wale wanaokwisha kuhesabiwa haki kwa neema kutenda namna gani ndani ya maisha yao ya kila siku?* Paulo anafundisha namna inavyotupasa kutendea waamini wengine, watu ambao

tunakaa katikati yao, adui zetu, seri-kali, na ndugu zetu walio zaifu katika imani.

A. Kujitoa mzima kwa Mungu 12:1, 2

12:1 Kuwaza sana pamoja na kubabdu juu ya **reheema za Mungu** zili-zoeleza ndani ya sura 1-11 kunatunya-yesha neno moja wazi kabisa – inatupasa **kutoa miili** yetu iwe **zabihu hai, takatifu**, na ya **kupendeza Mungu**. **Miili** yetu ndiyo viungo vyote vya mwili, na maisha yetu mazima.

Kujitoa mzima ni **utumishi** wetu **ulio na maana**. Ni **utumishi** wetu **ulio na maana** kwa sababu kama Mwana wa Mungu alinikufia, neno dogo zaidi ninaloweza kufanya ni kuishi kwa ye. C.T. Studd, mwingelesi Mkristo mmoja na mshindani wa michezo wa kujulikana sana, alisema, “Kama Yesu Kristo ni Mungu, na alinikufia, hakuna zawadi ninayoweza kumtolea ni kubwa zaidi.”¹⁷ Wimbo wa kujulikana, ulio-andikwa na Isaac Watts, unasema, “Mapendo ya ajabu ya Mungu yanastahili kupokea moyo wangu, maisha yangu, na vyote nilivyo navyo.”

Tafsiri nyingine kwa **utumishi ulio na maana** ni “ibada ya roho.” Kama waamini-makuhani hatutokei mbele ya Mungu na vitumba vya nyama zili-zochinjwa, lakini na zabihu ya roho, ndiyo maisha ambayo tunamtolea. Tunamtolea utumishi wetu vilevile (Rom. 15:16), sifa yetu (Ebr. 13:15), na mali yetu (Ebr. 13:16).

12:2 Halafu Paulo anatuonya vile-vile **tusifananishwe kwa namna ya dunia hii**. Wakati tunapofikia ufalme wa Mungu, inatupasa kuachana na mawazo na desturi za dunia.

Maana ya **dunia** hapa ni chama ambacho watu walitayarisha kwa ushirika wao na kufurahi bila Mungu. Ni ufalme wa uadui na Mungu. Shetani

ni mungu mkubwa wa dunia hii (2 Kor. 4:4; Yn. 12:31; 14:30; 16:11). Wasioamini wote ni ndani ya ufalme wake. Anajaribu kuvuta na kufunga watu kwa njia ya tamaa ya macho, tamaa ya mwili, na kiburi cha uzima (1 Yn. 2:16). Dunia hii ina desturi, muziki, dini, furaha, na michezo yake, na inataka watu wote kukubali maneno haya na kushirikiana nayo. Inachukia wale wasiopatana nayo – kama Kristo na wafuata wake.

Kristo alikufa kutuponyesha toka **dunia hii**. Dunia imesulibishwa kwetu, na sisi tumesulibishwa kwa dunia. Haifai hata kidogo kwa waamini kupenda dunia. Mtu ye yote anayepeenda dunia ni adui ya Mungu.

Waamini si wa dunia hii kama vile Kristo si wa dunia. Lakini wanatumwa duniani kutoa ushuhuda kwamba kazi zake ni mbaya, na ya kwamba watu wote wanaoamini Bwana Yesu Kristo wanaweza kuokolewa. Haitoshi kwa sisi kutengwa tu na dunia. Zaidi ya ile inatupasa **kugeuzwa kwa kufanya upya nia zetu**, na kufikiri namna Mungu anavyofikiri, kama inavyofunu-liwa ndani ya Biblia. Halafu tunawaza kujuana na kuongozwa na Mungu ndani ya maisha yetu. Na tutaona kwamba **mapenzi** yake si ya kuchukiza, lakini ni **mema, na ya kupe-ndeza, na makamilifu**.

Hivi tunaona hapa njia tatu kujulisha mapenzi ya Mungu. **Kwanza** ni kumtolea mwili wetu; ya *pili* ni kujitenga na dunia, na ya *tatu* ni kugeuzwa kwa kufanya upya nia yetu.

B. Utumishi kwa njia ya zawadi za roho (12:3-8)

12:3 Paulo anasema hapa **kwa neema aliyopewa** akiwa mtume wa Bwana Yesu. Atasema juu ya maneno namna namna, mengine mema na mengine mabaya.

Kwanza anasema kwamba hakuna

neno ndani ya Habari Njema litakilosukuma mtu kujivuna. Anatuonya kutumika na unyenyekevu na zawadi tulizopewa. Haifai tufikiri kamwe kwamba tuko watu wakubwa. Tufahamu kwamba kila mtu ni namna nyingine, na ya kwamba sisi sote tumepewa kazi fulani kufanya kwa Bwana wetu. Ingetupasa kufurahi juu ya **pahali ambapo Mungu alitugawia** katika Mwili wa Kristo, na ingetupasa kutumika na nguvu yote na zawadi zetu ambazo Mungu anatupa sisi.

12:4 Mwili wa mtu una **viingo vingi**, na kila kiungo kimepewa kazi fulani. Mwili utakuwa na afya njema kama kila kiungo kikifanya kazi yake vizuri.

12:5 Ni vivyo hivyo ndani ya **mwili wa Kristo**. Kuna umoja (**mwili mmoja**), tofauti (**vingi**), vinavyotegemeana (**kila mmoja kwa mwenzake**). Zawadi zote tulizo nazo si kwa faida yetu au kwa kujivuna juu yao, lakini ni kwa kusaidia **mwili**. Hakuna zawadi inatosha peke yake, na hakuna zawadi isiyohitajiwa. Wakati tunapofahamu maneno haya yote, tunawaza kwa akili (12:3).

12:6 Halafu Paulo anatoa mafundi-sho juu ya namna gani kutumika na nyingine za **zawadi** hizi. Hataji zawadi zote.

Tunapewa **zawadi** namna mbalimbali **kwa kadiri ya neema tuliyopewa**. **Neema** ya Mungu inatolea watu mbalimbali **zawadi** namna mbalimbali. Na Mungu anatoa nguvu, au anatuwezesha kutumika na **zawadi** zetu. Inatupasa kutumika vizuri na zawadi ambazo Mungu alitutolea kama wakili wema.

Sharti wale waliopewa zawadi ya **unabii** watabiri kwa kadiri ya **imani** yao. Nabii ndiye anayesema kwa ajili ya Mungu, na kutangaza neno la Bwana. Labda ni kutabiri maneno yatakayotokea, lakini unabii si juu ya

habari za kuja tu. Mwandishi mmoja, jina lake Hodge, aliandika kwamba kwa wakati wa mwanzo wa kanisa manabii walikuwa “watu walioongozwa na Roho ya Mungu, na walitoa habari toka Mungu juu ya kweli fulani ya doctrine, kazi fulani ambayo inapasa kufanywa, matokeo kwa wakati wa kuja, vivi hivi.”¹⁸ Mafundisho yao yanachungwa ndani ya Agano Jipy. Hii ndiyo imani walijopewa watakatifu mara moja (ona Yuda 3), na hakuna mafundisho toka Mungu yatakayongezwa juu yake. Hivi kwa wakati wa sasa nabii ni mtu anayetangaza nia ya Mungu iliyo funuliwa ndani ya Biblia. Strong anasema:

“Kwa wakati wa sasa unabii wa kweli unatoa mara ya pili habari ambazo Kristo alitangaza mbele. Ni kutangaza na kueleza kweli zilizofunuliwa mbele ndani ya Maandiko.”¹⁹

Inatupasa sisi tulio na zawadi ya **unabii** kutabiri kwa **kadiri ya imani yetu**. Labda maana yake ni kupatana na mafundisho ya Kristo ndani ya Maandiko. Au ni kwa kipimo ya imani tuliyopewa na Mungu.

12:7 Maana ya **utumishi** ni kazi mwamini wo wote anayoweza kufanya kwa Bwana. Si kazi ya wenye daraja kanisani tu. Mtu mwenye zawadi ya **utumishi** ni mwenye roho ya utumishi. Yeye ni tayari kusaidia kila mara anapopata njia.

Mwenye kufundisha, ndiye mwaliimu, ni mtu anayeweza kueleza Neno la Mungu, na kuonyesha kama ikipasa Neno hili kuzaa matunda gani ndani ya roho za wasikiasi.

12:8 Kuonya ni zawadi ya kumsha roho za watakatifu waachane na kutenda ubaya wo wote, na waende mbele kutumikia Kristo katika utakatifu na kufanya kazi kubwa mpya kwaye.

Ni Mungu ambaye anatuwekeea

zawadi ya *kutoa*, kutambua mahitaji ya watu wengine, na kuwasaidia. Inatupasa kufanya hivi **na ukarimu**.

Zawadi ya *kusimamia* ni sehemu ya kazi ya wazee wa kanisa (na hata na watumishi wa kanisa vilevile). Mzee ni kama mchungaji anayesimama mbele ya kundi na kuwaongoza na uangalifu na **bidi**.

Zawadi ya kuonyesha **rehema** inatolewa na Mungu. Ni uwezo kusaidia watu wanaotaabishwa. Ingepasa watu walio na zawadi hii kutumika nayo **na furaha**. Ndiyo, ingetupasa sisi sote kuwa na rehema kwa watu, pamoja na roho ya furaha.

Siku moja mwanamke mwamini alisema, “Wakati mama yangu alipogeuka mzee na alihitaji kusaidiwa, mume wangu na mimi tulimwomba kuja kukaa pamoja nasi ndani ya nyumba yetu. Nilifanya maneno yote kumwikalisha vizuri. Nilipika chakula chake na kuvua mavazi yake. Tulusafiri ndani ya motakaa pamoja, na nilijaribu kumpatia vitu vyote alivyohitaji. Lakini sikuwa na furaha rohoni. Kuchunga mama kulikula saa nydingi nilizowenza kukaa pamoja na jamaa yangu mbele. Mara nydingine mama alisema nami, ‘Kwa sababu gani hukai na furaha sasa kama mbele? Kwa sababu gani hucheki kwa wakati wa sasa?’ Ndiyo, nilikuwa na rehema, lakini si pamoja na furaha.”

C. Namna gani kutendea waamini na wasioamini (12:9-21)

12:9 Sasa Paulo anatajaa nydingine za desturi zinazofaa kwa kila mwamini kuwa nazo ndani ya mwenendo wake na Wakristo wengine na wasioamini.

Mapendo yawe **pasipo udanganyifu**. Sharti tupende na roho ya kweli, si kwa kuonekana tu.

Inatupasa **kuchukia** namna zote za uovu na **kuambatana** nalo lililo **jema**. Inatupasa **kuchukia** maneno na matendo

yote yanayokosa mapendo, matendo ya uovu na kuchukia. Lakini **jema** linasema juu ya kila neno linaloonyesha mapendo yasiyo ya ulimwengu huu.

12:10 Inatupasa kuwa na mapendo ya kweli kwa waamini wenzetu.

Ingetupasa kufurahi kuona watu wengine wakipata heshima kupita sisi. Wakati siku moja mtumishi wa Kristo, wa kujulikana, alipoingia nyumba kwa kuhubiri, watu wote walimtolea sifa na sauti kubwa. Alisimama kando mara moja na kushiriki ndani ya matoleo ya sifa kwa sababu alifikiri sifa yao ili-kuwa kwa watu wengine watako-ingia nyumba nyuma yake.

12:11 Shairi hili linatukumbusha masemo ya Yeremia 48:10: "Alaaniwe mtu anayefanya kazi ya BWANA kwa ulegevu!" Tumtumikie na bidii.

12:12 Si neno kama tukiwa na hali gani, tunaweza, na ingetupasa, **kufurahi kwa tumaini** – tukitazamia kuja kwa Mwokozi, ukombozi wa miili yetu, na utukufu wetu wa milele. Tunaagizwa **kusubiri katika mateso** – maana kuyavumilia na uhodari. Kustahimili na roho namna hii ni njia ya pekee inayoweza kugeuza taabu hii **kuwa utukufu**. **Sharti tudumu katika kuomba**. Kazi ya Bwana inaendelea vizuri, pamoja na kushinda, kwa sababu ya **maombi**.

Wakati tunapoomba, Roho Mtakatifu anajaza maisha yetu na uwezo, na mioyo yetu na salama. Wakati tunapoomba kwa jina la Bwana Yesu, tunafikia Mwenyezi karibu zaidi inayowezekana kwa mtu wa dunia kuweza kufika angali yeye ni kwanza duniani. Hivi haifai kwetu kulegea katika maombi.

12:13 Kuna **waamini** wenge mahitaji pahali pote, ndio wenge kukosa kazi, wale waliomaliza mali yao kwa njia ya kulipa waganga na dawa, watumishi wa Mungu wanaotumikia Bwana kwa pahali pasipojulikana na

wasiosaidiwa na waamini wengine, wazee wenye upungufu wa mali. Inapasa viungo vya Mwili wa Kristo, ndio waamini, kusaidia wenye mahitaji.

Sharti tupokee wagoni na furaha, si neno kama kufanya hivi kunatu-ongezea kazi, na kupunguza vyakula na mali yetu. Haifai tusahau ya kwamba wakati tunapopokea watu wa Mungu, ni sawasawa na kupokea Bwana mwenyewe. Ingepasa nyumba zetu kuwa kama nyumba ile katika Betania, pahali Yesu alipopenda kufika.

12:14 Tunaagizwa kutendea mema wale ambao wanatutesa. Haifai tuwateendee mabaya namna walivyotutendea sisi. Tunahitaji kuwa na uwezo toka Mungu kutuwezesha kutendea na adabu mtu ambaye anatumizwa. Tabia yetu ya zamani inatusukuma kulaani na kulipa maovu na maovu.

12:15 Ni vizuri kuweza kushiriki ndani ya furaha na huzuni za watu wengine. Ni jaribu kwetu kuwa na wivu wakati watu wengine wana-pofurahi, na kukosa kusaidia wenge huzuni. Mungu anataka tushiriki ndani ya furaha na huzuni za watu ambao tunakaa katikati yao.

12:16 Maana ya **kuwa na nia moja ninyi kwa ninyi** haiko ya kwamba inapasa mawazo yetu kuwa sawasawa juu ya kila neno. Ni kukaa na upatano mzuri pamoja.

Inatupasa kuepuka kuwa na majivuno. Vizuri tutendee watu wanyenye-kevu namna tunavyotendea wenge mali na heshima. Wakati Mkristo mmoja mwenye kujulikana alipofikia mji pahali alipoitwa kuja kuhubiri, viongozi wa kanisa lile walikutana naye wampeleke kwa hoteli nzuri sana. Aliuliza kama ilikuwa desturi ya wanani kupokea wahubiri nyumbani mwao. Wakristo walijibu kwamba ni mume na mke wazee waliokaa karibu, ndani ya nyumba ndogo. Mkristo mge-

ni alijibu, “Ningependa zaidi kukaa nyumbani mwao.”

Mtume anatuonya vilevile **tusiji-wazie kuwa wenze akili**. Tukumbuke kwamba hatuna kitu tusichopokea. Neno hili litatusaidia kuepuka kiburi.

12:17 Ni desturi ya watu wa dunia kulipa mtu **ubaya kwa ubaya** aliotenda. Haifai kwa Wakristo kufurahi kujilipiza kisasi, lakini kutenda kwa haki wakati wo wote, na hata kama wakitendewa mabaya. Maana ya **ku-angalia ni kuweka roho, au kufanya yaliyo mema**.

12:18 Haifai Wakristo kuwa wenze kukasirisha watu bure. Haiwezekani kutimiza haki ya Mungu kwa njia ya kufanya vita na gazabu. Ingetupasa kupenda salama, kufanya salama, na kuwa na salama. Wakati tunapokwisha kuumiza roho ya mtu mwagine, au wakati mtu mwagine alipokwisha kutuumiza sisi, shart tujaribu kwa kila njia kutengeneza neno hili, tuweze kupatana tena vizuri.

12:19 Haifai tujilipize kisasi kwa mabaya tunayotendewa. Labda maana ya **kukiacha kwa gazabu** ni kuacha *Mungu* kutengeneza neno hili kwa ajili yako, au labda maana yake ni kwa wewe kunyenyeka tu ubaya uliotendewa bila kushindana na mwenye kuutenda. Ni kama baki la shairi hili linasimamia maana ya kwanza – ndiyo kuacha **gazabu** ya Mungu kutengeneza neno lenyewe. Ni haki ya Mungu kujilipiza **kisasi** na haifai kwa sisi kumzuiza. Yeye atalipiza mtenda mabaya kwa saa nzuri, na kwa namna inavyofaa.

12:20 Lakini Wakristo hawaepuki kujilipiza kisasi tu, lakini wanatenda mema vilevile. Hawaharibu adui zao na jeuri, lakini kwa njia ya kuwanyeshea mapendo wanawaongoza kupata wokovu. Wanakulisha **adui** wakati alipo na **njaa** na kumkunywesha saa ya kiu, na kwa njia hii

wanaweka **makaa ya moto juu ya kichwa** cha mtu mwenyewe. Ni mfano wa kumpatisha haya kwa uadui wake, na kumshangaza na wema ambao usiotazamiwa.

12:21 George Washington Carver, mwenye elimu wa science, alisema, “Sitaacha kamwe mtu mwagine kuharibu maisha yangu kwa njia ya kunilazimisha kumchukia.”²⁰ Alikuwa mwamini na hakukubali ubaya kumshinda.

Lakini ushinde ubaya kwa wema. Ni desturi ya mafundisho ya Wakristo kukataza maneno mabaya, lakini zaidi ya kufanya hivi, kutoa maonyo ku-tenda yaliyo mema. Inawezekana kushinda **uovu na wema**. Wema ndio silaha ambayo tunahitaji kutumia mara na mara.

D. Na Serikali (13:1-7)

13:1 Ni lazima kwa watu wanaokwisha kuhesabiwa haki kwa njia ya imani, **kutii** serikali. Inapasa watu wote kufanya hivi, lakini mtume Paulo anafikiri zaidi juu ya waamini. Mungu alisimamisha utawala wa watu nyuma ya garika, wakati alipoagiza, “Yeye anayemwanga damu ya mtu, kwa mtu vilevile damu yake itamwangwa” (Mwa. 9:6). Amri hii iliwapa watu mamlaka kuhukumu matendo yanayovunja sheria, na kuazibu waasi.

Kila pahali chama cha watu wanapokaa pamoja na utaratibu, inapasa watu kunyenyeka mwenye amri. Kama isipokuwa hivi, kutakuwa na fujo na machafuko, na watu hawataweza kudumu kuishi na salama kwa siku nyingi. Hivi Mungu alisimamisha mamlaka ya wenze amri, na hakuna mamlaka ila ile inayosimamishwa kwa kutaka kwake. Si kusema kwamba anakubali maneno yote watawala wa dunia wanayofanya! Hakubali rushwa na ukali na uzalimu! Lakini hata hivi **serikali inayokuwa, imewekwa na Mungu**.

Waamini wanaweza kuishi maisha ya kushinda hata ndani ya inchi inayotawaliwa na watu waliochaguliwa na wenyehi wa inchi, au na mfalme wa jamaa ya asili, au na serikali kali. Hakuna mamlaka ya dunia ni nzuri kupita watu wake wenyehi amri, hivi hakuna mamlaka duniani iliyo kamilifu. Mamlaka njema ya pekee ni ufalme wa Mfalme Bwana Yesu Kristo. Ni vizuri tukumbuke kwamba Paulo aliandika mafundisho haya juu ya kunyenyeka watawala wa dunia wakati mtu mwovu sana, Nero, alipokuwa mfalme. Wakristo walipata taabu nyiingi kwa wakati wa utawala wake. Nero aliwashitaki juu ya moto ulioteketeza nusu ya mji Roma (labda yeye mwenyewe aliagiza moto huu kuwashwa). Alilazimisha wengine wa waamini kuingizwa ndani ya lami, na kuwakishwa moto wawe taa hai kuleta nuru kwa karamu zake za ulafi na ulevi na uasherati. Wengine walishonwa ndani ya ngozi za nyama, na kutupwa kwa imbwa wakali ambazo ziliwapasua na kuwameza.

13:2 Hata hivi mtu ye yote anayesi mamlaka anaasi serikali ambayo Mungu alisimamisha. Mtu ye yote anayeshindana na amri ya Mungu anastahili kuazibiwa.

Lakini Mkristo anaweza kuasi kwa sababu moja. Si lazima kwa Mkristo kutii serikali kama akiagizwa kufanya zambi, au neno lo lote litakaloamsha shaka ndani ya roho za watu juu ya uaminifu wake kwa Yesu Kristo (Mdo. 5:29). Hakuna serikali iliyo na ruhusa kutawala zamiri ya mtu. Hivi mara nyingine, saa mwamini anapotii Mungu, anakasirisha watu. Halafu inampasa kuwa tayari kuvumilia azabu bila kunungunika. Haifai ashindane na serikali kamwe, wala kufungana na wengine wanaojaribu kuiharibu.

13:3 Watu wanaotenda haki hawa-hitaji kuogopa serikali. Ni wale wana-

oasi sheria wanaohitaji kuogopa azabu. Hivi kama mtu akitaka kuishi na salama, bila mashitaki mbele ya wamuza kutii sheria na maagizo ya serikali. Halafu wakubwa watamfurahia, si kumhamakia.

13:4 Mwenye mamlaka ni **mtumishi** wa Mungu anayesimamia Bwana. Labda hajuanini na Mungu yeye mwenyewe, lakini hata hivi yeye ni mtumishi aliyewekwa na Mungu. Hivi wakati Daudi aliposema juu ya mfalme mwovu Saulo, alimwita tena na tena mpakaliwa wa Bwana (1 Sam. 24:6,10; 26:9, 11, 16, 23). Hata kama Saulo alijaribu kumwua tena na tena, Daudi hakuruhusu watu wake kuumiza mfalme. Kwa nini? Kwa sababu Saulo aliwa mfalme aliyewekwa na Mungu.

Watawala wakiwa watumishi wa Mungu, kazi yao ni kusaidia watu kukaa **vizuri** (mema) – na salama, bila hatari. Kama mtu akiweka roho kabisa kuasi sheria, ajue kwamba ataazibowi, kwa sababu serikali ina amri kumhukumu na kumwazibu. Maneno haya: “**habebi upanga bure**” yanaonyesha wazi amri ambayo Mungu alitolea serikali. **Upanga** si fimbo ya mfalme tu, lakini ni mfano wa uwezo mkubwa zaidi wa mtawala – ndio kuhukumu mtu kuuawa. Hivi tunaona kwamba watu hawakuhukumiwa kufa kwa wakati wa Agano la Kale tu, lakini kwa wakati wa Agano Jipy ailevile. Shairi hili la Agano Jipy linaonyesha wazi kwamba serikali ina amri kuondosha uzima wa mtu aliyetenda neno baya sana linalostahili mauti. Watu wanashindana na mawazo haya kwa njia ya kutaja Kutoka 20:13: “Usiue.” Lakini shairi hili linasema juu ya kuua mtu na kusudi saa ya magomvi. Kuna agizo ndani ya sheria ya Agano la Kale kuhukumu mtu kufa kwa zambi mbaya sana.

Mtume alitukumbusha tena kwa-

mba mtawala ni **mtumishi wa Mungu**, lakini mara hii anaongeza kwamba **analipiza kisasi mwenye kufanya mabaya**. Hivi yeze ni **mtumishi** wa Mungu kwetu **kwa mema**, lakini anatumikia Mungu vilevile kwa njia ya kuazibu wale wanaoasi sheria.

13:5 Hivi inatupasa kutii serikali kwa sababu mbili – kuepuka azabu, na kuweza kuwa na **zamiri** safi.

13:6 Pamoja na kutii serikali, inatupasa kuisaidia kwa njia ya kulipa **kodi**. Ni faida kwa sisi kukaa pamoja katika jamii taratibu ya watu wanaotii sheria, na kuchungwa na polisi, na wenyе kazi ya kuzima moto mjini. Hivi inatupasa kushiriki ndani ya mali inayohitajiwa kulipa mishahara yao. Watu wa serikali wanatumika na saa na akili yao tuweze kukaa na salama, na wanastahili kusaidiwa na mali kwa mahitaji yao.

13:7 Ndiyo, waamini ni wenyеji wa mbingu (Flp. 3:20), lakini hata hivi ni sharti kwao kutimiza madaraka yao kwa serikali. Sharti walipe **kodi** kwa sehemu ya mali waliyopokea kwa njia ya mishahara, biashara, ushuru, vivi hivi. Sharti wawe na **heshima** na woga kwa wasimamizi wa sheria.

Haifai kamwe kwa Mkristo kushiriki na watu wengine kwa kuzarau au kuaibisha mfalme, au waziri mkuu. Imeandikwa, “Usiseme mabaya juu ya mkubwa wa watu wako.” (Mdo. 23:5).

E. Juu ya wakati wa kuja (13:8-14)

13:8 Sehemu ya kwanza ya shairi hili linatufundisha kulipa deni zetu kwa saa inayofaa. Haitukatazi kuwa na deni. Mara nyingine haiwezekani kuepuka kuwa na deni. Watu wengine wenyе nyumba mjini wanapaswa kulipa kwa taa ya umeme kila mwezi, na maji, vivi hivi. Maonyo ya shairi hili ni tulipe deni hizi kwa saa nzuri bila kuziacha kuongezeka kuwa kubwa.

Lakini sharti tukumbuke maneno

mengine juu ya kuwa na deni. Haifai tuingie deni kwa vitu tusivyo hitaji kabisa. Haifai tuingie deni kwa kitu kikubwa wakati tunapojuu hatutaweza kulipa deni hii kamwe. Haifai kununua kitu na kusudi kukilipa nusu nusu kila mwezi, kwa sababu desturi hii inaongeza bei yake. Ni vizuri kuwa na mali tayari kwa kununua kitu cho chote tunachotaka kujipatia na kuepuka kuropa mali. Tukumbuke kwamba yeze anayekopa ni mtumishi wake anayekopesha (ona Mez. 22:7).

Kuna deni moja tusiyoweza kumaliza kamwe, ndiyo deni ya **mapendo**. Neno linalotafsiriwa *mapendo* katika Waroma (ila mara moja, ona Rom. 12:10) ni *agape* kwa Kiyunani, na linasema juu ya mapendo makubwa sana, mapendo yasiyojifikiri yenyewe, mapendo yanayotoka kwa Mungu, ambayo mtu anaweza kuwa nayo kwa mtu mwengine. Mwenye **mapendo** haya yanayotoka kwa Mungu hapendi mtu mwengine kwa sababu ya uzuri wake, kwani mtu yule hastahili kupeendwa hivi. Mapendo ya mtu huyu ni namna nyingine kabisa na mapendo yo yote nyingine, kwa sababu anapenda hata adui zake.

Mapendo haya yanaonekana kwa njia ya kutoa, zaidi kujinyima kwa kuweza kutoa. Tunasoma ya kwamba Mungu alipenda ulimwengu hata alitoa Mwana wake wa pekee. Kristo alipenda kanisa na kujitoa kwa sababu yake.

Kupenda ni neno la *kutaka* kwetu, si neno tunalosikia rohoni tu (kama furaha, huzuni, sikitiko, chuki). *Tunagizwa kupenda*, hivi tunaona kwamba tunaweza kuchagua kufanya hivi.

Mara nyingi tunasikia mapendo haya rohoni mwetu vilevile.

Haiwezekani kwa msiyeamini kuongyesha mapendo yale ya Mungu. Hata mwamini hawesi kufanya hivi kwa nguvu yake mwenyewe. Yana-weza kuonekana kwa uwezo wa Roho

Mtakatifu tu anayekaa ndani yake.

Mapendo haya yalionekana kwa utimilifu duniani ndani ya Bwana Yesu Kristo.

Sisi tunaonyesha mapendo yetu kwa Mungu kwa njia ya kutii maagizo yake.

Mtu **anayependa** jirani yake **ameti-miliza sheria**, ndiyo sehemu ile ya sheria ambayo inatufundisha kupenda watu tunaokaa katikati yao.

13:9 Mtume anataja matendo haya yanayokatazwa na **sheria** na yasiyofaa kwa sisi kutendea jirani yetu. Ni **uzini, uuaji**, kuiba, ushuhuda wa uwongo, kutamani. Mwenye mapendo hataharibuu mwili wa mtu mwingine na uzini; hatamwondolea uzima wake; hataiba mali yake; hatamtolea ushuhuda wa uwongo. Mwenye mapendo hatatamani vitu vya mtu mwingine.

Na kama ikiwa amri nyingine yo yote. Paulo angaliweza kutaja amri moja nyingine, ndiyo hii: “Heshimu baba yako na mama yako.” Maagizo haya yote yanaweza kujumlishwa na amri hii moja: “**Penda jirani yako kama wewe mwenyewe.**” Tendea watu wengine na mapendo namna unavyoitenda mwenyewe.

13:10 Mwenye **mapendo** hafanyii mtu mwingine **mabaya**. Anajaribu kusaidia na kuheshimu watu wote. Hivi mwenye kutenda na mapendo anatimiza amri 6-10 za **sheria**.

13:11 Mwisho wa sura hii ni manonyo kwa mwamini kukaa tayari kwa kazi ya Mungu na kuishi na usafi na utakatifu wa mwili. **Saa** inabaki nusu tu. Muda wa neema unakaribia mwisho. Sharti tuache kuwa walegevu na tuwake kwa kazi ya Bwana. **Wokovu wetu ni karibu kuliko wakati tulipoamini.** Mwokozi atakuja na kutupeleka kwa nyumba ya Baba wetu.

13:12 Muda wa sasa ni kama **usiku** wa zambi, na ni karibu kwisha. **Mchana** wa utukufu wa milele ni

karibu kupambazuka kwa mwamini. Hivi sharti **tuachane** na matendo machafu ya dunia, maana uzalimu na uovu wote. Na sharti **tuvae silaha ya nuru**, ndiyo kuishi maisha matakatif. Kuna mafundisho juu ya vipande vya silaha hii katika Waefeso 6:14-18. Ni alama za tabia mpya ya Mkristo wa kweli.

13:13 Ona maonyo ya nguvu kwa mwenendo wetu. Tukiwa watu wa **mchana**, ni lazima kwetu **kutembea** kama wana wa nuru. Mkristo anapaswa kukaa mbali na ulafi na ulevi, na usherati na tamaa mbaya, magomvi na wivu.

13:14 Neno zuri zaidi ambalo tunaweza kufanya ni **kuvaa Bwana Yesu Kristo**, maana yake kuishi namna yeze alivyoishi, na kumfuata kama mwoongozi na mfano wetu.

Pamoja na ile, **haifai tufikiri mahitaji ya mwili, kutimiza tamaa zake.** **Mwili** ndio tabia yetu ovu ya zamani inayotamani saa zote kubembelezwa na maneno ya anasa, uzini, furaha bure za dunia, ulevi, mali, vivi hivi. **Tunafikiri mahitaji ya mwili** wakati tunaponunua vitu ambavyo vinatusaidia kufanya zambi, wakati tunapoweka roho juu ya mwili kupita maneno ya roho. Haifai tufikiri mapendeleo ya mwili hata kidogo.

Hili ndilo shairi Mungu alilotumika nalo ndani ya roho ya Augustin, mwenye akili zaidi aliyependa anasa ya dunia sana. Lilimgeuza kabisa hata aliamini Kristo na kuishi maisha matakatif. Wakati aliposoma shairi 14, alijitoa kwa Bwana, na tangu wakati ule watu wanamwita “Mtakatifu” Augustin.

F. Pamoja na waamini wengine

(14:1 – 15:13)

14:1 Ndani ya 14:1–15:13 tunapata mafundisho kuonyeshea watu wa Mungu namna gani kutenda kwa maneno

yasiyo makubwa sana. Mara nyingi maneno namna hii yanaleta magomvi katikati ya waamini, lakini magomvi namna hii si mema hata kidogo.

Mkristo **zaifu** ana shaka juu ya maneno madogo yasiyo na msingi. Mara nyingi alikuwa Myuda aliyeokolewa, lakini aliyekaa kwanza na shaka juu ya kula vyakula vilivyo-katazwa kwa Wayuda, au juu ya kutumika kazi siku ya saba.

Neno la kwanza tunalojifunza ni hili: sharti Mkristo **zaifu** apokewe kanisani, lakini haifai kubishana naye juu ya mashaka yake. Wakristo wanaweza kukaa pamoa na furaha na salama bila kupatana juu ya maneno yasiyo ya lazima.

14:2 Mwamini anayefurahi ndani ya imani yake inayosimamia mafundisho ya Agano Jipy, anaamini ya kwamba vyakula **vyote** ni safi. Vinnatasawa na neno la Mungu na maombi (1 Tim. 4:4, 5). Labda mwamini mwenye zamiri zaifu ana shaka juu ya kula nyama ya nguruwe, au nyama namna nyininge.

14:3 *Neno la pili* linalohitajiwa ni kwa waamini kuwa na uvumilivu. Haifai kwa Mkristo wa kukomea katika imani **kuzara** ndugu yake aliye zaifu. Na haifai ndugu zaifu **kuhukumu** Mkristo anayependa kula vyakula vinavyokatazwa na dini ya Wayuda. **Mungu amempokea** katika jamaa yake na salama.

14:4 *Neno la tatu* ambalo inatupasa kujua ni ya kwamba kila mwamini ni **mtumishi** wa Bwana, na ya kwamba hatuna ruhusa kumhukumu. Kila mtu atasimama au kuanguka mbele ya **Bwana wake mwenyewe**. Haifai tufikiri rohoni kwamba mtu fulani hatasimama imara katika imani kwa sababu mawazo yake juu ya maneno haya hayapatani na mawazo yetu. Mawazo namna hii hayafai. **Mungu** ataweba kusimamia Wakristo wenye

imani ya nguvu, na wenye imani zaifu vilevile. Uwezo wake unatosha kufanya hivi.

14:5 Wengine wa Wakristo Wa-yuda walikaa kufikiri kwamba ni lazi-ma kwao kushika Sabato kama siku takatifu. Walikuwa na shaka juu ya kufanya kazi siku ya saba. Kwa njia hii walihesabu **siku moja kupita nyi-nge**.

Waamini wengine hawakuwa na mashaka namna hii. Waliona **kila siku kuwa sawasawa**. Hawakufikiri kwamba siku sita ni siku za kazi, na siku moja ni takatifu. Kwa mawazo yao siku zote zilikuwa takatifu.

Basi Siku ya Bwana, siku ya kwanza ya juma? Siku ile ina nafasi kubwa ndani ya maisha ya Wakristo. Tunasoma katika Agano Jipy kwamba Bwana wetu alifufuliwa siku ile (Lk. 24:1-9). Siku ya Bwana ya nyuma, Kristo alikutana na wanafunzi wake, na siku ya Bwana ya nyuma vilevile (Yn. 20:19, 26). Roho Mtakatifu alikuja Siku ya Pentekote, ndio siku ya kwanza ya juma. Pentekote ilikuwa siku za Bwana saba nyuma ya siku kubwa ya Matunda ya Kwanza (Law. 23:15,16; Mdo. 2:1), iliyo mfano wa ufufuko wa Kristo (1 Kor. 15:20, 23). Wanafunzi walikutana kuvunja mkate siku ya kwanza ya juma (Mdo. 20:7). Paulo alisema na Wakorinto kukusanya sadaka siku ya kwanza ya juma. Hivi katika Agano Jipy Siku ya Bwana inaonekana kweli kuwa siku kubwa. Lakini haikuwa siku ya *lazima*, kama sabato, lakini siku ya *mapendeleo*. Hatufungwi na kazi ya mshahara siku ile, hivi tunaweza kutumika na siku ile kuabudu na kutumikia Bwana wetu.

Wakristo hawaagizwi hata mara moja ndani ya Agano Jipy kushika sabato. Lakini hata hivi tunaona kawaida ya siku moja ya pumziko nyuma ya siku sita za kazi.

Basi hata mtu akiwaza nini juu ya mambo haya, neno kubwa ndilo hili: **kila mtu ajue kabisa katika akili zake mwenyewe.** Sharti tufahamu kwamba maonyo haya ni juu ya maneno yaliyo mema. Lakini, wakati tunaposema juu ya mafundisho wa **msingi** wa imani ya kikristo, hakuna nafasi kwa shauri la kila mtu mmoja mmoja. Hata hivyo si mbaya kwa watu kuwa na mawazo namna namna juu ya maneno yasiyo mazuri wala mabaya. Haifai maneno namna hii kuzuiza mtu asipokewe kanisani.

14:6 Ndani ya shairi hili, mtu yule **anayeshika siku** ni mwamini Myuda anayekaa kwanza na zamiri mbaya juu ya kufanya kazi siku ya sita. Hafikiri kwamba inampasa kushika sabato kwa kuweza kuokolewa, au kusudi asipoteze wokovu wake, lakini ya kwamba anapendeza **Bwana** kwa njia ya kushika siku ile. Vivyo hivyo mtu **asiyeshika siku** anafanya hivi kuhe-shimu Kristo anayetimiza mifano yote ya imani (Kol. 2:16,17).

Mtu asiyeshitakiwa na zamiri yake juu ya kula vyakula vinavyokatazwa kwa Wayuda, anainamisha kichwa chake **na kushukuru Mungu.** Mwamini mwenye zamiri zaifu anakula vyakula vile tu vinavyofaa kwa Wayuda, naye anashukuru Mungu vilevile. Wao wawili wanaomba Mungu kubariki vyakula vyao, na **Mungu** anapokea heshima na mashukuru. Hivi kwa sababu gani neno hili litazaa magomvi na mapigano?

14:7 Kristo ni Bwana wa kila sehemu ya maisha ya mwamini. Hatuishi kwa sisi wenyewe lakini kwa Bwana. Hatukufi kwa sisi wenyewe lakini kwa Bwana. Ni kweli ya kwamba maneno tunayofanya na kusema yanagusa maisha ya watu wengine, lakini neno kubwa Paulo analofundisha hapa ni ya kama ingepasa Bwana kuwa kwa pahali pa

kwanza katika maisha ya watu wake.

14:8 Kila kitu tunachofanya tungali na uzima kinatazamwa na Kristo kwa ukubali wake. Sisi tunajaribu maneno kwa namna yanavyoonekana machoni mwake. Hata wakati wa mauti, saa tunapofikia Bwana, tunajaribu kumtukuzza. Tuko mali yake tungali tunapoishi na wakati wa mauti.

14:9 Kwa sababu hii **Kristo ali-kufa, na alifufuka awe Bwana** wetu, na sisi tuwe watumishi wake amba wanamtumikia na roho za asante na furaha. Yeye ni Bwana wetu hata wakati wa kufa kwetu, saa miili yetu inapolala kaburini, na roho na nafsi zetu zinapokwisha kufika kwake.

14:10 Kwa sababu neno hili ni kweli, ni upumbavu wa Mkristo Myuda mwangalifu sana kuhukumu **ndugu** asiyeshika kalenda ya Wayuda na kula vyakula visivyokubaliwa na Wayuda. Vivyo hivyo ni vibaya kwa ndugu mwenye imani ya nguvu ku-zarau **ndugu** zaifu. Sisi sote **tutasi-mama mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo.**²¹ Hii itakuwa hukumu ya pekee ya kweli.

Hukumu hii ni juu ya *utumishi* wa mwamini, si juu ya *zambi* zake (1 Kor. 3:11-15). Ni saa ambayo kazi yake itapimwa naye atapewa zawabu. Hukumu hii si Hukumu ya Mataifa (Mt. 25:31-46), wala Hukumu ya Kiti cha Ufalme Kikubwa Cheupe (Ufu. 20:11-15), iliyo hukumu ya mwisho ya wauvu wote waliokwisha kufa.

14:11 Tuliona mbele katika Isaya 45:23 kwamba hakika sisi sote tutatokea mbele ya *bema* ya Kristo. Pale Bwana mwenyewe anasema na nguvu kwamba **kila goti litapigwa** mbele yake na kukubali kwamba yeye ni mwenye mamlaka yote.

14:12 Hivi ni wazi kwamba kila mmoja wetu atatoa habari zake mwenyewe, si habari za ndugu zetu, **mbele**

ya Mungu. Mara nyingine tunahukumu ndugu zetu mbio zaidi, bila kujuu maneno yao vizuri wala kuwa na amri kuwahukumu.

14:13 Kwa pahali pa kuhukumu Wakristo wenzetu juu ya maneno haya yasiyo maneno mabaya wala maneno ya doctrine, afazali **tukusudi** tusifanye kamwe kitu kitakachozuiza ndugu Mkristo asipate nguvu katika imani, au **kumkwalisha**.

14:14 Paulo alijua, na sisi vilevile tunajua ya kwamba vyakula vilivyo-kuwa **vichafu** kwa Wayuda walioishi kwa wakati wa sheria, si vichafu tena kwa wakati wa sasa. Vyakula tunavyo-kula vinatakaswa na neno la Mungu na maombi (1 Tim. 4:5). Maana ya kutakaswa na Neno hapa ni ya kwamba Biblia inasema wazi kwamba ni vema. Vinatakaswa na maombi wakati tunapoomba Mungu kuvibariki kwa utukufu wake, na kwa kupatisha mili yetu nguvu kwa kazi yake. Lakini ndugu zaifu akifikiri ni vibaya kwa yeYe kula nyama ya nguruwe, ni vibaya kweli kwaye kuikula. Kama akikula nyama hii ataasi zamiri ambayo Mungu alimpa.

Wakati Paulo anaposema hapa kwa-mba **hakuna kitu kichafu kwa asili yake**, sharti tufahamu kwamba anasema juu ya maneno haya *yasiyo mabaya kwa njia ya roho au dini*. Kuna vitu vingi vilivyo vichafu, kama vitabu vichafu, sinema nyingine, na usherati na uovu namna namna. Lakini Wakristo hawachafuwi kwa njia ya kula vyakula vilivyoitwa vichafu na sheria ya Musa.

14:15 Wakati ninapoketi pamoja na **ndugu** zaifu ili tule chakula pamoja, ni vizuri kwa mimi kuweka roho juu ya kula chakula fulani, nikifahamu kwamba ndugu huyu anafikiri ni kibaya? Kama nikikula chakula chenyewe, sitendi na **mapendo**, kwani mwenye mapendo hajifikiri mwenyewe, lakini mahitaji ya watu wengine. Mwenye mapendo anajinyima kitu kizuri kusudi

aweze kusaidia roho ya ndugu yake. Chakula fulani ni kitu bure wakati kinaposawanishwa na hali nzuri ya roho ya **mtu yule Kristo alikuwa kwa ajili yake**. Kama hata hivi na kiburi ninafanya maneno namna hii, matendo yangu yanaweza kuumiza kabisa imani ya ndugu zaifu. Neno hili halifai wakati tunapokumbuka bei kubwa sana ya ukombozi wa roho yake – ndio damu ya damani ya Mwana-Kondoo.

14:16 Hivi hata tukiwa na ruhusa kufanya maneno fulani, haifai tuyafanye, kama yakileta njia kwa watu wengine kutushitaki juu ya ukosefu wetu wa mapendo.

14:17 Maneno makubwa ndani ya **ufalme wa Mungu** si maagizo juu ya vyakula, lakini maneno ya hali ya roho. Mungu ndiye Mtawala mkubwa wa **ufalme huu**. Watu wote *wanaokiri kuheshimu* Mungu ni ndani ya ufalme wake, lakini kabisa kabisa ni wale tu waliozaliwa tena.

Haifai watu wa ufalme wapende vyakula na malofu sana, lakini wawe wenye maisha ya **haki, salama**, na amani, na wenye **furaha katika Roho Mtakatifu**.

14:18 Neno kubwa si kama mtu anavyokula, au kutokula vyakula gani. Akiishi maisha matakatifu, atahe-shimiwa na Mungu, na kukubaliwa na watu. Watu wanaoweka roho juu ya haki, salama, na furaha wanatumikia **Kristo** kwa njia ya kutii mafundisho yake.

14:19 Hivi tunaona kwamba kwa pahali pa kubishana juu ya maneno madogo, sharti tuweke roho kabisa juu ya kuchunga **salama** na amani ndani ya kusanyiko la Wakristo. Kwa pahali pa kuangusha wengine kwa njia ya kuweka roho juu ya maneno yaliyo ruhusa yetu, inatupasa kuweka roho zaidi juu ya kujenga wengine katika imani yao takatifu.

14:20 **Mungu** anafanya **kazi** ndani

yetu sisi sote. Ni neno la kuogopesha kuwaza kwamba tunaweza kuzuiza kazi hii ndani ya maisha ya ndugu zaifu kwa njia ya kuweka roho juu ya maneno madogo kama **vyakula**, vinyewe, au kushika siku fulani kuwa siku kubwa. Kwa mtoto wa Mungu, vyakula vyote ni safi sasa. Lakini ingekuwa vibaya kwaye kula vyakula fulani kama kwa njia hii ataumiza ndugu yake au kumkwaza ndani ya mwenendo wake kwa Kristo.

14:21 Ni vizuri zaidi kwa sisi kujinyima **nyama**, **mvinyo**, au **kitu cho chote** kingine kinachoweza kuumiza **ndugu** yangu, au kumrudisha nyuma katika imani yake. Kwa sisi kujinyima maneno yaliyo ruhusa yetu ni bei ndogo tunayoweza kulipa kwa kuchunga ndugu **zaifu**.

14:22 Mimi ni huru kula chakula cho chote kwani ninajua Mungu amekitoa ili niweze kukipokea na asante. Lakini haifai kwa mimi kujisifu bila sababu juu ya uhuru huu mbele ya wale walio zaifu katika imani. Ni vizuri kupita kwa mimi kula vyakula hivi wakati mimi ni peke yangu, na hakuna njia kwa mimi kuumiza roho za watu wengine.

Ni vizuri kwa Mkristo kufurahi katika uhuru wake, lakini ni vizuri kupita kujinyima maneno yaliyo haki yetu kusudi tusiumize watu wengine. Mtu yule anayeepuka kukwaza wengine ni mtu wa **heri**.

14:23 Lakini haifai ndugu zaifu kula chakula cho chote kama zamiri yake ikimshitaki juu yake. Ana shaka na hakuli na **imani**. Zamiri yake ikimshitaki juu ya kitu fulani, ni **zambi** kufanya kitu chenyewe.

Hata hivi maongozi ya damiri yetu si makamilifu kila mara. Ni lazima ifundishwe na neno la Mungu.

15:1 Mashairi kumi na tatu ya kwanza ya sura 15 yanaendelea na

mafundisho juu ya maneno yasiyo au mema au mabaya. Waamini toka dini ya Wayuda na waamini wa Mataifa walikuwa na mabishano, hivi Paulo aliwasihii kupatana vizuri.

Haifai wale walio wenye nguvu (maana wale wasioshitakiwa na zamiri zao juu ya maneno madogo) **ku-jipendeza wenyewe** kwa njia ya kufanya maneno haya. Kwa pahali pa kufanya hivi inawapasa kuonyeshea ndugu zao zaifu mapendo, pamoja na kukumbuka mashaka na uzaifu wao.

15:2 Haifai kwa Mkristo wa nguvu kuishi kwa ku-jipendeza yeze mwenyewe. Ni sharti kuishi **kupendeza jirani** yako, kumtenda mema, na kumpatisha nguvu katika imani.

15:3 **Kristo** ni mfano wetu. Hakuishi ku-jipendeza mwenyewe, lakini Baba yake. Alisema, “**Malaumu yao ambaao walikulaumu yaliniangukia mimi**” (Zab. 69:9). Aliwaza juu ya heshima ya Mungu tu, hivi wakati watu walipozarau Mungu, alipokea mazaraau haya kama mazaraau kwa yeze mwenyewe.

15:4 Maneno haya toka Zaburi yanatukumbusha kwamba Agano la Kale **liliandikwa kwa mafundisho yetu**. Hata kama liliandikwa kwanza kwa Wayuda, lina mafundisho ya faida sana **kwa sisi** vilevile. Kwa wakati wa masumbuko, vita, mateso na taabu, Maandiko yanatufundisha kusimama imara, na **yanatufariji**. Hivi hatuzami ndani ya mawimbi, lakini tuna **tumaini** kwamba Bwana atatushindisha.

15:5 Mafikiri haya yaliongoza Paulo kuonyesha hamu ya roho yake ya kwamba **Mungu** mwenye saburi na **faraja** atawezesha wenye nguvu na wazaifu, Wakristo Mataifa na Wayuda, kuishi pamoja na amani, **kupatana na mafundisho** na mfano wa **Kristo Yesu**.

15:6 Halafu watakatiwu watakuwa na moyo mmoja kuabudu **Mungu na Baba ya Bwana wetu Yesu Kristo**.

Neno la kushangaza kabisa! Waokolewa Wayuda na Mataifa wakiabudu Bwana na **kinywa kimoja!**

Kinywa kinatajwa mara ine ndani ya barua kwa Waroma, na kuonyesha kupatishwa nguvu kwa mwamini. Kwa mwanzo kinywa kinajaa laana na uchungu (3:14). Halafu kinywa chake kinafungwa, naye anafikishwa na hatia mbele ya Mwamuzi (3:19). Kisha anakiri na kinywa chake kwamba Yesu ni Bwana (10:9). Na mwishoni **kinywa** chake kinajaa na sifa na kuabudu kwa Bwana (15:6).

15:7 Neno kubwa moja lingine ambalo inatupasa kukumbuka ndilo hili: Hata tukiwa na mawazo mballimali juu ya maneno madogo, ni lazima kwetu **kukaribishana, namna**

Kristo alivyotukaribisha sisi. Huu ndio msingi wa kupokea mtu kanisani. Hatumpokei kwa sasbabu ametoka kanisa fulani, wala kama amekomea rohoni ama bado, wala kwa sababu ya mali, cheo, au hali yake. Sharti **tupokee** wale amba **walipokewa na Kristo**, kwa kuendeleza **utukufu wa Mungu**.

15:8 Ndani ya mashairi sita yanayofuata, mtume alionyesha kwamba utumishi wa **Yesu Kristo** ni kwa Wayuda na Mataifa. Neno hili linatufahamisha kwamba ingepasa utumishi wetu kuwa vivyo. Bila shaka Kristo alikuja kutumikia **tohara** – maana Wayuda. Mungu alikuwa ameahidi tena na tena kwamba atatumia Masiya kwa Israeli, na kuja kwa Kristo kuhakikisha kwamba **ahadi** hizi zili-kuwa **kweli**.

15:9 Lakini Kristo analeta baraka kwa **Mataifa** vilevile. Lilikuwa kusudi la Mungu kwa Mataifa kusikia Habari Njema vilevile, na kwa wale wanao-amin **kutukuza Mungu** kwa sababu ya **rehema yake kubwa**. Haifai wamaani Wayuda washangae juu ya neno hili, kwani lilitabiriwa tena na tena

ndani ya Maandiko yao. Kwa mfano ndani ya Zaburi 18:49, Daudi alitazamia mbele siku **Masiya** ataka-poimba sifa kwa Mungu katikati ya jeshi la waamini Mataifa.

15:10 Katika Torati 32:43 tunaona Mataifa wakifurahishwa na baraka za wokovu pamoja **na watu wake** Israeli.

15:11 Ndani ya Zaburi 117:1 tunasikia Waisraeli wakiita **Mataifa kusifu BWANA** kwa wakati wa utawala wa miaka elfu moja wa Masiya.

15:12 Mwishoni **Isaya** aliongeza ushuhuda wake kwamba **Mataifa** watakuwa ndani ya ufalme wa Masiya (Isa. 11:1, 10). Neno hili linatufahamisha kwamba **Mataifa** watashiriki ndani ya mapendeleo ya Masiya na Habari Njema yake.

Bwana Yesu ni **shina la Yese**, maana yeeye ni Mwumba wa Yese, si ya kwamba alitoka kwa Yese (hata kama neno hili ni kweli *vilevile*). Katika Ufunuo 22:16 Yesu anajiita mwenyewe shina na mzao wa Daudi. Akiwa Mungu, yeeye ni mwumba wa Daudi; kwa utu wake, yeeye ni mzao wa Daudi.

15:13 Halafu Paulo anamaliza mashairi haya na baraka ya neema. Anaomba **Mungu** anayeleta **tumaini** jema kwa njia ya neema, aweze kujaza watakatifu na **furaха yote na salama** katika kuamini. Labda alifikiri zaidi juu ya waamini Mataifa, lakini ni ombi zuri kwa waamini wote. Na waamini wanaozidi **katika tumaini kwa nguvu za Roho Mtakatifu** hawana saa kugombana juu ya maneno madogo. Tumaini letu lina uwezo kabisa kutufunganisha pamoja kuishi kwa Kristo.

G. Mashauri ya Paulo (15:14-33)

15:14 Ndani ya baki la sura 15 Paulo alipasha kwa sababu gani alikuwa akiandika kwa Waroma, na ya kwamba alitaka sana kuwaona.

Hata kama hakukutana na Waroma mbele, **alijua** kwamba watapokea ma-

onyo yake, kwa sababu ya habari alizosikia mbele juu ya **wema** wao. Alikuwa amesikia kwamba walijaa **elimu** juu ya mafundisho ya ukristo na waliweza kuonyana.

15:15 Aliamini kwamba walikuwa wameendelea katika imani, na hata akikumbuka kwamba hawakujuana naye, hakusita kuwakumbusha mengine ya mapendeleo na madaraka yao. Alifanya hivi kwa sababu ya **neema aliyopewa na Mungu** – ndiyo **neema** ambayo ilimweka kuwa mtume.

15:16 Aliwekwa na Mungu sawasawa mtumishi-kuhani **wa Yesu Kristo kwa Mataifa**. Aliona kazi hii ya kutangaza **Habari Njema ya Mungu** kama kazi ya kuhani, kwa njia ya kuletea **Mataifa** walookolewa kama **sadaka iliyokubaliwa** kwa Mungu, maana walikuwa wametakaswa **na Roho Mtakatifu ya Mungu** kwa njia ya kuzaliwa tena. G. Campbell Morgan aliandika na furaha kubwa:

Kila mtu anayeokolewa kwa njia ya mahubiri ya Habari Njema, na kufikishwa kwa pahali pa salama na baraka, ni sadaka kwa Mungu vilevile. Ni zawadi ambayo inamfurahisha, namna ya toleo anayotaka. Kila mtu anayefundishwa vizuri, na saburi, habari za Kristo, na kwa njia hii kufanannishwa naye, anapendeza Mungu Baba sana. Hivi tunasumbuka, si kwa wokovu wa roho za watu tu, lakini moyo wa Mungu uweze kutulizwa. Ni neno hili ambalo linatusukuma zaidi ndani ya kazi yetu ya kuhubiri Habari Njema na kufundisha waamini.²²

15:17 Paulo anajisifu, lakini si ndani yake mwenyewe, lakini katika **Kristo Yesu**. Hajisifu ndani ya kazi zake mwenyewe, lakini ndani ya maneno ambayo **Mungu** alipendezwa kufanya kwa njia yake. Mtumishi mnye-

nyekevu wa Kristo si mwenye kujisifu kusikofaa, lakini anafurahi kwa sababu Mungu anatumika naye kutimiza makusudi yake. Anafahamu kwamba ye ye mwenyewe hana kitu asichopewa, na ya kwamba hawezi kufanya neno kwa Kristo ila kwa uwezo wa Roho Mtakatifu.

15:18 Paulo **hakusubutu kusema** juu ya maneno ambayo **Kristo** alikuwa amefanya kwa njia ya utumishi wa watu wengine. Alisema tu juu ya namna Bwana alitumika na *yeye* kuongoza **Mataifa** kutii, kwa njia ya maneno aliyosema na kutenda – maana habari alizohubiri, na maajabu aliyofanya.

15:19 Bwana alithibitisha masemo ya mtume kwa njia ya maajabu yaliyofundisha maneno ya roho na kushangaza wasikiaji, na kwa manoyesho mbalimbali za uwezo wa Roho Mtakatifu. Alikuwa **amehubiri Habari Njema**, kuanza kwa **Yerusalem** kufika hata **Iliriko** (kwa upande wa kaskazini wa Makedonia, **kwa bahari ya Adriatigue**). **Toka Yerusalem ... kufika Iliriko** – maneno haya yanaonyesha urefu wa safari za utumishi wake, si namna matukio yalivyoatuana.

15:20 **Kusudi** lake kwa safari ile lilikuwa **kuhubiri Habari Njema** pahali watu wasipoisikia mbele. Wasikiaji wake walikuwa zaidi Mataifa wasiosikia habari za **Kristo** mbele. Kwa njia hii Paulo hakujenga juu ya **msingi** wa mtu mwengine. Lakini si lazima kwa wahubiri wengine kumwiga ndani ya neno hili. Wengine wanaitwa kwenda kusaidia makanisa mapya na mafundisho ya Neno la Mungu.

15:21 Kazi hii ya kuweka msingi katikati ya Mataifa ilitimiza unabii wa Isaya (52:15), kwamba Mataifa wasioambiwa kamwe **wataona**, na wale wasiosikia kamwe Habari Njema **watafa-**

hamu na kuipokea na imani ya kweli.

15:22, 23 Paulo alikuwa ameweka roho na nguvu yake yote kutangaza Habari Njema kwa inchi za watu ambao hawakuisikia mbele, hata ha-kuwa na saa kufikia Roma mbele. **Lakini sasa** msingi ulikuwa umewe-kwa kwa inchi ambayo tulisoma juu yake kwa 15:19. Wengine waliweza kujenga juu ya msingi ule. Hivi Paulo alikuwa huru sasa kufanya neno **alilotaka** kufanya tangu siku nyingi, ndilo kufikia Roma.

15:24 Shauri lake lilikuwa kusima-ma kwa Roma kwa safari yake kwenda **Spania**. Hataweza kushinda muda wa kutosha pamoja nao, lakini hata hivi **atafurahi kuweza kukaa pamoja nao**. Halafu alijua watamsaidia na vitu atakavyohitaji kwa kumaliza safari yake kwenda Spania.

15:25 **Lakini** sasa alikuwa akikwe-nda **Yerusalem** kufikisha mali ili-yokutanishwa na makanisa Mataifa, kusaidia **watakatifu** wenye hitaji katika Yudea. Tunasoma juu ya sadaka hii katika 1 Wakorinto 16:1 na 2 Korinto 8 na 9.

15:26, 27 Waamini wa **Makedonia na Akaya** walifurahi kutoa mali kwa sadaka hii kusaidia Wakristo **masikini**. Walifanya hivi na kutaka kwao wenye, na ilikuwa taratibu wafanye hivi. Wao wenye, na ilikuwa vizuri washiriki na ndugu zao Wayuda kwa njia ya **mali na vitu**.

15:28, 29 Mara moja nyuma ya **kutimiza kazi hii**, ndiyo kufikisha mali kama alivyoahidi kufanya, alikusudi kufikia Roma kwa njia ya safari yake kwenda **Spania**. Aliamini kabisa kwa-mba atakuja kwa **utimilifu wa baraka ya Habari Njema** ambayo **Kristo** anamwanga kila mara neno la Mungu linapohubiriwa kwa uwezo wa Roho Mtakatifu.

15:30 Paulo anamaliza mashairi haya na kusihi wasomaji **kumwombea** na bidii. Anafanya hivi kwa sababu ya umoja wao na **Bwana Yesu Kristo**, na **mapendo** yao yaliyotoka kwa **Roho Mtakatifu**.

15:31 Anawasihi kwa maneno mane. Kwanza Paulo anataka waombe aweze **kuokolewa** toka watu wasioamini **katika Yudea**, walioshindana sana na Habari Njema, namna Paulo alivyo-shindana na Habari Njema yeye mwenyewe mbele.

Neno la pili ambalo anataka Waroma kuomba ni kwa **watakatifu** Wa-yuda kupokea na roho nzuri zabihu hii ambayo aliwapelekeea kuwasaidia. Wa-yuda wa dini walichukia waamini wa Mataifa pamoja na wale ambao wa-liwahubiri Habari Njema. Inawezekana vilevile kwa watu kutokutaka kupokea kusaidiwa na watu wengine. Mara nyi-ningine mwenye kupokea zawadi anahitaji neema kupita yule ambaye anaito!

15:32 *Neno la tatu* Paulo alilo-omba lilikuwa kufika kwake kwa Roma liweze kuwa wakati wa furaha. Maneno haya **kwa mapenzi ya Mungu**, yanayonyesha kwamba Paulo alitaka Bwana kumwongoza ndani ya maneno yote.

Mwishoni, aliomba ili kufika kwake kuweze kumpa yeye mwenyewe njia **kupumzika** katikati ya utumishi wake wa machafuko na wa kuchokeza.

15:33 Halafu Paulo anamaliza sura hii na maombi ili **Mungu wa salama** awe pamoja nao. Ndani ya sura 15 Bwana aliitwa *Mungu wa saburi na faraja* (sh.5), *Mungu wa tumaini* (sh.13), na sasa **Mungu wa salama**. Kwake yanatoka mambo mema yote yanayo-hitajiwa na mwenye zambi kwa wakati wa sasa na kwa milele. **Amina**.

H. Sifa ya Paulo kwa kazi ya watu wengine (Sura 16)

Kwanza wakati tunapoangalia sura hii tunafikiri kama ni faida gani kusoma

majina haya yote yasiyo na maana kwa sisi kwa wakati wa sasa. Lakini wakati tunapoisojoma tena na kuwaza sana juu yake, tutaona mafundisho mengi ya faida kwa mwamini.

16:1 Foibe anaitwa hapa **mtumishi wa kanisa lililo katika Kenkurea**. Hatuhitaji kufikiri juu yake kama mtu wa chama fulani ya dini. Kila mwanamke anayetumikia Bwana ndani ya kanisa anaweza kuwa "mtumishi."

16:2 Wakati wa mwanzo wa kanisa, saa Wakristo waliposafiri toka kanisa moja kufikia kanisa lingine, walikwenda na barua toka kanisa lao. Neno hili liliwasaidia, na lilisaidia vilevile kanisa walilofikia.

Hivi Paulo alituma barua hapa kwa waamini wa Roma kupokea Foibe kama mwamini wa kweli, **kama inavyopasa** kupokea watakatifu. Alikuwa amejitoa kusaidia watu wengine, hata Paulo vilevile. Labda alikuwa mmoja wa wanawake wale waliotumika bila kuchoka kupokea nyumbani mwao wahubiri na waamini wengine kwa Kenkurea.

16:3 Kisha Paulo anatuma salamu kwa **Prisila na Akila**, walikuwa wametumika na uhodari **pamoja naye katika kazi ya Kristo Yesu**. Tushukuru Mungu kwa waume na wake wao ambao wanajitoa kabisa kwa kazi ya Kristo!

16:4 Siku moja Prisila na Akila walikuwa tayari **kutoa uzima wao** kwa **ajili ya** Paulo. Hatujui habari za hatari hii, lakini mtume alikuwa na mashukuru rohoni, na **makanisa** ya waamini wa **Mataifa** vilevile.

16:5 Musalimu kanisa lililo katika nyumba yao. Walikuwa na makusanyiko nyumbani mwao. Wakristo walianza kusimanisha vyumba kwa makusanyiko ya kanisa karibu na 200 A.D. Wakati Prisila na Akila walipokaa katika Korinto mbele, ndugu za kanisa walikutana nyumbani mwao vilevile.

Maana ya **Epeneto** ni "ya kustahili

sifa." Alikuwa mtu wa kwanza aliye-aminii Kristo katika Asia. Bila shaka alistahili kuitwa na jina hili. Paulo alimwita **mpenzi wangu**.

16:6 Tunaona majina ya wanawake wengi ndani ya sura hii. Neno hili linaonyesha faida kubwa ya utumishi wao kwa njia mbalimbali (mash. 1, 3, 6, 12, na mengine). **Maria** alifanya kazi nyingi kwa ajili ya watakatifu.

16:7 Hatujui kwa wakati gani **Androniko na Yunia** walikuwa **wafungwa pamoja** na Paulo. Hatujui kama hapa maana ya neno hili **jamaa** ili kuwa kwamba walikuwa ndugu za Paulo, au Wayuda wengine. Hatujui vilevile kama maana ya **wanaojulikana katika mitume** ni kwamba waliheshimiwa *na mitume* au kama wao wenyewe walikuwa **mitume** ya kujulikana. Tunajua neno moja tu: walipokea Kristo **mbele** ya Paulo.

16:8 Kisha tunasoma juu ya **Ampuliato, mpenzi** wa mtume. Tusingalisikia kamwe habari za watu hawa kama wasingalikuwa Wakristo. Uku-bwa wa pekee ambao tunalo ni tunda la Kalvari.

16:9 Paulo aliita **Urbano, mtenda kazi pamoja nami**, na aliita **Staki, mpenzi wangu**. Waroma 16 ni kama mfano mdogo wa kiti cha hukumu cha Kristo, pahali Kristo atakapotoa sifa kwa kila tendo aminifu ambalo watu wake walimfanya.

16:10 Apele alikuwa ameshinda vizuri wakati alipopata taabu kubwa, na **alikubaliwa katika Kristo**.

Paulo alisalimu **watu wa nyumba ya Aristobulo**. Tunafikiri aliwaza juu ya watumwa Wakristo wa mjukuu wa Herode Mkubwa.

16:11 Tunafikiri **Herodio** alikuwa mtumwa vilevile. Alikuwa wa inchi ya Paulo, na labda alikuwa mtumwa *Myuda* wa pekee nyumbani mwa Aristobulo.

Wengine wa watumwa wa **Narkiso** walikuwa waamini vilevile, na walisa-

limiwa na Paulo. Hata kama watu wanafikiri watu fulani ni chini sana kwa mawazo wa watu wengine, ndani ya Kristo hakuna neno namna hii kututenga tena, kwa sababu ndani yake sisi sote tuko moja.

16:12 Maana ya majina na **Tirifena** na **Tirifosa** ni “ya kupendeza” na “ya kupenda anasa,” lakini walitumikia Bwana na nguvu yao yote. **Persimpenzi** alikuwa mmoja wa wanawake wale wanaotumika na wanaohitajiwa sana sana bila kupata sifa mbele ya mauti yao.

16:13 Labda **Rufo** alikuwa mwana wa Simoni, aliyebeba msalaba kwa Yesu (Mt. 27:32). **Alichaguliwa katika Bwana**, si kwa sababu ya kupokea wokovu tu, lakini kwa sababu ya masha yake mazuri sana. **Mama** ya Rufo alitendea Paulo mema, na kwa sababu hii Paulo alimwita na mapendo “mama yangu.”

16:14, 15 Labda **Asinkrito, Fulego, Herme, Patroba**, na **Herma** walitumikia Bwana ndani ya moja la makanisa waliokutana nyumbani, kama lile nyumbani mwa Prisila na Akila (16:3, 5). Labda **Filologo na Yulia, Nero na ndugu yake mke, na Olimpa** walikuwa ndani ya kanisa nyumbani nytingine.

16:16 Ilikuwa desturi ya wataka-tifu wa wakati ule kusalimiana na **busu takatifu**. Kuna watu wa inchi nytingine wanaofanya hivi hata sasa. Inaitwa busu **takatifu**, lisiwe neno lisilofaa. Katika Congo ni desturi kushika mkoно kwa pahali pa kubusu.

Makanisa katika Akaya (ndipo pahali Paulo alipokuwa wakati alipandika barua hii) waliwasalimu.

16:17 Mtume hakuweza kumaliza barua hii bila maonyo kwa waamini wakae na ange kwa walimu waouwatakaojribu kuingia ndani ya kanisa. Wakristo wakae na ange kwa wale wanaofanya matengo, na kuleta makwazo kufunganisha waamini karibu

nao na kuwatega kuharibu imani yao. Sharti wakae na ange na kutambua watu wale wanaofundisha maneno yaliyo **mbalimbali na mafundisho** Wakristo **waliyofundishwa**, na **kuwaepuka** kabisa.

16:18 Walimu hawa wa uwongo hawatii **Bwana wetu Yesu Kristo**. Wanatii tamaa **zao wenyewe**, na wanadanganya watu na **masemo yao matamu ya kupendeza**.

16:19 Paulo **alifurahi** kwa sababu watu walijua kwamba wasomaji wake walikuwa wenye **kutii** Bwana. Lakini hata hivi alitaka waweze kutambua na kutii mafundisho **mazuri** na kukataa yaliyo **mabaya**.

16:20 Kwa njia hii, **Mungu** mwenye kutoa **salama** atawawezesha kushinda **Shetani** mbio.

Kama alivyofanya ndani ya barua zake nytingine, Paulo anaomba neema ya Bwana Yesu Kristo awe pamoa nao kwa safari yao kwenda mbinguni.

16:21 Tunajuana na **Timoteo**, ndiye mwana wa Paulo katika imani na mwenye kutumika pamoa naye na uaminifu. Hatujui habari za **Lukio**, ila ya kwamba alikuwa Myuda kama Paulo. Labda tulisoma mbele juu ya **Yasona** (Mdo. 17:5), na **Sosipateri** (Mdo. 20:4), waliokuwa Wayuda vilevile.

16:22 **Tertio** alikuwa karani aliyeandika **maneno** ambayo Paulo alimwambia kuandika. Tertio aliongeza salama yake kwa wasomaji.

16:23 Kulikuwa na wanaume wane (au hata kupita) ndani ya Agano Jipy walioitwa **Gayo**. Tunafikiri huyu katika shairi hili ndiye anayetajwa katika 1 Kor. 1:14. Alijulikana kwa sababu ya kupokea wagoni na furaha, si Paulo tu lakini Wakristo wengine vilevile. **Erasto** alikuwa **mchungaji wa mali wa mji**, ndio Korinto. Hatujui kabisa kama ni Erasto huyu aliyetajwa ndani ya Matendo 19:22, au yule katika 2 Timoteo 4:20. **Kwarto** aliitwa **ndugu** tu, lakini hili vilevile ni jina la heshima kabisa!

16:24 Neema ya Bwana wetu Yesu Kristo iwe pamoja nanyi wote ni baraka Paulo aliyotoa kwa mwisho wa karibu kila barua. Ni sawasawa na ile ndani ya sh. 20b, ila hapa katika shairi 24 aliongeza **wote**. Ni njia nzuri kumaliza kitabu, na Paulo alikimaliza na **Amina**.

16:25 Barua hii inakwisha na wimbo kwa kusifu Mungu **anayeweza** kusimamisha watu wake imara sawasawa na **Habari Njema** ambayo Paulo alihubiri. Aliiita **Habari Njema yantru**. Kuna Habari Njema moja tu, lakini Paulo alipewa kazi ya kuihubiri kwa sababu alikuwa “Mtume kwa Mataifa,” lakini Petro alihubiri kwa Wayuda. Ni matangazo ya habari juu ya **Yesu Kristo** juu ya **ufunuo** wa kweli ya ajabu **iliyokuwa siri tangu mwanzo wa dunia**. Siri ndani ya Agano Jipyä ni kweli iliyofichwa, na watu wenye nia ya binadamu wasiyo-weza kuvumbua kamwe. Sasa kweli hii ilikuwa imefunuliwa.

16:26 Sasa **kweli hii ilionyeshwa kwa maandiko ya manabii** – si manabii ya Agano la Kale, lakini wale ndani ya **maandiko ya unabii wa muda** wa Agano Jipyä (ona Efe. 2:20; 3:5)

Ni Habari Njema ambazo Mungu **ameagiza zitangazwe kwa mataifa yote** ili watu wawze kutii **iman** na kuokolewa.

16:27 Kwa Mungu peke yake uwe utukufu kwa Yesu Kristo, Mpatanishi wetu, **kwa milele**.

Tumefikia mwisho wa barua hii nzuri sana ya Paulo. Tunashukuru Bwana sana kwa barua hii. **Amina**.

NOTES

¹ (2:4) A. P. Gibbs, *Preach the Word*, ukurasa 12/4

² (2:6) Lewis S. Chafer, *Systematic Theology*, III:376.

³ (3:24) Arthur T. Pierson, *Shall We Continue in Sin?* ukurasa 23.

⁴ (4:24) C. H. Mackintosh, *The Mackintosh Treasury: Miscellaneous Writings* by C. H. Mackintosh, ukurasa 66.

⁵ (6:5) Charles Hodge, *The Epistle to the Romans*, ukurasa 196.

⁶ (6:11) C. E. Macartney, *Macartney's Illustrations*, kurasa 378, 379.

⁷ (7:15) Harry Foster, article in *Toward the Mark*, ukurasa 110.

⁸ (8:31) Shairi hili lilikuwa ushuhuda wa maisha ya John Calvin.

⁹ (9:16) G. Campbell Morgan, *Searchlights from the Word*, kurasa 335, 336.

¹⁰ (9:21) Albert Barnes, *Barnes's Notes on the New Testament*, ukurasa 617.

¹¹ (9:23) Charles R. Erdman, *The Epistle of Paul to the Romans*, ukurasa 109.

¹² (10:10) William Kelly, *Notes on the Epistle to the Romans*, ukurasa 206.

¹³ (10:10) James Denney, quoted by Kenneth Wuest in *Romans in the Greek New Testament*, ukurasa 178.

¹⁴ (11:1) Ni huzuni kuona kwamba wale wanaokamata baraka za Israeli kwa kanisa hawafikiri juu ya laana zilitzotabiriwa!

¹⁵ (11:32) George Williams, *The Student's Commentary on the Holy Scriptures*, ukurasa 871.

¹⁶ (11:33) Arthur W. Pink, *The Attributes of God*, ukurasa 13.

¹⁷ (12:1) Norman Grubb, C. T. Studd, *Cricketer and Pioneer*, ukurasa 141.

¹⁸ (12:6) Hodge, *Romans*, ukurasa 613.

¹⁹ (12:6) A.H. Strong, *Systematic Theology*, ukurasa 12.

²⁰ (12:21) George Washington Carver (further documentation not available).

²¹ (14:10) Maandiko mengine ya zamani yanasema “kiti cha hukumu ya Mungu” kwa pahali pa “Kristo”. Lakini tunajua Kristo atakuwa Mwamuzi kwa sababu Mungu aliweka hukumu yote mikononi mwake (Yoane 5:22).

²² (15:16) Morgan, *Searchlights*, ukurasa 337.

BIBLIOGRAPHIE

- Cranfield, C. E. B. *The Epistle to the Romans. Vol. I (ICCC)*, Edinburgh: T. & T. Clark Ltd., 1975.
- Denney, James. "St. Paul's Epistle to the Romans," *The Expositor's Greek Testament, Vol. II*. Grand Rapids: Wm. B. Eerdmans Publishing Company, 1961.
- Erdman, C. R. *The Epistle of Paul to the Romans*. Philadelphia: The Westminster Press, 1925.
- Gahan, Charles. *Gleanings in Romans*. Published by author.
- Hodge, Charles. *Commentary on the Epistle to the Romans*. New York: George H. Doran Company, 1886.
- Kelly, William, *Notes on the Epistle to the Romans*. London: G. Morrish, 1873.
- Lenski, R. C. H. *St. Paul's Epistle to the Romans*. Minneapolis: Augsburg Publishing House, 1961.
- Newell, William R. *Romans Verse by Verse*. Chicago: Moody Press, 1938.
- Rainsford, Marcus. *Lectures on Romans VI*. London: Charles J. Thynne, 1898.
- Shedd, William G. T. *A Critical and Doctrinal Commentary on the Epistle of St. Paul to the Romans*. Grand Rapids: Zondervan, 1967.
- Stifler, J.M. *The Epistle to the Romans: A Commentary Logical and Historical*. Chicago: Moody Press, 1960.
- Wuest, Kenneth S. *Romans in the Greek New Testament*. Grand Rapids: Wm. B. Eerdmans Publishing Company, 1964.

BARUA YA KWANZA KWA WAKORINTO

Utangulizi

I. Nafasi ya pekee katika Kanuni

Ndani ya 1 Wakorinto Paulo ali-fundisha juu ya mambo magumu ambayo waamini katika mji mwovu ule, ndio Korinto, walishindana nayo. Ma-fundisho haya yanahitajiwa sana kwa makanisa ya wakati wa sasa vilevile kwani waamini wanashindana na maneno kama magawanyiko, viongozi wanao-heshimwa kupita kipimo, uzini, mashitaki mbele ya waamuzi, mume na mke wasiopatana, kawaida ya zawadi za roho, na maneno mengine yasiyo taratibu.

Lakini hatusomi juu ya maneno magumu tu ndani ya barua hii. 1 Wakorinto sura 13 ni andiko zuri zaidi juu ya mapendo, si katika Biblia tu, lakini katika maandiko *yote* duniani. Ndani ya sura 15 tunapata mafundisho ya ajabu sana juu ya ufufuko – ufufuko wa Kristo, na ufufuko wetu vilevile. Kuna mafundisho juu ya utaratibu kwa Meza ya Bwana (sura 11), na agizo kushiriki ndani ya sadaka ya mali kwa watakatifu (sura 16).

Kweli 1 Wakorinto ni hazina ya ma-fundisho kwa maisha na mwenendo wa Wakristo.

II. Mwandishi

Walimu wote wanakubali kwamba Paulo aliandika barua hii. 1 Wakorinto 5:9 linatufikirisha kwamba Paulo ali-andika barua nyingine mbele isiyohesabiwa kuwa sehemu ya kanuni ya kanisa, na Wakorinto walikosa kufahamu maana yke vizuri..

Kwa mwaka A.D. 95 mkubwa mmoja, ndiye Clement ya Roma, aliita barua hii “Barua ya Mtume mbarikiwa Paulo.” Waandishi wengine kwa wakati wa mwanzo wa Kanisa walitaja masemo toka barua hii. Walikuwa Polycarp, Justin Martyr, Athenagoras, Irenaeus, Clement wa Alesanduria, na Tertullian.

Maneno yaliyoandikwa ndani ya ba-rua hii yanaonyesha wazi kwamba ili-andikwa na Paulo. Mwandishi alijiita mwenyewe Paulo katika 1:1 na 16:21. Habari katika 1:12-17; 3:4, 6, 22 yanatu-fikirisha kwamba yaliandikwa na Paulo. Maneno mengine yaliyoandikwa ndani ya 1 Wakorinto yalitajwa ndani ya Matendo na barua nyingine za Paulo vilevile.

III. Tarehe

Paulo litujulisha kwamba alikuwa katika Efeso wakati alipoandika barua hii (16:8,9; pamoja na sh. 19). Alitumikia Bwana katika Efeso kwa miaka mitatu, hivi ni kama aliandika barua hii kwa sehemu ya mwisho wa muda huu, karibu na 55 au 56 A.D. Walimu wengine wanafikirishi iliandikwa mbele ya muda huu.

IV. Msingi na Jambo Kubwa

Mji wa Korinto ulikuwa kwa sehemu ya kusini ya Yunani, na ungali pale hata sasa. Ulikuwa kwa upande wa mangaribi wa Atene, pahali pazuri kwa wenye kufanya biashara toka inchi imbalimbali kufikisha vitu vyao. Kwa sababu ya upotovu wa Wakorinto kwa maneno ya dini yao, uasherati na uzini zilizidi. Watu

walitunga neno juu ya mji huu, *kɔrɪnθiazomai*, maana yake *kuishi maisha mapotovu*.

Mtume Paulo alifikia Korinto mara ya kwanza kwa safari yake ya pili ya kuhubiri (Matendo 18). Alitumika katikati ya Wayuda kwanza pamoja na Prisila na Akila, wenyewe kufanya hema kama yeche. Wakati zaidi ya Wayuda walipokataa mafundisho yake, alianza kuhubiri kwa Mataifa katika Korinto. Wengine waliokolewa wakati waliposikia Habari Njema, na kanisa lilisimamishwa.

Baada ya karibu na miaka mitatu, wakati Paulo alipokuwa akihubiri katika Efeso, alipokea barua toka Korinto. Barua hii ilipasha habari za matata kanisani, na iliuliza namna gani inapasa

waamini kutenda. Barua hii ya kwanza kwa Wakorinto iliandikwa na kusudi la kujibu maulizo haya.

Jambo kubwa la barua ni namna gani inapasa kutengeneza maneno ya kanisa linalofungana na maneno ya dunia, bila kuweka roho juu ya kuanguka kwa mawazo na matendo yao yasiyofaa. Maneno haya yalisumbusha roho ya mtume Paulo sana. Kama mwaliimu mmoja, ndiye Moffat, alivyosema, "Kanisa halikuweza kuepuka kukaa duniani, lakini haikufaa kwa dunia kukaa ndani ya kanisa."

Hii ndiyo hali ya makanisa mengi hata kwa wakati wa sasa, hivi faida ya mafundisho ya 1 Wakorinto inadumu.

HABARI YALIYOMO

1. MWANZO (1:1-9)
 - A. Salamu (1:1-3)
 - B. Mashukuru (1:4-9)
2. MACHAFUKO KANISANI (1:10-6:20)
 - A. Magawanyiko katikati ya waamini (1:10-4:21)
 - B. Uzini katikati ya waamini (Sura 5)
 - C. Mashitaki ya waamini mbele ya waamuzi (6:1-11)
 - D. Ukosefu wa usafi wa mwenendo wa waamini (6:12-20)
3. MAJIBU YA MTUME KWA MAULIZO YA KANISA (Sura 7-14)
 - A. Juu ya ndoa na kutokuo (Sura 7)
 - B. Juu ya vyakula viliwyotolewa kwa sanamu (8:1-11:1)
 - C. Juu ya vifuniko vya vichwa vya wanawake (11:2-16)
 - D. Juu ya Meza ya Bwana (11:17-34)
 - E. Juu ya zawadi za Roho na kazi yao kanisani (Sura 12-14)
4. MAJIBU YA PAULO KWA WALE WANAOOKANA (Sura 15)

UFUFUKO

 - A. Hakika ya ufufuko (15:1-34)
 - B. Mawazo juu ya mabishano ya ufufuko (15:35-57)
 - C. Maonyo ya mwisho kwa sababu ya ufufuko (15:58)
5. MAONYO YA MWISHO YA PAULO (Sura 16)
 - A. Juu ya sadaka (16:1-4)
 - B. Juu ya mashauri yake mwenywewe (16:5-9)
 - C. Maonyo ya mwisho na salamu (16:10-24)

Maelezo

1. MWANZO (1:1-9)

A. Salamu (1:1-3)

1:1 Paulo aliitwa kuwa mtume wa Yesu Kristo kwa safari yake kwenda Damasiki. Hakuitwa na watu, lakini na Bwana Yesu mwenyewe. **Mtume** ni “mtu anayetumwa.” Watume wa kwanza walikuwa washuhuda wa ufufuko wa Kristo. Waliweza kufanya maajabu vile-vile kuhakikisha kwamba habari walizofundisha zilitoka kwa Mungu.

Saa Paulo alipoandika barua hii, **ndugu** mmoja alikuwa pamoja naye, jina lake **Sositeni**. Hatujui kama alikuwa Sositeni ambaye tulisoma habari zake katika Matendo 18:17, aliyejewa mwoongozi wa sunagogi, na aliyejigwa na Wayunani. Labda kiongozi huyu aliokolewa wakati aliposikia mahubiri ya Paulo, na sasa alimsaidia ndani ya kazi ya kuhubiri Habari Njema.

1:2 Barua hii iliandikwa kwa **kanisa la Mungu lililo katika Korinto**. Ni neno la kusaidia roho zetu kufahamu kwamba iliwezekana kwa kanisa kusimamishwa hata katika mji huu mwovu sana. Watu wa kanisa hili **walitakaswa katika Yesu Kristo, walioitwa ... watakatifu**. Maana ya **kutakaswa** ni kuwekwa mbali kwa Mungu toka dunia. Ni hali ya Wakristo wote. Inawapasa konyesha hali hii kila siku kwa njia ya mwenendo na maisha yao matakatifu.

Watu wengine wanafundisha kwamba utakaso ndiyo kazi ya neema, kwa njia yake tabia ya zambi inaondoshwa ndani ya mtu. Mafundisho haya hayapatani na mafundisho ya shairi hili. Waamini wa Korinto hawakuwa wenye mwenendo mtakatifu hata kidogo, lakini hata hivi kwa maneno ya hali yao ndani ya Kristo, **walitakaswa** na Mungu.

Wakiwa watakatifu walishiriki na

wale walioitakaswa katika Yesu Kristo, walioitwa kuwa watakatifu **pamoja na wote wanaoitia jina la Bwana Yesu Kristo** katika kila pahali, **Bwana wao na Bwana wetu**. Barua hii iliandikwa kwanza kwa watakatifu katika Korinto, lakini mafundisho yake ni kwa watu wote duniani pote wanaokiri Kristo kuwa Bwana wao.

1:3 1 Wakorinto inafundisha sana kwamba Yesu ni Bwana. Wakati Paulo alipoandika juu ya maneno mbalimbali kanisani na ndani ya maisha ya waamini mmoja mmoja, alikumbusha waamini wake tena na tena ya kwamba Kristo ni Bwana, na ya kwamba inatupasa kufanya maneno yote tukikumbuka kweli hii kubwa.

Ilikuwa desturi ya Paulo kusalimu watu na **neema na salama**. Maneno haya mawili yanajumlisha Habari Njema yake. Baraka zote zinatoka kwa **neema** ya Mungu. **Salama** ndiyo tunda ndani ya maisha ya mtu anayepokea **neema** ya Mungu. Baraka hizi kubwa **zinatoka kwa Mungu Baba wetu na Bwana Yesu Kristo**. Paulo hakusita kutaja **Bwana Yesu** pamoja na **Mungu Baba wetu**. Hili ni moja la mia za mashairi katika Agano Jipyaa yanayoonyesha kwamba Bwana Yesu ni ma-moja na Mungu Baba.

B. Mashukuru (1:4-9)

1:4 Nyuma ya kumaliza kusalimu wasomaji, mtume aliendelea na mashukuru kwa Wakorinto na kwa kazi ya ajabu ambayo Mungu alikuwa amefanya ndani ya maisha yao (mash. 4-9). Ilikuwa desturi nzuri ya Paulo kujaribu kuona saa zote neno zuri ndani ya maisha ya waamini wenzake ambalo aliweza kusifu Mungu juu yake. Labda hakukuta maneno mengi ndani ya mwe-

nendo wao aliyoweza kusifu, lakini hata hivi aliweza **kushukuru Mungu** wake kwa kazi ambayo alikuwa amewafanyia. Wakorinto hawakufuata Kristo karibu karibu. Hata hivi Paulo aliweza kuleta asante kwa **neema ya Mungu walipewa katika Yesu Kristo**.

1:5 Neema ya Mungu ilionekana kwa Wakorinto zaidi kwa njia ya zawadi nyingi za Roho Mtakatifu walizopewa. Paulo alitaja zawadi za **maneno** (usemi) **na maarifa yote**. Ni kama walipewa zawadi ya kuweza kusema kwa lugha na kutafsiri lugha, na walikuwa wenye maarifa sana. **Maneno** (usemi) ni juu ya kujulisha mambo waliyojua, na **maarifa** ni juu ya ufahamu wao.

1:6 Zawadi hizi zilihakikisha kwa mba Mungu alikuwa akitumika ndani ya maisha yao. Hii ndiyo maana ya maneno ya Paulo kwamba **ushuhuda wa Kristo ulisibitishwa ndani yenu**. Walikuwa wamesikia **ushuhuda wa Kristo**, wameuamini, na kwa njia ya kuwapa zawadi hizi za ajabu Mungu alitoa ushuhuda kwamba walikuwa wameokolewa kweli.

1:7 Kanisa la Wakorinto halikupungukiwa zawadi, lakini kuwa na zawadi hizi hakuhakikisha kwamba Wakristo walitembea karibu na Bwana. Paulo alikuwa akishukuru Mungu kwa zawadi ambazo Wakorinto hawakufanya neno kuzipokea. Bwana mfufuliwa alitoa zawadi hizi bila kufikiri ustahili wa wenye kuzipokea. Mtu akiwa na zawadi fulani, haifai ajivune juu yake, lakini atumike nayo kwa Bwana na unyenyekevu.

Maneno haya ni mbali na tunda la Roho. Kwa kuzaa tunda la Roho inapasa mwamini kujitoa mwenyewe kwa utawala wa Roho Mtakatifu. Mtume hakuweza kusifu Wakorinto kwa sababu ya kuonekana kwa matunda ya Roho ndani ya maisha yao, lakini kwa zawadi walizopewa na Bwana mwenye enzi.

Nyuma kidogo ndani ya barua hii tutaona kwamba ilipasa mtume kuha-

makia watakatifu kwa sababu hawakutumika vizuri na zawadi hizi, lakini hapa anatoa sifa kwa Mungu kwa sababu walikuwa wamepokea zawadi nyingi.

Wakorinto walikuwa **wakingojea na hamu ufunuo wa Bwana wetu Yesu Kristo**. Walimu wengine wanafikiri maneno haya ni juu ya kuja kwa Kristo kwa watakatifu wake (1 Tes. 4:13-18). Wengine wanafikiri ni juu ya kuja kwake pamoja na watakatifu (2 Tes. 1:6-10), au juu ya kuja kwa kwanza na kuja kwa pili vilevile. Mara ya kwanza Kristo atafunuliwa kwa waamini tu, lakini mara ya pili utakuwa ufunuo wake kwa dunia nzima. Waamini wanangojea kuja kwa kwanza na kwa pili na **hamu kubwa**.

1:8 Halafu Paulo alionyesha kwa mba aliamini Bwana atathibitisha wamini **hata mwisho**, wasilaumiwe **katika siku ya Bwana wetu Yesu Kristo**. Mara hii tena mashukuru yake ni zaidi kwa maneno Mungu atakayofanya, si kwa kazi Wakorinto walizofanya. Walikuwa wameamini Kristo, na Mungu alikuwa amesibitisha neno hili kwa njia ya kuwapa zawadi za Roho, hivi Paulo aliamini kwamba Mungu atawalinda kwa yeche mwenyewe kufika siku Kristo atakapokuja kwa watu wake.

1:9 Msingi wa maneno Paulo aliyoamini juu yao ulikuwa uaminifu wa **Mungu** aliyekuwa amewaita **katika ushirika wa Mwana wake**. Aliuja Mungu alikuwa amelipa bei kubwa sana kusudi waweze kushiriki ndani ya uzima wa **Bwana wetu**, na hatawaacha kamwe kupotea.

2. MACHAFUKO KANISANI

(1:10—6:20)

A. Matengano katikati ya waamini (1:10 – 4:21)

1:10 Mtume ni tayari sasa kusema juu ya matengano kanisani (1:10 – 4:21). Alianza kuwaonya na mapendo wawe na roho ya umoja. Akiwa mtume, aliweza kuwaagiza na amri, lakini hakufanya

hivi. Aliwasihii na roho ya mapendo ya ndugu kwa **jina la Bwana wetu Yesu Kristo**. Jina la Yesu linasema juu ya Yesu mwenyewe na maneno yote aliyofanya. Wakorinto walikuwa wakitkuza jina la watu tu, lakini neno hili lilileta matengano. Paulo atatukuza jina la Yesu tu, kwani alijua kwamba njia hii tu iliweza kuleta umoja katikati ya watu wa Mungu. Maana ya **kusema neno moja** ni kuwa **na nia moja** juu ya neno fulani. Ni kuwa na uaminifu na utii mmoja. Wakristo wana umoja huu wakati walipo na nia ya Kristo. Ndani ya mashairi yanayofuata Paulo atawajulisha namna gani waliweza kuwaza namna Kristo alivyowaza.

1:11 Watu wa **nyumba ya Kloe** walikuwa wamejulisha Paulo habari za **ugomvi** katikati ya waamini. Habari hizi zinatufundisha neno kubwa. Haifai tupitishe habari kwa watu wengine juu ya waamini wenzetu bila kuwa tayari kujulisha kwamba habari hizi zinatoka kwetu. Tukifanya hivi tunaweza kuzuiza mazungumuzo mengi bila maana yanayosumbusha kanisa sasa.

1:12 Jamii za watu zilikuwa zikanzwa kanisani, watu wa kila jamii wakifungana na kiongozi mmoja. Jamii moja walifungana na **Paulo**, nytingine na **Apolo**, nytingine na **Kefa** (ndiye Petro). Wengine walisema kwamba wao ni watu wa **Kristo**. Ni kama walifikiri wao tu peke yao walikuwa watu wake!

1:13 Paulo alikemea mawazo yale na ukali ndani ya mashairi 13-17. Jamii namna hizi zilikana umoja wa mwili wa **Kristo**. Kwa njia ya kufungana na kufuta viongozi vya dunia walikuwa wakizaraau Mwokozi wao ambaye alisulibishwa kwa ajili yao. Wakichagua kuitwa na jina la mtu, walisahau kwamba kwa wakati wa ubatizo wao walikuwa wamekiri kwa mba watakuwa wafuata waaminifu wa Bwana Yesu.

1:14 Kusimama kwa jamii hizi kuli-amusha asante rohoni mwa Paulo kwa

sababu **alikuwa amebatiza watu wachache** tu ndani ya kanisa lile. Alitaja majina ya watu wawili tu, ndio **Krispo**, na **Gayo**.

1:15, 16 Asingalitaka kamwe kwa mtu **kusema** kwamba alibatiza **katika jina lake mwenyewe**. Hakutaka kukokota watu wamfuate yeye, naye awe mkubwa wao. Alitaka neno moja tu, ndilo kufikisha wanaume na wanawake karibu na Bwana Yesu Kristo.

Halafu Paulo alikumbuka vilevile kwa mba alibatiza watu wa nyumba ya Stefano, lakini hakukumbuka kama alibatiza watu wengine.

1:17 Alieleza kwamba **Kristo hakumtuma** zaidi **kubatiza** watu, **lakini kuhubiri Habari Njema**. Hakutaka kusema kwamba ubatizo haukuhitajiwa. Alikuwa ametaja majina ya watu wachache ambao alibatiza yeye mwenyewe. Lakini ni kama aliweka kazi ya ubatizo mikonomi mwa watu wengine, labda Wakristo wengine wa kanisa. Lakini shairi hili linaonyesha kwamba mtu anaweza kupata wokovu bila kubatizwa. Kama ubatizo ungalihitajiwa kwa wokovu, ni kama Paulo angalisema alikuwa na asante kwa sababu alikuwa ameokoa Krispo na Gayo tu! Mawazo namna hii hayafai hata kidogo.

Ndani ya mwisho wa shairi 17, Paulo alienendelea kusema kwamba **hakuhubiri Habari Njema** kwa **akili ya maneno, msalaba wa Kristo usifanyizwe kuwa bure**. Alifahamu kwamba watu wakishangaa juu ya uzuri wa masemo yake, neno hili litaharibu neno alilotaka, ndilo kuonyesha maana ya kweli ya **msalaba wa Kristo**.

Itatusaidia kufahamu na kukumbuka kwamba Wakorinto walikuwa Wayunani waliopenda sana hekima ya watu. Waliheshimu wenye elimu sana, kama wangalikuwa wahodari wa taifa lao. Ni kama roho namna hii iliingia kanisa la

Korinto. Wengine wa waamini walitaka kugeuza Habari Njema kidogo kupeendeza akili ya wenyewe hekima kupita. Ni kama kutaka kwao kupendeza akili ya watu kupita kulikuwa moja la maneno yaliyosukuma watu kuanza jamii mballimbali, kila jamii wakiwa na kiongozi yake. Lakini haifai hata kidogo kujaribu kutengeneza Habari Njema kusudi ikubalilwe kupita na wenyewe elimu. Hekima ya Mungu inapita hekima ya watu sana, na ni bure kujaribu kuzipatanisha.

Halafu Paulo alionyesha kwamba ni pumbavu kutukuza watu, na ya kwamba kufanya hivi hapatani hata kidogo na Habari Njema (1:18 – 3:4). Neno la kwanza aliloonyesha ni ya kwamba habari za msalaba ni mbalimbali kabisa na maneno yote ambayo watu wanafikiri ni hekima ya kweli (1:18-25).

1:18 Neno la msalaba kwao wanapotea ni upumbavu. Barnes alianandika:

Mauti juu ya msalaba ilififikirisha watu juu ya mambo yote ya haya na aibu. Kusema juu ya wokovu kwa njia ya mateso na mauti ya mtu aliyesulibishwa kuliamsha zarau tu rohoni mwao.¹

Wayunani walipenda hekima, lakini hakuna neno ndani ya Habari Njema lililoweza kupendeza kiburi chao cha elimu.

Kwa wale waliokuwa wakiokolewa, Habari Njema ni **uwezo wa Mungu**. Wanasiakia Habari Njema kwa imani, na ajabu ya uzazi wa pili unafanywa ndani ya maisha yao. Ona ya kwamba ndani ya shairi hili kuna watu namna mbili tu, wale wanaopotea, na wale wanaokolewa. Watu wanapenda hekima yao ya mwanadamu, lakini Habari Njema tu inaongoza watu kupata wokovu.

1:19 Isaya alitabiri ya kwamba Habari Njema itachukizwa na akili ya watu (Isa. 29:14):

“... akili za watu wao wenyewe akili zi-

tapotea, na ufahamu wa wenyewe akili utafichwa.

Mungu anapenda sana kufanya mashaari yake kwa njia zinazoonekana pumbavu kwa watu, lakini hata wenyewe elimu wakizizarau, zinatimiza makusudi yake kwa njia ya ajabu. Kwa mfano, watu wa dunia wanafikiri wanaweza kufanya kazi kuwastahilisha kupokea wokovu. Habari Njema inaonyesha kwamba masumbuko yote ya watu kujiokoa wenyewe ni bure, na ya kwamba watu wanaweza kufikia Mungu kwa njia ya Kristo tu.

1:20 Halafu Paulo aliwauliza na roho kali: “**Mwenye akili ni wapi? Mwandishi ni wapi? Mwenye ubishi wa dunia hii ni wapi?**” Mungu alilizana nao wakati alipofanya shauri kwa wokovu wa watu? Wangaliweza peke yao, na akili yao wenyewe kutengeneza shauri namna hii kwa ukombozi wa watu? Waliweza hata mara moja kuhakikisha ya kwamba neno lo lote Mungu alilosema halikuwa kweli? Sivyo! **Mungu alifanya akili ya dunia hii kuwa upumbavu.**

1:21 Mtu hawezi na **hekima** yake mwenyewe kujua Mungu. Kwa mia za miaka Mungu aliwapa watu njia kujuana naye, lakini walishindwa. Halafu **ilipendeza Mungu**, kwa njia ya kuhubiri habari za msalaba, **habari** zilizokuwa pumbavu kwa mafikiri ya watu, **kuwaokoa wanaoamini**. Habari zilizokuwa **pumbavu** ndizo habari juu ya msalaba. Tunajua kwamba si habari za upumbavu, lakini kwa mtu mwenyewe nia iliyo kwanza giza zilikuwa kama upumbavu. Vizuri tuwaze sana juu ya shairi hili, na kweli kubwa tunayopata ndani yake.

1:22 Ilikuwa desturi ya **Wayuda kutaka kuona alama**. Walikuwa tayari kumaini ajabu. Lakini **Wayunani** walitafuta **hekima**. Waliweka roho juu ya mafikiri ya watu.

1:23 Lakini Paulo hakuwapendeza. Alisema, “**Tunahubiri Kristo aliyesulibiwa**.” Mtu mmoja alisema juu ya Paulo

kwamba "Hakuwa Myuda aliyetafuta alama, wala Myunani aliyependa hekima, lakini Mkristo aliyependa Mwokozi."

Kwa Wayuda, Kristo aliyesulibishwa alikuwa **kikwazo**. Walitazamia kiongozi mkubwa wa jeshi la askari kuwaponyesha toka taabu ya utawala wa Waroma. Lakini Habari Njema ilikuwa juu ya Mwokozi aliyefungwa juu ya msalaba wa haya. **Kwa Wayunani**, Kristo aliyesulibishwa alikuwa **upumbavu**. Iliwashinda kufahamu namna gani Mmoja aliye-shindwa na aliyekufa katika uzaifu mkubwa namna hii ataweza kuwasaidia ndani ya masumbuko yao.

1:24 Ni ajabu kuona kwamba maneno yale Wayuda na Wayunani waliyotafuta yanapatikana ndani ya Bwana Yesu. Kwa wale wanaosikia mwito wake na kumwamini, **Wayuda na Wayunani vile-vile, Kristo ni nguvu na akili ya Mungu**.

1:25 Lakini Mungu hana ujinga wala uzaifu. Paulo alikuwa akisema ndani ya shairi hili ya kwamba maneno ambayo watu wanafikiri ni **upumbavu** wa Mungu ni **akili kubwa kupita akili ya watu**. Na maneno watu wanayofikiri ni **uzaifu** wa Mungu ni maneno ya **nguvu kupita** neno lo lote **watu** wanalloweza kufanya.

1:26 Nyuma ya kusema juu ya Habari Njema, Paulo alianza kusema juu ya watu amba Mungu anaita na Habari Njema (mash. 26-29). Alikumbusha Wakorinto kwamba **si wengi wenye akili ya mwili, si wengi wenye nguvu, si watu wakubwa wengi wanaoitwa**.

Wakorinto hawakuwa wenye elimu sana, lakini walikuwa wameamini Habari Njema isiyokuwa nguvu kufahamu. Basi kwa sababu gani waliweka roho sana juu ya hekima ya watu wa dunia na kutukuza wahubiri waliojaribu kufanyiza Habari Njema kuwa tamu kupita kwa watu wa dunia?

Watu wakitaka kujenga kanisa, wata-andikisha watu wakubwa na wenye he-

shima zaidi wa mji kuwasaidia. Lakini shairi 26 linafundisha kwamba Mungu hafikiri watu waheshimiwa wa dunia. Anaita watu wale wasio wakubwa kwa macho ya watu.

1:27 Mungu alichagua vitu vipumbavu vy a dunia kupatiza wenye akili haya; na Mungu alichagua vitu zaifu vy a dunia kupatiza vitu vy a nguvu haya.

Alitumika na baragumu kuangusha kuta za Yeriko. Alipunguza jeshi la Gideoni toka watu 32.000 kufika watu 300 kwa kufukuza majeshi ya Midiani. Alitumika na fimbo ya ngombe mkononi mwa Samugari kushinda Wafilistini. Na mfupa wa kinywa cha punda aliwezesha Samusoni kushinda jeshi zima. Na .Bwana wetu alikulisha watu kupita 5000 na mikate na samaki wachache tu.

1:28 Paulo aliongeza ya kwamba Mungu alichagua vilevile **vitu vinyonge vy a dunia, na vitu vinavyozarauliwa, na visivyo**, na anatumika na vitu namna hii **kufanya vitu viliyyo viwe bure**. Mungu anapenda kukamata watu wasio na heshima duniani, na kutumika nao kuji-tukuza mwenyewe. Mashairi haya yan gepasa kukemea Wakristo wanaotafuta urafiki wa watu wa kujulikana duniani na wanaoona waamini wengine bure.

1:29 Mungu anachagua na kusudi watu wasio na heshima duniani ili ye ye mwenyewe apokee heshima yote, si watu. Wokovu ni wa Mungu pekee, hivi ye ye peke yake anastahili kupokea sifa.

1:30 Shairi hili linaonyesha tena kwamba vyote tulivyo vinatoka kwa Mungu – si kwa mawazo ya watu, hivi hakuna njia kwa watu kupata utukufu. Kristo **alifanyizwa kwetu akili**. Yeye ni akili ya Mungu (sh. 24), yule Mungu kwa akili yake alichagua kuwa njia ya wokovu. Yeye ni **haki** yetu vilevile. Kwa njia ya imani ndani yake Mungu mtakatifu anatuhesabia haki. Naye ni **utakaso** wetu. Sisi wenyewe hatuna utakatifu, lakini ndani ya Kristo na kwa uwezo

wake tunatakaswa kupita na kupita. Mwishoni, ye ye ni **ukombozi** wetu, zaidi kwa wakati wa mwisho, saa atakapokuja na kutupeleka kwake, na wakati tutakapokombolewa – roho, nafsi, na mwili pia.

1:31 Mungu alitayarisha baraka hizi zote kwa sisi **katika Bwana**. Hivi Paulo aliuliza, ‘‘Ni faida gani kujisifu ndani ya watu? Hawawezi kuwafanya nini hata moja la maneno haya.’’

2:1 Halafu Paulo alikumbusha wamini habari za utumishi wake katikati yao, na ya kwamba alijaribu kutukuza Mungu, si ye ye mwenyewe. Alifika kwao akihubiri **ushuhuda wa Mungu**, si kwa **maneno** (usemi) **makubwa, wala kwa maneno** (usemi) **ya akili**. Hakutaka watu kufikiri kwamba ye ye ni msemaji au mwenye elimu kubwa, lakini alihubiri kweli ya Mungu na kusudi la kutukuza Kristo, na kusaidia miyo na zamiri za wasikiaji wake.

2:2 Paulo alihubiri juu ya **Yesu Kristo, naye amesulibishwa**. Yesu Kristo linasema juu yake mwenyewe; **naye amesulibishwa** ni juu ya kazi yake. Hizi ndizo habari kubwa za Habari Njema.

2:3 Paulo alisema vilevile juu yake mwenyewe, kwamba hali yake haikuwa namna ya kuvuta roho za watu. Alikuwa katikati ya Wakorinto **katika uzaifu, na katika woga na katika matetemeko mengi**. Habari Njema ilikuwa ndani ya chombo cha udongo, hata ukubwa wa kuzidi wa uwezo uwe wa Mungu, si wa Paulo. Paulo alikuwa mfano ye ye mwenyewe wa namna Mungu anavyotumika na vitu zaifu kupatiza vitu vya nguvu haya.

2:4 Wala **neno** la Paulo wala **mahubiri** yake hayakuwa kwa **maneno ya akili ya kushawishi** watu, lakini **katika onyesho la Roho na la nguvu**. Watu wengine wanafikiri kwamba **neno** lake ndilo habari alizohubiri, na **mahubiri** yake ni namna alivyozihubiri. Wengine wanafikiri **neno** lake ni ushu-

hua wake kwa watu mmoja mmoja, na **mahubiri** zake ni hotuba zake kwa watu wengi. Labda watu wa dunia wasingalisi Paulo kuwa msemaji wa kuju likana, lakini **Roho ya Mungu** alitumika na hotuba zake kufahamisha watu zambi zao na kuwaleta kwa Mungu.

2:5 Paulo alifahamu kwamba ilikuwa hatari kwa watu kufikiri juu yake mwenyewe kupita kuweka roho juu ya Bwana aliye hai. Alijua vizuri ya kwamba hakuweza ye ye mwenyewe kubariki, wala kuokoa, hivi lilikuwa kusudi lake kuongoza watu kuamini **Mungu** peke yake, si kutegemea **akili ya watu**. Sharti hili liwe kusudi la wahubiri wote wa Habari Njema na la wenye kufundisha Neno la Mungu.

2:6 Kwanza, **akili** tunayoona ndani ya Habari Njema inatoka kwa Mungu (mash. 6, 7). **Tunasema akili katikati yao walio watimilifu**, ndio wenye kukomea. Lakini si **akili ya dunia hii**, na **watawala wa dunia hii** wasingalifiki ni akili. Akili yao, nao wenyewe ni kwa muda mfupi tu.

2:7 **Tunasema akili ya Mungu katika siri**. Siri ndani ya Agano Jipyaa ni kweli isiyofunuliwa mbele, lakini sasa mitume na manabii wa mwanzo wa muda wa kanisa walifunua kwa wamini. Siri hii ni **akili ya Mungu ili yofichwa**, Mungu aliyoomuru mbele **ya muda wa dunia, kwa utukufu wetu**. Siri ya Habari Njema ni kweli ya ajabu kwamba *sasa* Wayuda na Mataifa wanakutanishwa kwa umoja ndani ya Kristo; ya kwamba Bwana Yesu atakuja na kutupeleka kwake watu wake amba wanamngoeja; na ya kwamba si wamini wote watakufa, lakini wote watageuzwa.

2:8 **Labda watawala wa dunia hii** ndio pepo za Shetani katika pahali pa mbingu au watu amba wanawatumikia duniani. Hawakufahamu akili ya siri ya Mungu (ndiyo Kristo msalabani), na ya kwamba wao wenyewe wataharibiwa

kama wakimwua. **Kama wangalifa-hamu** shauri la Mungu **wasingalisulibisha Bwana wa utukufu.**

2:9 Ndani ya mashairi 9-16 tunasoma namna gani kweli hizi za ajabu zili-funuliwa kwa mitume na Roho Mtakatifu, namna gani mitume waliongozwa na Roho Mtakatifu kuzipitisha kwetu, na namna gani Roho Mtakatifu anatusaidia kuzifahamu.

Maneno toka Isaya 64:4 ni unabii ya kwamba Mungu aliweka akiba kweli hizi za ajabu ambazo watu hawakuweza kujua, lakini kwa wakati unaofaa atazi-funua kwa **wenye kumpenda**. Hata tukiwa na **macho** na **masikio** na **moyo** kujifunza maneno ya dunia, tunahitaji Roho ya Mungu kupokea kweli za Mungu.

Watu wengi wanafikiri shairi hili linasema juu ya utukufu wa mbingu, lakini lina maana nyingine vilevile. Paulo alikuwa akisema juu ya kweli zili-zofunuliwa mara ya kwanza ndani ya Agano Jipy. Watu hawakuweza kamwe kuvumbua kweli za Mungu.

2:10 Maneno haya, **Mungu aliya-funua kwetu kwa Roho yake**, yanahakikisha kwamba shairi 9 si juu ya mbingu. Kweli hizi zilizotabiriwa ndani ya Agano la Kale zilijulishwa kwa mitume ya muda wa Agano Jipy. Neno hili **kwetu** linasema juu ya waandishi wa Agano Jipy. Ni **Roho** ya Mungu aliyetia nuru mitume na manabii, kwa **sababu Roho anatafuta maneno yote, hata mafumbo ya Mungu**. Ni kusema, Roho ya Mungu, aliye mmoja wa Uungu, ni mwenye hekima na ufahamu bila mpaka, na anafahamu kweli zote za Mungu, na anaweza kuzipasha kwa watu.

2:11 Hata katikati ya watu hakuna mtu anayeweza kujua mafikiri ya mtu ila **mtu** mwenyewe. Hakuna mtu mweenge anayeweza kujua mafikiri yake kama asipomjulisha. Na zaidi ya ile, kwa kuweza kufahamu mawazo ya mtu,

inapasa mtu kuwa **na roho ya mtu**. Nyama haiwezi kufahamu mawazo yetu vizuri. Ni vivyo hivyo na Mungu. Kuna mmoja tu anayeweza kufahamu maneno ya Mungu, ndiye **Roho ya Mungu**.

2:12 Shairi hili linapasha juu ya waandishi wa Agano Jipy, hata kama maneno haya ni kweli juu ya waandishi wote wa Biblia. Mitume na manabii waliwuwa wamepokea Roho Mtakatifu, naye aliweza kuwajulisha kweli za Mungu. Hii ndiyo maana ya maneno aliyosema ndani ya shairi hili: “**Lakini hatukupokea roho ya dunia, lakini Roho anayetoka kwa Mungu; kusudi tupate kujua zawadi tulizopewa na Mungu.**” Ni kwa njia ya **Roho anayetoka kwa Mungu** tu mitume walilweza kupokea kweli toka Mungu ambazo Paulo alisema juu zao, na zinazochungwa kwa sisi katika Agano Jipy.

2:13 Nyuma ya kuonyesha namna gani waandishi wa Maandiko Matakatifu walipokea kweli toka Mungu, Paulo anaendelea kuonyesha namna gani, kwa njia ya maongozi ya Mungu, sisi tulijulishwa kweli hizi. Shairi hili ni moja la mashairi katika Biblia yanayoonyesha wazi zaidi kwamba kila neno moja moja linaongozwa na Mungu. Mtume Paulo alisema wazi saa alipotuambia kweli hizi, ya kwamba mitume hawakusema **maneno** wao wenyele waliyochagua, au **yaliyofundishwa na akili ya watu**. Yalikuwa maneno **ambayo Roho Mtakatifu** aliaongoza kusema. Hivi tunamini kwamba maneno yaliyoandikwa zamani ndani ya maandiko ya kwanza yalikuwa maneno ya Mungu mwenyewe (na ya kwamba tunaweza kuamini kabisa Biblia tulio nayo).

Watu wengi wananguunika ya kwamba maneno haya yanasema Mungu alilazimisha mwandishi kuandika maneno *kama mashini* bila namna ya mtu mwenyewe kuonekana ndani ya maandiko yake. Lakini kama mfano, tunajua kwamba namna ya kuandika ya

Paulo ilikuwa namna nyingine na ile ya Luka. Namna gani tunaweza kupatanisha neno hili na upuzio wa Roho Mtakatifu wa kila neno? Hatufahamu namna gani Mungu aliweza kutoa kila neno la Maandiko Matakatifu, pamoja na kuacha namna ya kuandika ya waandishi wenye we nyewe kuonekana ndani ya neno lake kamilifu.

Kuna njia mbalimbali kueleza maana ya **tukifananisha maneno ya Roho na maneno ya Roho**. Labda maana yake ni (1) kufundisha kweli za roho na masemo yanayoletwa na Roho; (2) kuptisha kweli za roho kwa watu wenye Roho; au (3) kufananisha kweli za roho ndani ya sehemu moja ya Biblia na zile ndani ya sehemu nyingine. Tunafikiri elezo la kwanza ni zuri kupita maelezo yale mengine. Paulo anasema kwamba maongozi ya kweli ya Mungu ni kuptisha kweli ya Mungu na masemo yanayochaguliwa na Roho Mtakatifu kwa kazi hii. Tungeweza kusema: “kunyaresha kweli za Roho na maneno ya Roho.”

Watu wengine wanasema mashairi haya hayawezi kuwa juu ya upuzio wa Roho Mtakatifu kwa sababu Paulo ali-sema, **tunasema**, si “tunaandika.” Lakin tunaona neno hili “kusema” mara nyingine vileyile katika maandiko yaliyoongozwa na Mungu (ona Yn. 12:38, 41; Mdo. 28:25; 2 Pet. 1:21).

2:14 Hivi tumeona kwamba ni Mungu aliyefunua na kuongoza Habari Njema. Sasa tunaona neno lingine: tunaweza kuipokea kwa uwezo wa **Roho ya Mungu tu**. Bila kusaidiwa, **mwenye kufuata tabia ya asili hapokei maneno ya Roho ya Mungu, kwa sababu maneno haya ni upumbavu kwake**. Hawezi hata kidogo kuyafahamu, **kwa sababu yanatambulikana na Roho tu**.

2:15 Lakini mtu yule anayetiwa nuru na Roho Mtakatifu wa Mungu anaweza kutambua kweli hizi za ajabu, hata kama **hatambuliwi vizuri yeye mwenye we**

na wasioamini. Labda yeye ni seremala, au mvuvi, lakini pamoja na kazi ile ana-jifunza sana Maandiko Matakatifu. Ni nguvu kwa watu wa dunia kumfahamu. Labda hakujifunza ndani ya université, au seminaire, lakini hata hivi anaweza kufahamu siri za neno la Mungu, na labda kuyafundisha kwa watu wengine.

2:16 Sasa mtume anauliza pamoja na Isaya: “**Nani aliyejua nia ya Bwana, amfundishe?**” Jibu lenyewe ni wazi. Haiwezekani kwa watu kujua Mungu kwa njia ya hekima au uwezo wao. Wanawea kumjua tu saa yeye mwenye we anapochagua kujifunua. Lakini watu wale walio na **nia ya Kristo** wanawea kufahamu kweli za ndani za Mungu.

Hivi ndani ya mash. 9-12 tunaona kwanza *ufunuo*. Kwa njia ya Roho Mtakatifu Mungu alifunua kweli watu wasizoja mbele.

Ndani ya shairi 13 tunaona *maongozi*. Mitume (na waandishi wote wengine wa Biblia) walitumika na maneno yale yale tu ambayo Roho Mtakatifu aliwapa kuptisha kwa watu wengine.

Mwishoni, iliwezekana kwa watu kufahamu kweli hizi za ajabu kwa njia ya *mwangaza* wa Roho Mtakatifu tu (mash. 14-16).

3:1 Wakati Paulo alipofikia Korinto kwanza, alikuwa amekunywesha waamini na ‘maziwa’ ya Neno la Mungu, maana aliwafundisha maneno yasiyokuwa nguvu kufahamu kwa sababu walikuwa waamini wa sasa na wenye imani zaifu. Wasingalipata faida kwa njia ya mafundisho ya kweli za ndani ya roho. Walikuwa waamini wa sasa tu, kama **watoto wadogo katika Kristo**.

3:2 Paulo alikuwa amewafundisha kweli za mwanzo tu aliyoita **maziwa** kwa sababu walipata nguvu nusu tu katika imani. Vivyo hivyo Bwana Yesu alisema na wanafunzi wake, “Ningali na maneno mengi kuwaambia ninyi, lakini hamuwezi kuyabeba sasa” (Yn. 16:12). Ilikuwa huzuni kwa sababu hata kwa wakati ule

Wakorinto walikuwa hawakukomea ya kutosha kupokea mafundisho ya kweli za ndani kupita.

3:3 Walikuwa **hata sasa** watu **wa mwili**, maana hawakufikiri maneno ya roho. Kwa sababu hii kulikuwa na **wivu** na **ugomvi** katikati yao. Maneno ya namna hii ni alama ya watu wa dunia hii, si wa watu wanaoongozwa na Roho ya Mungu.

3:4 Wakisimamisha jamii, na wakite-gemea uongozi wa binadamu, kama **Paulo** na **Apolo**, walitenda kama watu wa dunia. Hii ndiyo maana ya ulizo la Paulo, “ninyi si watu wa mwili?”

Kufika sasa Paulo alieleza Habari Njema kuonyesha ujinga wa kutukuza mtu. Sasa anaonyesha kwamba ndani ya utumishi kwa Bwana, ni upumbavu kupandisha viongozi wa dini kwa njia ya kjenga vyama kuwapendelea.

3:5 **Apolo** na **Paulo** walikuwa *watumishi kwa njia yao* Wakorinto waliamini Bwana Yesu. Walikuwa watendaji tu, si viongozi vya jamii mbalimbali. Ulikuwa ujinga kabisa kwa Wakorinto kufanyiza watumishi hawa kuwa viongozi.

3:6 Akitumika na mfano wa kulima shamba, Paulo alionyesha kwamba mlimajji anaweza kufanya maneno nusu tu. **Paulo** mwenyewe aliweza kupanda mbegu, na **Apolo** aliweza kutia mbegu hizi maji, lakini ni **Mungu** tu **anayekuza**. Ni vivyo hivyo leo. Wengine wanaweza kuhubiri Neno la Mungu na sisi sote tunaweza kuombea ndugu na rafiki zetu wasioamini bado, lakini ni Bwana tu anayeweza kuwaokoa.

3:7 Hivi tunaona kwamba mwenye kupanda na mwenye kutia maji hawana kazi kubwa. Hawawezi kutoa uzima. Kwa sababu gani watumishi Wakristo wata-shindana? Ingepasa kila mtu kufanya kazi aliyopewa, na kufurahi wakati Mungu anapobariki kazi yenyewe.

3:8 **Yeye anayepanda na yeye anayetia maji ni mmoja**, maana yake wao wawili wanashiriki ndani ya kazi moja.

Haifai wawe na uwivu. Mmoja wao hama heshima kupita ndugu yake. Kwa wakati wa kuja **kila mtu atapokea mshahara wake** mwenyewe kwa kipimo cha masumbuko yake. Siku ile ndiyo Kiti cha Hukumu cha Kristo.

3:9 Wote ni wenyewe madaraka kwa Mungu. Wote ni watumishi wake, **wafanya kazi pamoja** ndani ya **shamba** la mavuno la **Mungu**; au tungeweza kusema wakijenga **nyumba** moja pamoja. Erdman alitoa wazo hili: “Sisi ni watu wa kazi pamoja, na tuko mali ya Mungu, na tunatumika pamoja.”²

3:10 Paulo alikaa kufikiri juu ya jengo, na alikiri kwamba ilikuwa **neema ya Mungu** tu ambayo ilimwezesha kufanya kazi yake. Ni Mungu ambaye alimwezesha kufanya kazi ya mtume asiyostahili kufanya. Halafu aliendelea kupasha juu ya kazi yake kwa mwanzo wa kanisa hili kwa Korinto: “**Sawasawa mjenga mkubwa mwenye akili, niliweka msingi.**” Alifikia Korinto na kuhubiri habari za Kristo na kusulibishwa kwake. Watu waliokolewa na kanisa lilisimamishwa kwa pahali pale. Halafu aliongeza, “**Na mtu mwingine anajenga juu yake.**” Bila shaka alifikiri juu ya walimu waliofikia Korinto nyuma yake na kujenga juu ya msingi uliokwisha kuwekwa, na aliwaonya: “**Lakini kila mtu aangalie namna gani anavyojenga juu yake.**” Alitaka wasomaji kufahamu ya kwamba ni kazi nzito na ya heshima kufundisha Neno la Mungu kanisani. Wengine walikuwa wamefikia Korinto na mafundisho yaliyotenga waamini na yasi-yopatana na Neno la Mungu. Bila shaka Paulo alijua habari za walimu hawa wakati alipokuwa akiandika maonyo haya.

3:11 Nyumba inahitaji msingi mmoja tu. Nyuma ya kuuweka mara ya kwanza, hauhitaji kuwekwa tena kamwe. Mtume Paulo alikuwa ameweke msingi wa kanisa la Korinto. **Msingi** huu alikuwa **Yesu Kristo mwenyewe**, na kazi yake.

3:12 Labda si mafundisho yote ya walimu watafaofikia kanisa nyuma yatakuwa

na faida sawasawa. Kwa mfano, mafundisho mengine yatakuwa na faida sana ya kudumu siku nyingi, kama **zahabu, feza, au vito vya damani**, kama mawe magumu sana, au marimari yaliyotumiwa kujenga mahekalu ya bei kubwa. Au labda mafundisho ya walimu wengine yalikuwa na faida nusu, au labda kukosa faida. Mafundisho namna hii yanasaawanishwa na **miti au nyasi au majani**.

Mara nyingi watu wanatumika na mashairi haya kufundisha juu ya maisha ya Wakristo wote. Sisi sote tunajenga, kila siku, na matunda ya kazi hii yataonekana siku nyingine, lakini mwenye kujifunza Biblia sana atafahamu kwamba mashairi haya ni zaidi juu ya wahubiri na walimu, si juu ya waamini mmoja mmoja.

3:13 Siku nyingine, **kazi ya kila mtu itaonekana wazi**. **Siku** ile ndiyo siku ya Kiti cha Hukumu cha Kristo wakati utumishi wote kwa Bwana utakapoangaliwa. Kuangalia utumishi huu kutasawanishwa na moto. Kazi iliyotokuza Mungu na kubariki watu haitaumizwa na moto. Lakini kazi iliyoleta matata katikati ya watu wa Mungu na haikuwapatisha nguvu katika imani yao, itateketewa. **Moto utajaribu kazi ya kila mtu, ni ya namna gani**.

3:14 Kuna namna tatu za kazi wakati tunapowaza juu ya kanisa. Ndani ya shairi 14 tunaona namna ya kwanza – kazi ya mtumishi iliyokuwa na faida na inayobaki wakati inapoangaliwa kwa Kiti cha Hukumu cha Kristo. Mwenye kuitenda **atapokea zawabu**.

3:15 Namna ya pili ya kazi haina faida. Mtendaji wa kazi namna hii **atapata hasara**, hata kama **ye ye mwenyewe ataokolewa, lakini ni kama kwa moto**. Maana ya hasara hapa si kupoteza kitu mtu alichokuwa nacho mbele. Shairi hili linaonyesha wazi kwamba Kiti cha Hukumu ya Kristo si juu ya zambi za mwamini na azabu yao. Bwana Yesu Kristo mwenyewe alibeba azabu ya zambi zake kwa msalaba wa Kalvari. Kiti cha hukumu cha Kristo hakiangalii wokovu

wa mwamini, lakini utumishi wake.

Kanisa Katoliki halifahamu tofauti katikati ya wokovu na zawabu, na wanatumika na shairi hili kusimamisha mafundisho yao ya purgatoire. Lakini tukiangalia shairi hili karibu karibu tunaona ya kwamba moto huu si juu ya kusafisha tabia ya mtu hata kidogo. Moto huu una-jaribu kazi ya mtu, kama ni nzuri au mbaya. Mtu mwenyewe anaokolewa, hata kama kazi zake zinachomwa.

Mara nyingine Neno la Mungu lina-sawanishwa na moto (ona Isa. 5:24 na Yer. 23:29). Tunaweza kutumika na neno hili la Mungu hata sasa. Tukijenga kupatana na mafundisho ya Biblia, kazi yetu haitachomwa siku ya Kiti cha Hukumu cha Kristo.

3:16 Paulo anakumbusha waamini ya kuwa wao ni **hekalu la Mungu** (mahali takatifu), na **ya kwamba Roho ya Mungu anakaa** ndani yao. Kila mwamini ni hekalu la Mungu vilevile, lakini hapa Paulo anafundisha juu ya kanisa zima, jamii moja, na anataka wafahamu ya kwamba mwito huu mtakatifu ni heshima kubwa.

3:17 Namna ya tatu ya kazi kanisani ni kazi ya kuleta uharibifu. Ni kama walimu wa uwongo walikuwa wamefikia kanisa, na mafundisho yao yaliongoza waamini katika zambi, si katika mwenendo mtakatifu. Hawakufikiri ni neno kubwa kuleta maangamizi makubwa namna hii kanisani. Kwa sababu hii Paulo alitangaza na ukali, “**Kama mtu akiharibu hekalu la Mungu, Mungu atamharibu yeye**.” Maana yake, kama mtu akiingia kanisa la pahali fulani na kuharibu ushuhuda wake, **Mungu atamharibu yeye**. Mashairi haya ni juu ya walimu wa uwongo wasio waamini wa kweli. Mwisho wa shairi 17 unaonyesha ukubwa wa kosa hili, “**Kwa sababu hekalu la Mungu ni takatifu, ninyi ni hekalu lile**.”

3:18 Ni hatari kwa Wakristo kujidanganya wenyewe kwa maneno ya mwenendo na utumishi wao. Labda wengine

wa wale waliofikia Korinto walisema wao ni walimu wenye elimu nyingi. Ni lazima kwa wale wanaowaza wao ni wenye hekima nyingi ya dunia wajifunze kwamba inapasa wageuke wapumbavu kwa macho ya watu wa dunia ili wageuke **wenye akili** kwa macho ya Mungu.

3:19 Akili ya dunia hii ni upumbavu mbele ya Mungu. Mtu na akili yake asingaliweza kamwe kujua Mungu, wala kutengeneza njia kwa Mungu kugeuka Mtu na kusudi la kufia wenye zambi, waovu na wenye hatia. Shairi hili linataja maneno toka Yobu 5:13 kuonyesha kwamba Mungu anashinda akili ya watu, na kutimiza makusudi yake mwenyewe. Hata watu wakijifunza sana, hawawezi kuzuiza mashauri ya Mungu, na mara nyingi Mungu anawaonyesha kwamba hata wakiwa na elimu nyingi ya dunia, wao wanakosa uwezo, nao ni masikini kabisa.

3:20 Maneno ya Zaburi 94:11 yanatajwa hapa kuonyesha kwamba **BWANA anajua** mawazo yote ya **watu wenye akili** ya dunia, na ya kwamba **mawazo yale ni bure** na bila faida. Basi kwa sababu gani Paulo anaweka roho sana kuonyesha kwamba elimu ya dunia ni bure? Kwa sababu Wakorinto waliheshimu elimu namna hii sana, na waliufata viongozi wenye kuonekana kuwa na elimu nyingi.

3:21 Nyuma ya maneno yote yaliyosemwa, haikufaa kwa **mtu ye yote kusifia watu**. Na tukiwa mmoja wa watumishi wa kweli wa Mungu, haifai tujisifu juu ya neno hili lakini tufahamu kwamba wao wote ni wetu. Ndiyo, **vyote ni vyenu**.

3:22 Mtu mmoja alisawanisha shairi 22 na “orodha ya vyote vilivyo mali ya mtoto wa Mungu.” Watumishi, kama **Paulo**, ndiye mhubiri wa Habari Njema, au **Apolo**, mwalimu, au **Kefa**, mchungaji. Kama wao wote ni wetu, ni upumbavu kwa sisi kuwa mali ya *mmoja* wao. Halafu **dunia** ni yetu. Kama wariti pamoja na

Kristo, tutaipokea siku nyingine, lakini kufika wakati ule, ni yetu kwa ahadi ya Mungu. Watu wanaochunga na kutembeza maneno ya dunia hawafahamu kwamba wanafanya kazi hii kwa sisi. **Uzima** ni wetu, si uzima wa dunia tu, lakini uzima wa kutimia. Na **mauti** ni yetu. Hatuogopi mauti tena kama adui. Ni injumbe wa Mungu kuleta nafsi zetu mbinguni. **Vitu vyta sasa na vitu vyta kuja – vyote ni vyetu vilevile.** Imesemwa kwamba vitu vyote vinatumikia mtu yule anayetumikia Kristo.

3:23 Wakristo wote ni mali ya Kristo. Wengine katika Korinto walisema wao tu ni watu wake, si watu wengine wo wote. Walianza “chama cha Kristo.” Paulo alikataa mawazo namna hii. Alisema sisi sote ni watu **wa Kristo, na Kristo ni wa Mungu**. Alionyesha wazi upumbavu wa kuanza chama na magawanyiko kanisani.

4:1 Paulo hakutaka waamini kumhe Shimu yeye na mitume wengine kupita kipimo, hivi alisema vizuri watu waha-hesabu kama **watumishi** au wasaidizi **wa Kristo na mawakili ya siri za Mungu**. Wakili ni mtumishi anayelinda mtu mwiningine, au mali yake. **Siri za Mungu** zilifichwa mbele, lakini Mungu alizifunua sasa kwa mitume na manabii wa muda wa Agano Jipy.

4:2 Sharti mawakili waonekane kuwa waaminifu. Watu wa dunia wanaweka roho zaidi juu ya akili na hekima, mali, na wenye kuendelea vizuri ndani ya kazi yao; lakini Mungu anatafuta watu watakaokuwa watumishi waaminifu kwa Yesu ndani ya maneno yote.

4:3 Ni nguvu kupima na kufahamu uaminifu wa mawakili. Kwa sababu hii Paulo alisema kwamba kwa macho yake **ni neno dogo sana ahukumiwe** na Wakorinto au **kwa hukumu ya watu**. Alifahamu kwamba haiwezekani kwa mtu kutambua kipimo cha kweli cha uaminifu wa mtu fulani kwa Mungu. Hivi aliongeza kusema, “**sijihukumu mimi mwenye-we**.” Alifahamu kwamba alikuwa mtu tu,

na ya kwamba ni desturi kwa watu kujisifu wenyewe.

4:4 Paulo alisema, “**Sijui neno juu yangu.**” Maana ya masemo haya ilikuwa kwamba ndani ya utumishi wake kwa Kristo hakufahamu kwamba alitenda neno lo lote kwa kutokuaminifu lililohitaji kuhukumiwa. Maana ya masemo haya haikuwa kwamba alifikiri hakutenda zambi yo yote, na kwamba alikuwa mkamilifu. Ndani ya shairi hili inatupasa kuwaza zaidi juu ya utumishi mwaminifu kwa Kristo. Lakini hata kama Paulo hakujua kwamba alikuwa amefanya neno baya lililstahili kuhukumiwa, neno hili **halikumhesabia haki.** Hakuweza kupima neno hili yeze mwenyewe, na alikumbuka kwamba Bwana ndiye Mwamuzi.

4:5 Tukijua maneno haya, inatupasa kukaa na ange wakati tunapowaza juu ya utumishi kwa Kristo. Tunajaribiwa kusifu kazi ya kuonekana mbele ya watu, na kuona bure kazi ya chini na ya maficho. Ni vizuri zaidi **kutokuhukumu neno mbele ya wakati wa kuja kwa Bwana.** Yeye ataweza kuhukumu kazi zote na haki, pamoja na *kwa sababu gani* zilifanywa. **Atafunua makusudi ya miyo**, na hatatoa zawabu kwa kazi yo yote tuliyofanya kujitukuza wenyewe na kusifiwa na watu.

Maana ya “**kila mtu atapata sifa yake toka Mungu**” haiko kwamba kazi ya kila mtu itaonekana kuwa njema siku ile. Maana yake ni kwamba kila mtu *anayestahili*, atapokea sifa **toka Mungu**, si toka watu.

Ndani ya mashairi manane yanayofuata mtume anapasha wazi kwamba magawanyiko katika kanisa kwa Korinto yalianzwa na kiburi ya watu.

4:6 Alieleza kwanza ya kwamba wakati alipofundisha juu ya utumishi kwa Kristo na majaribu ya watu kufuata viongozi vya dunia (3:5–4:5), alitaja jina lake mwenyewe pamoja na lile la **Apolo** kama mifano. Wakorinto hawakufuata

Paulo na Apolo tu, lakini wanaume wengine kanisani vilevile. Kwa sababu ya adabu **Paulo alisema juu yake mwenyewe na Apolo tu** ili kwa njia ya mfano huu waamini wajifunze wasiheshimu viongozi vyao kupita kipimo na wasisimamishe jamii kwa sababu ya kiburi yao wenyewe. Alitaka waamini kupima kila kitu na kila mtu na Maandiko Matakatifu.

4:7 Mwalimu Mkristo akiwa na zawadi kuliko mwalimu mwingine, ni kwa sababu Mungu alimwumba hivi. Kila kitu alicho nacho, alikipewa na Bwana. Maneno yote ambayo tunayo tulipokea kwa Bwana. Kwa nini basi tutakuwa na kiburi? Zawadi zetu si tunda la akili yetu wenyewe.

4:8 Wakorinto walikuwa **wamekwisha kuziba.** Ni kama hawakuhitaji kitu. Walijivuna kwa sababu wengi wao walikuwa na zawadi za roho. Walikuwa wamepata **mali nyangi** na kukaa katika anasa bila hitaji. Walitawala kama wafalme, lakini si pamoja na mitume. Paulo angetaka saa ya kutawala ingalfika ili **aweze kutawala pamoja** nao! Lakini inatupasa kufikiri juu ya saa tunayoishi hapa duniani kama muda wa kututayarisha kwa wakati wa kuja saa tutakapotawala pamoja na Bwana Yesu wakati atakapokuja kusimamisha ufalme wake hapa duniani. Kufika wakati ule ni heshima kwa watu kushiriki naye katika mazarau na kukataliwa kwake. H. P. Barker anatuonya:

Si aminifu hata kidogo kwa sisi kujaribu kupata taji yetu mbele ya Mfalme kupewa taji yake. Lakini hili ndilo neno Wakristo wa Korinto walilofanya. Mitume walikuwa wakilaumiwa kwa ajili ya Kristo. Lakini Wakristo wa Korinto walikuwa “watajiri” na “walihesimiwa” pahali Bwana na Mwalimu wao alipotaabishwa sana.³

Ni desturi kwa mtawala kutiwa taji yake mbele ya saa wakubwa wengine

wanapoweka taji zao. Lakini Wakorinto waligeuza utaratibu huu. Walikuwa wakitawala hata wakati Bwana alipokataliwa!

4:9 Paulo alisawanisha majisifu ya Wakorinto na hali ya **mitume**. Kwa mfano alisema juu yao wenyewe kama wenyewe kutupwa kwa nyama wakali, wa-uwe mbele ya macho ya **watu** na **malaika**.

4:10 Mitume walitendewa kama **wapumbavu kwa ajili ya Kristo**, lakini Wakristo waliheshimiwa kama wenyewe **akili**. Mitume **walikuwa zaifu**, lakini Wakorinto walikuwa na nguvu mwilini. Mitume hawakuheshimiwa, lakini watatifu walipata utukufu.

4:11 Mitume hawakufikiri saa yao ya kushinda au kutawala ilikuwa imefika. Walikuwa wakitaabishwa na **nja na kiu** na ukosefu wa mavazi, na walipata mateso. Walifukuzwa na kukosa **makao**.

4:12 **Walitumika kazi na mikono yao wenyewe** kujipatia vitu walivyohitaji. Walibariki wale ambao waliwatukana. Walivumilia na saburi wakati **walipoteswa** na hawakupigana na watesaji wao.

4:13 Wakati **waliposingiziwa**, wali-sihi watu kupokea Bwana Yesu. Walitendewa kama **uchafu wa dunia, takataka ya vitu vyote**. Habari hizi za mateso kwa ajili ya Kristo zingepasa kugusa roho zetu sisi sote. Kama mtume Paulo angaliishi kwa wakati wa sasa, angaliweza kusema nasi, kama alivyosema na Wakorinto (sh. 8), "Mumetawala kama wafalme pasipo sisi"?

4:14 Ndani ya mashairi 14-21 Paulo anatolea waamini maonyo ya mwisho juu ya matengo. Alieleza ya kwamba **hakusema** maneno haya **kupatiza Wakristo haya**, lakini **kuwaonya kama watoto wake wapenzi**. Hakusema na uchungu, lakini kusaidia roho zao.

4:15 Mtume aliwakumbusha ya kwamba hata **wangeweza kuwa na walimu elfu kumi katika Kristo**, walikuwa na

baba mmoja tu katika imani. Paulo ye ye mwenyewe aliwafikisha karibu na Bwana; alikuwa baba yao kwa maneno ya roho. Watu wengine wengi waliweza kufika kuwafundisha, lakini wasinge-fanya hivi na roho ya mapendo kama yule ambaye aliwafikisha karibu na Mwana-Kondoo. Paulo hakutaka mase-mo yake kupunguza faida ya mafundi-sho ya maneno ya Mungu. Alisema tu kwamba watu wengi wanaweza kufanya kazi kwa Kristo bila kuwa na roho ya mapendo ya kweli kwa waamini, kama mwamini yule ambaye aliwafikisha kwa Kristo.

4:16 **Hivi** Paulo aliwasahi kumwiga ye ye kwa namna alivyojitoa kabisa kwa Kristo bila kujifikiri mwenyewe, na namna alivyopenda na kutumikia wa-amini wenzake bila kuchoka, kama alivyoonyesha ndani ya mashairi 9-13.

4:17 Kwa kuwasaidia ndani ya maneno haya, Paulo alitura **Timoteo, mwana wake mpenzi katika Bwana, karibu nao**. Alitaka Timoteo **kwakumbusha desturi** za Paulo **katika Kristo**, desturi alizofundisha ndani ya kila kanisa. Paulo alisema kwamba alitenda ye ye mwenyewe maneno aliyohubiri. Ingetupasa sisi sote kufanya hivi.

4:18 Wakati Paulo aliposema alikuwa akituma Timoteo, labda wengine wa wa-chongezi wake katika Korinto walisema Paulo aliogopa kufika ye ye mwenyewe. Watu wale **walijivuna** wakati walipofikiri Paulo **hatafika** ye ye mwenyewe.

4:19 **Lakini** aliahidi kwamba **atafika** ye ye mwenyewe nyuma kidogo, **kama Bwana anavyopenda**. Halafu kwa wakati ule ataonyesha wazi kiburi ya watu wale waliokuwa wakisema na ukaramisu, lakini waliokosa **uwezo** wa Roho.

4:20 Lakini ulikuwa **uwezo** uliohitajiwa, kwani **ufalme wa Mungu** ni zaidi juu ya matendo, **si** juu ya masemo.

4:21 Halafu wakiwa na roho ya uasi, **atafika** kwa na **fimbo**. Lakini wakiwa na roho ya utii na unyenyekevu, atafika

kwao na roho ya **mapendo na upole**.

B. Uzini katikati ya waamini (Sura 5)

Sura 5 inafundisha juu ya hitaji la kuzibuzi mwamini mmoja kanisani aliye-kwisha kutenda uzini. Neno hili linahitajiwa kabisa kwa kulinda utakatifu kanisani na kwa macho ya watu wa dunia, na vilevile Roho Mtakatifu aweze kutumika ndani ya kanisa bila kizuizo.

5:1 Imesemwa kwamba mmoja wa wanaume wa kanisa katika Korinto alikuwa ametenda **uzini** mbaya sana, namna hata **Mataifa** wasiojua Mungu hawakutenda. Mtu huyu alikuwa amezini na **mke wa baba yake**. Ni kama mama ya mtu huyu alikuwa amekufa, na baba yake alioa mwanamke mwingine. Tunafikiri hakuwa mwamini kwa sababu hatusomi neno juu yake, maana kanisa halikuwa na amri juu yake.

5:2 Wakristo wa Korinto walitenda nini wakati waliposikia habari hizi? Kwa pahali pa kuhuzunishwa sana, walikuwa na kiburi. Labda walijivuna juu ya uvumilivu wao kwa sababu hawa-kuazibu mkosayi. Au walikuwa wenye kiburi kwa sababu walikuwa na zawadi nyingi za roho kanisani, na kwa sababu hii hawakuwaza sana juu ya neno liliko-kwisha kutokea. Au labda waliweka roho zaidi juu ya *hesabu* ya waamini kanisani kupita juu ya *utakatifu* wa waamini hawa. Labda hawakuwaza kwamba zambi hii ilikuwa neno baya sana.

Munajivuna, wala hamukusikitika hata yeye aliyefanya neno hili aondoshwe katikati yenu. Maneno haya yanatuongoza kufikiri kwamba waamini wangalikuwa na roho ya unye-nyekevu mbele ya Bwana, Bwana yeye mwenyewe angalitenda kuhukumu mkosaji huyu. Erdman alisema:

Ingaliwapasa kufahamu kwamba utukufu wa kweli wa kanisa la Kristo si uwezo kusema vizuri na zawadi za walimu wakubwa wao,

lakini ni utakatifu wa roho na mwenendo wa waamini.⁴

5:3 Hata kama Wakristo hawakuweka roho juu ya kuhukumu tendo baya la ndugu yao, Paulo alisema kwamba yeye **alikuwa amemhukumu** yule ali-yetenda zambi hii, hata kama **hakuwa pamoja** nao yeye mwenyewe.

5:4 Aliwaza juu ya ndugu za kanisa wakikusanyika pamoja kuhukumu mko-saji huyu. Hata kama Paulo hakuwa pale yeye mwenyewe, alikusanyika pamoja nao katika **roho** wakati walipokusanyika **kwa jina la Bwana wetu Yesu Kristo**. Bwana Yesu alikuwa ametolea kanisa na mitume amri kuhukumu matokeo yote ya namna hii. Hivi Paulo alisema angetenda na **uwezo** (amri) **wa Bwana wetu Yesu**.

5:5 Angetolea Shetani mtu huyu, ili mwili uharihiwe, hata roho yake iokolewe katika siku ya Bwana Yesu. Walimu hawapatani wote juu ya maana ya shairi hili. Wengine wanafikiri ni kuondosha mtu huyu kanisani. Inje ya kanisa ndipo pahali pa Shetani (1 Yn. 5:19). Hivi maana ya “kutolea Shetani” ingewondosha kanisani tu. Walimu wengine wanafikiri mitume walipewa uwezo huu kwa wakati ule tu.

Kuna mawazo mbalimbali juu ya maana ya **kuharibiwa kwa mwili**. Watu wengi wanafikiri ni maumivu mwili-ni ambayo Mungu anatumika nayo kuharibu tamaa na desturi za zambi ya mtu huyu. Wengine wanaamini yanasema juu ya kufa polepole ambako kunaleta mtu mwenyewe saa kutubu na kupona.

Sharti tukumbuke ya kwamba mwamini akiazibiwa, kusudi la azabu hii ni kumrudisha tena kwa upatano mzuri na Bwana, **hata roho yake iokolewe katika siku ya Bwana Yesu**. Hatalaaniwa kwa milele. Anaazibiwa na Bwana kwa zambi yake wakati wa maisha ya sasa, lakini **anaokolewa siku ya Bwana Yesu**.

5:6 Sasa Paulo anahamikia Wakorinto juu ya **kujisifu** au kiburi yao. Labda walitoa uzuru na kusema neno hili lilitokea mara moja tu. Ingaliwapasa kujua kwamba **chachu kidogo inachacha fungu zima**. **Chachu** ni mfano wa zambi na uasherati. Mtume alisema kwamba wakiruhusu zambi nusu tu kanisani, zambi hii itaongezeka na kuchafua kanisa zima. Hivi ni lazima kuhukumu zambi na haki na utawa, kwa kulinda usafi na utakatifu wa kanisa.

5:7 Hivi Wakristo waliagizwa **kujisafisha na kutoa chachu ya zamani**. Ni kusema watende na nguvu kuhukumu uovu wote ili waweze kuwa fungu **jipyä**, ndilo **fungu** safi. Halafu Paulo aliongeza: **Kama mulivyo pasipo chachu**. Mungu anawaona ndani ya Kristo kama watakatifu, wenyewe haki, na safi. Hivi mtume anasema kwamba inapasa mwenendo wao kupatana na hali yao.

Kwa sababu Kristo, Pasaka yetu, amekwisha kutolewa kwa ajili yetu. Saa Paulo alipowaza juu ya mkate bila chachu, mafikiri yake yanarudi kwa Karamu ya Pasaka. Mangaribi ya siku ya kwanza ya karamu ilipasa Myuda kuondosha chachu nyumbani mwake. Alipaswa kusafisha nyumba nzima, na kuangalia na nuru ya taa ili ajue kabisa kwamba hata chachu nusu ndogo sana isibaki nyumbani. Kisha alinyanya mikono yake kwa Mungu na kusema, “Eh Mungu, nimeondosha chachu yote nyumbani mwangu, na kama hata hivi nusu ndogo ikibaki, nisijoju, ninaitoa vilevile na roho yangu yote.” Habari hizi ndizo mfano wa namna inavyopasa Mkristo kwa wakati wa sasa kujitenga na uovu wote.

Kuuawa kwa mwana-kondoo ya Pasaka kulikuwa mfano wa mauti ya Bwana wetu Yesu Kristo msalabani. Kuna mashairi mengi mengine katika Agano la Kale yanayoonyesha kwa *mfano* maneno yatakayotokea kwa wakati wa nyuma. Mingi ya *mfano* hii

inatazamia kuja kwa Bwana Yesu kundoa zambi zetu kwa njia ya kujitoa mwenyewe kuwa zabihu kwa zambi.

5:8 Karamu ndani ya shairi hili haiko Pasaka wala Meza ya Bwana, lakini inatufikirisha maisha mazima ya mwamini. Maisha yetu mazima yaye karamu ya furaha. Haitupasi kuifanya na **chachu za zamani** ya zambi, **wala na chachu ya uovu na ubaya**. Wakati tunapofurahi ndani ya Kristo, haifai kwetu kuwa na mawazo mabaya rohoni juu ya watu wengine. Neno hili linaonyesha kwamba mtume Paulo hakusema juu ya chachu namna inayotumiwa kuoka mkate, lakini kama mfano kuonyesha namna zambi inavyochafua kila kitu ambacho inagusa. Tunaagizwa kuishi maisha yetu kwa **mkate usiochachwa, ndio moyo safi na kweli**.

5:9 Paulo aliwaandikia barua mbele kusema kwamba **haifai wachangananyane** na **wazini**. Barua ile ilipotea, lakini neno hili halionyeshi kwamba kuandika Biblia nzima hakuongozwa na Mungu. Mungu hakuongoza kila barua ambayo Paulo aliandika. Barua zile tu Mungu alizoongoza Paulo kuandika zi-meingizwa ndani ya Biblia takatifu.

5:10 Halafu Paulo aliendelea kueleza kwamba wakati alipowakataza kuchanganyana na **wazini**, hakutaka kusema kwamba iliwapasa kujitenga kabisa na watu wa zambi namna zote. Wakati tuko hapa duniani, tuna kazi na wasioamini, na hatuwezi kujua kama waliwisha kufanya zambi gani. Kwa kujitenga nao wote, **ingetupasa kutoka katika dunia**.

Hivi Paulo alisema kwamba hakutaka kusema wajitenge kabisa na **wazini wa dunia hii, wala na wenyewe tamaa, wanyanganyi, au wenyewe kuabudu sanamu**. Wenyewe **tamaa** ndio wale wasiotenda kwa haki kwa maneno ya biashara na mali. Kwa mfano mtu anayehukumiwa kwa sababu hakulipa kodi alikuwa katika hatari ya kuondo-

shwa kanisani kwa sababu ya tamaa. **Wanyanganyi** ndio wale ambao wana-tumika na jeuri kwa kujipatia mali wakiogopesha watu na maumivu au mauti. **Waabudayi sanamu** ndio watu wanaoabudu kitu cho chote au mtu ye yote ila Mungu wa kweli, na wanao-tenda zambi zile mbaya za uasherati zilizo sehemu ya kuabudu sanamu.

5:11 Paulo alitaka sana kuonya Wa-kristo wasiwe na ushirika na mtu anayekiri kuwa **ndugu** katika Kristo, lakini anayetenda zambi hizi. Tunaweza kujumlisha maneno yake hivi:

Neno nililotaka kusema, na ni-nalosema tena sasa ni ya kwamba haifai ninyi kula pamoja na mtu anayekiri kuwa Mkristo, lakini aliye mzini, au mwenye tamaa, au mwabudayi sanamu, au mtukanayi, au mlevi, au mnyanganyi.

Inatupasa mara nyingi kukutana na wasioamini namna hii, na mara nyingine tunapata njia kuwatolea ushuhuda. Neno hili si hatari. Lakini ni hatari kwa mwamini kushiriki na wale wanaokiri kuwa Wakristo, lakini wanaoishi na kutembea katika zambi hizi. Haifai tu-fanye kamwe neno lo lote ambalo litawafikirisha kwamba tunakubali zambi zao.

Juu ya zambi Paulo alizotaja ndani ya shairi 10, Paulo aliongeza zambi namna mbili nyingine ndani ya shairi 11. **Mtukanaji** ni mtu anayesema kwa mtu mwingine na masemo ya nguvu na makali yasiyofaa. Lakini tunauliza kama mtu akikasirika sana mara moja na kusema maneno makali bila kufikiri vizuri, inapasa aondoshwe? Hatufikiri hivi, lakini mtu akifanya hivi tena na tena, ye ye ni mtukanaji na inapasa kumwondosha. Maneno haya yawe ma-onyo kwetu, tuangalie maneno sisi wenyewe tunayosema.

Mlevi ndiye mtu anayekunywa mvi-nyo au malofu kupita kipimo.

Maana ya masemo haya ya mtume

Paulo ni kwamba **haifai tule chakula pamoja na Mkristo anayefanya maneno haya?** Ndiyo, haya ndiyo ma-fundisho ya shairi hili! Haifai tule pamoja naye kwa Meza ya Bwana, wala wakati tunapokutana kula pamoja na rafiki wengine. Hata hivi inafaa kwa mke Mkristo kukaa kula pamoja na mume wake aliyeondoshwa kanisani. Lakini inapasa kuondosha kwa ushirika na urafiki wa waamini watu wale wanaokiri kuwa waamini, lakini wan-aotenda zambi namna hii. Kusudi la kuwaondosha ni kuwafahamisha ubaya mkubwa wa matendo yao, na warudi kutubu. Labda watu wengine wanasema kwamba Bwana alikula pamoja na wa-toza kodi na wenyе zambi, lakini watu hawa hawakusema walikuwa wafuata wake. Bwana hakuwatambua kama wanafunzi wake wakati alipokula pamoja nao. Mafundisho ya mashairi haya ndiyo ya kwamba haifai kwetu kushiriki na *Wakristo* wenyе maisha maovu.

5:12 Maulizo mawili ya Paulo ndani ya shairi 12 yanaonyesha kwamba si kazi ya Wakristo kuhukumu wasioamini. Bwana ye ye mwenyewe atahukumu waovu ambao wanatzunguka duniani kwa wakati wa kuja. Lakini ni kazi yetu kuhukumu wale walio **ndani ya kanisa**.

Basi, labda wengine wanasema kwa-mba Bwana alifundisha, “Musihukumu ili musihukumiwe wenyewe.” Tuneg-wajibu kwamba Bwana alisema juu ya makusudi ya roho hapa. Tunakatazwa kuhukumu makusudi ya watu kwa sababu hatuwezi kutambua makusudi yao. Lakini Neno la Mungu linaonyesha waziwazi kwamba inatupasa kuhukumu zambi yo yote inayojulikana ndani ya kanisa la Mungu, na kuchunga utakatifu wake, na vilevile kurudisha ndugu ali-yeanguka kwa ushirika na Bwana.

5:13 Paulo anaeleza kwamba **Mungu** atahukumu wale **walio inje**, maana yake wasioamini. Lakini sasa ilipasa Wako-rinto kuhukumu zambi, kama Mungu

alivyowaagiza, na kuondosha **mtu yule mbaya** katikati yao. Kwa kutii agizo hili la Bwana ilipasa habari hizi kutangazwa mbele ya watu wote wa kanisa kwamba ndugu huyu si ndani ya kanisa hili tena. Lazima tangazo hili lifanywe na huzuni na unyenyekevu, na sharti waamini wa kanisa wadumu katika maombi kwa yule aliyeondoka katikati yao, aweze kuruudi karibu na Mungu tena.

C. Mashitaki ya waamini mbele ya waamuzi (6:1-11)

Mashairi 1-11 ya kwanza ya sura 6 ni juu ya mashitaki katikati ya waamini. Paulo alisikia habari kwamba wengine wa Wakristo walikuwa wakishitaki waamini wenzao – mbele ya waamuzi wa dunia hii. Hivi alitoa mafundisho haya ya faida, si kwa kanisa la Korinto tu, lakini kwa makanisa yote hata sasa. Ona ya kwamba alisema tena na tena, “Hamujui” (mash. 2, 3, 9, 15, 16, 19).

6:1 Shairi hili linaonyesha kwamba Paulo alishitushwa kabisa kusikia kwamba wengine katikati yao walifikiri kuhitaki ndugu wenzao **mbele ya wasio haki**, maana yake mbele ya waamuzi wasioamini. Kwa mafikiri yake haikufaa kwa watu waliokwisha kujua haki ya kweli kufika mbele ya watu wasio wenye haki. Waza kwanza juu ya Wakristo kutafuta kuhukumiwa kwa haki ya kweli na watu wale wasiokuwa wenye haki wao wenyeewe!

6:2 Na maneno mengine yasiyofaa hata kidogo ni kwa watu wale **watakao-hukumu dunia** siku nyingine kushindwa kupatana na kutengeneza maneno na magomvi madogo katikati yao wenyeewe. Maandiko Matakatifu yanafundisha ya kwamba waamini watatawala pamoja na Kristo juu ya dunia wakati atakaporudi na uwezo na utukufu, na ya kwamba waamini watahukumu maneno mengine. Kama Wakristo **watahukumu dunia**, bila shaka ingewapasa kupatana ndani ya

maneno madogo ambayo yanaanza magomvi katikati yao sasa!

6:3 Paulo alikumbusha Wakorinto ya kwamba **watahukumu malaika**. Ni neno la kushangaza namna Paulo alivyo-taja habari hizi kubwa hapa. Bila maneno makubwa ya kushangaza watu, alisema tu neno hili kubwa sana ya kwamba siku nyingine Wakristo **watahukumu malaika**. Tunasoma kwa Yuda sh. 6 na 2 Pet. 2:4,9 kwamba malaika watahukumiwa. Tunajua vilevile kwamba Kristo atakuwa Mwamuzi mwenye (Yn. 5:22). Kwa sababu tunafungwa pamoja naye inaweza kusema kwamba tutahukumu malaika siku nyingine. Basi kama tukiweza kuhukumu malaika, ingetupasa kuweza kuhukumu maneno madogo yanayotokea kila siku kwa **maisha yetu ya sasa**.

6:4 **Basi ikiwapasa ninyi kuhukumu maneno ya maisha ya sasa, mutachagua watu wenyewe heshima ndogo zaidi na kanisa kuhukumu?** Waamuzi wasioamini hawapewi heshima ndani ya kanisa letu. Ndiyo, tunawaheshimu kwa kazi wanayofanya duniani. Lakini hawana mamlaka kwa maneno ya kanisa. Hivi Paulo anauliza Wakorinto:

Wakati kuna maneno katikati yenu yanayohitaji kuhukumiwa na mtu mwininge, munachagua mtu asiye mtu wa kanisa na anayekosa ufa-hamu wa maneno ya roho?

6:5 Paulo anauliza neno hili kuamsha **haya** ndani ya roho zao. Inawezekana kwa kanisa hili waliojivuna juu ya hekima yao na uwingu wa zawadi zao za roho **kukosa hata mtu mmoja mwenye hekima** atakayeweza kumaliza magomvi haya **katikati ya ndugu zake**?

6:6 Ni kama mtu wa namna hii haku-patikana, kwa sababu **ndugu** Mkristo alikuwa akishitaki **ndugu** yake Mkristo mbele ya waamuzi wasioamini wa dunia. Ilikuwa haya kabisa!

6:7 Maneno haya “**Basi kuna kosa katikati yenu**” yanaonyesha kwamba

walikuwa wameanguka kabisa ndani ya neno hili. Haikuwa vizuri kwao kushitakiana. Halafu labda mmoja wa Wakristo alisema na Paulo: "Paulo, hufahamu neno hili vizuri. Ndugu huyu alinidanganya ndani ya biashara." Ona jibu la Paulo: "**Kwa sababu gani hamuvumilii ubaya? Kwa sababu gani hamutaki kunyanganywa mali?**" Ingalipasa Wakristo kuwaza hivi. Kutendewa mabaya ni vizuri kupita kutenda mabaya.

6:8 Lakini Wakorinto hawakufikiri hivi. Kwa pahali pa kukubali kutendewa mabaya na kudanganya, walitendea wengine **mabaya**, hata ndugu zao Wakristo.

6:9 Walikuwa wamesahau kwamba watu wanaoishi **maisha ya uzalimu hawatariti ufalme wa Mungu?** Kama ni hivi, atawakumbusha wenyewe zambi kwamba hawatakuwa ndani ya **ufalme** wa Mungu. Hakutaka kusema kwamba Wakristo wanaweza kutenda zambi hizi na kupotea, lakini ya kwamba watu wanaokaa kutenda zambi namna hii si Wakristo.⁵

Wazini ni namna nyingine na **washerati**. Hapa uasherati unatendwa na mtu asiyeolewa, na uzini na mtu aliyeolewa. Waabudaji sanamu wanatajwa tena. Walitajwa mara mbili mbele ndani ya sura 5. **Wakike** wanaacha miili yao kutumiwa kwa zambi, na **wafiraji** wanatendea wengine zambi ya mwili.

6:10 Tunaona tena **wizi**, na **wenye tamaa**, na **walevi**, na **watukanaji**, na **wanyanganyi**. **Wizi** ndio watu wanaokamata vitu visivyo vyao. Ona ya kwamba **tamaa** inatajwa kila mara pamoja na zambi mbaya zaidi. Hata kama si zambi kubwa kwa macho ya watu, Mungu anaihukumu na ukali. **Mwenye tamaa** anasukumwa na hamu kubwa kwa vitu fulani, hata anajaribu mara nyingine kujipatia vitu hivi kwa njia isiyo haki. **Walevi** ndio wenye kuniywa malofu kupita kipimo. **Watu-**

kanaji wanasema maneno mabaya na kushutumu watu wengine. **Wanya-nganyi** wanajipatia faida kubwa kwa njia ya kuibia wamasikini vitu ambavyo wanahitaji.

6:11 Paulo hakutaja zambi hizi zote kwa sababu alifikiri Wakristo wa Korinto walizitenda, lakini aliwaonya ya kwamba walizitenda mbele wakati wasipookolewa bado. "**Wengine kwenu mulikuwa hivi; lakini mulioshwa, lakini multakaswa, lakini mulihesabiwa kuwa na haki.**" Walikuwa **wameoshwa** toka zambi zao kwa njia ya damu ya damani ya Kristo, na Neno la Mungu lilikaa kuwasafisha wasichafuwe. **Walitakaswa** kwa njia ya Roho Mtakatifu na kuwekwa mbali kwa Mungu toka dunia. **Walihesabiwa kuwa na haki katika jina la Bwana Yesu Kristo, na katika Roho ya Mungu.** Walikuwa wamehesabiwa haki mbele ya Mungu kwa sababu ya kazi ya Bwana Yesu msalabani kwa ajili yao.

D. Ukosefu wa usafi wa mwenendo wa waamini (6:12-20)

6:12 Ndani ya mashairi ya mwisho ya sura hii mtume anatoa mafundisho kutusaidia kufahamu maneno gani ni mazuri na yale yaliyo mabaya. Neno la kwanza ndilo ya kwamba neno fulani linaweza kukubaliwa, lakini hata hivi si neno la kusaidia. Wakati Paulo aliposema, "**Vitu vyote ni halali kwangu**," hakufikiri juu ya vitu vyote pia. Alifikiri tu juu ya maneno yasiyo zambi. Kwa mfano, isingalikuwa halali kwaye kufanya moja ya zambi alizotaja mbele. Anasema tu juu ya maneno yasiyokuwa zambi. Kwa mfano, Wakristo wa wakati ule walifazaika sana juu ya kula nyama ya nguruwe. Kwa mawazo ya Mungu neno hili lilikuwa halali. Paulo alikuwa akisema tu kwamba, hata kama neno fulani ni halali, labda halina faida. Kuna maneno fulani yanayokubaliwa kwa

mimi kufanya, lakini labda mtu mwininge akiniona nikiyafanya, yatakuwa vikwazo kwake. Hivi si vizuri kwa mimi kufanya maneno haya.

Neno la pili ni hili: Inawezekana kwa neno fulani kuwa **halali**, lakini kuna hatari kwamba litageuka desturi kwetu. Paulo aliandika kwamba "**sitatiwa chini ya uwezo wa kitu cho chote.**" Kwa wakati wa sasa vitu namna hii ni malofu, tumbako, na dawa mbaya. Vitu hivi na vingine vingi vinaingiza watu katika utumwa, na haifai Mkristo kukubali kufungwa navyo.

6:13 Neno la tatu ndilo hili: vitu vingine ni halali kwa mwamini, lakini faida yao ni kwa muda mdogo tu. Paulo alisema: "**Vyakula ni kwa tumbo, na tumbo ni kwa vyakula: lakini Mungu ataharibu vyote viwili, tumbo na vyakula.**" Ni kusema kwamba **tumbo** la mtu limeumbwa kuweza kupokea **vyakula** na kutumika navyo kusaidia mahitaji ya mwili. Na vilevile Mungu aliumba **vyakula** vizuri sana kwa **tumbo** la mtu. Hata hivi haifai tuishi kwa kula vyakula tu, kwani faida ya vyakula hivi ni kwa muda mdogo tu. Usiweke roho kupita kipimo juu ya kutimiza hamu kwa vyakula vitamu.

Ndiyo, Mungu alitayarisha mwili wa ajabu kabisa kupokea vyakula na kuitumia kupatisha mwili nguvu, lakini kuna neno moja tunalojua hakika: **mwili si kwa uzini, lakini ni kwa Bwana, na Bwana ni kwa mwili.** Halikuwa kusudi kamwe la Mungu kwa mwili kutumiwa kwa zambi na uzini. Shauri lake lili-kuwa kwa mwili huu kutumiwa kwa utukufu wa Bwana na utumishi wake.

Haifai tukose kuona neno lingine kutsuhangaza kabisa ndani ya shairi hili: **Mwili ni kwa Bwana**, lakini neno la kutsuhangaza hata kupita ndilo hili: **Bwana ni kwa mwili.** Ni kusema kwamba Mungu anafikiri miili yetu, hali yao, na kazi yao. Mungu anataka tu-

mtolee miili yetu kama zabihu iliyo hai, takatifu, na ya kupendeza (Rom. 12:1).

6:14 Kuna elezo lingine hapa juu ya Bwana akiwa kwa mwili. **Mungu alifufua Bwana Yesu** toka wafu, na **atatufufua sisi toka wafu vilevile kwa uwezo wake.** Haachi kuweka roho juu ya miili yetu saa ya kufa. **Atafufua** mwili wa kila mwamini kuufanyiza sawasawa na mwili wa utukufu wa Bwana Yesu. Hatutakuwa roho tu bila miili kwa milele. Roho na nafsi yetu zitakutanishwa tena pamoja na mwili wetu uliotukuzwa, na kufurahi katika utukufu wa mbingu kwa milele.

6:15 Paulo alikaa kusema kwamba sharti tuchunge miili na maisha yetu safi. Anatukumbusha kwamba **miili yetu ni viungo vya Kristo.** Kila mwamini ni kiungo cha mwili wa Kristo. Basi, inge-kuwa vizuri **kutwaa viungo vya Kristo na kuvifanya viungo vya kahaba?** Paulo alijibu ulizo hili na nguvu, **Hapania, hata kidogo!**

6:16 Kwa njia ya kusalana, miili mwili inageuka **mmoja.** Ilikuwa hivi kwa wakati wa kuumbwa kwa dunia: Kwa **sababu anasema: "Wale wawili watakuwa mwili mmoja"** (Mwa. 2:24). Hivi mwamini **akiungwa na kahaba**, ni sawasawa na kufanyiza kiungo cha Kristo kiungo cha kahaba. Wale wawili wangaligeuka **mwili mmoja.**

6:17 Kama kwa njia ya miili miwili wakilalana, na kuungana kuwa mmoja, vivyo hivyo wakati mtu anapoamini Bwana Yesu Kristo na **kuungwa** naye, mwamini huyu na Kristo wanaungwa pamoja kabisa, na kuwa **roho moja.** Hakuna umoja wa karibu **kupita** ule. Paulo anasema kwamba haifai wale **wanaofungwa** hivi **kwa Bwana** kukubali umoja wo wote mwininge ambao unaoweza kushindana na ndoa hii takatifu ya roho.

6:18 Hivi mtume anaonya Wakorinto **kukimbia uzini.** Haifai wawaze wala kusemezana juu yake. Anawaagiza **ku-**

ukimbia! Kuna mfano mzuri ndani ya Biblia wakati Yosefu alipojaribiwa ku-zini na mke wa Potifari (Mwa. 39).

Halafu Paulo aliongeza kwamba: **“Kila zambi mtu anayofanya ni inje ya mwili; lakini yeye anayefanya uzini anafanya zambi juu ya mwili wake mwenyewe.”** Zaidi ya zambi zetu hazi-mizi **miili** yetu, lakini **uzini** ni namna nyingine, na unagusa mwili; mtu anazaa matunda ya zambi hii ndani ya mwili wake mwenyewe. Kuna zambi nyingine kama ulafi na ulevi zinazoumiza mwili vilevile, lakini si kwa kipimo cha uharibifu unaotendwa mwilini mwa mtu anayetenda uzini inje ya ndoa.

6:19 Paulo alikumbusha Wakorinto kwamba walikuwa na mwito mtakatifu. Aliwauliza kama walikuwa wamesahau kwamba miili yao ni **hekalu la Roho Mtakatifu?** Ni kweli kubwa ya kwa-mba Roho Mtakatifu wa Mungu anakaa ndani ya kila mwamini. Namna gani tutafikiri kutumika na mwili huu una-okaliwa na Roho *Mtakatifu* kwa kazi *ovu* kabisa? Na zaidi ya ile sharti tukumbuke kwamba **sisi si mali yetu wenyewe.** Hatuna ruhusa kutumika na miili yetu kufanya neno lo lote tun-alotaka. Miili hii si mali yetu; lakini ni mali ya Bwana.

6:20 Tuko mali ya Bwana kwa njia mbili: alituumba, na alitukomboa. Shairi hili linasema zaidi juu ya ukombozi. Tuko mali yake tangu siku alipotukufia kwa Kalvari. **Tulinunuliwa kwa bei.** Kwa msalaba, tunaona ukubwa wa bei ile. Bwana Yesu alifikiri sisi ni damani sana hata alikuwa tayari kulipa bei kubwa ya damu yake ya damani. Kweli Yesu alitupenda na mapendo makubwa sana hata alibeba azabu ya zambi zetu katika mwili wake msalabani!

Ikiwa hivi, siwezi kufikiri tena juu ya mwili wangu kama mali yangu mwenyewe. Kama nikutumika nao na-mna ninavyotaka, mimi ni mwizi,

kwani ninakamata kitu kisicho mali yangu. Sharti nitumike na **mwili** wangu **kutukuza Mungu**, kwani ni mali yake.

Na vilevile inatupasa kutukuza Mungu **ndani ya roho zetu**, kwani mwili na roho ya mtu ni **ya Mungu**.

3. MAJIBU YA MTUME KWA MAULIZO YA KANISA (Sura 7–14)

A. Juu ya ndoa na kutokuo (Sura 7)

7:1 Kufika hapa Paulo aliandika juu ya maneno mbalimbali yasiyokuwa taratibu ndani ya kanisa kwa Korinto. Sasa alianza kujibu maulizo ya waamini. La kwanza linakuwa juu ya ndoa na kukaa bila kuoa. Alianza na kusema kwamba kwa kawaida **ni vema kwa mwana-mume asiguse mwanamke. Maana ya “kugusa” mwanamke** ni kulala naye. Mtume hakutaka watu kufikiri kwamba kukaa bila kuoa ni alama ya maisha matakatifupita, lakini ya kuwa ni vizuri kupita kwa mtu ambaye anataka kujitao kwa kazi ya Bwana bila mazuizo. Mawazo haya yataelezwa nyuma.

7:2 Lakini Paulo alifahamu kwamba mtu asiyeoa atajaribiwa sana kuzini. Hivi anaongeza juu ya maneno aliyosema mbele, **“Kwa sababu ya uzini, kila mwana-mume awe na mke wake mwenyewe, na kila mwana-mke awe na mume wake.”** Maana ya kwa kila mwana-mume kuwa na mke wake mwenyewe ni awe na mke mmoja tu, ndio utaratibu amba Mungu alisimamisha kwa mwanzo, ndio kwa mwana-mume kuwa na mke mmoja tu.

7:3 Katika ndoa inapasa kila mmoja **kumpa** mwenzake haki yake. Hivi tukisoma **“Mume ampe mke wake haki yake,”** ni kusema atimize kwake maneno ambayo mume anapaswa kutendea mke wake. Inapasa mke wake kutenda **vivyo hivyo** kwa mume wake.

7:4 Ndani ya ndoa mume na mke sharti wafahamu kwamba wanatumainia, ndilo neno la lazima.

7:5 Christenson aliandika:

Kusema wazi, mmoja wao akitaka kulala na mwenzake, mwenzake anyenyekkee kutaka kwake. Mume na mke wakinyenyekeana hivi, wataona kwamba kulalana hivi ni sehemu tamu ya ndoa.⁶

Labda wakati wengine wa Wakorinto walipookolewa, walianza kufikiri ya kwamba kulala katika ndoa hakupatani na utakatifu wa maisha ya Wakristo. Paulo alwaondolea mawazo ya namna hii. Alifundisha waziwazi ya kwamba haifai kwa mume na mke **kunyimana** kwa maneno ya miili yao bila **kupatana** kufanya hivi, labda ili waweke saa kwa **kufunga na kuomba**. Sharti nyuma ya muda fulani **wakuje pamoja tena**, ili Shetani asipate njia kuwajaribu kwa sababu ya **kupunguka kiasi**.

7:6 Watu wamebishana sana juu ya shairi hili. Paulo alisema: “**Lakini ninasema maneno haya kwa ruhusa, si kwa agizo.**” Watu wengine wamefikiri maana ya masemo haya ni ya kwamba hayakuongozwa na Mungu. Mafikiri yao si sawa kwa sababu ndani ya 1 Wakorinto 14:37 Paulo alisema waziwazi kwamba maneno alioandikia Wakorinto yalikuwa maagizo ya Bwana. Tunafikiri neno Paulo alilotaka wafahamu ni kwamba mara nyingine ni taratibu kwa mume na mke kutokulalana, kwa ruhusa, **si kwa sababu ni agizo**. Si lazima kwa mume na mke kutokulalana ili waweze kujitoa kwa maombi na roho moja. Watu wengine wanafikiri shairi 6 ni juu ya ndoa, na ya kwamba ni ruhusa kwa Wakristo kuoa, lakini hawaagizwi kufanya hivi.

7:7 Halafu Paulo alianza kutoa mafundisho kwa wale wasiooa. Tunaona mara moja kwamba alifikiri ilikuwa vizuri kukaa bila kuoa, lakini alifahamu vilevile ya kwamba neno hili linawe-

zekana tu kwa uwezo wa Mungu. Wakati aliposema: “**Ninapenda watu wote wawe kama mimi mwenyewe,**” maana yake ilikuwa “**bila kuoa.**” Watu wengine wanafikiri labda Paulo hakuo kamwe au labda mke wake alikufa. Aliendelea kusema: “**Lakini kila mtu ana zawadi yake mwenyewe kutoka kwa Mungu, huyu hivi, na yule hivi.**” Maana yake ni ya kwamba Mungu anawezesha watu wengine kukaa bila kuoa, na anaongoza watu wengine kuoa. Anaongoza kila mtu kwa njia mbalimbali. Hakuna sheria juu ya neno hili kwa watu wote.

7:8 Hivi alisema vizuri **wale wasiooa bado, na wajane wabaki kama yeze.**

7:9 Lakini kama hawawezi **kujizuiza** wenyewe bila kuoa, basi wana ruhusa **kuoa, kwani ni afazali kuoa kuliko kuwaka na tamaa.** Kuwaka na tamaa ni majaribu makubwa kufanya zambi.

7:10 Shairi hili na shairi 11 ni kwa Wakristo waliokuwa **wamefunga ndoa. Nao waliokwisha kuoana, ninawa-agiza, wala si mimi, lakini Bwana** ni kusema Paulo alikuwa akifundisha tena maneno **Bwana** Yesu *aliyokwisha kufundisha mbele wakati alipokuwa duni-ani*. Kristo alikuwa amefundisha waziwazi juu ya maneno haya. Kwa mfano alikataza watu kuachana ila kama mmoja wao alizini (Mt. 5:32; 19:9). Paulo alisema tu **mke asiachane na mume wake.**

7:11 Hata hivi alifahamu kwamba mara nyingine ni lazima kwa mke kuongdokea mume wake. Akifanya hivi, **abaki pasipo mume, au apatane na mume wake tena.** Hata mume na mke wakiachana, neno hili halivunjifungo cha ndoa. Linaleta njia kwa Bwana kuponyesha maumivu yaliyotenga mume na mke, na kuwapatanisha tena, na kuwarudisha kwa upatano mzuri na yeze mwenyewe. **Mume anakatazwa kuacha mke wake** kwa sababu yo yote.

7:12 Mashairi 12-14 ni juu ya ndoa

kama mmoja tu ni mwamini. Paulo anaanza mafundisho haya na: “**Lakini kwa watu wengine ninawaambia, wala si Bwana.**” Alisema tena ya kwamba hakusema mafikiri yake mwenyewe, lakini mawazo ya Bwana. Alieleza tu ya kwamba maneno ali-yokuwa karibu kusema **hayaku-fundishwa** na **Bwana** Yesu mbele wakati alipokuwa hapa duniani. Hakuna mafundisho ndani ya vitabu vya Habari Njema yanayofanana na maneno haya. Bwana Yesu hakufundisha juu ya ndoa namna hii wakati mmoja wa wenye kuoana alipokuwa msiyeamini. Lakini sasa Kristo alikuwa amefundisha mtume wake juu ya maneno haya, hivi maneno Paulo aliyo sema hapa yanaongo-zwa na Mungu.

Lakini kwa watu wengine, ndio wale wasioamini. Mashairi haya *hayaruhusu* Mkristo kuoa msiyeamini. Tunafikiri mmoja wao aliokolewa nyuma ya ndoa yao.

“**Kama ndugu mmoja ana mke asiyeamini, naye anakubali kukaa pamoja naye, asimwache yeye.**” Kufahamu shairi hili vizuri tukumbuke agizo la Mungu kwa watu wake katika Agano la Kale. Wakati Wayuda walipoaa wake wapagano na kuzaa watoto nao, walilagizwa kuondosha wanawake hawa pamoja na watoto wao. Ona Ezra 10:2, 3 na Nehemia 13:23-25.

Halafu waamini katika Korinto waliliza kama mke aliyeamini Bwana nyuma ya kuolewa alipaswa kufanya nini juu ya mume na watoto wake, au kama ilipasa mume aliye kuwa na mke msiyeamini afanye nini juu ya neno hili. Amwondoshe? Hapana. Agizo hili la Agano la Kale si tena kwa watu wa Mungu kwa wakati huu wa neema. Mkristo akiwa na mke msiyeamini, na mke huyu **akikubali kuishi pamoja naye**, haifai mume kumwacha. Lakini neno hili halimpi mwamini ruhusa kuoa msiyeamini, lakini mume akiokolewa

nyuma ya kuoa mke msiyeamini, haifai amwache.

7:13 Vivyo hivyo, **mwanamke aki-wa na mume** asiyeamini **anayekubali kukaa pamoja naye**, anapaswa kukaa pamoja na mume wake. Labda kwa njia ya ushuhuda wake na upole wake ataweza kumleta karibu na Bwana.

7:14 Kuwa na mwamini nyumbani kunatakasa nyumba. Kama tulivyoona mbele, maana ya *kutakasa* ni kuweka mbali. Maana yake hapa haiko ya kwamba mume msiyeamini anaokolewa kwa njia ya mke wake, au ya kwamba anafanyizwa takatifu. Ame-wekwa kwa pahali pa baraka kwa sababu ana mke Mkristo ambaye anamwombea. Maisha na ushuhuda wake kwa Mungu ni baraka ndani ya nyumba yao. Ni vivyo hivyo kama **mume** ni mwamini na **mke** wake **ni msiyeamini**. Halafu **mke msiyeamini anatakaswa**.

Halafu mtume anaongeza: “**kama sivyo, kama watoto wenu wangkuwa si safi; lakini sasa ni watakatifu.**” Tumesema mbele kwamba katika Agano la Kale ilipasa kuondosha watoto pamoja na mke mpagano. Sasa Paulo alionyesha kwamba kwa wakati wa muda wa neema, watoto wenye mzazi mmoja aliye mwamini na wa pili asiyemwamini, ni **watakatifu**. Maana yake haiko ya kwamba watoto hawa wanatakswa wao wenyewe, au kwamba wana maisha safi. Ni kusema wamekuwa kwa pahali pa mapendeleo. Mmoja wa wazazi wao anapenda Bwana na anawapasha Habari Njema. Wanakaa katika nyumba pahali hata mzazi mmoja anapokaliwa na Roho Mtakatifu. Kwa njia hii, wanatakswa. Shairi hili linatufahamisha vilevile ya kwamba si zambi kuzaa watoto wakati mzazi mmoja ni mwamini na mwingine hajaamini bado. Mungu anakubali ndoa yenye, na watoto si wa haramu.

7:15 Lakini Mkristo afanye nini

kama mtu wa pili wa ndoa asipokuwa mwamini na anataka kuondoka? Inapasa kumruhusu **kuondoka**. Ni nguvu kueleza maana ya maneno haya, “**ndugu mume au ndugu mke si mfungwa katika maneno kama haya.**” Watu wengine wanafikiri kama msiyeamini akiacha mwamini, na inaonekana wazi kwamba hatarudi tena, halafu mwamini ana ruhusa kutenga ndoa. Wale wanaofikiri hivi wanafundisha kwamba sh. 15 ni maneno yanayoingizwa katikati (entre parenthèses); na sh. 16 linafungana na sh. 14 hivi:

1. Shairi 14 linafundisha kwamba ni vizuri zaidi kwa mwamini kukaa pamoja na msiyeamini kwa sababu ya maongozi yake ya kikristo nyumbani.
2. Shairi 16 linatufikirisha ya kwamba labda kwa njia ya kubaki pamoja na msiyeamini, mwamini atawea ku-mwongoza kuamini Kristo.
3. Shairi 15 ni maneno yanayoingizwa katikati, yakiruhusu mwamini kutenga ndoa (na labda kuoa tena), kama ameachwa na msiyeamini.

Tumaini kwamba msiyeamini atakolewa ni kubwa kupita kama akikaa pamoja na Mkristo nyumbani.

Lakini waamini wengine wanasema na nguvu ya kwamba shairi 15 ni juu ya kuachana tu, si juu ya kutangua ndoa. Wanafikiri maana yake ni kama msiyeamini akitaka kuondoka, ana ruhusa kuondoka na salama. Si lazima kwa mke kukaa kujaribu kuchunga ndoa bila kutengana. **Mungu ametuita katika salama**, na si sharti kuomba wamuzi kusaidia kuzuiza msiyeamini asiondoke.

Elezo gani ni maana ya haki? Hatuwezi kujua kabisa. Ni kama ndani ya Matayo 19:9 Bwana alifundisha kwamba kuna ruhusa kwa kutenga ndoa kama mmoja wao amekwisha kutenda uasherati. Tunaamini kama neno hili linatokea, mtu asiyezini anaweza kuoa

tena. 1 Wakorinto 7:15 halifundishi wazi kama kutenga ndoa, na kuoa tena kuanakubaliwa wakati msiyeamini alipokwisha kuacha mwenzi wake Mkristo. Lakini ni kama karibu kila mara mtu anapofanya hivi, anafungana na mtu mwagine nyuma kidogo, na ndoa ya kwanza inatengwa. J. M. Davies aliandika:

Msiyeamini anayeondoka ataolewa na mtu mwagine nyuma kidogo, na tendo hili litavunja ndoa ya mbele. Kuamuru wale walioachwa kukaa bila kuoa tena ni kuwabebesha mzigo ambao utashinda zaidi yao kubeba.⁷

7:16 Ona tena maneno yaliyoandi-kwa mbele juu ya shairi hili.

Mtu anayeamini kwamba shairi 15 linakataza kwa ndoa kutengwa, anasi-mamisha mawazo yake juu ya shairi 16. Anasema vizuri mtu mwenyewe akubali kuachana, lakini haifai atengete ndoa yake na msiyeamini kwa sababu kufanya hivi kungalizuza njia kwa ndoa hii kuteengenezwa tena, na labda hata wokovu wa yule msiyeamini. Lakini kama mtu akiamini kwamba kutangua ndoa kuanakubaliwa wakati mwamini anapokwisha kuachwa, shairi 16 linafungana na shairi 14, na shairi 15 ni maneno yanayoingizwa katikati.

7:17 Mara nyininge waamini wa sasa wanafikiri lazima wajitenge kabisa na maneno yote ya maisha yao ya mbele, hata maneno kama ndoa yasiyo zambi, si neno kama ikiwapasa kupiga vita kufanya hivi. Lakini Wakristo hawapigi vita kutimiza makusudi yao. Wanageuze maneno kwa njia ya salama kupendeza Mungu. Ndani ya mashairi 17-24 mtume alionyesha ya kwamba si lazima kwa mwamini kushindana kugeuza namna alivyokaa mbele ya kuokolewa. Bila shaka alifikiri zaidi juu ya maneno ya ndoa, lakini ni kweli kwa maneno mengine vilevile, kama kabilia na jamaa.

Inapasa kila mwamini kuishi katika

mwito wa Mungu kwa yeye. Kama ndoa ni mwito wa Mungu kwa yeye, inampasa kuishi katika mwito huu na woga wa Bwana. Kama Mungu alimpa neema kuishi bila kuo, halafu inampasa kukaa katika mwito huu. Kama saa mtu alipookolewa alikuwa na mke asiyeamini, hahitaji kutangua ndoa hii, lakini kukaa kujaribu kumwongoza kupata wokovu. Paulo hakusema maneno haya kwa Wakorinto peke yao; aliyafundisha **katika makanisa yote.**

Vine alandidka:

Wakati Paulo aliposema, “na hivi ni navyoagiza katika makanisa yote,” hakutoa maagizo toka nyumba kubwa ya dini, lakini alijulisha kanisa kwa Korinto tu kwamba haya yaliyuwa mafundisho yake ndani ya kila kanisa.⁸

7:18 Ndani ya mashairi 18 na 19 Paulo alandidka juu ya maneno ya kabila. Kama mtu alikuwa Myuda saa alipookolewa, na alikuwa na alama ya tohara mwilimi mwake, haifai achukizwe na neno hili na kujaribu na nguvu kuongosha alama hii ya maisha yake ya mbele. Vivyo hivyo, kama mtu alikuwa mpagano wakati wa wokovu wake, hahitaji kujaribu kuficha alama za maisha yake ya kishenzi ya mbele, na kupokea alama za Myuda.

Elezo lingine la maana ya shairi hili ni kama Myuda akiokolewa, haifai aogope kuishi pamoja na mke wake Myuda, na Mtaifa akipokea Mwokozi, asijaribu kuficha kwamba alikuwa Mtaifa mbele. Mambo haya ya inje si kitu.

7:19 Kwa Wakristo, **kutahiriwa si kitu, na kutokutahiriwa si kitu.** Neno kubwa ndilo **kuangalia amri za Mungu.** Mungu anaweka roho juu ya hali ya ndani, rohoni, si juu ya maneno yanayoonekana inje.

7:20 Inapasa **kila mtu kukaa** pamoja na Mungu **katika hali ile alipokuwa wakati alipoitwa.** Lakini kama mtu alikuwa akifanya kazi mbaya ya zambi

saa alipoamini Mwokozi, itampsasa kuacha kazi ile. Neno hili linahaki-kishwa ndani ya mashairi yanayofuata juu ya utumwa.

7:21 Inapasa **mtumwa** kufanya nini wakati anapookolewa? Inampasa kuasi bwana wake na kutaka kwa nguvu amfungue toka utumwa wake? Inapasa Wakristo wajaribu na nguvu kusimamia yaliyo “haki” yao? Ona jibu la Paulo: **“Ulikuwa mtumwa wakati ulipoitwa? Usione kama ni vibaya.”** Maana yake unaweza kufurahishwa na baraka kubwa zaidi za ukristo hata kama wewe ni mtumwa.

Lakini kama ukiweza kuwa huru, afazali uutumie. Kuna njia mbili kueleza maneno haya. Watu wengine wanafikiri maana ya masemo ya Paulo ni, “Kama kuna njia kwa wewe kupata uhuru, ujipatie uhuru.” Wengine wanafikiri mtume anasema ya kwamba hata kama ikiwezekana kwa mtumwa kupata uhuru, si lazima kwa Mkristo kufanya hivi. Anaweza kutumika katika utumwa wake kama ushuhuda kwa Bwana Yesu. Zaidi ya watu wanafikiri elezo la kwanza ni zuri kupita (na tunazani ni elezo la haki), lakini tukumbuke vilevile ya kwamba elezo la pili linapatana kupita na mfano ambao Bwana Yesu mwenye alituachia.

7:22 Yeye aliyeitwa katika Bwana, akiwa mtumwa, ni huru ya Bwana. Maana ya maneno haya si mtu aliyezaliwa huru, lakini mtumwa aliywewekwa huru. Ni kusema kama mtu alikuwa mtumwa wakati alipookolewa, haifai asumbuke juu ya neno hili, kwa sababu **yeye ni huru ya Bwana.** Amefunguliwa toka zambi naye si mtumwa wa Shetani. Lakini mtu aliye huru saa alipookolewa, afahamu ya kwamba kuanza sasa yeye ni **mtumwa**, mwili wake mzima, wa Mwokozi.

7:23 Kila Mkristo amenunuliwa kwa bei. Sasa yeye ni mali ya Yule ambaye alimnunua, ndiye Bwana Yesu.

Inatupasa kuishi kama watumwa wa Kristo; haifai kwetu **kugeuka watumwa wa watu**.

7:24 Hata mtu ni katika hali gani saa ya wokovu wake, akae katika hali hii **pamoja na Mungu**. Maneno haya matatu *pamoja na Mungu* ndiyo maneno makubwa. Mtu akiwa **pamoja na Mungu**, hata utumwa wake unawenza kugeuka uhuru wa kweli.

7:25 Ndani ya mashairi 25-38 mtume anaandika kwa wanaume na wanawake wasioolewa, na wanaoweza kuitwa wote **mabikira**. Hili ni shairi lingine linalotumiwa na watu wengine kufundisha kwamba labda maneno ya sura hii hayakuandikwa kwa maongozi ya Mungu. Wengine wanasema ya kwamba Paulo aliandika hivi kwa sababu hakuo ye ye mwenyewe! Mawazo haya ndiyo kupiga vita na maongozi ya Maandiko Matakatifu. Wakati Paulo anaposema **hana amri ya Bwana kwa maneno ya mabikira**, maana yake ni ya kwamba Bwana hakuacha mafundisho juu ya neno hili wakati alipokuwa duniani. Hivi Paulo alitoa **shauri lake mwenyewe, kama ye ye aliyepata rehema ya Bwana kuwa mwaminifu**, na shauri hili liliongozwa na Mungu.

7:26 Ni vizuri kukaa bila kuoa **kwa sababu ya matata ya sasa**. Hatujui kama **matata ya sasa** ilikuwa matukio gani kwa wakati ule. Matata yanaendelea duniani hata sasa, kufika wakati wa kuja kwa Bwana.

7:27 Paulo alisema kwa wale walikuwa wameeo ya kwamba **haifai watafute** kufunguliwa toka ndoa. Lakini kama mtu **amefunguliwa na mke, asitafute mke**. Maneno haya **umefunguliwa na mke** hayasemi juu ya kufiwa mke, au kutengwa kwa ndoa tu. Maana yao ni kuwa huru toka kifungo cha ndoa, labda hata watu wasiooa kamwe.

7:28 Paulo hakusema neno linaloweza kutufikirisha ya kwamba ni zambi kuoa. Alikuwa Mungu aliyesimamisha

utaratibu wa ndoa shambani mwa Edeni mbele ya kuingia kwa zambi duniani. Alikuwa Mungu mwenyewe aliyesema: “Si vema mtu awe peke yake” (Mwa. 2:18). “Ndoa iheshimiwe na watu wote, na kitanda kisiwe na uchafu” (Ebr. 13:4). Paulo alisema pahali pengine juu ya watu wanaokataza ndoa kama alama ya ukafiri wa kuja (1 Tim. 4:1-3).

Hapa alisema, “**Lakini kama ukioa, huna zambi; na kama bikira akio-lewa, hana zambi**.” Haifai waamini wa sasa kufikiri kamwe ya kwamba ni vibaya kuoa. Lakini alisema vilevile ya kwamba wanawake wanaolewa watakuwa na **mateso katika mwili**. Labda alifikiri maumivu wakati wa kuzaa watto, na maneno mengine. Wakati Paulo aliposema, “**Lakini ninataka kuwazui-za**,” labda alifikiri (1) maumivu ya mwili kwa njia ya ndoa, na zaidi masumbuko ya jamaa, au (2) **Ninataka kuzuiza** msomaji kutaja masumbuko haya yote moja moja.

7:29 Paulo alisema na nguvu ya kwamba **inabaki wakati kidogo**. Hata kama maneno haya ni halali, inatupasa kuweka roho zaidi juu ya kutumikia Bwana. Kuja kwa Kristo ni karibu, na hata kama inafaa waume na wake kutimiza mahitaji ya ndoa yao na uaminifu, sharti wampe Kristo pahali pa kwanza ndani ya maisha yao.

Ironside alisema:

Inapasa kila mtu kuishi akikumbuka kwamba saa inapita mbio, kurudi kwa Bwana kunakaribia, na ya kwamba haifai tuache hali yetu ya raha kuzuiza bidii yetu kufanya mapenzi ya Mungu.⁹

W. E. Vine alisema:

Maana ya shairi hili haiko ya kwamba inapasa mume kuacha kute-ndea mke namna inavyofaa, lakini ya kwamba sharti hata ndani ya maneno haya ya nyumba Bwana apewe pahali pa kwanza.¹⁰

7:30 Haifai tuweke roho zaidi juu ya huzuni na furaha na mambo mengine ya maisha yetu, na kuyaacha kuzuiza utii wetu. Kupita maneno haya yote inatupasa kujitoa kabisa kutumikia Bwana kwa kila njia tunayoweza tungali tunapata njia.

7:31 Tungali tunapoishi duniani, hatuwezi kuepuka kukutana na maneno ya kidunia, na maneno haya ni halali kwa mwamini. Lakini Paulo alituonya kuka na ange tusiyatumie kwa njia **yasiyofaa**. Kwa mfano, haifai Mkristo kuweka roho sana juu ya vyakula, mavazi na maasi. Haifai aache maneno haya kugeuka kama mungu kwake. Maneno yote kama ndoa, mali, biashara, mambo ya serikali, musiki, na mengine yana pahali pao duniani, lakini yanaweza kuondosha mafikiri yetu juu ya maneno ya roho kama tukiyacha kufanya hivi.

Maneno haya **mambo ya dunia hii yanapita** yanatukumbusha ya kwamba vyote tunavyoona na macho yetu ni kwa wakati mfupi tu na vinakaa kubadilika.

7:32 Paulo alitaka Wakristo kuwa **pasipo masumbuko**. Alifikiri masumbuko yasiyofaa kuwazuiza wasitumikie Bwana. Aliendelea kueleza kwamba mtu **asiyeoa anasumbukia maneno ya Bwana – namna gani apate kupendeza Bwana**. Si kusema ya kwamba waamini wote wasiooa wanajitotoa bila mazuizo kwa Bwana, lakini ya kwamba watu wasiooa wana njia kufanya hivi kupita watu waliokwisha kuoa.

7:33 Na vilevile maana yake haiko ya kwamba **mume mwenye mke** hawezi kuweka roho sana juu ya maneno ya Bwana, lakini tunaona ndani ya maisha ya kila siku kwamba inampasa **kupendeza mke wake**. Ana masumbuko mengine zaidi ya masumbuko ya kazi ya Bwana. Kama Vine alivyoonyesha: “Kwa kawaida, mtu aliyeoa ameweza mpaka kwa eneo ya utimishi wake. Yule asiyeoaa , anaweza kwenda hata mwisho

wa dunia na kuhubiri Habari Njema.”¹¹

7:34 Mwanamke asiyeolewa anasumbuka juu ya maneno ya Bwana, awe mtakatifu katika mwili na roho: lakini ye ye anayeolewa anasumbuka juu ya maneno ya dunia – apate kupendeza mume wake. Ni kusema kwamba **mwanamke asiyeolewa, bikira**, anaweza kushinda saa nyingi kupita kwa **maneno ya Bwana**. Maana ya maneno haya “**awe mtakatifu katika mwili na roho**” si kusema ya kwamba ye ye ni mtakatifu kupita kwa sababu hakuolewa, lakini ya kwamba **anaweza kuwekwa mbali katika mwili na roho** kwa kazi ya Bwana. Si kusema ye ye ni safi kupita, lakini ana saa kupita kwa kazi ya Bwana.

Vilevile, **ye ye anayeolewa anasumbuka juu ya maneno ya dunia**, maana kazi ya kupika chakula, kuchunga watoto na nyumba, vivi hivi. Maneno haya ni mazuri na yanahitajiwa, na Paulo hayahukumu; alisema tu ya kwamba mwanamke asiyeolewa ana njia nyingine vilevile kwa kazi ya Bwana, na saa kupita mwanamke aliyeolewa.

7:35 Paulo hakutoa mafundisho haya na kusudi la kuingiza watu katika utaratibu ulio kama utumwa. Aliwafundisha kwa **faida** yao wenye tu, ili wakati wa-napowaza juu ya maisha yao, na kazi ya Bwana, watambue maongozi ya Bwana ndani ya maisha yao. Yeye mwenye tu alifikiri kwamba ni vizuri kukaa bila kuoa, kwani inawezesha mtu **kutumikia Bwana pasipo mazuizo ya mambo mengine**. Kwa mafikiri yake, mtu anaweza kuchagua kuoa au kukaa bila kuoa. Hakutaka **kutia mtego** mbele yao au kuwaingiza katika utumwa.

7:36 Mashairi 36-38 ndiyo mashairi yaliyo nguvu zaidi kufahamu ndani ya sura hii, na labda ndani ya barua hii nzima. Elezo moja ndilo hili: Kwa wakati wa Paulo wanaume walitawala

watu wa nyumba zao sana. Baba alichagua kama binti zake wataolewa au sivyo. Hawakuweza kufanya hivi bila ruhusa yake. Hivi watu wanafikiri kama baba akikataa kuruhusu binti zake kuoa, neno hili ni jema, lakini si zambi kama akiwaruhusu kuolewa.

Mwandishi mwininge, jina lake Kelly, alitoa elezo zuri kupita ndani ya kitabu chake. Kelly anaamini kwamba neno hili **bikira** (*parthenos*) linaweza kutafsiriwa “ubikira.” Hivi mashairi haya si juu ya binti ya mtu aliye bikira, lakini juu ya *ubikira wake mwenyewe*. Kama tukikubali tafsiri hii, maana ya mashairi haya ni ya kwamba ni vema kwa mtu kubaki bila kuoa, lakini kama akichagua kuoa, **hafanyi zambi**.

John Nelson Darby alitafsiri shairi hili hivi vilevile ndani ya tafsiri yake ya Biblia.

Hivi tunafikiri maana ya shairi 36 ni kama mwanamume aliyepata nguvu, na asiyeweza kujitawala mwenyewe, na anafahamu kwamba ikihitajiwa, **afanye kama anavyotaka**, na aoe.

7:37 Lakini kama mtu amefanya shauri kutumikia Bwana bila mashaka, na anaweza kujitawala mwenyewe, na **hana lazima** kuoa, kama akikusudi kubaki bila kuoa ili aweze kutumikia na kutukuza Mungu, **anafanya vema**.

7:38 Paulo alijumlisha neno hili hivi: **Yeye ambaye anajitoa kwa kuoana** anafanya vema, na yeye ambaye anakaa bila kuoa ili aweze kutumikia Bwana kupita **anafanya vema zaidi**.

7:39 Ndani ya mashairi mawili ya mwisho kuna maonyo kwa wajane. **Mke anafungwa na sheria kwa wakati mume wake ni hai**. Sheria hii ni sheria ya ndoa, iliyosimamishwa na Mungu mwenyewe. **Kama** mume wake amekufa, **yeye ni huru kuolewa kwa** mtu mwininge. Hii ni kweli tunayoona ndani ya Waroma 7:1-3, ya kwamba mauti inavunja ndoa. Lakini hapa katika 1 Ko-

rinto Paulo aliongeza neno moja lingine, ya kwamba anaweza kuolewa kwa mtu **anayetaka; katika Bwana tu**. Sharti mtu ambaye anamwoa awe Mkristo, lakini zaidi ya ile ndoa yenyewe iwe “katika mapenzi ya Bwana.” Ingewezekana kwa mjane kuolewa kwa Mkristo, lakini hata hivi ndoa yenyewe haiko kutaka kwa Mungu. Sharti aombe Mungu kumwo-ngoza ndani ya neno hili kubwa, na ku-olewa na mwamini yule ambaye Bwana anamchagulia.

7:40 Kwa mafikiri ya Paulo mjane **ana furaha zaidi** kama akikaa bila kuolewa. Mawazo haya hayabishi masemo yake kwa 1 Timoteo 5:14 kwamba wajane vijana wangepaswa kuolewa.

Halafu aliongeza, **“Ninazania ya kuwa nina Roho ya Mungu.”** Watu wengine wanaanguka wakati wanapofikiri Paulo alikuwa na shaka yeje mwenyewe wakati aliposema maneno haya. Tunakataa mawazo haya kabisa. Bila shaka Paulo aliongozwa na Mungu ndani ya maneno aliyoandika ndani ya mashairi haya. Wengine katika Korinto walikuwa na shaka juu ya mafundisho yake, na kama alikuwa mtume. Walisema mawazo yao yalitoka kwa Mungu. Paulo alisema na zihaka kidogo kwamba si neno kama watu waliwaza nini juu yake; yeje mwenyewe alifikiri kwamba alikwa na Roho ya Mungu vilevile. Bila shaka Wakorinto wale hawakufikiri wao peke yao walikuwa na Roho Mtakatifu!

Tunajua ya kwamba kweli Paulo alikuwa **na Roho Mtakatifu** ndani ya maneno yote ambayo alituandikia, na ya kwamba njia ya furaha kwa sisi ni kutii mafundisho yake.

B. Juu ya vyakula vilivyotolewa kwa sanamu (8:1-11:1)

Watu walioamini Kristo sasa tu walfazaika sana kama iliyapasa kula vyakula vilivyotolewa kwa sanamu. Labda mara nyingine waliitwa kwa

karamu kubwa hekaluni pahali vyakula vingine vilipokwisha kutolewa kwa sanamu. Au labda walikwenda kwa soko kununua vyakula, na walikuta mchinja nyama alikuwa akiuza nyama ili-yotolewa kwa sanamu. Neno hili halikugeuza faida ya nyama yenyewe, lakini Mkristo alifazaika kama ilimfaa kuinunua. Au mara nyingine mwamini aliitwa na rafiki nyumbani mwao kwa chakula kilichotolewa kwa sanamu yo yote. Akijua neno hili, ilikuwa vizuri kwa yeze kula chakula hiki? Ndani ya 8:1–11:1 Paulo alifundisha juu ya maneno haya.

8:1 Paulo alianza kusema kwamba Wakorinto na yeze mwenyewe walikuwa na elimu **juu ya vitu vilivyo-tolewa kama sadaka kwa sanamu**. Wao **wote** walijua kwamba kipande cha nyama hakigeuzwi kwa njia ya kutolewa kwa sanamu. Faida yake kama chakula kwa mwili haipunguki. Lakini Paulo alisema kwamba **elimu inaleta majivuno, lakini mapendo yanajenga**. Maana ya masemo yake ni ya kwamba elimu haitoshi katuongoza ndani ya maneno haya. Inaleta majivuno. Ndani ya maneno haya haitoshi kwa Mkristo kutegemea elimu yake tu, lakini mapendo vilevile. Inampasa kufikiri juu ya maneno yeze mwenyewe anayoweza kufanya, lakini vilevile juu ya yale yatakayosaidia watu wengine zaidi.

8:2, 3 Vine alifafanua shairi 2 hivi: “Mtu akizania anakwisha kujua maneno, hajaanza bado kufahamu namna gani kupata kuyajua.” Hakuna kujua kwa kweli bila mapendo. Lakini, **kama mtu akipenda Mungu, huyu anajulikana naye**, maana yake Mungu anapendezwa naye. Kwa njia moja, Mungu anajua kila mtu, lakini kwa njia nyingine anajua waamini zaidi. Hapa maana ya neno “kujua” linatumwiwa kuonyesha ukubali. Mungu anapendezwa sana na mtu ana-

yeongozwa na mapendo, si na elimu tu wakati anapochagua nini atafanya kwa maneno ya vyakula vilivyo-tolewa kwa sanamu.

8:4 Juu ya **sadaka kwa sanamu**, wa-amini wanafahamu ya kwamba sanamu si mungu wa hakika, wenye uwezo, ufahamu, na mapendo. Paulo hakukana kwamba kuna sanamu; alijua kwamba watu walichonga mifano toka miti au mawe. Nyuma alisema kwamba sanamu hizi zina uwezo wa pepo wachafu. Lakini neno alilosema juu yake hapa ni ya kwamba sanamu si mungu. **Hakuna Mungu ila mmoja tu**, ndiye Mungu na Baba wa Bwana Yesu Kristo.

8:5 Paulo alikubali kwamba katika maarifa ya hadizi za wapagano kulikuwa na mingine **iliyoitwa miungu**, kama Yupiteri, Yuno, na Merkurio. Watu wali-zani miungu hii iliishi **mbinguni**, na mingine, kama Ceres na Neptune, hapa **duniani**. Watu waliabudu miungu hii ya maarifa ya hadizi kama watumwa na kwa njia hii tunaweza kusema kulikuwa, na **miungu mingi na bwana wingi**.

8:6 Waamini wanajua kwamba kuna **Mungu mmoja, yeze Baba, na vitu vyote** vimetoka kwake, **nasi tunaishi kwake**. Maana yake ndiyo ya kwamba sisi tuliumbwa **kwa yeze, na tuko hai kwa kusudi hili**. Tunajua vilevile ya kwamba kuna **Bwana mmoja**, ndiye **Yesu Kristo, kwa yeze vitu vyote vimekuwa, na sisi kwa yeze**. Maneno haya kwa yeze **vitu vyote vimekuwa**, yanasema juu ya Bwana Yesu kama Mpatanishi, au kama Wakili, wa Mungu, na masemo haya **na sisi kwa yeze** yanaonyesha ya kwamba tuliumbwa na kukombolewa kwa njia yake.

Wakati Paulo aliposema **kuna Mungu mmoja, yeze Baba, na Bwana mmoja, Yesu Kristo**, hakutaka kusema kwamba Bwana Yesu Kristo si Mungu. Alitaka kuonyesha tu ya kwamba Mungu Baba na Mungu Mwana walikuwa na kazi

mbalimbali katika muumbo na ukombozi.

8:7 Lakini si Wakristo wote, zaidi waamini wa sasa, wanaofahamu uhuru wao ndani ya Yesu Kristo. Walikuwa waabudu sanamu na kujuana na sanamu, walifikiri waliabudu sanamu wakati walipokula nyama **iliyotolewa sadaka kwa sanamu**. Wanafikiri sanamu ni kitu cha hakika, na **zamiri yao ikiwa zaifu, imekuwa chafu**.

Uzaifu huu si **uzaiyu** wa mwili, au hata wa roho. Neno hili linatumwiwa hapa kwa watu wanaosumbuka zaidi juu ya maneno yasiyo mabaya. Kwa mfano, kwa mafikiri ya Mungu si vibaya kwa mtu kula nyama ya nguruwe. Ingaliyuwa zambi kwa Myuda katika Agano la Kale kufanya hivi, lakini Mkristo ni huru kula vyakula namna hii. Lakini inawezekana kwa zamiri ya Myuda aliyegeuka Mkristo sasa tu kukaa kumshitaki. Biblia inamwita ndugu zaifu, naye hafurahi ndani ya uhuru wake kama Mkristo. Angali anafikiri ni zambi kwa yeche kula nyama ya nguruwe, ingekuwa zambi kweli kwaye kula nyama ile. Hii ndiyo maana ya **zamiri yao ikiwa zaifu imikuwa chafu**. Zamiri yangu ikinifahamisha kwamba neno fulani ni zambi, lakini hata hivi ninafanya neno lenyewe, ninatenda zambi. “Kila tendo lisilotoka katika imani ni zambi” (Rom. 14:23).

8:8 Vyakula si neno kubwa kwa mafikiri ya **Mungu**. Hatupendezi Mungu kupita kwa njia ya kujinyima vyakula fulani, na hatugeuki Wakristo wazuri kupita kwa njia ya kula vyakula namna hii.

8:9 Lakini hata kama si faida kwa mimi kula vyakula hivi, labda vinegeuka hasara kubwa kama kwa sababu ninavikula ninakwalisha Mkristo **zaifu**. Nikitenda hivi sitendi na mapendo. Mkristo ni huru kula vyakula vilivytoplewa mbele kama sadaka kwa sanamu, lakini ingaliyuwa zambi kubwa kwa yeche kufanya hivi kama kwa njia hii

angalikwalisha ndugu au dada **zaifu**.

8:10 Ni hatari kwa ndugu zaifu kufanya neno fulani hata kama zamiri yake ikimshitaki juu yake, kwa sababu **anona** mwamini akitenda neno lenyewe. Ndani ya shairi hili, mtume anakataza mwenye elimu **kula ndani ya hekalu la sanamu** kwa sababu inaweza kuwa mwangukisho kwa watu wengine. Wakati Paulo aliposema juu ya **kula ndani ya hekalu la sanamu**, alifikiri matukio kama karamu au ndoa. Isingalifaa kamwe kula ndani ya hekalu namna hii kwa kuabudu sanamu. Paulo alihukumu neno hili nyuma (10:15-26). Maana ya **mtu akikuona wewe uliye na elimu** ni kama mtu ye yote akikuona wewe, Mkristo huru, ambaye unajua kwamba vyakula vilivytoplewa kwa sanamu, havichafuwi, vivi hivi. Neno kubwa ndilo hili: Haifai tuwaze tu kama tendo namna hii ni vizuri kwa sisi wenyewe, lakini kama litasaidia au kuangusha watu wengine.

8:11 Inawezekana kwa mtu kuonyesha **elimu** yake ya maneno gani ni halali kwa Mkristo kufanya, na kwa njia hii kukwalisha ndugu katika Kristo. Maana ya neno hili **angamizwa** hapa si ya kwamba atapoteza uzima wake wa milele, lakini hali yake njema itapotea. Neno hili litapunguza ushuhuda wa ndugu huyu zaifu. Maneno haya **na Kristo alikuwa kwa ajili yake** yanaonyesha ubaya mkubwa wa kuumiza ndugu zaifu. Kristo alipenda mtu huyu sana, hata alimkufia, hivi haifai hata kidogo kufanya neno lo lote ambayo litamzuiza asiendelee ndani ya imani yake.

8:12 Wala si neno la kukosea ndugu katika Kristo tu, na kuuzima **zamiri yake zaifu**. Ni kufanya zambi juu ya **Kristo** mwenyewe. Neno lo lote tunalotendea ndugu zake walio wadogo tunamtendea yeche. Kitu cho chote kinachoumiza mmoja wa viungo vya Mwili kinaumiza Kichwa vilevile. **Zambi juu ya Kristo** ndiyo zambi ku-

bwa kupita zote. Tukifahamu neno hili, inatupasa kuangalia matendo yetu yote sana tusifanye kitu cho chote kina-chowenza kuangusha ndugu yetu.

8:13 Akikumbuka kwamba ni zambi juu ya Kristo kufanya neno lo lote linaloweza **kuangusha ndugu**, Paulo alisema hatakula **nyama hata milele**, **asiangushe** ndugu yake. Kazi ya Mungu ndani ya maisha ya mtu mwingine ni kitu kikubwa kupita chakula kitamu! Kwa wakati wa sasa zaidi ya Wakristo hawasumbushwi na vyakula vikitolewa kwa sanamu, lakini Roho Mtakatifu anatutolea *mafundisho ya faida sana* juu ya maneno mengine namna hii. Kuna maneno mengi ndani ya maisha ya Wakristo kwa wakati wa sasa yasi-yokatazwa ndani ya neno la Mungu, lakini yanayoweza kuangusha Wakristo zaifu. Hata tukiwa na ruhusa kushiriki ndani ya maneno haya, ni vizuri zaidi kutoyafanya kwa ajili ya baraka ya waamini ambaو tunawapenda ndani ya Kristo, waamini wenzetu.

Ni kama sura 9 inaanza mafundisho juu ya neno lingine kabisa, lakini tutasoma juu ya vyakula vikitolewa sadaka kwa sanamu kwa sura mbili nyingine. Paulo anapasha kwanza juu ya maisha *yake mwenyewe* kama *mfano* wa kujinyima mwenyewe ili kusaidia watu wengine. Akiwa mtume ilikuwa haki yake kusaidiwa na mali kwa mahitaji yake, kama tulivoona ndani ya 8:13. Hivi sura 9 inafungana na sura 8.

9:1 Kama tulivoona, kulikuwa na watu wengine katika Korinto waliokuwa na shaka juu ya amri ya Paulo. Walisema hakuwa mmoja wa mitume kumi na wawili, hivi hakuwa mtume wa kweli. Paulo alikataa kwamba alikuwa chini ya amri ya watu wa dunia, akasema yeye ni **mtume** wa kweli wa Bwana Yesu. Alitaja maneno mawili kuhakikisha neno hili. 1) Alikuwa **ameona Yesu Kristo Bwana wetu** katika utukufu. Neno hili lilitokea wakati alipokwenda Damasiki.

2) Alitaja Wakorinto wenyewe kuhakikisha kwamba yeye ni mtume, kwa njia ya kuuliza, “**Ninyi si kazi yangu katika Bwana?**” Kama wakiwa na shaka juu ya utume wake, watafute roho zao. Waliikuwa wamepata wokovu? Bila shaka wangejibu, Ndiyo. Basi nani aliwangazia Habari Njema na kuwangoza kuamini Kristo? Paulo mwenyewe! Hivi imani yao wenyewe ili-hakikisha kwamba alikuwa mtume wa haki wa Bwana.

9:2 Labda **watu wengine** waliweza kuwa na shaka kama alikuwa **mtume**, lakini si Wakorinto! Wao wenyewe waliikuwa **muhuri** wa **utume wake** katika **Bwana**.

9:3 Paulo alisema maneno haya kujisimamia mwenyewe kwa wale **ambao walimwuliza** au waliokuwa na shaka kama alikuwa na amri ya mtume.

9:4 Ndani ya mashairi 4-14, mtume alisema kwamba ilikuwa **haki** yake kusaidiwa na mali kwa mahitaji yake kama mtume. Alitumwa na Bwana Yesu, na kwa sababu hii ilikuwa haki yake kupokea mali toka waamini. Lakini hakuomba apewe mali hii kila mara. Mara nyingi alitumika na mikono yake kufanya hema, ili aweze kuhubiri Habari Njema kwa wanaume na wanawake bila kuwalipiza mali. Bila shaka neno hili liliwapa wajuzi wake njia kusema Paulo alifanya hivi kwa sababu alijua hakuwa mtume wa kweli. Alianza kusema juu ya maneno haya: “**Hatuna uwezo wa kula na kunywa?**” – bila kutumika kazi? Hatustahili kusaidiwa na kanisa?

9:5 **Hatuna uwezo wa kupeleka pamoja na sisi mke aliye ndugu, kama mitume wengine, na kama ndugu za Bwana, na Kefa?** Labda wengine wa wajuzi walisema Paulo hakuoa kwa sababu alijua yeye na mke wake wasingestahili kusaidiwa wao wawili na mali ya makanisa. Petro na mitume wengine waliolewa, na **ndugu za Bwana** vilevile. Paulo alisema hapa

kwamba ilikuwa haki yake vilevile kuona kusaidiwa na Wakristo pamoja na mke wake. Maneno haya “**kupeleka pamoja na sisi mke aliye ndugu**” si juu ya haki ya kuoa tu, lakini juu ya haki ya kupokea mali wao wawili toka Wakristo. Labda **ndugu za Bwana** walikuwa ndugu wenyewe mama mmoja na baba mwininge. Mashairi mengine yanaonyeshaa kwamba Maria alizaa watoto wengine nyuma ya Yesu, Mzaliwa wake wa kwanza (Lk. 2:7; ona Mt. 1:25; 12:46; 13:55; Mk. 6:3; Yn. 2:12; Gal. 1:19).

9:6 Ni kama **Barnaba**, kama Paulo, alikuwa ametumika kazi kupata mali kwa mahitaji yake pamoja na kuhubiri Habari Njema. Paulo aliuliza kama wao wawili tu hawakuwa na ruhusa **kuacha kufanya kazi** na kuchungwa na watu wa Mungu?

9:7 Paulo alianza na kusema ya kwamba alistahili kupata kusaidiwa kama mitume wengine. Aliendelea na kutaja mifano toka maisha ya kila siku ya watu. Askari **anapokea mshahara** kwa mahitaji yake yeeye mwenyewe wakati anapokwenda kupiga vita. Mtu **anapanda shamba la mizabibu** pamoja na kupokea sehemu ya **matunda yake**. Mchungaji analinda kundi na ana ruhusa kunywa **la maziwa yake**. Utumishi wa Wakristo ni kama kazi ya askari, walmajji, na wachungaji. Ni kupiga vita na adui, ni kuchunga miti ya matunda ya Mungu, na kulinda kondoo zake. Kama watu wanaofanya kazi hii duniani wakistahili kusaidiwa na mali, kuzidi sana wale wanaotumikia Bwana!

9:8 Halafu Paulo alionyesha kwamba maneno haya yalifundishwa hata ndani ya Agano la Kale.

9:9 Iliandikwa wazi ndani ya Torati 25:4 ya kwamba **haifai kufunga kinywa cha ngombe anayekanyaga ngano** wakati wa kuvuna. **Mungu anaangalia maneno ya ngombe?** Ndiyo, Mungu anaangalia ngombe,

lakini hakuandikisha maneno haya ndani ya Agano la Kale kwa ajili ya nyama zisizouja kitu. Neno hili linatufundisha sisi neno kubwa kwa maisha na utumishi wetu kwa Bwana.

9:10 Au liliandikwa kwa ajili yetu? Ndiyo, Mungu alifikiri hali yetu wakati maneno haya **yalipoandikwa**. Wakati mtu **anapolima** shamba **alime** kwa matumaini ya kupata mshahara. Vivyo hivyo, wakati mtu **anapopura** ngano apurie na matumaini ya kwamba atapewa nusu ya mavuno. Utumishi wa Wakristo unafanana na kulima na kuvuna, na Mungu ameamuru ya kwamba haifai wale ambao wanamtumikia kwa njia hii walipe kwa mahitaji ya kazi hii wao wenyewe.

9:11 Paulo alisema juu yake mwenyewe kama mwenye **kupanda vitu vya roho kwa Wakristo** kwa Korinto. Ni kusema alifikia Korinto kuhubiri Habari Njema, na kuwafundisha kweli za roho. Hivi ni neno kubwa kwa yeeye kuwaomba kumsaidia na **mali yao au vitu** vingine? Mawazo yake ndiyo ya kwamba “mshahara wa mhubiri ni mdogo tu wakati unaposawanishwa na baraka kubwa za roho walizopokea.”

9:12 Paulo alijua kwamba kanisa kwa Korinto walikuwa wakisaidia **wengine** waliokuwa wakihubiri au ku-fundisha pale. Walifahamu kwamba ili-wapasa kusaidia watu wale, lakini si mtume Paulo, hivi aliuliza: “**Ikiwa wengine wanashiriki amri hii juu yenu, si sisi zaidi?**” Kama wakifahamu kwamba iliwapasa kusaidia watu wale, kwa sababu gani hawakufahamu ya kuwa yeeye, baba yao katika imani, alistahili kusaidiwa vilevile? Bila shaka wale waliokuwa wakisaidiwa na mali walikuwa walimu ambao waliwfundisha kufungana na maneno ya dini ya Wayuda. Paulo aliongeza kusema kwamba hata alikuwa na **uwezo huu**, hakuutumia na Wakorinto, lakini alivumilia

maneno yote asizuize Habari Njema ya Kristo. Kwa pahali pa kusema nao na nguvu wamsaidie na mali, alivumilia ukosefu na taabu namna hii, ili Habari Njema isizuiwwe.

9:13 Halafu Paulo alisema juu ya watu wale waliotumika ndani ya hekalu la Wayuda. Wale waliokuwa na kazi hekaluni walisaidiwa na mali ambayo hekalu lilipokea. Kwa njia hii **walikula sehemu ya vitu vya hekalu**. Vilevile makuhani wenyewe waliotumikia **kwa mazabahu** walipewa sehemu fulani **ya matoleo** yaliyoletwa kwa **mazabahu**. Hivi Walawi waliokuwa na kazi ya kila siku hekaluni, na makuhani wenyewe kazi takatifu kupita, walisaidiwa na mali ndani ya kazi yao.

9:14 Mwishoni Paulo alitaja agizo la **Bwana mwenyewe**. **Aliagiza kwamba ingepasa wale wanaohubiri Habari Njema wapate maisha yao kwa Habari Njema**. Agizo hili lilitosha ku-hakikisha kwamba ilikuwa haki ya Paulo kusaidiwa na mali ya Wakorinto. Kwa sababu gani hakuomba wafanye hivi? Jibu la ulizo hili ni ndani ya mashairi 15-18.

9:15 Alieleza ya kwamba **hakutumia mambo haya hata moja**. Wala hakuandika **maneno haya** kwa wakati ule kusudi wamtumie mali. Angetaka **kufa kuliko kwa mtu** kufanya bure **kujisifu** yake.

9:16 Paulo alisema kwamba hawezi **kujisifu** juu ya kuhubiri Habari Njema. Aliwekewa **lazima toka Mungu**. Hakuwa kazi ambayo alijichagulia mwenyewe. Angalikuwa mtu wa huzuni kubwa zaidi kama asingalitii amri toka Mungu. Si kusema kwamba hakutaka kuhubiri Habari Njema, lakini si yeze aliyechagua kufanya hivi, lakini ilikuwa agizo la Bwana.

9:17 Kama mtume akihubiri Habari Njema kwa **mapenzi** yake, ameaminiwa zawabu, ndio mali kusaidia mahitaji yake. Ilionekana wazi ndani ya Agano la

Kale na Agano Jipy ya kwamba ni haki ya wale wanaotumikia Bwana kupokea mali toka watu wa Bwana. Maana ya masemo haya ya Paulo haiko kwamba hakutaka kutumikia Bwana, lakini kuliwa na lazima toka Mungu ndani ya utume wake. **Kama** hakuhubiri kwa **mapenzi yake**, maana kama akisukumwa na moto uliowaka ndani ya roho yake ambao ulimlazimisha kuhubiri, **aliaminiwa uwakili** wa Habari Njema. Aliagizwa kuhubiri, na hakuweza kujisifu juu ya neno hili.

Ni nguvu kufahamu maana ya shairi hili, lakini Paulo hakutaka kujikamatia haki yake toka Wakorinto kwa mahitaji yake, kwa sababu hakujichagulia utumishi huu yeze mwenyewe. Aliupewa na Mungu. Walimu wa uwongo katika Korinto wangeweza kusema ilikuwa haki yao kusaidiwa na waamini, lakini mtume Paulo alitazamia kupokea zawaibu yake toka pahali pengine.

Knox alitafsiri shairi hili hivi: “Ninawenza kuomba zawaibu kwa kazi ninayofanya kwa kutaka kwangu; lakini kama nikiagizwa kufanya kitu fulani, ninatii amri tu.”

Ryrie alisema:

Paulo hakuweza kuepuka kazi yake kuhubiri Habari Njema, kwa sababu alipewa uwakili, na aliagizwa kuhubiri Habari Njema hata kama hakupokea mshahara (ona Lk. 17:10).¹²

9:18 Basi, kama hakuweza kujisifu juu ya kuhubiri Habari Njema, atawea kujisifu juu ya nini? Aliweza kujisifu juu ya neno alilochagua yeze mwenyewe, ndilo ya kwamba aliweza kufanya **Habari Njema pasipo bei**. Ni neno hili alilokusudi kufanya. Atahubiri Habari Njema kwa Wakorinto, pamoja na kutumika kazi kupata mali kwa mahitaji yake wenyewe, bila kutumia haki yake ya kusaidiwa na mali toka kwao **kwa Habari Njema**.

Kujumlisha mawazo ya mtume, alionyesha tofauti ya maneno ya lazima na maneno yasiyokuwa lazima. Hakuna neno lililoonyesha kwamba Paulo hakutaka kuhubiri Habari Njema. Alihubiri na furaha. Lakini ilikuwa lazima kwake, amri toka Mungu, na hakuna njia kwa Paulo kujisifu juu ya kutii amri hii. Kama akihubiri Habari Njema, angeweza kuomba na nguvu kusaidiwa na mali, lakini hakufanya hivi. Alikusudi kuhubiri Habari Njema kwa Wakorinto **bila bei.** Kwa sababu ye ye mwenyewe alikusudi kufanya hivi, ataweza kujisifu. Tulsionyesha mbele ya kwamba wajuzi wa Paulo walisema kwamba kazi yake ya kufanya hema ilionyesha ya kuwa hakufikiri ye ye ni mtume wa kweli. Hapa Paulo alionyesha kwamba kwa njia ya kutumika kazi alihakikisha ya kuwa alikuwa hata hivi mtume wa hakika.

Ndani ya mashairi 19-22 Paulo aliandika kwa sababu gani alichagua kutokeopea kusaidiwa na mali iliyokuwa haki yake, kwa sababu ya Habari Njema. Wakati tunaposoma mashairi haya, sharti tukumbuke ya kwamba hakuacha kamwe kushikamana na kweli kubwa za Maandiko. Alitenda namna watu ambao alitumika nao walivyotenda kusudi waweze kukubali kusikia Habari Njema. Lakini hakutenda kamwe neno lo lote lililoasi kweli ya Habari Njema.

9:19 Kwa njia moja alikuwa **huru toka watu wote.** Hakuna mtu aliye weza kumlazimisha kufanya neno. Hata hivi alijifanya mwenyewe mtumwa wa **wote ili aweze kupata watu wengi zaidi.** Alikuwa tayari kufanya kila neno lililowezekana bila kupunguza kweli ya Habari Njema, ili aweze kupata watu kwa Kristo.

9:20 Kwa Wayuda alikuwa kama Myuda, apate Wayuda. Si kusema ali-jiweka chini ya amri ya sheria ya Musa tena ili Wayuda waokolewe. Mfano wa maana ya masemo yake ni namna ali-

vyotenda kwa maneno ya tohara ya Timoteo na Tito. Juu ya Tito, kulikuwa na watu wengine waliosema na nguvu hawezu kuokolewa bila kutahiriwa. Paulo alifahamu kwamba watu wale walikuwa wakishindana na Habari Njema ya neema ya Mungu, hivi alikataa kabisa kwa Tito kutahiriwa (Gal. 2:3). Lakini kwa maneno ya Timoteo, hakuna mashindano ya namna hii. Hivi Paulo alikubali kwa Timoteo kutahiriwa ili kwa njia hii watu wengi kupita watasikia Habari Njema (Mdo. 16:3).

Kwa wale walio chini ya sheria, nilikuwa kama chini ya sheria,²⁹ nipaye wale walio chini ya sheria. Wale walio chini ya sheria ndio Wayuda. Lakini Paulo alikuwa amesema mbele juu ya mambo yake na Wayuda ndani ya sehemu ya kwanza ya shairi hili. Kwa sababu gani alisema juu ya maneno yao tena? Elezo ambalo lilitolewa mara nyingi ni ya kama wakati Paulo aliposema juu ya Wayuda ndani ya shairi hili, alifikiri juu ya desturi zao kama taifa la Wayuda, lakini hapa alifikiri maisha yao ya dini.

Kama Myuda Paulo alizaliwa chini ya sheria. Alijaribu kupendeza Mungu kwa njia ya kutii sheria, lakini ilimshinda kufanya hivi. Sheria ilimwonyeshea tu ya kwamba ye ye ni mwenye zambi mbaya sana, na ilimhukumu kabisa. Mwishoni alijifunza kwamba haiwezekani kupokea wokovu kwa njia ya sheria. Ilikuwa njia ya Mungu kufunulia mtu uovu wake na hitaji lake kwa Mwokozi. Halafu Paulo aliamini Bwana Yesu Kristo, na wakati alipofanya hivi, alifunguliwa toka mashitaki ya sheria. Bwana Yesu alikuwa amelipa azabu ya sheria ambayo Paulo alikuwa amevunja.

Nyuma ya kuokolewa kwake, mtume alijifunza kwamba sheria si njia ya wokovu, wala namna gani inapasa Mkristo kuishi. Mwamini si chini ya sheria lakini chini ya neema. Neno hili

halimpi njia kufanya neno lo lote analotaka. Sasa, akijuana na neema ya Mungu, neno hili litamzuiza asitake kufanya maneno yasiyofaa. Sasa, kwa sababu Roho Mtakatifu anakaa ndani yake, Mkristo anataka kuishi maisha matakatifu kupita mbele, si kwa sababu ya woga wa azabu kwa sababu ya kuasi sheria, lakini kwa sababu ya mapendo yake kwa Kristo, ambaye alimkufia na kufufuliwa tena. Wakati alipokuwa chini ya sheria, alisukumwa na woga. Sasa, akiwa chini ya neema, anasukumwa na mapendo. Neno hili ni zuri zaidi. Watu wanakubali kufanya maneno kwa sababu ya mapendo, wasiyoweza kufanya kamwe kwa sababu ya woga.

Nyuma ya maelezo haya, turudi tena kwa sehemu ya pili ya shairi 20. **Kwa wale walio chini ya sheria, nilikuwa kama chini ya sheria, hata mimi mwenyewe si chini ya sheria, nipate wale walio chini ya sheria.** Wakati alipokuwa pamoja na Wayuda, alitenda kama Myuda kwa maneno mema. Alikula vyakula Wayuda walivyokula na hakula vyakula kama nyama ya nguruwe walivyokatazwa kula. Labda ha-kufanya kazi siku ya sabato aki-jua akifanya hivi, labda watu watakuwa na roho tayari zaidi kusikia Habari Njema.

Paulo akiwa mwamini, mwenendo wake haukutawaliwa na sheria. Alijilanganisha tu na desturi na mazoea ya watu ili aweze kuwaongoza kuamini Bwana.

9:21 Ryrie aliandika:

Paulo hakuwa mtu wa kugeukageuka, lakini alikuwa mwenye kujitawala mwenyewe saa zote ili aweze kusaidia watu wa kila namna.¹³

Kwa wale wasio na sheria, Paulo alitenda **kama** mtu asiye na sheria (hata kama yeye mwenyewe **hakuwa bila sheria mbele ya Mungu, lakini chini**

ya sheria ya Kristo). Wale **wasio na sheria** si waasi wasiotambua sheria yo yote, lakini ni Mataifa. Sheria ilitolewa kwa taifa la Wayuda, si kwa Mataifa. Hivi wakati Paulo alipokuwa pamoja na Mataifa aliambatana na desturi zao kwa kipimo alichowenza bila kukana Mwo-kozi. Alieleza ya kwamba hata wakati alipotenda kama mtu **bila sheria, hakuwa bila sheria kwa Mungu.** Hakufikiri alikuwa huru kufanya neno lo lote alilotaka, lakini **alikuwa chini ya sheria ya Kristo.** Hivi ilimpasa kuperenda, kuheshimu, kutumikia, na kuperendeza Bwana Yesu, si sasa kwa sababu ya sheria ya Musa, lakini kwa sababu ya sheria ya mapendo.

9:22 Shairi hili linasema juu ya wale waliokuwa **zaifu** na kufikiri kupita kipimo juu ya mambo yasiyokuwa maneno makubwa. **Kwa wenye uzaifu** Paulo **alikuwa zaifu**, apate wazaifu. Angekula mboga tu, kama ikitajijiwa, ili asiumize roho zao kwa njia ya kula nyama. Kwa ufupi, alikuwa **vitu vyote kwa watu wote, hata kwa njia zote apate kuokoa wengine.** Haifai kamwe kutumika na mashairi haya kutoa uzuru kwa kufanya neno lo lote lisilopatana na mafundisho ya Neno la Mungu. Yanafundisha tu kujaribu kupatana na desturi za watu kusudi waweze kuwa tayari kusikia Habari Njema. Wakati Paulo aliposema **nipate kuokoa wengine**, haku-fikiri hata kidogo kwamba atawenza kuokoa mtu mwingine. Alijua kwamba Bwana Yesu tu aliweza kuokoa watu. Lakini ni ajabu kuona kwamba wale wanaotumikia Kristo kwa njia ya kuhubiri Habari Njema, wanafanywa mamoja sana naye, hata anawaruhusu kutumika na neno hili **okoa** kupasha juu ya kazi yao. Neno hili linaheshimu na kutukuza sana kazi ya kutangaza Habari Njema.

Mashairi 23-27 yanaonyesha hatari ya kupoteza zawabu yetu kama tusipo-jitawala mwenyewe. Paulo alikataa ku-saidiwa na mali toka Wakorinto kwa

sababu ya kujitawala mwenyewe.

9:23 Na ninafanya haya yote kwa sababu ya Habari Njema niishiriki pamoja na ninyi. Ndani ya mashairi yaliyotangulia shairi 22, Paulo akaeleza kwamba alizamisha haki na kutaka kwake mwenyewe kwa ajili ya kufanya kazi ya Bwana. Alifanya hivi kwa sababu gani? Alifanya hivi **kwa sababu ya Habari Njema**, ili aweze kushiriki pamoja nao ndani ya kushinda kwa Habari Njema kwa wakati wa kuja.

9:24 Wakati Paulo alipoandika shairi hili, bila shaka aliwaza juu ya mashindani ya michezo kwa Isthmia, karibu na Korinto. Wakristo wa Korinto wangejuana na mashindano haya. Paulo aliwakumbusha kwamba hata watu wengi **wanapiga mbio** katika mashindano, si wote wanaopokea **zawadi**. Maisha ya Mkristo ni kama shindano. Inampasa kujitawala mwenyewe. Inampasa kutumika na nguvu na kuwa na bidii sana. Lakini shairi hili halifundishi kwamba ndani ya shindano la kikristo mtu mmoja tu anaweza kupata zawadi. Linafundisha kwamba inatupasa sisi sote kupiga mbio kama washindaji. Ingetupasa sisi sote kujitawala wenyewe kama Paulo. Ndani ya shairi hili zawadi si wokovu, lakini zawaabu kwa utumishi mwaminifu. Hatusomi kamwe juu ya kupokea wokovu kwa sababu ya kupiga mbio na uaminifu katika shindano. Wokovu ni zawadi, bila malipo toka Mungu ambayo tunapokea wakati tunapoamini Bwana Yesu Kristo.

9:25 Mtume anakaa kusema juu ya kushindana. Kila mtu anayeshiriki ndani ya mashindano, ana kiasi katika **maneno yote**. Paulo anafikiri juu ya mshindaji anayeitwa kutokea mbele ya watu kupokea zawadi yake. Atapokea zawadi gani? **Taji ya kuharibika**, maua au majani yanayosokotwa kama taji, na yanayokauka mbio. Halafu alisema ya kuwa wote waliotumikia Kristo na uaminifu watapokea **taji isiyoharibika**.

9:26 Akifikiri juu ya taji hii isiyoharibika, Paulo alisema kwamba ana-piga mbio vivyo hivyo, **si kama ovyo**; anapigana, si kama mwenye **kupiga hewa**. Utumishi wake haukuwa ovyo na bila faida. Alikuwa na kusudi fulani, na alitaka matendo yake yote kusaidia kutimiza kusudi hili. Hakutaka kupoteza saa wala nguvu yake bure.

9:27 Alitesa **mwili** wake **na kuutumikisha**, isiwe, akikwisha **kuhubiri kwa wengine**, ye ye mwenyewe atakataliwa. Sharti Mkristo ajitiishe mwenyewe na kuwa na kiasi.

Mtume Paulo alifahamu pamoja na woga mkubwa ya kwamba inge-wezekana kwa ye ye mwenyewe **ku-kataliwa** nyuma ya **kuhubiri kwa watu wengine**. Watu wanatafsiri shairi hili kwa njia mbalimbali. Wengine wana-fikiri mtu anaweza kuokolewa, lakini anaweza kupotea tena. Mawazo haya hayapatani hata kidogo na mafundisho ya Agano Jipyä ya kwamba hakuna kondoo ya kweli ya Kristo atakayepotea kamwe.

Wengine wanasema neno hili **kukataliwa** ni neno kali sana na linasema juu ya laana ya milele. Wanafikiri kwamba Paulo hafundishi ya kuwa mtu ye yote aliyekolewa kweli ataweza kukataliwa kamwe, lakini ya kwamba mtu ambaye hajitawali mwenyewe hakuokolewa kamwe. Paulo aliwaza juu ya walimu wa uwongo na namna walivyotenda anasa namna namna. Alionyesha ya kwamba mtu asiyetiisha mwili wake, neno hili linahakikisha kwamba hakuzaliwa tena. Hata akihubiri kwa watu wengine, ye ye atakataliwa.

Elezo la tatu ni ya kwamba Paulo hakusema juu ya wokovu, lakini juu ya utumishi. Hakufikiri kwamba atapotea kamwe, lakini ya kwamba utumishi wake hautakubaliwa na Bwana, naye hatapokea zawadi. Paulo aliogopa sana kwamba nyuma ya **kufundisha watu wengine**, ye ye mwenyewe atakataliwa,

na Mungu hataweza kutumika naye tena kwa kazi yake.

Inapasa kila mtu anayetaka kutumikia Bwana kuwaza sana juu ya mashairi haya, na kutafuta roho yake. Vizuri kila mtu akusudi kwa neema ya Mungu ya kwamba hatajuana na neno hili kamwe ndani ya maisha yake mwenyewe.

Wakati Paulo alipowaza juu ya hitaji la kujitawala mwenyewe, alikumbuka mfano wa Waisraeli zamani. Ndani ya sura 10 anakumbuka kwamba walijipendelea wenyewe na hawakutiisha miili yao, na hivi walikataliwa.

Kwanza alisema juu ya mapendeleo ya Israeli (mash. 1-4); halafu juu ya azabu ya Israeli (sh. 5); na mwishoni juu ya kuangamizwa kwao (mash. 6-10). Halafu anaeleza namna gani maneno haya ni mfano kwetu (mash. 11-13).

10:1 Mtume alikumbusha Wakorinto ya kwamba **baba** Wayuda **zote walikuwa chini ya wingu**, na **wote walipita katika bahari**. Neno kubwa ni **wote**. Alikumbuka wakati walipoponyeshwa toka Misri, na kuongozwa kwa njia ya ajabu na nguzo ya **wingu** mchana, na nguzo ya moto usiku. Alikumbuka wakati walipovuka Bahari Nyekundu na kupona jangwani. Wao wote walipendeleta kwa njia ya kuongozwa na kuponyeshwa na Mungu.

10:2 Zaidi ya ile, wao wote wakabatizwa na Musa katika wingu na katika bahari. Maana yake ndiyo ya kwamba walifanywa mamoja naye na kukubali kuongozwa naye. Wakati Musa alipoongoza wana wa Israeli toka Misri kwenda Inchi ya Ahadi, taifa zima waliahidi kumtii kwanza, na walimtaambua kuwa mwokozi wao toka Mungu. Maneno haya “chini ya wingu” yanasema juu ya kufanywa mamoja na Mungu, na maneno haya “katika bahari” yanasema juu ya maneno ambayo yaliwatenga na Misri.

10:3 Wao **wote wakakula chakula kile cha roho**. Ni mana ambayo Mungu

aliwapatia kwa njia ya ajabu wakati wali-posafiri jangwani. Maneno haya **chakula cha roho** si kusema kwamba hawakuweza kukiona na macho, lakini ya kwamba chakula hiki kilikuwa mfano wa vyakula ambavyo viliwasaidia rohoni. Ni vyakula viliviyotoka kwa Mungu.

10:4 Katika safari zao zote Mungu aliwapatia maji kunywa. Yalikuwa maji ya namna ya dunia, lakini yaliitwa vilevile **kinyweo cha roho**. Yaliwaburudisha rohoni, na waliyapata kwa njia ya ajabu. Wangalikufa kwa kiu kama Bwana asingaliwapatia maji. Masemo haya, **walikunywa katika mwamba ule wa roho ambao uliwafuata**, si kusema kwamba mwamba wa inchi ulisafiri nyuma yao. Mwamba ni mfano wa mto wa maji uliotoka kwake na kufuata Waisraeli. Na **mwamba ule ni Kristo**. Yeye ndiye mwenye kuleta maji ya uzima kwa watu wake.

10:5 Nyuma ya kutaja baraka hizi zote, ilipasa mtume kukumbusha Wakorinto ya kwamba **Mungu hakupendezwa na watu wengi katikati yao: kwa maana waliangamizwa jangwani**. Waisraeli wote walikuwa wameondokea Misri, na wote walikiri kufungana na mwongozi wao, ndiye Musa, na roho moja. Ilikuwa huzuni kwa sababu miili yao ilikuwa jangwani, lakini roho zao zilibaki kwa Misri. Walifurahi kufunguliwa toka utumwa wa Farao, lakini walikaa kutamani anasa ya zambi ya inchi ile. Askari wenyе miaka kupita miaka 20 wote waliondokea Misri, lakini wawili tu walipokea zawadi, ndio Kalebu na Yosua – wakafikia Inchi ya Ahadi. Maiti za wote wengine ziliangamizwa **jangwani** kama ushuhuda ya kwamba Mungu hakupendezwa nao.

Ona kwamba ndani ya mashairi 1-4 tulisoma tena na tena “**wote**,” lakini ndani ya shairi 5 tunasoma “**wengi katikati yao**.” Wote walikuwa wenyе mapendeleo, lakini **wengi katikati yao** waliangamizwa.

10:6 Matukio haya kwa wakati wa Kutoka yana mafundisho kwa sisi. Watto wa Israeli walikuwa **mifano** kwa sisi. Wanaonyesha nini itatupata sisi kama **tukitamani vitu vibaya kama wao** walivyotamani. Wakati tunaposoma Agano la Kale tuone ndani yake mafundisho kwa sisi kwa wakati wa sasa.

Ndani ya mashairi yanayofuata mtume anataja mengine ya makosa waliyofanya. Mengi yalikuwa matunda ya tamaa za mwili.

10:7 Shairi 7 ni juu ya kuabudu kwa ndama ya zahabu na karamu iliyofuata, ona Kutoka 32. Wakati Musa aliposhuka mlima Sinai, alikuta watu walikuwa wamefanya ndama ya zahabu na walikuwa wakiiabudu. Ndani ya Kutoka 32:6 tunasoma kwamba **watu waliketi kula na kunywa, wakasimama kucheza**.

10:8 Zambi inayotajwa ndani ya shairi 8 ilitukia wakati wana wa Israeli walipooa binti za Moabu (Hes. 25). Nabii Balama aliwashawishi kutenda zambi, wakaasi neno la Bwana na walienda uasherati. Tunasoma ndani ya shairi 8 ya kwamba kwa siku moja **watu elfu makumi mbili na tatu walanguka**. Ndani ya Agano la Kale iliandikwa kwamba watu elfu makumi mbili na ine walikufa kwa sababu ya pigo (Hes. 25:9). Wajuzi wa Biblia wametumika na habari hizi mara nyingi kujaribu kuonyesha ya kwamba habari nyingine hazipatani ndani ya Maandiko Matakatifu. Hapa ndani ya sura 10 iliandikwa kwamba watu *elfu makumi mbili na tatu* walikufa kwa siku moja. Ndani ya Agano la Kale hesabu *elfu makumi mbili na ine* ni hesabu ya wote waliokufa kwa muda mzima wa pigo.

10:9 Halafu Paulo alitaja ndani ya masemo yake wakati Waisraeli walipungunika juu ya vyakula, na kuonyesha shaka kama Bwana alikuwa mwema kweli. Kwa wakati ule Mungu alituma **nyoka** katikati yao, na watu wengi wa-

likufa (Hes. 21:5, 6). Hapa tena hamu kwa vyakula iliwaangusha.

10:10 Mwandishi alikumbuka habari za Kora, Datani, na Abiramu hapa (Hes. 16:14-47). Mara ile tena Waisraeli walinungunikia Bwana kwa sababu ya vyakula (Hes. 16:14). Hawakutawala na kutiisha miili yao. Waliruhusu tamaa za mwili kuwatawala, wakaangushwa.

10:11 Mashairi matatu yanayofuata yanaeleza maana ya matukio haya. Haikuwa kwa wakati ule wa zamani tu. **Yaliandikwa** kama maonyo kwa sisi tunoaishi nyuma ya muda wa Wayuda, na kwa wakati wa muda wa Habari Njema.

10:12 Ni maonyo kwa wenye kujutumainia wenyewe. **Yeye anayezania anasimama, aangalie asianguke**. Labda maonyo haya ni zaidi kwa mwamini wa nguvu anayefikiri anaweza kupima maneno haya kidogo bila kuumizwa rohoni. Mtu namna hii ni katika hatari kubwa zaidi ya kuazibowi na Mungu.

10:13 Halafu Paulo aliongeza maneno mazuri sana kusaidia roho za wengine wanaojaribiwa. Alifundisha ya kwamba **watu wote** wanashindana na taabu na mateso na majaribu. Lakini **Mungu ni mwaminifu ambaye hatuachi kujaribiwa kuliko tunavyoweza**. Haahidi kutuponyesha toka majaribu, lakini anaahidi ya kwamba hatayaacha kuwa makubwa kupita uwezo wetu kuyashinda. Na zaidi ya ile **atafanya njia ya kukimbia, ili tuweze kuyavumilia**. Bila shaka shairi hili limekuwa faraja kubwa sana kwa watu wa Mungu katika mia za miaka inayopita, waamini wa sasa, na waamini wa zamani. Labda wengine wa wasomaji wa Paulo walijaribiwa sana kuabudu sanamu. Shairi hili lingewafariji ya kwamba Mungu hataacha majaribu makubwa kupita uwezo wao kuwafikia, na kuwaonya vilevile wapeku majaribu.

10:14 Mafundisho toka shairi hili kufika 11:1 yanarudi tena kwa maneno ya nyama inayotolewa kwa sanamu. Paulo

anaanza na ulizo kama ni vizuri kwa waamini kushiriki ndani ya karamu katika mahekalu ya sanamu (mash.14-22).

Kwa sababu hii, wapenzi wangu, kimbieni kuabudu sanamu. Labda lilikuwa jaribu kubwa wakati waamini wa Korinto walipoitwa kushiriki ndani ya karamu ya sanamu ndani ya moja la mahekalu haya. Labda wengine wali-fikiri neno hili si jaribu kwao. Labda kwenda mara moja tu hakuwezi kuwa-umiza. Mtume aliongozwa na Mungu wakati alipoonya, **kimbieni kuabudu sanamu.** Hakusema, mujifunze juu yao, au kuchezacheza nayo. Iliwapasa kuzikimbia.

10:15, 16 Paulo alijua kwamba ali-kuwa akisema na wenyewe akili walioweza kufahamu maneno yake vizuri. Ndani ya shairi 16 anasema juu ya meza ya Bwana. Anasema kwanza: “**Kikombe cha baraka tunachobariki, si ushirika wa damu ya Kristo?**” **Kikombe cha baraka** ndicho **kikombe** cha mvinyo kinachotumiwa kwa Meza ya Bwana. Ni **kikombe** kinachosema juu ya **baraka** kubwa sana tuliyopokea kwa njia ya kufa kwa Kristo; kwa sababu hii kinaitwa **kikombe cha baraka**. Maana ya neno hili **tunachobariki** ni “tunacholeta asante.” Wakati tunapokunywa toka kikombe, ni kama tunasema sisi tunashiriki ndani ya faida yote inayotoka kwa damu ya Kristo.

Ni vivyo hivyo na **mkate tunaovunja** kwa meza ya Bwana. Wakati tunapokula mkate huu, ni kama tunasema sisi sote tuliolewa kwa njia ya kutolewa kwa mwili wake juu ya msalaba wa Kalvari, na kwamba kwa sababu hii sisi ni viungo vya mwili wake. Hivi kikombe na mkate inasema juu ya ushirika wetu pamoja na Kristo, na utumishi wake mtukufu kwa sisi.

Watu wameuliza kwa sababu gani damu inatajwa kwanza ndani ya shairi hili, lakini saa Meza ya Bwana iliposi-

mamishwa kwanza, ni mkate unaotajwa kwanza. Labda jibu moja ndilo ya kwa-mba Paulo alisema hapa juu ya namna maneno yanavyofuatana saa tunapo-pokewa katika ushirika wa Wakristo. Mara nyingi mwamini wa sasa anafahamu faida ya damu ya Kristo mbele ya kufahamu kweli ya mwili mmoja. Hivi labda shairi hili linaonyesha namna maneno haya yalivyofuatana.

10:17 Waamini wote **walio wengi ni mwili mmoja ndani ya Kristo.** Mkate **mmoja** ni mfano wa neno hili. **Wote wanapokea sehemu ya mkate ule mmoja**, maana wanashiriki ndani ya faida ya kutolewa kwa mwili wa Kristo.

10:18 Neno Paulo alilofundisha ndani ya mashairi haya ni ya kwamba kula kwa Meza ya Bwana kunaonyesha ushirika pamoja naye. Ilikuwa vivyo hivyo na Waisraeli waliokula **zabihu**. Walionyesha kwa njia hii ya kwamba walikuwa na ushirika na **mazabahu**. Bila shaka aliwaza juu ya sadaka ya salama. Watu walileta sadaka zao kwa hekalu. Sehemu ya sadaka iliteketewa kwa moto juu ya mazabahu; sehemu nyingine ilikuwa kwa makuhani; lakini sehemu ya tatu ilikuwa kwa mwenye kuleta sadaka hii na rafiki zake. Walikula wa sadaka hii siku ile ile. Paulo alionyesha kwamba wote waliokula ya sadaka ile walionyesha ushirika wao na Mungu, na taifa la Israeli, na maneno yote ambayo **mazabahu** ilisema juu yao.

Lakini namna gani habari hizi zinapatana na mashairi tunayojifunza sasa? Mkristo akishiriki kwa Meza ya Bwana ana upatano na Bwana, na Waisraeli wakikula sehemu ya sadaka ya salama, wanaonyesha upatano na mazabahu ya Bwana. Vivyo hivyo kula chakula kwa karamu ya sanamu hekaluni kunaonyesha upatano na sanamu.

10:19 **Basi ninasema nini? Kitu kilichotolewa sadaka kwa sanamu ni kitu, au kwamba sanamu ni kitu?**

Paulo alikuwa akisema ya kwamba nyama iliyotolewa sanamu inageuka namna nyingine? Au kwamba sanamu ni kitu cha hakika, ya kwamba kinaweza kusikia, kuona, na kina uwezo? Jibu kwa maulizo haya ni “Sivyo.”

10:20 Neno Paulo alilotaka kuonyesha wazi ni ya kwamba **vitu Mataifa wanavyotoa**, wanavitoa **kwa mashetani**. Kwa njia ya siri tusiyofahamu, kuabudu sanamu kunaungana na mashetani. Mashetani zinatumika na sanamu kutawala mioyo na nia za wale ambao wanaziabudu. Kuna Shetani mmoja, lakini kuna mashetani mengi, ndizo wajumbe wake. Paulo anaongeza: “**Sipendi ninyi kushirikiana pamoja na mashetani.**”

10:21 Hamuwezi kunywa kikombe cha Bwana na kikombe cha mashetani. Hamuwezi kushirikiana katika meza ya Bwana na katika meza ya mashetani. Ndani ya shairi hili **kipombe cha Bwana** ni mfano kuonyesha faida yote tunayopata kwa njia ya Kristo. Semo hili **meza ya Bwana** ni mfano vilevile. Lakini meza ya Bwana na chakula cha Bwana si kitu kimoja. Meza ndiyo chombo cha nyumba pahali vyakula vinapowekwa kwa watu kula na kushiriki pamoja. Ndani ya shairi hili **meza** inasema juu ya baraka zetu zote ndani ya Kristo.

Wakati Paulo aliposema kwamba **hamuwezi kunywa kikombe cha Bwana na kikombe cha mashetani**, na **hamuwezi kushirikiana katika meza ya Bwana, na meza ya mashetani**, hakuwaza kwamba neno hili haliwezekani kabisa. Ingewezekana kwa mwamini kufikia hekalu la sanamu na kushiriki ndani ya karamu pale. Lakini Paulo alitaka tufahamu kwamba neno hili halifai. Ingekuwa kutokuaminifu na hila kubwa kukiri kwamba Yesu ndiye Bwana wetu, na halafu kwenda kuwa na upatano na

wale wanaotolea sanamu zabihu. Tendo namna hii lingekuwa baya sana na lisingefaa hata kidogo.

10:22 Isingaliwezekana kufanya hihi bila **kutia Bwana vivu**. Ingepasa Mkristo kuogopa kukasirisha Bwana au kumtia uchungu. Tunawaza sisi tuna **nguvu kupita yeye?** Maana yake tunasubutu kumhuzunisha na kuamsha hukumu yake ya azabu juu yetu?

10:23 Halafu Paulo aliacha maneno ya kufundisha juu ya kushiriki ndani ya karamu za sanamu na alianza kuleta mafundisho juu ya maneno mengine yanayofaa kwa mwenendo wa kila siku ya Wakristo. Wakati aliposema **vitu vyote ni halali**, maana yake haiko ya kwamba kila kitu ni halali kabisa. Kwa maana, si halali hata kidogo kuua mtu mwingine, au kulewa! Anasema tu juu ya maneno yasiyo zambi. Kuna maneno mengine ndani ya maisha ya Mkristo yaliyo halali, lakini hata hivi si vizuri kushiriki ndani yao. Hivi Paulo alisema: “**Vitu vyote ni halali; lakini si vitu vyote vilivyo na faida.**” Kwa mfano, inawezekana kwa kitu fulani kuwa halali kwa mwamini kufanya, lakini hata hivi haifai akifanye kwa sababu ya desturi za watu wa inchi pahali anapokaa. Vitu vyote ni halali, lakini si vitu vyote vinavyojenga watu wengine ndani ya imani yao. Haifai nifanye na kiburi kitu kilicho halali kwa *mimi* kufanya, bila kukumbuka kwa njia gani ninaweza kusaidia ndugu yangu katika Kristo.

10:24 Ndani ya maneno yote tunayochagua kufanya, haifai tukumbuke tu na kiburi maneno yaliyo faida kwetu, lakini tufikiri nini itakuwa **faida** kwa jirani yetu. Ni vilevile mambo kama vyakula, mavazi, mapambo ya nyumba zetu, michezo, vivi hivi.

10:25 Mwamini akikwendea **soko** kununua **nyama**, haikuwa lazima kwa yeye kuuliza mwenye duka kama nyama

ile ilitolewa kwa sanamu mbele. Neno hili lisingaligeuza namna ya nyama, na haikukana imani yake kwa Kristo.

10:26 Kwa kueleza mafundisho haya, Paulo alitaja toka Zaburi 24:1: “**Dunia ni ya BWANA, na vyote ndani yake.**” Ni Bwana ambaye kwa neema yake alitutayarishia vyakula hivi vyote. Heinrici anatuambia ya kwamba ni desturi ya Wayuda kusema maneno haya toka Zaburi 24 kama mashukuru saa ya kula.

10:27 Halafu Paulo alifundisha juu ya neno lingine lililoweza kufazaisha mwamini. Atafanya nini kama msiyeyamini **akimwita kula** pamoja naye nyumbani mwake. Aende? Ndiyo, anaweza kwenda kama akitaka, na anaweza **kula kila kitu kinachowekwa mbele yake, pasipo kuuliza kwa sababu ya zamiri.**

10:28 Kama Mkristo mwingine ni pale vilevile, mwenye zamiri zaifu ambaye anakupasha nyama hii **ilitolewa kwa sanamu**, ni vizuri kwawe kula nyama ile? Sivyo, kwani labda ukikula, utaumiza zamiri yake. Na haifai kwa wewe kula vilevile kama kula kwako kukizuiza msiyeyamini asipokee Bwana. Kwa mwisho wa shairi hili tunasoma tena toka Zaburi 24:1: “**Dunia ni ya BWANA, na vyote ndani yake.**”

10:29 Ndani ya habari tulizosoma sasa tu, hukatazwi kula kwa sababu ya zamiri *yako mwenyewe*. Wewe, mwamini ni huru kula nyama ile. Lakini ndugu zaifu anayeketi pale, anachokozwa na zamiri yake, hivi wewe hukuli kwa sababu ya kukumbuka zamiri yake.

Tungeweza kuuliza, “**Kwa nini uhuru wangu unahukumiwa na zamiri ya mtu mwingine?**” Kipande cha nyama ni kitu kikubwa sana kwa mimi, hata kwa njia ya kukikula, mimi ni tayari kuangusha mwamini mwenza-nngu katika Kristo? (Watu wengine wanafikiri Paulo alitaja hapa ulizo la

Wakorinto, mbele ya kulijibu ndani ya mashairi yanayofuata.)

10:30 Ni kama mtume anaonesha hapa kwamba haifai **kushukuru** Mungu kwa kitu fulani pamoja na kuumiza ndugu. Ni vizuri kupita kujinyima kitu kilicho halali kwami, ambacho ningeweza kushukuru Mungu juu yake, lakini kinachoweza kuwapa watu wengine njia kusema maneno **mabaya** juu yangu kwa sababu hakikubaliwi na zamiri yao.

10:31 Kuna amri kubwa mbili kuttuongoza ndani ya maisha yetu kwa Kristo. Amri ya kwanza ni **utukufu wa Mungu**, na ya pili ni hali njema ya wenzetu. Tunaona ya kwanza ndani ya shairi hili: “**Kama mukikula au mukikunyuwa au mukifanya neno gani, fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu.**” Mara nyingi inapasa vijana Wakristo kuchagua kama ikiwapasa kufanya neno gani. Maulizo mazuri mawili ambayo inatupasa kujiuliza ni: 1) Neno hili linaleta **utukufu kwa Mungu?** 2) Ninaweza kuinamisha kichwa changu na kuomba Mungu atukuzwe kwa njia ya neno hili ninalotaka kufanya?

10:32 Neno la pili ni hali njema ya wenzetu. Haifai tufanye neno linaloweza kuangusha **Wayuda wala Wayunani wala kanisa la Mungu**. Hapa Paulo anatenga watu wote wa dunia kwa mafungu matatu. **Wayuda** ndio taifa la Israeli. **Wayunani** ni Mataifa wasionamini. **Kanisa la Mungu** ndio waamini wote wa kweli, si neno kama wao ni Wayuda au Mataifa. Ndiyo, inawezekana kwa sisi sote kukasirisha watu mara nyingine kama tukishuhudia Kristo na uaminifu, lakini hili si neno Paulo analosema juu yake hapa. Anafikiri juu ya kuangusha wengine *bila sababu* kwa njia ya namna tunavyofanya maneno yaliyo halali kwa sisi kutenda.

10:33 Paulo aliweza kusema na haki ya kwamba alijaribu **kupendeza watu wote katika maneno yote, bila kuta-**

futa faida yake mwenyewe, lakini faida ya watu wengi. Tunafikiri kuna watu wachache tu walioishi kwa faida ya watu wengine kwa kipimo cha mtume Paulo.

11:1 Shairi hili lingeweza kuwa sehemu ya mwisho wa sura 10. Paulo alikuwa ameonyesha kwamba alipima matendo yake yote kuona kama yakisaidia watu wengine. Sasa alisema na Wakorinto waweze **kumfuata** ye ye **namna** ye ye alivyoiga **Kristo**. Alijinyima maneno ambayo yaliweza kuwa ruhusa na faida kwake, aweze kusaidia watu ambaa alikaa katikati yao. Ilipasa Wakorinto kufanya vivyo hivyo, bila kujivuna juu ya uhuru wao kwa njia iliyoweza kuzuiza Habari Njema ya Kristo, au kukwalisha ndugu zaifu.

C. Juu ya vifuniko vya vichwa vya wanawake (11:2-16)

Mashairi 2-16 ya sura 11 ni juu ya vifuniko vya vichwa vya wanawake. Mashairi 17-34 ni juu ya maneno yasiyofaa kutenda kwa Meza ya Bwana. Watu wamebishana sana juu ya sehemu ya kwanza ya sura hii. Wengine wanafikiri mafundisho haya yalikuwa kwa wakati wa Paulo tu. Wengine wanasema mawazo yake yalionyesha kwamba hakupenda wanawake, na hakuo ye ye mwenyewe. Watu wengine **wanapokea** mafundisho haya, na kujaribu **kuyatii**, hata bila kuyafahamu yote.

11:2 Mtume alisifu Wakorinto kwanza kwa namna walivyomkumbuka **katika maneno yote**, na **kushika mafundisho kama alivywaletea**, ndiyo mafundisho yaliyoongozwa na Mungu.

11:3 Halafu Paulo alianza kusema juu ya vifuniko vya vichwa vya wanawake. Msingi wa mafundisho yake ni ya kwamba kila jamii ya watu inayokaa vizuri inasimama juu ya nguzo mbili – wenye mamlaka, na wale wanaopaswa kutii wenye mamlaka. Halafu alitaja

njia tatu zinazoonyesha mambo haya. Kwanza, **kichwa cha kila mwanamume ni Kristo**: Kristo ni Bwana, na mwanamume ni chini yake. Njia ya pilii, **kichwa cha mwanamke ni mwanamume**. Mwanamume amepewa pahali pa kichwa, na mwanamke ni chini ya amri yake. Njia ya tatu, **kichwa cha Kristo ni Mungu**. Hata katika Umungu, Mmoja ana mamlaka, na Mwingine anakubali pahali pa chini. Mungu ye ye mwenyewe alitengeneza maneno haya hivi, na ni msingi kwa utaratibu wake kwa ulimwengu.

Mbele ya kuendelea na maneno haya, sharti tufahamu kwamba kwa mtu kuyenyeyekea mtu mwingine *si* kuwa chini yake. Kristo alinyenyeyekea Mungu Baba, lakini hakuwa chini yake. Vivyo hivyo mwanamke si chini kupita mwanamume, hata kama anamnyenyeyekea.

11:4 **Kila mwanamume** akiomba au akitoa unabii **naye amefunikwa kichwa chake, anapatiza kichwa chake haya**, ndiye Kristo. Ni kusema mtu yule hakubali kwamba Kristo ni **kichwa chake**. Ni kuzarau, na ni ukosefu wa adabu kabisa.

11:5 **Kila mwanamke** anayeomba au anayetabiri pasipo kufunika **kichwa chake, anapatiza kichwa chake haya**, ndiye mwanamume. Ni kama hakubali kwamba Mungu aliweka mwanamume kuwa kichwa chake na anakataa kumnyenyeyekea.

Kama shairi hili lingalikuwa shairi la pekee ndani ya Biblia juu ya neno hili, tungeweza kufikiri ya kwamba ni vizuri kwa mwanamke kuomba au kutabiri kanisani¹⁴ kama akiwa na kifuniko juu ya kichwa chake. Lakini Paulo alifundisha pahali pengine kwamba inapasa wanawake kukaa kimya kanisani (1 Kor. 14:34), ya kwamba hawana ruhusa kufundisha au kuwa na amri juu ya mwanamume, lakini wanapaswa kukaa kimya (1 Tim. 2:12).

Kwa kweli, shairi hili ni gumu. Neno

moja lililo wazi ndilo ya kwamba kwa maneno ya kufunika kichwa, daraka la mwanamke ni mbalimbali na ile ya mwanamume. Ni taratibu kwa kichwa cha mwanamke *kufunika* na *haipasi* kwa kichwa cha mwanamume kufunika wakati maombi na kutabiri.

11:6 Kama kichwa cha mwanamke kisipofunikwa, nyele zake zikatwe vilevile. Lakini kama ikiwa haya kwa mwanamke kukata au kunyoa nyole zake, afunikwe. Kichwa cha mwanaamke kisichofunikwa, na kichwa kilicho-nyolewa ni haya.

11:7 Ndani ya mashairi 7-10, Paulo alirudi kwa kuumbwa kwa mwanamume na mwanamke kwa mwanzo wa dunia kufundisha kwamba hali ya mwanamke ni chini ya mwanamume. Mafundisho haya yananyamazisha masemo ya watu wengine ya kwamba ni mafundisho kwa wakati wa ule tu, na si kwa watu wa wakati wa sasa. Ni utaratibu uliosimamishwa na Mungu tangu mwanzo kwa mwanamume kuwa kichwa cha mwanamke, na hali ya mwanamke kuwa chini ya mwanamume.

Mwanamume ni **mfano wa utukufu wa Mungu**, lakini **mwanamke ni utukufu wa mwanamume**. Maana ya neno hili ni ya kwamba mwanamume aliwekwa duniani kuwa mjambe wa Mungu, na kuitawala. Kichwa cha mwanamume kisichofunikwa ni ushuhuda kimya wa neno hili. Mwanamke hakupewa pahali pa kichwa, lakini yeze ni **utukufu wa mwanamume**, maana yake “anafanyiza amri ya mwanamume kuonekana,” kama W. E. Vine alivyo-sema.

Haifai kwa mwanamume kufunika kichwa chake wakati wa maombi, kwani akifunika kichwa chake, ni kama anaficha **utukufu wa Mungu**, na kuza-rau Enzi yake.

11:8 Halafu Paulo alitukumbusha kwamba **mwanamume hakuumbwa**

toka mwanamke, lakini mwanamke aliumbwaa **toka mwanamume**. Mwanamume aliumbwaa kwanza, kisha mwanamke alikamatwa toka ubavu wa mwanamume. Neno hili linasimamisha vilevile mafundisho ya Paulo juu ya ukuu wa mwanamume.

11:9 Halafu tunaona kwa sababu gani mwanamume na mwanamke waliumbwaa. **Mwanamume hakuumbwa kwa ajili ya mwanamke, lakini mwanamke kwa ajili ya mwanamume.** Bwana alisema wazi kwa Mwanzo 2:18, “Si vema mtu awe peke yake; nitamfanyia msaidia anayefaa kwake.”

11:10 Kwa sababu daraja la mwanamke ni chini ya mwanamume, **inampasa kuwa na alama ya utii kwa kichwa chake.** Ni alama ya kwamba mwanamke ni chini ya amri ya mume wake.

Kwa sababu gani Paulo aliongeza **kwa ajili ya malaika?** Tunafikiri **malaika** wanaangalia maneno yanayotokea duniani sasa, namna walivyo-fanya wakati wa kuumbwa kwa dunia. Wakati dunia ilipoumbwa, waliona namna mwanamke alijitwalia ujumbe juu ya mwanamume. Alifanya neno ambalo lingalipasa Adamu tu kuchagua kufanya. Kwa njia hii zambi iliingia ujamaa wa watu wa dunia, na kuzaa taabu na mau-mivu kupita kipimo. Mungu hataki maneno yaliyotokea wakati dunia ilipoumbwa mara ya kwanza kutokea tena katika uumbo mpya. Wakati malaika wanapoangalia sasa, Mungu anataka waone mwanamke akitii mwanamume, na akionyesha neno hili kwa njia ya kufunika kichwa chake.

Ni vizuri tufahamu ya kwamba kifuniko cha kichwa ni alama ya kuonekana kwa macho tu. Kina faida tu kama kin-aonyesha roho ya utii ya mwenye kuki-vaa. Inawezekana kwa mwanamke kufunika kichwa chake bila kunyenyeka mume wake rohoni. Kama ni hivi, kifuniko chake cha kichwa ni bure

kabisa. Hakina faida hata kidogo. Neno kubwa zaidi ni kuwa na roho ya utii ya kweli; halafu kifuniko cha mwanamke kichwani kina maana ya kweli.

11:11 Paulo hasemi kwamba mwana-mume hana hitaji la mwanamke, hivi anaongeza: “**Mwanamume si pasipo mwanamke, wala mwanamke si pasipo mwanamume, katika Bwana.**” Ni kusema, mwanamume na mwanamke wanahitajiana, hata kama mmoja wao ni mwenye kutii.

11:12 Mwanamke alitoka kwa mwanamume kwa wakati wa kuumbwa, maana aliumbwu toka ubavu wa Adamu. Lakini Paulo alionyesha kwamba **mwanamume anazaliwa vilevile na mwanamke.** Mwanamke anazaa mtoto mume. Mungu aliweka utaratibu huu kuonyesha kwamba mmoja hawezi kuwa bila mwingine.

Vitu vyote vimetoka kwa Mungu, maana ni yeye aliyetayarisha **vitu** hivi **vyote**, hivi hakuna sababu kwa kununguni. Ni Mungu aliyesimamisha maneno haya yote, na yote ni kwa utukufu wake. Ingepasa mwanamume kuwa na unyenyekevu na mwanamke kukaa na utulivu.

11:13 Halafu Paulo alisema na Wakorinto **kuhukumu** wao wenyewe kama ni **vizuri kwa mwanamke kuomba Mungu pasipo kufunika kichwa chake.** Si heshima wala adabu kwa mwanamke kutokea mbele ya Mungu bila kufunika kichwa chake.

11:14 Haionekani wazi namna gani **asili yenye** inatufundisha kwamba ni haya kwa **mwanamume** kuwa na **nyole ndefu**. Watu wengine wanasema nyole za wanaume hazioti kuwa ndefu kama zile za wanawake. Nyole ndefu zinafanyaiza mwanamume kuonekana kama mwanamke. Wanaume wa zaidi ya makabila wana nyole fupi kupita zile za wanawake.

11:15 Watu wengi hawafahamu shairi hili **vizuri**. Wengine wanafikiri ya kwa-

mba mwanamke **akipewa nyole ndefu kuwa kifuniko**, hahitaji kifuniko kingine. Lakini mawazo haya hayafai hata kidogo. Sharti tufahamu kwamba kuna vifuniko *viwili* ndani ya sura hii. Kwa mfano wa neno hili soma tena shairi 6 la sura hii. Pale tunasoma “kama kichwa cha mwanamke kisipofunika, nyole zake zikatwe vilevile.” Kupatana na mawazo ya watu wale kwa mwanzo wa shairi 15, shairi 6 lingesema kama mwanamke “asipovaa nyole zake,” vizuri nyole zake zikatwe. Kusema hivi ni neno la kuchekesha. Kama mwanamke “asipovaa nyole zake,” nyole zake zinaweza kukatwa namna gani!

Kwa asili Mungu alimpa mwanamke kifuniko cha **utukufu** namna asichompa mwanamume. Neno hili lina maana ya roho kwa sisi. Linatufundisha ya kwamba wakati mwanamke anapoomba Mungu, inampasa kufunika kichwa chake. Jambo la hakika kwa maneno ya asili linapaswa kuwa jambo la hakika kwa maneno ya roho vilevile.

11:16 Paulo alimaliza fungu hili akisema: “**Lakini kama mtu akitaka kuleta fitina, sisi hatuna desturi kama hii, wala makanisa ya Mungu.**” Watu walijaribu kueleza masemo haya kwa njia mbalimbali yasiyo taratibu, lakini zinazokubaliwa na watu wengine.

Kuna maelezo mazuri mawili au zaidi yanayokubaliwa na mafundisho ya baki la Maandiko Matakatifu. Ni kama Paulo alifikiri kwamba **kutakuwa na fitina** juu ya mafundisho haya, hivi alisema **hatuna desturi kama hii**, maana desturi ya kubishana namna hii. Elezo lingine lililokubaliwa na William Kelly, ndilo ya kwamba **makanisa ya Mungu** hawa-kuwa na desturi kwa wanawake kuomba au kutabiri bila kufunika vichwa vyao.

D. Juu ya Meza ya Bwana

(11:17-34)

11:17 Mtume alihamakia Wakorinto kwa sababu kulikuwa na mitengo

katikati yao wakati walipokusanyika (mash. 17-19). Tunasoma maneno haya “wakati munapokusanyika” au maneno mengine namna hii tena na tena, Ona mashairi 17, 18, 20, 33, 34; 14:23, 26. Katika 11:2 Paulo aliweza kuwasifu kwa sababu walikuwa wameshika ma-fundisho yake, lakini kulikuwa na neno moja ambalo **hakuweza kuwasifu** juu yake. Walikusanyika, **si kwa faida, lakini kwa hasara.** Maneno haya ni maonyo kwetu sisi sote ya kwamba inawezekana kwetu kutoka kanisa kwa mwisho wa kusanyiko, nyuma ya kupata hasara pahali pa baraka rohoni.

11:18 Neno la **kwanza** ambalo ali-wahamakia juu yake lilikuwa **matengo** yaliyokuwa katikati yao. Si kusema ya kwamba wengine walikuwa wame-ondokea kanisa na kuanza makusanyiko mengine, lakini kulikuwa na jamii ndogo za watu kanisani waliokuwa na urafiki sana. Haikuwa nguvu kwa Paulo **kuamini** habari hizi kwa sababu alijua Wakorinto hawakutembea karibu na Bwana. Ilimpasa kuwakemea mbele juu ya matengo.

11:19 Paulo alifahamu ya kwamba jamii zilizokwisha kuanza katika Korinto zitakaa kuongezeka na kugeuka hatari. Neno hili litaumiza kanisa, lakini litazaa neno zuri moja. Litafunua wale **waliokubaliwa** na Bwana na **kuone-kana** katikati ya Wakorinto. Wakati Paulo aliposema ndani ya shairi hili: “**sharti matengo yawe katikati yenu,**” maana yake haiko kwamba ilikuwa lazima kwa matengo haya kutokeea. Mungu hakubali matengo kanisani. Maana ya masemo ya Paulo hapa ni ya kwamba kwa sababu ya baridi ya roho zao ilikuwa sharti kwa **matengo** haya kutokeea. **Matengo** yanahakikisha kwa-mba watu wengine hawakutambua nia ya Bwana.

11:20 Halafu Paulo aliwakemea juu ya maneno yasiyofaa wakati walipokusanyika kwa **Meza ya Bwana.** Matendo

yao yalikuwa mabaya sana hata haikuwezekana kwa kukumbuka Bwana namna alivyoamuru. Hata kama matendo yao yalionekana vizuri, hayaku-patana na hali ya roho zao.

11:21 Kwa wakati wa mwanzo wa kanisa Wakristo walikula “agape,” ndiyo karamu ya mapendo, pamoja na Meza ya Bwana. Kwa karamu hii ya mapendo Wakristo walikula na kushiriki pamoja na roho ya mapendo. Mara nyingi kwa mwisho wa karamu hii walikumbuka Bwana na kuvunja mkate na kunywa mvinyo. Lakini nyuma kidogo desturi mbaya ziliingia, na shairi hili linaonyesha kwamba nyuma ya wakati maana yake ya mapendo ilipotea. Wakristo tajiri walianza kuleta vyakula vingi na vizuri bila kuvishiriki na wengine, na kupatisha ndugu zao masikini haya. Wengine walikwenda zao **na njaa**, na wengine **walilewa!** Kwa sababu Meza ya Bwana ilifuata karamu ya mapendo mara nyingi, wangkuwa wangali waki-lewa wakati walipoketi kushiriki Meza ya Bwana.

11:22 Mtume aliwahamakia na hasira juu ya matendo yao mabaya. Kama wa-kitaka kukaa kutenda namna hii, haifai kufanya hivi **kanisani.** Kulewa kwa wakati wa namna hii na **kuhayarisha** ndugu wamasikini hakupatani hata ki-dogo na imani ya Wakristo. Kwa njia ya **kutosifu** waamini kwa sababu ya ku-tenda hivi, anawahukumu na nguvu.

11:23 Kwa kuonyesha tofauti ya matendo yao na maana ya kweli ya Meza ya Bwana alirudi tena kuwakumbusha kwa wakati Meza hii iliposimamishwa. Alionyesha kwamba haikuwa saa kwa watu kula pamoja tu, au karamu, lakini agizo la ibada toka Bwana. Paulo **ali-pokea** maneno haya **toka Bwana** mwenyewe. Alitaja neno hili kuonyesha kwamba kutokufanya hivi kulikuwa kuasi. Maneno aliyofundisha yalifu-nuliwa kwake na Mungu.

Kwanza alitaja kwamba **Bwana Yesu**

usiku ule **aliotolewa alitwaa mkate**. Wakati watu wabaya inje ya nyumba walipokuwa wakitaryarisha shauri lao ovu kumtoa kwa adui zake, **Bwana Yesu** alikuwa akikusanyika na wana-funzi wake na **alitwaa mkate**.

Ulikuwa usiku, lakini maana ya neno hili si kwamba ilipasa kula Meza ya Bwana usiku tu. Kwa wakati ule mangaribi yaliwu mwanzo wa siku nyingine kwa Wayuda. Siku yetu inaanza na mapambazuko. Vizuri tufahamu vilevile kwamba kuna tofauti katika maneno mitume *waliyofanya* wao wenyewe na maneno *waliyofundisha*. Si lazima kwa sisi *kufanya* maneno yote mitume *waliyofanya*, lakini ni sharti kwa sisi kutii maneno yote *waliyofundisha*.

11:24 Bwana Yesu alitwaa mkate kwanza, na **kushukuru**. Mkate huu ulikuwa mfano wa mwili wake, hivi alishukuru Mungu kwa mwili wa mtu aliopewa ili aweze kuja na kufa kwa zambi za dunia.

Wakati Mwokozi aliposema, “**Huu ni mwili wangu**,” alikuwa akisema kwamba mkate huu *uligeuka* mwili wake? Kanisa Katoliki linafundisha kwamba mkate na mvinyo zinageuzwa kuwa mwili na damu ya Kristo. Kanisa la Luther linafundisha kwamba mwili na damu ya Kristo ni ndani ya, pamoja na, na chini ya mkate na mvinyo juu ya meza.

Kujibu mawazo haya, inapasa tukumbuke ya kwamba wakati Bwana Yesu aliposimamisha ukumbusho huu, mwili wake ulikuwa haukutolewa bado, na damu yake haikumwangika. Wakati Bwana Yesu aliposema, “**Huu ni mwili wangu**,” alikuwa akisema, “Huu ni mfano wa mwili wangu uliovunjika kwa ajili yenu.” Kula mkate ni kukumbuka kufa kwake kwa upatanisho kwa sisi. Aliongeza kusema na mapendo na huruma “kwa kunikumbuka mimi.”

11:25 Vivyo hivyo Bwana Yesu **ali-twaa kikombe nyuma ya kula karamu ya Pasaka, akisema:** “Kikombe hiki ni agano jipyka katika damu yangu; fanyeni hivi, kila mara munapokunyuwa kwa kunikumbuka mimi.” Ukumbusho wa Bwana ulisimamishwa mara moja nyuma ya karamu ya Pasaka. Kwa sababu hii tunasoma Bwana Yesu **alitwaa kikombe nyuma ya kula**. Juu ya **kikombe** alisema kikombe hiki ni **agano jipyka katika damu** yake. Agano jipyka hili ndilo agano Mungu aliloagiza kwa taifa la Israeli katika Yeremia 31:31-34. Lilikuwa agano bila masharti, kwa njia yake alikubali kuwa na rehema kwa uzalimu wao, na kutokukumbuka zambi na uovu wao tena. Tunasoma juu ya agano jipyka hili katika Waebrania 8:10-12 vilevile. Linasimama kwa wakati wa sasa, lakini kwa sababu ya kutokuamini kwao taifa la Israeli halifurahiwi nalo. Wote wanaoamini Bwana Yesu wanapokea faida yake. Wakati Waisraeli watakaporudi kwa Bwana, watafurahia baraka za agano jipyka, kwa wakati wa utawala wa Kristo kwa miaka elfu moja duniani. **Agano jipyka** lilisibitishwa na **damu** ya Kristo, na kwa sababu hii anasema juu yake kama **kikombe cha agano jipyka katika damu** yake. Msingi wa agano jipyka uliwekwa kwa njia ya msalaba.

11:26 Shairi hili linatufikirisha kama ikitupasa kushika Ukumbusho wa Bwana mara ngapi. **Kila mara munapokula . . . na kunywa . . .** Hakuna agizo kwamba inatupasa kukutana mara ngapi. Ni kama Matendo 20:7 linaonyesha kwamba ilikuwa desturi ya wanafunzi kukutana siku ya kwanza ya juma kukumbuka Bwana. Masemo haya **hata atakapokuja** yanaonyesha wazi ya kwamba ukumbusho huu haukuwa kwa wakati wa mwanzo tu wa kanisa.

Ndani ya mafundisho haya yote hatu-somi hata neno moja juu ya kuongozwa kwa makusanyiko na kuhani au padre.

Ni kusanyiko kwa watu wote wa Mungu. Wakristo wanakusanyika kama waamini-makuhanu kutangaza kwa njia hii mauti ya Kristo **hata atakapokuja**.

11:27 Nyuma ya kufundisha juu ya mwanzo na kusudi la ukumbusho wa Bwana, mtume anaonyesha tunda la kushiriki ndani yake kwa njia isiyofaa. Kila **mwenye kula mkate huu na kunywa kikombe cha Bwana isivyostahili, atakuwa amejipatia kosa juu ya mwili na damu ya Bwana**. Sisi sote hatustahili kushiriki ndani ya ukumbusho wa ibada hii. Ndiyo, hatustahili wema na rehema yo yote ya Bwana. Lakini Bwana hasemi hapa juu ya kutokustahili kwetu wenyewe. Tumesafishwa na damu ya Kristo, hivi tunaweza kukaribia Mungu ndani ya ustahili wa Mwana wake mpendwa. Lakini Paulo alisema hapa juu ya mwenendo wa aibu wa Wakorinto wakati walipokusanyika kwa Meza ya Bwana. Walitenda namna isivyofaa, na kwa njia hii **walijipatia kosa juu ya mwili na damu ya Bwana**.

11:28 Sharti tujihukumu wenyewe mbele ya kufikia Meza ya Bwana. Sharti tukiri zambi zetu na kuziacha, turudishie mtu kitu tusichokuwa na ruhusa kumamata, kuomba usamehe karibu na wale ambaao tuliumiza na masemo. Inapasa tuwe wenye roho safi mbele ya Mungu.

11:29 Mtu akikula na kunywa bila kujihukumu kwanza na bila roho iliyo-safishwa, anakula na kunywa **hukumu kwake mwenyewe, asipotambua mwili wa Bwana**. Tufahamu kwamba mwili wa Bwana ulitolewa ili zambi zetu ziweze kuondoshwa. Kama tukikaa kuttenda zambi, pamoja na kula Meza ya Bwana, tunaishi maisha ya uwongo. F. G. Patterson aliandika, “Tukikula kwa Meza ya Bwana pamoja na zambi tuisiyokiri, hatutambui mwili wa Bwana uliovunjwa kuondosha zambi hii.”

11:30 Ilipasa Mungu kuazibu na kuhukumu wengine katika kanisa la Korinto kwa sababu hawakujihukumu we-

nyewe. **Wengi wao walikuwa zaifu na wagonjwa**, na wengi wamelala, maana walikufa na kupelekwa mbinguni. Hawakuhukumu zambi ndani ya maisha yao, hivi ilipasa Mungu kuwaazibu.

11:31 Lakini kama tukijihukumu **sisi wenyewe**, hatutahukumiwa.

11:32 Mungu anatutendea sisi kama watoto wake wenyewe. Kwa sababu anatupenda sana hawezi kukubali kwa sisi kuendelea ndani ya zambi. Nyuma ya muda mdogo tu atatuazibu na mapendo kuturudisha karibu naye. Mtu mmoja alisema kwamba “Inawezekana kwa Mkristo kuwa tayari kwa mbingu (kwa sababu yeeye ni ndani ya Kristo) lakini hastahili kubaki duniani kuwa mshuhuda mwema kwa sababu ya mwendendo wake mbaya.”

11:33 **Wakati** waamini **wanapuktana** kwa agape, ndiyo karamu ya mapendo, ingewapasa **kungojeana**. Haifai waanze kula mara moja bila kungojea waamini wengine, kama waamini walivyofanya ndani ya shairi 21.

11:34 **Mtu akipata njaa, ale nyumbani mwake**. Karamu hii ya mapendo, iliyofungana na ukumbusho wa Bwana, haikuwa sawasawa na chakula cho chote. Sharti wakumbuke kwamba ni chakula kitakatifu, ili **wasikutanike pamoja kwa hukumu**.

Bila shaka Wakorinto waliuliza mtume juu ya maneno mengine vilevile ndani ya barua yao. Halafu Paulo alisema atatengeneza maneno yale **wakati atakapokuja** kuwaona.

E. Juu ya zawadi za Roho na kazi yao kanisani (Sura 12-14)

Sura 12-14 zinafundisha juu ya zawadi za Roho. Waamini katika kanisa kwa Korinto hawakutumika vizuri na zawadi hizi, zaidi na zawadi ya kusema kwa lugha. Hivi Paulo alifundisha juu ya neno hili sasa.

Waamini wengine wa Korinto wali-kuwa wamepewa zawadi ya kusema na

lughu, ndio uwezo wa kusema kwa lugha nyingine wasizojifunza mbele.⁴³ Lakini kwa pahali pa kutumika na zawadi hii kutukuza Mungu na kujenga waamini katika imani, walitumika nayo kwa kuji-tukuza wenyewe. Walisimama ndani ya makusanyiko ya waamini na kusema kwa lugha watu wengine wasizoweza kufahamu. Walitaraji watu wengine watawasifu juu ya kuweza kufanya hivi. Walitkuza zawadi za kuonekana mbele ya watu kupita zawadi nyingine, na walfikiri kwamba wenyewe kusema kwa lugha walitembea karibu zaidi na Mungu. Mawazo haya yalizaa kiburi ndani ya roho zao, na wivu rohoni mwa wengine waliowaza hawana faida wao wenyewe. Ilipasa mtume kutoa mafundisho kuonyesha ubaya wa mafikiri haya, na namna gani iliwapasa kutumika na zawadi hizi, zaidi zawadi za kusema kwa lugha na kutabiri.

12:1 Paulo **hakutaka** watakatifu **ku-kosa ufahamu** juu ya kuonekana kwa zawadi **za roho**. Labda aliwaza juu ya pepo wachafu vilevile.

12:2 Mbele ya kuokolewa kwaao Wakorinto waliabudu sanamu na walikuwa watumwa wa pepo wachafu. Waliogopa pepo hizi na **kuongozwa** nazo. Waliona maneno yasiyokuwa ya ulimwengu na kusikia maneno yaliyoongozwa na pepo. Mara nyingine, wakiongozwa na pepo wachafu, wakajitoa kutawaliwa nao, na walisema na kufanya maneno bila kujua.

12:3 Lakini sasa walikuwa waamini, na iliwapasa kuweza kutambua manyesho yote ya roho, kama ni masemo ya pepo wachafu, au sauti ya Roho Mtakatifu. Kama mtu akisema, “**Yesu amelaaniwa**,” tunajua hakika kwamba ameongozwa na pepo mchafu, kwa sababu ni desturi ya pepo wachafu kutukana na kulaani jina la Yesu. **Roho ya Mungu** hataongoza mtu ye yote kusema hivi juu ya Mwokozi. Kazi ya Roho Mtakatifu ni kutukuza Bwana Yesu. Anaongoza watu **kusema** ya kwamba

Yesu ni Bwana, si na midomo yao tu, lakini kukiri hivi na miyo na maisha yao.

Ona vilevile ya kwamba ndani ya shairi 3, na ndani ya mashairi 4-6 vilevile Mungu Baba, Mwana na Roho Mtakatifu wanatajwa wote watatu.

12:4 Paulo alionyesha ya kwamba hata kuna **zawadi mbalimbali** za Roho Mtakatifu ndani ya kanisa, kuna umoja wa Umungu, ndio Mungu Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu.

Kwanza, kuna zawadi mbalimbali, lakini Roho ni moja. Wakorinto walitenda sawasawa kulikuwa na zawadi *moja* tu – ndiyo zawadi ya kusema na lugha. Paulo alisema, “Sivyo, hamuna umoja kwa sababu ninyi wote pamoja muna zawadi *moja*, lakini kwa sababu muna Roho Mtakatifu, mwenye kutoa zawadi *zote*.”

12:5 Halafu Paulo anaonyesha kwamba kuna **utumishi mbalimbali** kansi. Sisi sote tuna kazi mbalimbali. Lakini tunashiriki ndani ya neno moja, ndilo hili: kazi yo yote tunayofanya tunafanya kwa **Bwana mmoja** na tunatumikia watu wengine (hapana sisi wetenye).

12:6 Na vilevile kuna **kazi mbalimbali** kwa njia ya zawadi za roho, lakini ni **Mungu mmoja** anayewezesha kila mwamini. Labda zawadi moja inaonekana kuwa nzuri kupita na ya uwezo kupita, lakini neno hili si kwa sababu mwenye zawadi hii ni mzuri kupita watu wengine. Ni Mungu anayetoa uwezo kwa kazi hizi zote.

12:7 Roho anajifunua ndani ya maisha ya **kila** mwamini kwa njia ya kumtolea zawadi. Hakuna mwamini anayekosa kazi ambayo inampasa kufanya. Na zawadi hizi ni **kwa faida ya mwili** mzima, ndio waamini wote. Si kusudi kwa mwenye zawadi kujivuna juu yake, lakini kusaidia watu wengine. Hili ndilo neno kubwa la mafundisho haya.

Halafu tuone nyingine za zawadi za Roho.

12:8 Neno la akili ni uwezo usio wa dunia kusema na hekima toka Mungu, kukata mambo magumu, kusimamia imani, kutoa shauri kuleta salama kwa pahali pa mashindano, kuleta maonyo, au kujisimamia mbele ya serikali wenyewe uadui. Tunaona neno hili ndani ya maisha ya Stefano aliyekuwa na roho ya akili hata adui zake “hawakuweza kushindana na hekima yake wala na Roho Mtakatifu aliyesema naye” (Matendo 6:10).

Neno la kujuua ni uwezo kutangaza habari zilizofunuliwa na Mungu. Tunaona neno hili ndani ya maisha ya Paulo wakati aliposema maneno kama haya: “Tazameni, ninawaambia ninyi siri” (1 Kor. 15:51), na “Kwa sababu tunawaambia ninyi hili kwa neno la Mungu” (1 Tes. 4:15). Hatuna zawadi yenyewe maana hii sasa, kwa sababu watakatifu walipewa imani mara moja tu (Yuda 3). Jumla la mafundisho ya Ukristo limekamilishwa. Lakini ni kama **neno la kujuua** lenye maana nyingine ni pamoa nasi hata sasa. Ni kama Mungu anajulisha maneno ya siri kwa wale wanaokaa na upatano wa karibu na Bwana (Zab. 25:14). Kujulisha maneno haya na watu wengine ndilo **neno la kujuua**.

12:9 Zawadi ya **imani** ni uwezo toka Mungu kuondosha mambo magumu yaliyo kama milima wakati tunapojaribu kufanya mapenzi ya Mungu (13:2), na kufanya kazi kubwa kwa Mungu kwa sababu ya agizo au ahadi fulani ndani ya Neno la Mungu. George Müller ni mfano wa mwenye zawadi ya imani. Bila kujulisha mahitaji ya kazi yake kwa mtu ye yote ila Mungu, alichunga yatima 10.000 kwa muda wa miaka 60.

Zawadi ya kuponyesha ni uwezo wa ajabu kuponyesha gonywa.

12:10 Mengine za **matendo ya uwezo** yalikuwa kutoa pepo wachafu toka watu, kufufua wafu, na kutawala tufani, na machafuko ya bahari. Filipo alifanya

maajabu kwa Samaria, na kwa njia hii watu walikuwa tayari kusikia Habari Njema (Matendo 8:6-7).

Zawadi ya **unabii** ilipewa kwa mtu aliyepokea funuo toka Mungu na kuzipitisha kwa watu wengine. Mara nyingine manabii walitabiri maneno yatakayotokea nyuma (Mdo. 11:27, 28; 21:11); lakini zaidi walijulisha mawazo ya Mungu. Kama mitume, waliweka roho juu ya kuweka msingi wa kanisa (Efe. 2:20). Wao wenyewe hawakuwa msingi, lakini waliweka msingi kwa njia ya kufundisha juu ya Bwana Yesu. Nyuma ya kuwekwa kwa msingi, hitaji kwa manabii lilikwisha. Tunabaki na kazi yao ndani ya maandiko ya Agano Jipy. Biblia imetimia sasa, hivi tunakataa mafundisho ya mtu ye yote ambaye anajiita nabii na anayesema analeta kweli nyingine toka Mungu kupita kweli iliyoufunuliwa ndani ya Maandiko.

Sasa mtu ye yote anayetangaza neno la Mungu na amri na uwezo anaitwa “nabii” vilevile. Unabii unaweza kuwa sifa kwa Mungu vilevile (Lk. 1:67, 68), na neno la kutia moyo, na kupatisha watu wa Mungu nguvu (Mdo. 15:32).

Kutambua roho ni uwezo kutambua kama nabii au mtu mwininge anasema kwa uwezo wa Mungu au Shetani. Mwenye kuweza kutambua roho anaweza kufahamu kama mtu ni mdanganyi. Hivi Petro aliweza kuonyesha ya kama Simoni alikuwa mwenye uchungu wa nyongo, na katika kifungo cha uovu (Mdo. 8:20-23).

Kama tulivyoonyesha mbele, zawadi ya **lugha** ni uwezo wa kusema na lugha nyingine bila kujifunza lugha hii mbele. Lugha zilikuwa alama zaidi kwa Israeli.

Kueleza maana ya lugha kulikuwa uwezo wa ajabu kwa mtu kufahamu lugha asiyojua mbele na kuitafsiri kwa lugha ya watu ambao alikaa katikati yao.

Ona ya kwamba ndani ya mashairi haya tunasoma kwanza juu ya zawadi za

akili, na kwa mwisho tunasoma juu ya zawadi za roho. Lakini Wakorinto waliweka zawadi za roho kwanza. Hivi walitakuza zawadi ya lugha kupita zawadi zote nyingine. Ni kama walifikiri kwamba mtu akiwa na sehemu kubwa ya Roho Mtakatifu, nguvu hii itamtawala kupita nguvu yake ya umtu. Hawakufahamu kwamba nguvu ile haikuwa uwezo wa Roho.

12:11 Roho huyu mmoja ndiye ali-yetoe na kutawala zawadi zote tulizosoma juu yao ndani ya mashairi 8-10. Hapa tunaona tena ya kwamba anatoa zawadi mbalimbali kwa watu mbalimbali. Anagawia **kila mtu peke yake kama anavyopenda**. Neno hili ni neno kubwa vilevile – Roho Mtakatifu kwa enzi yake anagawa zawadi. Kama tukifahamu neno hili kwelikweli, hatutakuwa na kiburi kwa sababu ya zawadi hii. Wala hatutanungunika kwa sababu Mwenye Hekima na Mapendo bila mpaka alichagua kama ilitupasa kupata zawadi gani. Ingekuwa vibaya kwa kila mtu kutamani zawadi fulani moja.

12:12 Mwili wa mtu ni mfano mzuri wa umoja pamoja na tofauti. **Mwili ni mmoja**, lakini **una viungo vingi**. Waamini wote ni mbalimbali na wanafanya kazi namna namna, lakini wao wote pamoja wanafanya pamoja kuwa mwili mmoja – ndio **mwili**.

Vivyo hivyo na Kristo. Hapa hatusomi tu juu ya Bwana Yesu Kristo aliyetukuzwa mbinguni, lakini juu ya Kichwa aliye mbinguni na viungo vyake hapa duniani. Waamini wote ni viungo vya Mwili wa Kristo. Kwa njia ya mwili wake, mtu anaonyeshea mtu mwagine mawazo na kutaka kwake. Vivyo hivyo Kristo anatumika na Mwili wake hapa duniani kujionyesha kwa ulimwengu.

12:13 Paulo anaendelea kueleza namna gani tuligeuka viungo vya Mwili wa Kristo. **Katika Roho mmoja sisi sote tulibatizwa katika mwili mmoja**. Labda maana yake ni ya kama tunaba-

tizwa ndani ya Roho namna mwamini anavyobatizwa ndani ya maji. Au labda mwenye kubatiza ni Roho, hivi tunasoma **katika Roho mmoja**. Tunafikiri hii ndiyo maana ambayo inatupasa kufahamu.

Ubatizo wa Roho Mtakatifu ultokea siku ya Pentekote. Kanisa lilizaliwa kwa wakati ule. Tunashiriki ndani ya faida ya ubatizo ule wakati tunapozaliwa tena. Tunageuka viungo vya **Mwili** wa Kristo.

Tuone maneno makubwa mengine hapa. Kwanza inatupasa tujue kwamba ubatizo wa Roho Mtakatifu ni kazi ya Mungu inayoweka waamini ndani ya Mwili wa Kristo. Matayo 3:11; Yoane 1:33; na Matendo 1:5 yanaonyesha wazi kwamba si ubatizo ndani ya maji. Si kazi ya neema nyuma ya wokovu wakati waamini wanapogeuka watu wa roho kupita. Wakorinto **wote** walikuwa **wamebatizwa** katika Roho, lakini Paulo aliwahamakia kwa sababu hawakuwa kama watu wa Roho, lakini kama watu wa mwili (3:1). Kusema na lugha *si* alama kila mara ya kwamba mtu fulani alibatizwa kwa Roho. Wakorinto **wote** walikuwa **wamebatizwa**, lakini si wote walisema na lugha (12:30). Inawezekana mara moja moja kwa wakati wa tukio la hatari ya gafula kwa mwamini kujitoa kutawaliwa na Roho na kupewa uwezo toka mbingu. Tukio namna hii ni *namna nyingine* na ubatizo wa Roho.

Shairi hili linaendelea kusema kwa mba **waamini wote walikunyweshwa katika Roho mmoja**. Ni kusema wao wote wanashiriki katika Roho ya Mungu kwani wanapokea kukaa ndani yao na wanapokea faida ya utumishi wake katika maisha yao.

12:14 Huwezi kuwa na **mwili** wa mtu bila viungo mbalimbali. Lazima viungo viwe **vingi**, kila kiungo kikiwa namna nyingine na viungo vingine, na kila kiungo kikitii kichwa na kukitumika pamoja na vingine.

12:15 Kufahamu kwamba viungo

mbalimbali vinahitajiwa ndani ya mwili wenyewe afya, kunatuzuiza tusianguke kwa njia mbili – tusifikiri sisi wenywewe hatuna faida (mash. 15-20), na tusifikiri watu wengine hawana faida (mash. 21-25). Ingekuwa pumbavu kwa **mguu** kufikiri hauna faida kwa sababu hauwezi kufanya kazi ya **mkono**. Kumbuka kwamba mguu unaweza kusimama, kutembea, kukimbia, kupanda, kucheza, na maneno mengi mengine.

12:16 Haifai **sikio** kujaribu kukataa kufanya kazi kwa sababu **si jicho**. Mara nyingi hatukumbuki faida ya masikio yetu kufika wakati uwezo wetu wa kusikia unapoanza kupunguka. Halafu tunafahamu kwamba masikio yanafanya kazi kubwa.

12:17 Kama mwili mzima ukiwa jicho, ungekuwa kitu cha kuchekesha watu. Au mwili ukiwa na masikio tu, bila pua, usingeweza kusikia, wala kunusa hewa mbaya inayoingia nyumba.

Neno kubwa ambalo Paulo alitaka Wakorinto kufahamu ni ya kama mwili ukiwa ulimi tu, mwili huu ungekuwa ki-umbe kigeni na kitu cha kutia hofu tu. Lakini Wakorinto waliweka roho kupita kipimo juu ya zawadi ya kusema na lugha na kusimamisha kanisa lililokuwa *ulimi* tu. Liliweza kusema tu, lakini halikuweza kufanya kazi nyingine.

12:18 Mungu hakutenda na upumbavu namna hii. Akiwa mwenye hekima isiyo na kipimo, ametia **viungo ... katika mwili, kama ilivyompendeza yeze**. Ingetupasa kumshukuru kwa zawadi yo yote ambayo alituletea, na kutumika nayo kwa utukufu wake na kwa kupatisha wengine nguvu. Kuwa na wivu juu ya zawadi ya mtu mwagine ni zambi. Ni kukataa shauri timilifu la Mungu kwa maisha yetu.

12:19 Haiwezekani kuwa na mwili wenyewe **kiungo kimoja** tu. Vivyo hivyo Wakorinto wakumbuke ya kwamba wa-kiwa na zawadi ya kusema kwa lugha tu, wasingalikuwa na **mwili**. Walihitaji za-

wadi nyingine vilevile, hata zile zisi-zoonekana sana kama lugha.

12:20 Lilikuwa shauri la Mungu kwa **viungu kuwa vingi, lakini mwili mmoja**. Maneno haya ni wazi wakati tunapowaza juu ya mwili wa mtu. Yanepasa kuwa wazi vilevile ndani ya utumishi wetu kanisani.

12:21 Kama ulivyo upumbavu kwa mtu mmoja kuwa na wivu juu ya zawadi ya mtu mwagine, vivyo hivyo ni upumbavu vilevile kwa mtu mmoja kuona zawadi ya mtu mwagine kuwa bila faida asiyohitaji. **Jicho haliwezi ku-uaambia mkono: Sihitaji wewe; wala tena kichwa hakiwezi kuiambia mi-guu: Sihitaji ninyi.** Jicho linaweza kuona maneno yanayohitaji kutengenezwa, lakini haliwezi kuyatengeneza. Linatazamia mkono kufanya hivi. Na vilevile kichwa kinajua kwamba ni lazima kwenda pahali fulani, lakini linategemea miguu kukipeleka pale.

12:22 Ni kama **viungo vingine** nya **mwili ... vinaonekana kuwa zaifu** kupita vingine. Kwa mfano figo hazionekani kuwa na nguvu nyingi kama mikono. Lakini figo ni viungo nya lazima kabisa kwa afya ya mwili. Sivyo na mikono. Tunaweza kuishi bila mikono na miguu, na hata bila ulimi, lakini hatuwezi kuishi bila moyo, pumu, maini, au akili. Lakini viungo hivi vilivyo lazima kwa uzima wetu, havioneckani kwa macho ya watu. Vina-fanya tu kazi yao kama kwa siri.

12:23 Viungo vingine nya mwili havioneckani **vizuri**, hivi tunavilinda kwa njia ya kuvifunika na mavazi.

12:24 Viungo vingine nya mwili vinaonekana vizuri na havihitaji kusaidiwa. **Lakini Mungu** aliunganisha viungo mbalimbali vyote nya **mwili** kuwa umbo moja. Viungo vingine vinaonekana vizuri kupita vingine katikati ya watu. Mungu amefahamisha watu kwamba wao wote wanahitajiana, nao wote wanapaswa kusaidiana.

12:25 Viungo vikisaidiana hivi, hakutakuwa na **matengo mwilini**. Ingepasa kuwa hivi ndani ya kanisa. Kuweka roho zaidi juu ya zawadi fulani moja kupita nyingine kunazaa magomvi na matengano.

12:26 Neno lo lote likiumiza **kiungo kimoja** cha mwili wa mtu, viungo **vyote** vinaumia pamoja. Mtu akiwa na homa, homa hii haigusi sehemu moja tu ya mwili, lakini mwili mzima. Ni vivyo hivyo na gonywa na maumivu mengine vilevile. Mara nyingi mganga wa macho anaweza kuona ugonjwa mwingine mwilini mwa mgonywa kwa njia ya kuangalia ndani ya jicho lake. Hata kama viungo vya mwili ni namna namna, viungo hivi vyote ni sehemu ya mwili mmoja na vi-naungwa na uzima mmoja. Hivi neno lo lote likigusa kiungo kimoja linavigusa vyote. Hivi haifai tunungunike juu ya hali yetu, au kuwaza kwamba tunawenza kujisimamia wenyewe. Sivyo, ingetupasa sisi sote kushirikiana na roho ya umoja ndani ya Mwili wa Kristo. Neno lo lote linaloumiza Mkristo mwingine lingepasa kutuhuzunisha sana. Vilevile, haifai kwa sisi kuwa na wivu wakati Mkristo mwingine **anapoheshimiwa**, lakini **kufurahi pamoja** naye.

12:27 Paulo alikumbusha Wakorinto kwamba **wao ni mwili wa Kristo**. Maana yake haiko kwamba wao ni Mwili wake mzima. Wao wote pamoja ni mfano mdogo wa Mwili wa Kristo. **Kila Mkristo mmoja mmoja peke yake** ni kiungo cha ushirika ule mkubwa wa jamii. Mkristo, akikumbuka neno hili, inampasa kufanya kazi yake bila kiburi au wivu, na bila kufikiri kwamba yeche mwenyewe hana faida, na hahitaji kusaidiwa na wengine.

12:28 Sasa Paulo aliletta orodha nyingine ya zawadi. Hakuna orodha inayotaja zawadi zote. **Na Mungu ameweka wengine katika kanisa, wa kwanza mitume**. Neno hili **kwanza**

linaonyesha kwamba si wote ni mitume. Wanaume wale kumi na wawili walilagizwa na Bwana kuwa wajumbe wake. Walikuwa pamoja naye wakati ali-pokuwa hapa duniani (Mdo. 1:21, 22), nao wote, ila Yuda, walimwona nyuma ya ufufuko wake (Mdo. 1:2, 3, 22). Lakini kulikuwa na watu wengine waliokuwa mitume vilevile. Mwenye kujulikana zaidi alikuwa Paulo. Wengine walikuwa Barnaba (Mdo. 14:4, 14); Yakobo, ndugu ya Bwana Yesu (Gal. 1:19); Sila na Timoteo (1 Tes. 1:1; 2:6). Pamoja na manabii wa Agano Jipy, mitume waliweka msingi wa mafundisho wa kanisa ndani ya maneno waliyofundisha juu ya Bwana Yesu Kristo (Efe. 2:20). Hatuna mitume sasa namna ya wale wa kwanza. Tuna wajumbe na wenyewe kusimamisha makanisa, wanaotumwa na Bwana. Tunawaita **wajumbe**, si mitume, kwa sababu hawana amri na uwezo wa mitume ya wakati wa mwanzo.

Halafu tunaona **manabii**. Tumeonyesha mbele ya kwamba manabii walisema kwa ajili ya Mungu. Walisema maneno ya Mungu kabisa wakati kuandika kwa Neno la Mungu kusipokwisha bado. **Walimu** ndio watu wanaoleza neno la Mungu kwa watu. **Matendo ya uwezo** yangeweza kufufua wafu, kutoa pepo wachafu, vivi hivi. **Kuponyesha** wagonjwa ni juu ya kuponyesha mara moja gongwa za mwili za watu, kama tulivyoonyesha mbele; **wenyewe kusaidia** ni zaidi wenyewe kufanya kazi ya watumishi kanisani, kuchunga maneno ya mali ya kanisa. Zawadi ya **kuongoza**, ndio wazee au waaskofu wanaolinda roho za Wakristo kanisani. Zawadi ya mwisho inayotajwa ni zawadi ya **lugha**. Tunafikiri Paulo alitaja mitume kwanza na kusudi, na lugha kwa mwisho. Wakorinto walikuwa wakiweka lugha **kwanza** na hawakuheshimu mtume!

12:29, 30 Sasa mtume aliuliza kama zawadi ya kila mwamini ni sawasawa na ile ya watu wengine – au mtume, au nabii, au mwalimu, maajabu, kuponyesha, kusaidia, kuongoza, lugha, na kutafsiri lugha. Anajua kwamba watajibu “Sivyo.” Hivi haifai kusema kwamba inapasa *kila mtu* kuweza kusema kwa lugha. Wazo hili halipatani na kweli ya neno la Mungu ya kuwa kuna mwili mmoja wenyewe viungo vingi, na kwamba kila kiungo kina kazi yake chenyewe.

Hivi, kama tunaona hapa, si kila mtu aliye na zawadi ya lugha, na haifai kufundisha kwamba kuweza kusema na lugha ni alama ya ubatizo wa Roho Mtakatifu. Ikiwa hivi, si kwa kila mtu kutazamia ubatizo huu. Na tukumbuke kweli hii vilevile ya kwamba *kila mwamini* amekwisha kubatizwa na Roho (sh. 13).

12:31 Wakati Paulo aliposema, “**muwe na hamu sana kupata zawadi kubwa zaidi**,” alisema na Wakorinto kama kanisa la pahali pale, si kwa watu mmoja mmoja. Alisema kwamba ingepasa kanisa kuwa na zawadi zinazoweza kujenga waamini. Zawadi nzuri zaidi ndizo zawadi zilizo na faida zaidi, si zile zinazoonekana vizuri zaidi. Ni Roho Mtakatifu anayetoa zawadi zote, hivi haifai kuzarau zawadi yo yote. Hata hivi zawadi nyingine zina faida kupita nyingine kwa mwili. Kila kanisa lingepasa kuomba Bwana kusimamisha katikati yao watu wenyewe zawadi hizi.

Lakini nitawaonyeshea ninyi njia nzuri zaidi. Halafu Paulo aliendelea na sura 13, ndiyo sura inayofundisha zaidi juu ya mapendo. Alisema ya kwamba ni vizuri kuwa na zawadi hizi na kutumika nazo, lakini ni vizuri zaidi kutumika nazo na roho ya mapendo. Wenyewe mapendo wanafikiri juu ya mahitaji ya watu wengine, si juu yao wenyewe. Ni vizuri sana kuona mtu aliyepewa zawadi kubwa toka Roho Mtakatifu. Ni vizuri

zaidi kama mtu yule hatumiki na zawadi hii kukokota macho ya watu juu yake mwenyewe, lakini kwa kujenga watu wengine katika imani.

Ni kama namna watu walivyotumika na zawadi ya lugha ililetu magomvi kanisani. Walitumika nayo kwa ku-jituza wenyewe, kuwijenga na kujipe-ndeza wenyewe, lakini hawakutenda na mapendo. Wao wenyewe walisaidiwa kwa njia ya kusema kwa lugha wasiyojifunza katikati ya watu, lakini ilikuwa nguvu sana kwa watu wale kuketi pale na kusikiliza habari wasizofahamu. Paulo alisema sana kwamba inapasa kutumika na zawadi zote na roho ya mapendo. Kusudi la mapendo si kujipendeza mwenyewe lakini kusaidia watu wengine.

Na labda watu wale wasiosema kwa lugha hawakutenda na mapendo hata kidogo. Labda walisema kwamba kusema na lugha kunatoka kwa Shetani! Labda ukosefu wao wa mapendo ulikuwa hata vibaya kupita namna wengine walitumia lugha.

Hivi ilikuwa vizuri kwa Paulo kuwakumbusha kwamba wao wote walihitaji mapendo. Kama wakitendeana na mape-ndo, mengi ya maneno yaliyoleta matata katikati yao yangetengenea. Hayakuhi-taji matengo wala kuondosha watu wengine kanisani. Neno lililohitajiwa li-likuwa mapendo.

13:1 Hata kama mtu akiweza **kusema** na lugha zote, za watu na za malaika, bila kutumika na uwezo huu kusaidia watu wengine, neno hili si faida kupita au la kupendeza kupita **kelele la shaba** inayolia. Hakuna faida kama watu wasipoweza kufahamu maneno yanayosemwa. Ni makelele bure tu. Ni lazima kwa lugha hizi kutafsiriwa, na masemo yenye yawe maneno ya kujenga. Labda **luga za malaika** ni mfano kusema juu ya masemo mema sana. Si masemo kwa lugha watu wasi-

yojua. Kila mara malaika waliyosema na watu katika Biblia, walisema na maneno watu waliyoweza kufahamu vizuri.

13:2 Vivyo hivyo labda mtu ali-funuliwa mambo ya ajabu toka Mungu. Labda ataweba **kufahamu siri** kubwa za Mungu, kweli kubwa sana zisizofunuliwa mbele lakini anazojulishwa sasa, na kupewa **maarifa** kubwa toka Mungu. Labda anapewa **imani** kubwa sana hata anaweza **kuhamisha milima**. Lakini kama akitumika na zawadi hizi za ajabu kwa faida yake mwenyewe tu, na kama hatumiki nazo kujenga viungo vingine vya Mwili wa Kristo, zawadi hizi hazine faida, na mwenye zawadi hizi **si kitu**, maana yake hasaidii watu wengine.

13:3 Kama mtume akitoa **mali** zake zote **kulisha masikini**, au akitoa **mwili** wake **aungue kwa moto**, matendo haya hayamletei faida kama yakifanywa bila **mapendo**. Kama akiyafanya kukokota watu kumtazama na kumsifu yeye, matendo haya mazuri ni bure.

13:4 Hodge alionyesha kwamba Wakorinto walikosa saburi na furaha, walikuwa na wivu, wenye kiburi, wenye kujifikiri wenyewe, bila adabu, na hawakuweka roho juu ya mahitaji ya watu wengine.

Hivi mtume anasawanisha sasa matendo haya na mapendo ya kweli. Neno la kwanza analoonyesha ni ya kwamba **mapendo yanavumilia, ni upole**. Yana saburi hata wakati yanapokasirishwa, na yanatenda mema na kusaidia wengine. Wenye mapendo **hawaonei watu wengine wivu**, lakini wanafurahi wakati wanapoheshimiwa. **Mapendo hayajisifu; hayajivuni**. Yanafahamu kwa-mba maneno haya yote ni zawadi toka Mungu, na ya kwamba mtu hana kitu ambacho anaweza kuwa na kiburi juu yake. Ni Mungu, kwa enzi yake, anayetolea watu zawadi za Roho Mtakatifu, na haifai mtu kujisifu na

kuwa na kiburi kwa sababu yao, si neno kama ni zawadi ya uwezo mkubwa na ya kujulikana sana.

13:5 Mapendo **hayakosi kuwa na adabu**. Kama mtu akitenda na mapendo, atakuwa na adabu na kufikiri watu wengine. Mwenye mapendo **hatafuti maneno yake mwenyewe**, lakini maneno gani yatakayosaidia watu wengine. **Hakasiriki mbio**, lakini anavumilia mazaru. **Hahesabu mabaya**, maana hafikiri wengine wanatenda na maku-sudi mabaya.

13:6 Mapendo **hayafurahi kwa uzalimu, lakini yanafurahi pamoja na kweli**. Ni kama sisi watu tunafurahi ndani ya kutenda kwa uzalimu, kama tendo hili likiweza kuwa faida kwetu. Hii si roho ya mapendo. Mwenye mapendo **anafurahi** kila mara **kweli** inaposhinda.

13:7 Labda maana ya **yanahimili maneno yote** ni ya kwamba mwenye mapendo yanavumilia **maneno yote** na saburi, au ya kwamba anaficha upungufu wa watu wengine. Neno hili **himili** linaweza kutafsiriwa “funika.” Mwenye mapendo hatangazi kuanguka kwa watu wengine bure, lakini anawahamakia na kuwaonya kama ikihitajiwa.

Mapendo **yanaamini maneno yote**, maana yanafikiri mema juu ya matendo na matukio. Mapendo **yanatumaini maneno yote**, ya kwamba mwisho wao utakuwa mema. Mapendo **yanavumilia maneno yote**, kama mateso na mau-mivu.

13:8 Nyuma ya kusema juu ya tabia ya wale wanaotumika na zawadi yao na mapendo, mtume alionyesha kwamba mapendo yanadumu, lakini zawadi ni **kwa wakati tu**. **Mapendo hayapunguki hata kidogo**. Yataendelea hata kwa milele, na tutakaa kupenda Bwana, na kuperdana na wenzetu kwa milele. Lakini zawadi zile zitadumu kwa wakati tu.

Watu wanaeleza mashairi 8-13 kwa njia mbili. Njia ya kwanza ni ya kwamba zawadi za unabii, lugha, na kujua zitakoma wakati waamini wana-poinga hali ya milele. Njia ya pili ni ya kwamba zawadi hizi zimekoma hata sasa, wakati kanuni ya Maandiko Matakatifu ilipomalizwa. Kuonyesha njia hizi mbili tutafafanua mashairi 8-12 kwa safu mbili.

Safu moja inaitwa

HALI YA MILELE, na ya pili
UKAMILIFU WA KANUNI.

HALI YA MILELE

~ **UKAMILIFU WA KANUNI**

Mapendo hayatakoma kamwe, lakini unabii wa wakati wa sasa utakoma wakati watu wa Mungu watakapokuwa mbinguni. Tuna zawadi ya kujua sasa, lakini zawadi hii itakoma vilevile wakati tutakapofika mbinguni. (Wakati Paulo aliposema maarifa yataondoshwa, si kusema kwamba hakutakuwa na marifa mbinguni. Bila shaka aliwaza juu ya zawadi ya kujua, kwa njia yake kweli za Mungu zinafunuliwa.)

~ **UKAMILIFU WA KANUNI**

Mapendo hayatakoma kamwe. Ukiwa unabii (kwa wakati wa Paulo), funuo hizi toka Mungu hazikuhitajiwa tena wakati kuandika kwa vitabu vyote vya Agano Jipyä kulipokwisha. Kwa wakati wa Paulo, watu wengine walisema kwa lugha, lakini neno hili lilikoma wakati kuandika kwa vitabu makumi sita na sita vya Biblia vilipokwisha. Lugha hazitahitajiwa tena kuhakikisha mahubiri ya mitume na manabii (Ebr. 2:3, 4). Mungu alifunulia mitume na manabii kweli zake, lakini neno hili lilikoma vilevile wakati kanuni nzima ya Wakristo ilipokwisha.

13:9 Kwa maisha yetu ya sasa tunajua kwa sehemu tu, na tunatabiri kwa sehemu. Kuna maneno mengi ndani ya Biblia ambayo hatufahamu, na maongozi mengi ya Mungu ni siri kwetu.

~ Sisi (maana mitume) tunajua kwa sehemu, (maana Mungu anakaa kutufunulia kweli nyingine), na tunafanya unabii kwa sehemu tu (kwa sababu tunawenza kuonyesha tu sehemu funuo tunazopokea).

13:10 Lakini wakati iliyo kamilifu itakayokuja, maana wakati tutakapofika hali ya ukamilifu katika ulimwengu wa milele, zawadi za maarifa na unabii wa sehemu zitaondolewa.

~ Lakini wakati iliyo kamilifu imekuja, maana wakati kanuni ilipokwisha kwa njia ya kuongezwa kwa kitabu cha mwisho kwa Agano Jipyä, halafu kweli za Mungu hazikufunuliwa na kuhubiriwa tena sehemu sehemu, na wakati na wakati, kwa sababu tuna Neno zima la Mungu.

13:11 Tunawenza kusawanisha maisha yetu ya sasa na utoto wetu, saa masemo yetu, ufahamu wetu na mafikiri yetu ni nusu kwanza. Hali ya mbinguni inaweza kusawanishwa na kukomea kwa mtu. Saa ile hali yetu ya utoto itakwisha.

~ Zawadi za alama zilikuwa kwa muda wa utoto wa kanisa. Hazikuwa alama za utoto; zilikuwa zawadi zilizohitajiwa za Roho Mtakatifu. Lakini wakati ufunuo wa Mungu ulipotimia na ulikuwa tayari kwa watu, zawadi hizi za ajabu hazikuhitajiwa tena. Maana ya mtoto hapa ni mtoto mchanga asiyeweza kusema kama mtu wa kukomea.

13:12 Wakati tulipo kwanza duniani, hatuoni vitu waziwazi, lakini kama kwa kioo. Katika mbingu tutaona vitu uso kwa uso, bila kitu kuzuiza kuona kwetu. Sasa tunajua kwa sehemu, lakini siku ile tutajua namna tunavyo juliwa. Hatutajua maneno yote kamwe, hata mbinguni.

~ Sasa (kwa muda wa mitume) tunajua kama kwa kioo, si wazi. Hata mmoja wetu (sisi mitume) aliyepokea ufunuo mzima wa Mungu. Mungu tu anajua maneno yote; sisi tunapewa se-

hemu sehemu. Wakati wa kwisha kwa kanuni ya Maandiko, maneno yote yanonekana wazi na tunajua maneno mengi kupita mbele.

13:13 Imani, tumaini, na mapendo ni matunda ya Roho, nayo ni makubwa kupita na yanaendelea muda mrefu kupita zawadi za Roho vilevile. Ndiyo, *tunda* la Roho ni kubwa kupita *zawadi* za Roho.

Na **mapendo ni makubwa zaidi**, kwa sababu yanasaidia watu wengine zaidi. Hayajifikiri yenyewe.

Mbele ya kuacha sura hii, tunataka kuonyesha kwamba waamini wengi wanafikiri kusudi la zawadi za alama lilikuwa kuhakikisha mahubiri ya mitume mbele ya kuandikwa kwa Neno la Mungu. Sasa Agano Jipyia zima lili-andikwa na hivi zawadi hizi hazihitajiwi. Haiwezekani kuhakikisha mawazo haya kabisa. Kama Mungu akitaka, angeweza kutumika na zawadi za alama hata wakati wa sasa. Lakini tunajua neno moja kabisa, ndilo ya kwamba hata kama zawadi za Roho ni kwa sehemu na wakati tu, tunda la Roho ni la milele, na ni vizuri zaidi. Kama tukitenda na mapendo, tutaepuka kutumia zawadi vibaya, na kwa njia ile kuamsha ugomvi na matengo.

14:1 Si nguvu kuona namna shairi hili linafungana na sura 13. Inafaa Wakristo **kufuata mapendo**, ndiyo kujaribu kutumikia watu wengine wakati wote. Ingewapasa kuwa na hamu kwa **zawadi za Roho** kwa kanisa lao vilevile. Hata kama ni Roho anayegawa zawadi namna anavyotaka, tunaweza kuomba kupewa vilevile zawadi zile zitakazosaidia makanisa yetu zaidi. Kwa sababu hii, ni wazi ya kwamba kwa mafikiri ya Paulo zawadi ya kutabiri ina faida kupita zawadi za Roho.

14:2 Yeye anayesema kwa lugha bila kueleza maneno anayosema, hasemi kusaidia watu wa kanisa. **Mungu** anafa-

hamu maneno anayosema, lakini kwa watu ni kama lugha ya kabilia lingine. Labda mtu mwenyewe anaeleza kweli za ajabu, watu wasiyojua mbele, lakini haina faida kwa sababu watu hawawezi kufahamu masemo yake.

14:3 Lakini mtu **anayetabiri** ana-jenga watu, na kupatisha roho zao nguvu, na kuwafariji. Ni faida kwao kwa sababu anasema na lugha ambayo wanafahamu. Wakati Paulo aliposema kwamba nabii anajenga, ni kuonyesha kwamba hili ndilo tunda wakati watu wanaposikia mafundisho kwa lugha wanayojuua.

14:4 Mara nydingi watu wanataja shairi 4 kueleza kwamba si mbaya kusema na lugha kwa kujijenga mwenyewe. Lakini neno hili “kanisa” linapatikana mara tisa ndani ya sura hii (mash. 4, 5, 12, 19, 23, 28, 33, 34, 35), na linatuaminisha ya kwamba Paulo hakuwaza juu ya maisha ya mwamini akiabudu Mungu nyumbani peke yake, lakini juu ya kusema kwa lugha kanisani. Mtume hakuonyesha ukubali wa kusema na lugha kwa kujijenga mwenyewe hata kidogo, lakini alikataza Wakristo kutumika na zawadi hii kanisani kwa njia isiyosaidia watu *wengine*. Mwenye mapendo anasaidia watu wengine, si yeze mwenyewe. Zawadi ya lugha ikitumikiwa na mapendo, itasaidia watu wengine, si mwenye zawadi tu.

Yeye anayetabiri anajenga kanisa. Haonyeshi zawadi yake kwa faida yake mwenyewe, lakini anasema na lugha watu wanayofahamu na kujenga kanisa.

14:5 Paulo hakuzarau zawadi ya lugha, lakini alifahamu kwamba ni zawadi ya Roho Mtakatifu. Hakuweza na hakutaka kuzarau kitu cho chote kili-chotoka kwa Roho. Wakati aliposema, “**Ninataka ninyi wote museme kwa lugha**,” alionyesha kwamba hakutamani zawadi hii kwa yeze mwenyewe na watu wachache tu. Hamu yake ilifanana

na ile ya Musa aliyesema: “Ingekuwa heri kama watu wote wa BWANA wangekuwa manabii na kama BWANA angewatia roho yake!” (Hes. 11:29b). Lakini hata kama Paulo alisema hivi, alijua kwamba hayakuwa mapenzi ya Mungu kwa waamini wote kuwa na zawadi fulani moja (ona 12:29, 30).

Angetaka *zaidi* Wakorinto **watabiri**, kwani wangefanya hivi, wangejengana katika imani, lakini kama wakisema kwa lugha bila mwenye kutafsiri, wasikiaji wao wasingefahamu wala kupata faida.

Maana ya “**kama haelezi maana**” inaweza kuwa “kama yeye anayesema kwa lugha hatafsiri” au “kama mtu mwingine hatafsiri.”

14:6 Hata kama Paulo mwenyewe akifikia Korinto **akisema kwa lugha**, isingalikuwa **faida** kwao kama wasingalifahamu maneno aliyosema. Inge-wapasa kuweza kutambua masemo yake kuwa **ufunuo na kujuua**, au **unabii na mafundisho**. Walimu wanapatana ya kwamba **ufunuo na kujuua** ni juu ya kupokea habari toku Mungu, na **unabii na mafundisho** ni juu ya kupatisha habari hizi kwa watu wengine. Paulo alitaka wafahamu kwamba sharti watu waweze kufahamu mafundisho wanayosikia. Kwa njia ile tu yatakuwa na faida kwa kanisa. Anaendelea kuhakikisha neno hili ndani ya mashairi yanayofuata.

14:7 Anasema kwanza juu ya vitu vya kufanya muziki. Hata vitu visivyo na uhai kama **filimbi au kinubi** vikitoa sauti **pasipo tofauti**, namna gani neno **linalopigwa** litatambulikana na kuendeza masikio?

14:8 Ni vivyo hivyo na **baragumu**. Sharti sauti yake ijulikane wazi. Kama sivyo, **hakuna mtu ambaye atajitayarisha kupiga vita**.

14:9 Ni vivyo hivyo na ulimi wa mtu. (Maana ya “ulimi” ndani ya sura hii si lugha.) Kwa kupata faida, sharti watu waweze kufahamu maneno tunayosema. Kama sivyo, masemo yetu ni kama kwa

hewa tu na **hayana faida**. Na vilevile mafundisho yawe nyepesi kwa watu kufahamu. Kama ni mafundisho ya ‘jambo gumu’, hayatakuwa na faida kwa watu wa Mungu.

14:10 Paulo alikuwa amesema juu ya watu wakisema na lugha mbalimbali. Ndani ya shairi hili alionyesha kwamba **kuna sauti nyingi nyingine vilevile**. Labda aliwaza juu ya sauti mbalimbali za nyama na ndege. Alionyesha tu ya kwamba **hapana moja pasipo maana**.

14:11 Ni vivyo hivyo na masemo ya mtu. Kama hasemi wazi, hakuna mtu anayeweza kumfahamu. Ni nguvu sana kuzungumuza na mtu asiyefahamu lugha yako.

14:12 Kwa sababu hii inapasa Wakorinto, pamoja na bidii yao kwa **zawadi za roho**, wawe na hamu vilevile kujenga **kanisa**. Ona ya kwamba Paulo hukujaribu kamwe kupunguza bidii yao kwa zawadi za roho, lakini alijaribu kuwongoza kutumika na zawadi hizi kwa faida kubwa zaidi.

14:13 Mtu **akisema kwa lugha**, inampasa kuomba **aweze kutafsiri maana yake vilevile**. Au labda maana yake ni aombe kwa **mtu mwingine** kusatikana kueleza maana. Mara moja moja mtu mwenye zawadi ya lugha ana zawadi ya kueleza maana vilevile.

14:14 Kwa mfano, mtu akiomba **kwa lugha** nyingine katika kusanyiko la kanisa, **roho** yake inaomba, lakini haonyeshi na masemo ya watu maneno anayosikia rohoni mwake. **Akili yake haizai matunda**, maana yake hakuna mtu mwingine katika kusanyiko anayepata faida. Ndani ya mafundisho juu ya 14:19 tutaonyesha kwamba tunafikiri maana ya **akili yangu** ni “ufahamu wa watu wengine wa maombi yangu.”

14:15 Hivi **kwa sababu ya maneno haya** Paulo **hataomba kwa roho tu**, lakini **ataomba kwa akili vilevile**, kusudi watu waweze kufahamu. Maana ya **nitaomba kwa akili vilevile** si kusema

ataomba na akili *yake* mwenyewe, lakini ataomba ili watu wengine waweze kufahamu. Vivyo hivyo **ataimbä kwa roho** na **ataimbä kwa akili vilevile**, ili watu waweze kufahamu.

14:16 Shairi hili linaonyesha wazi kwamba hii ndiyo maana ya kweli. Kama Paulo asingeomba namna watu walivyoweza kumfahamu, namna gani wataweza kusema “**Amina**” kwa mwisho wa ombi lake?

Yeye anayeketi katika pahali pa mjinga ni mtu asiyejua lugha ya mnenaji. Habari hizi zinaonyesha vilevile ya kwamba kusema “**Amina**” kunakubaliwa ndani ya makusanyiko ya kanisa.

14:17 Hata **ukishukuru** Mungu kwa lugha, wengine **hawajengwi** kama wasipofahamu maneno unayosema.

14:18 Ni kama mtume aliweza kusema na lugha mbalimbali **kuliko wao wote**. Tunajua kwamba Paulo alikuwa amejifunza lugha nyingine, lakini bila shaka alisema hapa juu ya zawadi yake ya lugha.

14:19 Hata kama aliweza kusema na lugha nyingi, Paulo alisema kwamba **alipenda kusema maneno matano** kwa **akili** yake, kusudi watu waweze kumfahamu, zaidi ya kusema **maneno elfu kumi kwa lugha**. Hakutaka hata kidogo kutumika na zawadi ya lugha kujipatia sifa katikati ya watu. Neno alilotaka kupita yote lilikuwa kusaidia watu wa Mungu. Hivi alikusudi kusema tu na maneno watu walivyoweza kufahamu.

14:20 Halafu Paulo alionya Wakorinto wasiwe kama watoto wanaopenda michezo na vitu vya kungaa. Wasijifurahishe na zawadi hizi za kuonekana mbele ya watu. Ndiyo, katika **uovu** ili-wapasa kuwa kama watoto, lakini katika akili wawe kama watu wazima kwa maneno yote mengine.

14:21 Halafu Paulo alitaja toka Isaya kwamba lugha ni alama kwa **wasioamini**, si zaidi kwa waamini. Mungu alisema ya kwamba sababu wana wa

Israeli walikataa habari zake na kuzirau, hivi atasema nao kwa lugha nyingine (Isa. 28:11). Neno hili lilitimizwa wakati Waasuria walipoingia inchi ya Israeli, na Waisraeli waliposikia watu wakisema lugha ya Waasuria katikati yao. Neno hili lilikuwa alama kwao kwamba walikuwa wamekataa neno la Mungu.

14:22 Mtume alitaka kuonyesha ya kwamba Mungu alikusudi **lugha** kuwa **alama** kwa **wasioamini**, hivi haifai kwa Wakorinto kuweka roho sana juu ya kusema kwa lugha ndani ya makusanyiko kwa waamini. Ingekuwa vizuri kupita watabiri, kwani kutabiri ni alama kwa waamini, **si kwa wasioamini**.

14:23 **Kama kanisa zima limekusanyika, na** Wakristo **wote wanasema kwa lugha** bila mtafsiri, wageni wangefikiri nini? Usingalikuwa ushuhuda mzuri; watafikiri Wakristo ni wazimu.

Inaonekana sawasawa shairi 22 na mashairi 23-25 hayapatani. Ndani ya shairi 22 tunasoma ya kwamba lugha ni alama kwa wasioamini, na unabii ni kwa waamini. Lakini ndani ya mashairi 23-25, Paulo alisema kwamba waamini waki-sema kwa lugha kanisani, neno hili lingeweza kuwa kikwazo kwa wasioamini, lakini unabii ungeweza kuwasaidia.

Hili ndilo elezo la neno hili: Wasioamini ndani ya shairi 22 ni watu waliokataa neno la Mungu na kufunga nia zao kwa kweli. Lugha ni alama ya hukumu ya Mungu kwao, kama katika shairi toka Isaya (sh. 21). Wasioamini ndani ya mashairi 23-25 walikuwa tayari kupokea mafundisho. Walifikia kusanyiko la Wakristo kwa sababu walitaka kusikia neno la Mungu. Kama wakisikia Wakristo wakisema kwa lugha bila tafsiri, watatatanishwa, hawatasaidiwa hata kidogo.

14:24 Wageni wakifikia kusanyiko pahali Wakristo wasiposema kwa lugha lakini wanapotabiri, mgeni anasikia na kufahamu maneno anayosikia, na **ana-**

hamakiwa na wote, na anahukumiwa na wote. Mtume anaonyesha hapa kwamba msiyeamini hataweza kufahamu kwamba ye ye ni mwenye zambi kama asipofahamu maneno anayosikia. Ni wazi ya kwamba wageni wakisikia lugha bila tafsiri, hawasaidiwi hata kidogo. Ingepasa wenye kutafsiri kufanya hivi kwa lugha ya watu wa inchi pahali wanapokaa, hivi maneno wasikiaji wanayosikia yatakuwa faida kwo.

14:25 Siri za moyo wa mtu **zinafunuliwa** wakati anaposikia unabii, ndiyo mahubiri ya Neno la Mungu. Ni kama mhubiri anasema naye peke yake. Roho ya Mungu anatumika ndani ya roho yake na kumwonyesha zambi zake. **Hivi akianguka kifudifudi, ataabudu Mungu, akisema ya kuwa kweli Mungu ni katikati** ya watu hawa.

Hivi Paulo alionyesha ndani ya mashairi 22-25 ya kwamba lugha bila mwenye kutafsiri maana yao hazifa-hamishi wasioamini zambi zao, lakini unabii unaweza.

14:26 Kwa sababu zawadi ya lugha ilizaa maneno yasiyokuwa taratibu kanisani, ilipasa Roho ya Mungu kusimamisha utaratibu kwa namna gani kutumika na zawadi hii. Tunaona utaratibu huu ndani ya mashairi 26-28.

Nini ilitokea wakati waamini **walipokutana pamoja** kwa wakati wa mwanzo wa kanisa? Roho ya Mungu aliweza kutumika na zawadi mbalimbali alizokwisha kumpa kanisa. Kwa mfano, mtu mmoja alisoma **zaburi** moja, na nwingine alikuwa na **mafundisho**. Mwingine alisema kwa **lugha** kigeni. Mtu mwingine alihubiri **ufunuo** ambao alipokea toka Bwana. Mwingine atatafsiri lugha iliyosemwa mbele. Paulo alikubali kwa Roho ya Mungu kusema kwa njia ya wanaume mbalimbali, lakini alisema vilevile ya kwamba haifai kufanya maneno yo yote kwa kuonekana tu, lakini sharti yote **yafanywe** na kusudi

la **kujenga** watu wa Mungu na kuwapatisha nguvu rohoni.

14:27 Neno la pili lilikuwa ya kwamba ndani ya kusanyiko lo lote hesabu ya wenye kusema kwa lugha isipite watatu. **Kama mtu akisema kwa lugha, waseme wawili, au wasipite watatu.** Haifai kwa watu wengi kusimama pamoja ndani ya kusanyiko moja kuonyesha uwezo wao kusema kwa lugha nyingine.

Halafu tunaona ya kwamba haifai watu wale wawili au watatu waliopewa ruhusa kusema kwa lugha ndani ya kusanyiko moja waseme wote kwa saa moja. Sharti waseme mmoja **nyuma ya** mwingine. Neno hili litazuizaa machafuko.

Pamoja na ile, lazima mtu **mmoja aelege maana**. Mtu akitaka kusimama na kusema kwa lugha kigeni, lazima aone kwanza kama kuna mtu mwingine pale atakayeweza kutafsiri maneno atakayosema.

14:28 Kama hakuna mmoja wa kuleleza, halafu anyamaze katika kanisa. Anaweza kuketi pale na kusema kwa Mungu kwa lugha kigeni bila kusikiwa, lakini hana ruhusa kufanya hivi mbele ya watu.

14:29 Kuna amri ndani ya mashairi 29-33a juu ya zawadi ya unabii. **Manabii wawili au watatu** waseme, na **wengine wapime** maneno. Si kupita watu **watatu** waseme kwa kusanyiko moja, na Wakristo waliosikiliza wata-mbue kama masemo yao yalitoka kweli kwa Mungu, au kama msemaji alikuwa nabii wa uwongo.

14:30 Tulisema mbele kwamba nabii alipokea habari toka Bwana na alizifunua kwa kanisa. Lakini labda nyuma ya kutoa ufunuo huu, aliendelea kuhubiri kwa watu. Hivi mtume alitoa amri nyingine kusema kama wakati nabii mmoja alipokuwa akisema, nabii mwingine aliyeketi pale **alipopewa ufunuo**, ilipasa **mtu wa kwanza** kunyamaza

kusudi nabii wa pili apate njia kutoa ufunuo ambaeo alipokea sasa. Sababu kwa amri hii ni ya kwamba mtu akikaa kusema saa ndefu, labda atasema mafikiri yake mwenyewe, si maneno anayongozwa na Mungu kusema.

14:31 Vizuri manabii wote wapate njia kutabiri **mmoja mmoja**. Haifai kwa nabii mmoja ahubiri kwa saa nzima ya kusanyiko. Kwa njia hii kanisa litapata faida kubwa zaidi – watu **wote watafundishwa, na kufarijiwa**.

14:32 Shairi hili linaonyesha kwamba Wakorinto walianguka wakati walipofikiri ya kuwa kwa kipimo mtu alichotawaliwa na Roho Mtakatifu, ha-kuweza kujitawala mwenyewe. Walfikiri kwamba mtu aliyetawaliwa na Roho alishindwa kutawala maneno aliyosema, kama alisema kwa muda gani, na matendo yake mengine. Mashairi haya yanakana mawazo namna hii kabisa. **Roho za manabii zinatii manabii**. Maneno haya yanaonyesha kwamba mtu hasukumwi kufanya neno bila ukubali wake. Yeye mwenyewe anaweza kuweka mpaka kwa wakati gani na kwa muda gani anapaswa kufundisha.

14:33 Kwa sababu Mungu si Mungu wa machafuko, lakini wa salama. Ni kusema, kama kusanyiko ni pahali pa makelele, *tunajua kwamba kusanyiko* hili halitawaliwi na Roho Mtakatifu.

14:34 Sehemu ya mwisho ya shairi 33 ingepasa kuwa mwanzo wa shairi 34. Mafundisho ya Paulo kwa Wakorinto yalikuwa kwa **makanisa yote ya watakatifu**. Agano Jipyia linafundisha kwamba wanawake Wakristo wanawenza kutumikia Mungu kwa njia nyingi, lakini si kwa njia ya kufundisha Neno la Mungu kwa kanisa zima. Wamepewa kazi kubwa sana ya kuchunga nyumba na kulea watoto. Inawapasa kunye-nyekea mwanamume na hawana ruhusa kusema mbele ya watu wote kanisani.

Tunaamini kwamba semo hili: **Kama**

sheria inavyosema vilevile ni juu ya utii wa mwanamke kwa mwanamume, kama ilivyofundishwa ndani ya Agano la Kale. Kwa mfano, ona Mwanzo 3:16, “*kutaka kwako kutakuwa kwa mume wako, naye atakutawala.*”

Mara nyingi watu wanasesma Paulo alikataza wanawake kuzungumuza wakati wa makusanyiko, lakini elezo hili si vizuri. Maana ya neno linalotafsiriwa kusema (*laleo*) si kuzungumuza kwa Kiyunani. Ni neno lililotumiwa kwa Mungu akisema ndani ya shairi 21 la sura hii, na ndani ya Waembrania 1:1. Maana yake ni kusema na amri.

14:35 Ndiyo, wanawake hawakuwa na ruhusa kuuliza neno katikati ya watu kanisani. **Wakitaka kufundishwa ne-no, waulize waume wao wenyewe katika nyumba zao**. Inawezekana kutoa mafundisho kwa njia ya maulizo, lakini agizo hili linazuiza wanawake kufanya hivi.

Watu wakiuliza kama agizo hili ni kwa mwanamke asiyeolewa vilevile, na kwa mjane, ni vizuri kufahamu kwamba Maandiko hayataji maneno haya yote moja moja, lakini mwanamke asiye na mume, angeweza kuuliza baba yake, ndugu yake, au mmoja wa wazee wa kanisa. Maneno haya yanaweza kutfafsiriwa, “*Waulize wanaume nyumbani mwao.*” Neno kubwa ambalo inapasa kukumbuka ni ya kwamba **ni haya kwa mwanamke kusema katika kanisa**.

14:36 Ni kama Paulo alifahamu ya kwamba mafundisho haya yataleta ugomvi. Ni kweli. Hivi aliuliza na zihaka ndani ya shairi 36, **Neno la Mungu lilitoka kwenu? au liliwafikia ninyi peke yenu tu?** Ni kusema, kama Wakorinto walijua kupita mtume juu ya maneno haya, angeuliza kama kanisa lao lilitoa **neno la Mungu**, au kama walikuwa **watu wa pekee** ambaeo walilipokea? Ni kama walijionyesha kuwa wenye amri kwa maneno haya. Lakini

hakuna kanisa lililotoa neno la Mungu, na hakuna kanisa peke yake lililostahili kulipata.

14:37 Paulo alitaka wafahamu kwa-mba maneno ambayo aliandika na kueleza hayakuwa mawazo na tafsiri zake mwenyewe, lakini yalikuwa **ma-agizo ya Bwana**, na ya kwamba mtu ye yote aliye **nabii** wa Bwana, au **ali-yeweka roho sana** juu ya kweli ya Mungu **angekubali** neno hili. Shairi hili linatosha kujibu watu wale wanaosema kwamba mengine ya mafundisho ya Paulo, zaidi yale juu ya wanawake, ni mawazo yake mwenyewe tu. Sivyo! Yote ni **maagizo ya Bwana**. Hakuna njia nyininge; basi abaki mjinga.

14:38 Bila shaka watu wengine wangekataa neno hili. Jibu la Paulo kwa watu namna hii ni kwa mtu **aliye mjinga awe mjinga**, maana anakataa kuamini na kunyenyekaa mafundisho haya yali-yotolewa kwa maongozi ya Mungu.

14:39 Kwa kujumlisha mafundisho juu ya kutumika na zawadi, Paulo ali-waambia ndugu sasa **wawe na hamu sana kutabiri**, lakini **wasikataze** watu **kusema kwa lugha**. Shairi hili lina-onyesha kwamba zawadi ya kutabiri ina faida kupita zawadi ya lugha: **wawe na hamu sana** kutabiri, lakini **wasikataze** kusema kwa lugha. Unabii una faida kupita lugha kwa sababu kwa njia yake wasioamini wanafahamishwa zambi zao, na waamini wanapatishwa nguvu katika imani. Lugha, bila kutafsiriwa, hazina faida ila kwa mtu kusema kwa Mungu, na kwa roho yake mwenyewe, na kuonyesha akili yake kusema na lugha ile, ndio akili ambayo alipewa na Mungu.

14:40 Maonyo ya mwisho ya Paulo ndio **maneno yote yafanyike kwa uzuri na kwa utaratibu**. Ni maonyo ya maana sana. Katika miaka inayopita watu waliosema kwamba wanaweza kusema kwa lugha hawakujulikana kama wenye utaratibu kwa makusanyiko

yao. Mara nydingi yamekuwa makusanyiko ya machafuko.

Kwa kujumlisha mafundisho yake juu ya kusema na lugha kanisani, Paulo alitaja maneno saba:

1. Haifai kukataza watu kusema kwa lugha (sh. 39).
2. Haifai mtu kusema kwa lugha kama hakuna mtafsiri (mash. 27c, 28).
3. Haifai watu kupita watu watatu kusema kwa lugha ndani ya kusanyiko moja (sh. 27a).
4. Mtu mmoja tu aseme kwa lugha kwa saa moja (sh. 27b).
5. Lazima maneno wanayosema yawe maneno ya kujenga watu (sh. 26b).
6. Inapasa wanawake kukaa kimya (sh. 34).
7. Lazima yote **yafanywe kwa uzuri na kwa utaratibu** (sh. 40).

Maagizo haya ni kwa makanisa ya wakati wa sasa vilevile.

4. MAJIBU YA PAULO KWA WALE WANAOOKANA UFUFUKO (Sura 15)

Hii ni sura kubwa juu ya ufufuko. Walimu wengine walikuwa wameingia kanisa kwa Korinto, waliokana kwamba miili ya watu itafufuliwa. Hawakukana kwamba watu watakuwa na uzima tena nyuma ya mauti, lakini tunazania wali-fikiri watakuwa roho tu, bila miili. Mtume alionyesha sasa kwa sababu gani mawazo haya si kweli.

A. Hakika ya ufufuko (15:1-34)

15:1, 2 Paulo aliwakumbusha Habari Njema ambayo **aliwahubiri** na **waliyopokea**, na **kusimama** ndani yake. Haya hayakuwa mafundisho napya kwa Wakorinto, lakini walihitaji kukumbushwa juu yake kwa wakati huu. Walikuwa **wameokolewa** kwa njia ya Habari Njema hii. Halafu Paulo aliongeza maneno haya, **ikiwa munashika sana maneno ambayo niliwahubiri – kama isipokuwa muliamini bure**. Wa-

likuwa wameokolewa kwa Habari Njema ya Ufufuko – lakini kama usingalikuwa na ufufuko, wasingaliokolewa. Neno hili **kama** halionyeshi kwamba mtume alikuwa na shaka juu ya wokovu wao. Halifundishi vilevile kwamba waliokolewa kwa njia ya kushika sana. Paulo alisema tu kwamba wasingaliokolewa, kama hakuna ufufuko. Hivi watu waliokana kwamba kuna ufufuko wa mwili walishindana na kweli nzima ya Habari Njema. Kwa mafikiri ya Paulo, ufufuko ulikuwa msingi wa ukristo. Hivi shairi hili ni maonyo kwa Wakorinto kushika sana Habari Njema waliyopokea, hata kama watu wengine walikuwa wakishindana nayo kwa wakati ule.

15:3 Paulo alikuwa **amepasha** Wakorinto habari za maneno **aliyopokea vilevile** toka Mungu, **kwamba Kristo alikufa kwa sababu ya zambi zetu kama maandiko yanavyosema**. Shairi hili linaonyesha kwamba Kristo hakufa kwa zambi zake mwenyewe, au kwa sababu ya kukana dini yake. **Alikufa kwa zambi zetu**. Alikufa kama malipo **kwa zambi zetu**. **Maandiko** hapa ni Maandiko ya Agano la Kale, kwa sababu Agano Jipyä lilikuwa halijandikwa bado. Basi Agano la Kale linatabiri kwamba Kristo atakufa kwa zambi za watu? Ndiyo! Mashairi 5 na 6 ya Isaya 53 yanahakikisha neno hili.

15:4 Kuzikwa kwake kulitabiriwa katika Isaya 53:9, na ufufuko wake ndani ya Zaburi 16:9, 10. Ona namna Paulo aliviyotaja ushuhuda wa **Maandiko**. Ingetupasa sisi kufanya vivyo hivyo, kwa maneno yote ya imani yetu.

15:5 Ndani ya mashairi 5-7 tunasoma juu ya washuhuda wa ufufuko. Bwana alionekana kwanza kwa **Kefa** (Petro). Neno hili ndilo alama ya humura yake. Mwanafunzi huyu aliyeckana Bwana wake mara tatu alibarikiwa kwa njia ya kuona Bwana huyu peke yake nyuma ya ufufuko wake. Kweli neema

ya Bwana Yesu Kristo ni kubwa sana! **Kisha** Bwana alionekana kwa mitume **kumi na wawili**. Kabisa kabisa mitume kumi na wawili hawakuwa wote pamoja kwa wakati ule. Ni kama fungu la mitume liliitwa **kumi na wawili**, hata wakati wasipokuwa wote pamoja kwa saa fulani. Vizuri tufahamu vilevile kwamba ndani ya vitabu nya Habari Njema tunasoma juu ya kuonekana kwa Bwana kwa watu mara nyine zaidi ya mara hizi. Roho ya Mungu alichagua matukio ya ufufuko wa Kristo yaliokuwa na faida zaidi.

15:6 Watu wanafikiri kwamba Bwana alikuwa katika Galilaya wakati alipo-onekana kwa **ndugu zaidi ya mia tanu**. Kwa wakati Paulo alipoandika habari hizi, zaidi ya ndugu hawa walikuwa kwanza hai, hata kama wengine walikuwa wamekuwa. Lakini kama watu wakiwa na shaka juu ya maneno haya Paulo aliyoandika, kulikuwa na washuhuda wenye uzima ambao waliweza kuuliza.

15:7 Hatuwezi kujua kama **Yakobo** huyu ni Yakobo gani. Zaidi ya walimu wanafikiri alikuwa ndugu ya Bwana kwa njia ya Maria. Shairi 7 linatupasha vilevile ya kwamba Bwana alionekana kwa **mitume wote**.

15:8 Halafu Paulo aliandika juu ya mara ya kwanza yeeye alipokutana na Bwana nyuma ya ufufuko wake. Neno hili lilitokea kwa njia inayokwenda Damasiki wakati alipoona nuru kubwa toka mbinguni na alipokutana na Kristo mtukufu uso kwa uso. Paulo alisema yeeye ni mdogo kupita baki la mitume, kama mimba isiyokomea kwanza. Alisema hivi kujilaumu mwenyewe aki-kumbuka wakati alipotesa kanisa mbele.

15:9 Wakati alipofikiri juu ya heshima ya kukutana na Mwokozi uso kwa uso, alijazwa rohoni na mawazo ya ukosefu wa kustahili kwake. Alikumbuka namna aliviyotesa **kanisa la Mungu**, na namna hata hivi Bwana

alimwita kuwa mtume. Hivi aliinama hata udongo na kukiri kwamba yeye ni **mdogo katikati ya mitume, asiyesta-hili kuitwa mtume.**

15:10 Anaongeza kusema mara moja kwamba **kwa sababu ya neema ya Mungu** amegeuka kuwa namna alivyo. Hakupokea neema hii kama kitu bure, lakini kwa sababu yake alikuwa na deni kubwa, na alitumikia Kristo ambaye alimwokoa bila kuchoka. Alifahamu kwamba hakuwa yeye, lakini **neema ya Mungu** iliyokuwa ikitumika pamoja naye.

15:11 Sasa Paulo alifungana na mitume wengine na kusema kwamba si neno nani katikati yao aliyehubiri, kwani wao wote walikuwa pamoja ndani ya ushuhuda wao wa Habari Njema, na zaidi juu ya ufufuko wa Kristo.

15:12 Ndani ya mashairi 12-19 Paulo alitaja matunda ya kukana ufufuko wa mwili. Kwanza, kama hakuna ufufuko, Kristo mwenyewe asingalifufuka. Watu wengine walisema kwamba haiwezekani kwa mwili kufufuka. Kama ni hivi, Paulo alisema, Kristo asingalifufuka. Wakorinto walikubali neno hili? Sivyo. Kwa kuhakikisha kwamba neno lo lote ni kweli, inapasa kuonyesha tu kwamba neno hili linakwisha kutokea. Kuhakikisha ufufuko wa mwili, Paulo alitaja tu ya kwamba **Kristo** alikuwa **amefufuliwa toka wafu.**

15:13 Lakini kama hakuna ufufuko wa wafu, ni wazi ya kama **Kristo hakufufuliwa.** Mawazo namna hii yanjalijaza Wakorinto na huzuni kubwa bila tumaini.

15:14 Kama Kristo hakufufuliwa, basi **mahubiri** ya mitume yalikuwa **bure.** Kwa sababu gani? Kwa sababu Bwana Yesu mwenyewe alikuwa amehadi kwamba atafufuliwa toka wafu siku ya tatu. Kama *asipofufuliwa* kwa wakati ule, kama alikuwa mdanganyifu, au alianguka na asingalistahili kwa watu kumwamini. Hakuna wokovu isipokuwa

Kristo amefufuka. Kama Bwana Yesu asingalifufuliwa toka wafu, kama hakuna njia kwa watu kujua kwamba kufa kwake kulikuwa na faida kubwa kupita kufa kwa mtu ye yote mwininge. Lakini kwa njia ya kumfufua toka wafu, Mungu alishuhudu kwamba alipendezwa kabisa na kazi ya ukombozi wa Kristo.

Ni wazi ya kama mahubiri ya mitume yasipokuwa kweli, **imani** itakuwa bure vilevile. Si faida kutegemea habari bure zisizokuwa kweli.

15:15 Na vilevile kama mitume walihubiri maneno yasiyokuwa kweli, walishuhudia **Mungu uwongo.** Walishuhudia **Mungu kwamba alifufua Kristo** toka wafu. Kama Mungu asipofanya hivi, mitume walishuhudia Mungu **uwongo.**

15:16 Kama haikuwezekana hata kidogo kwa watu kufufuliwa toka mauti, hata Kristo hakufufuliwa. Lakini kama ufufuko ulitukia mara moja, kama wakati Kristo alipofufuliwa, ni wazi ya kwamba ufufuko ni tukio la hakika.

15:17 Na kama **Kristo** hakufufuliwa, **imani** ya waamini **ni bure** na bila uwezo. Na hakuna usamehe wa **zambi.** Hivi kukataa ufufuko ni kukataa faida ya kazi ya Kristo msalabani.

15:18 Na hakuna tumaini kwa waamini waliokufa **katika Kristo.** Kama Kristo hakufufuka, imani yao haikuwa na faida. Maneno haya **wao waliolala** yanasema juu ya miili ya waamini. Hatusomi kamwe ndani ya Agano Jipyu juu ya nafsi ikilala usingizi. Wakati mwaamini anapokufa, nafsi yake inafika karibu na Kristo, na tunasoma juu ya mwili ukilala kaburini.

Inatupasa kusema kidogo juu ya neno hili **potea.** Maana yake haiko kamwe maangamizi au kutokuwa. Linasema juu ya uharibifu wa kusudi ambalo mtu huyu aliumbwa.

15:19 Kama Kristo hakufufuka, waamini walio hai ni katika hali mbaya sawasawa na wale waliokufa. Wamedanganywa vilevile. Wao ni **masikini ku-**

liko watu wote. Bila shaka Paulo alifikiri juu ya huzuni, maumivu, na mateso Wakristo wanayopata. Ingekuwa huzuni kabisa kuvumilia mateso namna hii bure.

15:20 Halafu Paulo alitangaza na sauti ya kushinda ya kwamba Kristo alifufuliwa kweli. **Lakini sasa Kristo amefufuliwa toka wafu, ... malimbuko yao waliolala.** Ndani ya Maandiko tunasoma juu ya ufufuko *wa* wafu, na ufufuko *toka* wafu. Ndani ya mashairi yaliyotangulia tulisoma zaidi juu ya ufufuko *wa* wafu. Ndani yao Paulo alionyesha kwamba wafu wanafufuliwa kweli. Lakini Kristo alifufuliwa *toka* wafu, maana yake si wafu wote waliofufuliwa wakati Kristo alipofufuka. Wafu wote watafufuliwa, lakini ufufuko wa Kristo na wa waamini tu ni ufufuko *toka katikati ya* wafu.

15:21 Kufa kuliletwa na mtu ulimwenguni. **Mtu** huyu alikuwa Adamu. Kwa sababu ya zambi yake, kufa kuliletwa kwa watu wote. Mungu alituma Mwana wake duniani kama **Mtu kurejeza** kazi ya mtu wa kwanza na kuyanyua waamini kwa hali ya baraka kipimo wasichoweza kujua kamwe ndani ya Adamu. Hivi **ufufuko wa wafu uliletwa** kwa njia ya **Mtu** Kristo Yesu.

15:22 Adamu na Kristo wanajulikana kama wakubwa wa jamii mbili za watu. Ni kusema kwamba matendo yao yanagusa maisha ya watu ndani ya jamii zao. Wazao **wote wa Adamu wanakufa.** **Hivyo wote katika Kristo watapatizwa uhai.** Watu wengine wamesema shairi hili linafundisha kwamba watu wote wataokolewa. Wanasema watu wote waliokufa katika Adamu watapatizwa uhai ndani ya Kristo, na ya kwamba mwishoni wataokolewa. Lakini shairi hili halisemi hivi. Maneno makubwa ndani ya shairi hili ni **katika Adamu na katika Kristo.** **Wote walio katika Adamu wanakufa.** **Wote walio katika Kristo watapatizwa uhai,**

maana waamini ndani ya Bwana Yesu Kristo tu watafuliwa toka wafu na kukaa pamoja naye kwa milele. Ndani ya shairi 23 tunasoma juu ya **wote watapatizwa uhai**, ndio wale walio watu wa Kristo wakati atakapokuja, lakini si adui za Kristo – wao watawekwa chini ya miguu yake (sh. 25).

15:23 Halafu tunaona mafungu ya wale waliofufuliwa kwa **ufufuko** wa kwanza. Ufufuko wa kwanza ni wa **Kristo** mwenyewe. Anaitwa **malimbuko** hapa. Malimbuko ndiyo nusu ya ngano ya kukomea toka shamba li-lilokuwa karibu kuvunwa. Walikuwa arabuni ya ufufuko utakaofuata. Maana yake haiko ya kwamba Kristo alifufuliwa kwanza. Tunasoma juu ya wengine waliofufuliwa katika Agano la Kale. Ndani ya Agano Jipyä tunasoma juu ya ufufuko wa Lazaro, mwana wa mjane, na binti ya Yairo. Lakini ufufuko wa Kristo ulikuwa namna nyingine. Wafu wale waliofufuliwa walikufa tena, lakini Kristo alifufuliwa na hatakuwa tena kamwe. Alifufuliwa kuishi na uwezo wa uzima usiokwisha kamwe. Alifufuka na mwili uliotukuzwa.

Fungu la pili katika ufufuko wa kwanza wanaitwa **watu wa Kristo kwa kutokea kwake.** Fungu hili ni waamini watakaofufuliwa wakati Kristo atakapokuja tena mara ya kwanza kwa mawingu. Vilevile ni waamini wale watakaokufa kwa wakati wa Mateso na watakaofufuliwa kwa mwisho wa muda ule wa taabu, wakati Kristo atakaporudi kutawala. Kama Kristo atakavyokuja kwa mafungu, ni vivyo hivyo na ufufuko wa watakatifu wake. Si watu wote waliokufa tangu zamani watakaofufuliwa kwa wakati wa ufufuko wa kwanza, lakini watu walioamini Kristo tu.

Watu wengine wanafundisha kwamba waamini waaminifu tu wa Kristo, au wale waliokuwa washindaji watafufuliwa kwa wakati huu, lakini Maandiko yanaonyesha wazi kwamba neno hili si

kweli. Wote **walio watu wa Kristo** watafufuliwa wakati atakapokuja.

15:24 Tunaamini ya kwamba maneno haya: **Halafu mwisho unakuja**, yanasema juu ya **mwisho** wa *ufifuko*. Kwa mwisho wa utawala wa Kristo kwa miaka elfu moja, wakati atakapokwisha kushinda adui zake zote, waovu waliokufa ndani ya zambi zao watafufuliwa. Huu utakuwa ufufuko wa mwisho. Wote waliokufa bila kuamini Kristo watasi mama mbele ya Kiti Kikubwa Cheupe na kusikia habari za hukumu yao.

Kwa mwisho wa utawala wa Kristo kwa miaka elfu moja, na kuangamizwa kwa Shetani (Ufu. 20:7-10), Bwana Yesu atatoa **ufalme kwa Mungu Baba**. Kwa wakati ule atakuwa ameondosha **utawala wote, na mamlaka yote, na uwemo wote**. Kufika saa ile Bwana Yesu Kristo atakuwa ametawala kama *Mwana wa watu*, kama Mpatanishi wa Mungu na watu. Kwa mwisho wa miaka elfu moja makusudi yote ya Mungu kwa dunia yatakuwa yametimizwa vizuri. Adui zote watakuwa wameharibiwa. Halafu utawala wa Kristo kama *Mwana wa watu* utakombolewa na ufalme wa milele mbinguni. Utawala wake kama *Mwana wa Mungu* mbinguni utaendelea kwa milele.

15:25 Shairi hili linasema tena wazi-wazi ya kwamba Kristo atakaa kutawala kufika wakati maasi na uadui wote pia utakapokwisha kushindwa.

15:26 Hata ndani ya muda wa utawala wa miaka elfu moja wa Kristo watu watakufa, zaidi wale wanaoasi Bwana waziwazi. Lakini kwa wakati wa hukumu ya Kiti Kikubwa Cheupe **mauti** na Gehena zitatupwa ndani ya ziwa la moto.

15:27 Mungu ameamuru kwa **vitu vyote kuwekwa** chini ya **miguu** ya Bwana Yesu. Ndiyo, wakati Mungu anapoweka vitu vyote chini ya miguu ya Kristo, ni wazi ya kwamba hajiweki mwenyewe chini yake.

15:28 Hata wakati **vitu vyote** vita-

kapokwisha kuwekwa chini ya Mwana, Mwana mwenyewe atakaa kuwa **chini ya Mungu** kwa milele.

15:29 Ni nguvu sana kufahamu shairi hili. Watu wamelieleza kwa njia mbalimbali. Kwa mfano, wengine wamesema kwamba waamini waliokuwa hai waliweza kubatizwa kwa ajili ya wale waliokuwa bila kubatizwa. Hakuna mawazo namna hii ndani ya Biblia, hivi tunakataa elezo hili. Watu wengine wanafikiri kwamba maana ya kubatizwa kwa ajili ya wafu ni ya kwamba tunaji-hesabu wenyewe kama tumefariki. Labda hii ndiyo maana yake, lakini hailingani na maneno yanayotangulia na kufuata.

Elezo linalolingana vizuri kupita ndilo hili: Kwa wakati Paulo alipoandika, Wakristo walioonyesha imani yao wazi waliteswa sana, zaidi kwa wakati wa ubatizo wao. Mara nydingi wale walioshuhudia Kristo wazi mbele ya watu waliuawa nyuma ya ubatizo wao. Lakini neno hili halikuzuiza wengine hata kidogo wasiokolewe, na kuchukua nafasi yao wenyewe kubatizwa. Ni kama kuli-kuwa na waamini wapya tayari kila mara kuingia pahali pa wale walioteswa na hata kuuawa kwa ushuhuda wao kwa Kristo. Wakati Wakristo wapya hawa walipoingia maji, ilikuwa sawasawa **walibatizwa kwa au kwa pahali pa** (Kiyunani *huper*) wafu. Hivi maana ya **wafu** ndio wale waliokuwa wamekuwa kwa sababu ya ushuhuda mhodari wao kwa Kristo. Halafu mtume alionyesha kwamba si faida kubatizwa kwa pahali pa wale waliokwisha kufa kama hakuna ufufuko toka wafu. **Kama wafu hawafufuliwi kamwe, kwa nini wanabatizwa kwa ajili yao?**

15:30 Na sisi, **kwa nini tunasimama katika hatari kila saa?** Mtume alikuwa katika hatari saa zote. Kwa sababu ya kuhubiri Habari Njema bila woga alikutana na adui kila pahali alipokwenda. Watu wengine walifanya shauri ku-

mwua. Angaliweza kuepuka maneno haya yote kwa njia ya kuacha kukiri kwamba yeze ni Mkristo. Ndiyo, ingalikuwa akili njema kwaye kufanya hivi kama hakuna ufufuko.

15:31 Ndiyo, ndugu, kwa sababu ya kujisifu kwangu juu yenu katika Kristo Yesu, ninakuwa kila siku. Alifurahi juu yao kama watoto wake katika Kristo, na alikuwa katika hatari ya kufa kila siku.

15:32 Mtume alikumbuka sasa mteso makali aliyopata kwa **Efeso**. Hatufikiri kwamba alipigana na nyama wakali pale, lakini alisema juu ya watu waovu kama **nyama** wakali. Hatujui kama alisema juu ya tukio gani. Ni wazi ya kwamba ingalikuwa upumbavu kwa yeze kupiga vita ya hatari namna hii kama asipojua kabisa kwamba wafu watafufuliwa. Ingalikuwa akili njema kupita kwaye kusema: “**Kama wafu hawatafufuliwa, ‘Tule, tunywe, kwa sababu kesho tutakufa.’**”

Mara nyingine tunasikia watu wakisema, wangalichagua kuwa Wakristo hata kama hakuna neno lingine nyuma ya maisha haya ya sasa. Lakini Paulo hakufikiri hivi. Kama watu hasingefufuliwa, watafikiri vizuri wajipendeze na maneno mazuri yote ya maisha *ya sasa*. Hakuna furaha nyingine wanayoweza kutazamia. Lakini tukijua kwamba kuna ufufuko, haifai hata kidogo kwa sisi kuishi kwa maneno ya dunia ya sasa tu.

15:33 Haifai Wakorinto **wadanganyike**, lakini wakumbuke kwamba **mzungumuzo mabaya yanaharibu adabu**. Paulo alisema juu ya walimu wa uwongo ambaa walikuwa wameingia kanisa kwa Korinto na waliokana kwamba kuna ufufuko. Wakristo wafahamu kwamba haiwezekani kukaa pamoja na watu **waovu** au mafundisho maovu bila kuchafuwa nayo. Mafundisho mabaya hayatuongozi kuishi maisha matakatifu.

15:34 Ilifaa Wakorinto kuamka kwa haki, wasifanye zambi. Haifai wadanganywe na mafundisho maovu. **We-ningine hawajui Mungu: ninasema hili kwa kuwapatiza ninyi haya.** Watu wengi wanafikiri mafundisho ya shairi hili ni ya kwamba kuna wanaume na wanawake wengi wasiosikia Habari Njema kamwe, na ya kwamba inapasa Wakristo kuwa na haya kwa sababu hawajahubiri Habari Njema kwa dunia nzima. Ni kweli, lakini tunafikiri maana ya mashairi haya ni ya kwamba ndani ya kanisa kwa Korinto kulikuwa na watu **wasiojua Mungu**. Hawakuwa waamini wa kweli. Walikuwa mbwa za mwitu waliovaa mavazi ya kondoo, ndio walimu wa uwongo waliopata njia kuingia kanisa kwa siri. Ilikuwa **haya** kwa Wakorinto walioruhusu watu hawa kukaa pamoja na Wakristo na kufundisha mafundisho maovu. Ukosefu wa uangalifu wa viongozi uliacha watu wale waovu kukaa katikati ya Wakristo na kupunguza roho safi ya kanisa, na ulifungua njia kwa mafundisho namna namna ya uwongo kuingia.

B. Mawazo juu ya mabishano ya ufufuko (15:35-57)

15:35 Ndani ya mashairi 35-49 mtume alijibu maulizo mawili ya watu walikuwa na shaka juu ya ufufuko wa mwili. Ulizo la kwanza ndilo: “**Wafu wanafufuliwa namna gani?**” Ulizo la pili ni: “**Wanakuwa kwa mwili gani?**”

15:36 Jibu la ulizo la kwanza ni ndani ya shairi 36. Mfano mzuri sana wa ufufuko ndio mbegu. Inapasa mbegu kupandwa ndani ya udongo na kufa mbele ya pando kutoka. Ni ajabu kubwa kuwaza juu ya siri ya uzima unaofichwa ndani ya kila mbegu ndogo. Kweli ni siri kubwa tusiyyeweza kufahamu. Tunajua tu ya kwamba mbegu inawekwa ndani ya udongo, ndio mwanzo wa uzima unaotoka ndani ya mbegu iliyokufa.

15:37 Halafu tunasoma juu ya ulizo

la pili. Paulo alieleza ya kwamba wakati **unapopanda** punje, **hupandi** mwili ule **utakaokuwa**, **lakini** unapanda **mbegu** tupu, **hakose ya ngano**, **hakose ya namna nyingine**. Neno hili linatufahamisha nini? Pando linaloota ni sawasawa na mbegu? Sivyo, pando si sawasawa na mbegu; lakini mbegu na pando yanaunganika. Hakuna pando bila mbegu. Na vilevile pando linapata maneno mengine toka mbegu. Ni vivyo hivyo kwa ufufuko.

15:38 **Mungu** anatoa **mwili** kwa namna ya mbegu iliyopandwa, na hivi **kila mbegu** ina namna yake ya pando. Maneno yote yanayoonekana ndani ya pando, rangi yake, ukubwa wake, ua na jani lake, yanatoka kwa mbegu iliyopandwa.

15:39 Halafu Paulo alionyesha kwamba utukufu wa mwili wa ufufuko utakuwa namna nyingine na utukufu wa miili yetu ya sasa. Nyama ndiyo mfano wa kweli hii. **Nyama yote si nyama sawasawa.** Kuna **nyama** ya watu, **mnofu ya nyama**, nyama ya **samaki**, na ya **ndege**. Nyama hizi zote zinafanana, lakini si sawasawa kabisa.

15:40 Kama kuna tofauti ya utukufu wa **miili** ya mbingu (ndiyo nyota, vivyo hivyo) na miili ya dunia, vivyo hivyo mwili wa mwamini wakati wa sasa ni namna nyingine na ule ambaa atakuwa nao nyuma ya kufa.

15:41 Kuna tofauti ya **utukufu** hata kwa miili ya mbingu, ndiyo juu, mwezi, na nyota. Kwa mfano, **juu** linangaa kupita **mwezi**, na kungaa kwa nyota zote **si sawasawa**.

Zaidi ya wenye kueleza maana ya Maandiko wanafikiri Paulo alifundisha kwamba utukufu wa mwili wa ufufuko utakuwa mbali na utukufu wa mwili ambaa tunao duniani kwa wakati wa sasa. Hawafikiri shairi 41 linaonyesha kwamba waamini mbinguni watakuwa na utukufu wa vipimo mbalimbali.

Lakini mashairi mengine ya maandiko yanaonyesha wazi kwamba hatutakuwa wote mfano mmoja mbinguni. Hata kama tukifanana na Bwana Yesu kwa roho, maana hatutakuwa na zambi, si kusema kwamba *tutaonekana* kama yeze kwa njia ya mwili. Ataonekana wazi kama Bwana Yesu kwa milele. Vivyo hivyo kila Mkristo atajulikana kwa njia ya nafsi yake mwenyewe iliyo namna nyingine na ile ya waamini wengine. Na zawabu watakayopokea kwa kitu cha hukumu cha Kristo itakuwa kipimo mbalimbali kupatana na kipimo cha uaminifu wa utumishi wao. Wote watakaa na furaha tele mbinguni, lakini kipimo cha furaha ya wengine kitakuwa kikubwa kupita. Kama wapotevu katika ziwa la moto watakapoteswa kwa kipimo mbalimbali, kupatana na zambi walizotenda, vivyo hivyo waamini watafurahi kwa kipimo mbalimbali, kupatana na maneno waliofanya kama waamini.

15:42 Mashairi 42-49 yanaonyesha kwamba miili tulio nayo itageuka kuwa namna nyingine kwa milele. **Mwili wa mwamini unapandwa katika kuoza, utafufuliwa katika kutokuoza.** Kwa wakati wa sasa miili yetu inapata ugonjwa, na inakufa. Wakati inapoweckwa ndani ya kaburi imageuka vumbi tena. Lakini haitakuwa hivi na miili ya ufufuko. Haitapatwa na ugonjwa na kuoza tena.

15:43 Mwili wa sasa **unapandwa katika haya**. Maiti haioneekani vizuri na yenye utukufu. Lakini mwili huu **utafufuliwa katika utukufu**. Hautakuwa na vikunjo vya ngozi, alama za vidonda na uzee, na zambi.

Unapandwa katika uzaifu, unafufuliwa katika uwezo. Wakati tunapogeuka wazee, **uzaiyu** wetu unaongezeka kufika saa ya mauti yetu. Kwa wakati wa milele miili yetu haitataabishwa na vizuizo hivi tena, lakini itakuwa na uwezo ambaa haikuwa nao

kwa wakati wa sasa. Kwa mfano, nyuma ya ufufuko wake, Bwana Yesu Kristo aliweza kuingia chumba chenye milango iliyofungwa.

15:44 Unapandwa mwili wa asili, unafufuliwa mwili wa roho. Maana ya roho hapa *haiko* ukosefu wa kuonekana. Watu wengine wanafikiri kwamba wakati wa ufufuko tutakuwa roho bila miili. Hii si maana ya mashairi haya, na *haiko* kweli. Tunajua kwamba mwili wa ufufuko wa Bwana Yesu ulikuwa na mwili na mifupa, kwa sababu alisema, “Roho haina mwili na mifupa, kama munavyoniona mimi kuwa nayo” (Lk. 24:39). **Mwili wa asili** ndiyo mwili kwa dunia hii, na **mwili wa roho** unafaa kwa kuishi mbinguni. Mwili wa asili unatawaliwa karibu saa zote na nafsi, lakini **mwili wa roho** utatawaliwa na roho, na utakuwa kweli mtumishi wa roho.

Mungu aliumba mtu na roho, nafsi na mwili. Alitaja roho kwanza kila mara kwa sababu alitaka roho kujulikana zaidi. Lakini wakati zambi ilipoingia duniani, neno hili liligeuka, na watu wanasema kila mara “mwili, nafsi na roho.” Walimpa mwili pahali pa kwanza, ndipo Mungu alikusudi kwa roho kuwa napo. Haitakuwa hivi wakati wa ufufuko. Roho itakuwa kwa pahali pa amri na utawala, kama Mungu alivyokusudi toka mwanzo.

15:45 Hivi ilivyoandikwa: “**Mtu wa kwanza, Adamu, alikuwa nafsi ya uhai.**” **Adamu wa mwisho alikuwa roho yenye kupatiza uhai.** Hapa tena tunona tofauti ya **Adamu ya kwanza** na Bwana Yesu Kristo. Mungu alipuliza pumzi ya uzima ndani ya pua ya Adamu, naye alikuwa nafsi ya uhai (Mwa. 2:7). Wazao wake wote wana tabia yake. **Adamu wa mwisho**, Mwokozi, **alikuwa roho yenye kupatiza uzima** (Yn. 5:21, 26). Adamu wa kwanza *alipewa uzima* wa mwili, lakini Kristo *analeta uzima* wa milele kwa watu wengine.

Eerdman anatoa elezo hili:

Kama wazao wa Adamu, tulifanywa kuwa sawasawa naye, nafsi zilizo hai ndani ya miili yenye kufa, na tukifanana na wazazi wetu wa dunia. Lakini kama wafuata wa Kristo tutavikwa na miili isiyokufa, na kufanana na ule wa Bwana wetu wa mbinguni.¹⁵

15:46 Halafu mtume anaonyesha kweli kubwa ya utaratibu wa Mungu ndani ya ulimwengu, ndiyo ya kwamba **ule wa roho si wa kwanza, lakini ule wa asili, kisha ule wa roho.** Neno hili linaweza kuelezwa kwa njia tatu: Adamu, mtu **wa asili**, alikuwa kwanza tangu mwanzo wa historia ya watu duniani; Yesu, Mtu **wa roho**, alitokea nyuma. Neno la pili ndilo hili: tulizaliwa duniani kama viumbe vyta **asili**; wakati tunapozaliwa tena, tunageuka viumbe vyta **roho**. Mwishoni, tulipokea kwanza miili ya **asili**, kisha kwa ufufuko tunapozaliwa miili ya **roho**.

15:47 Mtu wa kwanza alitoka katika dunia, mwenye udongo. Ni kusema mwanzo wake ulikuwa **wa dunia** na ya kwamba tabia yake ilikuwa wa dunia. **Alifanywa** toka **mavumbi** ya udongo, na ni kama maisha yake yali-fungana na dunia hii. **Mtu wa pili ni Bwana aliyetoka mbinguni.**

15:48 Watu wawili walitajwa ndani ya shairi 45. Yesu alikuwa wa pili. Alikuwa tangu milele, lakini kama Mtu, alikuja nyuma ya Adamu. Alikuja toka mbingu, na kila kitu alichofanya kilikuwa cha **mbingu** na cha roho, si cha dunia na nafsi.

Watu wote wanafuata mmoja wa wakubwa hawa. Wale wanaozaa na Adamu wanariti tabia yake. Na wale wanaozaliwa na Kristo ni watu wa **mbingu**.

15:49 Kama tulivyochukua tabia Adamu wakati tulipozaliwa duniani, **vivyo hivyo tutachukua sura ya Kristo** ndani ya miili yetu ya ufufuko.

15:50 Halafu mtume alianza kusema juu ya namna gani miili ya waamini walio hai, na wa wale watakaokwisha kufa, itakavyogeuzwa kwa wakati wa kurudi kwa Bwana. Alianza na kusema ya kwamba **nyama na damu haziwezi kuriti ufalme wa Mungu**. Ni kusema kwamba mwili tulio nao sasa haufai kwa **ufalme wa Mungu**, ndipo pahali tutakapokaa kwa milele. Na vilevile **kuoza** hakuwezi kuriti **kutokuoza**. Miili yetu inayoshikwa na ugonjwa, uharibifu na ubovu haifaa kwa pahali pasipo kuoza. Basi namna gani miili ya waamini iliyo hai inaweza kutayarishwa waweze kuishi mbinguni?

15:51 Jibu kwa ulizo hili ni **siri**. Kama tulivyosema mbele, **siri** ni kweli watu wasiyojua mbele, lakini sasa Mungu aliifunua kwa mitume, nao walifunua kwa sisi.

Sisi sote hatutalala, maana si waamini wote watakuwa wamekufa wakati Bwana atakaporudi. Lakini si neno kama tulikufa, au tungali hai, **sisi sote tutabdalika**. Kweli ya ufufuko si siri, kwani tunasoma juu yake ndani ya Agano la Kale, lakini habari ya kwamba watu wengine hawatakufa, na ya kwamba watakatifu walio kwanza hai watabadilika wakati Bwana atakaporudi, ni habari watu wasizoja mbele.

15:52 Watabadilika kwa dakika moja, **kwa kufunga na kufungua jicho, kwa baragumu ya mwisho**. Maana ya **baragumu ya mwisho** hii si mwisho ya dunia, wala baragumu ya mwisho ndani ya kitabu cha Ufunuo. Ni **baragumu ya Mungu** itakayosikiwa wakati Kristo atakapokuja kwa hewa kwa watakatifu wake (1 Tes. 4:16). Wakati **baragumu** itakaposikiwa, **wafu watafufuliwa wasiwe na kuoza, na tutabdalika**. Lita-kuwa tukio la kushangaza sanasana wakati uvumbi wa wafu wote wali-oamini Bwana tangu mia za miaka utakapotoka udongo na bahari! Ni nguvu kwa sisi watu kulifahamu, lakini

mwamini mnyenyeketu anaweza ku-likubali kwa imani.

15:53 Tunafikiri shairi 53 linasema juu ya waamini namna mbili wakati Kristo atakaporudia. **Wenye kuoza** ndio wale wenye miili iliyogeuka kuwa uvumbi. **Watavaa kutokuoza**. Lakini **huu wa mauti** ndio wale walio kwanza hai, lakini walio katika hatari ya kufa. Miili yao **itavaa kutokufa**.

15:54 **Wakati** wafu walioamini Kristo watakapofufuliwa, na walio hai wanapobadilishwa pamoja nao, **wakati ule litakapotimia neno lililoandikwa: “Mauti imemezwa kwa kushinda”** (Isa. 25:8). Neno bora kabisa!

15:55 Labda waamini wataimbamano neno haya na kuzihaki kidogo saa watakapopanda kukutana na Bwana katika hewa. Ni kama wanacheka **mauti** kwani **haina uchungu** tena kwa waamini na ilishinda kuwafunga. Hawaogopi **mauti** tena kwa sababu wanajua zambi zao zimesamehewa, na wanasmama mbele ya Mungu kwa sababu wamekubaliwa ndani ya Mwana wake mpendwa.

15:56 **Mauti** yana **uchungu** kwa mtu kwa sababu ya **zambi** tu. Ni watu walio na zambi wasizokiri wanaoogopa kufa. Hatuhitaji kuogopa mauti kama tukijua zambi zetu zimesamehewa. Lakini kama zamiri zetu zikikaa kutushitaki juu ya zambi, mauti ni neno la kuogofya – mwanzo wa azabu ya milele.

Nguvu ya zambi ni sheria, maana ni **sheria** inayohukumu mwenye zambi. Inatangaza maangamizi ya wote wasiotii maagizo matakatifu ya Mungu. Imesemwa kwamba hakuna mauti bila zambi. Na kama sheria isivyokuwa, hukumu isivyokuwa vilevile.

15:57 Kwa njia ya kuamini Bwana **tunashinda** mauti na kaburi. Mauti haina uchungu kwa sisi tena kwa sababu ya mauti ya **Bwana wetu Yesu Kristo** juu ya msalaba.

C. Maonyo ya mwisho kwa sababu ya ufufuko (15:58)

Kwa sababu ya hakika ya ufufuko, na kwa sababu si neno bure kuamini Kristo, mtume Paulo alionya ndugu zake wapenzi, “**musimame imara, musitikisike, mukizidi siku zote kutenda kazi ya Bwana, kwa sababu munajua ya kuwa kazi yenu si bure katika Bwana.**” Kweli ya ufufuko imageuza maneno yote. Inaleta tumaini na kutusimamisha bila kusikitika, na inatuwezesha kudumu hata katika maneno magumu.

5. MAONYO YA MWISHO YA PAULO (Sura 16)

A. Juu ya sadaka (16:1-4)

16:1 Shairi la kwanza la sura 16 ni juu ya **sadaka** ambayo kanisa katika Korinto watakusanya na kutuma kwa **watakatifu** wenyewe mahitaji katika Yerusalem. Hatujui sababu ya umasikini wao. Labda ulikuwa tunda la wakati wa njaa (Mdo. 11:28-30). Au labda Wayuda wale walioamini Kristo waliondolewa katika jamii na rafiki wasioamini, na watu wa inchi. Bila shaka hawakuwa na kazi ya mshahara tena, na waliteswa kwa njia mbalimbali, na ukosefu wa mali uliwasukuma kuacha kuamini Kristo. Paulo alikuwa **ameamuru makanisa ya Galatia** mbele juu ya neno hili, na sasa alionya Wakorinto kufanya vivyo hivyo.

16:2 Hata kama maagizo ndani ya shairi 2 yalikuwa kwa sadaka ile moja, ni maagizo kwa wakati wa sasa vilevile. Tunaona kwanza ya kwamba iliwapasa **kuweka akiba** ya mali **siku ya kwanza ya juma**. Neno hili linaonyesha kwamba Wakristo wa kwanza hawakufikiri kwamba iliwapasa kushika siku ya saba, ndiyo sabato. Bwana alikuwa amefufuliwa siku ya kwanza ya juma. Siku ya Pentekote ilikuwa siku ya kwanza ya juma, na wanafunzi walikutana siku ya kwanza ya juma kuvunja mkate (Mdo. 20:7). Sasa waliagizwa **kuweka akiba**

kwa watakatifu **siku ya kwanza ya juma**.

Neno kubwa la pili ndilo hili: maagizo haya yalikuwa kwa **kila mtu**, si neno kama alikuwa tajiri au masikini, mtumwa au huru. Ilipasa kila mtu kushiriki ndani ya sadaka hii ya kutoa ya mali yao.

Zaidi ya ile, iliwapasa kufanya hivi na utaratibu. **Siku ya kwanza ya juma** iliwapasa **kuweka akiba** toka mali nyingine **kwa kadiri ya mapato yao**, ndiyo mali waliyokwisha kupokea.

Ili sadaka zisifanyike wakati nitakapokuja. Mtume alitaka wawaze juu ya sadaka hii mbele, na kuitayarisha mbele ya kufika kwake.

16:3 Mashairi 3 na 4 yanaonyesha namna gani inapasa kulinda mali Wakristo wanayotoa. Haifai kwa mtu mmoja peke yake kulinda mali ile. Haikufaa hata kwa Paulo kupokea mali hii peke yake. Tuone vilevile ya kwamba haikufaa kwa Paulo peke yake kuchagua nani atapeleka za-wadi hii kwa Yerusalem. Watu wa kanisa walichagua wajumbe hawa. Wakati walipokwisha kufanya hivi Paulo **atawatuma kwa Yerusalem**.

16:4 Kama ikifaa kwa kwa mtume **kwenda** vilevile, ndugu za kanisa watakwenda pamoja naye. Ona ya kwamba alisema “**watasafiri pamoja nami.**” Hakusema “nitakwenda pamoja nao.” Labda neno hili lilionyesha amri yake kama mtume.

B. Juu ya shauri lake mwenyewe (16:5-9)

16:5 Ndani ya mashairi 5-9 Paulo ali-julisha shauri lake. Alikuwa katika Efeso wakati alipoandika barua hii. Toka pale alikusudi **kupita kati ya Makedonia**. Nyuma yake alitaraji kwenda kusini hata Korinto.

16:6-8 Labda atashinda pamoja na waamini katika Korinto **kwa wakati wa baridi**, na halafu wataweza kumsafarisha **pahali gani** atakapokwenda toka

pale. Lakini hatawaona sasa wakati alipokwenda Makedonia, lakini nyuma alitaraji kushinda pamoja nao kwa wakati, **kwa ruhusa ya Bwana.** Mbele ya kuondokea Makedonia, Paulo alifikiri **atacaa kwa Efeso hata Pentekote.** Shairi hili 8 linaonyesha kwamba 1Wakorinto iliandikwa toka Efeso.

16:9 Paulo aliona mlango wazi sana kwa kutumikia Kristo kwa Efeso kwa wakati ule. Pamoja na ile alifahamu vilevile kwamba kulikuwa na **adui wengi.** Ni vivyo hivyo sasa kwa utumishi wetu kwa Kristo: Mashamba ni tayari kwa mavuno, lakini kuna adui asiyelala kamwe, anayejaribu kuzuiza, kuleta matengo, na kushindana na kazi ya Bwana kwa kila njia!

C. Maonyo ya mwisho na salamu (16:10-24)

16:10 Halafu mtume alisema neno juu ya **Timoteo** aliyekuwa mtumishi kijana aliyetumikia Bwana na roho yote. Timoteo akifikia Korinto, ilipasa waamini kumpokea **pasipo woga.** Labda Timoteo alikosa ukaramisu. Au labda maana ya onyo hili ilikuwa aweze kukaa pamoja nao **bila woga** kama mtumishi wa Bwana. Masemo ya Paulo, “**Anafanya kazi ya Bwana kama mimi**” yanatufikirisha kwamba hili ndilo maana ya kweli.

16:11 Kwa sababu ya utumishi mwanminifu wa Timoteo kwa Kristo, **haifai mtu ye yote kumzaraau**, lakini **wamsindikize kwa safari yake katika salama**, ili aweze kurudi karibu na Paulo. Mtume alitazamia kukutana na Timoteo **na ndugu zetu.**

16:12 Lakini kwa habari za Apolo, Paulo alikuwa **amensihi** kufika kwa Korinto **pamoja na ndugu.** Apolo hakufikiri kwamba neno hili lilikuwa mapenzi ya Mungu kwaye kwa wakati ule, lakini alisema atafikia Korinto wakati atakapopata nafasi nyuma. Shairi 12 lina faida

kwa sisi na katuonyesha namna watumishi wa Bwana walivyopendana na kuheshimiana. Linaonyesha vilevile ya kwamba kila mtumishi alikuwa huru kuongozwa na Bwana tu bila kutii magizo ya wengine. Hata Paulo mwenyewe hakuwa na amri kusema na Apolo nini ilimpasa kufanya. Ironside alisema kwamba shairi hili “linaonyesha namna gani Mungu anaongoza watumishi wake ndani ya kazi yao kwa yeye.”¹⁶

16:13, 14 Sasa Paulo alikuwa na maonyo mengine kwa waamini. Sharti **wangalie** wakati wote, **wasimame imara katika imani**, wawe **wahodari** na wenye **nguvu.** Labda Paulo alikumbuka tena hatari ya walimu wa uwongo. Lazima waamini wakae na ange kwa kila saa. Watende na uhodari wa kweli. Mwishoni, wawe **wenye nguvu** katika Bwana. **Maneno yao yote** yafanyewe katika **mapendo.** Hivi wataishi maisha ya kujitoa wenyewe kwa Mungu na kwa watu wengine.

16:15 Halafu kulikuwa na maonyo juu ya **nyumba ya Stefano.** Wakristo hawa walikuwa **malimbuko ya Akaya**, maana walikuwa waamini wa kwanza katika **Akaya.** Ni kama tangu wokovu wao walijitoa kabisa **kutumikia watakatifu.** Tulisoma juu ya **nyumba ya Stefano** mbele ndani ya 1:16. Pale tulisoma ya kwamba Paulo alibatiza watu wa nyumba ile. Watu wengine wamefikiri ya kwamba kulikuwa na watoto wachanga nyumbani. Hivi wanawaza ni vizuri kubatiza watoto wachanga. Lakini shairi hili linaonyesha kwamba watoto wachanga hawakuwa ndani ya nyumba ile, kwani linasema wazi ya kwamba **wamejitoa wenyewe** katika kazi ya **kutumikia watakatifu.**

16:16 Mtume alionya Wakristo **kutii watu kama hawa, na kila mtu anayefanya kazi pamoja nao na kuji-taabisha.** Agano Jipyä linatufundisha ya kwamba inapasa kuonyesha heshima na mapendo kwa watu wale ambao wanaji-

toa kutumikia Kristo. Kama Wakristo wakikaa kufanya hivi, kama wangeepuka matengo na wivu nyinyi.

16:17 Kufika kwa Stefano, Fortunato na Akaiko kulifurahisha Paulo sana. **Walimtimilizia** maneno Wakorinto waliyokosa kufanya. Au labda watu hawa walitimiza maneno Wakorinto *wasiyoweza* kufanya kwa sababu hawakuwa karibu.

16:18 Waliletea Paulo habari toka Wakorinto, na walipeleka habari za Paulo kwa kanisa lao. Paulo alisema tena kwa waamini wa Korinto kwamba iliwapasa kuheshimu na kupenda watu wa namna hii.

16:19 Makanisa ya Asia yalikuwa makusanyiko ya Wakristo ndani ya wilaya ya Asia (kwa wakati wa sasa inaitwa *Asia Ndogo*). Efeso ulikuwa mji mkubwa wa wilaya hii. Ni kama **Akila na Prisila** walikaa pale kwa wakati ule. Mbele walikaa kwa Korinto vilevile. Kazi ya **Akila** ilikuwa kufanya hema na alifanya kazi hii pamoja na Paulo. Maneno haya **kanisa linalokutana ndani ya nyumba yao** yanatuonyesha namna Wakristo kwa wakati wa mwanzo walikusanyika ndani ya nyumba zao kwa ibada, maombi, na ushirika. Kisha wali-kwenda kuhubiri Habari Njema kwa pahali pa kazi, kwa soko, gerezani, na pahali po pote Mungu alipowaweka.

16:20 Ndugu zote kanisani walituma salamu yao kwa waamini wenzao katika Korinto. Mtume alisema na waamini **kusalimiana kwa busu takatifu**. Kwa wakati ule ilikuwa desturi hata kwa wanaume kusalimiana na **busu**. Maana ya **busu takatifu** ni salamu bila unafiki wala uchafu. Kwa wakati wa sasa watu wengi wanatawaliwa na tamaa ya mwili, na kusalimiana na busu kunaweza kuwa majoribu kwa maneno mabaya. Hivi mara nyinyi kushika mkono kunakomboa kuleta busu.

16:21 Ilikuwa desturi ya Paulo ku-andikisha barua zake kwa njia ya mmoja

wa wale waliokuwa pamoja naye. Lakini kwa mwisho wa barua aliandika maneno machache ye ye mwenyewe na kuongeza **salamu** yake.

16:22 Neno hili **amelaaniwa** ni *anathema* kwa Kiyunani. Watu **wasiopenda** Bwana Yesu wanalaaniwa hata **sasa**, lakini hukumu yao itaonekana wakati wa kuja kwa Bwana Yesu Kristo. Mkristo ndiye mtu anayependa Mwokozi. Anapenda Bwana Yesu kupita mtu ye yote au kitu cho chote duniani. Kukosa kupenda Mwana wa Mungu ni kukosea Mungu mwenyewe. Ryle aliandika:

Mtume Paulo hakuachii mtu asiypenda Kristo njia kuepuaka hukumu. Inawezekana kwa mtu wa akili nusu tu kuokolewa. Inawezekana kwaye kukosa uhodari, na kushindwa na woga, kama Petro. Inawezekana kwa mtu kuanguka kabisa na kuttenda zambi kubwa, kama Daudi, na kusimama tena. Lakini kama mtu hapendi Kristo, mtu huyu anakosa uzima. Analaaaniwa. Yeye ni kwa njia pana inayofikisha watu kwa ucharibifu.¹⁷

Bwana, kuja! Maneno haya mawili ni tafsiri ya *maranatha*, neno kwa Aramaic, ndiyo lugha iliyotumiwa na Wakristo kwa wakati wa mwanzo.

16:23 Paulo alipenda sana kuandika juu ya **neema**. Alianza na kumaliza barua zake na neno hili kubwa. Ilikuwa alama iliyohakikisha kwamba ye ye ndiye mwandishi wa barua yenye.

16:24 Ndani ya barua hii nzima tulisoma mafundisho ya mtume huyu wa Kristo ambaye alimtumikia na roho yake yote. Alionya, kufariji na kufundisha watto wake katika imani. **Mapendo** yake kwa Wakristo hawa yalioneckana wazi. Wakati waliposoma maneno haya ya mwisho, labda walipata haya kwa sababu waliruhusu walimu wa uwongo kuingia kanisani, na kwa sababu walikuwa na shaka kwamba ye ye ni kweli mtume wa

Kristo, na waliacha mapendo yao ya kwanza kwaye kupunguka.

NOTES

¹ (1:18) Albert Barnes, *Notes on the New Testament, 1 Corinthians*, p. 14.

² (3:9) Charles R. Erdman, *The First Epistle of Paul to the Corinthians*, ukurasa 40.

³ (4:8) H. P. Barker, *Coming Twice*, ukurasa 80.

⁴ (5:2) Erdman, *First Corinthians*, ukurasa 55.

⁵ (6:9) Shairi hili linafundisha juu ya watu wasiozaliwa tena.

⁶ (7:5) Larry Christenson, *The Christian Family*. ukurasa 24.

⁷ (7:15) J. M. Davies, further documentation unavailable.

⁸ (7:17) W. E. Vine, *The Divine Plan of Missions*, ukurasa 63.

⁹ (7:29) Harry A. Ironside, *First Epistle to the Corinthians*, ukurasa 223.

¹⁰ (7:29) Vine, *First Corinthians*, ukurasa 104.

¹¹ (7:33) *Ibid.*, ukurasa 105.

¹² (9:17) Charles C. Ryrie, *The Ryrie Study Bible*, New King James Version, ukurasa 1771.

¹³ (9:21) Charles C. Ryrie, *The Grace of God*, ukurasa 83.

¹⁴ (11:5) Lakini 11:2-16 si zaidi juu ya makusanyiko ya kanisa tu. Watu wengine wanafikiri kwamba wakati mwanamke anapofundisha wanawake au watoto, inampasa kufunika kichwa chake konyesha kwamba ananyenyekea Bwana na viongozi vya kanisa.

¹⁵ (15:45) Erdman, *First Corinthians*, ukurasa 148.

¹⁶ (16:12) Ironside, *First Corinthians*, ukurasa 542.

¹⁷ (16:22) C. Ryle, *Holiness*, ukurasa 235.

tament. (Vol. V, 1 Corinthians). London: Blackie & Son, n.d.

Davies, J.M. *The Epistles to the Corinthians*. Bombay: Gospel Literature Service, 1975.

Erdman, Charles R. *The First Epistle of Paul to the Corinthians*. Philadelphia: Westminster Press, 1928.

Godet, F. L. *The First Epistle to the Corinthians*. Grand Rapids: Zondervan Publishing House, 1971.

Grant, F. W. "I Corinthians," *The Numerical Bible*. Vol. 6, Acts to 2 Corinthians. New York: Loizeaux Bros., 1901.

Hodge, Charles. *An exposition on the First Epistle to the Corinthians*. New York: George H. Doran Company, 1857.

Ironside, H. A. *Addresses on the First Epistle to the Corinthians*. New York: Loizeaux Brothers, 1955.

Johnson, S. Lewis. "First Corinthians," in *The Wycliffe Bible Commentary*. Chicago: Moody Press, 1962.

Kelly, William. *Notes on the First Epistle to the Corinthians*. London: G. Morish, 1878.

Luck, G. Coleman. *First Corinthians*. Chicago: Moody Press, 1958.

Morgan, G. Campbell. *The Corinthian Letters of Paul. An Explanation of I and II Corinthians*. New York: Fleming H. Revell Company, 1946.

Morris, Leon, *The First Epistle of Paul to the Corinthians*. Grand Rapids: Wm. B. Eerdmans Publishing Company, 1966.

Robertson, Archibald and Alfred Plummer. *A Critical and Exegetical Commentary on the First Epistle of St. Paul to the Corinthians*. Edinburgh: T & T Clark, 1911.

Vine, W. E. *First Corinthians*. London: Oliphants Ltd., 1951.

Bibliographie

Barnes, Albert. *Notes on the New Tes-*

BARUA YA PILI KWA WAKORINTO

Utangulizi

I. Nafasi ya pekee katika Kanuni

Walimu wengi wanahubiri juu ya 1 Wakorinto, lakini walimu wachache tu wanafundisha juu ya 2 Wakorinto, lakini ni barua yenye mafundisho ya faida sana.

Barua hii ni *ngumu* kufahamu. Mana ya mashairi mengi si wazi. Kwa nini? 1. Mara nydingine Paulo alisema pamoja na kuzihaki kidogo, lakini haionekani wazi *wakati gani* anafanya hivi. 2. Kwa kufahamu sehemu nydingine za barua hii vizuri tunahitaji habari nydingine juu ya pahali Paulo aliposafiri, watu waliosafiri pamoja naye, na barua alizoandika. 3. Ndani ya barua hii Paulo alionyesha mawazo ya ndani ya roho yake, na si nyepesi kuyafahamu kila mara.

Lakini haifai kuacha maneno haya kutuzuiza, kwani hayafichi kweli kubwa za barua hii.

Mwishoni, watu *wanapenda* barua hii sana na *wanataja* mengi ya mashairi yake.

II. Mwandishi

Karibu watu wote wanakubali kwamba 2 Wakorinto iliandikwa na Paulo. Namna ilivyoandikwa inaonyesha kwamba iliandikwa muda mfupi nyuma ya 1 Wakorinto, na neno hili likubaliwa na walimu wa kujulikana kama Polycarp, Irenaeus, Clement wa Alexandria, Tertulian, Cyprian, na wengine. Kuanza na 175 A.D. maneno mengi yanashuhudu kwamba Paulo aliandika 2 Wakorinto.

Namna barua hii iliandikwa inafunua roho ya Paulo wazi kabisa, kama vilevile barua yake kwa Filemono. Barua hizi mbili zina mafundisho ya elimu nusu kupita barua nydingine za Paulo. Maneno mengine ndani yao yanatufikirisha maandiko ya 1 Wakorinto, Wagalatia, Waroma na Matendo na kuhakikisha kwamba Paulo aliandika barua hii.

III. Tarehe

Ni kama barua ya 2 Wakorinto iliandikwa toka Makedonia, mbele ya mwisho wa mwaka mmoja tangu saa 1 Wakorinto ilipoandikwa. Maandiko mengine ya zamani yanatufikirisha kwamba iliandikwa toka Filipi, karibu na 57 A.D.

IV. Msingi na Jambo Kubwa

Tunapenda barua hii sana kwa sababu inatufunulia roho ya Paulo kupita maandiko yake mengine yote. Inatuonyesha mapendo na bidii yake kubwa kwa kazi ya Bwana, ndiyo kazi ya heshima zaidi. Tunasoma na kushangaa juu ya taabu na mateso ali-yovumilia, na kufahamu uchungu rohoni mwake kwa sababu ya wajuzi wake wabaya.

Habari za kufika kwa Paulo mara ya kwanza kwa Korinto ni ndani ya Matendo 18. Ilikuwa kwa safari yake ya pili ya kuhubiri, na nyuma ya hotuba yake juu ya mlima kwa Atene.

Katika Korinto alitumika pamoja

na Akila na Prisila, na kuhubiri Habari Njema ndani ya sunagogi. Sila na Timoteo walifika toka Makedonia na walifungana pamoja naye ndani ya kazi ya kutangaza Habari Njema kwa mwaka mmoja na nusu (Mdo. 18:11).

Wakati zaidi ya Wayuda walipokataa mahubiri yake, Paulo alianza kuhubiri kwa Mataifa. Wakati watu walipokolewa, Wayuda na Mataifa, viongozi Wayuda walifikisha Paulo mbele ya liwali, ndiye Galio. Lakini Galio aliona mabishano yao bure na alikataa kuhukumu neno hili akisema hana mammaka kuhukumu maneno namna hii.

Nyuma ya hukumu hii Paulo alibaki katika Korinto kwa siku nyingi, kisha alikwenda Kenkurea na Efeso, na safari yake ndefu kurudi Kaisaria na Antiochia.

Kwa safari yake ya tatu ya kuhubiri, Paulo alirudia Efeso na kubaki pale kwa miaka miwili. Kwa wakati ule wajumbe toka Korinto walifika kuulizana na Paulo juu ya maneno mengi. Aliandika 1 Wakorinto kujibu maulizo haya.

Nyuma ya wakati Paulo alianza kusumbuka kama Wakorinto walifikiri nini juu ya barua yake, zaidi juu ya maneno

aliyoandika juu ya mtu yule aliyeanguka kwa zambi. Hivi aliondokea Efeso, akakwenda kwa Troa pahali alipotaraji kukutana na Tito. Lakini wakati Tito asipokuwa pale, Paulo alivuka maji kwenda Makedonia, akakutana na Tito pale aliyeleta habari nzuri na mbaya. Wakristo walikuwa wameazibu mwanmini aliyekuwa ameanguka, na azabu hii ilisiaidia kumrudisha karibu na Bwana. Hizi ziliikuwa *habari njema*. Lakini Wakristo hawakutuma zawadi yao ya mali kusaidia waamini masikini katika Yerusalem, namna walivyokusudi kufanya. Habari hizi hazikuwa njema. Mwishoni Tito alileta habari ya kwamba walimu wa uwongo walitumika sana kwa Korinto, wakijaribu kubomoa kazi ya Paulo, na kuamsha mashaka rohoni mwa watu kama alikuwa na amri kweli ya mtumishi wa Kristo. Hizi ziliikuwa *habari mbaya!*

Ndani ya barua yake ya kwanza tunona Paulo zaidi kama mwalimu, lakini ndani ya barua ya pili alifanya kazi ya mchungaji. Tunaweza kuona wazi mapendo yake makubwa kwa watu wa Mungu ambayo yalimsukuma kujitoa mzima kuwasaidia. Wakati tunaposoma barua hii tuombe Roho Mtakatifu kusaidia ufahamu wetu.

HABARI YALIYOMO

- | | |
|----------------------------------------------------------------|---------------|
| I. MAELEZO YA PAULO YA UTUMISHI WAKE | (Sura 1-7) |
| A. Salamu | (1:1, 2) |
| B. Utumishi wa kufariji wakati wa mateso | (1:3-11) |
| C. Kwa sababu gani Paulo aligeuza shauri lake | (1:12 – 2:17) |
| D. Barua ya kusadikisha amri ya Paulo | (3:1-5) |
| E. Tofauti ya Agano la Kale na Agano Jipyä | (3:6-18) |
| F. Lazima ya kuhubiri Habari Njema waziwazi | (4:1-6) |
| G. Chombo cha udongo kinachotayarishwa kwa mbingu | (4:7-18) |
| H. Kuishi tukikumbuka Kiti cha Hukumu ya Kristo | (5:1-10) |
| I. Utumishi wa Paulo na zamiri njema | (5:11 – 6:2) |
| J. Utumishi wa Paulo na mwenendo wake | (6:3-10) |
| K. Paulo alisihii washirikiane naye na roho wazi
na mapendo | (6:11-13) |

- | | |
|-----------------------------------------------------------------------------------|----------------|
| L. Paulo aliwasih i kujitenga na zambi za dunia | (6:14 – 7:1) |
| M. Paulo alifurahi kusikia habari nzuri toka Korinto | (7:2-16) |
| 2. MAONYO YA PAULO WATIMIZE SADAKA KWA WAAMINI WA YERUSALEMA | (Sura 8, 9) |
| A. Wengine waliota na ukarimu | (8:1-9) |
| B. Maonyo mazuri watimize sadaka | (8:10, 11) |
| C. Mashauri mema matatu kuongoza watu kutoa na ukarimu | (8:12-15) |
| D. Ndugu wema watatu watayarische sadaka | (8:16-24) |
| E. Paulo alisihi Wakorinto kuonyesha kwamba hakujisifu
bure juu yao | (9:1-5) |
| F. Zawabu njema kwa wenye kutoa na ukarimu | (9:6-15) |
| 3. PAULO ALISIBITISHA UTUME WAKE | (Sura 10–13) |
| A. Jibu la Paulo kwa washitaki wake | (10:1-12) |
| B. Shauri la Paulo: Kuhubiri Habari Njema ya Kristo
pahali isipohubiriwa mbele | (10:13-16) |
| C. Kusudi kubwa la Paulo: Sifa ya Bwana | (10:17, 18) |
| D. Paulo anasimamia utume wake | (11:1-15) |
| E. Mateso ya Paulo kwa Kristo yanahakikisha utume wake | (11:16-33) |
| F. Funuo toka Mungu yalihakikisha utume wa Paulo | (12:1-10) |
| G. Alama za Paulo zilisimamisha utume wake | (12:11-13) |
| H. Kufika kwa Paulo kwa Korinto kulikuwa karibu | (12:14 – 13:1) |
| I. Wakorinto wenyewe walihakikisha utume wa Paulo | (13:2-6) |
| J. Paulo alitaka kutenda Wakorinto mema | (13:7-10) |
| K. Salamu ya neema ya Paulo | (13:11-14) |

MAFUNDISHO

1. MAELEZO YA PAULO YA UTUMISHI WAKE (Sura 1–7)

A. Salamu (1:1, 2)

1:1 **Paulo** alijulisha mara moja wale watakaopokea barua hii kwamba **ye ye ni mtume wa Yesu Kristo kwa mapenzi ya Mungu**. Alihitaji kufanya hivi kwa mwanzo wa barua hii kwa sababu watu wengine katika Korinto walikuwa na shaka kama alitumwa kweli na Bwana. Paulo alijibu kwamba haku-chagua utumishi huu ye ye mwenyewe, wala watu hawakumtia mikono, lakini alitumwa kwa kazi hii na Kristo Yesu kwa **mapenzi ya Mungu**. Aliitwa kuwa mtume wakati alipokuwa akisafiri kwa Damasiki. Lilikuwa tukio asiloweza kusahau kamwe, na lilimpatisha nguvu tena kwa wakati wa taabu na mambo

magumu ambayo yalimpata. Mara nyi-
ngi wakati alipotaabishwa kupita ki-
pimo, angetaka kuacha kazi na kurudi
kwake, isipokuwa alijua kabisa kwamba
aliitwa na Mungu kuifanya.

Tunaona jina la **Timoteo** hapa, si kwa sababu aliandika barua hii pamoja na Paulo, lakini kwa sababu alikuwa pamoja na Paulo kwa saa ile. Zaidi ya ile hatujui maneno mengi juu ya safari za Timoteo kwa muda huu.

Barua hii iliandikwa kwa **kanisa la Mungu lililo katika Korinto**, pamoja na watakatifu wote walio katika inchi yote ya **Akaya**. Maana ya **kanisa la Mungu** ni kusanyiko la waamini walio mali ya Mungu. Halikuwa kusanyiko la wapagano, au watu wasiokumbuka Mungu, lakini kusanyiko la Wakristo, watu waliozaliwa tena walioitwa toka

dunia kuwa mali ya Bwana. Wakati Paulo alipoandika maneno haya, bila shaka alikumbuka mara ya kwanza alipofika kwa Korinto na kuhubiri Habari Njema pale. Wanaume na wanawake waliozama ndani ya zambi za anasa na kuabudu sanamu walipokea Yesu Kristo kuwa Bwana, na kuokolewa kwa neema yake ya ajabu. Hata kama kwa wakati wa nyuma kulikuwa na matata mengi ndani ya kanisa hili, Paulo alifurahi wakati alipokumbuka namna maisha ya watu hawa wapenzi yalikuwa yamegeuka. Aliandika barua hii si kwa Korinto tu, lakini **kwa watakatifu wote walio katika inchi yote ya Akaya.** Akaya ilikuwa sehemu ya kusini ya inchi ya Yunani. Tutasoma nyuma juu ya Makedonia iliyokuwa sehemu ya kaskazini ya inchi ile.

1:2 Neema ... na salama ndiyo salamu ya Paulo aliyotaka zaidi kwa watu wa Mungu. Hakuomba waweze kupewa vitu vya dunia, kama feza na zahabu, vitakavyopotea mbio. Aliomba waweze kupokea baraka za roho, kama **neema na salama** pamoja na mambo mema yote mwenye zambi anayoweza kupokea mbele ya kufika mbinguni. Baraka hizi zinatoka kwa **Mungu Baba wetu** kwa njia ya **Bwana Yesu Kristo.** Paulo hakuwa na shaka kutaja **Bwana Yesu Kristo** pamoja na **Mungu Baba**, kwa sababu **Kristo, kama mmoja wa Utatu, ni mamoja na Baba.**

B. Utumishi wa kufariji wakati wa mateso (1:3-11)

1:3 Ndani ya mashairi 3-11 Paulo anashukuru Mungu kwa namna alivyo-farijiwa hata katikati ya taabu na mateso. Bila shaka **faraja** hii zilikuwa habari njema zilizoletwa na Tito toka Makedonia. Halafu mtume alieleza ya kwamba hata akiteswa, au kufarijiwa, mwishoni maneno haya yote yalikuwa kwa baraka ya waamini ambao alitumikia. Alileta mashukuru haya kwa **Mungu na Baba**

wa Bwana wetu Yesu Kristo. Hili ndilo jina zima la Mungu ndani ya Agano Jipy. Hakuitwa tena Mungu wa Abraham, Mungu wa Isaka, au Mungu wa Yakobo. Sasa ye ye ni **Mungu na Baba wa Bwana Yesu Kristo.** Jina hili linatufahamisha kweli kubwa kwamba Bwana Yesu ni Mungu na Mtu pamoja. Mungu ni *Mungu* wa Bwana wetu Yesu Kristo; neno hili linaonyesha udugu wake na **Yesu**, Mwana wa watu. Lakini Mungu ni *Baba* ya Bwana wetu Yesu Kristo vilevile; neno hili linaonyesha udugu wake na Kristo, Mwana wa Mungu. Zaidi ya maneno haya anaitwa **Baba ya rehema, na Mungu wa faraja yote. Rehema** na faraja zote zinatoka kwake.

1:4 Katikati ya mateso yake yote Paulo alijuana na faraja ya Mungu. Hapa anataja moja ya sababu Mungu alizomfariji. Alimfariji ili ye ye **aweze kufariji** wale walio **katika mateso yo yote, kwa faraja aliyofarijiwa mwenyewe na Mungu.** Maana ya faraja hapa ni vilevile kuonya na kutia roho nguvu tunayopokea toka mtu mwingine saa ya mahitaji. Maneno haya ni maonyo kwa sisi sote. Sharti tukumbuke ya kwamba wakati sisi tunapofarijiwa, inatupasa kushiriki faraja hii na watu wengine. Vizuri tufikie wagonjwa, na wale waliofiwa wapenzi na kuwafariji. Tukumbuke kwamba tulifarijiwa kusudi tuweze kufariji wengine.

1:5 Paulo aliweza kufariji wengine kwa sababu faraja ya **Kristo** ilikuwa kipimo kimoja na mateso aliyovumilia kwa ajili ya Kristo. **Mateso ya Kristo** hapa si mateso Mwokozi aliyovumilia kama malipo kwa zambi zetu. Mateso yake yalikuwa namna nyingine, na hakuna mtu anayeweza kushiriki ndani yao. Lakini inawezekana kwa Wakristo kuteswa kwa sababu ya ushirika wao na Bwana Yesu. Wanalaumiwa, kukataliwa, wanajuana na uadui, kuchukia, kuktaliwa, kutolewa kwa mikono ya adui, vivi hivi. Maneno haya yanaitwa

mateso ya Kristo kwa sababu aliyavumilia yote wakati alipokuwa duniani, na kwa sababu anayavumilia hata sasa wakati viungo nya Mwili wake wanapoyapata (ona Isa. 63:9). Lakini Paulo anataka tufahamu kuna zawabu kwa mateso haya yote, ndiyo kuwa mshiriki ndani ya faraja ya Kristo. Faraja hii inatosha kabisa.

1:6 Paulo aliona wema ukitoka ndani ya **mateso** yake, na vilevile ndani ya **kufarijiwa** kwake. Mateso haya yalitakaswa na msalaba. **Akiteswa**, ili-kuwa kwa **faraja** na **wokovu** wao – si wokovu wa nafsi yao, lakini uwezo wa kuwashindisha katika majoribu yao. Wakiona uvumilivu wa Paulo, watafikiri kama Mungu akiwezesha kumpa Paulo neema **kuvumilia** mateso yake, atawea kuwapa neema vivyo hivyo. Labda mfano wa Paulo uliwafundisha kujaribu kuona baraka ndani ya taabu yao yote.

Kuona namna mtume alivyofarijiwa kungejaza Wakorinto na **faraja** vilevile na kuwapa nguvu kuvumilia na saburi mateso namna yeze aliyopata. Watu wale tu waliopata taabu kubwa wao wenyewe wanaweza kufariji wengine wanaoteswa vivyo hivyo. Mama aliye-fiwa mtoto wake wa pekee anaweza vizuri zaidi kufariji mama mwingine mwenye roho ya kuvunjika kwa sababu ya huzuni kubwa ile ambayo ilimpata sasa tu. Na zaidi Baba aliyeptewa Mwana wake wa pekee anaweza kufariji wale wanaopotewa wapenzi kwa njia ya mauti.

1:7 Halafu mtume alionyesha tumaini lake ya kwamba Wakorinto walikwisha kujuana na mateso kwa ajili ya Kristo, watasaidiwa na faraja ya Kristo vilevile. Hakuna Mkristo anayepata **mateso** tu peke yake. Kila mara **faraja** ya Kristo yanayaafuata. Sisi tuna tumaini hili vilevile, kama Paulo.

1:8 Nyuma ya kusema maneno haya juu ya mateso na faraja, Paulo alipasha sasa habari za taabu ambayo ilimpata

yeze. Hakutaka wasijue habari za **mateso ambayo yalimpata katika Asia**. (**Asia** hapa si bara kubwa, ndiyo moja ya mafungu matano ya dunia, lakini wilaya ndani ya sehemu ya mangaribi ya inchi inayoitwa sasa Asia Ndogo.) Hatujui kama Paulo aliandika juu ya **mateso** gani. Labda lilikuwa kelele lile la hatari kwa Efeso (Mdo. 19:23-41). Watu wengine wanafikiri ulikuwa ugonjwa mbaya, na wengine wanafikiri zilikuwa habari mbaya toka Korinto. Mashairi haya yana faida kwa sisi hata kama hatujui habari hizi.

Lakini taabu yenye ililemea Paulo sana kuliko **nguvu** yake hata alifikiri alikuwa **karibu na mauti**.

1:9 Alifikiri alikuwa amehukumiwa **kufa**. Kama mtu angemwuliza kama alifikiri ataishi au kufa, angelazimishwa kujibu “kufa.” Mungu aliacha mtumishi wake kupata taabu hii kubwa **asijitegeme mwenye**, lakini **ategeme Mu-ngu anayefufua wafu**, ndiye Mungu Mwenyezi. Paulo alifikiri alikuwa amehukumiwa kufa, na Mmoja anayeweza kufufua wafu ni tumaini la pekee la mtu namna hii.

1:10 Ndani ya shairi hili Paulo alisema juu ya kuokolewa na Mungu **mbele**, na **sasa**, na kwamba atafanya hivi kwa **wakati wa kuja** vilevile. Labda alifikiri juu ya machafuko kwa Efeso yaliyokwisha gafula na Paulo aliweza kukimbia (Mdo. 20:1). Mtume alijua kwamba Mungu yule ambaye **ali-mwokoa** mbele aliweza **kumwokoa** kila siku, na **atakaa kufanya hivi** kufika wakati atakapofunguliwa kabisa toka taabu na mateso ya dunia hii.

1:11 Paulo alisadiki kwamba Wakristo wa Korinto walikuwa wame-mwombea wakati alipokuwa akipata taabu hii kubwa. Lakini wengi wa waamini hawa walikuwa wamegeuka wajuzi wa mtume mkubwa huyu na hawakumwombea. Paulo, kwa neema, alikaa kuamini kwamba walifungana

pamoja naye. **Zawadi tuliyopewa** ndiyo zawadi ya kuponyeshwa kwake kwa sababu ya maombi ya **watu wengi**. Kwa mafikiri yake kuponyeshwa kwake kuliwa tunda la maombi ya watakatifu. Alisema ya kuwa kwa sababu watu wengi waliomba, **watu wengi** waliweza kutoa **asante** sasa kwa jibu la maombi yao.

C. Kwa sababu gani Paulo aligeuza shauri lake (1:12–2:17)

1:12 Paulo alifikiri aliweza kutegemea maombi ya waamini kwa sababu alitenda na kutembea bila hila mbele yao. Zamiri yake ilimshuhudia kwamba alitenda kwa **weupe wa moyo mbele ya Mungu** na watu. Hakutenda kwa hila ya watu wa dunia, **lakini** kwa nguvu (**neema**) **toka Mungu**. Ingepasa Wakorinto kuona neno hili wazi.

1:13 Weupe wa moyo wake ulionekana wazi ndani ya barua hii vilevile. Aliandika **waziwazi mawazo ya roho yake**. Alitaraji kwamba watajua neno hili hata mwisho, maana **hata mwisho** wa maisha yao.

1:14 Kanisa la Korinto walimjua **kwa sehemu**, maana waamini wengine hawakumkubali hata kidogo. Wale waliosimama pamoja naye walifahamu maneno mawili – ndiyo ya kwamba wao watajisifu juu yake, kama yeye vilevile atajisifu juu yao **katika siku ya Bwana Yesu**. **Siku ya Bwana Yesu** inatazamia kiti cha hukumu cha Kristo, wakati faida ya utumishi wa waamini itakapopimwa nao watapewa zawabu. Wakati Paulo alipotazamia kiti cha hukumu kile, bila shaka angeweza kuona nyuso za wale waliookolewa kwa njia ya utumishi wake. Watakuwa furaha na taji ya kumfurahisha (1 Tes. 2:19), nao vilevile watafurahi kwa sababu Mungu alitumika naye kuwafikisha karibu na Kristo.

1:15 Maana ya **katika tumaini hili** ndiyo **tumaini** kwamba walifurahi kwa sababu alikuwa mtume wa haki wa Yesu Kristo. Alitaka **kufika** kwao akijua

kwamba walimwamini, kumheshimu, na kumpenda. **Alitumaini** kufika kwao **mbele** ya kwenda ya kwenda Makedonia, na halafu kuwafikia tena wakati aliporudi toka Makedonia. Kwa njia hii wangepata **faida mara mbili**.

1:16 Alieleza **neema** (faida) **ya pili** ndani ya shairi hili. Kama tulivyoona mbele, shauri la Paulo lilikuwa kuondokea Efeso na kupita kwa Akaya, pa-hali Korinto ulipokuwa, kisha kusafiri kwa upande wa kaskazini hata **Makedonia**. Nyuma ya kuhubiri kule alikusudi kwenda kwa kusini tena kwa Korinto. Alitaraji ya kwamba waamini wa pale watamsindikisha **kwenda Yudea** – kwa njia ya kumpangisha nyumbani mwao, na kwa maombi yao, lakini si kwa njia ya mali, kwani tutasoma nyuma ya kwamba alikusudi kutokupokea mali toka kwao (11:7-10).

1:17 Shauri la Paulo kwa safari hii halikufanyikana. Alisafiri toka Efeso hata Troa, na wakati asipokutana na Tito pale, aliendelea na safari yake kwenda Makedonia mara moja bila kufikia Korinto. Hivi hapa anauliza, “**Wakati nilipotaka maneno haya, nilifanya kama kugeukageuka?**” Tunazania wachongezi walifikiri hivi, na kusema yeye ni mtu wa kugeukageuka anayesema neno moja na kufanya lingine. Mtu namna hii ni mtume wa kweli? Mtume aliuliza Wakorinto kama haiwezekani kumtgemea. Wakati alipokusudi **kufanya neno**, alifanya hivi kwa faida ya mwili na kusema kwanza **Ndiyo**, kisha kugeuka na kusema **Hapana?** Aliongozwa na kutaka kwake tu, kwa faida yake? Ilimpasa kugeuza shauri lake, hivi yeye ni mtu wa kugeukageuka?

1:18 Ni kama Paulo aliacha sasa kusema juu ya **shauri** la safari yake na alisema juu ya mahubiri yake. Labda wachongezi wake walikuwa wakisema kama haiwezekani kuamini masemo yake ya kila siku, basi haifai kutegemea mahubiri yake vilevile.

1:19 Paulo alisema kwamba waliweza kutegemea matendo yake kwa sababu alihubiri juu ya Mwokozi aliye Mungu asiyeweza kugeuka wala kubadilibadili. Wakati alipofika kwa Korinto mara ya kwanza pamoja na **Silvano** na **Timoteo** (Matendo 18:5), walihubiri juu ya **Mwana wa Mungu** anayeweza kuminawa. Mahubiri yao hayakugeukageuka, kwa sababu yalikuwa juu ya **Mwana wa Mungu** asiyebadilibadili. Hakuna mtu anayehubiri juu ya Bwana Yesu Kristo akiongozwa na Roho Mtakatifu angeweza kutenda namna wachongezi wake walivyosema. Namna gani angeweza kuhubiri juu ya Mungu mwaminifu bila kuwa mwaminifu ndani ya masemo yake mwenyewe?

1:20 Ahadi zote za Mungu zinatimizwa *ndani ya Kristo*. Wote wanaokutta **ndani ya Kristo** kutimizwa kwa ahadi za Mungu wanasema **Amina**:

Unafungua Biblia yako na kusoma ahadi, unanyanya macho yako kwa Mungu, na Mungu anasema, “Unaweza kupata maneno haya yote kwa njia ya Kristo.” Tukiamini Kristo, tunasema, “Amina” kwa Mungu. Mungu anasema kwa njia ya Kristo, nasi tunaamini Kristo ... na kila ahadi ya Mungu inatimizwa ndani ya Yesu Kristo, na tunaiamini na kuipokea kwa sisi wenyewe.”¹

Maneno haya yote ni **kwa utukufu wa Mungu kwa njia yetu**. Maneno haya **kwa njia yetu**, yalikumbusha Wakorinto ya kwamba **kwa njia ya** mahubiri ya watu kama Silvano, Timoteo, na Paulo, atapokea ahadi za Mungu katika Kristo. Kama mtume angalikuwa mdanganyi, kama wachongezi walivyosema juu yake, kama Mungu angalitumika na mdanganyi na mwongo kutimiza maneno mazuri namna hii? Jibu la ulizo hili ni sivyo, hata kidogo.

1:21 Halafu Paulo alionyesha kwamba Wakorinto na yeye mwenyewe walifungwa pamoja katika imani. **Mungu** alikuwa amewasimamisha katika imani **ndani ya Kristo**, kwa utumishi wa Neno la Mungu. **Alikuwa amewapakaa** na kuwawezesha na kuwafundisha vilevile na **Roho Mtakatifu**.

1:22 Aliwitia mhuri vilevile na **kuwapa** arabuni ya **Roho Mtakatifu** miyoni mwao. Hapa tunaona kazi kubwa mbili nydingine za Roho Mtakatifu. Mhuri ni alama ya kwamba mtu ni mali ya fulani, naye analindwa na bwana wake. **Roho** anayekaa ndani ya mwamini ni alama kwamba mwamini ni sasa mali ya Mungu na anakaa na salama kwa milele. Mhuri huu hauonekani kwa macho ya watu. Watu hawajui kwamba tuko Wakristo kwa sababu ya alama fulani tunayovaa, lakini kwa njia ya matunda ya Roho Mtakatifu ndani ya maisha yetu. Mungu **amewapa** vilevile **arabuni** ya Roho **miyoni** mwao, kama ahadi kwamba watapokea uriti wa kutimia kwa wakati wa kuja. Wakati Mungu anapookoa mtu, anampa **Roho** Mtakatifu kukaa ndani yake, na hakika atapokea uriti mzima wa Mungu. Baraka zote tunazopata kwa njia ya Roho Mtakatifu kwa wakati wa sasa zitakuwa zetu na kipimo cha kutimia kwa wakati wa kuja.

1:23 Toka shairi hili kufika 2:4 Paulo alirudi tena kwa mashitaki ya wachongezi ya kwamba yeye ni mtu wa kugeukageuka, na kwa sababu gani hakufikia Korinto kama alivyokusudi mbele. Hakuna mtu aliyeveza kujua na kutambua makusudi rohoni mwa Paulo, hivi aliita **Mungu** kuwa **mshuhuda** wa neno hili. Kama mtume angalifikia **Korinto** kwa wakati alipokusudi kufika, angalilazimishwa kuhukumu maneno yao na ukali sana. Ingalimpasa kuwahukumu uso kwa uso kwa sababu walikubali na kuvumilia zambi kanisani.

Hakufikia **Korinto** kwa saa ile kwa sababu aliwahurumia na hakutaka wapate maumivu na huzuni ile.

1:24 Lakini nyuma ya kusema maneno haya, Paulo hakutaka mtu ye yote kufikiri kwamba alitawala Wakorinto. **Hivi alisema, "Si kwamba tunatawala imani yenu; lakini sisi ni wasaidizi wa furaha yenu; maana munasimama kwa imani."** Hakutaka wafikiri alitaka kutawala **imani** yao kama sultani. Yeye nao waliotumika pamoja naye walikuwa wasaidizi tu wa **furaha** yao, maana alitaka kuwasaidia kutembea na furaha zaidi katika imani yao.

Sehemu ya nyuma ya shairi 24 inaonyesha kwamba walikuwa wame-simama vizuri katika imani yao. Maneno Paulo aliyotaka kutengeneza kanisani hayakuwa maneno ya doctrine, lakini namna walivyotenda ndani ya kanisa.

2:1 Ndani ya shairi hili Paulo ali-endelea kueleza kwamba hakufikia Korinto kama alivyokusudi mbele kwa sababu ingalimpasa kuwakemea, na hakutaka kuwahuzunisha. Ni kama masemo haya **Nilikusudi ... nisije kwenu tena katika huzuni** yanaonyesha kwamba aliwaleta huzuni wakati alipofika kwao mara ya kwanza katika Matendo 18:1-7. Ni kama 2 Wakorinto 12:14 na 13:1 ni juu ya kufika kwake mara ile vilevile.

2:2 Kama mtume angefikia Korinto na kusudi la kuwakemea, angehuzunisha Wakristo. Halafu ye ye mwenyewe angehuzunishwa vilevile kwa sababu aliwatazamia wamfurahishe. Kama Ryrie alivyosema, "Kama nikiwahuzunisha ninyi, nani atabaki kunifurashisha ila wenye huzuni? Neno hili lisingenifariji."

2:3 Hivi kwa pahali pa kuhuzunishana kama angefika ye ye mwenyewe, mtume Paulo aliwaandikia barua. Alitaraji barua hii itawafahamisha kwamba ilipasa wahukumu ndugu huyu aliye-

kuwa ametenda zambi. Halafu wakati atakapofika nyuma, hakuna neno lita-kaloharibu upatano wake na watu hawa amba o alipenda sana.

Labda barua hii iliyotajwa ndani ya sehemu ya kwanza ya shairi hili ilikuwa 1 Wakorinto au barua nyingine tusiyo nayo kwa wakati wa sasa? Watu wengi wanafikiri si 1 Wakorinto kwa sababu shairi 4 linasema ya kuwa iliandikwa katika mteso mengi, na taabu ya moyo, na machozi. Labda Paulo aliandika barua nyingine kali kwa Wakorinto tusiyo nayo kwa wakati wa sasa. Tunazani aliandika barua namna hii nyuma ya kukaa kwao na huzuni (2 Kor. 2:1), na alituma Tito kuifikisha kwao. Labda ilikuwa barua namna hii iliyotajwa ndani ya 2:4, 9; 7:8, 12.

Tunajua tu ya kwamba Paulo **ali-andika** maneno ya shairi 3 kwa sababu hakutaka **kuhuzunishwa** na wale amba o wangepasa **kumfurahisha** ye ye wakati atakapofika tena. Aliamini kwamba maneno haya ambayo **yangemfurahisha** ye ye **yatawafurahisha** vilevile, ndiyo kutengenezwa vizuri kwa neno ambalo lilihitaji hukumu.

2:4 Ndani ya shairi hili tunaweza kuona roho ya mchungaji mkubwa. Paulo aliumia kabisa **moyoni**, na hata **kutoa machozi** kwa sababu Wakristo walivumilia kuwa na zambi kanisani. Ni wazi ya kwamba zambi katika kanisa la Korinto iliumiza roho ya Paulo kupita Wakorinto wenyewe. Haikufaa wafikiri kwamba kusudi la barua hii lilikuwa kuumiza roho yao. Kusudi lake lilikuwa kuhakikisha **mapendo** yake kwa wa-amini. Kwa njia ya kutuma barua hii alifikiri watakuwa na saa ya kutosha kutengeneza neno hili kusudi kufika kwa Paulo mara ya nyuma kutakuwa wakati wa furaha. "Vidonda rafiki anavyotia ni vya uaminifu" (Mez. 27:6). Haifai tuchukizwe wakati Mkristo mwingine anapotufundisha au kutuonya kupatana na mafundisho ya Biblia.

Vizuri tufahamu kwamba ndugu huyu anafanya hivi kwa sababu anataka sana kutusaidia. Ingepasa tupokee makemeo ya haki kama kutoka kwa Bwana, na roho ya asante.

2:5 Toka shairi 5 kufika shairi 11 mtume anafikiri tena juu ya neno lilloamsha matata yenyewe. Ona adabu ya kikristo anayoonyesha wakati anaposema juu yake. Hakutaja zambi au jina la mwenye kuitenda hata mara moja. Labda maneno haya “**ikiwa kama mtu amehuzunisha**” yanasema juu ya mzini huyu katika 1 Kor. 5:1, au mtu mwininge aliyeleta matata kanisani. Tunawaza yalikuwa juu ya mtu wa kwanza. Paulo hakufikiri kwamba mtu huyu alimhuzunisha ye ye mwenyewe tu, lakini ya kwamba waamini **wote walihuzunisha**.

2:6 Waamini walikubali kuazibu mtenda zambi. Ni kama walimwondosha kanisani. Kwa sababu hii alitibu na roho ya kweli na alirudi karibu na Bwana. Sasa mtume aliwaambia Wakorinto kwamba **azabu** ya mtu huyu **ilitosha**. Watu wengine wanafikiri kwamba maana ya **aliyopewa na** “walio wingi” ni kwamba **zaidi ya** Wakorinto walikubali aazibiwe hivi. Wengine wanafikiri kama waamini wakitawaliwa kweli na Roho, wao **wote** wangepatana ndani ya neno hili.

2:7, 8 Mtu huyu alikuwa ametubu kweli sasa, hivi ilipasa Wakorinto **ku-msamehe** na kumpatisha nguvu kwa njia ya kumpokea tena kanisani. Haifai kumwacha **kumezw na huzuni nyinying sana**, maana asiwe na shaka kama walimsamehe kweli.

Ingepasa Wakorinto **kusibitisha** mapendo yao kwake.

2:9 Paulo alikuwa **amepima** Wakorinto wakati alipoandika barua yake ya kwanza. Sasa walikuwa na njia kuonyesha kwamba **walitii** neno la Bwana ambalo mtume Paulo aliwfundisha. Ndani ya barua yake ya kwanza alisema

nao vizuri waondoshe mtenda zambi toka kanisa. Walifanya hivi, na kuhakikisha **utii** wao. Sasa Paulo alisema nao kufanya neno moja lingine, ndilo kumpokea tena kanisani.

2:10 Paulo alitaka waamini kujuwa kwamba alishiriki nao ndani ya tendo la kusamehe mtenda zambi yule. Kama ye ye mwenyewe angekuwa na **neno** ambalo ilimpasa kusamehe, **analisa-mehe** kwa ajili ya Wakorinto na **mbele ya Kristo**.

Kuna mafundisho mengi ndani ya barua hii juu ya hitaji la kuazibu zambi kanisani, lakini watu wa makanisa mengi hawaweki roho juu yao neno hili. Wanaamini ya kwamba Maandiko yali-andikwa kwa maongozi ya Mungu, lakini hawayatii wakati wanapofikiri si faida kwoo.

2:11 Ni hatari kwa kanisa kama waamini wasipoazibu mwenye kuanguka kwa zambi, na ni hatari vilevile kama wasipomsamehe wakati anapotubu na roho ya kweli. **Shetani** ni mwenye hila sana. Kwanza atajaribu kuharibu ushuhuda wa kanisa kwa njia ya kutokuhukumu mwenye kuanguka. Kisha Shetani ataacha mwenye kutubu kushindwa na huzuni kubwa zaidi kama waamini wasipomrudisha katika ushirika wa kanisa.

Juu ya **“hatukosi kujuwa hila zake”** J. Sidlow Baxter anasema:

Shetani ana njia mbalimbali kuondosha waamini toka kweli ya Mungu: kuwapetpa kama ngano (Lk. 22:31), “miiba kusonga” neno la Mungu (Mt. 13:22), “hila” kudanganya (Efe. 6:11), simba ya kunguruma kuogopesha (1 Pet. 5:8), kujionyesha kama malaika (2 Kor. 11:14), na “mitego” kuwafunga (2 Tim. 2:26).²

2:12 Sasa Paulo alirudi tena kueleza sababu yake ya kugeuza shauri lake, ona shairi 4. Hakwendea Korinto kama alivyosema mbele atafanya. Mashairi

yaliyotangulia yalieleza kwamba hakuwafikia kwa sababu hakutaka kufika kwao na roho ya uchungu. Ndani ya mashairi 12-17 alieleza nini ilitokea kwa wakati ule. Paulo aliondokea Efeso na kusafiri kwa **Troa**. Alitaraji atakutana na Tito pale na kusikia habari toka Korinto. Wakati alipofikia Troa, mlango mzuri sana **ulifunguliwa** kwake katika **Bwana** kwa kuhubiri **Habari Njema ya Kristo**.

2:13 Lakini hata hivi Paulo alisumbuka sana **rohoni**. **Tito** hakuwa pale kukutana naye. Maneno ya kanisa la Korinto yalikuwa mzigo mzito kwa roho yake. Ilimpasa kufanya nini, kukaa kwa Troa na kuhubiri Habari Njema ya Kristo? Au aendelee na safari yake kwenda Makedonia? Alichagua kwenda **Makedonia**. Labda Wakorinto walifikiri nini wakati waliposoma habari hizi? Walikuwa na haya kidogo wakati walipofahamu kwamba matendo *yao* yalisumbusha roho ya mtume hivi, hata hakuingia mlango ule kwa kuhubiri Habari Njema kusudi apate habari ya hali ya kanisa lao?

2:14 Lakini Paulo hakushindwa hata pahali gani alipokwenda ndani ya utumishi wake kwa Kristo. Hivi na roho ya kujaa sifa alisema, “**Lakini asante kwa Mungu, ambaye anatushindisha sisi siku zote katika Kristo.**”

Alitaja mfano wa washindaji Warama saa waliporudi toka vita, wakitembeza wafungwa wao katika njia za mji. Kulikuwa na watu wakibeba uvumba wakitembea pamoja nao kwa kuume na kushoto, na **harufu** ya uvumba ilijaza hewa. Hivi kwa mfano Paulo alionyesha Bwana akitembea kama mshindaji toka Troa hata Makedonia, akiongoza mtume kumfuata. Bwana alishinda, pahali gani alipokwenda, kwa njia ya mtumishi wake, na **harufu ya kujua** Kristo kulienezwa kwa njia ya mtume katika kila pahali.

Hivi Paulo hakufikiri kwamba alishindwa ndani ya vita yake na Shetani, lakini ya kwamba Bwana alikuwa ameshinda, na Paulo alishiriki ndani ya kushinda kwake.

2:15 Paulo alikuwa amesema juu ya harufu ya uvumba iliyozunguka washindaji wakati waliporudi toka vita. Harufu ile ilisema juu ya utukufu wa kushinda kwao, lakini ilisema vilevile juu ya maangamizi ya wafungwa. Hivi Paulo alionyesha kwamba mahubiri ya Habari Njema yana matunda ya namna mbili. **Katika watu wanaookolewa** ni ahadi ya utukufu kwa wakati wa kuja; kwa wengine ni alama ya maangamizi. Lakini Mungu anatukuzwa kwa njia mbili zote, ni manukato ya neema au harufu ya hukumu. F.B. Meyer alieleza neno hili vizuri:

Hivi wakati tunapoambiwa kwamba tunaweza kuwa manukato ya Kristo kwa Mungu, ni kusema ya kwamba inapasa maisha na mwenendo wetu kukumbusha Mungu maisha ya Yesu wakati alipokuwa hapa duniani. Ni kama wakati Mungu anapotutazama kila siku, ingempasa kuweza kuona Yesu, na kukumbushwa maisha yake ya baraka yaliyotolewa kama zabihu kwa Mungu kama manukato tamu.³

2:16 Kwa watu waliookolewa, Wakristo ni **harufu ya uzima kwa uzima**, lakini kwa wale wanaopotea, ni **harufu ya mauti kwa mauti**. Wakati Paulo alipowaza juu ya madaraka makubwa ya kuhubiri Habari Njema, analalamika, “**Na nani anayetosha kwa maneno haya?**” Ona 3:5 pahali Paulo aliposema, uwemo wake unatoka kwa Mungu.

2:17 Alisema kwamba yeze si kama wengi, **wanaoharibu Neno la Mungu**. Walikuwa wanani? Walikuwa walimu wa dini ya Wayuda waliojaribu kundoshsha Wakorinto toka mafundisho ya Paulo. Paulo alisema watu wale wa-

likuwa wakiharibu **Neno la Mungu** kwa kujipatia wenyewe faida. Walichanganya Neno la Mungu na mafundisho yao wenyewe. Kwa mfano, walijaribu ku-changanya sheria na neema.

Paulo hakutumika hivi na Neno la Mungu. Hakuchanganya Neno la Mungu na mafundisho mengine, kwa faida yake mwenyewe. Alisema maneno makubwa mane juu ya mafundisho yake. **Neno la kwanza** lilikuwa **weupe wa moyo**. Yalikuwa haki. Hakujaribu kuficha kitu.

Neno la pili, maneno aliyosema **yali-toka kwa Mungu**. Ni Mungu ambaye alimpa nguvu kwa kazi yake. *Halafu* aliongeza kwamba utumishi wake ulikuwa **mbele ya macho ya Mungu**. Alikumbuka saa zote kwamba Mungu alikuwa akitazama utumishi wake, na ya kwamba haikuwezekana kumfichia kitu. **Mwishoni** aliongeza, **tunasema katika Kristo**. Alisema kwa jina la **Kristo**, na amri ya **Kristo**, na kwa ajili ya **Kristo**.

D. Barua ya kusadikisha amri ya Paulo (3:1-5)

3:1 Ndani ya sehemu ya mwisho ya shairi 17 Paulo alisema maneno mane juu ya utumisihi wake. Alifahamu ya kwamba watu, zaidi wajuzi wake, watafikiri kwamba alijisifu mwenyewe. Hivi alianza sura hii na ulizo, **Tunaanza tena kujisifu wenyewe?** Maana ya neno hili **tena** hapa haiko ya kwamba alikuwa amefanya hivi mbele. Alitaka kusema tu kwamba *alishitakiwa* kwamba alifanya hivi, na alifikiri atashitakiwa hivi tena.

Au tunahitaji, kama wengine, barua za sifa kwenu, au kutoka kwenu? Wakati Paulo alipotaja **wengine**, alisema juu ya walimu wa uwongo wa 2:17. Walifikia Korinto na **barua za sifa**, labda toka Yerusalem. Na labda wakati walipoondokea Korinto walikuwa na **barua za sifa toka** kanisa la pale. Kwa wakati wa mwanzo wa kanisa Wakristo walipewa barua za sifa kwa wakati wa

kusafiri toka pahali pamoa kwenda pahali pengine. Mtume hakusema neno hili lilikuwa baya, lakini ni kama alisema barua hizi za sifa zilikuwa *neno la pekee* ambalo lilisimamia wajuzi hawa.

3:2 Walimu wa dini ya Wayuda waliofikia Korinto walikuwa na shaka juu ya amri ya mtume Paulo. Walikataa kwamba alikuwa mtumishi wa kweli wa Kristo. Labda waliamsa shaka ndani ya nia za Wakorinto kusudi Wakorinto waombe barua ya sifa toka mtume Paulo wakati atakapofika mara ya nyuma. Paulo alikuwa amewauliza mbele kama alihitaji barua namna hii. Alifikia Korinto wakati wao wote walipokuwa wapagano walioabudu sanamu. Hakuwa Paulo ambaye aliwaleta karibu na Kristo? Na Bwana alionyesha ukubali wake wa utumishi wa Paulo kwa njia kuokoa roho za damani za watu katika Korinto. Hili ndilo jibu la Paulo. Wakorinto wenyewe walikuwa **barua ya Paulo, iliyoandikwa** katika moyo wake, lakini **iliyojulikana na kusomwa na watu wote**. Hivi Paulo hakuhitaji barua iliyoandikwa na kalamu na wino. Walikuwa tunda la utumishi wake na aliwapenda sana. Zaidi ya ile, **waliujulikana na kusomwa na watu wote**. Wokovu wao ulikuwa umeonekana kwa watu wote kando kando. Walifahamu kwamba watu hawa walikuwa wamegeuka, ya kwamba waliacha kuabudu sanamu na waligeuka kwa Mungu, na waliishi sasa kwa yeye. Maneno haya yalishuhudia utumishi wa Paulo kwamba ultoka kwa Mungu.

3:3 Tufafikiri kwanza ya kwamba shairi 3 halipatani na shairi 2. Paulo alikuwa amesema kwamba Wakorinto walikuwa barua yake; ndani ya shairi 3 anasema wao ni **barua ya Kristo**. Ndani ya shairi 2 alisema barua yenyewe iliandikwa katika moyo wake; ndani ya sehemu ya mwisho wa shairi 3 ni kama Kristo aliandika barua hii juu ya miyo

ya Wakorinto wenyewe. Inawezekana kupatanisha mawazo haya namna gani? Ndani ya shairi 2 Paulo alisema Wakorinto walikuwa barua yake ya sifa. Shairi 3 linaleza neno hili. Labda ingetusaidia kulifahamu kama tukiunganisha sehemu za mashairi haya kwa njia hii: "Ninyi ni barua yetu ... kwa sababu **munaonyeshwa wazi** kuwa **barua ya Kristo.**" Wakorinto walikuwa barua ya sifa ya Paulo kwa sababu watu wote waliweza kuona wazi kwamba Bwana alikuwa amefanya kazi ya neema ndani ya maisha yao. Ilionekana wazi kwamba walikuwa Wakristo. Kwa sababu Bwana alitumika na Paulo kufanya neno hili, Paulo alisema **kazi ya utumishi wetu.** Bwana Yesu ndiye aliyefanya kazi yenyewe ndani ya maisha yao kwa njia ya utumishi wa Paulo.

Barua za sifa za adui za Paulo zili-andikwa **kwa wino;** lakini barua ya Paulo iliandikwa kwa **Roho ya Mungu aliye hai,** na hivi ilitoka kwa Mungu. **Wino** inaweza kukauka, kuzimishwa na kuharibishwa, lakini maneno yanayo-andikwa na **Roho ... ya Mungu** ndani ya miyo ya watu ni kwa milele. Halafu Paulo aliongeza kwamba barua ya Kristo **haikuandikwa katika mbao za mawe,** lakini **katika mbao** za miyo **ya mwili.** Watu waliofikia Korinto hawakuona barua ya Kristo iliyo-chongwa ndani ya jiwe kubwa na kusimamishwa pahali pa kujulikana kwa soko, lakini barua yenyewe iliandikwa ndani ya miyo na maisha ya Wakristo waliokaa pale.

Wakati Paulo aliposawanisha mbao za mawe na mbao za miyo za mwili, bila shaka alifikiri vilevile juu ya tofauti ya sheria na Habari Njema. Sheria ilikuwa imeandikwa katika mbao za mawe kwa Mlima Sinai, lakini kwa Habari Njema watu wanatii Mungu kwa njia ya habari za neema na mapendo zina-zoandikwa ndani ya miyo yao. Paulo

ataandika kupita juu ya neno hili nyuma kidogo.

3:4 Mtume alikuwa akisema na matumaini juu ya utume na utumishi ambao Mungu alimpa. Tungeweza kuuliza, "Namna gani unaweza kuwa na uhodari kusema hivi, Paulo?" Tunaona jibu kwa ulizo hili ndani ya shairi 4. Paulo alikana hapa ya kwamba alikuwa akijisimamia mwenyewe, lakini alisema tumaini lake ni **mbele ya Mungu.** Ni kusema hakuogopa kwa Mungu kumtazamia sana. Hakujitumainia mwenyewe wala uwezo wake mwenyewe, **Iakini kazi Kristo aliyofanya** ndani ya Wakorinto iliha-kikisha utumishi wa Paulo. Maisha yao yalikuwa yamegeuka kabisa.

3:5 Hapa Paulo alisema tena kwamba ndani yake mwenyewe hakuwa na kitu ambacho kilimstahilisha kuwa mtume wa Kristo. Uwezo kwa utumishi wake haukutoka ndani yake mwenyewe, lakini toka juu, toka Mungu. Paulo hakujitafutia sifa. Alifahamu ya kwamba utumishi wake ungalikuwa bila faida na matunda kama **Mungu** asimwezesha kwa kazi hii.

E. Tofauti ya Agano la Kale na Agano Jipyä (3:6-18)

3:6 Nyuma ya kusema juu ya kustahilishwa kwa utumishi *wake mwenyewe*, Paulo aliendelea kueleza utumishi wa Mungu. Ndani ya mashairi yanayofuata, anaonyesha kwa njia gani Agano la Kale (sheria) na **Agano Jipyä** (Habari Njema) ni mbalimbali. Alifanya hivi kwa sababu wajuzi wake wakali katika Korinto walikuwa watu walio-changanya sheria na neema ndani ya mafundisho yao. Walifundisha kwamba ilipasa Wakristo kushika sehemu nyininge za sheria ya Musa kusudi wa-kubaliwe na Mungu. Hivi mtume ali-onyesha hapa kwamba Agano Jipyä linapita Agano la Kale mbali na uzuri. Alianza na kuonyesha kwamba Mungu alimwezesha kuwa mtumishi wa **Agano**

Jipyा. Agano ndilo ahadi au mapatano. Agano la Kale lilikuwa kawaida ya sheria ambayo Mungu alitolea Musa. Kama watu wakittii maagizo haya watabarikiwa. Lilikuwa agano la matendo. Na lilikuwa mapatano ya watu na Mungu. Watu wakittii, Mungu atatimiza ahadi zake vilevile. Lakini kwa sababu lilisimamia watu, halikuzaa haki. **Agano Jipyा** ndilo Habari Njema. Kwa agano hili Mungu kwa neema yake anabariki watu kwa sababu ya ukombozi kwa njia ya Yesu Kristo. Maneno yote ya Agano Jipyा yanategemea Mungu, si watu. Hivi Agano Jipyा linaweza kufanya maneno Agano la Kale lisiyoweza kufanya kamwe.

Paulo alitaja maneno mengine kwa njia yao sheria na Habari Njema ni mballimbalii. Alianza hapa ndani ya shairi 6 kwa njia ya kusema, **Si kwa andiko, lakini kwa Roho, kwa sababu andiko linaua, lakini Roho anapatiza uzima.** Wengine wanaeleza maneno haya kusema ya kwamba ukitaka kutii masomo ya Maandiko na akili tu, bila kuyatti na roho, hutasaidiwa, lakini utaumizwa. Wafarisayo ni mfano wa neno hili. Waliweka roho sana juu ya kutoa zaka za vitu vidogo sana, lakini hawakuwa na rehema na mapendo kwa watu wengine (Mt. 23:23). Neno hili ni *mfano mzuri*, lakini si *elezo* la shairi hili. Ndani ya shairi 6 *andiko* ndilo Sheria ya Musa, na *roho* inasema juu ya Habari Njema. Wakati Paulo aliposema kwa-mba **andiko linaua**, alisema juu ya utumishi wa sheria. Sheria inahukumu watu wote wasiotii maagizo yake matakatifu. “Kwa njia ya sheria zambi inajulikana” (Rom. 3:20). “Amelaaniwa kila mtu asiyedumu katika yote yaliyoandikwa katika kitabu cha torati ayafanye” (Gal. 3:10). Halikuwa kusudi kamwe la Mungu kuleta uzima kwa njia ya sheria. Kusudi lake lilikuwa kusibitisha watu hatia ya kosa. Agano Jipyा linaitwa *roho*

hana. Linatimiza mifano na vivuli vya Agano la Kale. Maneno yaliyoagizwa na sheria, lakini sheria haikuweza kuzaa ndani ya watu, yanafanyikana sasa na Habari Njema.

3:7 Ndani ya mashairi 7 na 8 tunaona kwa njia gani maagano hawa mawili ni mballimbalii. Hapa mtume anasawanisha zaidi **utukufu** kwa wakati sheria ilipotolewa na utukufu ulioshikana na Habari Njema. Tunaona neno hili **utukufu** mara 17 ndani ya sura 3 na 4. Agano la Kale linaitwa **utumishi wa mauti, ulio-andikwa na kukatwa katika mawe.** Bila shaka ni Amri Kumi. Zinaleta mauti kwa watu wote ambaa hawazitii (Kutoka 19:13). Paulo *hasemi* ya kwamba utukufu haukuonekana kwa wakati sheria ilipotolewa. Wakati Mungu alipotolea Musa Amri Kumi juu ya Mlima Sinai, kulikuwa na maonyesho makubwa ya Mungu na uwezo wake (Kut. 19). Wakati Musa aliposimama pale mbele ya Mungu, uso wake mwenyewe ulianza kungaa na kuonyesha utukufu wa Mungu. Hivi **wana wa Israeli hawakuweza kutazama sana uso wa Musa, kwa sababu ya utukufu wa uso wake**, maana ulingaa sana. Lakini Paulo aliongeza maneno haya ya maana sana, **na utukufu huu uliondoshwa.** Uso wa Musa haukungaa daima. Utukufu ule ulikuwa kwa wakati tu. Maana ya roho ya neno hili ndiyo ya kwamba **utukufu** wa Agano la Kale ulikuwa kwa wakati tu. Sheria ilikuwa na kazi kubwa, ndiyo kufunua zambi. Ilikuwa onyesho la masharti matakatifu ya Mungu, na kwa sababu hii ilikuwa na utukufu. Sheria ilitolewa kufika wakati wa Kristo. Kristo ni mwisho wa sheria kwa wale wana-oamini (Rom.10:4). Sheria ilikuwa *ki-vuli*. Ilikuwa mfano wa mambo mazuri zaidi yanayotimizwa ndani ya Mwokozi wa dunia.

3:8 Kama sheria ilikuwa na utukufu, **utumishi wa Roho Mtakatifu hau-**

tazidi kuwa na utukufu? Neno hili “**utumishi wa Roho Mtakatifu,**” linasema juu ya Habari Njema. Roho Mtakatifu anatumika kwa njia ya mahubiri ya Habari Njema, na vilevile watu wanaopokea Habari Njema wanapokea Roho Mtakatifu.

3:9 Hapa Agano la Kale linaitwa **utumishi wa hukumu.** Mwisho wake ulikuwa **hukumu.** Lilileta hukumu kwa watu wote kwa sababu hakuna mtu aliyezeza kulitii ndani ya maneno yote. Hata hivi likuwa na **utukufu.** Likuwa na kusudi na mafaa kwa wakati ule. Lakini **utumishi wa haki una utukufu unaozidi sana.** Hodge anasema, “Utumishi wa haki ndio utumishi unaofunua haki, na kwa njia hii watu wanahesabiwa haki, na halafu wanafunguliwa toka hukumu ya sheria.”⁴ Utukufu wa Habari Njema haupendezi macho, lakini ni utukufu wa roho unaodumu. Utukufu wa Kalvari unashinda mbali utukufu wa Sinai.

3:10 Hata kama kwa njia nyingine **sheria ilitukuzwa,** wakati iliposawnishwa na Agano Jipy, **haikuwa na utukufu** hata kidogo. Wakati Agano Jipy na Agano la Kale yanaposawnishwa, kungaa kwa utukufu wa Agano Jipy kunapita sana kungaa kwa Agano la Kale.

3:11 Kwa maana **kama ule ulioondoshwa ulikuwa na utukufu,** zaidi sana **ule unaokaa una utukufu.** Likuwa na utukufu wakati Agano la Kale lilipotolewa, lakini Habari Njema ya neema ya Mungu *yenyewe* ndiyo **utukufu.**

Shairi hili linaonyesha vilevile kwa-mba sheria ilikuwa kwa wakati tu, lakini Habari Njema inadumu. Bila shaka **ule ulioondoshwa** ni Amri Kumi – “utumishi wa mauti ulioandikwa na kukatwa katika mawe” (sh. 7). Hivi shairi hili linakana mafundisho ya wafuata wa dini ya Septième Jour, ya kwamba kawaida

ya kuabudu kwa sheria imeondoshwa, lakini Amri Kumi zingali.

3:12 Taraja ambalo Paulo alisema juu yake ni kwamba alisadiki kabisa ya kuwa utukufu wa Habari Njema hautapunguka. Kwa sababu ya kuamini neno hili kabisa, alisema na **uhodari** sana. Hakuhitaji kuficha kitu. Hakuhitaji kitambaa kuficha uso wake. Kuna dini nyingi duniani leo zilizo na siri. Wamini wa sasa wanalazimishwa kuifunza siri hizi polepole. Habari Njema si hivi. Inatujulisha waziwazi juu ya habari za wokovu, Mungu aliye Tatu ndani ya Moja (Mungu Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu), mbingu, na gehena.

3:13 Si kama Musa alivyotia kitambaa juu ya uso wake, kusudi wana wa Israeli wasitazame sana mwisho wa ule ulioondoshwa. Tunasoma juu ya habari hizi katika Kutoka 34:29-35. Pale Musa, wakati aliposhuka toka mlima Sinai nyuma ya kupokea sheria toka Mungu, hakujuwa kwamba uso wake ulingaa. Waisraeli waliogopa kumkaribia kwa sababu ya kungaa kwa uso wake. Lakini aliwaita kufika karibu, nao walfanya hivi. Halafu aliwatolea kama amri maneno yote ambayo Bwana alimwambia. Katika Kutoka 34:33 tunasoma: “Wakati Musa alipomaliza kusema nao, akatia shela juu ya uso wake.” Ndani ya 2 Wakorinto 3:13, mtume alieleza kwa sababu gani Musa alifanya hivi. Alifanya hivi **kusudi wana wa Israeli wasitazame sana mwisho wa ule ulioondoshwa.** Utukufu wa uso wake ulikuwa utukufu usiodumu, maana sheria ambayo aliyotolewa ilikuwa na utukufu usiodumu. Ulikuwa ukipunguka hata kwa wakati ule, na Musa hakutaka waone **mwisho** wake. Hakutaka kuficha utukufu wenyewe, lakini *kuondoshwa* kwa utukufu. F.W. Grant alisema vizuri, “Sharti utukufu kwa uso wa Musa ukombolewe na utukufu kwa uso wa Mwingine.”⁵ Neno hili lilitokea saa

Bwana Yesu Kristo alipofika. Halafu mtumishi wa Agano Jipyahahitaji kuficha uso wake. Utukufu wa Habari Njema hautapunguka wala kuondoshwa kamwe.

3:14 Lakini mawazo yao yalitiwa giza. Waisraeli hawakufahamu maana ya neno Musa alilofanya. Kwa mia za miaka Wayuda hawakufahamu. Hata kwa wakati Paulo alipoandika maneno haya, walishikamana na sheria kama njia ya wokovu na walikataa kupokea Bwana Yesu Kristo.

Hata leo, wakati wanaposoma Agano la Kale, kitambaa kile kinabaki. Wakati mtume alipoandika maneno haya, saa Wayuda waliposoma **Agano la Kale**, hawakuvumbua siri Musa ali-yoficha kwa wazazi wao chini ya **kitambaa**. Hawakufahamu kwamba utukufu wa sheria ulikuwa utukufu uliokaa kwa wakati tu, na ya kwamba sheria ilikuwa imetimizwa ndani ya Bwana Yesu Kristo.

Kitambaa kinaondolewa katika Kristo wakati mtu anapoamini Bwana, na si nguvu tena kwaye kufahamu **Agano la Kale**. Hodge anaeleza neno hili hivi:

Inawezekana kufahamu Maandiko ya Agano la Kale tu wakati tunapofahamu ya kwamba yanatabiri na kuonyesha Kristo mbele. Kujuu Kristo kunaondosha kitambaa toka Agano la Kale.⁶

3:15 Mfano mwenyewe unageuka kidogo ndani ya shairi hili. Ndani ya mfano wa Agano la Kale, kitambaa kilifunika *uso* wa Musa, lakini sasa kitambaa kinafunika *mioyo* ya Wayuda. Wanakaa kujaribu kupokea haki kwa njia ya *matendo* yao, na hawafahamu hata kidogo kwamba kazi yenyeve imekwisha *kufanywa* na Mwokozi juu ya msalaba wa Kalvari. Wanajaribu kujipatia wokovu kwa njia ya ustahili wao wenyewe, na hawafahamu kwamba she-

ria inawahukumu kabisa, na ingewapasa kukimbia karibu na Bwana Yesu kupata rehema na neema.

3:16 Wakati Myuda *mmoja* (au *taifa* la Israeli) **anapogeuka kwa Bwana** na kupokea Yesu kama Masiya, **kitambaa kinaondolewa**, na giza rohoni lina-kwisha. Halafu wanafahamu kwamba kweli mifano na vivuli vyote vya sheria vinatimizwa ndani ya Mwana mpendwa wa Mungu, Masiya wa Israeli. Kama shairi hili linasema juu ya *taifa* la Israeli, halafu linatazamia wakati wa kuja saa baki waamini watakapogeuka **kwa Bwana**, kama ilivyotabiriwa katika Waroma 11:25, 26, 32.

3:17 Paulo alikuwa amesema kwa-mba Kristo ni ufunguo kwa Agano la Kale. Sasa anasema juu ya kweli hii tena, kwamba **Bwana ni Roho yule**. Maneno haya yanatufikirisha ya kuwa Bwana ni roho ya Agano la Kale, kama vile “ushuhuda wa Yesu ni roho ya unabii” (Ufu. 19:10). Mifano na vivuli vyote katika Agano la Kale vinatimizwa ndani ya Kristo. **Pahali Roho⁷ ya Bwana anapokuwa, kule kuna uhuru**, maana yake pahali gani watu wana-potambua Kristo kama Bwana au Yehova, **kuna uhuru**, uhuru toka utumwa wa sheria, uhuru toka giza na siri saa ya kusoma Maandiko, na uhuru kutazama uso wa Kristo bila kitambaa.

3:18 Kwa wakati wa Agano la Kale Musa peke yake alikuwa na ruhusa kuona Mungu na utukufu wa Bwana. Kwa wakati wa Agano Jipyahahitaji **sisi sote** tunaweza **kutazama utukufu wa Bwana**. Ilipasa uso wa Musa kufunikwa wakati alipomaliza kusema na watu, lakini nyuso zetu **hazifunikwi**. Tunaweza kuchunga nyuso zetu **bila kufunikwa** kwa njia ya kukiri na kuacha zambi zetu, kutenda kwa haki tu bila kuficha maneno.

Kisha tunatazama sana utukufu wa Bwana kama katika kioo. Kioo ni neno la Mungu. Wakati tunaposoma

Biblia tunaona Bwana Yesu akifunuliwa na uzuri wake wote. Hatumwonni kwanza uso kwa uso, lakini katika kioo cha neno la Mungu.

Na ona ya kwamba tunatazama **utukufu wa Bwana**. Hapa Paulo hakufikiri zaidi juu ya maisha mema ya Yesu wakati Yesu alipokuwa kama Mtu duni-ani, lakini juu ya utukufu wake kwa wakati wa sasa kwa mkono wa kuume wa Mungu. Denny alionyesha ya kwamba utukufu wa Kristo ni ya kwamba:

Kristo anashiriki kitu cha kifalme cha Baba, naye ni kichwa cha kanisa. Ana neema ya kutimia ya Mungu, na anaitoa. Yeye ni mwa-muzi wa ulimwengu, mweneye kushinda adui zote, na anaombea watu wake, naye ni mwenye enzi yote ya kifalme.⁸

Wakati tunapowaza juu ya utukufu wa Bwana Yesu Kristo aliyefufuliwa, na kupanda mbinguni, na kutukuzwa, **tuna-badilishwa tufanane na mfano wake**. Hii ndiyo siri ya maisha matakatifu ya Mkristo: ni kukaa kuwaza juu ya Kristo. Haifai tukae kuwaza juu yetu wenyewe, kwani tukifanya hivi tutashindwa tu. Si kukaa kuwaza juu ya maneno ya watu wengine. Kufanya hivi kunaleta uchungu tu. Lakini kwa njia ya kuwaza sana juu ya utukufu wa Bwana kama katika kioo, tunabdalishwa tufanane na mfano ule pole pole, **toka utukufu hata utukufu**, kama vile utukufu unaotoka kwa Bwana, aliye Roho.

Darby aliona neno hili ndani ya maisha ya Stefano wakati alipokuwa akitupiwa mawe:

Alitazama juu na aliona utukufu wa Mungu na Yesu. Kristo alikuwa amesema: "Baba, uwasamehe kwa sababu hawajui wanaloofanya." Stefano akiona Yesu katika utukufu, aliomba, "Bwana, usiwahesabie zambi hii." Na toka msalaba, Kristo alisema, "Baba, katika

mikono yako ninatoa roho yangu"; na Stefano alisema, "Bwana Yesu, pokea roho yangu." Alikuwa aki-geuzwa kwa sura ya Kristo.⁹

Halafu Paulo anamaliza maelezo yake juu ya Agano Jipy, na namna gani linafanana na Agano la Kale.

F. Lazima ya kuhubiri

Habari Njema waziwazi
(4:1-6)

4:1 Ndani ya mashairi 1-6 ya sura 4 Paulo anasema na nguvu kwamba ni kazi ya kila mtumishi wa Kristo kueleza Habari Njema wazi kabisa. Haifai wafiche neno lo lote. Lazima waeleze maneno yote wazi na roho ya haki.

Alikuwa amesema juu ya ajabu Mungu aliyotenda kumtayarisha na kumwezesha kuwa mtumishi wa faida wa Agano Jipy. Anaendelea kuonyesha kwamba heshima ya **utumishi** wa Kristo inamzuiza **kulegea**. Ndiyo, kuna maneno mengi kulegeza na kuhuzunisha mtumishi wa Kristo, lakini Bwana analeta rehema na neema kwa kila wakati wa hitaji. Hivi maneno ya kutia moyo ni makubwa kupita yale yanayoshusha roho.

Paulo **hakulegea**. Hakutenda na woga, lakini na uhodari, hata wakati alipokutana na vizuizo vikubwa sana.

4:2 Bila shaka mtume aliwaza tena juu ya walimu wa uwongo waliofikia kanisa la Korinto. Bila shaka walitumika na desturi ambazo walimu wa uwongo wanatumia kila mara, ndizo kuamsha hamu kutenda zambi, na **kuchanganya kweli ya Neno la Mungu na uwongo**. Bila shaka Paulo alikuwa akiwaza juu ya neno walimu hawa walipenda sana kufanya, ndiyo kuchanganya sheria na neema.

Desturi ya mtume ilikuwa namna nyininge. **Alionyesha wazi maneno ya kweli akijionyesha kuwa na haki kwa zamiri ya watu mbele ya Mungu. Maneno ya kweli yanaweza kuonyeshwa**

kwa njia mbili. Tunaonyesha **kweli** wakati tunapoitangaza waziwazi na maneno watu wanayoweza kufahamu. Lakini tunaionyesha vilevile ndani ya namna tunavyoishi maisha yetu ya kila siku mbele ya watu wengine. Paulo alionyesha kweli kwa njia hizi mbili. Alihubiri Habari Njema, na alitii Habari Njema ndani ya maisha yake mwenyewe. Kwa njia hii alijionyesha kuwa na haki **kwa zamiri ya watu mbele ya Mungu.**

4:3 Mtume alikuwa ameonyesha kwa-mba aliweka roho sana kufahamisha watu kweli ya Mungu, kwa njia ya ma-fundisho na matendo yake. Kama Habari Njema **ilifichwa** au kufunikwa kwa watu wengine, neno hili si kosa la Mungu, wala kosa la Paulo. Hata hivi wakati Paulo alipoandika maneno haya, alijua kwamba kulikuwa na watu wengine walioshindwa kuyafahamu. Watu gani? Wale wanaopotea. Kwa sababu gani walitiwa giza hivi?

4:4 Shairi 4 linaonyesha jibu la ulizo hili. Ni Shetani ambaye aliwatia giza. Anaitwa hapa **mungu wa dunia hii.** Amepofusha mafikiri ya wasioamini, kusudi wakae katika giza daima, **ili nuru ya Habari Njema ya utukufu wa Kristo ... isiwaangazie** na waokolewe.

Ndani ya dunia yetu juu linawaka wakati wote. Hatulioni saa zote kwa sababu kitu kingine kinaingia katikati yetu na juu. Ni vivyo hivyo na Habari Njema. **Nuru ya Habari Njema** inangaa wakati wote. Mungu anajaribu saa zote kuingaza ndani ya mioyo ya watu. Lakini Shetani anaweka vizuizo namna namna katikati ya wasioamini na Mungu. Labda ni kiburi, au uasi, au kuji-hesbu mwenyewe haki, au maneno mengine. Yote yanazuiza **nuru ya Habari Njema** isiiingie rohoni mwao. Shetani hataki watu kuokolewa.

Habari Njema ni juu ya **Kristo** katika **utukufu.** Yule anayeonyeshwa kwa waamini si mseremala wa Nazareti,

wala Kristo juu ya msalaba wa haya. Ni Bwana Yesu Kristo aliyekufa, aliyezikwa, aliyefufuliwa tena, na hata sasa yeye ni kwa mkono wa kuume wa Mungu mbinguni.

4:5 Ndani ya shairi hili moja tunasoma habari juu **yetu wenye**, ndizo habari mbaya zaidi, na juu ya *Kristo Yesu Bwana*, habari nzuri kupita zote.

Ni kama walimu wa uwongo wali-penda sana kuhubiri juu yao wenye. Paulo alijitenga na watu wale. Hakutaka kupoteza saa ya watu akihubiri juu ya neno lisilostahili. Mahubiri yake ya-likuwa juu ya **Kristo Yesu Bwana.** Ali-jaribu kuongoza watu kupiga magoti mbele ya Yesu Kristo na kumheshimu kama Bwana wa maisha yao.

Halafu mtume alijificha mwenyewe pamoja na watu waliotumika pamoja naye kwa njia ya kujiita **watumwa wenu kwa ajili ya Yesu.** Walikuwa watumwa tu, tayari kusaidia kwa njia yo yote kuleta watu karibu na Bwana Yesu.

4:6 Halafu Paulo anasawanisha wokovu wa mwenye zambi na kuingia kwa nuru wakati dunia ilipoumbwa.

Kwa asili **Mungu aliagiza nuru kungaa toka katika giza.** Aliagiza, “‘Nuru iwe;’ na nuru ilikuwa” (Mwa. 1:3).

Sasa Paulo anasema kwamba **Mungu yule aliyeagiza** kwa asili **kwa nuru kungaa toka katika giza ndiye aliyengaa katika miyo yetu.** Neno hili ni zuri sana. Wakati Mungu alipoumba dunia kwanza, *aliagiza* nuru kungaa. Lakini sasa kwa muumbo mpya, **Mungu mwenyewe anangaa katika miyo yetu.** Neno hili linagusa roho yetu zaidi!

Maneno yaliyotokea kwa mwanzo wa sura ya kwanza ya Mwanzo ni mfano wa maneno yanayotokea kwa muumbo mpya. Kwa asili Mungu aliumba mtu bila zambi. Lakini zambi iliingia, na giza kubwa pamoja na zambi.

Wakati Habari Njema inapohubiriwa, Roho ya Mungu anagusa moyo wa mtu,

namna alivyotulia juu ya uso wa maji wakati wa umbo wa kwanza.

Halafu Mungu anangaa ndani ya moyo wa mtu huyu, na kumwonyesha kwamba yeche ni mwenye zambi na anahitaji Mwokozi. Halafu shairi hili linakaa kueleza kwa sababu gani **Mungu alingaa ndani ya miyo yetu, ndiyo kutupa sisi nuru ya elimu ya utukufu wa Mungu katika uso wa Yesu Kristo.** Sasa ni kazi yetu kupitisha nuru ya elimu hii kwa watu wengine.

Tunaona mfano wa neno hili ndani ya maisha ya Paulo mwenyewe. Wakati aliposafiri kwa njia kwenda Damasiki, Mungu alingaa ndani ya moyo wake. Alifahamu kwamba yule ambaye alichukia, na alifikiri alikuwa amezikwa ndani ya kaburi moja kwa Yudea, alikuwa Bwana wa utukufu. Kuanza siku ile alikwenda kutangaza **nuru ya elimu ya utukufu wa Mungu** katika uso wa Yesu Kristo.

G. Chombo cha udongo kinachotayarishwa kwa mbingu (4:7-18)

4:7 Nyuma ya kusema kwamba ni lazima kutangaza Habari Njema na masemo watu wanayoweza kufahamu mtume Paulo anafikiri juu ya watu waliopewa hazina nzuri sana ya Habari Njema. **Hazina** ndiyo habari tukufu za Habari Njema. Lakini **chombo cha udongo** ni mwili zaifu wa mtu. Ni mballimbalii kabisa. Habari Njema ni kama almasi ya kugaa kabisa. Ni ajabu kufikiri ya kwamba almasi ya damani namna hii kinawekwa ndani ya chombo zaifu cha udongo kinachowenza kuvunjika upesi!

Kwa sababu gani Mungu aliamuru kwa **hazina hii** kuwa ndani ya **vyombo vya udongo?** Jibu kwa ulizo hili ni kusudi **ukubwa wa uwezo uwe wa Mungu, wala si wetu wenyewe.** Mungu hataki watu kuwaza juu ya watumishi wa dunia, lakini juu ya uwezo na ukubwa wake mwenyewe. Kwa sababu

hii aliweka Habari Njema na kusudi mikononi mwa watu zaifu, na mara nyingine kwa mikono ya watu wasioonekana vizuri. Ni lazima Mwumba apokee sifa na utukufu wote, si kiumbe.

Jowett alisema:

“Utumishi kwa Kristo ni kama kitu cha kufa kama ‘**ukubwa wa uwezo**’ ni wetu, na si wa Mungu. Uwezo namna hii haudumu, lakini unakauka mbio kama majani.”¹⁰

Wakati Paulo alipoandika shairi 7, bila shaka alikumbuka habari za Waamuzi 7. Pale tunasoma kwamba Gideoni aliwapa watu wa jeshi lake baragumu, na mitungi yenye taa ndani yao. Wakati alipowapigia mkono askari wake walagizwa kupiga baragumu zao na kuvunja mitungi. Wakati mitungi ilipovunjwa, nuru za taa ilingaa sana na kuogopesha adui zao kabisa. Walifikiri walikuwa wakifukuzwa na jeshi kubwa sana, si na watu mia tatu tu. Mafundisho ya habari hizi ni ya kwamba nuru ya jeshi la Gideoni ilingaa wakati mitungi ilipovunjika tu. Ni vivyo hivyo na Habari Njema. Wakati watu wanapokuwa na roho za kuvunjika na za kunyenyekeua tu mbele ya Bwana, Habari Njema inaweza kuonekana kwa njia yao na kungaa sana.

4:8 Mtume aliendelea kueleza ya kwamba hazina hii ikiwekwa kwa vyombi zaifu vya dunia, ni kama itashindwa, lakini sivyo. Inashinda wakati wote. Kwa macho ya watu inaonekana zaifu, lakini kwa kweli ina nguvu sana sana. Wakati mtume anaposema, **Tunasongwa pande zote, lakini hatufungwi,** maana yake ni kwamba **alisongwa** saa zote na adui na mambo magumu, lakini hakuzuizwa asitangaze Habari Njema waziwazi.

Tunaona mashaka, lakini hatushindwi. Mara nyingi Paulo, akiwa mtu, hakuwa na jibu kwa masumbuko yake, lakini Mungu hakumwacha kamwe

kukata tamaa. Kila mara alimfungulia njia ya kupona.

4:9 Tunateswa, lakini hatuachwi. Ni kama mara nyngine adui walikuwa karibu kumshinda, lakini Bwana hukumwacha kamwe kushindwa nao. **Tunatupwa chini, lakini hatuangamizwi,** maana yake hata kama Paulo aliumizwa mara nyngi ndani ya utumishi wake, Bwana alimsimamisha tena aweze kudenleka kutangaza Habari Njema ya utukufu.

Labda tunafazaika kwa sababu gani Bwana aliacha mtumishi wake kupata mteso na majoribu mengi sana. Tungefikiri angeweza kutumika vizuri kupita kama Bwana angalimwezesha kufanya hivi bila magumu haya yote. Lakini shairi hili linatufundisha maneno mengine kabisa. Mungu, mwenye akili ya ajabu sana, anaona kwamba ni vizuri kuacha watumishi wake kuteswa na ugonjwa, huzuni, mteso, maumivu, masumbuko na taabu. Kusudi lake ni kuvunja vyombo vya udongo ili nuru ya Habari Njema iweze kungaa vizuri kupita.

4:10 Maisha ya mtumishi wa Mungu ni pamoja na **kufa** wakati wote. **Bwana Yesu** mwenyewe, wakati alipoishi hapa duniani, alikutana na jeuri na mteso wakati wote, na wafuata wake watateendewa vivyo hivyo. Lakini hawashindwi. Tukikufa hivi kila siku watu wengine wanabarikiwa.

Kwa njia hii moja tu uzima wa Yesu unaweza kuonekana ndani ya miili yetu. Maana ya **uzima wa Yesu** hapa si zaidi uzima wake kama mtu duniani, lakini uzima wake kwa wakati wa sasa kama Mwana mtukufu wa Mungu mbinguni. Watu duniani wanaweza kuona uzima wa Kristo namna gani wakati yeze mwenyewe si duniani? Jibu hili ndilo: Wakati Wakristo wanapoteswa ndani ya utumishi wao kwa Bwana, uzima wake **unaonyeshwa katika miili yetu.**

4:11 Ndani ya shairi 11 tunaendelea kuwaza juu ya **uzima** toka **mauti.** Ni neno la asili kabisa la maisha yetu. Tunapata nyama tunayokula kwa sababu nyama ile ilikufa. Ni vivyo hivyo kwa maneno ya roho. Kwa kipimo Wakristo wanachoteswa na kumwanga damu yao kwa sababu ya imani yao, kanisa linalopata nguvu. Na Habari Njema inakaa kuenea kwa kipimo kanisa linaloteswa na kufukuzwa.

Ni nguvu kwa sisi kukubali kweli hii. Wakati mtumishi wa Bwana anapouawa, tunafikiri neno hili ni msiba mkubwa. Lakini ni desturi ya Mungu kutenda hivi. Si neno linalotukia mara moja moja tu. Kwa Wakristo kukaa saa zote katika **hatari ya kufa kwa ajili ya Yesu** ni njia ya Mungu kwa **uzima wa Yesu** **kuonyeshwa ndani ya miili yetu ya mauti.**

4:12 Mtume alijumlisha sasa maneno yote aliyokwisha kusema kwa njia ya kukumbusha Wakorinto ya kwamba walipokea **uzima** kwa sababu ya taabu na mteso mengi yeze mwenyewe ali-yopata. Alivumilia magumu mengi kwa kufikia Korinto na Habari Njema. Lakini yalikuwa faida, kwa sababu walikuwa wameamini Bwana Yesu na walikuwa na uzima wa milele sasa. Masumbuko na maumivu ya Paulo mwilini mwake yalikuwa faida ya roho kwa watu wengine.

Mara nyngi tunasihi Bwana kuituponyesha toka ugonjwa kusudi tuweze kumtumikia vizuri kupita. Labda inatupasa kushukuru Mungu mara nyngine kwa taabu na uzaifu namna hii ili uwezo wa Kristo uweze kuonekana ndani ya maisha yetu.

4:13 Mtume alikuwa amesema juu ya uzaifu wa mtu daima, ndicho chombo cha kibinadamu kilichowekewa Habari Njema. Habari hizi zilimshinda na kumelegeza rohoni? Sivyo. Imani yake ilimwezesha kukaa kuhubiri Habari

Njema kwa sababu alijua ya kwamba utukufu kupita kusema utafuata mateso haya yote.

Ndani ya Zaburi 116:10 mwandishi alisema. “**Ninaamini, na kwa sababu hii nitasema.**” Aliamini Bwana, na maneno aliyosema yalikuwa matunda ya imani yake kubwa. Paulo alisema hapa kwamba alikuwa na roho ile ya imani ya mwandishi wa zaburi, na hivi alisema, “**sisi vilevile tunaamini, na kwa sababu hii tunasema.**”

Taabu na mateso Paulo aliyopata hayakufunga kinywa chake. Mtu mwe-nye imani ya kweli hawezi kunyamaza.

4:14 Kwa sababu gani Paulo aliweza kuvumilia hatari ya kufa saa zote bila kutikisika? Aliweza kukaa kuhubiri Habari Njema bila woga kwa sababu uzima wa sasa si mwisho. Alijua ya kwamba Mkristo atafufuliwa nyuma ya mauti. Mungu yule **aliyefufua Bwana Yesu atafufua** mtume Paulo vilevile **pamoja na Yesu** na **kumsimamisha pamoja** na Wakorinto.

4:15 Akijua kabisa kwamba atafufuliwa nyuma ya mauti, mtume alikuwa tayari kuvumilia taabu kubwa. Alijua kwamba mateso haya yote yalizaa matunda namna mbili. Kwanza yali-kuwa baraka kubwa kwa Wakorinto, na neno hili lilizaa **mashukuru kuzidi kwa utukufu wa Mungu**. Haya yali-kuwa makusudi mawili yaliyoongoza Paulo ndani ya maneno yote aliyosema na kufanya. Aliweka roho juu ya **utukufu wa Mungu**, na baraka kwa wenzake.

Paulo alifahamu kwamba kwa kipimo alichoteswa, kwa kipimo hiki watu wengine walibarikiwa na **neema** ya Mungu. Kwa kipimo watu waliokolewa, kwa kipimo hiki kulikuwa na **mashukuru kwa Mungu**. Na kwa kipimo **mashukuru** yalipanda kwa **Mungu**, **Mungu** alitukuzwa.

4:16 Paulo alikuwa ameeleza kwa- mba alikuwa tayari kuvumilia taabu na

hatari yo yote kwa sababu alikuwa na tu- maini ya kwamba bila shaka atafufuliwa nyuma ya kufa kwake. Kwa sababu hii **hakulegea**. Hata kama nguvu ya mwili wake ilikaa kupunguka, mtu wake wa ndani alikuwa akifanywa mpya kila siku na kumwezesha kwenda mbele hata katika maneno magumu.

Hatuhitaji kueleza ya kwamba nguvu ya **mwili wetu wa inje inapooza**. Tu-naona neno hili wazi ndani ya miili yetu wenye. Lakini Paulo alifurahi kwa sababu Mungu anatoa kila siku uwezo ambao tunahitaji kwa utumishi wetu kwa Bwana.

4:17 Nyuma ya kusoma habari za mambo magumu yote yaliyopata mtume Paulo, ni nguvu kwa sisi kufahamu namna gani aliweza kuyaita **mateso mapesi**. Hayakuwa mapesi hata kidogo. Yalikuwa machungu na makali.

Lakini tunaweza kufahamu masemo yake wakati *alipoyasawanisha* na **utukufu wa milele** kwa wakati wa kuja. Na vilevile **mateso yale mapesi ni kwa dakika tu**, lakini utukufu ni **kwa milele**. Maneno tunayojifunza kwa wakati wa sasa duniani yatazaa matunda mazuri zaidi kwa sisi kwa wakati wa kuja.

F. E. Marsh aliandika maneno ya shairi hili kama jengo la mawe linalo-pumzisha na kufariji roho:

Utukufu

Utukufu mzito

Utukufu wa uzito wa milele

Utukufu wa uzito mkubwa na wa milele

Utukufu wa uzito mkubwa zaidi na wa milele

Utukufu wa uzito unaozidi mwingi sana na wa milele¹¹

4:18 Ndani ya shairi hili **kuangalia** si kuona na macho tu. Ni kuwaza kama vitu vina faida. **Vitu vinavyoonekana** kwa macho si maneno makubwa ya maisha ya sasa. Ni zaidi maneno magumu na mateso Paulo aliyovumilia. Vitu vikubwa vyta utumishi wake **havikuonekana**. Labda vilikuwa utu-

kufu wa Kristo, baraka aliyokuwa kwa wenzake, na zawabu inayongojea mtumishi mwaminifu wa Kristo kwa kiti cha hukumu.

H. Kuishi tukikumbuka Kiti cha Hukumu cha Kristo (5:1-10)

Maneno yanayofuata yanafungana na habari zilizotangulia. Paulo alikuwa akisema juu ya maumivu na mateso aliyokuwa akivumilia kwa saa ile, na utukufu uliotangulia. Masemo haya yalimfikisha kwa habari za mauti. Ndani ya mashairi haya tunapata mafundisho mengi zaidi ndani ya maandiko mazima ya Mungu, juu ya Mkristo na kufa.

5:1 Ndani ya shairi 1, mtume anasema juu ya mwili wetu wa sasa kama **nyumba yetu ya dunia, ndiyo hema. Hema** si kao mtu analokaa ndani yake siku zote. Ni kao wasafiri kwenda nao kwa safari yao.

Kufa kunasawanishwa na kuvunjwa kwa **hema hii**. Kwa wakati wa mauti **hema** inabomolewa. Mwili unazikwa ndani ya kaburi, lakini roho na nafsi za mwamini zinafikia Bwana.

Kwa mwanzo wa sura hii Paulo alionyesha kwamba alijua kabisa ya kama **nyumba yake ya dunia iki-haribiwa** (kwa njia ya mateso tulioona ndani ya sura 4) ana **jengo linalotoka kwa Mungu, nyumba isiyofanywa kwa mikono, iliyo ya milele katika mbingu**. Ona ya kwamba **hema** ni mbali na **jengo**. Hema inayotumiwa kwa wakati tu inabomolewa, lakini **nyumba mpya, nyumba ya milele katika mbingu** ni tayari kwa mwamini. Ni **nyumba linalotoka kwa Mungu**, maana ni Mungu ambaye anatupa sisi jengo hili.

Zaidi ya ile, ni **nyumba isiyofanywa kwa mikono**. Kwa nini Paulo alitupasha sisi neno hili? Miili yetu ya sasa haikufanywa kwa mikono. Basi kwa nini atasema vilevile ya kwamba miili yetu kwa wakati wa kuja, miili ya utukufu, haitafanywa kwa mikono? Maana ya

isiyofanywa na mikono ni “isiyo ya ulimwengu huu.” Tunaona neno hili katika Waebrania 9:11. Tunasoma pale, “Lakini Kristo akikwisha kuja kama kuhani mkubwa la maneno mema yatakayokuja, kwa hema iliyo kubwa na kamilifu zaidi, *isiyofanyika kwa mikono, maana yake, isiyo ya ulimwengu huu.*” Ndani ya 2 Wakorinto 5:1 Paulo alisema ya kwamba miili yetu ya sasa inafaa kwa maisha yetu ya sasa kwa dunia hii, lakini miili yetu kwa wakati wa kuja, miili yetu ya utukufu, haitakuwa ya dunia hii. Itafanywa kwa maisha mbinguni.

Mwili wa mwamini kwa wakati wa kuja utakuwa vilevile wa **milele katika mbingu**. Hautashindwa tena na go-njwa, kuoza, na mauti, lakini utakaa milele kwa kao letu mbinguni.

Labda msomaji akisoma shairi hili anafikiri mwamini atapokea jengo hili toka Mungu mara moja wakati atakopokufa, lakini neno hili si kweli. Hatapokea mwili wake wa utukufu kufika wakati Kristo atakaporudi kwa kanisa lake (1 Tes. 4:13-18). Wakati mwamini anapokufa, roho na nafsi yake zinafikia karibu na Kristo na kufurahishwa na utukufu wa mbingu. Mwili wake una-zikwa kaburini. Wakati Bwana atakaporudi, uvumbi utafufuliwa toka kaburi, Mungu atautengeneza kuwa mwili mpya wa utukufu, kisha mwili huu utakutanihwa tena na roho na nafsi. Kwa muda nyuma ya mauti ya mwamini kufika wakati wa kuja kwa Kristo kwa watakatifu wake, mwamini hana mwili, lakini hata hivi anajuana na furaha na baraka zote za mbingu.

Mbele ya kuacha shairi 1, vizuri tuonyeshe kwamba kuna maelezo matatu kwa maneno haya **nyumba isiyofanywa kwa mikono, iliyo ya milele katika mbingu**:

1. Mbingu.
2. Mwili kwa muda nyuma ya mauti na mbele ya ufufuko.

3. Mwili wa utukufu.

Haiwezekani kwa nyumba hii kuwa mbingu, kwa sababu ni **ya milele katika mbingu na “toka mbinguni”** (5:2). Hatu-somi kamwe ndani ya Maandiko juu ya mwili wa muda nyuma ya mauti na mbele ya ufufuko. Na vilevile nyumba isiyofanywa kwa mikono inasemwa kuwa ya *milele* katika mbingu. Neno hili lisingaliwezekana kwa mwili ulio kwa muda fulani tu. Ni kama elezo la tatu, kwamba nyumba ni mwili wa ufufuko na utukufu, ni elezo la haki.

5:2 Ndani ya mwili wetu wa sasa tunalazimishwa kuugua mara nyingi, maana unatuzuiza ndani ya maisha yetu ya roho. Tunataka sana **kuvikwa na makao yetu yanayotoka mbinguni.**

Ni kama ndani ya shairi hili Paulo alikomboa mfano wa hema na mfano wa mavazi. Labda alifanya hivi kwa sababu kazi yake ilikuwa kufanya hema, na alifahamu kwamba namna ya nguo iliyotumiwa kufanya hema ilitumiwa kufanya mavazi vilevile. Neno lililokuwa wazi kabisa ni ya kwamba alitaka sana kupokea mwili wake wa utukufu.

5:3 Maana ya uchi ni nini ndani ya shairi hili? Ni kusema kwamba mtu yule ni msiyeamini na hafuniki na haki ya Mungu? Au kwamba mtu aliyeokolewa atakosa kupokea zawabu kwa kiti cha hukumu cha Kristo? Au kwamba mtu aliyeokolewa hana mwili kwa muda nyuma ya kufa kufika ufufuko wake, na hivi ni roho bila mwili?

Mwandishi wa kitabu hiki anafikiri ni kuwa bila mwili, maana bila vazi. Paulo hakutazamia mauti na kuwa bila mwili. Alitazamia kuja kwa Bwana Yesu, wakati waamini wote waliokaza watakapopokea miili yao ya utukufu.

5:4 Shairi 4 linaonyesha ya kwamba tafsiri hii ni tafsiri ya haki. Mtume alisema ya kwamba **sisi tulio katika hemu hii** ya dunia hii **tunaugua kwa kulemewa; si kwa sababu tunataka**

mavazi haya kuondolewa, lakini tunataka kuvikwa, kusudi iliyo ya mauti imezwe na iliyo ya uzima. Hakutazamia hali ile *nyuma ya mauti na mbele ya kuja* kwa Kristo kwa kanisa, lakini neno litakalotukia *saa ya kuja* kwake wakati waamini watakapopokea mwili usiowezwa kufa tena.

5:5 Ni Mungu ... ambaye aliturenzenza sisi kwa ajili ya neno hili, ndilo ukombozi wa mwili. Neno hili litatimiza makusudi yake ya utukufu kwa sisi. Kwa wakati wa sasa roho na nafsi yetu zimekombolewa, lakini kwa wakati ule mwili wetu utakombolewa vilevile. Tunashangaa wakati tunapowaza juu ya Mungu akitufanya na kusudi hili – kwa hali ya utukufu – kuwa na nyumba isiyofanywa na mikono, *milele mbinguni!*

Tunaweza kujuu namna gani ya kwamba hakika tutakuwa na mwili wa utukufu? Tunaweza kujuu kwa sababu **Mungu ... ametupa sisi arabuni ya Roho.** Kama ilivyoelezwa mbele, **Roho** ya Mungu anakaa ndani ya kila mwamini, naye ni arabuni ya kwamba ahadi *zote za Mungu* kwa mwamini zitatimizwa. **Roho** ya Mungu mwenyewe ni arabuni ya kwamba maneno ambayo Mungu amekwisha kutupa sisi sasa kwa sehemu yatatimizwa kwetu siku nyiningine.

5:6 Kwa sababu Paulo aliamini kabisa ya kwamba ahadi hizi za damani zitatimizwa kweli, alikuwa na roho ya uhodari saa zote. Alijua angali alikuwa **katika mwili**, alikaa **mbali na Bwana.** Hakutaka neno hili zaidi, lakini alikubali iwe hivi kama ikimwezesha kutumikia Kristo hapa duniani na kusaidia watu wa Mungu.

5:7 Tunatembea kwa imani, wala si kwa kuona. Maneno haya yanahakikisha kwamba tuko mbali na Bwana. Hatuyatazama Bwana na macho ya miili yetu. Tumemwona kwa njia ya imani tu. Wakati tunapokaa kwanza ndani ya miili

yetu, bila kumwona na macho, hatuko karibu sana naye.

5:8 Ndani ya shairi hili tunarudi tena kwa mawazo ya shairi 6. Paulo alikaa na roho nzuri na ya uhoodari kwa sababu ya tumaini la mambo mema yaliyo mbele yake, na aliweza kusema kwamba **anapenda zaidi kutoka katika mwili, na kukaa pamoja na Bwana.**

Labda inaonekana kwamba shairi hili halipatani na maneno Paulo aliyosema sasa tu. Ndani ya mashairi yaliyopita alionyesha hamu yake kupata mwili wa utukufu. Lakini ndani ya shairi 8 anasema yeye **anapenda zaidi kutoka katika mwili, na kukaa pamoja na Bwana**, maana yeye ni tayari kukaa bila mwili kwa muda nyuma ya mauti na mbele ya kurudi kwa Bwana kwa kanisa.

Lakini hakuna mabishano. Kuna njia tatu zinazowezekana kwa Mkristo: Ya kwanza ni kukaa duniani ndani ya mwili wa dunia. Neno la pili ndilo kuwa bila mwili, lakini hata hivi kwa roho na nafsi kukaa na furaha pamoja na Kristo. Mwishoni ni kutimia kwa wokovu wakati tutakapopokea miili yetu ya utukufu kwa wakati Bwana Yesu atakapokuja tena. Kwa mawazo ya Paulo njia ya kwanza ni nzuri, ya pili ni nzuri kupita, na njia ya tatu ni nzuri zaidi.

5:9 Ingepasa mwamini **kujaribu sana kupendeza Bwana**. Mwamini haokolewi kwa sababu ya matendo mema, lakini kipimo cha zawabu atakayopokea siku nyingine kitapatana na uaminifu wake kwa Bwana. Inapasa mwamini kukumbuka ya kwamba *imani* na *wokovu* zinafungana pamoja, na *matendo* na *zawabu* zinafungana pamoja. Mwamini anaokolewa kwa neema ya Mungu kwa njia ya imani, si kwa njia ya matendo, lakini nyuma ya kuokolewa, inampasa kuweka roho sana juu ya kutenda kazi njema, na akifanya hivi atapewa zawabu.

Ona ya kwamba Paulo alitaka sana **kupendeza Bwana, au akiwa hapa, au kama asipokuwa hapa**. Alitaka utumishi wake duniani kupendeza Bwana wake, si neno kama alikuwa kwanza duniani, au kama alisimama mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo.

5:10 Kujua ya kwamba itatupasa sisi sote **kuonekana** mbele ya **kiti cha hukumu** cha Kristo, kunatusukuma sana kujaribu kumpendeza. Wala *hatuttaonekana* tu. Maana ya neno hili **kuonekana** ni kufunuliwa wazi. Maneno yote ya maisha yetu mazima yatafunuliwa wazi. Maisha na utumishi wetu mzima zitaonekana wazi mbele ya Bwana, si *kipimo* na *uzuri* wake tu, lakini hata *makusudi* yetu vilevile.

Hata kama ikiwezekana kwa mwa-minni kufanya zambi nyuma ya kuokolewa, zambi hizi hazitaangaliwa na kuhukumiwa kwa wakati ule. Miaka zaidi ya 1900 imepita tangu wakati Bwana Yesu alipobeba zambi zetu katika mwili wake juu ya msalaba. Alibeba deni nzima ya zambi, na Mungu hatazihukumu tena (Yn. 5:24). Kwa **kiti cha hukumu cha Kristo** utumishi wetu kwa Bwana utahukumiwa, na tutaona kama tutapata zawabu au hasara. Tumejua mbele kwamba tumeokolewa.

I. Utumishi wa Paulo na zamiri njema (5:11–6:2)

5:11 Watu wengi wanafikiri ya kwamba Paulo alikuwa akiwaza juu ya hukumu ya kuogofya ya zambi na hofu ya Gehena, na kwa sababu hii alikwenda pahali po pote akitafuta wapotevu na kuwavuta kupokea Habari Njema. Hata kama alifanya hivi, hii si maana kubwa zaidi ya shairi hili.

Paulo hawazi hapa zaidi juu ya mao-gofya ya Bwana kwa wasioamini, lakini juu ya kujaribu kutumikia na kupendeza **Bwana na heshima na woga**. Alijua ya kwamba maneno yote ya maisha yake yalikuwa wazi mbele ya Bwana. Alitaka

Wakorinto wajue vilevile ya kwamba alihubiri Habari Njema na haki na uaminifu.

5:12 Paulo alifahamu mara moja ya kwamba wasikiaji wataweza kufikiri ya kwamba alikuwa akijisifu mwenyewe. Hakutaka watu kufikiri hivi hata kidogo!

Hivi aliongeza, **Hatujisifu mbele yenu tena**. Si kusema ya kwamba alifanya hivi mbele, lakini watu walikuwa *wamemshitaki* tena na tena juu ya kufanya hivi, na alitaka kuondosha mafikiri namna hii ndani ya nia zao kabisa.

Basi kwa sababu gani alisema maneno mengi hivi kusimamia utumishi wake? Paulo alijibu kusema, “**Tunawapa ninyi sababu ya kujisifu kwa ajili yetu, hata mupate kuwa na maneno ya kuwajibu wale wanaojisifu kwa maneno ya inje, wala si kwa maneno ya moyo.**” Hakuweka roho juu ya kujisifu mwenyewe, lakini alifahamu ya kwamba walimu wa uwongo walimchambua na ukali mbele ya Wakristo wa Korinto. Alitaka wamaini kujua namna gani kujibu watu ambaao walimshitaki hivi mbele yao.

Alisema washitaki wake walikuwa watu **waliojisifu kwa maneno ya inje, wala si kwa maneno ya moyo** (sawanisha na 1 Sam. 16:7). Hakuweka roho juu ya uaminifu na haki ya roho.

5:13 Ni kama watu wengine walisema Paulo alikuwa mwenye wazimu. Hakukana neno hili. Alisema tu **kama amerukwa na akili, ni kwa ajili ya Mungu**. Neno washitaki wake walilowaza ni wazimu lilikuwa mapendo na ibada yake kubwa kwa Bwana. Lakini **akiwa na akili njema zote**, ni kwa ajili ya Wakorinto. Kulikuwa na njia mbili kueleza matendo ya Paulo: au yalikuwa tunda la bidii yake kwa Mungu, au aweze kusaidia waamini wenzake. Makusudi yake hayakuwa kujipatia mwenyewe faida. Makusudi ya washitaki wake yalikuwa nini?

5:14 Kila mtu anayejifunza habari za maisha ya Paulo atajiuliza, pamoja na kushangaa, nini ilisukuma Paulo kutumika na bidii kubwa hivi bila kuchoka wala kukumbuka faida yake mwenyewe. Tunaona jibu kwa ulizo hili hapa – **mapendo ya Kristo**.

Ni **mapendo ya Kristo** kwa sisi, au mapendo yetu kwa Yeye? Bila shaka ni mapendo yake kwa sisi. Tunampenda yeye kwa sababu moja tu: alitupenda sisi kwanza. Ni **mapendo** ya ajabu ya **Kristo** kwa Paulo ambayo yalimsukuma kutumikia Bwana wake wa ajabu.

Yesu alikufa badala yetu. Wakati yeye alipokufa sisi **sote tulikufa** – ndani yake. Kama zambi ya Adamu ilivyo-geuka zambi ya wazao wake, vivyo hivyo mauti ya Kristo yaligeuka mauti ya wale ambaao wanamwamini (Rom. 5:12-21; 1 Kor. 15:21, 22).

5:15 Hakuna njia kushindana na mafikiri ya Paulo. Kristo alikufa **kwa ajili ya wote**. Kwa sababu gani alikufa **kwa ajili ya wote**? Ili wale **walio hai** kwa imani **wasiwe hai tena kwa ajili yao wenyewe, lakini kwa ajili yake**. Mwokozi hakufa kwa ajili yetu ili tukae kuishi kujipendeza wenyewe, tukifanya maneno sisi wenyewe tunayotaka. Alikufa kwa ajili yetu ili tujitoe kwake tumtumikie na mapendo. Hili ni elezo la Denny:

Wakati Kristo alipokufa kwa sisi, alifanya hivi na mapendo makubwa sana, kusudi tuweze kuwa mali yake, mali yake tu, kwa milele. Hili lilikuwa kusudi kubwa la mauti yake.¹²

5:16 Labda Paulo alirudi tena kwa shairi 12 ndani ya mawazo yake pahali aliposema washitaki wake ni wenye kujisifu juu ya mambo ya kuonekana, si maneno ya roho. Aliendelea na habari hizi sasa na kufundisha ya kwamba wakati tunapofika kwa Kristo, kuna umbo mpya. **Tangu sasa hatuhukumu**

watu tena kwa namna ya dunia na kuonekana kwao, na taifa, na kazi yao. Tunawaona kama roho za damani ambao Kristo alikufia. Aliongeza ya kwamba hata **angalijua Kristo namna ya mwili**, maana kama mtu tu, haku-mjua hivi tena. Ni kusema hakumjua tena kama jirani yake kwa Nazareti, au hata kama masiya ya dunia. Sasa tunamjua kama Kristo aliyetukuzwa na aliye kwa mkono wa kuume wa Mungu. Tunajua Bwana Yesu karibu kupita mbele kwani anafunuliwa kwetu ndani ya Neno la Mungu kwa njia ya Roho Mtakatifu. Tunamjua karibu kupita watu wa dunia ambao walimjua wakati ali-pokuwa hapa duniani.

5:17 Kama mtu akiwa ndani ya Kristo, maana ameokolewa, **yeye ni kiumbe kipyä**. Wakati asipookolewa bado, angehukumu watu wengine kwa kipimo cha watu wa dunia. Lakini maneno haya yote yamegeuka sasa. Maneno ya **zamani yamepita; tazama maneno yote yamekuwa mapya**.

Mara nyingi watu waliookolewa sasa tu wanapenda kutaja shairi hili wakati wanapotoa ushuhuda wao. Lakini si vizuri kila mara. Inawezekana kwa wasikiaji kuwaza kwamba wakati mtu anapookolewa, desturi zake za mbele, mawazo maovu na ya tamaa, yanaondoshwa mara moja, na maneno yote yanageuka mapya ndani ya maisha yake. Tunajua neno hili si kweli. Shairi hili halionyeshi matendo ya mwamini, lakini pahali pake. Ona ya kwamba linasema juu ya mtu ye yote aliye **ndani ya Kristo**. Maneno haya matatu ni maneno makubwa. **Ndani ya Kristo, maneno ya zamani yamepita na maneno yote yamekuwa mapya**. Lakini ni huzuni kwa sababu “ndani yangu” neno hili si kweli mara moja! Lakini wakati ninapokaa kuendelea na kupata nguvu katika imani, ninataka kwa mwenendo wangu uweze kupatana kupita na kupita

na pahali pangu. Halafu siku nyingine, wakati Bwana Yesu atakaporudi, hali na mwenendo wangu zitapatana kabisa.

5:18 Maneno yote yanatoka kwa Mungu. Yeye ni asili na mwanzo wa **yote**. Hakuna njia kwa watu kujisifu. Ni Mungu huyu **ambaye alitupatanisha sisi naye mwenyewe kwa Yesu Kristo, naye alitupa sisi utumishi wa upatanisho**.

5:19 Utumishi wa upatanisho ndiyo habari ya kwamba Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akipatanisha ulimwengu naye mwenyewe. Kuna njia mbili yanayokubaliwa na Maandiko, kueleza shairi hili. Tunaweza kulifahamu kusema **kwamba Mungu alikuwa ndani ya Kristo**, ndiye Mungu. Neno hili ni kweli. Na tunaweza kufahamu vilevile **kwamba Mungu alikuwa, ndani ya Kristo, akipatanisha ulimwengu kwa yeye mwenyewe**. Alikuwa **akipatanisha ulimwengu**, lakini alikuwa akifanya hivi **ndani ya Bwana Yesu Kristo**.

Si neno kama tukikubali elezo gani. Ni wazi kabisa ya kwamba Mungu alikuwa akiondosha kitu kile ambacho kilitenga watu na Yeye, ndicho zambi. Mungu hahitaji kupatanishwa, lakini mtu *anahitaji kabisa* kupatanishwa na Mungu.

Asiwahesabie makosa yao. Wakati tunaposoma habari hizi mara ya kwanza, labda tunafikiri maana yao ni ya kwamba watu wote wanaokolewa, kwa njia ya kazi ya Kristo. Lakini mafundisho namna hii hayapatani hata kidogo na mafundisho ndani ya baki la Biblia. Mungu ametayarisha njia ili watu wasihesabiwe makosa yao. Njia hii ni tayari kwa watu wote, lakini inafaa tu kwa watu walio ndani ya Kristo. Wasioamini wanahesabiwa makosa yao, lakini kwa dakika wanapopokea Bwana Yesu kuwa Mwokozi wao, wanahesabiwa haki ndani yake, na zambi zao zinazimwa.

Zaidi ya kazi yake ya upatanisho, Mungu **aliwekeea** watumishi wake kuhubiri **neno la upatanisho**. Ni kusema aliwapa mapendeleo mazuri sana ya kwenda na kuhubiri habari hizi za utukufu kwa watu wote na pahali pote. Hakuwapa malaika agizo tukufu namna hii, lakini watu masikini na zaifu.

5:20 Ndani ya shairi 19 mtume ali-sema alipewa habari za upatanisho, na alitumwa kuhubiri habari hizi kwa wanadamu. Ndani ya 5:20 kufika 6:2 tunapata *muhtasari* wa neno hili upatanisho. Paulo alituacha kusikiliza habari alizohubiri kwa wasioamini wakati aliposafiri kwa inchi mbalimbali. Ni vizuri tufahamu neno hili. Paulo hakuagiza hapa Wakorinto kupatanishwa na Mungu. Walikuwa wameamini Bwana Yesu. Lakini alijulisha Wakorinto ya kwamba hizi ndizo habari alizohubiri kwa wasioamini pahali po pote alipokwenda.

Mjumbe ndiye mtu anayesimamia mtawala wa inchi yake mwenyewe ndani ya inchi nyingine. Paulo alisema kila mara juu ya utumishi wa Mkristo kama mwito wa heshima kubwa. Aliji-sawanisha na mjumbe wa **Kristo** kwa ulimwengu pahali tunapokaa. Alisema kwa ajili ya Mungu na **Mungu ali-wasihi** kwa ajili ya Kristo. Si desturi kwa mjumbe **kusihi**, lakini huu ni utukufu wa Habari Njema. Ni kama Mungu anapiga magoti na machozi aki-sihi wanaume na wanawake kupatanishwa na yeye mwenyewe. Mungu anakwisha kuondosha mipaka yote inayoweza kutenga Mungu na watu wasiwe na upatano mzuri. Bwana ali-kwisha kufanya yote aliyoweza kufanya. Sasa inapasa mtu kuacha vita na maasi yake na ukaidi wake, na **kupatanishwa na Mungu**.

5:21 Shairi hili linaonyesha namna gani Mungu alifungua njia kwa watu kupatanishwa naye. Namna gani anaweza kupokea wenyе zambi wanaofika kwake

na toba na imani? Neno hili lina-wezekana kwa sababu ya kazi ya kufaa Bwana Yesu aliyofanya kwa maneno ya zambi zetu, kusudi sisi tuweze kupatanishwa na Mungu sasa.

Ni kusema, Mungu **alifanya** Kristo **kuwa zambi kwa ajili yetu** – Kristo **asiyejua zambi** – ili sisi **tuwe haki ya Mungu katika yeye**.

Lakini haifai hata kidogo tufikiri kwamba wakati Bwana Yesu Kristo alipokuwa juu ya msalaba aligeuka kuwa *mwenye zambi* yeye mwenyewe. Haya si mawazo ya haki. Zambi zetu ziliwekwa *juu* yake, lakini hazikuwa *ndani* yake. Mungu alimfanyiza kuwa sadaka ya zambi kwa ajili yetu. Wakati tunapomwamini, tunahesabiwa haki na Mungu. Mkombozi wetu aliondosha mashitaki yote ya sheria.

Ni kweli ya baraka kubwa ya kwamba Mwokozi huyu **asiyejua zambi alifanya kuwa zambi kwa ajili yetu**, ili sisi **tusiojua haki, tuwe haki ya Mungu katika yeye**. Hakuna mtu atakayeweza kamwe kutolea Mungu mashukuru ya kutosha kwa neema kubwa namna hii isiyo na kipimo.

6:1 Watu wengine wanafikiri ya kwamba *ndani* ya shairi hili Paulo alisema na Wakorinto waweze kutumia sana **neema** waliopewa.

Sisi tunafikiri Paulo alikuwa akiende-lea kupasha tena habari alizokuwa aki-hubiri kwa wasioamini. Alikuwa ame-waambia wasioamini mbele habari za neema ya ajabu Mungu aliyotaka ku-wapa. Sasa anawasihi **wasipokee neema ile bure**. Haifai waache mbegu ya Habari Njema kuanguka jangwani. Sharti wapo-kee habari hizi za ajabu na kupokea Mwokozi.

6:2 Halafu Paulo alitaja sehemu ya Isaya 49:8. Ndani ya shairi hili tunaona Mungu akibishana na watu wake kwa sababu walikataa Masiya. Ndani ya shairi 7 tunaona Bwana Yesu aki-

taliwa na taifa la Israeli, na tunajua kwamba mwisho wa kukataliwa kwake ulikuwa mauti yake. Kisha, ndani ya shairi 8 tunasikia Yehova akiyakinisha Bwana Yesu kwamba Mungu amesikia maombi yake na atamlinda.

Siku ya wokovu nilikusaidia. Maneno haya ni juu ya ufufuko wa Bwana Yesu Kristo. Ni Kristo aliyeleta **wakati wa kukubaliwa na siku ya wokovu** wakati alipofufuliwa toka wafu.

Wakati Paulo alipohubiri Habari Njema, alitangaza habari hizi za ajabu kwa wasikiaji wake. **Tazama sasa ni wakati wa kubaliwa; tazama sasa ni siku ya wokovu.** Wakati ule Isaya aliotabiri juu yake kama **siku ya wokovu** ilikuwa imefika, hivi Paulo alionya watu kupokea Mwokozi wakati ilipokuwa kwanza **siku ya wokovu**.

J. Utumishi wa Paulo na mwenendo wake (6:3-10)

6:3 Sasa Paulo aliacha kusema juu ya mahubiri yake, na alianza kusema juu ya namna gani alitenda yeeye mwenyewe katika **utumishi** wake kwa Kristo. Alifahamu kwamba kuna watu wengine wanaotafuta uzuru wakati wote wasiskilize habari za wokovu. Wanaangalia maisha ya wahubiri karibu karibu kutafuta kuona maneno yanayoweza kuwapatia uzuru kukataa Habari Njema. Hivi alikumbusha Wakorinto kwamba **hakuwa kwazo, hata kidogo. katika maneno yote, ili utumishi wake usilaumiwe.**

6:4 Ndani ya mashairi 4-10 Paulo alionyesha namna gani alijaribu kutiliza utumishi wake bila laumu. Hakusahau kamwe kwamba alikuwa mtumishi wa Mungu Mjuu, na alitaka kuwa na mwendo uliostahili mwito namna hii.

Mashairi 4 na 5 yanapasha habari za maumivu Paulo aliopata mwilini mwake, ambayo yalionyesha kwamba alikuwa mtumishi mwaminifu na wa

haki ya Mungu. Ndani ya mashairi 6 na 7 tunaona alama nyingine za neema ya Mungu ndani ya maisha yake. Halafu ndani ya mashairi 8-10 alitaja maneno mengine yasiyopatana kila mara ndani ya utumishi wa Mkristo.

Katika saburi nyingi – maneno haya yanasema bila shaka juu ya uvumilivu wa Paulo kwa watu mmoja mmoja, kwa makanisa, na kwa mateso yote yaliyoweza kumwondosha katika njia ya kufuata Bwana na uaminifu.

Labda **mateso** yalikuwa taabu aliopata kwa jina la Kristo.

Mahitaji yanaweza kusema juu ya ukosefu wa vyakula, mavazi, na pahali pa kupanga.

Maumivu yaliweza kuwa mambo mabaya ambayo yalimzunguka.

6:5 Ndani ya Matendo 16:23 tunasoma kwamba Paulo alipata **mapigo** mengi. Kwa 2 Wakorinto 11:23 tutasoma juu ya **vifungo**, nyuma ya mahubiri yake ya Habari Njema (ya kwamba Mataifa waliweza kuokolewa namna Wayuda walivyookolewa), bila shaka watu walileta machafuko na **fitina**. Labda **taabu** ilisema juu ya kazi yake kufanya hema na kazi nyingine na mikono, na safari zake nyingi. **Kulinda** kunatufikirisha kwamba ilimpasa saa zote kukaa na ange kwa hila ya Shetani na adui zake ambao walijaribu kumteendea mabaya. Labda **alifunga chakula** na kusudi mara nyingine, lakini tunafikiri hapa alisema juu ya kukosa vyakula kwa sababu ya umasikini.

6:6 Alitenda **na usafi** tu ndani ya utumishi wake wote. Hakuna mtu aliyweweza kumshitaki juu ya usherati.

Labda alipewa **elimu** hii na Mungu. Neno hili linaonekana wazi kwa njia ya kweli nyingi za Mungu zinazofunuliwa ndani ya barua za Paulo.

Hakuhitaji kuhakikisha **uvumilivu** wake kwa Wakorinto! Ulionekana wazi kwa namna alivyovumilia na saburi zambi na kuanguka kwa! Alikuwa

mwenye kujitoa **kutendea** watu wa Mungu **mema** na roho ya mapendo.

Bila shaka maana ya **katika Roho Mtakatifu** ni ya kwamba Paulo alitii na kufanya maneno yote kwa uwezo wa Roho Mtakatifu.

Mapendo pasipo udanganyifu yaliyoonekana wazi ndani ya utumishi wa Paulo yalikuwa mapendo ya haki. Hakuenda kwa hila.

6:7 Neno la kweli linaonyesha kwamba Paulo alifanya maneno yote akitii **neno la kweli**. Yalipatana na habari Paulo alizohubiri, ndilo **neno la kweli**.

Katika uwezo wa Mungu – bila shaka mtume hakufanya kazi yake kwa uwezo wake mwenyewe, lakini alitege-mea nguvu toka **Mungu**. Watu wengine wanafikiri kwamba maneno haya yanasema juu ya maajabu ambayo mtume aliwezesha kufanya kwa sababu alikuwa mtume.

Tunasoma juu ya **silaha za haki** ndani ya Waefeso 6:14-18. Ni mfano wa mwenye matendo ya haki bila kugeuka. Kama zamiri yetu ni safi mbele ya Mungu, ni nguvu kwa Shetani kutumiza.

Maana ya **kwa mkono wa kuume na kwa mkono wa kushoto** haionekani wazi kabisa. Elezo moja ni ya kwamba kwa wakati wa vita zamani askari walishika upanga na mkono wa kuume, na ngabo na mkono wa kushoto. Hivi upanga unasema juu ya kupiga vita, na ngabo juu ya kujilinda. Kama ni hivi, kwa Mkristo kuwa mwenye mwenendo wa haki ni njia nzuri zaidi kupiga vita kwa Bwana, na kwa kujilinda na mishale ya Shetani.

6:8 Hapa na ndani ya mashairi 9 na 10 Paulo alisema juu ya maneno mengine yaliyo mbalimbali ndani ya utumishi kwa Bwana Yesu. Mara nyiningine mtumishi wa Bwana anafurahishwa kabisa kwa sababu ya baraka ya Bwana ndani ya kazi yake, na saa

nyingine anahuzunishwa sana. Ni mai-sha ya **utukufu na aibu**, ya kushinda, lakini mara nyingine inaonekana kwamba anashindwa, ya kupata sifa na kushtakiwa. Mtumishi wa kweli wa Mungu **anasingiziwa na kusifiwa**. Watu wengine wanamsifu kwa sababu ya bidii na uhodari wake, lakini wengine wanamshitaki tu. Watu wanamtenda kama mdanganyi, lakini yeche ni mtu **wa kwelli**. Yeye si mdanganyi, lakini mtumishi wa kweli wa Mungu Mjuu Sana.

6:9 Paulo hakuJulikana kwa watu wa dunia ambao hawakumfahamu, **lakini alijulikana sana** kwa Mungu na kwa waamini wenzake.

Ni kama **alikufa** kila siku, na **tazama**, alikuwa hai! Alifikuzwa, kuteswa, na kufungwa gerezani, lakini wakati alipofunguliwa alihubiri Habari Njema na bidii kubwa kupita mbele. **Aliazibiwa, lakini hakuuawa**. Ilikuwa **azabu** aliyopata kwa mikono ya watu. Walifikiri tena na tena kwamba walikwisha kumaliza maisha yake ya machafuko – lakini nyuma kidogo waliskia juu ya mahubiri yake kwa Kristo ndani ya miji mingine!

6:10 Paulo alipata huzuni ndani ya utumishi wake kwa Bwana, **lakini** hata hivi **alifurahi siku zote**. Alihuzunishwa kwa sababu watu walikataa Habari Njema, wakati watu wa Mungu waliopoanguka, na juu ya uzaifu wa imani yake mwenyewe. Lakini wakati alipofunguliwa juu ya Bwana, na ahadi za Mungu, roho yake ilipata furaha tena.

Paulo alikuwa **masikini**. Hatusomi ya kwamba alikuwa na vitu vya dunia na mali nyingi. Lakini waza juu ya watu wote waliotajirishwa rohoni kwa njia ya utumishi wake. Hata kama **hakuwa na kitu**, kwa njia nyingine alikuwa na vitu **vyote** vilivyo na faida ya kweli.

K. Paulo alisihi washirikiane naye na roho wazi na mapendo (6:11-13)

6:11 Sasa Paulo alisihi **Wakorinto**

waweze kumfunulia mawazo yao wazi. Yeye alikuwa amewajulisha mapendo yake bila maficho. Kwa njia ya kufungua kinywa chake wazi alionyeshea watu hawa mapendo yake na ya kwamba **moyo wake ulikuwa wazi**, maana alikuwa tayari kuwapokea na mapendo.

6:12 Hakuna kizuizo cha **mapendo** katikati ya Paulo na Wakorinto. Labda walikuwa na mapendo nusu tu kwa Paulo, na kwa sababu hii walikuwa na shaka kama iliwapasa kumpokea, lakini mapendo ya Paulo kwao yalikuwa bila mpaka.

6:13 Kama wakitaka kumpenda kwa kadiri ambayo yeye aliwapenda (alisema na wale waliokuwa **watoto** wake katika imani), waonyeshe mapendo yao kwaye **wazi kupita**. Paulo alifikiri juu yao kama baba. Ingewapasa kumpenda kama baba yao katika imani. Neno hili liliwezekana kwa uwezo wa Mungu tu, lakini ilipasa wampe Mungu njia kufanya hivi ndani ya maisha yao.

L. Paulo aliwasihi kujitenga na zambi za dunia (6:14 – 7:1)

6:14 Ndani ya shairi 13 Paulo alikuwa amesema na waamini kumwonyesha mapendo yao wazi kupita. Ndani ya shairi 14 aliwaonyesha ya kwamba walilweza kufanya hivi kwa njia ya kujitenga na namna zote za zambi na uzalimu. Bila shaka alikuwa akiwaza juu ya walilimu wa uwongo vilevile walioingia kanisa kwa Korinto.

Nira isiyo sawasawa inatufikirisha Torati 22:10: “Usilime na ngombe ndume na punda wakikokota jembe pamoja.” Ngombe ndume ilikuwa nyama safi na punda haikuwa nyama safi, na hawakukokota jembe vizuri pamoja. Lakini wakati waamini wanapofungwa nira pamoja na Bwana Yesu, wanaona kwamba nira yake ni laini, na mzigo wake ni mwepesi (Mt. 11:29, 30).

Mashairi haya ya 2 Wakorinto ni mengine yanayofundisha na uwezo zaidi

ndani ya Neno la Mungu juu ya kujitenga na dunia na zambi. Yanafundisha wazi kwamba inapasa mwamini kujitenga na **wasioamini**, uovu, giza, Beliali, na sanamu.

Bila shaka yanafundisha juu ya ndoa. Haifai mwamini kuoa msiyeamini. Lakini kama mwamini *ameoa msiyeamini mbele ya kuamini Mwokozi* yeye mwe nyewe, mashairi haya si ruhusu kujitenga. Ni mapenzi ya Mungu kwa mume na mke kukaa pamoja na tumaini kwamba yule aliyekuwa msiyeamini mbele aweze kuokolewa (1 Kor. 7:12-16).

Mashairi haya ni juu ya kazi ya biashara vilevile. Haifai kwa Mkristo kufanya upatano kutumika pamoja na msiyeamini. Namna gani Mkristo mwaminifu atawenza kufungana ndani ya kazi na mtu asiyependa Bwana Yesu?

Kwa maneno ya watu tunaokaa katikati yao kila siku, inapasa Mkristo kuwa na adabu na roho nzuri kwa wasioamini kuwakokota karibu na Bwana Yesu, lakini haifai kushiriki ndani ya furaha zao za dunia na zambi. Haifai wasioamini wapewe njia kufikiri kwamba Wakristo ni sawasawa nao. Na haifai kwa Mkristo mwaminifu kuwa mshiriki wa kanisa linalopokea wasioamini kuwa washiriki wao vilevile.

Mashairi 14-16 yanafundisha juu ya maneno yote mengine ya maisha yetu yasiyopatana.

Haki na uovu zinasema juu ya mwenendo wa watu. Nuru na giza zinatufikirisha ufahamu wa maneno ya Mungu. Kristo na Beliali ni juu ya amri, maana ni nani aliye na amri juu ya maisha yetu. Mwamini na msiyeamini ni juu ya imani. Hekalu la Mungu na sanamu ni juu ya kuabudu kwa mtu. Haki na uzalimu ni mbalimbali kabisa. Vivyo hivyo nuru haina upatano na giza. Wakati nuru inapoingia chumba, giza inafukuzwa. Haiwezekani kwa nuru na giza kuwa pamoja chumbani.

6:15 Maana ya **Beliali** ni “bila faida” au “uvu.” Hapa ni jina moja kwa Shetani. Haiwezekani kwa **Kristo** na Shetani kukaa na salama. Vivyo hivyo **mwamini** hawezu kuwa na ushirika na **msiyeamini**. Akijaribu kufanya hivi ni maasi juu ya Bwana.

6:16 **Sanamu** hazina mapatano na **hekalu la Mungu**. Ikiwa hivi, namna gani waamini wanaweza kufanya biashara na sanamu, maana wao ni **hekalu la Mungu aliye hai**. Sanamu hapa si kitu kilichochorwa toka mawe au mti tu, lakini kitu cho chote kinachotenga roho ya mtu na Kristo. Labda ni mali, au fura za dunia, au sifa ya watu, au vitu vingine.

Mtume aliona mifano mingi ndani ya mashairi ya Kutoka 29:45, Walawi 26:12 na Ezekiel 37:27 inayohakikisha kwamba sisi ni **hekalu la Mungu aliye hai**.

6:17 Ikiwa hivi, Paulo aliita waamini **kutoka**. Alitaja Isaya 52:11. Ni maagizo wazi ya Mungu kwa watu wake kujitenga na uovu. Haifai kwa Wakristo kukaa katikati ya maneno haya na kujaribu kuyatengeneza. Ni kusudi la Mungu kwa watu wake **kutoka** na kuacha maneno yale **machafu**. Kwa wakati wa Paulo yalikuwa zaidi maneno machafu ya wapagano, lakini bila shaka ya kwamba ni uovu namna zote, wa biashara, wa ushirika na waovu, au na dini.

Haifai kutumika na shairi hili kufundisha waamini kujitenga na waamini wengine. Wakristo wanaagizwa “kuchunga umoja wa Roho katika kifungo cha salama” (Efe. 4:3).

6:18 Mara nyingi ni nguvu sana kwa Wakristo kujitenga na vifungo vyta maisha yao ya miaka mingi mbele ya kupokea Bwana, kwa kutii Neno la Mungu. Mungu alijua neno hili mbele, na kwa sababu hii alisema ndani ya shairi 17, “Nitawapokea ninyi.” Sasa ndani ya shairi 18 anaongeza, “Ni-

takuwa baba kwenu, nanyi mutakuwa kwangu wana na binti, **Bwana Mwenyezi anasema.**” Zawabu ya wale wanaosimama pamoja na Kristo inje ya kambi ya uovu ni kuwa na ushirika na **Baba** kwa njia mpya na wa karibu kupita. Si kusema kwamba *tunageuka* wana na binti kwa njia ya kutii neno lake, lakini kwamba *tunaonekana* kama **wana na binti** zake wakati tunapotenda namna hii, na tutakuwa na furaha kubwa zaidi ya kuwa wana wake.

“Baraka ya kujitenga kweli na dunia ni ushirika wa utukufu na Mungu mkubwa mwenyewe.” (*mwandishi*)

Wakristo ndani ya makanisa namna mbalimbali wanashindana na neno hili, na wanauliza, “Inanipasa kufanya mini?” Jibu la Mungu ni hapa. Inawapasa kuondokea chama cha watu wasioheshimu na kutukuza Bwana Yesu kama Mwana mpendwa wa Mungu na Mwokozi wa ulimwengu. Wanaweza kutumikia Mungu vizuri kupita inje ya chama namna hii.

7:1 Shairi hili linafungana na maneno ya shairi la mwisho la sura 6.

Ahadi hizi ndizo zile zinazotajwa ndani ya 6:17-18: “Nitawapokea ninyi ... nitakuwa baba kwenu ... mutakuwa kwangu wana na binti.” Kwa sababu ya **ahadi** hizi za ajabu za Mungu, **ingetupasa sisi kujisafisha kwa uchafu wote wa mwili na wa roho**. Uchafu wa **mwili** unasema juu ya matendo yote ya mwili yasiyo safi. Uchafu wa **roho** unasema juu ya makusudi na mawazo.

Lakini Mungu hasemi juu ya zambi na uovu tu. Anasema vilevile juu ya **kutimiza utakatifu katika woga wa Mungu**. Hatuagizwi kuondosha tu mambو ambayo yanatuchafua, lakini inatupasa kugeuka kupita na kupita kufanana na Bwana Yesu ndani ya maisha yetu ya kila siku. Tutakaa kuendelea kufanana naye kupita na kupita kwa maisha yetu mazima hapa duniani. Si kusema kwamba tutaweza kamwe kugeuka wataka-

tifu kabisa tungali hapa duniani. Tuttageuka kupita na kupita sawasawa na Bwana Yesu Kristo kufika siku tutakapoonana naye uso kwa uso, na halafu tutakuwa sawasawa kwa milele. Ni kama tukiwa na woga na heshima kwa Mungu, tunapata hamu moyoni kuwa na utakatifu. Kama mtumishi mwaminifu wa zamani, ndiye Robert McCheyne, tuombe, "Bwana, unigeuze kuwa mtakatifu kabisa kwa kipimo inachowezekana kwa mtu aliye kwanza hapa duniani."

M. Paulo alifurahi kusikia habari nzuri toka Korinto (7:2-16)

7:2 Mutupe sisi nafasi miyonyi mwenu. Hakuna neno lililofaa kuzuiza Wakorinto wasifanye hivi. Paulo alienendelea kusema ya kwamba **hakukosea mtu, hakuharibu mtu, na hakudanganya mtu.** Si neno kama washitaki wake walisema nini juu yake, Paulo hakuumiza mtu ye yote, na hakujipatia faida ya mali toka mtu ye yote.

7:3 Paulo hakusema, wala hasemi sasa, neno na kusudi la **kuhukumu** Wakorinto kwa njia yo yote. Alisema tena na tena ya kwamba atawapenda kufika mwisho wa maisha yake.

7:4 Kwa sababu alipenda Wakorinto sana sana, alikuwa na **ujasiri** sana kusema nao. Na **alijisifu sana juu yao** mbele ya watu wengine. Alisema nao waziwazi, lakini haifai wafikiri neno hili lilionyesha kwamba hakuwapenda. Lili-kuwa alama ya kuwa alijisifu sana juu yao pahali gani alipokwenda. Labda Paulo aliwasifu zaidi juu ya kuwa na roho tayari kukutanisha mali pamoja kusaidia waamini masikini katika Yerusalem. Atasema juu ya neno hili tena nyuma.

Ninajaa faraja: ninazidi kufurahi katika mateso yetu yote. Kwa nini Paulo alikuwa na **furaha** hivi hata kama alikuwa na **mateso** ningi? Kwa sababu Tito alikuwa amefika kwake na habari

nzuri toka Wakorinto. Habari hizi zilimfariji na kutia roho yake nguvu.

7:5 Tulisoma mbele kwamba Paulo alitoka Efeso na alisafiri Troa kutafuta Tito. Wakati asipomkuta pale, alivuka maji na **kwenda Makedonia.** Lakini hata neno hili **halikutuliza** roho yake. Alikuwa **akiteswa** pande zote na adui; **inje** vita zilikuwa; **ndani** woga rohoni – bila shaka kwa sababu hakukutana na Tito.

7:6 Halafu **Mungu** mwenyewe **ali-fariji** Paulo kwa njia ya **kufika kwa Tito.** Kwa wakati ule Paulo alijuana na kweli tunayosoma ndani ya Mezali 27:17, "Chuma kinanoa chuma; ndivyo mtu anavyonoa uso wa rafiki yake." Waza juu ya furaha kubwa ya watumishi hawa wawili waaminifu wa Kristo wakati walipokutana, na Paulo alitoa maulizo yake mengi juu ya hali ya Wakorinto, na Tito alijaribu kuyajibu mbiombio! (Soma vilevile Mezali 25:25.)

7:7 Lakini Paulo hakufurahi sana juu ya kuonana na rafiki yake **tu.** Alifurahishwa vilevile na habari ya kwamba Tito **alifarijiwa** na namna Wakorinto walivyopokea barua ya Paulo.

Alifurahi vilevile ya kwamba Wakorinto walikuwa na hamu kumwona, hata kama walimu wa uwongo walijaribu kutenga waamini na Paulo. Lakini waamini walitaka sana kumwona, na walionyesha **maombolezo** ya kweli. Labda **waliombolea** kwa sababu walivumilia zambi kukaa kanisani bila kuihukumu, au kwa sababu wamesumbusha Paulo. Tito alijulisha Paulo vilevile ya kwamba waamini walimheshimu na **walitaka sana** kumpendeza.

Hivi Paulo hakufurahi juu ya kuja kwa Tito tu, lakini kwa sababu Wakorinto walikuwa wametii maonyo ya Paulo, na walikaa kumpenda.

7:8 Kwa maana hata niliwahuzunisha ninyi kwa barua yangu, sijuti,

hata ikiwa nilijuta kwa sababu ni-naona ya kwamba barua ile ili-wahuzunisha ninyi, lakini ni kwa saa kidogo tu.

Labda **barua** Paulo aliyotaja ilikuwa barua tunayoita 1 Wakorinto, au barua nyingine tusiyo nayo sasa, iliyohamakia Wakristo na ukali.

Kwa neno la **huzuni** ya Paulo juu ya kuandika **barua** hii, tufahamu neno moja vizuri. Kama alifikiri juu ya kuandindika 1 Wakorinto, bila shaka kuandika kwa barua hii kuliongozwa na Mungu. Maneno Paulo aliyoandika ya-likuwa maagizo ya Bwana; lakini Paulo alikuwa mtu tu, na alijuana na kushusha kwa moyo na masumbuko kama watu wengine.

Kwa kujumlisha maneno Paulo ali-yosema: Wakati Wakorinto waliposoma barua yake kwanza, iliwakemea na walihuzunishwa. Nyuma ya kutuma barua yenye na kuwaza juu ya kazi itakayofanya ndani ya roho zao, ali-huzunishwa. Hakufikiri kwamba ali-kuwa ametenda neno haya. Zaidi, kwa sababu ndani ya utumishi wake kwa Bwana, mara nyingine ilimpasa kuhuzunisha watu wengine kwa wakati mfupi, ili makusudi ya Mungu yaweze kutilimizwa ndani ya maisha yao.

Kwa mwisho ya shairi 8 Paulo ali-sema kwamba hata barua hii **iliwahuzunisha**, ilikuwa **kwa saa kidogo tu**.

Habari hizi zinaweza kusawanishwa na kazi ya mganga mwenye kupasua watu. Akititaji kuondosha sehemu ya mwili wa mgonjwa ambayo inakuliwa na ugonjwa, inampasa kukata ndani ya mwili wake kabisa. Hafurahi kuumiza mgonjwa hivi, lakini anajua ni lazima afanye hivi kwa kumrudishia afya yake. Kama mgonjwa ni rafiki ya karibu, mganga anahuzunishwa kwa sababu inampasa kumwumiza. Lakini anajua kwamba ataumia kwa muda mfupi tu, hivi yeye ni tayari kufanya hivi ili rafiki yake aweze kuponyeshwa.

7:9 Paulo **hakufurahi** kuhuzunisha Wakorinto, lakini **huzuni** yao ilikuwa kwa wakati mfupi tu na iliwaongoza **kutubu**. Kwa sababu ya toba yao mawazo yao na namna walivyoishi iligeuka. Hodge anasema kwamba “**Toba** haiko kugeuza makusudi yetu tu, lakini inageuza roho yetu na kuhuzunishwa juu ya zambi na machukio yetu, na kutugeuza kwa Mungu.”¹³

Huzuni ya Wakorinto ilikuwa mbele ya Mungu; namna Mungu aliyopenda kuona. Kwa sababu walikuwa na huzuni na toba ya kweli, hawakupata hasara kwa sababu ya makemeo ya Mtume Paulo.

7:10 Hapa tunaona tofauti ya **huzuni mbele ya Mungu na huzuni ya dunia**. **Huzuni mbele ya Mungu** ni huzuni mtu anayopata nyuma ya kutenda zambi, na ambayo inamsukuma kutubu. Anafahamu Mungu anasema na roho yake, na anafungana na Mungu na kuacha zambi yake.

Wakati Paulo aliposema **huzuni iliyo mbele ya Mungu inafanyiza toba inayoleta wokovu**, labda hakufikiri wokovu wa roho tu. Wakorinto walikuwa wameokolewa. Hapa neno hili linatumwi kusema juu ya *kufunguliwa* toka utumwa wa zambi, au taabu yo yote ambayo mtu aliyo nayo.

Maneno haya **isiyo na majuto** yanasema juu ya toba, na juu ya wokovu vilevile.

Huzuni ya dunia si toba ya kweli. Ni majuto tu. **Inazaa** uchungu, roho ya nguvu, kukata tamaa, na **mauti**. Tunaona mfano wa neno hili ndani ya maisha ya Yuda. Hakuwa na huzuni juu ya taabu ambayo zambi yake ililettea Bwana Yesu, lakini alitibu tu kwa sababu ya taabu kubwa sana aliyovuna yeeye mwenyewe kwa njia yake.

7:11 Paulo alitaja Wakorinto wenye kama mfano wa maneno ali-yosema kwa mwanzo wa shairi 10. **Huzuni iliyo mbele ya Mungu** ili-

onekana kweli ndani ya maisha yao. Halafu aliendelea kutaja mengine ya matunda ya huzuni yao.

Kwanza, ilileta **bidii**. Ndani ya 1 Wakorinto waamini hawakuweka roho juu ya hali ya roho ya kanisa, lakini sasa walikuwa wamegeuka.

Ya pili, **walijionyesha kuwa wenyehaki kabisa**. Si kusema kwamba walijaribu *kujionyesha kuwa bila kosa* ndani ya neno hili. Walijaribu sana kuteengeneza maneno haya ili wasiwe na hatia ndani yao tena.

Na kukasirika gani. Labda walikasirikia mwenye zambi kwa sababu ya kulaumu jina la Kristo. Na labda walijihukumu wenyewe vilevile kwa sababu waliacha ubaya huu kuendelea kwa muda mrefu bila kuuhukumu.

Woga gani – bila shaka walitenda **wakiogopa** Bwana, lakini labda walikuwa wakiogopa vilevile kufika kwa mtume, kama ikimpasa kuja na fimbo.

Hamu gani – hamu kwa kufika kwa Paulo na kuonana naye, na labda **hamu** kwa ubaya huu uweze kutengenezwa.

Bidii gani – imeelezwa kuwa **bidii** kwa utukufu wa Mungu, kwa mwenye zambi kurudishwa karibu na Mungu, wao wenyewe waweze kusafishwa toka uchafu, au kusimama pamoja na mtume.

Kisasi gani – waliweka roho sana kuazibu yule aliyetenda zambi kanisani. Walikusudi kabisa kwa zambi kuazi-biwa.

Halafu Paulo aliongeza: **Katika maneno yote mumejionyesha kuwa safi katika neno hili**. Si kusema kwamba hawakuwa na hatia vilevile mara nyininge, lakini kwamba walikuwa wamefanya sasa kila neno ambalo ilipasa wafanye mbele.

7:12 Kuna maneno matatu ndani ya barua hii ambayo yanatufazaisha ndani ya shairi hili. Paulo alifikiri juu ya barua gani wakati alipoandika: **Hata nili-waandikia ninyi?** Ulizo la pili ni kama **mtu gani alikuwa amefanya zambi?**

Ulizo la tatu ndilo **mtu gani alikosewa?** Shairi hili linajibu maneno matatu yanayoweza kutufazaisha: Labda barua hii ilikuwa ile tunayoita 1 Wakorinto, au nyingine tusiyo nayo. Labda mtu aliye-fanya zambi alikuwa yule ambaye tulisoma habari zake katika 1 Wakorinto 5, au mwasi mwingine kanisani. Kama Paulo alisema juu ya mtu ambaye ali-fanya zambi, halafu yule aliyeumizwa alikuwa baba ya mtu mwenyewe. Au kama mtenda mabaya alikuwa mwasi, halafu yule aliyeumizwa alikuwa Paulo mwenyewe, au mtu mwingine.

7:13 Barua ya Paulo ilitimiza kusudi lake, na Paulo **alifarijiwa**. Wakorinto walikuwa wametubu na kufungana naye, na Paulo alifurahi juu ya **Tito alieburudishwa** na Wakorinto.

7:14 Ni kama Paulo alisifu Wakorinto kwa masikio ya **Tito** mbele ya kumtuma kwao. Sasa alisema kwamba **Tito** alikuta kwamba **kujisifu kwa Paulo** kulikuwa kweli.

7:15 Ni wazi ya kwamba Tito hakujuwa kwamba watu watampokea namna gani wakati atakapofikia upande wa kusini wa Yunani. Labda alifikiri ya kuwa atapata matata. Lakini wakati alipofika, Wakorinto walimpokea na mapendo, na walitii mafundisho yote ambayo Paulo aliwaletea.

Wakati mtume aliposema kwamba walipokea Tito kwa **woga na kutetemeka**, hakufikiri hofu kubwa, lakini na heshima mbele ya Bwana na kutaka sana kumpendeza.

7:16 Wakati Paulo aliposema alikuwa na **imani juu yao katika maneno yote**, hakufikiri ya kwamba alifikiri Wakorinto hawawezi kufanya zambi au kuanguka. Alitaka kusema kwamba alikuwa na **imani ndani yao**, hata juu ya mambo ambayo yaliwasumbusha ndani ya 1 Wakorinto.

Shairi hili linamaliza sehemu ya kwanza ya 2 Wakorinto. Sehemu hii ilikuwa juu ya utumishi wa mtume, na

kusudi la kupatisha nguvu ushirika wake na Wakorinto. Sura 8 na 9 ni juu ya “baraka ya kutoa.”

II. MAONYO YA PAULO WATIMIZE SADAKA KWA WAAMINI WA YERUSALEMA (Sura 8, 9)

A. Wengine waliotoa na ukarimu (8:1-9)

8:1 Paulo alitaka waamini kujua habari za ajabu ya namna **neema ya Mungu** ilionekana katikati ya Wakristo ndani ya **makanisa ya Makedonia** (upande wa kaskazini wa Yunani). Filipi na Tesalonika ndio miwili ya miji pahali makanisa yaliposimamishwa.

Makanisa haya walionyesha kwa njia ya **ukarimu** wao ya kwamba walikuwa wamepokea **neema ya Mungu**.

8:2 Wakristo hawa walikuwa wamepata **majaribu makubwa ya mateso**. Ni desturi ya watu wanaopatwa na taabu namna hii kuchunga mali yao kwa mahitaji yao kwa wakati wa kuja. Neno hili ni kweli kwa watu wasio na mali nyingi, kama Wamakedonia. Hata hivi walikuwa na **furaha** tele ndani ya Bwana, na wakati waliposikia habari za mahitaji ya waamini katika Yerusalem, waliongeza **ukarimu** juu ya **mateso, furaha na umasikini** wao wenyewe.

8:3 Na hawakutoa kwa kipimo cha mali ambayo walikuwa nao, lakini **zaidi ya uwezo wao**. Na walifanya hivi na **kutaka kwao wenyewe**, bila kusukumwa na mtu.

8:4 Walitaka sana kufanya hivi, hata walisihi Paulo kuwaruhusu kushiriki ndani ya zawadi hii kwa waamini katika Yerusalem. Labda Paulo alisita kupo-ke za zawadi yao, akijua kwamba wao wenyewe walikuwa masikini kwa wakati ule, lakini wao walitaka sana kufanya hivi.

8:5 Labda Paulo **alitumaini** ya kwamba watatoa kwa kipimo kilichokuwa

desturi kwa watu kutoa **tu** nyuma ya kusukumwa kufanya hivi. Lakini Wamakedonia walikuwa na roho namna nyingine! Wakristo hawa wapendwa **walitoa kwanza** zawadi kubwa kupita zote – **walijitoa wenyewe**. Nyuma yake ilikuwa nyepesi kwao kutoa mali yao. Wakati Paulo aliposema kwamba **kwanza walijitoa wenyewe, wakampa Bwana, na sisi vilevile kwa mapenzi ya Mungu**, maana ya maneno haya yali-kuwa kwamba walikuwa wamejitoa wenyewe mzima kwa Bwana kwanza, na sasa walikuwa tayari kusaidia Paulo na zawadi hii kwa Yerusalem. Ni kama walisema, “Utuambie nini inatupasa kufanya, kwani wewe ni mtume wa Kristo, Bwana wetu.” G. Campbell Morgan anasema, “Zawadi kwa kazi ya Bwana zina faida tu kama wale amba wanazitoa wamejitoa wenyewe kwa Mungu.”

8:6 Mtume alifurahi sana juu ya mfano wa Wamakedonia, hata sasa alitaka Wakorinto kuwaiga. Hivi **alionya Tito kutimiza** kazi aliyanza wakati alipowafikia mara ya kwanza. Wakati ule alikuwa amesema nao juu ya zawadi hii. Wakati aliporudia Korinto sasa, alitaka waamini watoe zawadi yao namna walivyokusudi kufanya mbele.

8:7 Wakorinto walikuwa wenyewe kujulikana kwa njia nyingi, hivi Paulo alitaka watoe zawadi ya kuzidi vilevile. Aliwasifu kwa **imani yao, kwa usemi, elimu, bidii, na kwa mapendo yao** kwaye. Ndani ya barua yake ya kwanza alikuwa amewasifu kwa elimu na usemi wao. Sasa aliongeza maneno mengine vilevile.

Kwa imani – inatufikirisha imani ya nguvu kwa Mungu, **zawadi** ya imani, au **uaminifu** wao ndani ya matendo yao na watu wengive.

Kwa usemi – ndio uwezo wao kusema kwa lugha. Tulisoma juu ya neno hili sana ndani ya barua ya kwanza.

Kwa elimu – labda inasema juu ya ufahamu wao wa kweli za Mungu.

Kwa bidii – kwamba waliweka roho sana juu ya maneno ya Mungu.

Mwishoni, **mapendo yao** kwa Paulo yalistahili sifa. Sasa Paulo alitaka kuongeza neno lingine, “ndilo ukarimu.” Denny anatuonya juu ya:

... mtu anayeweka roho sana juu ya maneno ya Mungu, aliye na bidii, mwenye roho ya maombi na mapendo, anayeweza kufundisha ndani ya Kanisa, lakini inamshinda kuachana na mali yake.¹⁴

8:8 Paulo hakutoa amri ya nguvu hapa. Alitaka kujaribu **kweli** ya **mapendo** ya Wakorinto, na kuyasawanisha na bidii ya Wamakedonia kwa neno la zawadi hii. Wakati Paulo aliposema kwamba **hasemi kama amri**, maana yake si kwamba hakusema kwa maongozi ya Mungu, lakini kwamba ingewapasa kutoa kwa sababu walitaka kufanya hivi. “Mungu anampenda ye ye anayetoa kwa furaha” (2 Kor. 9:7).

8:9 Halafu Paulo alianza kusema juu ya shairi lenye maana kubwa zaidi ya barua hii, na katuonyeshea Mwenye ukarimu mkubwa kupita watu wote walioishi tangu zamani.

Neno hili **neema** lina maana kupita moja ndani ya Biblia, lakini bila shaka hapa maana yake ni ukarimu. Bwana Yesu alikuwa mwenye ukarimu sana hata *alitoa yote aliyokuwa nayo* kwa ajili yetu ili sisi **kwa umasikini wake tupate kuwa watajiri** kwa milele.

Shairi hili linafundisha kwamba Bwana Yesu alikuwa mbele, tangu zamani. Wakati gani alikuwa **tajiri?** Hakuwa tajiri wakati alipokuja duniani kama Mtoto mchanga kwa Betelehemu! Na hakuwa tajiri kwa miaka makumi tatu na tatu alipoishi na kusafiri hapa duniani kama mgeni bila nyumba katika dunia hii ambayo aliumba. Alikuwa tajiri kwa zamani ya kale, wakati alipokaa pamoja na Baba mbinguni. Lakini **alikuwa masikini**, si kwa Betelehemu tu, lakini

kwa Nazareti, Getesemane, na Golgota vilevile. Ilikuwa kwa ajili yetu, hata sisi kwa **umasikini wake tupate kuwa watajiri**.

Neno hili ni kweli kabisa, na kwa sababu hii ingetupasa sisi kujitoa kwake na furaha kubwa zaidi, pamoja na vyote tulivyo navyo.

B. Maonyo mazuri watimize sadaka (8:10, 11)

8:10 Sasa Paulo aligeuka na kusema kwa Wakorinto. Walikuwa wamefikiri kukutanisha mali kwa watakatifu masikini hata mbele ya wakati Wamakedonia walipofanya shauri kufanya hivi. Wakorinto walikuwa wameanza kukutanisha mali hata mbele ya Wamakedonia. Vizuri wamalize sasa kukutanisha mali hii waliyokusudi kutuma tangu **mwaka mmoja**. Neno hili litahakikisha uaminiifu wao.

8:11 Paulo alisema nao kuacha neno ambalo liliwazuiza, na **watimize** neno hili ambalo **walikuwa tayari** kutenda. Wafanye hivi kwa kipimo walichoweza kwa saa yenye, bila kufikiri kwamba labda kwa wakati wa kuja watakuwa na mali kupita.

C. Mashauri mema matatu kuongoza watu kutoa na ukarimu (8:12-15)

8:12 Ni kama Wakorinto walikuwa wakikawa kukutanisha zawadi yao kwa watakatifu masikini kwa Yerusalem kwa sababu walitaraji watakuwa na mali kupita kutuma nyuma ya wakati. Sasa Paulo aliwakumbusha kwamba neno kubwa si hesabu ya mali waliyotuma. Kama wakitaka kweli kufanya hivi na kushiriki ndani ya neno hili jema, Mungu atapokea zawadi yao, si neno hata kama ni zawadi ndogo. Neno kubwa ni hali na hamu ya roho yao.

8:13 Paulo hakutaka kubebesha Wakorinto **mzigo wa mali**. Hakutaka kanisa la Yerusalem **litulie** na kanisa

kwa Korinto lilumiwe au kufanywa masikini.

8:14 Shairi hili linaonyesha namna gani Mungu anataka wenye mahitaji katika kanisa la Bwana Yesu Kristo ku-saidiwa. Wakati kuna mahitaji katikati ya Wakristo kwa pahali fulani, ni kusudi la Bwana kwa mali toka pahali pengine kuwafikia kusaidia watu wa pahali pale. Kwa njia hii watu wa makanisa pahali po pote duniani **watasaidiwa sawasawa**.

Hivi wakati Paulo alipokuwa aki-andika barua hii, mali ilitumwa toka Korinto, Makedonia, na pahali pengine kusaidia kanisa kwa Yerusalem. Lakini labda kwa wakati wa nyuma waamini wa Yerusalem watakuwa na mali ya kutosha, na watakatifu wa Korinto watakuwa na **mahitaji**. Kwa wakati ule watasaidiwa na waamini wa pahali pengine.

8:15 Tunaona mfano wa mafundisho yale kwa Kutoka 16:18. Wakati Wa-israeli walipotoka kukusanya mana, wengine waliweza kukutanisha kupita wengine. Si neno. Wakati mana iliyogawanywa, kila mtu alipokea kipimo sawasawa cha mana. Hivi “**Yeye aliyekusanya vingi hakuzidi, naye aliyekusanya vidogo hakuwa na hitaji.**” Mtu akijaribu *kujivimbisia* mana kupita, ilizaa mabuu!

Halikuwa ajabu kwa watu wote kupokea kila mtu kipimo sawasawa. Ilifanyikana kwa sababu watu wale waliokuwa na mana zaidi *walitoa nusu* yake kwa wale wasiokuwa ya kufaa.

Mtu mmoja ambaye hatujui jina lake aliandika:

Ni kusudi la Mungu kwa kila mtu kuwa na sehemu ya vitu vema nya maisha haya. Wengine wanakusanya kupita wengine. Ingepasa wale walio na vitu vingi kusaidia wale walio na vitu nusu. Mungu anakubali kwa watu kuwa na vi-

pimo mbalimbali nya mali, si kwa watajiri kujifurahisha nayo wao wenye tu, lakini wawze kui-shiriki na watu masikini.

D. Ndugu wema watatu watayarische sadaka (8:16-24)

8:16 Ndani ya mashairi 16 na 17 yanayofuata Paulo alisifu **Mungu** kwa roho nzuri ya **Tito**. Kwanza alishukuru Mungu aliyetia bidii ile ile kwa Wakorinto **katika moyo wa Tito**. Wao wa-wili walishiriki **mzigo ule** kwa waamini wale.

8:17 Paulo alikuwa ameonya Tito kwenda Korinto na barua hii, lakini hakuhitaji kufanya hivi. Tito alitaka kwenda **kwa mapenzi yake mwenye-we**. Bila shaka alikuwa Tito aliye-peleka barua hii kwa Wakorinto.

8:18 Ndani ya mashairi 18-22 tunasoma juu ya Wakristo wawili wengine waliokwenda pamoja na Tito kwa safari hii. Mashairi 18-21 yanatujulisha habari za mtu wa kwanza, na shairi 22 habari za mtu wa pili. Hatujui majina yao.

Mashairi haya yana faida kuonyesha kwamba Paulo aliweka roho sana juu ya namna gani kuchunga mali hii ili hakuna njia kwa watu kumshitaki juu ya neno hili.

Ndugu ya kwanza aliitwa **aliye na sifa** kwa sababu ya kazi yake **katika Habari Njema**. Watu wengine wana-fikiri alikuwa Luka, wengine Sila, au Trofimo. Tunafikiri kwamba majina yao hayakutajwa na kusudi. Mara nyingi wanafunzi wa kweli wa Bwana wana-mfuata bila kuonekana katikati ya watu. Ilikuwa hivi na msichana mdogo ambaye Mungu alitumika sana naye ndani ya maisha ya Namani, mkoma. Ilikuwa vivyo hivyo ndani ya maisha ya kijana mdogo aliyetolea Bwana chakula chake nusu.

8:19 Ndugu huyu tusiyejua jina lake **alichaguliwa na makanisa** kusafiri nao kupeleka **zawadi hii**. Alichaguliwa kuwa mmoja wa wajumbe kubeba za-

wadi hii. Mtume alifikiri juu yake mwenyewe na wengine kama watumishi au wenye kusimamia kazi hii ya neema. Walifanya hivi kwa **utukufu wa Bwana mwenyewe**. Na walitaka kwa njia hii kuonyesha hamu yao kutumikia wamini masikini katika Yerusalem.

8:20 Mtume Paulo, akiwa mwenye akili alifahamu ya kwamba haifai kwa mtu mmoja peke yake kuchunga mali hii, au kuitoa kwa mikono ya mtu mmoja mwininge peke yake. Sharti watu wawili au zaidi waichunge pamoja. Hii ndiyo maana ya neno alilosema ndani ya shairi 20. Alitaka kuepuka neno lo lote baya lisemwe juu ya namna gani **zawadi hii** kubwa ichungwe.

8:21 Maana ya **kufikiri maneno yaliyo mema** ni kuweka roho yafanywe kwa haki. Paulo alitaka maneno yote aliyofanya kuwa haki, si **kwa macho ya Bwana tu**, lakini **mbele ya watu vilevile**.

8:22 Tunaona **ndugu** mwininge tusejua jina lake, ndani ya shairi hili. Paulo alimchagua kusaidia ndani ya kazi hii kubwa. **Alikuwa na bidii** katika maneno mengi mbele, na sasa alikuwa na bidii zaidi kwa sababu ya **tumaini lake kubwa** ndani ya Wakorinto.

8:23 Hivi Paulo alisema kama **mtu akitaka habari** juu ya wanaume hawa watatu, Wakorinto waliweza kuwaambia kwamba **Tito** alikuwa **mshiriki** wa Paulo na **mtenda kazi pamoja naye** kwa ajili ya Wakorinto, na ya kwamba ndugu wale wawili wengine walikuwa **mitume ya makanisa**, na **utukufu wa Kristo**. Ilikuwa sifa kubwa kwa watu hawa kwa sababu wao ni **mitume ya makanisa**. Walifanyaiza kazi ya Bwana kungaa mbele ya macho ya watu, na wanaonyesha utukufu wake.

8:24 Hivi inapasa Wakorinto kupo-kea watu hawa vizuri. Waonyeshe kwamba Paulo **hakujisifu bure** juu yao wakati alipowapa zawadi hii kubwa ku-

pelekewa waamini katika Yerusalem. Neno hili litaonyesha kwa makanisa mengine kando kando **mapendo** yao kwa Kristo.

E. Paulo alisihi Wakorinto kuonyesha kwamba hakujisifu bure juu yao (9:1-5)

9:1 Paulo hakuhitaji **kuandikia** Wakorinto juu ya kutuma mali kusaidia **waamini** wenye hitaji – lakini alifanya hivi hata hivi. Walikuwa wameonyesha toka mwanzo kwamba walitaka kushiriki ndani ya sadaka kwa waamini kwa Yerusalem. Walikuwa na roho tayari, lakini hawakutimiza neno walilokusudi kufanya. Ni neno hili ambalo lilimsukuma kuwaandikia barua nyingine.

9:2 Ilikuwa wazi ya kwamba walikuwa na **nia tayari**. Tangu mwanzo walikuwa wameonyesha **bidi** yao, hata Paulo alijisifu juu yao kwa Wakristo katika Makedonia. Aliwaambia kwamba **Akaya ilikuwa tayari tangu mwaka mzima**. **Akaya** ilikuwa kwa upande wa kusini wa Yunani, na hapa inasema juu ya mji wa Korinto uliokuwa pale. Wakati Wakristo wa Makedonia waliposikia kwamba Wakristo katika Korinto walikuwa tayari tangu mwaka mmoja, bidii yao (ya Wamakedonia) iliamshwa na walikusudi kutoa mali kwa hitaji hili na roho moja.

9:3 **Ndugu** watatu ambao Paulo alituma, ndio **Tito** na ndugu wawili wengine, ambao tulisoma habari zao katika sura 8. Aliwatumua kusudi kujisifu kwake juu ya Wakorinto na sadaka yao kusiwe bure. Alitaka waangalie kwamba Wakorinto walikuwa wametaryisha sadaka yao kweli saa Paulo atakapofika yeche mwenyewe.

9:4 Wakati mtume atakaposafiri toka Makedonia, kwenda kwa kusini hata Korinto, labda mmoja wa waamini wa Makedonia atasafiri pamoja naye. Ingekuwa haya kubwa kama nyuma ya kujisifu kwa Paulo juu ya Wakorinto

wangekuta Wakorinto hawajatayarisha bado zawadi yao kwa Yerusalem! Ingekuwa haya kubwa kwa Paulo, na kwa Wakorinto vilevile.

9:5 Kwa sababu hii Paulo alifikiri kwamba **ilimpasa kuonya ndugu** hawa watatu watangulie kufikia Korinto mbele ya kufika kwake yeche mwenyewe. **Watatengeneza mbele** zawadi yao ya ukarimu **waliyoahidi zamani** kutuma kwa waamini wa Yerusalem.

Ipate kuwa tayari, na hivi **iwe kama zawadi, wala si kama kitu cha kutolewa kwa nguvu.** Iwe alama ya ukarimu wao, walijotoa kwa kutaka kwa wenye.

F. Zawabu njema kwa wenye kutoa na ukarimu (9:6-15)

9:6 Ndani ya mashairi 6 kufika 15 mtume Paulo alitaja nyingine za zawaabu za ajabu na faida za zawadi zinazotolewa na Wakristo. Kwanza alitaja mavuno kama mfano. Ni lazima kupanda mbegu nyingi kwa kupata mavuno makubwa. Labda mpandaji ni tayari kupanda mbegu na anajiliza kama ingepasa apande nafaka nyingi au achunge nusu ya mbegu hii kwa chakula chake kwa wakati wa kuja. Vizuri mpandaji afahamu kwamba **akipanda** mbegu nyingi, **atavuna** nyingi kupita kipimo cha mbegu **alichopanda**.

Ni vivyo hivyo na kutoa kwa Wakristo. Mkristo akitoa zawadi kwa Bwana, hatapokea tena kipimo cha zawadi aliyotoa, lakini nyingi kupita, si zaidi mali ya dunia, lakini baraka ya roho.

9:7 Kila mtu afanye kama alivyokusudi katika moyo wake. Itampasa kuwaza kama atakuwa na mahitaji gani kwa maisha yake ya kila siku. Zaidi ya ile sharti akumbuke mahitaji ya Wakristo wenzake, na ya kwamba mali yake nyingine ni mali ya Bwana. Akikumbuka maneno haya yote, haifai atoe **na huzuni, wala si kwa lazima.**

Inawezekana kwa mtu kutoa bila furaha. Na inawezekana kwa mtu kutoa kwa sababu anasukumwa au kulazimishwa na watu wengine na hataki kupata haya. Maneno haya yote hayafai. **Mungu anampenda yeche anayetoe kwa furaha.**

Basi Mungu anahitaji mali yetu? Sivyo, ngombe juu ya vilima elfu ni zake, naye hahitaji kitu cho chote. Asingalitujulisha kama angalikuwa na hitaji (Zaburi 50:10-12). Lakini anaangalia sana hali ya roho yetu. Anapenda kuona Mkristo anayejaa na furaha tele ya Bwana, hata anataka kushiriki mali yake na watu wengine.

Mungu anampenda yeche anayetoe kwa furaha.

9:8 Hapa tunaona ahadi ya kwamba mtu akitaka kweli kuwa na ukarimu, Mungu atamwezesha. **Neema** hapa ni kusema mali. **Mungu anaweza kuzidisha** mali yote kwetu tuwe na **kuzidi**, na zaidi ya ile tuweze kuwa na mali kushiriki na watu wengine na **kuzidi sana katika kila kazi njema.**

Ona ndani ya shairi hili: **neema yote, kuzidi kwa kila namna, kila kazi njema.**

9:9 Sasa mtume alitaja sehemu ya Zaburi 112:9. **Amesambaza** inasema juu ya kupanda mbegu. Shairi hili linasema juu ya mtu aliypanda mbegu na ukarimu, na zaidi aliyetenda mema na ukarimu. Mema aliyotenda yalikuwa kusaidia **masikini**. Hatapata hasara kwa sababu ya matendo yake mema hata kidogo. **Haki yake inakaa kwa milele.** Maana yake nini? Kama tukisambaza mema namna mpandaji anavyosambaza mbegu, tutajivimbishia hazina mbinguni. Matendo yetu mema yatakaa kwa **milele**.

9:10 Na Mungu yule **anayempa mwenye kupanda mbegu na mkate kwa chakula**, ataweka roho vilevile kutoa zawaabu kwa wale wanaotendea

wengine mema. Nyingine za zawabu zinatajwa sasa. Kwanza, **atazidisha mbegu yenu ya kupanda**. Ni kusema kwamba atawafungulia ninyi njia kubwa kupita kutenda mema, na kuvuna matunda mengi zaidi kwa njia ya kusaidia watu wa Mungu. Na vilevile **ataongeza matunda ya haki yenu**. Wakorinto walitenda haki wakati walipotoa zawadi kwa waamini wa Yerusalem. Kwa sababu ya zawadi zao watapokea matunda yaliyo zawabu ya milele. Wakati Mungu alipoongeza uwezo wao kutoa, nao wanapotoa na ukarimu kupita mbele, zawabu zao **zi-taongezeka** vilevile.

9:11 Mashairi haya yanaonyesha wazi kabisa ya kwamba hakuna mtu anayegeuka masikini kwa njia ya kutoa mali kwa Bwana. Kuna zawabu kwa kila tendo jema, ndiyo zawabu inayopita zawadi mbali kwa ukubwa. Hivi Paulo alisema hapa kwamba Wakristo watakuwa **tajiri katika vitu vyote** na wataweza kuonyesha **ukarimu** wao hata kupita mbele. Wakati mitume walipotazama na kuona Wakorinto wakiongezeka katika neema ya kutoa, walishukuru **Mungu**.

9:12 Wakati waamini wa Yerusalem walipoanza kutumika na zawadi ya Wakorinto, mali hii haikusaidia **mahitaji yao** tu, lakini watu wengi wangeshukuru **Mungu**. Tumeona tena na tena kwamba Paulo aliweka roho sana juu ya maneno yanayozaa **mashukuru kwa Mungu**.

9:13 Faida nyingine ya zawadi ya Wakorinto ilikuwa **kuhakikisha** kwa Wakristo Wayuda hawa ya kwamba **Kristo** alikuwa amefanya kazi kweli ndani ya roho za waamini hawa wa Mataifa. Labda walikuwa na shaka kama waamini namna ya Wakorinto walikuwa Wakristo kabisa. Lakini tendo hili jema litasaidia sana kuhakikisha kwamba walikuwa waamini wa kweli,

nao watatukuza Mungu kwa kazi ya **Habari Njema ya Kristo** katika Akaya, na kwa zawadi ya **ukarimu** waliyopewa.

9:14 Kuna faida nyingine mbili! Kwa sababu ya zawadi Wakristo Wayuda waliyopokea toka Korinto wataombea waamini katika Korinto na bidi zaidi na kupendana nao. Wakristo katika Yerusalem watakuwa na **hamu** kuona Wakorinto kwa sababu ya **neema ya Mungu** **iliyozidi sana** ambayo Wakorinto waliyokuwa wameonyesha kwao.

9:15 Halafu Paulo alitoa kilio cha kushangaa! Walimu wengi wa Biblia wanafazaika namna gani shairi hili linafungana na maneno ambayo yanalitangulia. Na nini ndiyo maana ya **zawadi yake tusiyoweza kuisifu kama inavyopasa**.

Ni kama wakati mtume Paulo alipofikia mwisho wa mafundisho haya juu ya kutoa kwa Wakristo, alilazimishwa kuwaza juu ya Mwenye kutoa kupita wote – ndiye **Mungu** mwenyewe. Na alifikiri vilevile juu ya **zawadi** kubwa kupita zote – Bwana Yesu Kristo. Hivi aliachana na ndugu zake Wakorinto akiwakumbusha kwamba wao ni watoto wa Mungu na wafuata wa Kristo. Vizuri waafuate mifano hii ya kustahili kabisa!

3. PAULO ALISIBITISHA UTUME WAKE (Sura 10–13)

Ndani ya sura ine za mwisho za barua hii Paulo aliweka roho zaidi kusibitisha kwamba yeche ni mtume. Kama mtume Petro alivyosema, ni magumu kufahamu maneno mengine ya sura hizi (2 Pet. 3:16). Paulo alijibu mashitaki ya watu wengine, lakini hatujulishwi kama walimshitaki juu ya nini. Labda maneno haya yataonekana wazi nyuma, saa tutakaposoma majibu ya Paulo.

Ndani ya sura hizi Paulo alisema na zihaka tena na tena. Ni nguvu kujua wakati gani alifanya hivi.

Lakini ni sehemu ya faida nyingi ya Neno la damani la Mungu.

A. Jibu la Paulo kwa washitaki wake (10:1-12)

10:1 Ndani ya mashairi 1-6 tunaona jibu la Paulo kwa wale amba walisema alitenda namna ya watu wa dunia.

Alijtaja Nami, Paulo mwenyewe. Haku-agiza waamini na nguvu, lakini ali-waomba kwa **unyenyekevu na upole wa Kristo**. Bila shaka Paulo alikuwa akifikiri juu ya mwenendo wa Bwana Yesu wakati alipokuwa hapa duniani kama Mtu. Paulo alisema juu ya maisha ya Mwokozi hapa duniani mara moja moja tu. Zaidi alisema juu ya Kristo kama Yule aliyetukuzwa kwa mkono wa kuume wa Mungu.

Paulo aliendelea kusema juu yake mwenyewe, **mimi niliye mnyenyeketu wakati mimi ni pamoja nanyi, lakini nisipokuwa mimi ni mwenye uhodari kwenu**. Bila shaka alisema maneno haya na kuzarau. Washitaki wake walikuwa wakisema kwamba Paulo alikosa uhodari wakati alipokuwa pamoja na watu, lakini wakati alipokuwa mbali nao alikuwa mhodari kama simba. Neno hili lilionekana kwa namna alivyoandika barua zake.

10:2 Shairi hili linafungana na *sehemu ya kwanza* ya shairi la kwanza. Pale Paulo alisema alisihii Wakorinto, lakini hakutuambia kwamba aliwasihii juu ya nini. Ndani ya shairi 2 anaeleza: “**Ninawasihi ninyi ya kwamba wakati mimi ni pamoja nanyi, nisiwe na uhodari na taraja ile ninayofikiri kuwa kwa ukali juu ya wengine, amba wanatuhesabu sisi ya kama tunate-mbea kwa namna ya mwili.**” Hakutaka kuwa na **uhodari** kwao namna alivyokusudi kuwa na **uhodari** kwa wale amba walimshitaki kwamba alitenda namna ya watu wa mwili.

10:3 Hata kama mitume walikuwa wakiishi ndani ya **miili** ya dunia,

hawakupiga vita kwa **namna ya mwili**.

10:4 Silaha za vita ya Wakristo si za **mwili**. Wakristo hawatumiki na panga, bunduki, au vitu vingine watu wana-vyotumia kwa wakati wa sasa kwa kupiga vita, kwa kueneza Habari Njema ya Kristo pahali mbalimbali. Mkristo hatumiki na utajiri, utukufu, uwezo, use-maji, au akili kutimiza makusudi yake.

Sivyo, lakini zina **uwezo katika Mungu kuangusha maboma ya vita**. Imani ndani ya Mungu aliye hai, maombi, na kutii neno la Mungu ni silaha za faida za kila askari ya kweli ya Yesu Kristo. Kwa njia ya silaha hizi **maboma** yanaangushwa.

10:5 Ndani ya shairi hili tunaona kama maana ya “maboma” ndani ya shairi 4 ni nini.

Paulo alifikiri juu yake mwenyewe kama askari anayeshindana na mawazo ya kiburi yanaoshindana na kweli. Ni kila kitu kinachonyanyuliwa juu ya **elimu ya Mungu**. Kwa wakati wa sasa ni mabishano ya elimu, mabadiliko, wenye dini wasiokumbuka Mungu ndani ya mashauri yao. Mtume hakutaka kupatana hata kidogo na watu wa namna hii. Alilazimishwa rohoni **kutia kila wazo katika utumwa wa Kristo**. Lazima mawazo na mafundisho yote ya watu yapimwe na yahukumiwe na nuru ya mafundisho ya Bwana Yesu Kristo. Paulo hakuhukumu mawazo na elimu yote ya watu, lakini alituonya tusitumike na akili yetu kwa njia yo yote inayoshindana na kuasi Bwana.

10:6 Akiwa askari ya Kristo mtume alikuwa **tayari vilevile kuazibu uasi wote wakati** Wakorinto walipokwisha kuonyesha utii wao wenyewe. Hata-hukumu walimu wa uwongo kwa Korinto mbele ya kujua kwamba waamini walikuwa **wenye kutii** ndani ya maneno yote.

10:7 Ni kama walifikiri juu ya namna maneno yalivyoonekana kwa macho tu.

Mtu akiamini kabisa kwamba ye ye mwenyewe ni Mkristo, Paulo ni Mkristo vivyo hivyo. Labda Paulo aliwaza saa ile juu ya watu wale waliosema, “mimi ni wa Kristo” (1 Kor. 1:12), wakifikiri wao peke yao ni Wakristo wa kweli. Paulo alikuwa mtu wa Bwana Yesu kama wao.

10:8 Akiwa mtume wa Bwana Yesu Kristo, Paulo alipewa **amri** kwa maneno ya makanisa aliyokwisha kuanzisha. Kusudi la amri hii lilikuwa kujenga watakatifu katika imani yao. Lakini walimu wa uwongo walitumika na amri katikati ya Wakorinto wasiyopewa kamwe na Bwana. Walitumika na amri hii kubomoa imani yao, si kuwajenga. Hivi Paulo alisema kwamba hata alijisifu sana juu ya **amri aliyopewa na Bwana**, hatapata haya kwa sababu hii.

10:9 Alisema hivi ili **asioneokane kama alitaka kuogopesha** Wakristo na **barua zake**. Vizuri Wakristo wakumbuke kwamba alipewa amri hii kuwajenga katika imani, na kwamba alitumika nayo na kusudi hili.

10:10 Hapa tunaona mashitaki ya adui za Paulo. Walisema aliandika **barua** za kuogopesha, lakini kwamba **katika mwili ye ye ni zaifu, na masemo yake si kitu.**

10:11 Watu wote waliofanya mashitaki namna hii **wakumbuke** kwamba wakati Paulo atakapokuwa **pamoja** nao atakuwa namna alivyokuwa ndani ya **barua** zake. Si kusema kwamba Paulo alikubali kwamba alisema na roho ya utawala ndani ya barua zake. Hili ndilo neno adui zake *walisema* juu yake. Lakini Paulo alisema atawahukumu na ukali wakati atakapokutana nao uso kwa uso. Hatakuwa na woga.

10:12 Ni wazi ya kwamba walimu wale wa uwongo walikuwa na desturi ya kujisawanisha na watu wengine. Walisema kwa Wakorinto juu ya Paulo kwamba ye ye ni mtu anayestahili kuzi-

hakiwa. Walifikiri hakuna watu wakubwa kama wao. Hivi Paulo alisema na kuzihaki, “**Kwa sababu hatusubutu kujihesabu au kujifananisha nao wanaojisifu: lakini wao wenyewe wakijipima na wenyewe, na kujifananisha wenyewe na wenyewe, hawana akili.**” Hata alikuwa mhodari ndani ya barua yake, kama wao walivvyosema juu yake, alisema sasa hakuwa na uhodari wa kutosha kujihesabu pamoja na wale **wanaojisifu wenyewe**, au na wale wanaojipima na maisha yao wenyewe tu.

B. Shauri la Paulo: Kuhubiri Habari Njema ya Kristo pahali isipohubiriwa mbele (10:13-16)

10:13 Ndani ya mashairi 13-16 Paulo alisema kwamba anakusudi kujisifu tu juu ya kazi aliyopewa ndani ya **mahali Mungu alipomweka**. Haikuwa desturi yake kujuvuna juu ya kazi ya mtu mwingine. Ni wazi ya kwamba aliwaza juu ya walimu wa uwongo wakati aliposema maneno yale. Ilikuwa desturi yao kuingia makanisa yaliyosimamishwa na mtume Paulo au Mkristo mwingine, na kujenga juu ya msingi mtu mwingine alioweka. Wakati walipojisifu, walijisifu juu ya kazi ambayo mtu mwingine ali-fanya.

Paulo alisema kwamba **hatajisifu** juu ya maneno yasiyokuwa sehemu ya utumishi wake kwa Kristo. Atajisifu tu juu ya watu na pahali ilipopendeza Mungu kubariki kazi yake. Hivi atajisifu juu ya Korinto vilevile, kwani alikuwa amekwenda pale na Habari Njema na kanisa lilisimamishwa.

Alikuwa Bwana aliyeamri Paulo kuperleka Habari Njema kwa Mataifa. Hivi alitumwa kwa Korinto vilevile, ndio mji mtaifa. Mitume kwa Yerusalem wa likubali neno hili, lakini sasa walimu wa uwongo walifika toka Yerusalem na kuingia wilaya Paulo alizopewa na Mungu.

10:14 Mtume hakujisifu kupita kipi-

mo. Mungu alikuwa amemgawia pahali ambapo atamtumikia. Korinto ulikuwa sehemu ya pahali pale. Alikuwa amefikia Korinto, alihubiri Habari Njema na alianza kanisa. Kama asipofikia Korinto ndani ya safari yake, kama watu wangalilweza kumshitaki kujisifu juu ya kazi iliyofanywa kwa pahali ambapo Bwana hakumgawia.

Paulo alipata majaribu na masumbuko na mateso na magumu kusudi aweze kufikia Korinto. Sasa watu wengine walikuwa wakiingia pahali ambapo yeye alikuwa mhubiri wa kwanza, na labda walijisifu sana juu ya kazi yao.

10:15 Paulo alikusudi kwamba **hatajisifu** juu ya maneno yasiyokuwa matunda ya utumishi wake mwenyewe kwa Kristo. Hili lilikuwa neno walimu wa uwongo walilofanya: walijisifu juu ya kazi ya watu wengine. Walijaribu kuiba kondoo za Paulo (maana kushawishi watu walioamini Kristo kwa sababu ya ushuhuda wa Paulo, kuacha kufuata Bwana), waliharibu sifa njema ya Paulo, walikana mafundisho yake, na walijitwalia amri isiyo yao.

Paulo alitumaini ya kwamba **imani ya Wakorinto itaongezeka**, naye ataweza kwenda kuhubiri Habari Njema pahali pengine. Alitaraji wataonyesha **imani** yao kwa njia ya kumsaidia na mali na vitu ambavyo vitamsaidia kwenda hata mbali kupita kama mtume wa Mungu. Na atakaa kutokujisifu juu ya utumishi wa watu wengine.

Masumbuko kanisani mwa Korinto yalihitaji saa nyingi za Paulo, na yalmzuiza asitimize kazi yake pahali palipokuwa mbali kupita mpaka wao.

10:16 Kusudi la Paulo lilikuwa **kuhubiri Habari Njema katika inchi zilizo mbali kupita** inchi zao (labda sehemu ya mangaribi ya Yunani, Italia, na Spania), na **hatajisifu katika mpaka wa mtu mwingine katika maneno yaliyokwisha kutengenezwa**. Mtume

hakukusudi kuingia mashamba ya watu wengine bila ruhusa, wala kujisifu juu ya kazi watu wengine waliyokwisha kufanya mbele ya kufika kwake.

C. Kusudi kubwa la Paulo: Sifa ya Bwana (10:17, 18)

10:17 Mtu anayejisifu, **ajisifu katika Bwana**. Ni kusema bila shaka inampasa **kujisifu tu** ndani ya maneno ambayo yalipendeza Bwana kufanya kwa njia yake.

10:18 Hatujipatii ukubali wa Mungu kwa njia ya kujisifu wenyewe. Ingepasa washitaki wa Paulo kuuliza: Bwana amekusifu kwa njia ya kubariki utumishi wako na kuokoa wasioamini, kupatisha waamini nguvu katika imani, na kukuwezesha kuanza makanisa? Unaweza kuonyesha ukubali wa Bwana kwa njia ya kuonyesha watu waliokwisha kuokolewa kwa njia ya mahubiri yako? Paulo alikubali na aliweza kuonyesha kwa njia hizi ya kwamba Bwana alikubali utumishi wake.

Ndani sura hii na sura 11 Paulo alijiruhusu kusema na upumbavu, na kujisifu mwenyewe. Si neno alilopenda kufanya hata kidogo. Aliomba Wakorinto wamvumilie wakati anapotenda kwa upumbavu.

Ni kama walimu wa uwongo walikuwa wamejisifu sana. Walitoa habari nzuri za kushangaza za utumishi wao na usitawi wao. Paulo hakufanya hivi kamwe. Alihubiri juu ya Kristo, si juu yake mwenyewe.

Ni kama Wakorinto walitaka zaidi utumishi ambao waliweza kujisifu juu yake, hivi Paulo aliwaomba wamruhusu kutenda hivi vilevile kwa wakati.

D. Paulo alisimamia utume wake (11:1-15)

11:1 **Ninataka munivumilie mimi katika upumbavu wangu kidogo: lakini kweli munanivumilia.** Alitaka waweez kuvumilia kujisifu kwake.

Lakini ni kama alifahamu kwamba waliikuwa wakifanya hivi, na ombi hili halikuhitajiwa.

11:2 Aliomba hivi kwa sababu tatu: Alikuwa na **uwivu** juu ya Wakorinto, **na uwivu wa Mungu**. Alikuwa **amewapatanisha kwa mume mmoja**, ili **aletee Kristo bikira safi**. Aliweka roho sana juu ya hali ya roho ya waamini wa Korinto. Siku ya kuja, ndiyo wakati Kristo atakaporudi kwa bibi arusi yake, alitaka sana kuwaleta kwa Kristo, bila kuchafuwa rohoni na mafundisho mabaya yaliyoenea kwa wakati ule. Aliwapenda na uwivu, na kwa sababu hii alikuwa tayari kutenda yaliyoonekana kama upumbavu.

11:3 Sababu ya pili iliyosukuma Paulo kutenda kama mpumbavu ilikuwa **woga** wake ya kwamba **mawazo yao yataharibiwa**, na wataacha kupenda **Kristo** peke yake na **moyo safi**. Alitaka vilevile mapendo yao kwa Bwana yawe safi bila kipako.

Mtume alikumbuka namna **nyoka alivyodanganya Hawa kwa hila yake**. Alifanya hivi kwa njia ya kusema na nia au akili yake. Walimu wa uwongo walifanya vivyo hivyo katika Korinto. Lakini Paulo alitaka sana waamini wa Korinto wafuate Bwana na roho moja na bila kipako.

Tunaona hapa ya kuwa Paulo aliamini kwamba habari hizi za Hawa na nyoka hazikuwa hadizi tu, lakini zilitukia kweli.

11:4 Sababu ya tatu iliyokubalisha Paulo kutenda kwa upumbavu ilikuwa kuona kwamba Wakorinto walikuwa tayari kusikiliza walimu wa uwongo.

Mtu akifikia Korinto na kuhubiri **Yesu mwingine**, au habari za **roho nyiningine** asiyé Roho Mtakatifu, au kuhubiri **Habari Njema nyiningine**, Wakorinto walikuwa tayari kumpokea. Ni kama Paulo aliuliza na zihaka, “Mukipokea watu wa namna hii, na kuvumilia mawazo yao, kwa sababu gani hamunipokei mimi?”

Mtume hakukubali mafundisho ya uwongo, lakini alihamakia Wakorinto kwa sababu ya kudanganywa mbio na kukosa uchaguzi wema.

11:5 Iliwapasa kuvumilia Paulo kwa sababu **hakupungukiwa hata kidogo mitume walio wakubwa sana**. Alisema hivi na zihaka.

11:6 Labda Paulo **hakuja kusema vizuri**, lakini **hakukosa elimu**. Ingalipasa Wakorinto kufahamu neno hili vizuri, kwa sababu walipokea toka Paulo elimu ya imani ya Wakristo. Hata kama labda Paulo hakuweza kusema vizuri, ni wazi ya kwamba ingepasa waamini katika Korinto kukubali kwamba walikuwa wamemfahamu vizuri.

11:7 Labda kulikuwa na sababu nyiningine iliyozuiza Wakorinto wasihe-shimu Paulo namna ilivyofaa. Labda ilikuwa kwa sababu alifanya zambi kwa **kujinyenyekiza** mwenyewe ili **wao wanyanyuliwe**. Baki la shairi hili linaleaza masemo haya ya Paulo. Wakati alipokuwa pamoja na Wakorinto, hawakumsaidia na mali kwa mahitaji yake. Labda walifikiри ilikuwa zambi kwa Paulo kujinyenyekiza hivi ili wao wa-weze kunyanyuliwa.

11:8 Masemo haya, “**Niliibia makanisa mengine**,” yalikuwa mfano kuchokoza wasikiaji wake. Paulo hakuiba makanisa mengine. Alitaka kusema tu kwamba wakati alipokuwa akitumikia Bwana kwa Korinto, **makanisa mengine** walimsaidia na mali ili aweze katumikia Wakorinto bila kupokea mali toka kwao kwa mahitaji yake.

11:9 Mara nyiningine wakati mtume Paulo alipokuwa kwa Korinto, alikuwa na **mahitaji** kabisa. Alijulisha Wakorinto habari za **mahitaji** haya na kuwomoba kumsaidia? Sivyo, hata kidogo. **Ndugu waliokuja toka Makedonia** walimpa vitu ambavyo **alihitaji**.

Kwa njia zote alizoweza, mtume **aliepuka kuwa mzigo** kwa Wakorinto, na alikusudi kukaa kufanya hivi. Ilikuwa

haki yake kusaidiwa na Wakorinto, lakini alikataa kuwaomba wamlinde.

11:10 Paulo alikusudi kwamba **hakuna mtu** ambaye atamkataza **kujisifu katika inchi ya Akaya**, pahali mji wa Korinto ulipokuja. Bila shaka aliwaza juu ya wachunguzi wake waliotumika na kujinyima kwake kusema mabaya juu yake. Walisema alifahamu kwamba hakuwa mtume wa kweli, na kwa sababu hii hakuomba Wakristo kumsaidia na mahitaji yake (1 Kor. 9). Hata wachunguzi wake wakisema nini, Paulo ataendelea kujisifu juu ya kutumikia Wakorinto bila kupokea mali yao.

11:11 **Kwa nini** atajisifu hivi? **Kwa sababu hakupenda** Wakorinto? **Mungu** anajua kwamba neno hili si kweli! Aliwapenda na roho yake yote. Si neno kama alifanya nini, walimshitaki. Kama angalipokea mali ya Wakorinto, adui zake wangalisema alihubiri kwa sababu ilikuwa faida kwake. Kwa sababu alikataa kupokea mali yao, walisema **hakuwapenda** kweli. Lakini **Mungu anajua** kweli, hivi Paulo aliacha maneno haya mikononi mwake.

11:12 Ni kama walimu wale wa uwongo walitazamia, waliomba, na walipokea mali toka Wakorinto. Kama ilivyo desturi ya walimu wa uwongo, wasingalihubiri bila kupokea mali. Paulo alikusudi kwamba **ataendelea** kukataa kutopokea mali toka waamini wa Korinto. Alijua kwamba kwa njia hii walimu wa uwongo walitaka kushindana naye kwa njia ya kujisifu juu ya neno hili watashindwa kabisa.

11:13 Sasa mawazo ya Paulo rohoni mwake juu ya watu hawa yalionekana wazi. Hakuweza kuyaficha tena. Alisema wazi ya kwamba watu hawa **walikuwa mitume ya uwongo**, ndio watu wasioamriwa kamwe na Bwana Yesu Kristo. Au walijitwalia amri hii wao wenyewe, au walipewa na watu wengine. **Walitenda kazi kwa hila** wakienda kwa makanisa mengine wa-

kitafuta wafuata watakaopokea ma-fundisho yao ya uwongo. **Wakijigeuza wenyewe kuwa kama mitume ya Kristo**, walifanya hila kusema wao ni wajumbe wake. Paulo hakutaka hata kidogo kuwa sawasawa na watu wa **namna hii**.

Maneno Paulo aliyosema juu ya walimu hawa wa uwongo ni kweli juu ya walimu wa uwongo wa wakati wa sasa vilevile. Tusingalitambua uovu wao kama wasingalijaribu kufundisha maneno yaliyoonekana kuwa mema.

11:14 Mtume alisema sasa tu ya kwamba wajuzi wake katika Korinto walijionyesha kuwa kama mitume ya Kristo, neno lisilokuwa kweli. Lakini neno hili **haliwezi kutushangaza, kwani bwana yao, ndiye Shetani, ali-jigeuza awe malaika ya nuru**.

Kwa wakati wa sasa watu wanafanya picha ya Shetani kuonekana kama ki-umbe kiovu cha rangi nyekundu, chenye mkila. Lakini hii si namna anavyojionyeshi kwa watu sasa.

Watu wengine wanafikiri juu ya Shetani kama mtu anayekwisha kulewa na analala kwa udongo. Lakini hata neno hili halituonyeshi hali ya kweli ya Shetani.

Shairi hili linatuonyesha kwamba anajionyesha kama **malaika ya nuru**. Mfano wa neno hili ni kwamba anajionyesha kama mhubiri wa Habari Njema, akivaa mavazi ya mhubiri na kusimama ndani ya mimbara ya nyumba ya mapambo ya kanisa. Anatumika na masemo ya dini kama *Mungu, Yesu, na Biblia*. Lakini anadanganya wasikiaji wake kwa njia ya kufundisha kwamba wanaweza kuokolewa kwa njia ya matendo mema, au kwa sababu wanastahili kupokea wokovu. Hahubiri kwamba ukombozi unapatikana kwa njia ya damu ya Kristo.

11:15 Kama Shetani akijigeuza kuonekana namna nytingine, hatuwezi

kushangaa kama watumishi wake wakifanya vivyo hivyo. Hawajionyeshi kama walimu wa uwongo, au watu wasioamini kwamba kuna Mungu, au mtu asiye na dini yo yote. Sivyo. Wanajionyesha kuwa **watumishi wa haki**. Wanasema wanaongoza watu ndani ya njia ya kweli na **haki**, lakini wao ni wajumbe wa Shetani.

Mwisheso wao utakuwa sawasawa na kazi zao. Wanaharibu – na wataharibowi. Wanaongoza watu hata mauti; wao wenyewe watapotea kwa milele.

E. Mateso ya Paulo kwa Kristo yanahakikisha utume wake (11:16-33)

11:16 Paulo alitaraji watu **wasizanie** yeye ni **mpumbavu** mwenye kujivuna. Lakini hata wakizania hivi, **wamkubali kama mpumbavu, apate kujisifu kidogo vilevile**.

Ona neno hili **vilevile** kwa mwisheso wa shairi hili: **nipate kujisifu kidogo vilevile**. Walimu wa uwongo walikuwa wakijisifu sana. Ni kama Paulo alikuwa akisema, “Hata **kama** ikiwapasa ninyi kufikiri mimi ni **mpumbavu** (lakini neno hili si kweli), **munipokee** hata hivi ili niweze kujivuna kidogo vilevile kama watu wale wanavyofanya.”

11:17 Shairi hili linaweza kuelezwa kwa njia mbili. Watu wengine wanafikiri kwamba masemo ya Paulo hapa yалиongozwa na Mungu, lakini kwamba **hakuyaagizwa na Bwana**.

Elezo la pili ndilo ya kwamba neno Paulo alilofanya hapa, ndilo kujivuna, **si kama agizo la Bwana**, maana ha-kuiga Bwana wakati alipofanya hivi. Bwana Yesu hakujivuna kamwe.

Tunawaza kwamba elezo hili la pili ni zuri kupita, na ya kwamba **kujisifu hakuwa kama agizo la Bwana**. Ni kama ulikuwa upumbavu kwa Paulo kujisifu hivi.

11:18 Wakorinto walikuwa wamesikia maneno mengi kwa wakati ule toka

watu waliojisifu wenyewe, wakiongozwa na tabia yao ovu ya umtu. Kama Wakorinto walifikiri walimu hawa wa uwongo walikuwa na sababu kwa kujisifu, waone kama Paulo hakuwa na sababu kwa kujivuna vilevile.

11:19 Paulo alisema na zihaka tena. Walifikiri wao ni wenye **akili** wasiweza kudanganywa na upumbavu wa watu.

11:20 Walikuwa tayari **kuvumilia** mtu wa namna gani? Maneno tutakayosoma sasa yanaonyesha kwamba alikuwa mwalimu wa uwongo, asiye mtume wa kweli, aliyekuwa akiteka Wakorinto. Kwanza aliwatia katika **utumwa**. Bila shaka utumwa huu ulikuwa utumwa wa sheria (Mdo. 15:10). Mtu yule alifundisha kwamba kuwa na imani ndani ya Kristo hukutoshi, na ya kwamba inapasa watu kutii sheria ya Musa vilevile.

Neno la pili alilofanya lilikuwa kumeza watakatifu, maana aliwalazimisha kulipa mali nydingi. Hakuwatumikia kwa sababu ya mapendo, lakini kwa kujipatia mali.

Ilikuwa desturi ya watu wale kujitokuza na kiburi na kujisifu. Kwa njia ya kulaumu watu wengine, walijaribu kuongeza ukubwa wao wenyewe machoni mwa watu.

Mwisheso, walipiga **uso wa waamini**, ndilo tendo la kuwahayarisha kabisa. Neno hili halikuwa mfano, lakini lilitokea kweli. Viongozi vyaya kanisa wenye kiburi katika miaka iliyopita walifanya hivi kuonyesha amri yao kanisani.

Mtume alishangaa kwa sababu Wakorinto walikubali **kuvumilia** kutendewa mabaya hivi na walimu hawa wa uwongo, lakini hawakukubali kupokea maonyo yake ya mapendo.

11:21 Watu wengine wanafikiri kwamba ndani ya shairi hili ni kama Paulo alisema bila kujiheshimu mwenyewe, ya kwamba wakati alipokuwa pamoja nao yeye mwenyewe, alikuwa zaifu, na alio-

gopa kutenda na amri kama watu hawa walivyofanya.

Paulo alisema kama namna walimu hawa wa uwongo walivyotenda ndiyo nguvu ya kweli, itampasa kusema **na haya** kwamba yeche hakuonyesha namna hii ya nguvu lakini uzaifu. Lakini ali-ongeza mbio kwamba **katika neno gani** watu hawa wengine wanabutu **ku-jivuna**, yeche ana haki **ku-jivuna** vilevile. Halafu Paulo alianza kuonyesha kwa njia gani ni haki yake kusema yeche ni mtumishi wa kweli wa Bwana Yesu Kristo.

Utakumbuka ya kwamba watu wa kanisa la Korinto walikuwa wameuliza kama Paulo alikuwa mtume wa kweli. Kwa njia gani aliweza kuonyesha kwamba aliitwa kweli na Mungu? Namna gani aliweza kuhakikisha kwa watu kwamba alikuwa sawasawa na mtume kumi na wawili?

Alikuwa tayari kujibu ulizo lao, lakini jibu lake lilikuwa namna nyingine kidogo. Hakuonyesha hati ya cheo kuonyesha kwamba alikuwa amemaliza darasa zao vizuri. Na hakuwa na barua toka ndugu za Yerusalem kusema walikuwa wamemtia mikono kwa kazi hii. Hakutaja mbele ya Wakorinto maneno na kazi alizokwisha kufanya. Sivyo, alitaja mateso aliyopata kwa njia ya kazi ya kuhubiri Habari Njema. Waza juu ya Paulo akisafiri bila kuchoka kwa inchi kavu na bahari, akisukumwa na mapendo ya Kristo, tayari kuvumilia magumu namna zote ili watu wasikose kusikia Habari Njema ya Kristo. Hatuwezi kusoma mashairi haya bila kupta haya rohoni mwetu.

11:22 Walimu wa uwongo walijisifu sana juu ya wazazi wao. Walisema wao ni **Waebrania**, wazao wa Israeli, na **uzao wa Abrahamu**. Walifikiri maneno haya yaliwakubalisha na Mungu. Hawakufahamu kwamba Mungu alikuwa ameweka kando watu wake wa zamani, ndio Waisraeli, kwa sababu walikataa

Masiya. Hawakufahamu kwamba kwa macho ya Mungu watu wote, Wayuda na Mataifa, ni sawasawa: wote ni wenye zambi, na wote wanahitaji kuokolewa kwa njia ya kuamini Bwana Yesu Kristo peke yake.

Hivi haikuwa na faida wajivune juu ya uzao wao, kwa sababu Paulo alikuwa Mwebrania vilevile, Mwisraeli, na wa **uzao wa Abrahamu**. Lakini maneno haya hayakuhakikisha kwamba alikuwa mtume wa Kristo. Hivi aliendelea na habari za taabu na maumivu yake. Hawakuweza kumshinda ndani ya maneno haya.

11:23 Wao walikuwa **watumishi wa Kristo**, maana hii ilikuwa kazi yao. Yeye alikuwa mtumishi wa Kristo zaidi: katika taabu kuzidi sana, katika mapigo kuzidi sana. Mtume hakuweza kusahau kamwe kwamba alikuwa mfuata wa Mwokozi *aliyeteswa*. Alifahamu kwamba mtumishi si mkubwa kuliko Bwana wake, na ya kwamba haifai mtume kufikiri kwamba atatendewa vizuri kupita bwana wake duniani. Paulo alifahamu kwamba kwa kipimo alichotumikia Kristo na uaminifu na kuonyesha Mwokozi ndani ya maisha yake, kwa kipimo kile atateswa na watu. Kwa mafikiri yake, mateso yalikuwa alama ya watumishi wa Kristo. Hata kama alifikiri alisema kama **mwenye wazimu** wakati alipojisifu hivi, lazima aseme kweli, ndiyo ya kwamba walimu hawa hawakujulikana kama wenye kuvumilia mateso. Waliepuka laumu, fukuzo na aibu. Kwa sababu hii Paulo alifikiri kwamba haifai washindane naye, ndiye mtumishi wa Kristo.

Tuone sasa taabu na shida Paulo alizotaja kuhakikisha kwamba yeche ni mtume wa kweli. **Katika taabu kuzidi sana**. Alifikiri juu ya safari zake ndefu karibu na Bahari Mediterrané kuhubiri Habari Njema. **Katika mapigo kuzidi sana**. Alipata mapigo haya kwa mikono ya adui za Kristo, wapagano na Wayuda.

Katika vifungo kuzidi sana. Tunasoma juu ya mara moja tu Paulo aliyofungwa kufika wakati alipoandika maneno haya, ndio kwa Matendo 16:23, saa ye ye na Sila walipofungwa gerezani kwa Filipi. Sasa tunaona kwamba alifungwa mara nyingi kupita. **Katika mauti mara nyingi.** Wakati Paulo alipoandika neno hili, bila shaka aliwaza kwamba alikuwa karibu sana na mauti kwa Listra (Matendo 14:19). Aliweza kuwaza juu ya mara nyingi nyingine vilevile wakati alipokuwa karibu na kufa kwa sababu ya mateso ya adui.

11:24 Sheria ya Musa ilikataza Wayuda kupiga mtu kupita mara makumi ine kwa saa moja (Torati 25:3). Hawakutaka kuvunja sheria hii, hivi ilikuwa desturi yao kumpa mtu mapigo 39 tu. Walileta mapigo haya kama azabu kwa makosa makubwa tu. Mtume Paulo anatuambia hapa kwamba watu wa taifa lake mwenyewe walimwazibu kwa kipimo hiki kwa saa mbalimbali mara **tano**.

11:25 Mara tatu nilipigwa kwa fimbo. Mara ya pekee tunayosoma juu ya tukio hili ilikuwa kwa Filipi (Matendo 16:22), lakini Paulo alihayarishwa na mapigo ya fimbo mara mbili nyingine.

Mara moja nilipigwa kwa mawe. Bila shaka neno hili lilitokea kwa Listra kama tulivyosema mbele (Matendo 14:19). Alipigwa sana sana wakati ule, hata walikokota mwili wake inje ya mji, wakifikiri alikuwa amekufa.

Mara tatu nilipata kuvunjika kwa merikebu. Paulo hakuteswa kwa mikono ya watu tu, lakini kwa mawimbi wa bahari vilevile. Habari za kuvunjika kwa merikebu hazikuandikwa hapa. (Kuvunjika kwa merikebu katika Matendo 27 kwa safari yake kwenda Roma kulitukia nyuma ya saa alipoandika habari hizi.)

Mchana na usiku nimekaa katika bahari. Hatusomi juu ya tukio hili katika Matendo. Kama alikuwa ndani ya

bahari kama angeweza kuponyeshwa na Bwana tu kwa njia ya ajabu.

11:26 Katika safari mara nyingi. Labda Biblia yako ina ramani kwa upande wa mwisho inayoitwa “Safari za kuhubiri za mtume Paulo.” Tukumbuke kwamba motokari au lori hazikuwa kusaidia wasafiri kwa wakati ule.

Halafu Paulo aliendelea kutaja hatari namna nane ambazo alikutana nazo. Kulikuwa na **hatari ya mito**, ndio mito iliyofurika na maji. Kulikuwa na **hatari za wanyanganyi**, kwani kulikuwa na wizi wingi kwa njia alizokwenda kwa safari zake. Katika **hatari za watu wa taifa lake mwenyewe**, ndio Wayuda, na **Mataifa** ambao aliwahubiri Habari Njema. Kulikuwa na **hatari ya miji**, kama Listra, Filipi, Korinto na Efeso. Alikutana na **hatari za jangwa**, kama sehemu za inchi katika Asia Ndogo na Europe zilizokaliwa na watu wachache tu. Alikutana na **hatari za bahari** – tufani, mawe yaliyofichwa ndani ya maji, na labda haramia.. Mwishoni **hatari za ndugu za uwongo** – bila shaka Wayuda waliokaa kufundisha sheria, wakisigizia kuwa walimu Wakristo.

11:27 Kazi na taabu – Paulo alitumika bila kuacha, na kuteswa sana kwa sababu ya kuchoka sana.

Katika kungoja zamu mara nyingi. Bila shaka kwa safari zake nyingi iliimpasa kulala inje usiku. Lakini kwa sababu alizungukwa na hatari nyingi hakupata usingizi lakini alitazamia hatari iliyoaribia.

Katika njaa na kiu, katika kufunga mara nyingi. Mtume yule wa kujulikana alilazimishwa kuteswa na njaa na kiu mara nyingi wakati alipotembea pa-hali mbalimbali kutumikia Bwana. Mara nyingine watu wanafunga chakula na kusudi, lakini tunawaza hapa alifunga kwa sababu ya ukosefu wa chakula.

Katika baridi na utupu. Bila shaka alikosa mavazi na viatu vy ya kutosha mahitaji yake. Hodge aliandika:

Tunaona hapa mtume aliyejikuwa mkubwa kupita mitume yote wengine, mwenye mgongo uliopasuliwa na mapigo mengi, na mwili zaifu kwa sababu ya njaa, kiu, na ukosefu wa mavazi ya kutosha, akiteswa na Wayuda na Mataifa, akifukuzwa toka pahali pamoja hata pengine na akikosa kao la kupanga. Mashairi haya, kupita mashairi yote mengine, yanalaizimisha watumishi wa wakati wa sasa wanaotumikia Bwana na nguvu sana kuficha nyuso zao na haya. Wamefanya kazi gani, au kuvumilia mateso gani yaliyoweza kufananishwa na matendo na mteso mtume huyu aliyopata? Tunafarijiwa wakati tunapokumbuka kwamba kwa wakati wa sasa anatukuzwa kwa kipimo alichoteswa mbele.¹⁵

11:28 Na pamoja na maneno yale mengine, Paulo alibeba **kila siku** mzigo na masumbuko ya kulinda **makanisa yote** ya Wakristo kwa roho yake. Neno hili lilikuwa kubwa kupita taabu yote nyingine! Paulo alikuwa mchungaji wa kweli. Alipenda na kulinda watu wa Bwana. Hakuwa mchungaji wa mshahara, lakini mchungaji wa hakika chini ya amri ya Bwana Yesu. Ni neno hili alilojaribu kuhakikisha ndani ya mashairi haya.

11:29 Shairi hili linafungana na shairi 28. Ndani ya shairi lile alisema alibeba kila siku masumbuko ya kulinda makanisa yote. Sasa ndani ya shairi 29 ali-eleza maana ya masemo haya. Kama alisikia habari za Mkristo ye yote aliyejikuwa **zaifu**, alishiriki naye ndani ya uzaifu huu. Alibeba mateso ya watu wengine pamoja nao na huruma. Wakati aliposikia habari kwamba ndugu mmoja katika Kristo alikwazwa, yeye mwenyewe **aliumizwa**. Neno lo lote liligusa watu wa Mungu lilimgusa yeye. Alihuzunishwa pamoja nao wakati

walipokuwa na huzuni, na alifurahi pamoja nao wakati waliposhinda. Maneno haya yote yaliweza kupunguza nguvu ya mtumishi wa Mungu.

11:30 Paulo hakujisifu juu ya kushinda kwake, wala akili yake, lakini juu ya uzaifu wake, na laumu na haya alizopata. Si desturi za watu kujisifu juu ya maneno ya namna hii wala kupata sifa toka watu.

11:31 Wakati Paulo alipowaza juu wa maneno haya na kujisifu juu ya uzaifu wake, hakuweza kusahau tukio la haya zaidi la maisha yake mazima, kwa Damasiki. Si desturi hata kidogo kwa mtu kujisifu juu ya tukio la haya kubwa namna hii, hivi Paulo aliomba **Mungu** kushuhudia kweli ya maneno aliyosema.

11:32 Tuliona habari nyingine juu ya tukio hili ndani ya Matendo 9:19-25. Nyuma ya kuokolewa karibu na **Damasiki**, Paulo alianza kuhubiri Habari Njema ndani ya masunagogi ya mji. Watu waliskiliza mahubiri yake vizuri kwanza, lakini nyuma ya wakati, Wayuda walifanya shauri kumwua. Walileweka zamu kwa malango ya mji mchana na usiku **wapate njia kumkamata**.

11:33 Halafu usiku mmoja wafuata walikalisha mtume **ndani ya kitunga** na kumshusha **kutoka dirisha la ukuta** inje ya mji, naye aliweza kuponyoka.

Basi kwa sababu gani Paulo alitaja habari hizi? Haya ndiyo mawazo ya J. B. Watson:

Alitaja habari hizi watu walizowaza ni neno la aibu na haya, na kuhakikisha kwa njia hii vilevile kwamba neno kubwa zaidi la maisha yake lilikuwa kutumikia Bwana Kristo. Kwa ajili hii alikuwa tayari kuacha kiburi yake mwenyewe, na kuonekana kama mwoga machoni mwa watu.¹⁶

F. Funuo toka Mungu zilihakikisha utume wa Paulo (12:1-10)

12:1 Mtume hakutaka **kujisifu** hata kidogo. Hakukawa na **faida**, lakini kulihitajiwa kwa wakati ule. Hivi nyuma ya kupasha juu ya habari za haya zaidi za utumishi wake alipita kusema juu ya tukio la utukufu zaidi. Alipasha juu ya kusikia **Bwana** mwenyewe akisema naye.

12:2 Paulo alijua **mtu** aliyeutana na maneno haya **miaka kumi na mine mbele**. Hataji kama mtu mwenyewe alikuwa nani, lakini ni wazi ya kwamba alikuwa akisema juu yake mwenyewe. Akisema juu ya tukio la utukufu mkubwa namna hii, hakutaka kujitaja mwenyewe, lakini alisema juu ya **mtu** fulani tu aliyeuwa **katika Kristo**, maana alikuwa **Mkristo**.

12:3 Paulo hakujuu kama mtu huyu alikuwa **katika mwili au kama inje ya mwili** kwa wakati ule. Watu wengine wanafikiri neno hili lilitukia kwa wakati Paulo alipoteswa mara nyingine, kama kwa Listra. Wanasema labda alikuwa kwa wakati ule na kwenda mbinguni. Lakini hatuoni tafsiri namna hii hata kidogo ndani ya shairi hili. Ikiwa Paulo mwenyewe hakujuu kama alikuwa **katika mwili au inje ya mwili**, maana kama alikuwa hai au mfu kwa wakati ule; basi haiwezekani kwa walimu wa wakati wa sasa kueleza habari hizi kupita!

Neno kubwa ndilo ya kwamba mtu huyu alichukuliwa juu hata **Paradiso**, inayoitwa vilevile mbingu ya tatu. Mandiko yanaonyesha kwamba kuna mbingu tatu. Ya kwanza ndiyo ile tuna-yoona wakati tunaponyanya macho yetu juu. Ya pili ndipo pahali pa nyota. Ya tatu ni juu zaidi, pahali pa kiti cha kifalme cha Mungu.

Habari zinazofuata zinatufahamisha kwamba Paulo alikuwa kwa pahali pa baraka, ndipo Bwana Yesu alipopeleka mwizi aliyetubu nyuma ya kufa kwake msalabani, ndipo kao la Mungu.

12:4 Paulo alisikia lugha ya **Paradiso**, alifahamu maneno yaliyosemwa, lakini hakuwa na ruhusa kuyapasha kwa watu wengine wakati aliporudi duniani. Yalikuwa **maneno yasiyoweza kusemwa** kwa sababu yalikuwa matakatifu sana. G. Campbell Morgan aliandika:

Kuna watu wengine wanaotaka sana kusema juu ya maono na funuo zao. Labda kutaka kwao kufanya hivi ni alama kwamba maono na funuo hizi "hazitoki kwa Bwana." Wakati Bwana anapotolea watumishi wengine maono na funuo, watu hawa wanashindwa nazo kabisa na hawasemi juu yao na wepesi wa moyo. Lakini matunda ya maono na funuo hizi zi-taonekana ndani ya maisha na utumishi wao.¹⁷

12:5 Wakati mtume alipojisifu juu ya uzaifu, hakusita kusema juu yake mwenyewe. Lakini wakati alipojisifu juu ya maono na funuo za Bwana, hakusema kwamba yeze mwenyewe alipewa maono na funuo hizi, lakini kwamba zilipewa kwa mtu mwagine ambaye alijua. Hakukana kwamba yeze mwenyewe alizipewa, lakini alikataa kujitaja mwenyewe.

12:6 Paulo aliweza **kujisifu** juu ya matukio mengi mengine. Asingalikuwa **mpumbavu** kama **angalitaka** kufanya hivi. Maneno yote ambayo angesema yangetuwa kweli. Lakini alijizuiza, kwa sababu hakutaka **mtu ye yote kumhe-sabia** zaidi ya ile anayoona kwake, au anayosikia akisema kwa kinywa chake.

12:7 Shairi hili linatuonyesha maneno yanayopata mtumishi wa Kristo tena na tena. Mara nyingine ananyenyekewa kabisa, kama Paulo kwa Damaski. Na mara nyingine anapewa ufunuo wa kufurahisha sana. Lakini nyuma ya kupewa funuo za kufurahisha sana, Bwana ana-acha mtumishi wake kuteswa na **mwiba mwilini** mwake. Ilikuwa hivi ndani ya maisha ya Paulo.

Shairi hili linatufundisha maneno ya

faida nyingi. Kwanza, linaonyesha kwa-mba tukipokea ufunuo toka Mungu, ufu-nuo huu hautengenezi **tabia yetu ya zambi**. Hata nyuma ya kusikia masemo ya Paradiso, kulikuwa na hatari kwamba Paulo atategwa na kiburi. R. J. Reid ali-sema:

“Mtu katika Kristo” anakaa na salama saa ye ye ni pamoja na Mungu na kusikia maneno yan-yosemwa katika Paradiso, masemo yasiyoweza kutafsiriwa, lakini ana-hitaji “mwiba katika mwili” wakati anaporudi duniani, kwani tabia yake ya zambi ingependa kujisifu juu ya kufika kwake kwa Paradiso.”¹⁸

Mwiba katika mwili wa Paulo uli-kuwa nini? Tunaweza kusema tu kwamba ulikuwa maumivu fulani ambayo Mungu aliacha kumpata mwilini. Labda ulikuwa ugonjwa wa macho,⁴⁷ au maumivu ya sikio, au kuumwa wa kichwa, au usemi wake. Bila shaka Bwana hakufunua neno hili wazi kwa kusudi ili waamini wanaoteswa kwa wakati wa kuja waweze ku-saidiwa na kutiwa roho ya nguvu wakati watakpowaza juu ya magumu ambayo yalipata Paulo.

Mtume aliita **mwiba mwilini mwa-ke mjambe wa Shetani aliyetumwa ampige**. Ni kama Shetani alijaribu kuzuiza Paulo ndani ya kazi yake kwa Bwana. Lakini Mungu ni mkubwa kupita Shetani, naye alitumika na **mwiba** ule kuendeleza kazi ya Bwana kwa njia ya ku-saidia Paulo kuwa mnyenyekemu. Utumi-shi mzuri kwa Kristo unafanywa na mtumishi zaifu tu. Kwa kipimo cha uza-ifu wake, uwezo wa Kristo utaonekana ndani ya mahubiri yake.

12:8 Paulo alisihi Bwana mara tatu ili mwiba huu **uweze kumwondokea**.

12:9 Mungu alijibu ombi la Paulo, lakini si namna alivyotumaini. Ni kama alisema na Paulo, “sitaondosha mwiba, lakini nitafanya neno lililo zuri kupita: Nitakupa neema kuuvumilia. Na kumbuka, Paulo, hata kama sikukupa kitu uli-

choomba, ninakupa kitu unachohitaji zaidi. Unataka kuwa na uwezo na nguvu yangu kuwa pamoja nawe saa unapohu-biri, sivyo? Njia nzuri zaidi kwa neno hili kufanyakana ni kwa wewe kuchungwa katika hali ya uzaifu.”

Mungu alijibu hivi tena ombi Paulo aliloomba mara tatu. Na hili linakaa kuwa jibu la Mungu kwa watu wake wa-naoteswa duniani pote. Neno lililo zuri kupita kuondolewa kwa majaribu na mateso ni kuwa na urafiki wa Mwana wa Mungu ndani yao, na kujuana na nguvu na neema yake ambayo inatuwezesha kushinda.

Ona ya kwamba Mungu anasema, **Neema yangu iNAfaa kwako**. Hatuhitaji kumwombwa kufanyiza neema yake ku-tosha kwasi. Inatosha **hata sasa!**

Roho ya mtume ilitulizwa kabisa na jibu la Bwana, hivi alisema, “**Afazali ni-tajisifu katika uzaifu wangu, uwezo wa Kristo ukae juu yangu**.”

Wakati Bwana alipoeleza akili ya matendo yake, ni kama Paulo alisema asingetaka neno lingine. Hivi kwa pahali pa kununguniya juu ya mwiba, atataka zaidi **kujisifu katika uzaifu wake**. Atapiga magoti yake na kushukuru Bwana kwa sababu yake. Atafurahi kuuvumilia na furaha kama kwa njia hii uwezo wa Kristo utakaa juu yake. J. Oswald Sanders alisema vizuri:

Watu wa dunia wanasesma, “Kama haiwezekani kuponyesha kitu, ina-pasa kukivumilia.” Lakini Paulo anashuhudu na furaha, “Kama hai-wezekani kuponyesha kitu, ina-wezekana kukifurahia. Ninafurahia mateso, uzaifu, ukosefu wa vitu, na magumu.” Aliona kwamba neema ya Mungu ni ajabu sana ndani ya maisha yake, hata aliweza kusema, “Ninasifu, na hata kufurahia mwiba wangu.”¹⁹

12:10 Haiwezekani kwa sisi watu **ku-furahia** namna ya maneno yanayotajwa hapa. Maneno mane yanatusaidia kufa-

hamu, ndiyo “**kwa ajili ya Kristo.**” Ingetupasa kukubali kuvumilia kwa ajili yake, na kwa kuendelesha Habari Njema, maneno tusingevumilia kwa sisi wenyewe au kwa ndugu mpendwa.

Wakati tunapofahamu uzaifu wetu, na ya kwamba sisi si kitu, tunategemea uwezo wa Mungu zaidi. Na wakati tunapolazimishwa kumtegemea kabisa, tujanuana na uwezo wake, na tuko wenye nguvu kweli.

Ndani ya shairi hili Paulo anatii neno la Bwana ndani ya Matayo 5:11,12. Alifurahi wakati watu walipomtukana na kumtesa.

G. Alama za Paulo zilisimamisha utume wake (12:11-13)

12:11 Ni kama sasa Paulo alichoka na kuonekana kama mwenye kujisifu. Alifikiri **amegeuka mpumbavu akijisifu** hivi. Haikuwa vizuri kwaye kufanya hivi, lakini Wakorinto **walimlazimisha**. Ingalipasa Wakorinto kumsifu wakati wajuzi wake walipomshitaki na ukali. Hata kama yeeye mwenyewe **hakuwa kitu**, hakupungukiwa hata kidogo **mitume walio wakubwa** ambao Wakorinto walitukuza.

12:12 Aliwakumbusha ya kwamba wakati alipokwenda kuhubiri Habari Njema, Mungu alisibitisha kuhubiri kwake na **alama za mtume**. Alama hizi zilikuwa uwezo kufanya maajabu ambayo mitume waliwezeshwa na Mungu kufanya ili wasikiaji wao wajue kwamba walitumwa na Bwana.

Alama na maajabu na matendo ya uwezo si namna tatu za maajabu, lakini watu wanafikiri juu yao kwa njia mbalimbali. **Alama** zilikuwa maajabu yenye maana kwa akili ya watu. **Maajabu** yaliamsisha furaha na huzuni ndani ya roho zao. **Matendo ya uwezo** yalifanywa kwa uwezo wa Mungu tu.

Ni vizuri kuona namna Paulo alivyo-sema habari za **alama za mtume zilifanywa** katikati yao. Hakujisifu juu yao, lakini alisema ya kwamba Mungu alizifanya kwa njia yake.

12:13 Na kwa maneno ya maajabu na matendo ya uwezo, Wakorinto **hawakupungukiwa kuliko makanisa mengine**, lakini waliona namna zote mtume Paulo alizotenda katikati yao, sawa na yale alizotenda ndani ya **makanisa mengine**. Walipungukiwa nini kuliko makanisa mengine? Paulo alifahamu ya kwamba kuliwa na neno moja tu asilofanya, ndilo **hakulemea** Wakorinto. Hakuwaruhusu kumsaidia na mali. Aliomba usamehe kwa **kosa hili** kama neno hili **liliwapungukiza**. Ilikuwa “alama” ya pekee ya mtume asi-yotaka!

H. Kufika kwa Paulo kwa Korinto kuliwa karibu (12:14–13:1)

12:14 Tazama mara hii ni mara ya tatu mimi ni tayari kuja kwenu. Labda maana ya maneno haya ni ya kwamba mtume alikuwa *tayari* kufikia Korinto mara tatu, lakini *alikuwa pale* mara moja tu. Hakwenda mara ya pili, kwa sababu hakutaka kutendea waamini na ukali. Sasa alikuwa **tayari** kwenda **mara ya tatu**, na atawafikia mara ya pili.

Au labda maana yao ni ya kwamba yeeye ni karibu kufika kwao mara ya **tatu**. Tumesoma katika Matendo 18:1 juu ya kufika kwake mara ya kwanza. Mara ya pili aliyofika ulikuwa wakati wa huzuni (2 Kor. 2:1; 13:1). Sasa atakuja mara ya **tatu**.

Paulo alikusudi ya kwamba **hatawalemea** wakati atakapokuja, maana yake hatapokea mali toka kwao kwa mahitaji yake. Kwa nini? Hakutaka mali yao lakini roho zao. Aliweka roho juu ya watu kupita vitu. Alitaka kuwatendea kama baba. **Haipasi watoto kuwekea wazazi akiba, lakini wazazi kwa watoto.** Ni vivyo hivyo hata sasa. Ni **wazazi** wanaotumika sana kusudi **watoto** wawe na vyakula na mavazi. Si desturi ya watoto kuchunga **wazazi** wao na kuwapatia vitu hivi. Paulo alisema hapa kwamba angetaka kupewa ruhusa kuwatendea kama mzazi.

Lakini maana ya shairi hili haiko ya kwamba inapasa wazazi kuwekea watoto akiba kwa wakati wa kuja. Shairi hili linafundisha juu ya mahitaji ya saa ile tu wakati Paulo alipokuwa akitumikia Bwana kwa Korinto. Aliweka roho kabisa ya kwamba hatategemea waamini wa pale kwa mahitaji yake. Hakufikiri kwamba iliwapasa kumwekeea akiba kwa uzee wake, au ya kwamba ilimpasa ye ye kuwafanya hivi.

12:15 Hapa tunaweza kuona nusu ya mapendo yasiyoweza kuzimika ya mtume Paulo kwa watu wa Mungu katika Korinto. Alikuwa tayari kujitoa na **furaha** kuwatumikia bila kuchoka kusaidia hali ya roho zao. Aliwapenda kupita walimu wa uwongo waliokaa katikati yao, lakini Wakorinto **walimpenda nusu kupita**. Lakini hakuweka roho juu ya neno hili. Hata kama alikosa tumaini kwamba watampenda ye ye vilevile, atakaa kuwapenda. Alikuwa mfuata wa kweli wa Bwana kwa neno hili.

12:16 Halafu Paulo alitumika na mashitaki ya wajuzi wake. Ni kama walisema, "Ndiyo, Paulo hakupokea mali toka kwenu. Lakini alijipatia mali kwa hila. Alituma wajumbe wake kwenye, nao walirudi kwake na mali yenyewe."

12:17 Hivi Paulo aliwaliza kama ye ye mwenyewe hakupokea mali toka kwao, **alituma** watu wengine kufanya hivi? Mtume aliuliza Wakorinto kama mashitaki yale yalikuwa kweli.

12:18 Anajibu ulizo lake ye ye mwenyewe. **Nilonya Tito** *kuwafikia ninyi*. Lakini hakutuma Tito peke yake. **Ali-tuma ndugu** mwingine **pamoja naye**, ili watu wasiwe na shaka juu ya makusudi yake. Nini ilitokea wakati Tito alipofikia Korinto? Aliomba kupewa yaliyokuwa haki yake? Aliomba Wakorinto kumsaidia na mali kwa mahitaji yake? Alijipatia faida kwa njia yao?

Sivyo; ni kama shairi hili linaonyesha kwamba Tito alitumika kazi kujipatia mali kwa mahitaji yake. Hii ndiyo maana ya maulizo ya Paulo, "**Hatukutembea kwa Roho mmoja na katika nyayo zile zile?**" Ni kusema kwamba Tito na Paulo vilevile walitumika kazi ili wasihitaji kusaidiwa na mali toka Wakorinto.

12:19 Masemo haya ya Paulo yangefikirisha Wakorinto kwamba Paulo alikuwa akitaka **kutoa uzuru** mbele **yao** kama mbele ya wajuzi. Lakini haikuwa hivi. Alikuwa akiwaandikia maneno haya kama mbele **ya Mungu**, kusudi waweze kujengwa. Alitaka kuwapatisha nguvu katika maisha yao kwa Kristo na kuwaonya kwamba watakutana na hatari. Alitaka kuwasaidia, kupita kuji-heshimu mwenyewe.

12:20 Paulo alitaka sana wakati atakapofikia Korinto aweze kukuta Wakristo wakikaa pamoja na furaha, nyuma ya kujitenga na walimu wa uwongo, na wakikubali amri ya mitume.

Na vilevile alitaka kuwafikia na roho ya furaha, si na huzuni. Angehuzunishwa sana kama akikuta **fitina, vivu, kasirani, ugomvi, masingizio, manongono, majivuno, na makelele**, na vita namna nyingine ya mwili.

12:21 Wakorinto hawa walikuwa furaha na taji ya kujisifu ya Paulo (1 Tes. 2:19). Walikuwa utukufu wake. Hakutaka kufika kwao na kupata haya kwa sababu yao. Wala hakutaka kulazimishwa **kulilia wengi** waliokuwa **wamekosa na wasiotubu uchafu, na uasherati na tamaa mbaya**.

Paulo alikuwa akisema juu ya watu **wengi gani waliokosa** zambi hizi? Tunawaza walikuwa ndani ya kanisa, lakini hatuna njia kujua kwamba walikuwa waamini wa kweli. Imeandikwa tu kwamba **walifanya** zambi hizi. Pahali pengine Paulo alisema wazi kwamba mtu ye yote aliye na mwenendo namna

hi hawezu kuriti ufalme wa Mungu (1 Kor. 6:9, 10). Mtume **ataombolea** kwa sababu yao, kwa sababu hawakutubu, na itapasa kuwaondoshea kanisani.

Darby alionyesha kwamba sura hii inaanza na habari za mbingu ya tatu, na sura yenyewe inakwisha na habari za zambi mbaya sana duniani. Na katikati ya mwanzo na mwisho ni matengenezo – uwezo wa Kristo ukikaa juu ya mtume Paulo.²⁰

13:1 Paulo alikuwa karibu na kufikia Korinto. Wakati atakapokuja, zambi zilitendwa na waamini zitachunguzwa. Uchunguzi namna hii utafanywa kama ulivyoagizwa ndani ya Torati 19:15: **“Kwa kinywa cha washuhuda wawili au kwa kinywa cha washuhuda watatu neno litasimamishwa.”** Paulo hakusema kwamba yeeye ataongoza uchunguzi huu. Neno hili litafanywa na waamini wa kanisa, na yeeye mwenyewe atawasaidia kwa njia ya kutoa shauri.

I. Wakorinto wenyewe walihakikisha utume wa Paulo (13:2-6)

13:2 Paulo alikuwa amewaonya kwa safari yake ya pili ya kwamba atahukumu na nguvu wenyewe kutenda mabaya. Hatusomi juu ya habari nyingine juu ya safari ile. **Sasa**, hata mbele ya kufika kwake yeeye mwenyewe, aliwaambia wote kwamba wakati atakapofika **tena hatahurumia wale** waliokuwa wakifanya zambi.

13:3 Wakorinto walikuwa wamedanganywa na walimu wa uwongo walioamsha shaka ndani ya roho zao kama Paulo alikuwa mtume wa kweli. Walisema naye **kuhakikisha** kwamba alikuwa na amri kusema kwa ajili ya Mungu. Nini ilihakikisha kwamba **Kristo** alikuwa **akisema** kweli kwa njia yake? Mtume alianza jibu lake kwa njia ya kusema tena ulizo lao, **“mukitafuta alama, kama ni kweli Kristo anayesema ndani yangu ...”**

Halafu aliwakumbusha kwamba Kri-

sto alikuwa amejifunua kwao kwa **uwezo**. Hakuna **uzaifu** kwa namna maisha yao yaligeuka wakati walipomamini Habari Njema.

13:4 Maneno haya “**uzaifu**” na “**uwezo**” yalikumbusha Paulo ya kwamba nguvu toka uzaifu ulionekana ndani ya maisha ya Mwokozi, na unaonekana ndani ya maisha ya watumishi wake. Bwana wetu **alisulibowi katika uzai-fu, anaishi kwa nguvu za Mungu**. Na wafuata wake ni zaifu tu, lakini Bwana anaonyesha **uwezo** wake kwa njia yao. Wakati Paulo aliposema, **tutaishi pa-moja kwa uwezo wa Mungu kwenu**, hasemi juu ya ufufuko. Maana ya maneno yake ni ya kwamba wakati anapowafikia, ataonyesha **uwezo** mku-bwa **wa Mungu** kwa namna atakavyotendea wale waliokuwa wakifanya zambi. Walisema yeeye ni zaifu; atawaonyesha kwamba anaweza kuwa na nguvu wakati inapompsa kuazibu wataenda mabaya!

13:5 Shairi hili linaungana na sehemu ya kwanza ya shairi 3. **“Muki-tafuta neno kuonyesha kwamba Kristo akisema ndani yangu ... mujitafute wenyewe kama ninyi ni katika imani.”** Wao wenyewe walihakikisha kwamba alikuwa mtume. Ni kwa njia yake waliongozwa kuamini Mwokozi. Kama wakitaka kujuu kama kweli yeeye ni mtume, basi waijangalie wenyewe.

Mara nyingi watu wanataja shairi 5 **kutafuta roho zao** kama waliokolewa kweli. Neno hili si vizuri kwa sababu linaweza kushusha roho yao na kuamsha shaka ndani yao. Kwa njia ya Neno la Mungu tunaweza kujuu kwamba tuliolekolewa kweli. Dakika tunapoamini Kristo tunaweza kujuu kwa njia ya Biblia kwamba tumezaliwa tena. Wakati majuma na miezi inapopita, maneno mengine vilevile yanaonyesha kwamba tuna uzima mpya – mapendo mapya kwa mwenendo mtakatifu, kuchukia

zambi tusizochukia mbele, mapendo mapya kwa ndugu Wakristo, mwenendo haki, utii, na kujitenga na maneno ya dunia.

Paulo hakukataza Wakristo kutafuta roho zao kama waliokolewa kweli. Neno alilotaka ni waweze kufahamu kwamba wokovu wao unahakikisha ya kwamba ye ye ni mtume.

Kuna maneno mawili tu yaliyowezekana: au kwa **Yesu Kristo** kuwa **ndani** yao, au **walikataliwa**. Au Wakorinto walikuwa waamini wa kweli, au **walikataliwa**, maana walikuwa wa-wongo.

13:6 Kama walifahamu ya kuwa waliokolewa kweli, neno hili lilionyesha kwamba mtume Paulo alikuwa mtume wa hakika na **hakukataliwa**. Kugeuka kwa maisha ya Wakorinto kulikuwa ajabu kabisa lisilowezekana kwa njia ya mwalimu wa uwongo.

J. Paulo alitaka kutendea Wakorinto mema (13:7-10)

13:7 Sasa Paulo aliendelea na maneno ya kuazibu waamini kanisani waliofanya zambi. Alisema kwamba **aliomba Mungu** ili Wakorinto **wasi-fanye neno baya** kwa njia ya kukubali wengine katikati yao kutenda zambi. Aliwaonya kutumika na nguvu kuazibu wenyewe kutenda zambi na kuwarudisha kwa ushirika wa kanisa. Hakusema maneno haya ili ye ye mwenyewe **aone-kane** kama **mwenye kukubaliwa**. Hakutaka wafanye hivi ili aweze kusema kutii kwao kulikuwa alama ya amri yake. Alitaka wafanye yaliyo mema kwa sababu ni *haki*, hata kama ye ye **akionekana kama amekataliwa**.

Hapa tunaona tena ya kwamba Paulo hakuwa mtu wa kujifikiri mwenyewe. Aliombea watu wengine wakati wote waweze kubarikiwa, si kwa faida na heshima yake mwenyewe. Kama Paulo akikwendea Korinto na fimbo na kuyonyesha amri yake, na kulazimisha watu

kutii mafundisho yake juu ya azabu, angaliweza kutumia maneno haya kushindana na walimu wa uwongo. Angaliweza kusema kwamba matendo haya yangalihakikisha kwamba amri yake ilikuwa amri ya kweli. Lakini neno Paulo alilotaka zaidi lilikuwa kwa Wakorinto kuhukumu zambi wao wenyewe wakati Paulo asipokuwa pamoja nao, hata kama neno hili lingewapa walimu wa sheria njia kusema mabaya juu yake.

13:8 Tunafikiri ndani ya shairi hili Paulo alisema juu ya mitume. Sharti maneno yote waliyofanya yafanywe kundelesha kweli ya Mungu, si kwa faida yao wenyewe. Hata kwa maneno ya azabu, haifai watake kisasi. Lazima maneno yote yafanywe kwa utukufu wa Mungu na kwa kusaidia Wakristo wenzao.

13:9 Hapa tunaona tena ya kwamba kwa maneno ya Wakorinto Paulo haku-jifikiri mwenyewe hata kidogo. **Alifurahi** kama uzaifu, unyenyekevu na laumu yake ziliwapatisha nguvu kwa maneno ya Mungu. Na pamoja na furaha yake, aliomba vilevile waweze **kukamilishwa**. Akiwaza juu ya watenda zambi katikati yao, aliomba Wakorinto waweze kumaliza na kutimiza neno hili. Alitaka sana mapenzi ya Mungu yaweze kufanyikana ndani ya maisha yao.

13:10 Paulo aliwaandikia barua hii kwa kuwasaidia kutengeneza maneno yao wakati **asipokuwa pamoja nao**. Akiwa **pamoja** nao, ingempasa **kutumia ukali** kwa kadiri ya amri aliyopewa na **Bwana kujenga**, si **kubomoa**.

K. Salamu ya neema ya Paulo

(13:11-14)

13:11 Halafu Paulo alimaliza barua hii gafula na **kuagana** nao, mbele ya kuwatolea maonyo mane mengine. Kwanza, **wakamilishwe**. Ni neno linalotumiwa kwa kutengeneza mikila katika Matayo 4:21. Ilipasa Wakorinto

kuacha kugombana na kufanya zambi, na kuishi pamoja kwa salama.

Mufarijiwe. Maana yake ni “ku-pokea maonyo” vilevile. Mtume Paulo alikuwa amewatolea maonyo ya nguvu. Anasema nao sasa wapokee maonyo haya na roho nzuri, na kuyatii.

Muwe na nia moja. Kuna njia moja tu kuwa na **nia moja**, ndiyo kuwa na *nia ya Kristo*. Ni kuwaza namna yeche ana-vyowaza, na kutiisha mafikiri yetu yote na mapenzi yake.

Mukae katika salama. Ndani ya 12:20 tuliona ya kwamba kulikuwa na mabishano na magomvi katikati yao. Neno hili linatokea kila mara wakati watu wengine wanapopata njia kuingiza mafundisho ya sheria. Hivi Paulo aliwaonya kuazibu watenda mabaya, kisha kukaa na Wakristo wenzao na salama.

Kama wakifanya hivi, **Mungu wa mapendo na salama atakaa pamoja nao.** Ndiyo, Mungu ni pamoja na watu wake *wakati wote*. Lakini wakimtii ndani ya maneno haya, atajionyesha na ukaribu zaidi kwao.

13:12 Ilikuwa desturi ya Wakristo kwa wakati wa mitume kusalimiana na **busu takatifu**. Sharti iwe busu *takatifu* kuonyesha mapendo safi na ya kweli. Wakristo wa inchi nyingi wanashika desturi hii hata sasa. Lakini ndani ya inchi nyingine kwa wanaume kubusana ni alama ya zambi, na kufungana na desturi hii kungeleta haya na laumu juu ya ushuhuda wa Wakristo. Kwa inchi hizi ni vizuri kukomboa busu ile na kushikana mkono.

13:13 Salamu ya **watakatifu wote** ingekumbusha Wakorinto kwamba waliikuwa wameingizwa ndani ya ushirika mkubwa. Watakumbushwa vilevile ya kuwa makanisa mengine watatazama namna walivyoendelea katika imani na kutii Bwana.

13:14 Baraka hii ya mwisho ya Paulo ni moja ya baraka tamu sana katika

Agano Jipy, na inataja Mungu Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, ndiye nafsi tatu ndani ya Mungu mmoja.

NOTES

¹ (1:20) H. W. Cragg, *The Keswick Week*, p. 126.

² (2:11) J. Sidlow Baxter, *Awake My Heart*, taken from the Nov. 10 reading. “Intoxication with Error.”

³ (2:14, 15) Frederick Brotherton Meyer *Paul*, ps .77, 78.,

⁴ (3:9) Charles Hodge , *A Commentary on the Second Epistle to the Corinthians*, p. 61.

⁵ (3:13) F. W. Grant “*2 Corinthians*” The Numerical Bible, VI:.547

⁶ (3:14) Hodge, *2 Corinthians*, p. 71.

⁷ (3:17) Wenye kutafsiri Biblia kwa Anglais (NKJV) walifikiri shairi hili linasema juu ya Roho Mtakatifu.

⁸ (3:18) Denney *2 Corinthians*, pp. 139, 140.

⁹ (3:18) J. N. Darby *Notes on I and II Corinthians*,189, 190.

¹⁰ (4:7) J. H. Jowett, *Life in the Heights*, p.65.

¹¹ (4:17) F. E. Marsh, *Fully Furnished*, p. 103.

¹² (5:15) Denney, *2 Corinthians*, p. 199.

¹³ (7:9) Hodge, *2 Corinthians*, p. 182.

¹⁴ (8:7) Denney, *2 Corinthians*, p. 267.

¹⁵ (11:27) Hodge, *2 Corinthians*, p. 275.

¹⁶ (11:33) J. B. Watson, further documentation unavailable.

¹⁷ (12:4) G. Morgan, *Searchlights*, p. 346.

¹⁸ (12:7) R. J. Reid, *How Job Learned His Lesson*, p. 69.

¹⁹ (12:9) J. Oswald Sanders, *A Spiritual Clinic*, pp. 32, 33.

²⁰ (12:21) Darby, *I and II Corinthians*, p. 253.

BIBLIOGRAPHIE

Darby, J. N. *Notes on I and 2 Corinthians*, London: G. Morriss, n.d.

- Davies, G. M. *The Epistles to the Corinthians*. Bombay: Gospel Literature Service, 1975.
- Denny, James, *The Second Epistle to the Corinthians*. London: Hodder & Stoughton, 1894.
- Erdman, C. R. *Second Epistle of Paul to the Corinthians*. London: Philadelphia: Westminster Press, 1929.
- Grant, F. W. "2 Corinthians," *The Numerical Bible*, Vol. 6, Acts –2 Corinthians. New York: Loizeaux Brothers, 1901
- Hodges, Charles, *The Second Epistle to the Corinthians*. London: The Banner of Truth Trust, 1959.
- Hughes, Paul E. *Commentary on the Second Epistle to the Corinthians*.
- Grand Rapids: William B. Eerdmans Publishing Co., 1962.
- Kelly, William. *Notes on the Second Epistle to the Corinthians*. London: G. Morrish, 1882.
- Lenski, R. C. H. *The Interpretation of St. Paul's First and Second Epistles to the Corinthians*. Columbus: Wartburg Press, 1937.
- Luck, G. Coleman. *Second Corinthians*. Chicago: Moody Press, 1959.
- Robertson, A. T. *The Glory of the Ministry*. New York: Fleming H. Revell Co., 1911.
- Wilson, Geoffrey B. *2 Corinthians: A Digest of Reformed Comment*. London: The Banner of Truth Trust, 1973.

BARUA KWA WAGALATIA

Utangulizi

Baraka inatoka kwa Mungu kwa njia ya imani, si sheria. Imani inawapa watu uhuru kuzaa matunda ya haki kwa uwezo wa Roho.

I. Nafasi ya pekee katika Kanuni

Asili ya watu wengi wenye lugha ya anglais, na français, ni Wagalatia.

Karibu na 278 av. J.C. wengi wa Wagalatia hawa walihama toka Europe kwenda inchi inayoitwa Turquie sasa. Sehemu yao ya inchi ile iliitwa “Galatia.” Ni kama Wagalatia walikuwa wenye kugeuza mawazo yao mbio (ona Gal. 3:1).

Barua kwa Wagalatia ni barua ya maonyo kwa Wakristo wa kwanza. Watu wengine wanafikiri juu yake kama mwandiko wa ufupi tu wa barua kwa Waroma kwani inataja maneno mengine yanayotajwa ndani ya Waroma vilevile (kama Habari Njema ya neema, Abrahamu, sheria, vivi hivi.) Lakini ndani ya barua ya Wagalatia mwandishi anajaribu na ukali kuponyesha Ukristo usigeuke jamii ya Masiya tu ya dini ya sheria ya Wayuda. Hatujui kama Wagalatia waliwaza nini juu yake, lakini tunajua kwamba Habari Njema ya neema, bila kazi za sheria, *ilishinda*, na Ukristo uliendelea kuwa imani ya dunia nzima.

Kwa wakati wa Matengenezo ya Kanisa (la Réforme) barua kwa Wagalatia ilikuwa na maana kubwa kwa Luther ambaye aliipenda sana. Aliandika kitabu cha mafundisho juu yake kilichosaidia watu sana, na hata sasa watu wanaweza kukinunua na kukijifunza.

II. Mwandishi

Watu hawakuwa na shaka ya kumba Paulo alikuwa mwandishi wa barua hii. Polycarp, Ignatius, Justin Martyr, Origen, Irenaeus, Tertullian, na Clement wa Alexandria walimtaja kuwa mwandishi wa Wagalatia ndani ya mandiko yao.

Mashairi mengine ya Wagalatia (1:1 na 5:2), na semo ndani ya 6:11 kwamba barua hii iliandikwa na “herufi kubwa” yanaonyesha kwamba Paulo alikuwa mwandishi wake, na ya kwamba labda alikuwa na ugonjwa wa macho. Neno lingine ambalo linahakikisha neno hili ni ya kwamba mbele Wagalatia walikuwa tayari kungoa *macho* yao kusaidia Paulo. Habari nyingine za historia ndani ya barua hii zinapatana na habari zili zoandikwa ndani ya Matendo vilevile.

III. Tarehe

Ndani ya barua hii tunasoma mara nyingine juu ya “makanisa ya Galatia” na mara nyingine juu ya “Wagalatia.” Kama mwandishi alikuwa akisema juu ya sehemu ya kusini ya Asie Ndogo, barua hii iliandikwa hata mbele ya kusanyiko la Yerusalem. Kama alisema juu ya sehemu ya kaskazini, Wagalatia iliandikwa nyuma.

Sehemu ya kaskazini iliitwa “Galatia,” lakini kwa maneno ya serikali sehemu ya kusini iliitwa “Galatia” vilevile

– ndiyo ‘Galatia, wilaya ya Waroma.’ Ndani ya kitabu cha Matendo Luka aliandika juu ya safari ya kwanza ya Paulo kwa kuhubiri kwa sehemu hii ya inchi (Antioquia kwa Pisidia, Ikonio, Listra, na Derbe), na juu ya safari yake ya pili ya kuhubiri Habari Njema pale vilevile. Tunawaza iliandikwa mbele ya kusanyiko la Yerusalem (Matendo 15, 49 A.D.) na kulikuwa na mabishano mengi juu ya tohara kwanza. Walimu wengine wanafikiri iliandikwa nyuma, karibu 53 A.D.

IV. Msingi na Jambo Kubwa

Kwa safari zake za kwanza za kuhubiri Paulo alifikia Asia Ndogo na alihubiri habari tukufu ya kwamba watu wanaweza kuokolewa kwa njia ya kuamini Kristo tu. Wengi wa watu waliosikia habari hizi waliokolewa, na makanisa yalianzwa. Mengine ya makanisa yalikuwa kwa Galatia. Wenyeji wa Galatia walikuwa watu wa kugeukageuka na wa vita.

Wakati Paulo alipokwisha kuondokea sehemu ile ya inchi, walimu wa uwongo waliingga makanisa na kuleta mafundisho mabaya. Walifundisha kwamba wokovu ni kwa njia ya kuamini Kristo

pamoja na kushika sheria. Walichanganya Ukristo na dini ya Wayuda, neema na sheria, Kristo na Musa. Walijaribu vilevile kuondosha Wagalatia wasifuate Paulo wakisema yeye si mtume wa kweli wa Kristo, hivi haifai kupokea mafundisho yake. Masemo yao maovu yалиумиза Wakristo wengi wa Galatia.

Bila shaka Paulo alihuzunishwa sanasana wakati aliposikia habari namna hii toka Galatia. Masumbuko yake yote kwa Wagalatia yalikuwa bure? Itawezekana kuponyesha Wakristo toka dini ya Wayuda iliyolazimisha watu kutii mafundisho haya ya sheria? Paulo hakukawa kujaribu kutengeneza maneno haya kwa njia ya kuandika barua hii ya uchungu kwa watoto wake wapendwa katika imani. Ndani yake alionyesha kwamba wokovu unapatikana kwa njia ya neema peke yake tu, si kwa njia ya kushika sheria hata kidogo. Matendo mema si neno la lazima kwa kupata wokovu, lakini ni tunda la wokovu. Mkristo amekufa kwa sheria; sasa anaishi maisha ya utakatifu, si kwa uwezo wake mwenyewe, lakini kwa uwezo wa Roho Mtakatifu wa Mungu anayekaa ndani yake.

HABARI YALIYOMO

1. PAULO ALISIMAMIA AMRI YAKE (Sura 1, 2)
 - A. Paulo aliandika na kusudi gani (1:1-10)
 - B. Paulo alisimamia mafundisho na utumishi wake (1:11 – 2:10)
 - C. Paulo alihamakia Petro (2:11-21)
2. PAULO ALISIMAMIA KUHAKIKISHWA KWA NJIA YA IMANI (3:1 – 5:1)
 - A. Kweli kubwa ya Habari Njema (3:1-9)
 - B. Kushindana kwa sheria na ahadi (3:10-18)
 - C. Kusudi la sheria (3:19-29)
 - D. Watoto na wana (4:1-16)
 - E. Utumwa au uhuru (4:17 – 5:1)
- 3 . PAULO ALISIMAMIA UHURU WA MKRISTO KATIKA ROHO (5:2 – 6:18)
 - A. Hatari ya sheria (5:2-15)
 - B. Uwezo kwa maisha ya utakatifu (5:16-25)
 - C. Maonyo ya kufaa (5:26 – 6:10)
 - D. Mwisho (6:11-18)

Maelezo

I. PAULO ALISIMAMIA AMRI YAKE (Sura 1, 2)

A. Paulo alandidika na kusudi gani (1:1-10)

1:1 Mara moja kwa mwanzo wa barua hii **Paulo** alisema na nguvu ya kwamba Mungu alimwita kuwa **mtume**. Mwito huu **haukutoka** kwa **watu**, wala haukuletwa na Mungu **kwa njia ya mtu fulani**. Paulo aliitwa **na Yesu Kristo na Mungu Baba ambaye alimfufua toka wafu**. Mtu anayeitwa na kupewa kazi na Mungu peke yake ni huru kuhubiri habari za Mungu bila kuogopa watu. Hivi Paulo hakuhitaji ruhusa ya mitume kumi na wawili, wala ya mtu mwingine, kwa mahubiri na utumishi wake.

Ndani ya shairi hili uungu wa Kristo unaonyeshwa wazi kwa njia ya maneno haya: **wala kwa mtu, ila kwa Yesu Kristo**. Na namna Paulo alivyo sema **Yesu Kristo** pamoja na **Mungu Baba** inaonyesha usawa wao. Halafu tunasoma juu ya Mungu Baba kwamba **ndiye aliyefufua Yesu toka wafu**. Ilikuwa vizuri kwa Paulo kukumbusha Wagalatia neno hili, kwani ufufuko ulionyesha kwamba ufufuko ulihakikisha ya kuwa Mungu alipendezwa sana na kazi ya Kristo kwa wokovu wetu. Ni kama Wagalatia hawakufurahia kazi ya Mwokozi kabisa, kwani walijaribu kungeza juu yake kwa njia ya matendo yao ya kushika sheria.

Paulo aliitwa na Kristo *nyuma ya ufufuko* wake, lakini mitume kumi na wawili walii twa naye wakati alipoaniza kwanza duniani. Paulo alitaja ufufuko tena na tena ndani ya mafundisho yake.

1:2 Paulo alifungana na **ndugu zote** waliokuwa **pamoja** naye. **Ndugu** hawa walifungana pamoja kusihu Wagalatia kushika kweli ya Habari Njema. Labda kwa kusudi Paulo hakuonyesha mapendo ndani ya barua yake kwa **makanisa ya**

Galatia. Ilikuwa desturi yake ndani ya barua zake nyingine kuita waamini “kanisa la Mungu,” “watakatifu,” au “waaminifu katika Kristo Yesu.” Alileta asante mara nyingi kwa Wakristo, au kuwashukuru kwa wema wao. Alitaja watu wengine na majina yao. Hakufanya maneno haya yote ndani ya barua hii. Makanisa ya Galatia walikuwa wameanguka sana na kukubali mafundisho ya uwongo, hivi Paulo aliwaandikia barua hii na ukali.

1:3 Neema na salama ni mawili ya maneno makubwa ya Habari Njema. **Neema** ndiyo wema wa Mungu kwa wenye zambi wasiyostahili hata kidogo. Kwa pahali pa kuwaambia watu *kufanya* maneno fulani, neema inawaambia maneno Mungu *anayokwisha kufanya*, na inawaomba kupokea wokovu kama zawadi. Scofield anasema, “Kwa pahali pa kutafuta watu wema wanaoweza kupokea za-wadi hii, neema inatafuta watu wanaokwisha kuhukumiwa, wenye hatia, watu amba o hawawezi kujisaidia, ili iweze kuwaokoa, kuwatukasa, na kuwatukuza.”

Salama ni tunda la neema. Wakati mwenye zambi anapopokea Mwokozi, ana **salama** na Mungu. Anastarehe akiju kwamba zambi zake zote zimesamehewa, na hatahukumiwa kamwe. Lakini neema *haimwokoi* tu; *inamlinda* vilevile. Na hatuhitaji **salama na Mungu** tu, lakini **salama ya Mungu** vilevile. Hizi ndizo baraka ambazo Paulo alitaka Wagalatia kupokea wakati alipoanza kuandika barua hii. Bila shaka Wagalatia walifahamu kwamba hawatapokea baraka hizi kamwe kwa njia ya sheria. Sheria inalaani watu wanaoasi maagizo yake. Haikuleta salama kamwe kwa roho ya mtu ye yote hata mmoja.

1:4 Halafu Paulo alikumbusha wasomaji wake bei kubwa sana ya wokovu wao. Waza juu ya maneno haya: Bwana a:

wetu Yesu Kristo **ambaye alijitoa mwenyewe kwa zambi zetu**. Kama **alijitoa mwenyewe** kusudi zambi za watu ziweze kusamehewa, hatuhitaji, wala hatuwezi kamwe kuongeza kitu juu ya kazi ile kubwa, wala kufanya upatanisho kwa zambi zetu kwa njia ya kushika sheria. Kristo ni Mwokozi wa pekee anayetosha. Alikufa **atuokoe katika dunia hii mbovu ya sasa**. Na alituokoa toka ubovu wa serikali, na machanganyiko ya matendo ya dini na imani ndani ya Kristo. Hivi ilifaa kwa Wagalatia kukumbushwa kwamba walikuwa wakirudi kwa dini toka ile Kristo alikufa kuwaponyesha! Ukombozi wa Kristo ulikuwa **kama Mungu na Baba yetu alivyopenda**. Unaonyesha kwa nguvu kwamba Mungu alikusudi kwa Kristo kuwa njia ya pekee ya wokovu, na ya kwamba hakuna njia nyingine.

Sharti shairi 4 litukumbushe kwamba Mungu haweki roho juu ya kutengeneza dunia kugeuka nzuri kupita, wala juu ya kusaidia watu kukaa na raha ndani yake. Anataka kuwaokoa toka uovu wake. Ingepasa hili kuwa kusudi letu vilevile.

1:5 Kwa njia ya Habari Njema ya neema, Mungu Baba na Bwana Yesu Kristo wanapata **utukufu** wote kwa wokovu wa watu. Mtu hawezikushiriki ndani ya utukufu huu kwa njia ya kutii sheria.

Kila neno ndani ya mashairi haya matano lina maana, na linajulisha kweli nyingi. Yanaonyesha ya kwamba Paulo aliandika zaidi juu ya maneno makubwa mawili ndani ya barua hii – *amri yake mwenyewe kama mtume*, na *habari njema ya neema ya Mungu*. Sasa yeche ni tayari kusema na Wagalatia juu ya maneno haya.

1:6, 7 Aliulizana na Wagalatia mara moja kwa nini walikuwa tayari kupokea mafundisho ya uwongo. Alishangaa kwa sababu walikubali mbio sana kuacha kweli ya Habari Njema. Alisema walicha Mungu na kufuata habari njema

nyingine. Mungu alikuwa **amewaita** katika **neema ya Kristo**, lakini sasa walikuwa wakijilingiza chini ya laana ya sheria. Walikuwa wamepokea Habari Njema ya kweli, lakini sasa walikuwa wameiacha kwa **habari njema nyiningine** isiyo habari nzuri hata kidogo. Ilikuwa machanganyiko ya neema na sheria.

1:8, 9 Paulo alitangaza laana ya Mungu mara mibili juu ya mtu ye yote anayehubiri **habari njema nyiningine**. Mungu ana habari moja tu kwa wenye zambi waliohukumiwa. Anataka kuwapa wokovu kwa njia ya neema, bila kushika sheria. Lazima wale wanaotangaza njia nyingine ya wokovu walaaniwe. Ni neno baya sana kuhubiri habari zinazozaa uharibifu wa milele wa nafsi za watu! Paulo hakuvumilia walimu wa uwongo namna hii, na haifai sisi kuwavumilia vilevile. John Stott alitoa maonyo haya:

Haifai tushangazwe na kuonekana kwa watu kama walimu na viongozi kanisani. Labda wanafika kwetu kama wenye heshima kubwa, na amri na elimu. Labda ni askofu, walimu wa université, au hata askofu mkubwa wa kanisa la Roma. Lakini wakifika na habari njema isiyo Habari Njema ambayo mitume walihubiri na iliyoandikwa ndani ya Agano Jipyä, inafaa kuwakataa pamoja na mafundisho yao.”¹

Ona ya kwamba mtume alisema **malaika ya mbinguni**, si “malaika ya Mungu.” Labda ingewezekana kwa **malaika ya mbingu** kuleta mafundisho ya uwongo, lakini malaika kutoka kwa Mungu hawezikufanya hivi. Maneno haya yanaonyesha wazi kabisa kwamba kuna Habari Njema namna moja tu. Ni njia ya pekee ya wokovu. Watu hawawezi kufanya neno lo lote kustahili kuipokea. Habari Njema peke yake ni bila mali wala bei. Sheria inalaani watu ambao *hawaii*, na Habari Njema inalaani wale ambao wanajaribu *kuigeuza*.

1:10 Labda Paulo alikumbuka ya kwamba adui zake walimshitaki juu ya kugeuza mahubiri yake kupendeza wasikiiasi wake, hivi aliuliza kama kwa njia ya kusema kuna Habari Njema moja tu, alikuwa akijaribu **kupendeza watu, au Mungu?** Ni wazi ya kwamba haku-jaribu **kupendeza watu**, kwa sababu watu wanachukia mawazo kwamba kuna njia moja tu kufika mbinguni. Kama Paulo angaligeuza mahubiri yake kupendeza **watu**, kama **asingalikuwa mtumwa wa Kristo.** Angalifanyiza gazabu ya Mungu kumwangukia.

B. Paulo alisimamia mafundisho na utumishi wake (1:11– 2:10)

1:11, 12 Sasa mtume alitaja maneno sita kusimamia mahubiri na utumishi wake. Kwanza, Habari Njema ilifunuliwa na Mungu. **Haiko namna ya watu**, maana haikutoka kwa watu. Ndiyo, Habari Njema inatukuza Mungu tu, si mtu. Si namna ya Habari Njema ambayo watu wangaliweza kutayarisha! Paulo **hakupokea** toka mtu mwingine na **hakujifunza** juu yake kwa njia ya kusoma vitabu. **Ilifunuliwa** kwake na Yesu **Kristo** mwenyewe.

1:13, 14 Paulo alijuana sana na **dini ya Wayuda**, lakini hata hivi hakuingiza maneno ya sheria ndani ya Habari Njema yake. Alizaliwa Myuda, na alijifunza sheria tangu utoto wake. Yeye mwenyewe alichagua kutesa **kanisa**. Alikuwa na bidii sana kwa **dini** ya Wayuda kuliko watu wengi walioishi kwa wakati wake. Hakuna mtu aliyeweza kusema kwamba alihubiri Habari Njema ya wokovu kwa njia ya imani bila kutii sheria kwa sababu hakujuana na sheria. Kwa nini basi aliacha kuhubiri juu ya sheria? Kwa sababu Habari Njema haikuwa tunda la mawazo yake mwenyewe, lakini aliipokea toka Mungu.

1:15-17 Neno la tatu ndilo hili: Ali-shinda miaka michache ya kwanza ya utumishi wake peke yake, mbali na **mi-**

tume wengine. Sasa alieleza kwa sababu gani alihubiri bila kufungana na **watu** wengine. Nyuma ya kuokolewa, **hakufanya shauri mara moja** na watu wenye mwili na damu, na **hakwendea Yerusalem** pahali **mitume** wengine walipokuwa. **Alikwenda Arabia**, kisha **alirudia Damasiki**. Hakuepuka kwenda Yerusalem kwa sababu ya kukosa adabu kwa mitume wenzake, lakini kwa sababu alikuwa ameitwa na Bwana mfufuliwa mwenyewe, na kupewa utumishi wa namna nyingine kwa Mataifa (2:8). Hivi hakuhitaji kupewa ruhusa na watu kwa utumishi wake.

Inatupasa kufikiri juu ya masemo mengine ndani ya mashairi haya. Ndani ya shairi 15 tunasoma: **Mungu ... alintenga katika tumbo la mama yangu.** Paulo alifahamu ya kwamba hata mbele ya kuzaliwa kwake Mungu alimchagua kwa kazi kubwa fulani. Aliongeza kwamba Mungu **akanita kwa neema yake**, akikumbuka wokovu wake kwa njia iliyokwenda Damasiki. Kama siku ile angalipokea hukumu aliyostahili kupata, kama angalitupwa katika gehena. Lakini Kristo, na neema ya ajabu, alimwokoa na kumtuma kuhubiri habari za imani ambayo alijaribu kuharibu mbele.

Ndani ya shairi 16 alionyesha kwamba Mungu alikusudi **kufunua Mwana wake** ndani *yake*. Neno hili lina-onyeshea kusudi la ajabu la Mungu wakati alipotuita sisi – kufunua Mwana wake ndani *yetu*, ili tuweze kuonyesha Bwana Yesu kwa dunia. Anafunua Kristo kwa miyo yetu (sh. 16) ili aweze kuonyesha Kristo kwa njia yetu (mash. 16-23), kusudi Mungu aweze kuitukuzwa kwa njia hii (sh. 24). Kazi Paulo aliopewa ilikuwa kuhubiri Kristo kwa Mataifa.

Ndani ya shairi 17 alisema, “**Nili-kwenda zangu katika Arabia.**” Kila mtumishi wa Bwana anahitaji saa kukaa peke yake kwa kuwaza juu ya Mungu na

maneno yake, na kumwabudu. Musa alikaa jangwani kwa miaka makumi ine. Daudi alikuwa peke yake na Mungu wakati alipochunga kondoo vilimani mwa Yudea.

1:18-20 Neno la ine, wakati mwishoni Paulo alipofikia Yerusalem, alikutana na **Petro** na **Yakobo** tu. Zaidi ya ile, makanisa ya Yudea walimjua nusu tu (1:21-24). Kuonyesha tena ya kwamba hakufungana na mitume wengine, Paulo alipasha ya kuwa **miaka mitatu** ilikuwa imepita tangu kuokolewa kwake mbele ya kwenda kwake kwa Yerusalem kukutana na **Petro** kujuana naye kama rafiki – si kama mtu mkuu (Mdo. 9:26-29). Wakati alipokuwa pale, alikutana vilevile na **Yakobo, ndugu ya Bwana**. Alikaa pamoa na Petro kwa **siku kumi na tano**, muda fupi tu. Habari hizi zinaonyesha kwamba alikuwa hali moja na watumishi hawa wa Bwana.

1:21-24 Nyuma ya ile Paulo alishinda saa nyangi kidogo kwa **Suria na Kilikia** – na **makanisa ya Yudea** hawakujuana naye. Walijua tu ya kwamba mtu huyu aliyetesha Wakristo na ukali sana mbele alikuwa Mkristo yeye mwenyewe sasa na alihubiri Habari Njema ya Kristo kwa watu wengine. **Wakatkuza Mungu** kwa kazi aliyokwisha kufanya ndani ya maisha ya Paulo. (Watu wanatkuza Mungu juu ya maneno ambayo yamegeuka ndani ya maisha yetu?)

2:1 Neno la tano ndilo hili: Wakati Paulo alipofikia Yerusalem mara ya nyuma, mitume waliokuwa pale walikubali ya kwamba Habari Njema yake ilitoka kwa Mungu (2:1-10). Kanisa lilikuwa limeanza kwa Yerusalem, na kwa sababu hii ni kama mitume wali-fanyiza mji huu kuwa kao lao kubwa. Kwa sababu hii ni kama Paulo haku-heshimiwa kama mitume ya Yerusalem kwa sababu hakuwa mmoja wao. Paulo alisema juu ya neno hili wakati alipofikia **Yerusalem** tena. Hatujui kama ilikuwa miaka **kumi na ine** nyuma ya

kuokolewa wake, au nyuma ya safari yake ya kwanza kwenda kule. Lakini tunajua ya kwamba alipokea ufunuo toka Kristo aende, pamoa na **Barnaba** alireshiriki naye ndani ya kazi yake, na **Tito**, Mtaifa, aliyekolewa kwa njia ya utumishi wa Paulo. Walimu wa sheria walisema na nguvu kwamba ilipasa Tito kutahiriwa kwa kutimiza wokovu wake. Mtume Paulo alishindana na neno hili sana kwa sababu alifahamu kwamba neno hili lilikana kweli ya Habari Njema. (Kwa wakati wa nyuma Paulo alitahiri Timoteo yeye mwenyewe, lakini kwa wakati ule tendo hili halikushindana na Habari Njema – Mdo. 16:3.)

E. F. Kevan alisema:

Paulo alifahamu kwamba tohara haikuwa desturi isiyo na maana. Alijua kwamba saa mtu alipotaka kutahiriwa alitaka kuhesabiwa haki kwa njia ya kushika sheria, na ya kwamba neno hili lilikana msingi wa neema (ya kama neema ndiyo msingi wa Habari Njema.)

2:2 Wakati Paulo alipofikia Yerusalem, **aliwaelezea Habari Njema ile** aliyohubiri **katika Mataifa**, lakini kwa **siri kwa wenye heshima, isiwe hakose anapiga mbio bure, au amepiga mbio bure**. Kwa sababu gani alisema **kwa siri** kwa viongozi, si kwa kanisa zima? Alitaka wakubali Habari Njema yake, na ya kwamba hakuhubiri neno lisilokuwa taratibu? Sivyo, hata kidogo! Alikuwa amesema mbele ya kwamba habari zake zilifunuliwa kwake na Mungu. Hakuwa na shaka rohoni mwake ya kwamba mafundisho yake yalikuwa kweli. Lakini ilikuwa adabu kusema kwanza na viongozi, ili wao waweze kufahamu na kukubali kabisa ya kwamba Habari Njema ya Paulo ilikuwa Habari Njema ya kweli. Kama walikuwa na maulizo juu yake, Paulo alitaka kuyajua na kujibu na kuyaeleza kwanza. Halafu atawenza kusema na

kanisa zima, akijua kwamba mitume wengine walimsimamia. Kama Paulo asipofanya hivi kama labda kutakuwa na mabishano yatakayotenga kanisa, sehemu ya Wayuda na nyingine ya Mataifa. Neno hili likitokea, safari ya Paulo kwenda Yerusalem isingekuwa na faida. Labda hii ndiyo maana ya masemo yake **isiwe hakose ninapiga mbio bure, au nilipiga mbio bure.**

2:3 Hali ya **Tito** ilisukuma kanisa kwa Yerusalem kuwaza sana juu ya maneno ya sheria. Watapokea mwamini huyu Mtaifa kanisani, au watamlazimisha **kutahiriwa** kwanza? Nyuma ya mashindano na maneno mengi, mitume walikata shauri kwamba tohara si neno la lazima kwa wokovu. Paulo alikuwa ameshinda kabisa.²

2:4 Mwanzo wa shairi 2 na shairi 4 yanaonyesha kwa sababu gani Paulo aliongozwa kwendea Yerusalem: “Nilikwenda kwa ufunuo ... **kwa ajili ya ndugu za uwongo walioingizwa kwa siri.**” Neno hili lilitokea kwa Antiochia mbele (Mdo. 15:1, 2). Walimu Wayuda wengine toka Yerusalem, waliotenda kama Wakristo, walikuwa wameingizwa **kwa siri** katika kanisa kwa Antiochia, na walikuwa wakifundisha kwamba tohara ni lazima kwa wokovu.

2:5 Paulo na Barnaba walishindana sana na walimu hawa. Kwa kukata jambo hili, Paulo, Barnaba, na wengine walikwendea Yerusalem kuona kama mitume na wazee walifikiri nini juu ya neno hili.

2:6 Wenyewe heshima na viongozi kwa Yerusalem **hawakuongeza** Paulo kitu, au kwa maneno ya mafundisho yake, au kama mtume. Hili lilikuwa ajabu. Ndani ya sura 1 alisema wazi ya kwamba alikuwa saa nusu tu pamoja na mitume wengine. Lakini sasa wakati aliposemezana nao, wao wote walikubali kwamba Habari Njema aliyohubiri lilikuwa sawasawa na Habari Njema yao.

Neno hili lilikuwa neno kubwa! Viongozi hawa Wayuda walikubali kwamba Habari Njema yake haikupunguka kwa njia yo yote. Hata kama Paulo alikaa mbali nao na hakupokea mafundisho toka kwao, Habari Njema yao ilikuwa sawasawa na Habari Njema yake kwa maneno yote. (Paulo hakutaka kupunguza heshima ya mitume wengine. Alisema tu kwamba **namna** yao haikuwa kitu kwake, maana hata walikaa pamoja na Bwana Yesu wakati alipokuwa duniani, Paulo hakufikiri neno hili liliongeza amri yao. Mungu hakubali mtu kwa sababu ya maneno namna hii ya kuonekana.)

2:7, 8 Mitume kwa Yerusalem walikuwa wametambua kwamba Paulo alipewa heshima ya kupeleka Habari Njema kwa **wasiotahiriwa** (Mataifa), kama vile **Petro** alikuwa ametumwa kwa Wayuda. Habari Njema ambayo wao wawili walihubiri ilikuwa sawasawa, lakini walihubiri kwa mataifa mbalimbali.

2:9, 10 Hata **Yakobo, Kefa** (Petro), na **Yoane**, waliohesabiwa kama **nguzo** za kanisa, **walitambua** kwamba Mungu alikuwa akitumika kwa njia ya Paulo, wakampa ye ye **na Barnaba mkono wa kuume wa ushirika** ndani ya kazi yao kupeleka Habari Njema kwa Mataifa. Halikuwa tendo la kuwafanyiza viongozi kanisani, lakini lilionyesha ushirika wa mapendo nao ndani ya kazi ya Paulo. Waliomba Paulo na Barnaba kufanya neno moja tu, ndilo **kukumbuka masikini, ndilo neno ambalo** Paulo alitaka sana kufanya.

C. Paulo alihamakia Petro

(2:11-21)

2:11 Kwa jibu la sita, na la mwisho la Paulo kwa wale waliokuwa wakibishana naye juu ya utume wake, Paulo alipasha kwamba ilikuwa lazima kwaye kukemea mtume **Petro**. Wengi wa Wakristo Wayuda waliheshimu Petro kama mkubwa

wa mitume. (Shairi hili linaonyesha uwongo wa mawazo ya kwamba Petro alikuwa kiongozi bila zambi la kanisa.)

2:12 Wakati Petro alipofikia Antiokia kwanza, **alikula pamoja na Mataifa**, akifurahia uhuru wake kama Mkristo. Asingaliweza kufanya hivi kama angalifungwa na desturi za Wayuda. Nyuma ya wakati, watu wengine walifikia Antioquia **toka Yakobo** katika Yerusalem. Walisema walismamia Yakobo, lakini Yakobo alikana neno hili nyuma (Mdo. 15:24). Tunafikiri walikuwa Wakristo Wayuda waliofungana kwanza na desturi nyingine za sheria. Wakati watu hawa walipofika, Petro aliacha kushiriki na Mataifa kama mbele. **Aliogopa** kwamba habari za kushiriki kwake na Mataifa zitafikia Wakristo Wayuda walioshika sheria katika Yerusalem. Kwa njia ya kufanya hivi, Petro alikana moja ya kweli kubwa za Habari Njema – ndio umoja wa waamini wote ndani ya Kristo Yesu, si neno kama wakiwa watu wa taifa gani. Findlay anasema: “Kwa njia ya kukataa kula pamoja na watu wasiotahiriwa, Petro alionyesha wazi ya kwamba, hata watu hawa wakiwa waamini katika Kristo, kwa mafikiri yake walikuwa ‘si safi,’ na ya kwamba utaratibu wa sheria ya Musa ulileta utakaso mkubwa kupita haki ya imani.”

2:13 Wengine walifuata mfano wa Petro, hata Barnaba vilevile, ndiye mwenye kufungana sana na Paulo ndani ya kazi. Paulo alifahamu kwamba tendo hili lilikuwa baya sana, akashitaki Petro na uhodari, na kumwita **mnafiki**. Kemeo lake limeandikwa ndani ya mashairi 14-21.

2:14 Petro alikuwa Mkristo na alijua kwamba Mungu hakutambua makabila mbalimbali tena. Hivi alikuwa akiishi namna ya Mtaifa na alikula vyakula vyao, vivi hivi. Wakati sasa alipokataa kula pamoja na Mataifa, alionyesha kwa njia hii kwamba ilipasa kutii sheria na desturi za Wayuda kwa kuishi maisha mataka-

tifu, na ya kwamba ilifaa waamini wa Mataifa **waishi namna ya Wayuda**.

2:15 Ni kama tendo la Petro linaonyesha kama alifikiri kwa siri ya kuwa **Wayuda** ndio wenye heshima kupita **Mataifa** wazarauliwa. Haikuwa vizuri kwa Petro kuwa na mawazo namna hii. Mungu alikuwa amemfundisha mbele ya wokovu wa Kornelio kwamba haifai kuita mtu ye yote mchafu (Mdo. 10 na 11:1-18).

2:16 Wayuda waliokwisha kuokolewa walijuwa kwamba **sheria** haikuweza kuwaokoa. Sheria ilihukumu watu wote kufa ambao hawakuitii ndani ya maneno yote. Neno hili lilileta laana juu ya watu wote, kwa sababu wote wameasi maagizo yake matakatifu. Paulo alikumbusha Petro ya kwamba “**hata sisi Wayuda**” tumefahamu kwamba watu wanaokolewa **kwa imani ndani ya Kristo, wala si** kwa matendo ya sheria. Ilikuwa faida gani kwa Petro kusema ilipasa Mataifa kutii sheria? Sheria ilijulisha watu maneno gani ambayo iliwapasa kufanya, lakini haikuwapa uwezo kuyafanya. Kazi yake ilikuwa kufunua zambi zao, si kuwa mwokozi.

2:17 Paulo na Petro na wengine walikuwa wamefikia **Kristo**, Kristo peke yake, kuhesabiwa haki. Lakini ni kama matendo ya Petro kwa Antiokia yalionyesha ya kuwa hakuhesabiwa haki kabisa, lakini ilimpasa kurudi tena kutii sheria kutimiza wokovu wake. Ikiwa hivi, Kristo si Mwokozi mkamilifu na wa kufaa. Tukikwenda kwake kupata usamehe kwa zambi zetu, lakini nyuma yake inatupasa kwenda pahali pengine vilevile, ni kama Kristo ni **mtumishi wa zambi** asiyetimiza ahadi zake. Tukitegemea Kristo kutuhesabia haki, kisha tunarudi tena kwa sheria (inayoweza kuhukumu tu sisi wenye zambi), tunatenda kama Wakristo kweli? Tunaweza kutumaini Kristo atakubali matendo namna hii ambayo yanamfanyiza kuwa **mtumishi wa zambi?** Paulo alijibu

na nguvu, **Hapana, hata kidogo.**

2:18 Petro alikuwa ameacha kawaida ya sheria na aliamini Kristo. Alifahamu kwamba bila tofauti Wayuda na Mataifa vilevile waliweza kukaribia Mungu na kukubaliwa naye. Sasa, kwa njia ya kukataa kula pamoja na Mataifa, ali-jenga **tena** maneno **aliyobomoa** mbele. Kwa njia ya kufanya hivi alionyesha kwamba ye ye ni **mkosaji**. Au alianguka wakati alipoacha sheria kwa kufuata Kristo, au alianguka wakati alipoacha Kristo ili aweze kufuata sheria!

2:19 Azabu kwa mwenye kuasi sheria ilikuwa mauti. Mimi mwenye zambi, niliasi sheria, na ilinihukumu kufa. Lakini Kristo alipokea azabu ya sheria niliyovunja na alikufa kwa pahali pang. Hivi wakati Kristo alipokufa, mimi nilikufa. Alikufa kwa njia ya kutimiza maneno yote yaliyoagizwa na sheria. Hivi ndani ya Kristo, mimi **nilikufa kwa sheria** vilevile.

Mkristo alikuwa **amekufa kwa sheria**; hana neno na sheria tena. Ni kusema kwamba sasa mwamini ana ruhusa kuasi Amri Kumi kama akitaka? Sivyo, anaishi maisha matakatifu, si kwa sababu anaogopa kuasi sheria, lakini kwa sababu anapenda Mwokozi ambaye alikufa kwa ajili yake. Wakristo wanaotaka kutawaliwa na sheria tena ndani ya mwenendo wao hawafahamu kwamba neno hili linawaweka chini ya laana ya sheria. Na wakitaka kutii sheria moja tu, itawapasa kushika sheria nzima. Njia ya pekee kwa sisi **kuishi kwa Mungu** ni kuwa wafu kwa sheria. Sheria haikuweza kamwe kuzaa maisha matakatifu, na vilevile neno hili halikuwa kusudi la Mungu kamwe. Ndani ya shairi 20 njia yake kwa maisha matakatifu yanaelezwa.

2:20 Mwamini anafanywa **mamoja na Kristo** ndani ya mauti yake. *Si* Kristo tu aliyesulibishwa kwa Kalvari, *mimi nilisulibishwa* pale vilevile – ndani yake. Mimi si mwenye zambi tena kwa

macho ya Mungu. Nikiwa mtu wa dunia sijaribu tena kujipatia wokovu kwa njia ya matendo yangu mwenyeewe. Mimi si mtoto wa Adamu tena, mwanamume chini ya hukumu ya sheria, mtu wa zamaani mbele ya kuzaliwa tena. Tabia yangu ovu imesulibishwa na haina ruhusa tena ndani ya maisha yangu ya kila siku. Hii *ndiyo hali yangu* mbele ya Mungu; *ingepasa* kuwa hivi ndani ya mwenendo wangu wa kila siku vilevile.

Mwamini anakaa kuishi kama mtu mmoja wa dunia. Lakini yule ambaye Mungu anaona kama mfu si yule ana-yeishi. **Si tena mimi ninayeishi, lakini Kristo anayeishi ndani yangu.** Mwo-kozi hakufa kwami ili mimi nikae kuishi namna ninavyotaka. Alinikufia ili tangu wakati wa sasa aweze kuishi uzima wake ndani yangu. **Maisha ninayoishi sasa ndani** ya mwili huu wa dunia, **ninaishi kwa imani ndani ya Mwana wa Mungu.** Imani ni kutegemea. Mkristo anategemea Kristo wakati wote, kwa njia ya kumnyenyekoa, na kuacha Kristo kuishi maisha yake ndani yake.

Hivi mwamini anatawaliwa na Kristo, si na sheria. Si maisha ya kushindana, lakini ya kutumaini. Anaishi maisha matakatifu, si kwa sababu anaogopa azabu, lakini kwa sababu **anapenda Mwana wa Mungu, ambaye alimpenda na kujitoa kwa ajili yake.**

Umekwisha kutolea Bwana Yesu mai-sha yako pamoja na ombi ili uzima wake uweze kuonekana ndani ya mwili wako?

2:21 Neema ya Mungu inaonekana ndani ya zawadi yake ya wokovu ilio bila masharti. Mtu akijaribu kustahili wokovu kwa njia ya matendo yake atashindwa. Kama Petro angeweza kupa-ta kibali na Mungu kwa njia ya kutii sheria za Wayuda, **mauti ya Kristo** ingekuwa bure. Ni kama alipoteza uzima wake. Kristo alikufa kwa sababu watu hawakuweza kupa-ta **haki** kwa njia yo yote nyngine – wala kwa njia ya kushika sheria.

II. PAULO ALISIMAMIA
KUHAKIKISHWA KWA
NJIA YA IMANI (3:1 – 5:1)

A. Kweli kubwa ya Habari Njema (3:1-9)

3:1 Matendo ya Wagalatia yalionyesha kwamba walikosa ufahamu. Kuacha neema na kushika sheria tena kulikuwa **kulogwa**. Ni kama walilishwa na uchawi, na walipokea bila ufahamu mafundisho ya uwongo wakifikiri ni kweli. Wakati Paulo alipouliza: “**Ni nani aliye-waloga nini?**” neno hili *nani* lilisema juu ya *mmoja*, si juu ya *wengi*. Labda alifikiri kwamba mafundisho haya ya uwongo yalitoka kwa Shetani mwenyewe. Paulo alikuwa amehubiri **Yesu Kristo** kwa Wagalatia kama yule **aliye-sulibiwa** kuonyesha kwamba ingepasa msalaba wake kuwatenga kwa milele na laana na utumwa wa sheria. Namna gani waliweza kurudi tena kwa sheria, na kuna msalaba bure? Waliwaza tena matendo ya sheria ni kweli?

3:2 Wajibu basi ulizo moja tu. Wafikiri tena juu ya saa walipookolewa – saa Roho Mtakatifu alipokuja kukaa ndani ya miili yao. **Kwa njia gani walipokea Roho?** Kwa njia ya matendo, au kwa njia ya kuamini? Ni wazi ya kwamba walimpokea kwa njia ya kuamini. Hakuna mtu aliyepokea Roho kamwe kwa njia ya kushika **sheria**.

3:3 Kama wasipoweza *kupata* wokuvu kwa njia ya matendo yao, wanguweza kupata nguvu katika utakatifu au kukomea katika imani kwa njia ya sheria? Kama uwezo wa **Roho** ulihitajiwa kuwaokoa, wataweza kumaliza kazi yenyeve kwa njia ya matendo yao ya mwili?

3:4 Wakati Wagalatia walipoamini Kristo, walipata mateso mengi, labda kwa mikono ya Wayuda watawa walio-chukia Habari Njema ya neema. Taabu hii yote ilikuwa **bure**? Kwa njia ya kurudi kwa sheria, walikuwa wakionyesha

kwamba watesaji walitenda mema? **Ikiwa ni bure kweli.** Paulo alikaa kutaraji kwamba watarudi tena kwa Habari Njema **waliyoteswa** kwa sababu yake mbele.

3:5 Si wazi kama **yeye** ndani ya shairi 5 ni Mungu, Paulo, au mtu mwingine aliyekuwa akifundisha Wagalatia kwa wakati Paulo alipoandika barua hii. Baa-daye alikuwa Mungu, kwa sababu **yeye** tu anawenza kuleta **Roho** Mtakatifu. Labda Mungu alitumika na Mkristo mwingine kutimiza mapenzi yake. Ingekuwa heshima kubwa sana kwa mtumishi wa Kristo. Mtu *mmoja* alisema kwamba “Kazi ya kweli ya Kikristo – ya kila aina ya utumishi –ni kufikisha Roho Mtakatifu kwa watu weninge; ni kuwagawia Roho.”

Kama mtume alikuwa akisema juu yake mwenyewe, labda aliwaza juu ya maajabu yaliyofanywa saa alipohubiri, na namna Wagalatia walivyopokea Kristo (Ebr. 2:4). Lakini namna maneno haya yalivyoandikwa haionyeshi kwamba ni maneno yaliyotokea zamani, au maneno yaliyokuwa yaktiteka kwa wakati yalipoandikwa. Tunafikiri Paulo aliwaza juu ya zawadi za ajabu ambazo Roho Mtakatifu aliwapa waamini nyuma ya kuokolewa kwao, kama tunavyosoma ndani ya 1 Wakorinto 12:8-11.

Anafanya hivi kwa matendo ya sheria au kwa kusikia kwa imani? Jibu kwa ulizo hili ni: **Kwa kusikia kwa imani.** Waamini hawastahili kamwe kupokea Roho Mtakatifu na kazi yake ndani yao, kwani anatolewa kwa neema na kupokewa kwa **imani**. Ingepasa Wagalatia kufahamu kwa njia ya maneno yaliyotokea ndani ya maisha yao wenyewe ya kwamba wanabarikiwa kwa njia ya imani, si kwa njia ya kushika sheria.

Kwa kuhakikisha neno hili la pili, Paulo alitaja sasa maandiko ambayo walimu wa uwongo walitaja kuonyesha kwamba tohara ni neno la lazima! Basi, Agano la Kale lilisema nini?

3:6 Paulo alikuwa ameonyesha kwamba msingi wa matendo ya Mungu na Wagalatia ulikuwa imani. Sasa alionyesha kwamba watu waliokolewa kwa njia ya imani hata kwa wakati wa Agano la Kale. Ulizo ndani ya shairi 5 lilikuwa: “Ali-fanya hivi kwa njia ya matendo ya sheria, au kwa njia ya kusikia kwa imani?” Jibu kwa ulizo hili lilikuwa: “Kwa kusikia kwa imani.” Mwandishi akikumbuka jibu hili, shairi 6 linaanza na **“Kama vile Abrahamu ... alihakikishwa haki vivyo hivyo – kwa njia ya imani.**

Labda walimu Wayuda walifikiri juu ya Abrahamu kama mfano wao na walimheshimu sana. Walisimamisha mafundisho yao ya lazima kwa mtu kutahiriwa kwa kupata wokovu juu ya maneno ambayo yalimpata kwa Mwanza 17:24, 26. Paulo alishindana nao juu ya neno hili. Aliwajibu kwa njia ya kuuliza kama Abrahamu aliokolewa namna gani. **Abrahamu aliamini Mungu.** Hakukolewa kwa sababu kazi yake mwenyewe ilimstahilisha. Hakufanya kitu kumstahilisha. Ndiyo, mtu asiyeamini ni mpumbavu. Kuamini Mungu ni njia ya pekee kwa mtu kupata wokovu bila katumika kazi wala kujivuma. Si “kazi njema” ya mtu. Nini ni vizuri kupita kwa kiumbe: kuamini Mwumba wake, au kwa mtoto kuamini Baba yake?

Kuhesabu haki ni tendo la Mungu wakati anapotangaza watu wote wanomwamini kuwa wenyе haki. Mungu anaweza kutendea wenyе zambi hivi na haki kwa sababu Kristo alikufa kwa ajili ya wenyе zambi juu ya msalaba wa Kalvari kulipa deni ya zambi zao. Maana ya kuhesabu haki haiko ya kwamba anafanyiza mwamini kuwa haki bila zambi. Anamhesabu haki kwa sababu ya kazi ya Mwokozi, na kwa sababu hii hali ya mwenyе zambi ambaye anamwamini inafaa kwa mbingu sasa. Kisha inampasa kuishi maisha ya haki kwa kuonyesha shukrani yake kwa maneno mazuri yote aliyotendewa.

Sharti tufahamu kwamba msingi wa kuhesabiwa haki si kushika sheria hata kidogo. Ni imani kabisa.

3:7 Bila shaka walimu Wayuda walifikiri ilipasa Wagalatia kutahiriwa kusudi waweze kuwa wana wa kweli wa Abrahamu. Paulo alikataa mawazo haya. **Wana** wa kweli **wa Abrahamu** si wale waliozaliwa Wayuda, wala wale waliogeuka Wayuda, lakini wale waliookolewa kwa njia ya imani. Ndani ya Waroma 4:10, 11, Paulo alionyesha kwamba Abrahamu alihesabiwa kuwa haki *mbele* ya kutahiriwa, wakati alipohesabiwa kwanza kuwa *Mtaifa*.

3:8 Agano la Kale ni kama nabii anayetazama mbele kwa mia za miaka ya kuja, na kuona ya kwamba **Mungu atahesabia Mataifa haki kwa imani**, na Wayuda vivyo hivyo. Unabii ya kwamba **Mataifa watabarikiwa kwa imani**, haukutabiriwa ndani ya Agano la Kale tu, lakini ultangazwa kwa Abrahamu ndani ya Mwanza 12:3 – “Ndani yako jamaa zote za inchi watabarikiwa.”

Wakati tunaposoma shairi hili toka Mwanza kwanza, ni ngumu kufahamu namna gani Paulo aliona maana hii ndani yake. Lakini Roho Mtakatifu aliyeandika shairi hili ndani ya Agano la Kale, alijua kwamba lilisema juu ya Habari Njema ya wokovu kwa njia ya imani kwa mataifa yote. Paulo aliandika akiongozwa na Roho Mtakatifu, hivi aliwezeshwa kuleza maana ya maneno haya: **Kwa wewe** – maana, pamoja na Abrahamu, kama Abrahamu. **Mataifa yote** – Mataifa na Wayuda vilevile. **Watabarikiwa** – wataokolewa. Abrahamu aliokolewa namna gani? **Kwa njia ya imani.** Mataifa wataokolewa namna gani? Namna Abrahamu alivyookolewa – kwa imani. Na wataokolewa kama Mataifa, si kwa njia ya kugeuka Wayuda.

3:9 Na **wote walio na imani** ndani ya Mungu wanahesabiwa haki **pamoja na Abrahamu**. Huu ndio ushuhuda wa Maandiko ya Wayuda.

**B. Kushindana kwa sheria na ahadi
(3:10-18)**

3:10 Paulo alionyesha toka Maandiko Matakatifu ya kwamba sheria haileti baraka hata kidogo. Inaleta **laana** tu. Shairi hili halisemi “wote walioasi sheria,” lakini: **wote walio wa matendo ya sheria**, maana wanaojaribu kupendeza Mungu kwa njia ya kutii sheria. Wao ni **chini ya laana**, maana wamehukumiwa kufa. **Maana imeandikwa** (katika Tor. 27:26) “**Amelaaniwa kila mtu asiyedumu ...**” Haitoshi kutii sheria kwa siku moja tu, au kwa mwezi mmoja, au mwaka mmoja. Ni lazima **kudumu** kuitii. Ni lazima kuitii kwa kila neno. Haitoshi kutii amri kumi tu. Ni sharti kutii sheria mia sita na zaidi ndani ya vitabu vitano vya Musa!

3:11 Paulo alikaa kutumika na Agano la Kale kukana mafundisho ya walimbu wa uwongo. Alitaja mafundisho ya nabii Habakuki kuonyesha ya kwamba kila mara Mungu amehesabia watu haki **kwa imani**, si kwa sheria. Wale waliohesabiwa haki kwa imani, si kwa matendo, watakuwa na uzima wa milele. Wale waliokwisha kuhesabiwa haki kwa imani **wataishi**.

3:12 Sheria haiombi watu kuamini. Haiwaombi hata *kujaribu* kutii amri zenyewe. Inaagiza kuitii kabisa, kwa kila neno, kama tunavyoona wazi ndani ya kitabu cha Walawi. Sheria na imani ni mbalimbali kabisa. Sheria inasema: “Fanya na ishi.” Imani inasema: “Amini na ishi.” Haya ndiyo mawazo ya Paulo: Mwenye haki ataishi kwa imani. Mtu aliye chini ya **sheria** haishi kwa **imani**. Hivi yeye si *haki* mbele ya Mungu. Wakati Paulo aliposema: “**Mtu anayetenda maneno haya ataishi kwa maneno haya,**” alisema neno lisilowezekana kwa mtu kufanya.

3:13 Maana ya kukomboa ni kunnuna tena, au kuokoa kwa njia ya kulipa bei. **Laana ya sheria** ni mauti – ndiyo azabu kwa wenye kuasi maagizo

yake. Kristo ameokoa wale walio chini ya sheria, wasilipe azabu ya mauti ambayo sheria ilihitaji. (Bila shaka Paulo alisema juu ya Wayuda waamini wakati aliposema “**alitukomboa**”, lakini Wa-yuda hawa ni mfano wa mataifa yote ya watu.)

J. Cynddylan Jones alisema:

Wagalatia walifikiri kwamba Kristo aliwanunua kwa sehemu tu, na ya kwamba iliwapasa kutimiza kulipa bei yenewe kwa njia ya kuyenyeyekeea tohara na kawaida nyingine za Wayuda. Kwa sababu hii walikuwa tayari kudanganywa na walimu wa uwongo na kuchanganya dini ya Wakristo na Wayuda. Paulo anasema hapa, “Kristo ametununua *kabisa* toka laana ya sheria.”³

Kristo alikomboa watu kwa njia ya kufa kwa pahali pao, na kuvumilia gazabu kubwa ya Mungu kwa sababu ya zambi zao. **Laana** ya Mungu ilimwangukia yeye kwa pahali pa kuangukia watu. Hakugeuka mwenye zambi, lakini zambi za watu ziliwekwa juu yake.

Kristo hakukomboa watu **toka laana ya sheria** kwa njia ya kutii Amri Kumi bila kuanguka wakati alipoishi duniani. Maandiko matakatifu hayafundishi ya kwamba utii wake mkamilifu wa sheria ulihesabiwa kwetu. Alituokoa toka sheria kwa njia ya kuvumilia laana yake katika kufa. Hakuna wokovu kama Kristo asipokufa. Sheria ilifundisha kwamba wakati wavunja sheria waliohukumiwa walipotundikwa juu ya mti, ilikuwa alama kwamba walilaaniwa na Mungu (Tor. 21:23). Hapa Roho Mtakatifu anaona ndani ya shairi hili unabii juu ya namna gani Mwokozi atakufa akivumilia laana kwa ajili ya viumbi vyake. Alitundikwa katikati ya mbingu na dunia, kama hakustahili kuwa au mbinguni au duniani. Alikufa kwa njia ya kusulibishwa, akatundikwa **juu ya mti** (Mdo. 5:30; 1 Pet. 2:24).

3:14 Mungu alikuwa ameahidi kubariki Abrahamu na kubariki dunia nzima kwa njia yake. **Baraka ya Abrahamu** ndiyo wokovu wa neema kwa njia ya imani. Lakini Mungu alihitaji kwanza malipo ya azabu ya mauti kwa zambi. Hivi Bwana Yesu alifanywa laana ili Mungu aweze kuwa na neema kwa Wayuda na Mataifa vilevile. Sasa ndani ya Kristo (aliye mzao wa Abrahamu) mataifa yanabarikiwa.

Hatusomi juu ya Roho Mtakatifu ndani ya ahadi ya Mungu kwa Abrahamu katika Mwanzo 12:3. Lakini hapa Paulo alitujulisha, akiongozwa na Mungu, ya kwamba zawadi ya **Roho Mtakatifu** ilikuwa sehemu ya agano la Mungu na Abrahamu, ndilo agano la wokovu bila masharti. Lakini Roho hakuweza kuja angali sheria ilipomzuiza. Ilikuwa lazima kwa Kristo kufa na kutukuzwa kwanza, kisha Roho Mtakatifu aliweza kuja (Yn. 16:7).

Kwa njia ya habari za Wagalatia mtume alikuwa ameonyesha kwamba wokovu ni kwa njia ya imani, si kwa sheria. Alionyesha neno hili vilevile kwa njia ya ushuhuda wa Agano la Kale. Sasa anaendelea kupasha juu ya mfano wa maisha ya kila siku ya watu.

Mawazo ya Paulo ndani ya mashairi haya yanaweza kujumlishwa hivi: Ndani ya Mwanzo 12:3 Mungu aliahidi kubariki jamaa zote za dunia ndani ya Abram. Ahadi hii ya wokovu ilikuwa kwa Mataifa na Wayuda. Ndani ya Mwanzo 22:18 Mungu aliahidi vilevile: "Kwa uzao wako mataifa yote ya dunia watabarikiwa." Alisema *uzao* (mmoja), si "mbegu" (nyingi). Mungu alikuwa aki-sema juu ya Mmoja, Bwana Yesu Kristo, aliyekuwa mzao wa Abrahamu (Luka 3:34). Ni kusema Mungu aliahidi kubariki mataifa yote, Mataifa na Wayuda pia, kwa njia ya Kristo. Ilikuwa ahadi bila masharti, wala ya matendo mema wala kutii sheria. Lilikuwa kusudi la Mungu kwa watu kupokea ahadi hii na imani.

Basi nyuma ya miaka 430 Waisraeli walipewa sheria, lakini sheria haikuweza kuongezea ahadi kitu wala kui-geuza kwa njia yo yote. Watu wakijaribu kuigeuza, wangetenda uzalimu. Kwa maneno ya Mungu neno hili lisingali-wezekana hata kidogo. Hivi Mungu anaahidi kubariki Mataifa kwa njia ya Kristo, kwa njia ya imani, si kwa njia ya kushika sheria.

3:15 Watu wa dunia wakitia mkono, maana kuandika majina yao kwa **agano** au wosia, hakuna mtu atakayejaribu kuli-batili wala kuliongezea neno. Kama hai-vezekani kuvunja maagano ya watu, kuzidi sana Mungu hawezo kuvunja maagano yake!

3:16 Bila shaka Wayuda hawa waliwaza kwamba hata ahadi hizi zilitolewa kwanza kwa Abrahamu na uzao wake (Waisraeli) kwa imani, wakati wa nyuma watu hawa walitiishwa chini ya sheria. Hivi hata kama Wagalatia waliokolewa kwanza kwa imani, walipaswa sasa kutii Amri Kumi. Paulo aliwajibu kwamba **ahadi** zilitolewa kwanza kwa **Abrahamu na uzao wake** (mmoja), ndiye Kristo. (Labda sisi watu tusingeona neno hili saa tunaposoma Agano la Kale, lakini Roho ya Mungu anafunua ufahamu wetu.)

3:17 Ahadi ya Mungu kwa Abrahamu ilikuwa bila masharti; haiku-fungamana na matendo hata kidogo. Alimpa Abrahamu uzao (Kristo). Hata kama Abrahamu hakuzaa mtoto, aliamini Mungu, na aliamini Kristo atakayekuja, na alihesabiwa haki. **Sheria iliyotolewa nyuma ya miaka 430** haikuweza kugeuza **ahadi** ya wokovu kwa njia yo yote. Haikuweza kuiondoa wala kuongeza juu yake.

Labda walimu wa dini ya Wayuda walifikiri kwamba sheria, iliyotolewa miaka 430 nyuma ya ahadi, iliitangua. Paulo alisema, "Sivyo, hata kidogo!" Alisawanisha ahadi na agano lililosibitishwa na mauti (zabihu ya agano,

Mwa. 15:7-11; ona vilevile Ebr. 9:15-22). Haikuwezekana kuitangua.

Miaka ile 430 ilianza kwa wakati Mungu aliposibitisha agano la Abrahamu kwa Yakobo, saa Yakobo alipokuwa karibu kuingia Misri (Mwa. 46:1-4). Iliendelea kufika sheria ilipotolewa karibu miezi mitatu nyuma ya wakati Waisraeli walipotoka Misri.

3:18 Inapasa **uriti** kuwa au kwa njia ya imani, au kwa matendo. Hauwezi kuwa kwa imani na matendo pamoja. Maandiko yanaonyesha wazi ya kwamba Abrahamu alipewa uriti kwa **ahadi** peke yake. Ni vivyo hivyo na wokovu. Mungu anataka tuupokee kama zawadi bila masharti. Haiwezekani kuupokea kwa njia ya kutumika kazi.

C. Kusudi la sheria (3:19-29)

3:19 Basi kusudi la sheria ni nini?

Paulo alisema kwamba sheria haikutangua ahadi Mungu aliyotolea Abrahamu, wala kuiongezea masharti meginge. Basi, **kusudi la sheria lilikuwa nini?** Kusudi la sheria lilikuwa kuonyesha kwamba zambi ni uasi. Zambi ilikuwa duniani mbele ya kutolewa kwa sheria, lakini watu hawakutambua kwamba ni uasi. Kuvunja sheria yo yote ni uasi.

Sheria ilitolewa kwa taifa la wenye zambi. Hawakuweza kamwe kugeuka wenye haki kwa sababu hawakuwa na uwezo kuitii. Kazi ya sheria ilikuwa kuonyeshea watu kwamba walikuwa wenye zambi bila tumaini, ili waweze kulilia Mungu kuwaokoa kwa neema yake. Agano la Mungu na Abrahamu lilikuwa ahadi ya baraka bila masharti; mwisho wa sheria ulikuwa laana tu. Sheria ilionyesha kwamba watu hawastahili kupokea baraka ya Mungu bila masharti na bila bei. Inawezekana kwa watu kubarikiwa kwa njia ya neema ya Mungu tu.

Mzao ndiye Kristo. Hivi, sheria ilikuwa kwa wakati tu, kufika kuja kwa

Kristo. Baraka Abrahamu aliyotolewa itakuja kwa njia ya Mzao huyu. Watu wawili wakifanya agano, wanahitaji **mpatanishi** kusimama katikati yao. Ilikuwa vivyo hivyo na Mungu na Israeli. Musa alisimama katikati ya Mungu na Israeli (Tor. 5:5). Malaika walikuwa wajumbe wa Mungu waliotolea Musa sheria (Tor. 33:2; Zab. 68:17; Mdo. 7:53; Ebr. 2:2). Musa na malaika wakisaidia ndani ya kazi hii walionyesha kwamba Mungu na watu wake hawakuwa na upatano wa karibu. Watu hawakustahili kukaa karibu naye.

3:20 Kama kuna mmoja tu aliyefanya agano, naye akitoa ahadi bila masharti na mtu mwingine asiye hitaji kufanya neno, halafu **mpatanishi** hakuhitajiwa. Lakini sheria ilihitaji mpatanishi, na neno hili linaonyesha kwamba ilikuwa lazima kwa mtu kutimiza sehemu yake ya agano lenyewe. Huu ulikuwa uzaifu wa sheria. Ilitaka watu kuitii, lakini watu hawa hawakuwa na uwezo kufanya hivi. Wakati **Mungu** alipotolea Abrahamu ahadi yake, ye ye peke yake alitoa ahadi hii. Hii ilikuwa nguvu ya ahadi yake: ilisimamia Mungu kwa maneno yote, bila kutegemea mtu kwa kitu cho chote. Mpatanishi hakuhitajiwa.⁴

3:21 Hivi **sheria** haikuhitaji **ahadi** tena na ilizikomboa? **Sivyo, hata kidogo!** Kama ingaliwezekana kwa Mungu kutoa **amri** kuwezesha wenye zambi kujipatia ukamilifu Mungu anataka, kama watu wangaliweza kuokolewa kwa njia ya kushika sheria. Mungu asingalituma Mwana wake mpendwa kufa kwa ajili ya wenye zambi kama watu wangaliweza kuokolewa kwa njia yo yote yenye bei chini kupita. Lakini kulikuwa na *saa na watu* wa kutosha kuonyesha kwamba sheria haikuweza kuokoa wenye zambi. Kwa njia hii sheria ilikuwa “zaifu kwa sababu ya mwili” (Rom. 8:3). Sheria iliweza kuonyeshea watu ukosefu wa tumaini lao

tu, na kuwafahamisha kwamba wokovu unawezekana tu kwa njia ya neema ya Mungu, bila tendo lo lote la mtu.

3:22 Agano la Kale lilionyesha kwa-mba watu wote ni wenye zambi, hata wale waliotawaliwa na sheria. Hivi ilikuwa lazima kwa watu kufahamu kabisa kwamba walikuwa wenye zambi kusudi **wenye kuamini wapewe ahadi** ya wokovu **kwa imani ya Yesu Kristo**. Maneno makubwa tunayoona ndani ya shairi 22 ni **imani, wapewe, na amini**. Hatusomi juu ya “matendo” wala “ku-shika sheria.”

3:23 Imani hapa ni imani ya kikristo. Inasema juu ya muda ulioanza na mauti, kuzikwa, ufufuko, na kupanda mbinguni kwa Bwana Yesu, na mahubiri ya Habari Njema kwa Pentekote. Mbele ya wakati ule Wayuda **walichungwa chini ya sheria** kama ndani ya gereza. Walifungwa kabisa na maagizo ya sheria. Iliwashinda kuyatimiza, na hawakuweza kuwa na **imani** iliyohitajiwa kwa wokovu. Watu waliokuwa chini ya sheria walifungwa hivi kufika wakati habari za utukufu ambazo ziliwafungua toka utumwa wa sheria ilipotangazwa ndani ya Habari Njema.

3:24 Sheria ni kama mlinzi na mwongozi wa watoto, au kama **mwalimu**. Sheria ilifundisha juu ya utakatifu wa Mungu, uovu wa watu, na hitaji kwa upatanisho. Hapa neno hili linatumwi kwa mtu anayetiisha na kuongoza watu wasiokomea bado.

Shairi hili linaonyesha kwamba sheria ilikuwa mlinzi myuda kufika wakati **Kristo alipokuja**, au kutazamia kuja kwa Kristo. Ni kama sheria ilichunga watu wa Israeli kama taifa mbali na mataifa mengine kwa njia ya magizo juu ya ndoa, mali, vyakula, vivi hivi. Wakati “imani” ilipokuja, ili-tangazwa kwanza kwa taifa hili lililolindwa na ajabu kwa mia za miaka. Kwa watu kuhesabiwa

haki **kwa imani** kulikuwa ahadi kwa sababu ya kazi ambayo Kristo Mkombozi, alitimiza.

3:25 Sheria ni **mwalimu**, lakini tangu **imani** ya kikristo ilipokuja, Wayuda walio waamini **si chini ya** sheria tena. Kuzidi sana Mataifa, kama Wagalatia, wasiokuwa kamwe chini ya mwalimu huyu! Shairi 24 linafundisha kwamba mtu *hahesabiwi haki kwa njia ya sheria*; shairi 25 linaonyesha kwamba maisha ya wale wanaohesabiwa haki *hayatawaliwi na maagizo ya sheria*.

3:26 Ona ya kwamba Paulo aliacha kusema juu ya “sisi” ndani ya sh. 25, na anaanza kusema kwa “**ninyi**” ndani ya sh. 26. Wakati aliposema juu ya Wayuda kama “sisi”, Paulo alionyesha kwamba walichungwa chini ya sheria kufika wakati Kristo alipokuja. Sheria il-wachunga kuwa watu mbali na watu wengine, walioweza kusikia mahubiri juu ya kuhesabiwa kwa haki. Wakati walipohesabiwa haki, hawakuwa chini ya sheria tena, na hawakuwa namna nyingine na watu wengine tena. Hivi wakati tunaposoma juu ya “**ninyi**” kuanza sasa kufika mwisho wa sura hii, “ninyi” inasema juu ya Wayuda na Mataifa wote waliookolewa. Watu hawa **ni wote wana wa Mungu kwa njia ya imani katika Yesu Kristo**.

3:27 Watu wanafungwa pamoja na **Kristo** saa wanapookolewa, na wanakirineno hili saa ya kubatizwa ndani ya maji. Ubatizo huu haufanyizi mtu ki-ungo cha Kristo wala mriti wa ufalme wa Mungu. Unasibitisha mtu huyu pamoja na Kristo, au, kama Paulo alivyo sema, “amevaa” **Kristo**. Kama askari “anavyovaa” kivao cha askari kuonyesha yeye ni mtu wa jeshi lake, vivyo hivyo mwamini anaonyesha yeye ni mtu wa Kristo kwa njia ya **kubatizwa** ndani ya maji. Kwa njia hii anaonyesha mbele ya watu kwamba ananyenyekoa kuongozwa na amri ya Kristo. Anaony-

sha mbele ya watu kwamba yeye ni mwana wa Mungu.

Bila shaka mtume hakufikiri kwamba ubatizo ndani ya maji unafuniganisha mtu na Kristo. Mawazo namna hii yangalikana kabisa mafundisho yake ya mbele kwamba mtu anaokolewa kwa njia ya imani tu.

Wala Paulo hakusema juu ya ubatizo wa Roho, unaoingiza mwamini ndani ya mwili wa Kristo (1 Kor. 12:13). Ubatizo wa Roho Mtakatifu hauonekani kwa macho. Hakuna neno linalosema juu ya “kuva” Kristo mbele ya watu.

Kwa njia ya ubatizo wa maji mwamini anaonyesha kuzikwa kwa mwili unaojaribu kujipatia haki. Anaonyesha kwamba ameacha namna ya maisha yake ya mbele na anaanza maisha mapya. Kwa njia ya kubatizwa ndani ya maji Wagalatia walikiri kwamba walikufa pamoja na Kristo na wamezikwa pamoja naye. Kristo alikuufa kwa sheria, nao waliikuwa wafu kwa sheria vivyo hivyo, na haifai watake kutawaliwa nayo tena ndani ya maisha yao. Wakati Kristo alipokufa, alimaliza tofauti iliyotenga Wayuda na Mataifa. **Wamevaa Kristo**, maana wanaishi sasa maisha mpya kabisa – maisha ya Kristo.

3:28 Sheria iliweka tofauti kwa Wayuda na Mataifa. Tunaona neno hili kwa Torati 7:6 na 14:1, 2. Kwa maombi yake ya asubui mwanamume Myuda alishukuru Mungu kwa sababu haku-mwumba Mtaifa, mtumwa, au mwanaamke. **Ndani ya Kristo Yesu** maneno haya ambayo yanatutenga yanatoweka kwa macho ya Mungu. Myuda hana afazali kupita Mtaifa, mwanamume aliye huru haheshimwi kupita mtumwa, na mwamume hana mapendeleo kupita mwanamke. Watu hawa wote ni sawasawa kwa sababu wao ni **ndani ya Kristo Yesu**.

Lakini hata hivi kwa macho ya Mungu wanaume na wanawake *ni mbalimbali*

ndani ya shairi hili lililo juu ya maisha ya watu wa kila siku (na ndani ya kanisa vilevile). Maagizo kwa wanaume ni mbalimbali na yale kwa wanawake. Agano Jipyä lina maagizo kwa watumwa yaliyo namna nyingine ya yale kwa bwana za kazi. Lakini neno hili si kitu, kwa sababu wote wanabarikiwa sawasawa. Neno kubwa ni kuwa **ndani ya Kristo Yesu**. Kwa macho ya Mungu Myuda anayeamini si mwenye heshima kupita mpagano aliyeokolewa. Hivi ni upumbavu kwa Wakristo kujaribu kuwa watakatifu kupita kwa njia ya kuweka tofauti ambazo Kristo alikuwa ameondosha.

3:29 Wagalatia walidanganywa kufikiri waliweza kugeuka uzao wa Abrahamu kwa njia ya kushika sheria, lakini Paulo alionyesha kwamba neno hili si kweli. Kristo ni uzao wa Abrahamu; ahadi ya uriti iliyotolewa kwa Abrahamu ilitimizwa ndani ya Kristo. Wakati wenyewe zambi wanapomwamini, wanaageuka mmoja naye. Kwa njia hii wanageuka **uzao wa Abrahamu** na, ndani ya Kristo, wanariti baraka zote za Mungu.

D. Watoto na wana (4:1-16)

4:1, 2 Mashairi haya yanaonyesha mfano wa baba mtajiri anayekusudi kutia mali yake mikonomi mwa mwana wake wakati mwana atakapokwisha kukomea. Lakini **wakati** mwana huyu ni kwanza **mtoto**, hali yake ni sawasawa na hali ya **mtumwa**. Anaagizwa saa zote kufanya maneno fulani na kukatazwa maneno mengine. Yeye ni chini ya **mawakili** wanaochunga mali yake, na **walinzi** wanaochunga hali yake mweenyewe. Hivi, hata kama bila shaka uriti ni mali yake, hatapata faida yake kufika wakati atakapokwisha kukomea.

4:3 Hali ya Wayuda chini ya sheria iliweka hivi. **Walikuwa watoto** walio-agizwa na sheria kama watumwa. **Walfungwa** chini ya **desturi za dunia**,

maana mafundisho ya dini ya Wayuda. Kawaida za dini ya Wayuda zilikuwa kwa wale wasiojua Mungu Baba namna anavyofunuliwa ndani ya Kristo. Sheria ilikuwa na mifano mingi kusaidia ufa-hamu wao wa roho kwa njia ya vitu vya kuonekana. Tohara ilikuwa mfano wa namna hii. Dini ya Wayuda ilikuwa ya mwili, ya kuonekana, na kwa wakati tu. Ukristo ni wa roho, na daima. Maneno ya kuonekana ya wenyе dini ya Wayuda yalikuwa kama **utumwa kwa watoto**.

4:4 Wakati ulipomalizwa ndio wakati uliochaguliwa na Baba wa mbinguni wakati wariti watakapokomea (ona shairi 2).

Ndani ya shairi hili tunasoma na maneno machache juu ya uungu na umtu wa Mwokozi. Yeye ni Mwana wa milele wa Mungu; hata hivi **alizaliwa na mwanamke**. Kama Yesu angalikuwa mwanamume tu, hakuna hitaji kusema kwamba **alizaliwa na mwanamke**. Hakuna njia nyingine kwa mtu wa dunia kuzaliwa. Lakini juu ya Bwana Yesu maneno haya yanaonyesha kwamba yeye ni namna nyingine, na ya kwamba kuzaliwa kwake kulikuwa namna nyiningine.

Akizaliwa duniani kama Mwisraeli, alikuwa **chini ya sheria**. Akiwa Mwana wa Mungu, Bwana Yesu asingalikuwa kamwe chini ya sheria. Ni yeye aliyetoa sheria. Lakini kwa neema yake ali-jinyenyekeza na kujiweka mwenyewe **chini ya sheria** ambayo yeye mwenyewe aliyotoa, kusudi aweze kuitukuza ndani ya maisha yake, na kuvumilia laana yake wakati alipokufa.

4:5 Ilikuwa sharti kwa watu wasiotii sheria kulipa bei – bei ya mauti. Lazima bei hii ilipwe kwanza, kisha Mungu aliweza kupokea watu kama wana. Hivi Bwana Yesu, akiuja duniani kama mtu wa dunia na wa taifa la Wayuda, alilipa bei iliyoagizwa na sheria. Kwa sababu yeye ni Mungu, mauti yake ilikuwa na faida bila kipimo, maana ilitosha kwa

wenyе zambi bila hesabu. Kwa sababu alikuwa Mtu, aliweza kufa kwa pahali pa mtu. Govett alisema: “Kristo, aliye Mwana wa Mungu, aligeuka Mwana wa watu, ili sisi wana wa watu tuweze kuwa wana wa Mungu. Badilisho ya ajabu!”

Wakati watu walipokuwa kwanza watumwa, hawakuweza kuwa **wana**. Kristo aliwaponyesha toka utumwa wa sheria ili waweze kupokewa **kama wana**. Ona ya kwamba kugeuka *mtoto* wa Mungu ni namna nyingine na kuwa *mwana* wa Mungu. (ona Rom. 8:14, 16). Mwamini anazaliwa ndani ya jamaa ya Mungu kama *mtoto* (ona Yn. 1:12). Mkazo hapa ni juu ya kuzaliwa kama *mtoto* wa Mungu, si juu ya mapendeleo na madaraka ya mwana. Mwamini ana-pokewa ndani ya jamaa kama *mwana*. Kila Mkristo ni mwana mara moja, na anaingizwa ndani ya uriti ulio wake. Hivi hakuna mafundisho kwa Wakristo ndani ya Agano Jipyä kwamba kuna watoto wachanga katikati ya watakatifu. Wao wote wanatendewa kama wana wa kukomea.

Utaratibu wa Waroma kupokea na kulea *mtoto* kama mwana wao kulikuwa namna nyingine na utaratibu wa wakati wa sasa. Sisi tunakamata *mtoto* wa mtu mwingine kuwa *mtoto* wetu. Lakini katika Agano Jipyä ni kuweka waamini kuwa wana wa kukomea, wenyе mapendeleo na madaraka yote ya wana namna hii.

4:6 Ili wale **walio wana** wa Mungu waweze kufahamu heshima ya neno hili, **Mungu** alituma **Roho** Mtakatifu wakati wa Pentekote kukaa ndani yao. Roho anawafahamisha rohoni ya kwamba wao ni wana, na anawaongoza kuita Mungu **Baba**. “**Aba, Baba**” ni njia ya jamaa kusema na Mungu, na inatumia maneno kwa “baba” kwa lugha za Aramaik na Kiyunani pamoja. Hakuna mtumwa aliweze kuita mkubwa wa jamaa na jina hili. Watu wa jamaa tu walilitumia, na lilionyesha mapendo na matumaini.

Ona vileyile ya kwamba ndani ya shairi hili tunaona **Roho, Mwana na Baba** – wakifuatana hivi.

4:7 Mwamini **si mtumwa tena**; hatawaliwi na sheria. Sasa yeche ni **mwana** wa Mungu. Kristo, akiwa Mwana wa Mungu, ni mriti wa utajiri wote wa Mungu, na Mkristo ni **mriti wa Mungu kwa njia ya Kristo**. Mali yote ya Mungu ni yake kwa imani.

Madarasa ya Warabi katika Israeli kwa wakati wa sasa yanafundisha kwamba mtu si mwanamume kufika wakati anapofika miaka 40, na anakatazwa kusoma Wimbo wa Solomono na Ezechiel 1. (Wakati kijana Myuda anapofika umri wa miaka kumi na tatu kuna kusanyiko la *bar mitzvah* kumfanyiza “mwana wa agano.” Kuanza wakati ule inampasa kutii sheria.

Ni namna nyingine na waamini chini ya neema. Tangu dakika wanapookolewa, wanapokea uriti mzima. Watu wanawatendea kama wana na binti wa kukomea, wenye ruhusa kusoma, kufurahia, na kutii Biblia nzima.

4:8 Zamani Wagalatia walitawaliwa na sanamu. Mbele ya kuokolewa kwao walikuwa wapagano walioabudu sana-mu za miti na mawe – **miungu** ya uwongo. Sasa waliingga utumwa namna nyingine – utumwa wa sheria.

4:9 Kwa sababu gani walifanya hivi? Walikuwa wamejua **Mungu**. Au hata kama hawakumjua sana, **walijuliwa** na Mungu, maana yake, walikuwa wameokolewa. Hata hivi sasa waliachana na uwezo na utajiri wake (walikuwa wariti wa utajiri huu). Waligeuka tena kwa **maneno ya uzaifu na umasikini** wa sheria, kama maagizo juu ya tohara, siku takatifu, na vyakula. Walijiingiza **katika utumwa** tena wa vitu visi-vyoweza kuwaokoa, wala kuwataji-riisha, lakini vilivyoweza kuwafanya masikini tu.

4:10, 11 Wagalatia walifuata kalenda ya Wayuda, na kushika siku za sabato,

na siku kubwa, **na nyakati**. Paulo alikuwa na woga kwa wale waliosema wao ni Wakristo, na hata hivi walijaribu kupendeza Mungu kwa njia ya kutii maagizo ya sheria. Hata wasioamini wanaweza kushika **siku na miezi na miaka**. Watu wengine wanafurahishwa sana wakifikiri wanaweza kufanya kitu wao wenyewe kitakachopendeza Mungu. Lakini kwa njia hii wanaonyesha kwamba kwa kipimo cha nguvu yao wenyewe hawahitaji Mwokozi.

Kama Paulo aliandika hivi kwa Wagalatia, angaliandika nini kwa Wakristo kwa wakati wa sasa wanaojaribu kujipatia utakatifu kwa njia ya kutii maagizo ya sheria? Angehukumu desturi za Wayuda walizoingiza ndani ya ukristo – kama makuhani wanaochaguliwa na watu, mavazi ya makuhani hawa yaliyo namna nyingine na yale ya watu wengine, kushika sabato, pahali patakatifu, tawafa, maji matakatifu, vivi hivi?

4:12 Ni kama Wagalatia walikuwa wamesahau asante ambayo walikuwa nayo rohoni wakati Paulo alipowahubiri Habari Njema mara ya kwanza. Lakini Paulo aliwaita **“ndugu”** hata kama walianguka, naye alikuwa na woga kwa sababu ya hali ya roho zao. Paulo alikuwa Myuda mbele, akitawaliwa na sheria. Sasa, ndani ya Kristo, alikuwa huru na hakutawaliwa na sheria tena. Hivi alisema, **“Muwe kama mimi – maana muwe huru toka utawala wa sheria.”** Wagalatia waliokuwa Mataifa hawakutawaliwa kamwe na sheria. Hivi mtume alisema: **“Mimi niligeuka kama ninyi.** Mimi, niliyekuwa Myuda, ninafurahishwa sasa na uhuru toka sheria ambayo ninyi Mataifa mulikuwa nao tangu zamani.”

Hamukunitendea mabaya yo yote. Si wazi kabisa kama Paulo alifikiri nini hapa. Labda alisema hakuumizwa rohoni kwa sababu ya namna walivymtendea. Walikuwa wameacha kumfuta, na walifuata walimu wa uwongo.

Neno hili halikumwumiza mwenyewe, lakini lilikuwa kama walipiga kweli ya Mungu, na hivi walijiumiza wao wenyewe.

4:13 Aliwhubiri Habari Njema kwanza ... kwa uzaifu wa mwili.⁵ Mara nyingi Mungu anatumika na watumishi zaifu, wazarauliwa, na masikini kutimiza kazi yake ili yeye mwenyewe atukuzwe, si watu.

4:14 Ugonjwa wa Paulo ulikuwa **jaribu** kwa yeye, na kwa watu amba walimsikiliza. Lakini Wagalatia hawakumkataa kwa sababu ya kuonekana kwa mwili wake au kwa sababu ya namna ya masemo yake. **Walimpokea kama malaika ya Mungu**, maana kama mjumbe aliyetumwa na Mungu, **kama Yesu Kristo** mwenyewe. Kwa sababu alikuwa mjumbe wa Bwana, walimpokea namna wangepokea Bwana (Matayo 10:40). Walipokea maneno yake kama maneno ya Mungu mwenyewe. Maneno haya ni maonyo kwa Wakristo **wote** wataantee wajumbe wa Mungu mema. Wakati tunapowapokea vizuri, tunapokea Bwana vivyo hivyo (Lk. 10:16).

4:15 Wakati waliposikia Habari Njema kwanza, walikiri kwamba ilikuwa **baraka** kubwa kwa roho zao. Walikuwa na asante sana hata wangalimpa Paulo **macho yao wenyewe**, kama ingaliwezekana. (Labda maneno haya yali-onyesha kwamba “mwiba mwilini” mwa Paulo ulikuwa ugonjwa wa macho.) Basi roho yao ya asante ilipotea wapi?

4:16 Nini iligeuza mafikiri yao juu ya Paulo? Hakugeuza habari alizohubiri mbele, lakini alikaa kusimamia **kweli** ya Habari Njema na nguvu. Kama neno hili lilimgeuza kuwa **adui** yao, walikuwa katika pahali pa hatari kabisa.

E. Utumwa au uhuru (4:17 – 5 :1)

4:17 Makusudi ya walimu wa uwongo yalikuwa namna nyingine na yale ya

Paulo. Walimu wa uwongo walitaka kupaata wafuata, lakini Paulo aliweka roho juu ya hali ya roho ya Wagalatia (4:17-20). Walimu wa uwongo walijaribu na bidii sana kupendana na Wagalatia, lakini si na roho ya kweli. **Wanataka kuwafunga ninyi inje**. Walimu Wayuda walitaka kutenga Wagalatia na mtume Paulo, na walimu wengine vilevile. Walitaka watu kuwa fuata, na hivi walijaribu kusimamisha jamii ya watu wenye dini.

4:18 Ni kama Paulo alisema, “Si neno kwangu kama watu wengine wakiwabembeleza ninyi, hata wakati mimi si pamoa nanyi, kama wakifanya hivi kwa neno **jema** na makusudi safi.”

4:19 Kwa njia ya kuita Wagalatia **watoto** wake **wadogo**, Paulo aliwakumbusha kwamba ni yeye ambaye aliwafikisha kwa Kristo. Alikuwa na maumivu ya kuzaa kwa sababu yao, si kwa kusudi waweze kuokolewa, lakini ili **Kristo** aweze **kuonekana ndani** yao. Mungu anataka sana kwa watu wake kufananishwa kuwa sawasawa na Kristo (Efe. 4:13; Kol. 1:28).

4:20 Labda maana ya shairi hili ni ya kwamba Paulo alifazaika juu ya hali ya roho ya Wagalatia. Alikuwa na **shaka** juu yao kwa sababu walikuwa wameacha kweli. Angetaka kuwa pale pamoa nao na kusemezana nao. Au labda alifazaika kama walifikiri nini juu ya barua yake. Angependa kusemezana nao uso kwa uso. Kama wakipokea maonyo yake vizuri, angesema nao na sauti ya upole. Lakini kama wakiwa na roho ya kiburi na uasi, angesema nao na ukali. Basi alikaa kufazaika kama watafikiri nini juu ya barua yake.

Walimu Wayuda waliheshimu Abrahamu sana, na walifundisha na bidii kwamba ilipasa waamini kumwiga kwa njia ya kutahiriwa. Halafu Paulo alianza kusema juu ya habari za nyumba ya Abrahamu kuonyesha kwamba kutawaliwa na sheria ni utumwa, na ya kwamba haiwezekani kuchanganya sheria na neema.

Mungu alikuwa ameahidi Abrahamu kwamba atakuwa na mwana, si neno kama umri yake na ya Sara ulipita ule ya wenyewe kuzaa watoto. Abrahamu aliamini Mungu na alihesabiwa haki (Mwa. 15:1-6). Nyuma ya muda fulani saburi ya Sara, aliyengoja mwana wa ahadi, ilipunguka na alisema na Abrahamu vizuri apate mtoto kwa njia ya mtumwa wa Sara, ndiye Hagari. Abrahamu alikubali, na Isimaeli alizaliwa. Huyu hakuwa mriti ambaye Mungu aliahidi, lakini mwana wa Abrahamu aliyezaliwa kwa sababu ya ukosefu wa saburi wa Abrahamu, tamaa ya mwili, na ukosefu wa imani (Mwa. 16).

Halafu, wakati Abrahamu alipokuwa na miaka 100, mtoto wa ahadi, Isaka, alizaliwa. Kuzaliwa kwake kulikuwa ajabu, na kuliwezekana kwa uwezo mkubwa wa Mungu tu (Mwa. 21:1-5). Kwa karamu ya kuachisha maziwa ya Isaka, Sara aliona Isimaeli akizihaki mwana wake. Halafu aliagiza Abrahamu kufkuza Isimaeli na mama yake toka nyumba yao, akisema, "Mwana wa kijakazi huyu hatariti pamoja na mwana wangu, hata na Isaka" (Mwa. 21:8-11). Hizi ndizo habari Paulo alizokumbuka wakati alipoendelea na mafundisho yake ndani ya mashairi yanayofuata.

4:21 Sheria ndani ya shairi hili ina maana mbili. Ya kwanza ni njia kwa watu kufikia utakatifu, na ya pili ni vitabu vya sheria katika Agano la Kale (Mwanzo kufika Torati), zaidi kitabu cha Mwanzo. Paulo alisema, "**Muniambie, ninyi munaotaka kupata ukubali** na Mungu kwa njia ya kushika sheria, **hamusikii** habari za kitabu cha **sheria?**"

4:22, 23 Wana wawili walikuwa Isimaeli na Isaka. **Kijakazi** alikuwa Hagari, na **yule aliyekuwa huru** alikuwa Sara. Isimaeli alizaliwa kwa sababu ya shauri la hila la Abrahamu. Lakini Abrahamu alipewa Isaka kwa sababu ya **ahadi** ya Mungu.

4:24 Wanawake wale wawili ni mifano ya maagano mawili: Hagari ni mifano wa agano la sheria, na Sara ni mifano wa neema. Maana ya "Hagari" kwa Kiarabu ni "Mwamba," na Waarabe wanaita Mlima Sinai "Mwamba."

4:25 Tunda la agano lililotolewa kwa Sinai lilikuwa utumwa; hivi **Hagari**, msichana mtumwa, alikuwa mifano mzuri wa sheria. **Hagari** ni mifano wa **Yerusalem**, mji mkuu wa taifa la Wayuda, pahali pa kusanyiko pa Waisraeli wote wasiookolewa bado na walioCAA kutafuta kujipatia haki kwa njia ya kushika sheria. Waisraeli hawa, **pamoja na watoto** wao, wafuata wao, ni katika utumwa. Hivi Paulo alifunga Waisraeli wasioamini pamoja na Hagari na Isimaeli, si na Sara na Isaka, ndilo semo kali.

4:26 Mji mkuu wa wale wanaohesabiwa haki kwa njia ya imani ni **Yerusalem** wa juu. Ni **mama** ya waamini wote, Wayuda na Mataifa.

4:27 Shairi hili ni sehemu ya Isaya 54:1 lililo unabii ya kwamba hesabu ya watoto katika mji wa juu itapita mbali hesabu ya wale katika Yerusalem duni-ani. Sara alikuwa mwanamke aliyekuwa **tasa** kwa muda mrefu. Hagari ndiye mwanamke **aliyekuwa na mume**. Kwa wakati wa kuja Sara, au Yerusalem ulio juu utashinda. **Watoto** wa ahadi ni Mataifa na Wayuda wote wanaofikia Mungu kwa imani. Hesabu yao **itapita mbali** hesabu ya watoto wa Hagari wanaobaki chini ya sheria.

4:28 Waamini wa kweli hawazaliwi kwa mapenzi ya mwili, wala kwa mapenzi ya mtu, lakini kwa Mungu. Neno kubwa si kama baba na mama ni nani, lakini ni kuzaliwa kwa njia ya ajabu na Mungu kwa njia ya imani ndani ya Bwana Yesu Kristo.

4:29 Isimaeli alizihaki Isaka, na ni desturi ya wale wanaozaliwa na mwili **kutesa** wale **wanaozaliwa kwa Roho**.

Waza juu ya mateso Bwana wetu na mtume Paulo waliyopokea toka wasioamini. Labda sisi tungefikiri ni neno dogo kwa Isimaeli kuzihaki Isaka, lakini habari hizi ziliandikwa ndani ya Mandiko Matakatifu, na Paulo aliona kwamba ni neno linaloendelea hata wakati sasa – uadui wa wale **wanaozaliwa kwa mwili** na wale wanaozaliwa **kwa Roho**.

4:30 Basi Wagalatia watafute **Mandiko**. Wataona kwamba haiwezekani kuchanganya sheria na neema. Haiwezekani kwa watu kuriti baraka za Mungu kwa njia ya matendo yao mema.

4:31 Wale wanaokwisha kuamini Kristo hawana mwunganisho wo wote na sheria kwa kupata kibali cha Mungu. Wao ni watoto wa mwanamke aliye huru (ndiye Sara), na wanafuata desturi za mama yao.

5:1 Shairi la mwisho la sura 4 linaonyesha hali ya mwamini – ye ye ni huru. Shairi la kwanza la sura 5 linaonyesha mwenendo wake – ingempasa kuishi kama mtu **huru**. Tunaona hapa tofauti kati ya sheria na neema. Sheria inasema: “Ukiweza kulipa bei gali sana kujipatia uhuru, utakuwa huru.” Lakini neema inasema: “Umewekwa huru kwa njia ya bei gali ya mauti ya Kristo.” Ikiwa hivi, Paulo anashauri: “**Kristo anatufanya huru kwa uhuru: basi, simameni, musiingie tena katika kongwa la utumwa!**” Sheria inatutolea magizo, lakini bila kutuletea uwezo kuyatii. Neema inaleta maneno yanayoagizwa na sheria, na inawezesha mtu kuyafanya kwa uwezo wa Roho Matakifu. Na halafu anampa zawabu kwa sababu ya kuyatii.

C. H. Mackintosh alisema, “Sheria inataka mwenye zaifu kuwa na nguvu, na inamlani kama hawezi kuonyesha nguvu ile. Neema inampa nguvu mtu asiye kuwa na nguvu, na anambariki kama akionyesha nguvu hii.”

3. PAULO ALISIMAMIA UHURU WA MKRISTO KATIKA ROHO (5:2 – 6:18)

A. Hatari ya sheria (5:2-15)

5:2 Utawala wa sheria (français: légalisme) unafanyiza Kristo kuwa bila faida. Wenye kushika dini ya Wayuda waliagiza kwamba ni lazima kwa waminni Mataifa **kutahiriwa** ili waokoewe. Paulo, akisema na amri ya mtume, alisema na nguvu kwamba kutegemea toharu kunafanyiza **Kristo** kuwa bila faida. Jack Hunter alisema:

Paulo, akifikiri juu ya Wagalatia, hakusema juu ya toharu kama kazi ya daktari (mganga) wala desturi ya dini. Kwa mafikiri yake toharu ilikuwa mfano wa utaratibu wa wokovu kwa njia ya matendo mema. Ilitangaza kwamba watu waliweza kupata wokovu kwa nguvu yao wenye we bila neema toka Mungu. Ilikuwa sheria ikitwaa pahali pa neema; Musa ikitwaa pahali pa Kristo; maana *kuongeza* kitu juu ya Kristo ni *kumpunguzia* kitu. Kristo ni Mwokozi wa pekee – hakuna mwingine. Toharu ingekuwa kukatwa mbali na Kristo.⁶

5:3 Utawala wa sheria unalazimisha watu **kutii sheria nzima**. Watu wanaotawaliwa na sheria hawawezi kuchagua maagizo fulani yaliyo mepesi kutii, na kukataa kutii mengine. Mtu akijaribu kuperendeza Mungu kwa njia ya kutahiriwa, ni **lazima kwake kutii sheria nzima**. Hivi au mtu anatawaliwa na sheria ndani ya maneno yote, au ye ye si chini ya utawala wa sheria hata kidogo. Ni wazi ya kwamba mtu akitawaliwa na sheria ndani ya maneno yote, Kristo hana faida kwake hata kidogo. Bwana Yesu si Mwokozi *mtimilifu tu*, lakini Mwokozi *wa pekee*. Ndani ya shairi hili Paulo hasemi juu ya watu waliothiriwa zamaani, lakini juu ya wale tu wanaofikiri ni

lazima kwao kutahiriwa kwa kuhesabiwa haki, na kushika maagizo yote mengine ya sheria kusudi waweze kukubaliwa na Mungu.

5:4 Maana ya kujiweka chini ya utawala wa sheria ni kukataa kuamini kwamba **Kristo** ni tumaini la pekee la mtu kuhesabiwa haki. Watu wametoa maelezo mbalimbali kwa shairi hili. Tunaweza kuyagawa kwa mafungu matatu:

1. Watu wengi wanafikiri Paulo alifundisha hapa ya kwamba inawezekana kwa mtu kuokolewa, kisha kuanguka na kufanya zambi, na kupotea kwa milele.

Elezo hili si jema. Kwanza shairi hili halisemi juu ya Mkristo akianguka na kufanya zambi. Linasema juu ya watu wenye kutembea kwa haki na kutenda mema, wanaotumaini kwamba wataokolewa kwa njia hii. Lakini shairi hili halifundishi kwamba matendo yao mema yanaweza kuwachunga wasifanye zambi na kupoteza uzima wao wa milele. Biblia inafundisha wazi ya kwamba wote wanaojaribu kuhakikishwa kwa njia ya kutii sheria na matendo yao mema **wameanguka na kutoka katika neema**.

Vilevile Agano Jipyä zima linafundisha wazi kabisa kwamba kila mwamini wa kweli ndani ya Bwana Yesu Kristo anaokolewa kwa milele. Hakuna kondoo ya Kristo atakayepotea kamwe. Wokovu unategemea kazi Mwokozi aliyotimiza, si kazi zaifu za watu (Yn. 3:16, 36; 5:24; 6:47; 10:28).

2. Watu wengine wanafikiri kwamba shairi hili ni juu ya wale waliookolewa kwa njia ya imani ndani ya Bwana Yesu, lakini nyuma walijitia chini ya sheria ili wasipoteze wokovu wao, au kwa kupata utakatifu. Ni kusema kwamba waliookolewa kwa neema, lakini sasa wanajaribu kulindwa katika utakatifu kwa njia ya kushika sheria. Ni kuanguka toka neema, kuacha njia ya Mungu kukamilisha watakatifu wake kwa njia ya kazi ya Roho ndani yao. Watu hawa wana-

jaribu kufanya hivi kwa njia ya kawaida za dini na ibada ambazo watu wa dunia wanaweza kufanya vilevile, si watakatifu wa Mungu tu.

Mawazo haya hayapatani na ma-fundisho ya Biblia, kwa sababu shairi hili si juu ya Wakristo wanaotafuta utakatifu, lakini ni juu ya watu wasiookolewa, wanaotafuta *kuheshabiwa haki* kwa njia ya kutii sheria. Ona maneno haya – **munaotaka kuheshabiwa haki kwa sheria**. Na vilevile elezo hili lingeonyesha kwamba inawezekana kwa waamini wa kweli kutengwa na Kristo nyuma. Mawazo haya hayapatani na neema ya Mungu.

3. Labda Paulo alikuwa akisema juu ya watu waliokiri kuwa Wakristo, lakini wasiookolewa kweli. Wanajaribu kuheshabiwa haki kwa njia ya kushika sheria. Mtume alijaambia kwamba hawawezi kuwa na waokozi wawili; sharti wachague au Kristo au sheria. Kama wakichagua sheria, wanatengwa na Kristo, aliye tumaini la pekee la kuwa haki; **wameanguka na kutoka neema**. Neno hili linaleezwa wazi na Hogg na Vine:

Kristo ni mambo yote kwa mtu, au ye ye si kitu kwake. Haiwezekani kumheshimu kwa sehemu tu. Mtu anayehesabiwa haki kwa neema ya Bwana Yesu Kristo ni Mkristo; mtu anayejaribu kuheshabiwa haki kwa njia ya matendo ya sheria si Mkristo.

5:5 Mtume alionyesha kwamba tumaini la mwamini wa kweli ni namna nyingine kabisa na lile la mwenye kushika sheria. Mkristo wa kweli anangojea **tumaini la haki**. Anatumainia saa wakati Bwana atakapokuja, wakati atakapopokea mwili wa utukufu, na wakati asipotenda zambi tena. Ona ya kuwa hatusomi kwamba Mkristo anatumaini kupata haki; anakwisha kusimama na haki mbele ya Mungu katika Bwana Yesu Kristo (2 Kor. 5:21). Lakini ana-

ngojea dakika ile wakati atakapokuwa haki kabisa yeze mwenyewe. Hatumaini kwa neno hili kufanyikana kwa njia ya kazi yo yote anayoweza kufanya yeze mwenyewe, lakini kwa **njia ya Roho** na **kwa imani**. Roho Mtakatifu atatimiza kazi hii nzima, na mwamini anatazamia Mungu na imani ili ifanyikane. Lakini mwenye kushika sheria anatumaini kupata haki kwa njia ya kazi zake mwenyewe, kushika sheria, au kawaida ya dini. Ni tumaini bure, kwa sababu haiwezekani kupata haki kwa njia hii.

Ona ya kwamba Paulo alisema **sisi** ndani ya shairi hili, akisema juu Wakristo wa kweli; lakini ndani ya shairi 4 alisema **ninyi** wakati aliposema na watu wale ambao walijaribu kuhesabiwa haki kwa njia ya kazi ya sheria.

5:6 Kushika sheria **haifai** neno. Kwa mtu aliye **katika Kristo**, ndiye Mkristo, **tohara** haimfanyizi kuwa mtu mwema kupita, na **kutokutahiriwa** hakumfanyizi mbaya kupita. Neno Mungu analotaka kuona ndani ya mwamini ni **iman** inayotenda kazi **kwa mapendo**. **Imani** inategemea Mungu kabisa ndani ya maneno yote. **Imani** haikai bure; inaonekana kwa njia ya kutumikia Mungu na watu bila kujifikiri yenye. Kusudi la utumishi namna hii ni **mapendo**. Hivi **imani** inatumika kwa **mapendo**; inasukumwa na **mapendo**, si na sheria. Tunaona kweli hii mara nyingi ndani ya Mwandiko Matakatifu – ya kwamba Mungu haweki roho juu ya kawaida za dini, lakini juu ya maisha ambayo yanamtukuza.

5:7 Kutawaliwa na sheria (légalisme) ni kutokutii **kweli** ya Mungu. Wagalatia walikuwa wameanza kutembea vizuri katika imani, lakini **walizuiwza** na wahubiri wa dini ya Wayuda, ndio mitume ya uwongo, wale ambao waliwfundisha utawala wa sheria. Kwa njia ya kukubali mafundisho yao ya uwongo Wakristo waliasi **kweli** ya Mungu.

5:8 Utawala wa sheria si elimu ya

Mungu. Maana ya **kushawishi** hapa ni elimu. **Yeye ambaye aliwaita ninyi** ndiye Mungu. Hivi mafundisho kwamba inapasa kuongeza tohara na kushika sheria juu ya imani kwa Kristo hayatoki kwa Mungu, lakini kwa Shetani.

5:9 Utawala wa sheria unaingiza watu ndani ya mabaya mengine vilevile. Mara nyingi **chachu** ndani ya Biblia ni mfano wa uovu. Hapa inasema juu ya mafundisho mabaya ya walimu wa dini ya Wayuda. Ni desturi ya **chachu** kugusa kila kitu ambacho kinakutana nacho. Hapa inaonyesha kwamba mafundisho yao mabaya yatakaa kuongezeka kila mara. Uovu unageuka na kuongeza wongo nyingine. Watu wachache ndani ya kanisa wakifungana na mafundisho ya uwongo, watapata wafuata wengi wengine, kama neno hili halihukumiwi na ukali mara moja.

5:10 Walimu wa sheria watahukumiwa. Paulo aliamini kabisa kwamba Wagalatia watakataa mafundisho yao mabaya. Alikuwa na **matumaini katika Bwana**, maana akijuana sana na Bwana, aliamini kabisa kwamba Mchungaji Mkubwa atarudisha kondoo zake walikuwa wamekwenda mbali, labda hata kwa njia ya barua hii ambayo Paulo aliwaandikia.

Na walimu wale wa uwongo wataazibowiwa na Mungu. Ni vibaya sana kutoa mafundisho ya uwongo na kwa njia ile kuharibu kanisa (1 Kor. 3:17). Kwa mfano, ni vibaya kufundisha kwamba kulewa kunakubaliwa, kupita kuwa mlevi wewe mwenyewe, kwani mwalimu wa uwongo anageuza watu wengi wengine kufanana na yeze mwenyewe.

5:11 Utawala wa sheria unaondosha **kwazo la msalaba**. Paulo alijibu sasa mashitaki mapumbavu ya wengine kwamba mara nyingine alifundisha yeze mwenyewe ya kuwa tohara ilihitajiwa. Hata kwa wakati ule alikuwa **akiteswa** na Wayuda. Wangaliacha **kumtesa** mara moja kama angalihubiri **tohara** ni neno

la lazima, kwani kwa njia ile angaliacha kuhubiri habari za msalaba wa Kristo. Msalaba ni **chuki** kwa watu. Wanau-chukia kwa sababu unawajulisha kwa-mba hawawezi kufanya kazi hata moja kujipatia wokovu. Kama Paulo akianza kuhubiri kwamba kazi njema zinahita-jienda, kwa njia ya kufundisha ni lazima kutahiriwa, kama angeonyesha ya kuwa msalaba usipokuwa na maana hata ki-dogo.

5:12 Labda Paulo alitaka wale ambao waliwasumbua ... **wangejikata nafsi zao**. Walikuwa na bidii kutumika na kisu kutahiri watu wengine; basi sasa kisu kitumiwe kuwafanyiza wenyewe matowashi. Masemo haya ni mfano wa kutaka kwa Paulo kwa walimu hawa wa uwongo “kujikata nafsi zao,” maana kuondoshwa kabisa karibu na Wagala-tia.

Tangu zamani watu wanasema Habari Njema ya neema inaruhusu watu kufanya neno lo lote wanilotaka. Wanasema: “Kama wokovu ukipatikana kwa njia ya imani peke yake, hakuna njia kutawala na kuongoza matendo ya watu.” Lakini mtume alionyesha mara moja ya kwamba uhuru wa Mkristo haumpi ruhusa kufanya zambi. Maisha ya Bwana Yesu ni mfano kwa mwamini, na mapendo yake kwa Kristo inamsukuma kuchukia zambi na kupenda utakatifu.

Labda Paulo alihitaji kuonya wasomaji wake juu ya uhuru wao saa hii. Wakati watu walipotawaliwa na sheria kwa muda mrefu, na halafu wanapewa uhuru, ni hatari wageuke kabisa na kuanza kufanya maneno yasiyofaa. Sharti wafahamu kwamba Mkristo si chini ya sheria tena, lakini hata hivi inampasa kutii maagizo ya Bwana.

5:13 Uhuru wa Wakristo hauwaruhusu kufanya zambi, lakini unawsukuma kutumikia Bwana na mapendo. Kusudi la matendo yote ya Wakristo ndilo **mapendo**, lakini woga wa azabu

ni kusudi la wote walio chini ya sheria.

Uhuru wa Mkristo ni *katika Kristo Yesu* (2:4), na kwa sababu hii si uhuru kamwe kufanya zambi.

5:14 Ni ajabu kuona Paulo akisema juu ya **sheria** tena, kwani ndani ya barua hii nzima alifundisha kwamba waamini si chini ya sheria. Hakusukuma wasomaji kurudi kwa sheria; alionyesha tu kwamba neno sheria ililotaka hali-kuweza kutimiza ndani ya watu. Linawezekana kwa njia ya uhuru wa Wakristo tu.

5:15 Mara nyingi watu walio chini ya sheria wanaanza kugombana. Ni kama hili ndilo neno lililotokea katika Galatia. Ni neno la kutushangaza. Watu hawa walitaka kuwa chini ya sheria. Sheria iliwa-agiza kupenda majirani yao. Lakini waliumana na kuangamizana. Sheria ina-acha tabia ya zambi kutenda namna hii.

B. Uwezo kwa maisha matakifu

(5:16-25)

5:16 Ingepasa mwamini **kwenda kwa Roho**, si katika tamaa ya mwili. **Kwenda kwa Roho** ni kuacha Roho kufanya mapenzi yake. Ni kwa mwamini kuwa na upatano wa karibu naye. Ni kukumbuka utakatifu wake wakati inapotupasa kuchagua kama tutafanya nini. Ni kukaa kuwaza juu ya Kristo, kwa sababu ni kazi ya Roho kutia mawazo yetu juu ya Bwana Yesu. **Tukitembea hivi kwa Roho**, ni kama **tabia yetu** ya zambi imekufa. Hainezekani kwa sisi kutembea pamoja na Kristo na katika zambi vilevile.

Shairi hili na yale yanayofuata yanonyesha kwamba Mkristo angali na **tabia ya zambi**. Watu wengine wanafikiri tabia ya zambi imeondoshwa ndani ya Mkristo, lakini neno hili si kweli hata kidogo.

5:17 Roho anashindana na **mwili** wakati wote. Mungu angaliweza kuondosha tabia ya zambi toka waamini saa walipopokea Mwokozi, lakini haku-

fanya hivi. Kwa nini? Alitaka kukaa kuwakumbusha uzaifu wao, waweze kukaa kutegemea Kristo, Kuhani na Mwombezi wao; na waweze kusifu bila kuacha Yule ambaye aliokoa watu waovu kama wao. Kwa pahali pa kuongosha tabia ya zamani, Mungu alitupa sisi Roho Mtakatifu yake mwenyewe kukaa ndani yetu. Roho ya Mungu na tabia yetu ya zambi wanashindana wakati wote, na watakaa kufanya hivi kufika wakati tutakapopelekwa mbinguni. Ndani ya vita hii inapasa mwanmini kunyenyeka Roho.

5:18 Wale wanaoongozwa na Roho **si chini ya sheria**. Inaweza kueleza shairi hili kwa njia mbili: Wakristo wote **wanaongozwa na Roho**. Hivi Wakristo hawatawaliwa na sheria; hawategemei kazi yao wenyewe. Ni **Roho** anayeshindana na hamu ya kutenda zambi ndani ya roho zao, si wao wenyewe. Vilevile **kuongozwa na Roho** ni kuacha kufikiri juu ya sheria na tabia ya zambi, na kuwaza juu ya Bwana. Mtu anayewaza juu ya Bwana, hafikiri juu ya sheria au tabia ya zambi. Roho ya Mungu haongozi watu kutazamia sheria kwa kuhesabiwa haki. Anawaongoza kutazama Kristo mfufuliwa tu. Ni kwa njia yake tu tunaweza kukubaliwa na Mungu.

5:19-21 Tulisema mbele kwamba watu wanapenda kutii sheria na nguvu yao wenyewe. Wenye nia ya zambi wanafanya kazi gani? Si nguvu kutambua **matendo ya mwili**. Yanaonekana **wazi** kwa watu wote. **Uasherati** ni kufanya zambi na mtu asiye au mke au bwana wa mtu. **Uchafu** ni uovu wa roho na tamaa za mwili. **Uzini** ni zambi namna moja na uasherati, ndio tendo la mume na mke, kijana na msichana, isiyehalali. **Kuabudu sanamu** ni pamoja na uovu wa kuabudu pepo wachafu. **Ulozi** ni uchawi. **Uadui** ni kuwa na nia ya kuzuru mtu mwengine. **Ugomvi** ni kutokupatana. **Uwivu** ni kutamani, mali au

hali ya mwengine. **Hasira** ni gazabu ya kuwaka. **Fitina** ni kutokubaliana. **Farakka** ni mabishano na ugomvi. **Uzushi** ni elimu ya uwongo. **Husuda** ni vivu juu ya kusitawi kwa watu wengine. **Uuaji** ni kuua watu wengine isiyo halali. **Ulevi na ulafi** ni kuonyesha watu wanaokusanya kunywa pombe kupita kipimo.

Paulo alikumbusha wasomaji wake kwamba aliaonya mbele **ya kuwa watu wanaotenda maneno ya namna hii hawatariti ufalme wa Mungu**. Shairi hili halifundishi kwamba mlevi hawezi kuokolewa, lakini kwamba wale *wenye desturi* ya kutenda matendo ya tabia ya zamani hawakuokolewa.

Kwa sababu gani Paulo aliandika maneno haya kwa makanisa ya Wakristo? Kwa sababu si wote wanaokiri kwamba walikuwa wameokolewa ni watoto wa kweli wa Mungu. Tena na tena ndani ya Agano Jipyia Roho Mtakatifu anatoa maonyo ya nguvu sana nyuma ya kutoa mafundisho ya kweli za ajabu za roho kwa wote wanaokiri kuwa Wakristo.

5:22, 23 Ona ya kwamba Paulo alionyesha kwamba *kazi za mwili* ni namna nyingine na **matunda ya Roho**. Watu wanafanya kazi kwa nguvu ya mwili. **Matunda** yanaota wakati tawi linapokaa ndani ya mzabibu (Yn. 15:5). Ona ya kwamba **tunda** la Roho ni namna moja, ndilo kufanana na Kristo. Njema zote zinazotajwa hapa zinaonyesha namna ya maisha ya mtoto wa Mungu. Dr. C.I. Scofield ameonyesha kwamba hata moja ya njema hizi haioti ndani ya moyo wa mtu.

Mungu ni **mapendo**, na ingetupasa sisi kuwa mapendo vilevile. 1 Wakorinto 13 ni sura tamu sana inayoonyesha kutilmia kwa mapendo kwa msalaba wa Kalvari. **Tunafurahia** Mungu na maneno yote anayofanya. Kristo alionyesha furaha hii ndani ya Yoane 4:34. Tunaweza kuwa na **salama** na Mungu, na

kukaa na salama na Wakristo wenzetu. Ona salama ndani ya maisha ya Mkombozi kwa Luka 8:22-25. **Uvumilivu** ni saburi wakati wa mateso, machukizo na taabu. Ona mfano mkamilifu wa uvumilivu katika Luka 23:34. Mfano wa **wema** ndio upole wa Bwana Yesu kwa watoto (Mk. 10:14). Tunaonyesha **wema** na watu. Kwa mfano wa wema huu, ona Luka 10:30-35. Labda **uaminiifu** ni kutegemea Mungu, au kuwa na imani kwa mwenzetu. Lakini tunawaza ya kwamba maana yake ni uaminifu na utawa wetu ili kustahili kutegemewa. **Upole** ni kujinyenyekiza kama Yesu alivyofanya wakati aliponawa miguu ya wanafunzi wake (Yn. 13:1-17). **Ujizuiza** ni kujitawala mwenyewe, zaidi tamaa ya mwili na hasira yetu.

Paulo alimaliza maneno haya na kusema: “**Hakuna sheria juu ya maneno ya namna hii.**” Kabisa! Njema hizi zote zinapendeza Mungu, zinasaidia watu wengine, na hata sisi wenyewe. Lakini zinazaliwa namna gani? Ni kwa njia ya kazi ya watu? Sivyo, hata kidogo. Zinazaliwa wakati Wakristo wanapoishi na upatano wa karibu na Bwana. Wakati wanapokaa kumtazama, na kumwabudu, na kumtii ndani ya maisha yao ya kila siku, Roho Mtakatifu anafanya ajabu ndani yao. Anawageuza kufanana na Kristo. Kwa njia ya kumtazama wanageuzwa kufanana naye (2 Kor. 3:18). Kama tawi linavyopata uzima na chakula toka mzabibu, vivyo hivyo Mkristo anapata nguvu toka Mzabibu wa kweli, na anaweza kuzaa matunda kwa Mungu ndani ya maisha yake.

5:24 Nao walio watu wa Kristo wamesulibisha mwili. Ni neno lililoteka wakati tulipookolewa. Wakati tulipotubu, ni kama tulifunga tabia yetu ovu ya zamani na ya kuoza kwa msalaba, pamoja na mawazo mabaya na tamaa mbaya. Tulyakinisha ya kwamba hatu-

tapendeza tabia yetu ya zambi tena, na hatutaiacha kututawala. Ndiyo, inatupasa kufanya shauri hili tena na tena ndani ya maisha yetu. Ni lazima kwetu kuchunga tabia ya zambi kwa pahali pa mauti.

5:25 Tukiwa na uzima wa milele kwa sababu ya kazi ya **Roho** Mtakatifu ndani yetu, tuishi uzima huu mpya kwa uwezo wa **Roho** Mtakatifu **yule**. Watu hawa-kuweza kupokea uzima kamwe kwa njia ya sheria. Haikusudi kamwe kuwa kawaida kwa maisha ya Mkristo.

C. Maonyo ya kufaa (5:26 – 6:10)

5:26 Ndani ya shairi hili tunasoma juu ya maneno matatu ambayo inatupasa kuepuka:

1. Kiburi – **Tusijisifu bure**, maana tusifikiri kwamba tuko watu wazuri kupita kipimo. Mungu hataki Wakristo waliookolewa kwa neema kuwa wenye kujivuna na kujisifu. Mara nyingi watu wale wanaoishi chini ya sheria wanajivuna juu ya akili yao, na wanahafifisha wenye akili ndogo kuliko yao. Na mara nyingi Wakristo wanaoshika sheria sana wanazarau Wakristo wengine wasiokataa kufanya maneno yote ambayo wenye kiburi hawa wanalaumu.

2. Kuchokozana – **tukichokozana**. Hafifai kwa mtu anayejaa Roho kuchokoza au kusukuma mtu mwingine kupatana naye ndani ya maneno na matendo yake yote. Hawezi kujuua kama mtu yule mwingine anashindana na masumbuko na majaribu gani rohoni mwake.

3. Tamaa – **tukitamanana**. Tamaa ni zambi ya kutaka kitu kilicho mali ya mtu mwingine. Ni kuwa na wivu juu ya mtu mwingine mwenye uso wa kuonekana vizuri zaidi, na mwenye mali nyingi, na anayebarikiwa sana ndani ya kazi yake. Tamaa namna hii haipatani na neema. Ingepasa mwamini wa kweli kuhesabu wengine kuwa wazuri kupita yeze mwenyewe. Wenye kushika sheria wanajitafutia utukufu usio utukufu wa

kweli. Utumishi wa wenyewe ukubwa wa kweli hauonekani kwa watu.

6:1 Shairi hili tamu linaonyesha namna gani inapasa Wakristo kutendea mwamini aliyeanguka. Ni namna nyininge kabisa ya namna waliokuwa chini ya sheria wangalimhukumu na ukali. Hapa mtu **akipatwa katika kosa lo lote** ni mtu aliyetenda zambi moja, si mtu anayefanya zambi saa zote. Inapasa watu wa upole kusaidia mtu huyu. Mkristo mwenye roho ya nguvu asiyetembea karibu na Bwana angweza kuumiza hata kupita yule aliyeanguka. Na vile mtu aliyeanguka asingalikubali maonyo ya mtu asiyetembea karibu na Bwana yeye mwenyewe.

Tungeweza kuuliza kama mtu anayetembea karibu sana na Bwana yeye mwenyewe angekubali kwamba anaongozwa na Roho? Ni kama watu wenyewe kutembea kwa Roho wanafahamu uzaifu wao zaidi. Basi nani atakayefanya kazi ya kurudisha wenyewe kuanguka bila kuonyesha kwamba yeye mwenyewe ni mtu anayeongozwa kwa Roho? Jibu la ulizo hili ndilo hili: Mtu anayetembea kwa Roho kwelikweli hatajisifu juu ya hali yake, lakini atakuwa na roho ya upole ya mchungaji anayetaka kurudisha mwenye kuanguka. Hatafanya hivi na roho ya kiburi au ukubwa, lakini na **roho ya upole**, akikumbuka kwamba ingewezekana kwa yeye mwenyewe **kujaribiwa vile-vile**.

6:2 Mizigo ndiyo kushindwa na maneno magumu, majaribu, mapimo, na taabu. Kwa pahali pa kusimama mbali na kulaumu ndugu anayetaabishwa, inatupasa kufika karibu naye na kumsaidia kwa kila njia tunayoweza.

Sheria ya Kristo ndiyo maagizo yote ya Bwana Yesu kwa watu wake ndani ya Agano Jipy. Tunaweza kuyajumlisha na amri moja, "mupendane" (Yn. 13:34; 15:12). Tunafanya hivi wakati **tunapo-chukuliana mizigo yetu**. Sheria ya

Kristo ni namna nyininge na sheria ya Musa. Sheria ya Musa iliahidi kuleta uzima kwa wale ambao wanaitii, lakini haikuwapa uwezo kuitii. Iliweza kuwasukuma tu kuitii kwa sababu ya kuogopa azabu. Lakini **sheria ya Kristo** ndiyo mafundisho ya mapendo kwa wale waliokwisha kupata uzima. Waamini wanawezeshwa kutii maagizo yake kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Mapendo yao kwa Kristo yanawasukuma kufanya hivi.

6:3 Sisi sote tumefanywa toka uvumbi tu. Wakati tunapoona ndugu Mkristo akifanya zambi, inatupasa kukumbuka kwamba tungeweza kufanya vivyo hivyo. Mkristo anayefikiri yeye ni mwema zaidi anajidanganya mwenyewe. Haifai kwetu kamwe kuwaza ya kwamba tuko watu wakubwa zaidi tusioweza kubeba mizigo ya watu wengine.

6:4 Ni kama shairi hili linatuonya kuepuka desturi ya kujifurahisha kwa njia ya kujisawanisha wenyewe na watu wengine. Paulo alionyesha kwamba sisi sote, mmoja mmoja, tutahukumiwa kwa kiti cha hukumu cha Kristo, bila kusawnishwa na watu wengine. Hivi inatupasa kupima kazi yetu, ili tuweze kuwa na sababu kufurahia **kazi yetu**, si kwa sababu ya kuanguka kwa watu *wengine*.

6:5 Ndani ya shairi 2, Paulo alifundisha kwamba ingetupasa kushiriki ndani ya huzuni, mateso, na mapimo yetu ya sasa. Ndani ya shairi 5 tunaona kwamba sisi sote, mmoja mmoja, tutalazimishwa **kuchukua mizigo wake mwenyewe** kwa Kiti cha Hukumu cha Kristo.

6:6 Inapasa waamini kusaidia walimu wao Wakristo na mahitaji yao. **Kushiriki ndani ya maneno yaliyo mema ni kushiriki nao vitu** wanavyohitaji kwa maisha yao ya kila siku, na vilevile kukumbuka mahitaji yao ya roho, na kuwaombea.

6:7 Labda watu hawaoni ya kwamba

hatusaidii watumishi wa Mungu namna inavyofaa, lakini Mungu anaona na atatoa mavuno yanayofaa. **Tunavuna** yo yote tunayopanda, lakini tunavuna kupita mbegu tuliyopanda. Wakati mlimaji **anapopanda** ngano, atavuna ngano kupita ngano aliyopanda, mara nyiningine kupita mara makumi tatu, mara makumi sita, au hata mara mia moja. Scofield anasema kwamba “Roho hasemi hapa kwa wenyewe zambi juu ya zambi zao, lakini kwa waamini juu ya choyo yao.”

Habari hizi ni kweli vilevile kwa “wale “wanaolima uovu na kupanda mabaya, wanavuna maneno yale yale” (Yobu 4:8), na wale wanaopanda upepo ... watavuna tufani” (Hos. 8:7). J. A. Froude, mwandishi wa historia, alisema ya kwamba kuna neno moja tu linaloonekana wazi tena na tena, ndilo hili: ulimwengu huu unasimamishwa juu ya misingi mema, na mwishoni, watu wema watapata mema, lakini waovu watapata taabu.

6:8 Ni kweli ya kwamba tunavuna namna ya matunda tuliyopanda, lakini tukumbuke vilevile kwamba habari hizi zinafuata maonyo kwa Wakristo juu ya kutoa. Tunaona ya kwamba maana ya kupanda **kwa mwili** ni kwa mtu kutumika na mali yake kwa faida yake na kwa kuipendeza mwenyewe. Kupanda **kwa Roho** ni kwa mtu kutumika na mali yake kazi ya Mungu.

Mavuno ya wale wanaopanda kwa mwili ni uchungu na hasara hapa duniani. Wakati wanapogeu ka wazee, wanaona kwamba mwili wao ambao waliishi kubembeleza na kufurahisha unapooza na kufa. Halafu kwa muda wa kuja watapoteza zawabu zao za milele. Wale wanaopanda **kwa Roho, kwa Roho watavuna uzima wa milele**. Tunasoma juu ya uzima wa milele kwa njia mbili ndani ya Biblia: (1) Kila mwamini ana uzima wa milele wakati yeye ni kwanza hapa duniani (Yn. 3:36). (2) Halafu kwa

mwisho wa uzima wake hapa duniani anapata uzima wa milele (Rom. 6:22). Mtu **anayepanda kwa Roho** anafurahi na uzima wa milele hapa duniani kupita waamini wengine. Na atavuna zawabu kwa utumishi wake mwaminifu wakati atakafokia kao lake la milele.

6:9 Paulo hakutaka wasomaji wake kushushwa moyo, hivi aliwakumbusha kwamba labda hawatapokea zawabu mara moja, lakini bila shaka watazipokea kwa wakati wa kuja. Hupati mavuno toka shamba la ngano siku moja nyuma ya kupanda mbegu. Ni vivyo hivyo kwa maneno ya roho. Bila shaka kutakuwa na zawabu **kwa wakati wake** kama tukipanda mbegu na uaminifu.

6:10 Walio wa **nyumba ya imani** ni wote waliokwisha kuokolewa, si neno kama ni watu wa kanisa gani. Kupita ile inatupasa kutenda mema kwa watu wote, si kwa waamini tu, lakini zaidi kwa waamini. John Wesley alisema kwa ufupi: “Tenda mema yote unayoweza, kwa njia yo yote unayoweza, kwa watu wote unaoweza, na kwa muda yo yote unayoweza.”

D. Mwisho (6:11-18)

6:11 Tazameni, kwa herufi kubwa gani nimewaandikia ninyi kwa mkono wangu mwenyewe! Hakuagiza msaidia wake kuandika, kama ilivyokuwa desturi yake, lakini aliandika barua hii yeye mwenyewe. Labda **herufi kubwa** zinaonyesha mzigo mzito rohoni mwake wakati aliposhindana na walimu wa sheria, na ya kwamba alifikiri mafundisho yao yalikuwa hatari kubwa sana. Watu wengine wanafikiri ya kwamba shairi hili, na mashairi mengine yanaonyesha kwamba uwezo wake wa kuona na macho ulipunguka. Tunafikiri kwamba hili ndilo tafsiri la haki.

6:12 Walimu Wayuda walitaka **ku-onekana kuwa wazuri kwa mwili** kwa njia ya kuongeza hesabu ya wafuata wao. Waliweza kufanya hivi kwa njia ya

kulazimisha watu kutahiriwa. Mara nyingi watu ni tayari kutii kawaida ya dini kama hawalazimishwi kugeuza desturi zao. Kwa wakati wa sasa makanisa mengi yana washiriki wengi kwa sababu wanapungusa kipeo cha kawaida yao. Paulo alitambua hila ya walimu hawa wa uwongo, na aliwashitaki akisema walikuwa wakijaribu kuepuka **mateso kwa ajili ya msalaba wa Kristo**. Msalaba unaonyesha kwamba tabia ya zambi inayojaribu sana kupendeza Mungu imehukumiwa. Msalaba ni kifu kwa tabia ya mwili na bidii zake bora. Msalaba ni kutengwa na uovu. Kwa sababu hii, watu wanachukia habari za utukufu wa msalaba, na wanatesa watu wale ambaio wanazihubiri.

6:13 Walimu wa sheria hawakuweka roho zaidi juu ya kushika **sheria**. Neno walilotaka lilikuwa njia nyepesi kupata wafuata wengi ili waweze **kujisifu** juu yao.

6:14 Paulo hakujisifu juu ya miili ya watu, lakini **juu ya msalaba wa Bwana Yesu Kristo**. Juu ya **msalaba** huu dunia ilikufa kwa Paulo, na Paulo kwa dunia. Wakati mtu anapookolewa, dunia inagana naye, naye anaagana na **dunia**. Hafurahishwi tena na maneno ambayo yalimpendeza mbele, kwa sababu anakwisha kukutana na Mmoja ambaye anashibisha mahitaji yote ya roho yake kabisa. Hivi **msalaba** ni kizuizo kikubwa kinachotenga dunia na mtoto wa Mungu.

6:15 Hata kama haionekani wazi kwanza, shairi hili ni semo moja kubwa zaidi ya kweli ya Kikristo katika barua hii nzima.

Tohara ilikuwa kawaida ambayo watu waliweza kuona na macho. Walimu Wayuda waliweka roho sana juu yake. Ilikuwa msingi wa dini yao. Lakini Paulo alisema “**kutahiriwa** si kitu.” Na dini ya Wayuda na kawaida yake si kitu. Halafu Paulo aliongeza –

wala kutokutahiriwa. Watu wengine wanajisifu kwa sababu hawashiki desturi za dini. Lakini neno hili halina faida vilevile.

Neno lililo na faida ya kweli kwa macho ya Mungu ni **kiumbé kipyá**. Anataka maisha ya watu kugeuka. Findlay anasema: “Ukristo wa kweli una-geuza watu wabaya kuwa watu wazuri, na watumwa wa zambi kuwa wana wa Mungu.” Watu wote wanazaliwa duni-ani kama wenye zambi, wasioweza ku-jisaidia, na wanaohukumiwa. Maneno yote wanayofanya kujiokoa, au kusaidia Mungu kuwaokoa kwa njia ya mwe-nendo au kazi njema, ni bure, na hayawageuzi. **Kiumbe kipyá** kinaongozwa na Kristo mfufuliwa. Ni wote wanaokwisha kuokolewa na kupewa uzima mpya ndani ya Kristo. Maisha yao yanageuzwa kuwa maisha ya utukufu, si kwa njia ya kushika kawaida ya dini, lakini kwa njia ya kujitoa mzima kwa Kristo, na kumwacha ye ye kuishi uzima wake ndani yao. **Kiumbe kipyá** si kiumbe cha mbele kilichogezuwa kuwa kizuri kupita, wala kuongezewa kitu. Ni kiumbe namna kingine kabisa.

6:16 Paulo alisema juu ya **amri** gani hapa? Ni **amri** ya kiumbe kipyá. Ali-tangaza baraka ya **salama na rehema** kwa wote wanaopima mafundisho ya walimu na ulizo hili – “Haya ni ma-fundisho ya kiumbe kipyá?” – na wa-naokataa mafundisho yote mengine.

Na kwa Israeli wa Mungu. Watu wengi wamefikiri Israeli wa Mungu ni kanisa. Lakini **Israeli wa Mungu** ndio wote waliozaliwa Wayuda, na wanaopkea Bwana Yesu kama Masiya. Ha-kuna salama wala rehema kwa watu wanaotembea chini ya sheria, lakini wote walio ndani ya kiumbe kipyá wanabarikiwa na maneno haya mawili.

6:17 Paulo, aliyejikuwa mtumwa wa sheria mbele, alikuwa amefunguliwa toka utumwa huu na Bwana Yesu. Sasa

alikuwa mali ya Bwana, na alikuwa tayari kuwa mtumwa wake. Ilikuwa desturi kwa watumwa kuwekewa chapa kwa mwili wao na chuma chenye moto ya alama ya bwana wao. Vivyo hivyo Paulo alikuwa katika **mwili wake chapa** zilizoonesha kwamba alikuwa **mali ya Bwana Yesu**. Chapa hizi zilikuwa nini? Zilikuwa alama za vidonda alivyopokea kwa mikono ya watesaji wake. Sasa alisema: "Mtu asijaribu kuniondosha karibu na Bwana wangu mpya. Musiseeme nami juu ya tohara iliyo alama ya utumwa wa sheria. Mimi nina chapa ya Bwana wangu mpya, ndiye Yesu Kristo."

6:18 Halafu mtume alikuwa karibu kuweka kalamu yake chini. Lakini sharti aandike neno moja lingine kwanza kumaliza barua hii. Lilikuwa nini? **NEEMA** – neno linaloonekana sana ndani ya Habari Njema yake. **Neema**, si sheria. Alianza barua yake na kusema juu ya neema (1:3); na sasa ni neno lake la mwisho. **Neema ya Bwana wetu Yesu Kristo iwe pamoja na roho zenu. Amina.**

MAFUNDISHO JUU YA SHERIA

Nyuma ya kumaliza kusoma mafundisho haya kwa Wagalatia, tungeweza kufikiri kwamba Paulo alikuwa ameshinda mafundisho mabaya ya walimu wa sheria kabisa. Tungefikiri maneno haya hayatasumbusha kanisa tena kamwe. Lakini historia inaonyesha kwamba neno hili si kweli. Mafundisho ya sheria yameongezeka sana hata watu wengi wanaamini ni sehemu ya ukristo.

Ndiyo, walimu wa sheria wangali katikati yetu. Wanajiita watumishi wa Kristo na wanafundisha kwamba ni lazima kwa Wakristo kubatizwa, na kupokewa ndani ya kanisa kwa kupata wokovu. Wanafundisha kwamba inapasa mwamini kutii sheria, na ya kwamba tunaokolewa kwa imani, lakini tunalindwa kwa njia ya kufanya ma-

tendo ya sheria. Wanaingiza desturi za Wayuda ndani ya Ukristo, kama ukuhani unaochaguliwa na watu, na kuvikwa na mavazi yao. Namna ya nyumba zao za kuabudu zinafanana na hekalu la Wayuda na mazabahu zake, kawaida yao ya kuabudu, karamu zao, na kutockula kwao.

Mafundisho ya uwongo ya Wagalatia yanaonya waamini kwamba lazima washike siku ya sabato ili waokolewe. Kwa wakati wa sasa hesabu ya wahubiri wa sheria inaongezeka sana katikati ya watu wanaokiri kuwa Wakristo, hivi lazima waamini wote wapokee maonyo juu ya maneno haya na kujuu namna gani kujibu mafundisho yao ya uwongo.

Ni desturi ya manabii ya sabato kuanza na kuhubiri Habari Njema ya imani katika Kristo. Wanatumika na nyimbo za Habari Njema watu wanzopenda, kudanganya wajinga. Wanaonekana sawasawa wanaaheshimu Mandikio sana. Lakini nyuma kidogo wanaagiza wafuata wao kutii sheria ya Musa, zaidi amri ya sabato. (Sabato ni siku ya saba ya juma.)

Wana ukaramisu gani kufanya hivi wakati Paulo alipofundisha wazi kwamba Mkristo ni mfu kwa maneno ya sheria? Wanaeleza mafundisho ya barua ya Wagalatia namna gani? Ni kwa njia ya kuweka tofauti kwa sheria *adilifu* (ndiyo akili ya kuchagua mema au mabaya) na *kawaida* ya sheria. Amri Kumi ndizo sheria adilifu. Kawaida ya sheria ni maagizo yote mengine Mungu aliyotoa, kama maagizo juu ya vyakula visivyo safi, ukoma, matoleo kwa Mungu, vivi hivi.

Wanasema sheria adilifu haikuondoshwa kamwe. Ni onyesho la kweli ya milele ya Mungu. Kuabudu sanamu, uuaji, na uzini hazitapatani kamwe na sheria ya Mungu. Lakini kawaida ya sheria imeondoshwa ndani ya Kristo.

Hivi wanafikiri, wakati Paulo alipofundisha kwamba Mkristo ni mfu kwa sheria. alisema juu ya kawaida ya sheria, si juu ya Amri Kumi.

Wanasema kwa sababu sheria adilifu ingali, ni lazima kwa Wakristo kukaa kuitii. Ikiwa hivi, sharti washike sabato, na haifai wafanye kazi yo yote siku ile. Wanasema kwamba mmoja wa askofu wakubwa za Roma aliagiza kawaida hii ya sabato ihamishwe kwa siku ya kwanza ya juma, lakini agizo hili linakana mafundisho ya Neno la Mungu kabisa. Waza juu ya maneno haya:

1. Ndani ya 2 Wakorinto 3:7-11 tunasoma kwamba Amri Kumi zimeondoshwa kwa Mkristo. Ndani ya shairi 7, sheria inaitwa “utumishi wa mauti, ulioandikwa na kukatwa katika mawe.” Hii ilikuwa sheria safi, si kawaida ya sheria. Amri Kumi tu zilikatwa katika mawe na kidole cha Mungu (Kut. 31:18). Katika shairi 11 tunasoma ya kwamba utumishi wa mauti, hata kama ulikuwa na utukufu, *uliondoshwa*. Hakuna neno lililo wazi kupita hili. Sabato haina mamlaka juu ya Mkristo.

2. Hakuna mtaifa aliyeagizwa kamwe kushika sabato. Taifa la Wayuda peke yao walipewa sheria hii (Kut. 31:13. Hata kama Mungu mwenyewe alistarehe siku ya saba, hakuagiza mtu ye yote kufanya hivi kufika wakati alipotoa sheria hii kwa wana wa Israeli.

3. Wakristo hawakuacha kuabudu siku ya sabato na kuanza kuabudu siku ya kwanza ya juma kwa sababu ya agizo la askofu ye yote. Tumeweka Siku ya Bwana kwa kuabudu na kutumikia Bwana kwa sababu siku ile Bwana Yesu alifufuliwa toka wafu. Ufufuko wake ulihakikisha kwamba kazi ya ukombozi ilikwisha (Yn. 20:1). Vilevile siku ile wanafunzi wa wakati wa mwanzo walikutana pamoja kuvunja mkate, konyesha mauti ya Bwana (Mdo. 20:7). Na ilikuwa vilevile siku Mungu ali-

yochagua kwa Wakristo kuleta matoleo yao kwa kipimo walichobarikiwa na Mungu (1 Kor. 16:1, 2). Zaidi ya maneno haya, Roho Mtakatifu alitumwa toka mbingu siku ya kwanza ya juma. Wakristo hawachungi siku ya Bwana kwa sababu ya kutaka kugeuka watakatifu kupita, au kwa sababu ya kuogopa azabu; wanaweka siku ile kwa Bwana kwa sababu ya roho za kuja mapendo kwa Yule ambaye alijitoa mwenyewe kwa ajili yao.

4. Paulo hakuona tofauti kati ya sheria adilifu na kawaida ya sheria inayonekana kwa macho ya watu. Alifundisha na nguvu kwamba kuna sheria moja tu, na ya kwamba wote amba wanajaribu kujipatia haki kwa njia ya kuitii, bila kuweza kuitii ndani ya maneno yote, wanalaaniwa.

5. Tisa za Amri Kumi ziliandikwa tena ndani ya Agano Jipyä kama mafundisho mema kwa watoto wa Mungu. Ni magizo juu ya mambo mema au mabaya. Amri moja tu haikuandikwa tena, ndiyo amri juu ya kushika sabato. Kushika siku fulani si vizuri au vibaya. Hakuna agizo kwa Wakristo kushika sabato. Biblia inaanidika wazi ya kwamba Mkristo *hawezi kuhukumiwa* kwa sababu ya kuishika, au kutokuishika (Kol. 2:16).

6. Ndani ya Agano la Kale azabu kwa wale wasioshika sabato ilikuwa mauti (Kut. 35:2). Lakini sasa watu wanaosukuma waamini kushika sabato hawaazibu waasi. Hivi hawaheshimu sheria na wanaharibu amri yake kwa sababu hawalazimishi watu kuitii. Ni kama wanasema, “Hii ni sheria ya Mungu, na lazima uitii, lakini neno haya halitakupata kama ukiiasi.”

7. Kristo, si sheria, ni kawaida kwa maisha ya mwamini. Ingetupasa kute-mbea namna Yeye alivyotembea. Hiki ni kipimo hata juu kupita kile cha sheria (Mt. 5:17-48). Tunapewa uwezo toka Roho Mtakatifu ili tuweze kuishi maisha

matakatifu. Tunataka kuishi hivi kwa sababu ya mapendo yetu kwa Kristo. Haki ya sheria inatimizwa ndani ya watu wale wasiotembea kufuata maneno ya mwili, lakini wanaofuata maneno ya Roho (Rom. 8:4).

Hivi mafundisho ya kwamba inapasa waamini kushika sabato hayapatani hata kidogo na Maandiko (Kol. 2:16), lakini ni “habari njema nyingine inayolaaniwa na Mungu” (Gal. 1:7, 9).

Tuombe Mungu kutupa sisi hekima kutambua mafundisho maovu ya légalisme, (ndiyo mafundisho ya kutega watu ili washike sheria ya Musa kama amri kubwa ya maisha yao). Tusijaribu kamwe kuhesabiwa haki au kutakaswa kwa njia ya kazi yetu wenyewe. Sharti tutegemeet Bwana Yesu Kristo peke yake kwa mahitaji yetu yote. Tusingahau kamwe ya kwamba kutegemea sheria ni kutukana Mungu, kwa sababu kunatia sheria (kivuli) kwa pahali pa Kristo (mwenye hakika).



NOTES

¹ (1:8-9) John Stott, *Only One Way: The Message of Galatians*, pp. 27, 28.

² (2:3) Kwa tohara mwili wa mwana-mume unakatwa kidogo. Wakati Mungu alipoagiza neno hili kwa Abrahamu na wazao wake, alitaka neno hili kuwa alama ya agano lake nao, ndilo ya kwamba atakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wake (Mwa. 17:1-11). Halikuwa alama ya mwili tu, lakini alama ya roho vilevile. Abrahamu alitahiriwa kama alama ya kwamba alikuwa ame-amini Mungu (Rom. 4:11). Nyuma kidogo Wayuda walisahau maana ya *roho* ya tohara, na waliendelea na desturi ya tohara tu iliyokuwa bure kwa macho ya Mungu.

Hakuna agizo katika Agano Jipyä kwa watu kutahiriwa kwa sababu sasa Mungu anatendea Mataifa na Wayuda vilevile kwa neema. Kwa wakati wa mwanzo wa

kanisa waamini Wayuda wengine wali-sema na nguvu kwamba ni lazima kwa watu kutahiriwa kwa kupata wokovu. Watu wale waliitwa “waliothiriwa” (Gal. 2:12).

³ (3:13) J. Cynddylan Jones, *Studies in the Gospel According to St. John*, p. 113.

⁴ (3:20) Inaonekana kwamba habari hizi hapa hazipatani na neno tunalosoma nyuma, ya kwamba Kristo ni Mpatanishi wa Agano Jipyä (Ebr. 9:15). Neno hili *mpatanishi* linatumwiwa na maana mbalimbali ndani ya pahali hapa pawili. Musa alifanya kazi ya mpatanishi na kupokea sheria kutoka kwa Mungu na kuipitisha kwa watu wa Israeli. Ali-patanisha watu na Mungu. Kristo ni mpatanishi wa agano jipyä kubwa zaidi. Mbele ya Mungu kuweza kusambaza na haki baraka za agano hili, ilipasa Bwana Yesu kufa na kutia agano jipyä mhuri na damu yake. Ilimpasa kujitoa mwenyewe kuwa ukombozi kwa watu wote (1 Tim. 2:6). Anachunga baraka za agano kwa watu wake, na zaidi ya ile anachunga watu wake wa agano katika dunia hii ya uadui. Anafanya hivi kama Kuhani Mkubwa na Mwombezi, na hii vilevile ni sehemu ya kazi yake kama Mpatanishi.

⁵ (4:13) Watu walijaribu kueleza namna ya “*enzaifu*” wa Paulo kwa njia mbalimbali kama malaria, ugonjwa wa macho, au *enzaifu* wengine.

⁶ (5:2) Jack Hunter, *What the Bible teaches, Galatians – Philemon*, p. 78.

BIBLIOGRAPHIE

Cole, Alan. *The Epistle of Paul to the Galatians*. Grand Rapids: Wm. B. Eerdmans Publishing Company, 1965.

Eadie, John. *Commentary on the Epistle of Paul to the Galatians*. Edinburgh: T. and T. Clark, 1884.

Harrison Norman B. *His Side Versus Our Side*. Minneapolis: The Harrison Service, 1940.

Hogg, C. F., and W. E. Vine. *Epistle to*

- the Galatians.* Glasgow: Pickering and Inglis, 1922.
- Ironside, Harry A. *Expository Messages on the Epistle to the Galatians.* New York: Loizeaux Brothers, 1941.
- Kelly, William. *Lectures on the Epistle of Paul the Apostle to the Galatians.* London: G. Morrish, n.d.
- Lightfoot, J.B. *The Epistle of St. Paul to the Galatians.* Grand Rapids: Zondervan Publishing House, 1962.
- Stott, John R. *Only One Way: The Message of Galatians.* Downers Grove, IL.: Inter-Varsity Press, 1968.

BARUA KWA WAEFESO

Utangulizi

“Andiko timilifu la maandiko ya Paulo” – J. Armitage Robinson

“Barua ya tatu ya Paulo juu ya mbingu .” – A. T. Pierson

I. Nafasi ya peke yake katika Kanuni

Barua kwa Waefeso inafanana na barua nyingine za Paulo: inaanza na salamu, na inaendelea na mashukuru, mafundisho, na maelezo namna gani kutumika na mafundisho haya ndani ya mwenendo wetu, na inakwisha na kuagana.

Walimu wengi wanakubali semo la J. A. Robinson kwa mwanzo wa utangulizi huu, lakini kuna walimu wengine wa wakati wa sasa wasiofikiri barua hii iliandikwa na Paulo. Tuone kama wana msingi mzuri kwa mawazo haya.

II. Mwandishi

Hakuna barua nyingine inayoshuhudiwa kupita barua kwa Waefeso kuwa andiko la Paulo tangu zamani na walimu wa kujulikana, kama Clément wa Roma, Ignatius, Polycarp, Hermas, Clément wa Alesandurio, Irenaeus, na Hippolytus. Efeso inatajwa ndani ya maandiko ya Marcion, na Kanuni ya Muratori vilevile.

Ndani ya barua hii mwandishi alijiita Paulo mara mbili (1:1 na 3:1), na kwa njia *nyingine* barua yenye we inafanana sana na barua kwa Wakolosayi. Neno hili linatufikirisha kwamba barua hizi

mbili ziliandikwa karibu na muda mmoja. Katika Waefeso kuna mafundisho mengine yasiyokuwa ndani ya Wakolosayi.

Ni kama mwalimu wa Allemagne Schleiermacher alikuwa mwalimu wa kwanza wa muda wa sasa aliyekana kwamba Paulo aliandikwa barua hii. Walimu wengine walimfuata, kama Moffat na Goodspeed, wakitaja maneno mballimbali ambayo waliwaza yalihakikisha kwamba barua hii haikuandikwa na Paulo. Walimu wengi wengine wenye kujifunza sana wanaeleza kwamba mawazo ya watu wale si kweli, na ya kwamba barua hii iliandikwa kweli na Paulo.

III. Tarehe

Waefeso, pamoja na Wakolosayi, Wafilipi, na Filemono zinaitwa “Barua za kifungo.” Waefeso iliandikwa kwa wakati wa kifungo gani (3:1; 4:1)? Walimu wengine wanafikiri Paulo aliandikwa wakati alipokuwa katika kifungo kwa Kaisaria kwa miaka miwili, au labda katika kifungo kingine, lakini maneno mengi zaidi yanashuhudia kwamba iliandikwa wakati alipofungwa mara ya kwanza kwa Roma (bado kidogo nyuma ya 60 A.D.) Tikiko alipeleka barua kwa Kolosayi (4:7-9), na barua hii kwa

Waefeso vilevile (6:21, 22) katika wilaya ya Asia. Habari hizi zinatua saidia kufahamu kwa sababu gani barua hizi zinafanana kwa njia ya mafundisho na maneno mengine – Paulo alizilandika kwa muda mmoja, na mafundisho haya yalijaza kwanza nia yake.

IV. Msingi na Jambo Kubwa

Paulo aliita jambo kubwa la mafundisho ndani ya Waefeso “siri.” Haku-taka kusema kwamba haiwezekani kueleza siri hii, lakini kwamba ilikuwa kweli isiyofunuliwa kufika wakati ule.

Kweli hii bora sana ndiyo tangazo ya kwamba waamini Wayuda na waamini Mataifa ni moja sasa ndani ya Kristo Yesu. Wao ni viungo pamoja vya kanisa, Mwili wa Kristo. Kwa wakati wa sasa wanaketi ndani ya Kristo kwa pahali pa mbingu, na wakati wa kuja watashiriki utukufu wake aliye Kichwa juu ya vitu vyote.

Tunasoma juu ya siri hii ndani ya kila sura ya sura sita za Waefeso.

Ndani ya sura 1 inaitwa siri ya mapenzi ya Mungu, na inatazamia wakati wa kuja saa vitu vyote mbinguni na duniani vitakapojuumishwa ndani ya Kristo (mash. 9, 10). Waamini Wayuda (sh. 11, “sisi”) na waamini Mataifa (sh. 13, “ninyi”) watashiriki ndani ya utukufu wa wakati ule. Watatawala pamoja naye juu ya ulimwengu mzima kama mwili wake na utimilifu wake (mash. 22, 23).

Ndani ya sura 2 tunasoma namna gani Wayuda na Mataifa wanaokolewa kwa neema ya Mungu, namna gani wanapatanishwa na Mungu na waamini wenzao, namna gani wanageuka mtu mpya mmoja pamoja na Kristo, na kuwa hekalu takatifu katika Roho.

Ndani ya sura 3 tunaona elezo wazi kupita la siri. Linasema juu ya siri ya

Kristo aliye Kichwa, na waamini wote, ndio Mwili wake. Ndani ya Mwili huu, waamini Mataifa ni wariti pamoja, vi-ungo pamoja, na wenye kushiriki pa-moja wa ahadi ya Mungu (sh. 6).

Sura 4 inaonyesha zaidi umoja wa Mwili, na shauri la Mungu kwa Mwili huu kukua na kukomea (mash. 1-16).

Ndani ya sura 5, siri inaitwa Kristo na kanisa (sh. 32). Ushirika wa Kristo na kanisa ni mfano kwa ushirika wa mume na mke waamini.

Mwishoni, ndani ya sura 6, Paulo alisema juu ya siri ya Habari Njema, na ya kwamba yeche ni mjambe wa siri hii katika minyororo (mash. 19, 20).

Bila shaka waamini wa Mataifa walishangaa sana wakati habari hizi zilipotumwa kwao. Walio kolewa kwa neema kwa njia ya imani, kama waamini Wayuda, lakini zaidi ya ile, hii ilikuwa mara ya kwanza waliyokuwa wenye mapendeleo kama wao. Hawakuwa chini kupita kwa macho ya Mungu. Na kwa wakati wa kuja watakalishwa pamoja na Kristo kama Mwili wake na Bibi-Arusi yake, na kushiriki utukufu wa utawala wake wa ulimwengu mzima.

Jambo kubwa lingine katika Waefeso ni *mapendo* (*agape* kwa Kiyunani, ndiyo mapendo watu wanayoonyesha na kutaka kwao). Paulo alisema juu ya mapendo haya kwa mwanzo na mwisho wa barua yake (1:4; 6:24), na alitumika na maneno haya *penda* na *mapendo* ndani ya Waefeso kupita ndani ya barua zake zote nyininge. Labda Roho Mtakatifu, akijua maneno yatakayotokea nyuma ya miaka makumi tatu, alimwongoza kufanya hivi. Kwa wakati ule kanisa hili kubwa watakaa kutii agizo la kushindana na mafundisho ya uwongo, lakini Bwana wetu alialiambia ndani ya barua hii kwamba walikuwa wameacha *mapendo* yao ya kwanza (Ufu. 2:4).

HABARI YALIYOMO

1. PAHALI PA MWAMINI KATIKA KRISTO (Sura 1 – 3)
 - A. Salamu (1:1, 2)
 - B. Paulo alisifu Mungu kwa baraka za neema (1:3-14)
 - C. Mashukuru na maombi ya Paulo kwa watakatifu (1:15-23)
 - D. Wokovu wa Mataifa na Wayuda unaonyesha uwezo wa Mungu (2:1-10)
 - E. Umoja wa waamini Wayuda na Mataifa ndani ya Kristo (2:11-22)
 - F. Habari nyingine juu ya siri (3:1-13)
 - G. Maombi ya Paulo kwa watakatifu (3:14-19)
 - H. Wimbo wa sifa ya Paulo kwa Mungu (3:20, 21)
2. UTENDAJI WA MWAMINI KATIKA BWANA (Sura 4 – 6)
 - A. Maonyo kwa Wakristo kushiriki katika umoja (4:1-6)
 - B. Utaratibu kwa matumizi mazuri ya viungo vyya mwili (4:7-16)
 - C. Maonyo kwa waamini kuwa na mwenendo mpya (4:17 – 5:21)
 - D. Maonyo kwa watu nyumbani mwa Wakristo kuwa na utawa (5:22 – 6:9)
 - E. Maonyo juu ya vita inayopasa Wakristo kupiga (6:10-20)
 - F. Salamu ya Paulo (6:21-24)

Maelezo

1. PAHALI PA MWAMINI KATIKA KRISTO (Sura 1 – 3)

A. Salamu (1:1, 2)

1:1 Maana ya jina la **Paulo** ni “mdogo.” Labda kwa mwili alikuwa mtu mdogo, lakini kwa maneno ya roho alikuwa mwenye uwezo mkubwa ku-vuta na kuongoza watu. Alijiita **mtume wa Kristo Yesu**. Ni kusema aliagizwa na Bwana mfufuliwa kufanya kazi fulani. Kazi hii ilikuwa kuhubiri *Habari Njema* kwa Mataifa na kufundisha kweli kubwa juu ya *kanisa* (3:8, 9). Barua kwa Waefeso ni juu ya kanisa, na kweli hii ilifunuliwa kwanza kwa mitume na manabii (3:5), hivi ilikuwa taratibu kwa Paulo kujiita **mtume**. Hakufanya hivi kwa sababu ya kiburi, lakini kueleza kwa sababu gani alikuwa na amri kusema juu ya neno hili. Alipewa amri hii **na mapenzi ya Mungu**. Paulo hakuchagua kazi hii ye ye mwenyewe. Wala hakuna mtu ambaye alimwagiza

kuifanya. Ulikuwa mwito wa Mungu (Gal.1:1).

Alituma barua hii **kwa watakatifu walio katika Efeso, na kwao wanaoamini Kristo Yesu**. Watakatifu ndio watu waliowekwa kwa Mungu toka dunia. Ndani ya Agano Jipyä waamini wote waliozaliwa tena wanaitwa na jina hili. Neno hili linasema zaidi juu ya pa-hali pa mwamini **ndani ya Kristo**, si ndani yake mwenyewe. **Ndani ya Kristo** waamini wote ni **watakatifu**, hata kama hawatendi kama watakatifu wakati wote. Kwa mfano, Paulo aliita Wakorinto **watakatifu** (1 Kor. 1:2), hata kama maneno tunayosoma juu yao yanaonyesha kwamba si wote walioishi maisha matakatifu. Lakini Mungu ana-taka wale walio **watakatifu** ndani ya Kristo kutenda kama watakatifu ndani ya mwenendo wao.

Na kwao wanaoamini Kristo Yesu. Ni kusema waamini wote wa kweli. Ingepasa waamini wote kuwa **waaminifu** na ingepasa watu kuweza

kuwaamini. Lakini zaidi ni watu ambao walikiri Kristo Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wao wa pekee.

Walimu wengi wanafikiri kwamba barua hii iliandikwa kwa makanisa mengine vilevile, lakini kwamba kanisa kwa Efeso lilionekana zaidi.

1:2 Halafu mtume aliendelea na kusalimu watakatifu. Kila neno la salamu hii lina maana kubwa kwa roho zetu.

Maana ya **neema** ni msaada kwa maisha ya kila siku. Wasomaji wa Paulo walikuwa wameokolewa na neema ya Mungu. Neema hii ni upendeleo wake usiostahilishwa kwa wapotevu. Lakini sasa Paulo aliomba **Mungu kuwapa nguvu** waliyohitaji kushindana na masumbuko, mateso na huzuni za maisha ya sasa.

Salama ni roho ya utulivu kwa maneno yote yanayokaa kugeukageuka katika maisha yetu. Watakatifu walikuwa wamepokea salama *na* Mungu wakati walipookolewa. Lakini walihitaji **salama** ya Mungu kila siku, ndiyo roho ya utulivu, si neno kama mambo gani yaitokea. Roho namna hii ni tunda la kuomba Mungu juu ya mambo yote (Flp. 4:6, 7).

Ona ya kwamba Paulo alitaja **neema** kwanza, kisha **salama**. Ni hivi kila mara: Kwanza **neema**, nyuma yake **salama**. Nyuma ya kupata usamehe wa zambi kwa **neema** ya Mungu, mtu anaweza kuwa na **salama** rohoni. Na kwa njia ya kupewa na Mungu kila siku nguvu ambayo hastahili kupokea, mwanmini anaweza kujuana na salama timilifi ya Mungu, katika maneno yanayokaa kugeuka katika maisha yetu.

Neema (*charis*) ilikuwa neno la Wayunani. Neno Wayuda wanilotumia kusalimu watu *ni* **salama** (*Kiebrania: shâlom*). Tukiunga maneno haya mawili pamoja tunapata mfano mdogo wa Habari Njema kwa dunia nzima. Na ndani ya maneno haya mawili tunaona

vilevile kweli ya kanisa la Agano Jipyambayo Paulo aliyofundisha wazi sana ndani ya Waefeso – Wayuda na Mataifa wakiungwa pamoja kuwa mwili mmoja katika Kristo.

Neema ... na salama toka Mungu Baba yetu na Bwana Yesu Kristo. Paulo hakusita kutaja **Bwana Yesu** kwa cheo moja na **Mungu** Baba. Aliheshimu Mwana namna alivyoheshimu **Baba**. Ingetupasa sisi kufanya vivyo hivyo (Yn 5:23).

Tuwaze juu ya maneno haya: **Mungu Baba yetu.** Neno hili **Mungu** peke yake linatufikirisha juu ya Mmoja aliye mku-bwa na mjuu sana, ambaye ni nguvu kwa sisi kukaribia. Lakini jina hili **Baba** linasema juu ya Mmoja aliye karibu kabisa. Tukiwaza juu ya neno la tatu, ndilo **yetu**, tunashangaa kuona kwamba **Mungu** mjuu sana, Mungu wa milele, ni Baba ya mapendo ya kila mtu aliyeza-liwa tena kwa njia ya imani ndani ya **Bwana Yesu**.

Jina la heshima zima la Mwokozi wetu *ni* **Bwana Yesu Kristo**. Kama **Bwana** ye ye ni mwenye amri juu ya maneno yetu yote, maisha yetu na vitu vyetu. Kama **Yesu** ye ye ni Mwokozi wetu toka zambi. Kama **Kristo** ali-pakaliwa na Mungu kuwa Nabii, Kuhani, na Mfalme. Jina lake linatujaza na mawazo matamu mengi!

B. Paulo alisifu Mungu kwa baraka za neema (1:3-14)

1:3 Nyuma ya salamu hii fupi, mtume alipaza sauti yake na wimbo bora zaidi ya sifa na kuabudu katika Agano Jipyambayo. Aliabudu Mungu na moyo uliofuri-ka kwa baraka zote za neema, Ndani ya mashairi 3-14 Paulo alionyesha namna Mungu alivyotumika kuleta wokovu tangu milele, kwa wakati wa sasa, na kwa milele ya kuja. Na pamoja na ile ilimpasa kusema juu ya siri ya mapenzi ya Mungu – ndiyo kwa waamini Wayuda na Mataifa kushiriki

pamoja katika uriti wa utukufu.

Alianza na kuita wote wanaojua **Mungu** kumbariki, maana yake kufurahisha moyo wake na sifa na kuabudu kwa mapendo. **Mungu mbarikiwa ni Baba ya Bwana wetu Yesu Kristo.** Mara nyingine Yesu alisema na Mungu kama Mungu (Mt. 27:46). Mara nyingine alisema juu yake kama Baba (Yn. 10:30). **Mbarikiwa** ni yule anayebariki vilevile. Tunambariki kwa njia ya kumsifu. Yeye anatubariki sisi na kutufurahisha kwa njia ya kutumwangia utajiri wa neema yake.

Alitubariki kwa baraka zote za roho katika pahali pa mbingu ndani ya Kristo. Kwanza ona ukarimu wa Mungu – **baraka zote za roho.** Ona vilevile kwamba ni baraka za *roho*. Baraka hizi ni namna nyingine na baraka za Israeli chini ya sheria. Kwa wakati wa Agano la Kale, zawabu za Myuda mwaminifu zilikuwa maisha marefu, jamaa kubwa, mavuno mazuri mashambani, na kulindwa wasiumizwe na adui (Tor. 28:2-8). Baraka za Wakristo ni namna nyingine. Ni baraka za **roho**, hazina zisizo vitu vya dunia, visivyo-onekana kwa macho, na visivyo-haribika. Ndiyo, watakatifu wa Agano la Kale walibarikiwa na nyingine za baraka hizi za roho vilevile, lakini tutaona ya kwamba Mkristo wa wakati wa sasa anafurahishwa na baraka watu wa Agano la Kale wasizojuia.

Baraka zetu ni *katika pahali pa mbingu*. Si baraka za vitu kwa pahali pa dunia. Tunasoma mara tano ndani ya Efeso juu ya **katika pahali pa mbingu:**

- 1:3 Pahali pa baraka yetu ya **roho**
- 1:20 Kristo anakaalishwa sasa katika pahali pa mbingu
- 2:6 Pahali sisi tunapokalishwa sasa ndani ya Kristo
- 3:10 Ni toka pale malaika wanaona hekima ya Mungu ndani ya kanisa

6:12 Ni pahali tunaposhindana sasa na pepo wabaya

Wakati tunapokutanisha mashairi haya yote pamoja, tunafahamu maneno haya **pahali pa mbingu** vizuri kupita. Baraka zote za **roho** ni *ndani ya Kristo*. Ni yeye ambaye alitupatia baraka hizi kwa njia ya kazi yake kwa Kalvari. Sasa baraka hizi ni tayari kwa sisi kwa njia yake. Mambo yote Mungu aliyo nayo kwa mwamini ni ndani ya Bwana Yesu. Kwa kupokea baraka hizi zote, inatupasa kuunganishwa na *Kristo* kwa njia ya imani. Chafer aliandika, “Wote waliookolewa ni ndani ya Kristo, na wanashiriki ndani ya vyote Kristo aliyo-fanya, vyote alivyo, na atakavyo-kuwa kwa milele.”¹

Ndani ya Kristo ni usemi mmoja wenye maana sana katika Waefeso. Kuna kweli kubwa mbili ndani ya Agano Jipyä yanayofungamana – kweli ya pahali mwamini alipo, na kweli ya matendo yake.

Kwanza, pahali pa mwamini. Kila mtu duniani ni au “ndani ya Adamu” au “ndani ya Kristo.” Wale walio “ndani ya Adamu” wangali na zambi zao, na hivi wanahukumiwa na Mungu. Hawawezi kufanya kitu wao wenyewe kupendeza Mungu au kukubaliwa naye. Kama wangalipokea hukumu wangaliyostahili kupokea, wangalipotea kwa milele.

Wakati mtu anapookolewa, Mungu hamwonni tena kama mtoto mhukumiwa wa Adamu. Anamwona sasa na kumpokea **ndani ya Kristo**. Hili ni neno kubwa. Mwenye zambi anayeamini hakubaliwi na Mungu kwa sababu ya namna alivyo yeye mwenyewe, lakini kwa sababu yeye ni **ndani ya Kristo**. Wakati alipo **ndani ya Kristo**, anasimama mbele ya Mungu na kufurahi kwa sababu anakubaliwa kama Kristo mwenyewe. Na atafurahi katika ukubali wa Mungu kwa milele, kama Kristo mwenyewe.

Hivi cheo cha mwamini ni **ndani ya Kristo**. Cheo chake ni kikamilifu, lakini matendo yake si makamilifu. Lakini Mungu anataka matendo ya mwamini kugeuka kufanana kupita na kupita na cheo chake. Matendo yake hayatakuwa makamilifu kufika wakati atakapofika mbinguni. Lakini kufika wakati ule ingempasa kukaa kuongezeka katika utakaso, kukomea, na kufanana kupita na kupita na Kristo angali yeeye ni kwanza hapa duniani.

Wakati tunapofahamu tofauti kati ya cheo cha mwamini na hali ya matendo yake, tunaweza kufahamu mashairi yanayoonekana kufundisha maneno ya siyopatana:

Waamini ni wakamilifu (Ebr. 10:14).

Ingepasa waamini kuwa wakamilifu (Mt. 5:48)

Waamini ni wafu kwa zambi (Rom. 6:2)

Ingepasa waamini kujihesabu kuwa wafu kwa zambi (Rom. 6:11)

Waamini ni taifa takatifu (1 Pet. 2:9)

Ingepasa waamini kuwa watakatifu (1 Pet. 1:15)

Barua ya Paulo kwa Waefeso ina sehemu mbili zinazopatana na kweli hii:

(Sura 1–3): Cheo chetu – ndani ya Kristo;

(Sura 4–6): Matendo yetu – namna ingetupasa kuishi.

Sehemu ya kwanza ni mafundisho, sehemu ya pili ni juu ya kazi yetu.

Ndani ya sura 1–3 tunasoma juu ya pahali tulipo, ndipo “katika Kristo,” “katika Yesu Kristo,” “ndani yake.” Ndani ya sura 4–6 tunaona maneno haya mara nyingi, “katika Bwana,” kukumbusha mwamini kwamba Kristo ni Bwana wake na inampasa kumtumikia na kumtii. Mtu mmoja alisema sura 1–3 zinapasha juu ya mwamini katika Kristo mbinguni, lakini katika sura 4–6 tunamwona akitumika kazi ndani ya mafika.

Sasa sisi ni tayari kuwaza juu ya nyingine za baraka zetu za **roho ndani ya Kristo** katika **pahali pa mbingu**.

1:4 Baraka ya kwanza inaitwa mchaguo. **Kama vile aliviyotuchagua ndani yake mbele ya kuwekwa misingi ya ulimwengu**, ili tuwe watakatifu, na **pasipo kilema mbele yake** katika mapendo.

Waza kwanza juu ya neno hili: **Ali-vyotuchagua**. Nyuma yake waza juu ya pahali alipotuchagua: **ndani yake**. Makusudi yote ya Mungu kwa watu wake yanatimizwa ndani ya Bwana Yesu na kazi yake. Tunaona wakati gani Mungu alipotuchagua: **mbele ya kuwekwa misingi ya ulimwengu**. Alituchagua kwa kusudi gani? Ili **tuwe watakatifu, na pasipo kilema mbele yake** katika mapendo. Maneno haya hayatatimizwa pia kufika wakati tutakopokuwa pamoja naye mbinguni (1 Yn. 3:2), lakini yanepasa kuendelea mbele kila siku ndani ya maisha yetu hapa duniani.

Ombi: “Bwana, unigeuze kuwa matakatifu sasa, kwani hili ndilo kusudi lako kwa maisha yangu. Amina.”

MAFUNDISHO JUU YA MCHAGUO WA MUNGU

Mafundisho ya mchaguo yanafazaisha watu sana, hivi sharti tuangalie karibu karibu maneno yote Biblia inayofundisha (na kutokufundisha) juu ya neno hili.

Neno la kwanza, unafundisha kwamba Mungu anachagua watu kuokolewa (2 Tes. 2:13). Unaita waamini wale “wachaguliwa ambao alitangulia kuwajua” (1 Pet. 1:2). Inafundisha kwamba watu wanaweza kujua kama walichaguliwa kwa njia ya namna walivypokea Habari Njema: wale wanaoamini maneno wanayosikia wamechaguliwa (1 Tes. 1:4–7).

Lakini Biblia haifundishi kamwe ya kwamba Mungu anachagua watu ku-

potea. Hata kama anachagua wengine kuokolewa, si kusema kwamba anahukumu watu wote wengine. Hahukumu kamwe watu kufa wanaostahili kuokolewa (hakuna watu wa namna hii), lakini anaokoa wengine wanaostahili kuhukumiwa. Wakati Paulo alipotoa habari za wachaguliwa, aliyaita “vyombo vya rehema, ambavyo alivitengeneza tangu zามانى، vigate utukufu” (Rom. 9:23), lakini wakati aliposema juu ya wapotevu, alisema tu, “vyombo vya gazabu vilivyofanywa tayari kwa kuangamia (Rom. 9:22). Mungu anatayarisha vyombo vya rehema kwa utukufu, lakini hatayarishi watu kwa kuangamia: wanafanya hivi wao wenyewe kwa njia ya kutokuamini kwao.

Mafundisho ya mchaguo yanaonesha kwamba Mungu ni mwenye enzi. Anaweza kufanya neno lo lote analotaka, lakini hataki kamwe kufanya neno lililo na uzalimu. Kama watu wangaliachwa huru kufanya neno lo lote wanaloataka, wao wote wangalipotea. Basi Mungu ana ruhusa kurehemu wengine?

Lakini Biblia inayofundisha juu ya mchaguo wa Mungu inayofundisha vilevile juu ya madaraka ya watu. Hakuna mtu anayeweza kutoa uzuru kusema hakuokolewa kwa sababu ya mchaguo wa Mungu. Mungu anawapa watu wote pahali po pote njia kuokolewa (Yn. 3:16; 3:36; 5:24; Rom. 10:9, 13). Mtu ye yote anaweza kuokolewa kwa njia ya kutubu zambi zake na kuamini Bwana Yesu Kristo. Hivi mtu akipotea, ni kwa sababu yeye mwenyewe alichagua kupoetea, si kwa sababu yalikuwa mapenzi ya Mungu.

Biblia inayofundisha mchaguo, inayofundisha vilevile kwamba wokovu ni bila bei kwa watu wote ambaa wanatalaka kuupokea. Mafundisho juu ya maneno haya mawili ni ndani ya shairi moja: “Wote ambaa Baba ananipa watakuja

kwangu; naye anayekuja kwangu sitamtupa inje kabisa” (Yn 6:37). Sehemu ya kwanza ya shairi hili linasema juu ya mchaguo wake; ndani ya sehemu ya pili yeye ni tayari kurehemu watu wote.

Maneno haya ni nguvu kufahamu kwa nia ya mtu. Namna gani Mungu anaweza kuchagua wengine, na hata hivi kuwa tayari kutolea watu wote wokovu bila bei? Ndiyo, neno hili ni siri. Ni siri kwa sisi watu, lakini si kwa Mungu. Inatupasa kupokea na kuamini maneno haya yote mawili kwa sababu Biblia inayofundisha mawili yote. W.G. Blaikie anajumlisha maneno haya hivi:

Mafundisho juu ya enzi ya Mungu, madaraka ya watu, na utayari wa Mungu kurehemu, ni yote ndani ya maandiko matakatifu. Hata kama nia zetu haziwezi kuunganisha maneno haya yote, ingetupasa kuyamini.² ♦

1:5 Baraka kubwa ya pili ambayo Mungu anatutolea kwa sababu ya neema yake ni kutangulia kuchagua. Neno hili linafungamana na mchaguo, lakini ni namna nyingine kidogo. Mchaguo unaonyesha Mungu akichagua watu watakaokolewa. Lakini hata mbele ya ile Mungu alichagua ya kwamba wote watakaokolewa watapokewa vilevile ndani ya jamaa yake **kama wana**. Angaliweza kutuokoa bila kutufanyiza wana wake, lakini alichagua kufanya maneno haya yote mawili.

Tunaona hapa ya kwamba **alitangulia kutuchagua ili tufanywe wana wake**. Katika Agano Jipyaa maana yake ni kuweka mwamini ndani ya jamaa ya Mungu kama mwana wa kukomea, anayeshiriki ndani ya mapendeleo na madaraka ya mwana (Gal. 4:4-7). Roho ya kufanywa mwana inamsukuma kuita Mungu “Baba” (Rom. 8:15).

Tulifanywa wana **kwa njia ya Yesu Kristo**. Mungu asingaliweza kamwe kutufikisha **kwake** kwa pahali pale pa

ukaribu na mapendo wakati tulipokuwa ndani ya zambi. Hivi Bwana Yesu alifika duniani, na kwa njia ya kufa, kuzikwa, na ufuufuko wake alitengeneza neno hili namna Mungu aliviyotaka. Kwa sababu ya zabihu yake ya bei kubwa sana kwa Kalvari Mungu anaweza kutuweka **kama wana**.

Na maneno haya yote ni **sawasawa ilivyopendeza mapenzi yake**. Hili ni kusudi la Mungu wakati alipotangulia kutuchagua. Ni jibu kwa ulizo, "Kwa sababu gani alifanya hivi?" Kwa sababu **ilimpendeza**. Hakuweza kutuliwa kufika wakati alipojizungusha na wana waliofananishwa na Mwana wake mza-liwa pekee, pamoja naye na sawasawa naye kwa milele.

1:6 Kwa sifa ya utukufu wa neema yake ambayo alitupa sisi katika huyu Mpendwa. Wakati Paulo alipowaza juu ya neema ya Mungu ambaye alituchagua kwanza, na mbele ya ile alitangulia kutuchagua kuwa wana wake, ana-shangaa juu ya utukufu mkubwa wa kuzidi sana wa neema ya Mungu. Anaeleza ya kwamba kusudi la Mungu na namna Mungu aliviyotenda na neema kubwa hivi ni kwa **utukufu** wake mwényewe. Anastahili kupokea sifa na kuabudu kwa milele kwa upendeleo huu mkubwa. Waza juu ya **neema** yake. Alitupokea (bila bei) ndani ya **Mpendwa**. Mwishoni Paulo alituonya **tusifu** Mu-ngu kwa **neema** yake ya utukufu.

1:7 Wakati tunapowaza juu ya shauri bora sana la milele la Mungu kwa watu wake, tunakuta neno lingine, ndilo **ukombozi**. Ukombozi unatupasha juu ya kazi ya Kristo, kwa njia yake tulifunguliwa toka utumwa na hatia ya zambi, na kuanza maisha ya uhuru. Bwana Yesu ndiye Mkombozi (**Katika yeeye tuna ukombozi**). Sisi ndio wakombolewa. **Damu yake** ni bei ya ukombozi wetu. Hatukuweza kukombolewa kwa njia yo yote nyininge.

Tunda moja la ukombozi ni **usamehe wa zambi**. **Usamehe** si **ukombozi**; ni moja la matunda yake. Ilipasa Kristo kulipa kwa zambi zetu zote kwa msalaba mbele ya zambi hizi kuweza kusamehewa.

Kipimo cha **usamehe** kinaonyeshwa na maneno haya: **sawasawa na wingi wa neema yake**. Tukiweza kupima ukubwa wa **utajiri wa neema ya Mungu**, tunawenza kupima ukubwa wa usamehe wetu vilevile. **Neema** yake haina kipimo! Ni vivyo hivyo na **usa-mehe** wake!

1:8 Mungu kwa neema yake alituchagua, na alitangulia kwa sisi kuwa wana wake, na alitukuomboa. Alizidisha neema ile **kwetu katika hekima yote na akili**. Ni kusema kwamba kwa neema alishiriki nasi makusudi na mashauri yake. Alitaka kutujulisha na kutufahamisha makusudi yake kwa kanisa na kwa ulimwengu. Hivi alitufunulia mambo makubwa yatakayotokea kwa wakati wa kuja duniani.

1:9 Halafu Paulo alieleza sasa namna gani Mungu alikwisha **kutujulisha siri ya mapenzi yake**. Hii ndiyo kweli inayookeana zaidi ndani ya barua hii – kweli ya utukufu sana juu ya Kristo na kanisa. Ni **siri** isiyojulikana mbele, lakini inayofunuliwa sasa kwa watakatifu. Ni **siri ya mapenzi yake mema**. Shauri lake kubwa ni Bwana Yesu Kristo. Hii ndiyo maana ya maneno haya, **ilivyopendeza kukusudi ndani yake**.

1:10 Sasa Paulo alianza kueleza maneno ya ndani ndani ya siri ya Mungu. Katika sura hii anawaza zaidi juu ya maneno ya kuja ya siri hii. Ndani ya sura 2 na 3 tutaona maelezo mengine juu ya siri kwa wakati wa sasa.

Muda Paulo aliowaza juu yake ni **madaraka** (kwa kiyunani ni *oikonomia*) **ya kutimilika ya nyakati**. Tunafikiri muda huu ni miaka elfu moja wakati Kristo atakaporudi kwa dunia kutawala

kama Mfalme wa wafalme na Bwana wa wabwana. Mungu ana shauri kwa usimamizi wa muda wa mwisho wa watu juu ya dunia hii.

Shauri hili ni “kujumlisha vitu vyote ndani ya Kristo.” Kwa utawala wa miaka elfu moja, **vitu vyta mbinguni na vitu vyta duniani** vitajumlishwa **ndani ya Kristo**. Mwokozi anayekataliwa sasa atakuwa mwenye sifa zaidi kwa wakati ule, Bwana wa wote, mwenye kupokea kuabudu toka ulimwengu mzima. Hili ndilo kusudi la Mungu – kuweka **Kristo** kuwa Kichwa juu ya **vitu vyote**, vyta mbingu na vyta dunia, katika ufalme. Bellett aliandika:

Siri hii haikufunuliwa mbele. Ndani ya unabii wa Isaya tunaona mfano mzuri sana wa dunia wakati wa utawala wa miaka elfu moja; lakini tunaona Kristo akitawala juu ya mbingu kwa miaka elfu moja? Isaya alisema hata mara moja kwamba vitu vyote mbinguni na duniani vitatawaliwa na Mtu huyu mtukufu? ³

Mara nyingine watu wanatumika na shairi hili kusimamia mafundisho ya kwamba watu wote wataokolewa, lakini ni mafundisho ya uwongo. Wanageuzea mafundisho haya kusema mwishoni kila kitu na kila mtu watatengenezwa na kuzapanishwa ndani ya Kristo. Lakini shairi hili halifundishi maneno haya. Paulo alisema hapa juu ya *mamlaka* ya Kristo, si juu ya wokovu wa watu wote!

1:11 Neno kubwa moja la siri hii ndilo ya kwamba waamini Wayuda na waamini Mataifa wanashiriki ndani ya shauri hili kubwa la Mungu. Mtume alisema juu ya waamini Wayuda katika siri hii ndani ya mashairi 11 na 12; juu ya waamini Mataifa ndani ya shairi 13; kisha alisema juu yao wote pamoja ndani ya shairi 14.

Juu ya Wakristo wa taifa la Wayuda, Paulo aliandika, **Ndani yake vilevile tulifanywa uriti**. Hawakushiriki ndani

ya uriti kwa sababu walikuwa Wayuda mbele, lakini kwa sababu waliungwa na Kristo. **Uriti** hapa unatazamia wakati waamini Wayuda na waamini wa kweli wote watakapoonyeshwa na kushangaza sana watu wa dunia kama Mwili wa Kristo, na Bibi Arusi ya Mwana Kondoo.

Tangu milele yalikuwa mapenzi ya mwenyezi Mungu kuchagua Wakristo Wayuda kwa mapendeleo haya, **sawa-sawa na kusudi lake anayefanya maneno yote kwa shauri la mapenzi yake**.

1:12 Kusudi la kuwachagua mbele lilikuwa waweze **kuwa sifa ya utukufu wake**. Ni kusema ndani yao neema ya Mungu iweze kuonyesha kazi anayo-weza kufanya na watu wasio na faida, na hivi **kumtukuza** yeeye.

Mtume alisema juu yake mwenyewe na juu ya Wayuda wengine **sisi tulio-wekeea Kristo tumaini letu mbele**. Aliwaza juu ya baki la Wayuda watawa waliopokea Habari Njema wakati ilipohubiriwa kwanza. Ilihubiriwa kwanza kwa Wayuda. Zaidi ya taifa la Israeli waliikataa. Lakini kulikuwa na baki watawa walioamini Bwana Yesu. Paulo alikuwa mmoja wao.

Matukio yatakuwa namna nyingine wakati Mwokozi atakaporudi mara ya pili. Kwa wakati ule taifa la Israeli watatazama Huyu ambaye wali-mchoma na watamwomboleza kama Mwana mzaliwa pekee (Zek. 12:10). “Na hivi Israeli wote wataokolewa; kama ilivyoandikwa: Mwokozi atakua kutoka Sayuni, na ataondolea kutoku-ogopa Mungu katika Yakobo” (Rom. 11:26).

Paulo na waamini Wayuda wengine wa wakati ule waliamini Masiya mbele ya baki la taifa lao. Kwa sababu hii alisema, “sisi tulio-wekeea Kristo tumaini letu mbele.”

Wale waliotumaini Masiya mbele watatawala pamoja naye juu ya dunia.

Baki la taifa lao watakuwa ndani ya ufalme wake duniani.

1:13 Sasa Paulo aliacha kusema juu ya waamini waliozaliwa Wayuda na aligeuka kusema juu ya wale waliozaliwa Mtaifa. Alifanya hivi kwa njia ya kuacha kusema juu ya “sisi” na kuanza kusema juu ya “ninyi.” Waamini walikuwa wapagano mbele walishiriki ndani ya siri ya mapenzi ya Mungu, pamoja na Wayuda waliookolewa. Hivi Paulo alionyesha namna gani Waefeso na watu wa Mataifa wengine walifunganishwa na Kristo.

Waliskia Habari Njema. **Waliyamini** Kristo. **Walitiwa mhuri wa Roho Mtakatifu ya ahadi.** Kwanza waliskia neno la kweli, **Habari Njema ya wokovu** wao kwa njia ya kuamini Bwana Yesu Kristo. Lakini Habari Njema hii ni pamoja na mafundisho yote ya Kristo na mitume.

Nyuma ya kusikia habari hizi walijittoa kwa Kristo na imani. **Wokovu** unaapatikana ndani yake tu.

Mara moja nyuma ya kuamini **walitiwa mhuri wa Roho Mtakatifu ya ahadi.** Maana ya habari hizi ndiyo ya kwamba kila mwamini wa kweli anapokea **Roho** ya Mungu kama alama kuonyesha kwamba ye ye ni mali ya Mungu, na ya kwamba Mungu atamlinda kufika wakati atakapopokea mwili wake wa utukufu. Watu wa dunia wanawekea barua zao au vitu vyao vya faida mhuri kuonyesha kwamba ni mali yao. Ni vivyo hivyo na maneno ya Mungu. Roho Mtakatifu anayekaa ndani yetu ni mhuri ya kwamba sisi mali ya Mungu (1 Kor. 6:19, 20), na Yesu ni arabuni ya kwamba totalindwa kufika siku ya ukombozi (Efe. 4:30).

Mhuri wetu unaitwa **Roho Mtakatifu wa ahadi.** Kwanza, ye ye ni Roho Mtakatifu. Halafu ye ye ni Roho ya ahadi. Alikuwa ahadi ya Baba (Yoeli 2:28; Mdo. 1:4), na Bwana Yesu (Yn. 16:7). Zaidi ya ile, ye ye ni zamana

kwamba ahadi zote kwa mwamini zitakapotimizwa.

Tunasoma mara nyingi juu ya Utatu Mtakatifu ndani ya barua hii. Mara ya kwanza ni ndani ya shairi 13. Ndani ya shairi hili tunasoma juu ya Mungu Baba (sh. 3), Mwana (sh. 7), na Mungu Roho (sh. 13).

1:14 Halafu Paulo aligeuka tena. Ndani ya mashairi 11 na 12 alisema “yetu”, ndani ya shairi 13 alisema “yenu”, na ndani ya shairi 14 alifunganisha “sisi” na “ninyi” pamoja kuwa **wetu.** Ni kama mfano wa mafundisho ambayo tutaona kwa sura 2 na 3, kuonyesha kwamba waamini Wayuda na waamini Mataifa watafunganishwa pamoja kuwa mwungano, ndilo kanisa.

Roho Mtakatifu ni **arabuni ya uriti wetu.** Ni kama nusu ya malipo, na ni ahadi ya kwamba tutapokea uriti mzima kwa wakati wa kuja.

Mara moja, wakati tunapookolewa, Roho Mtakatifu anaanza kutufunulia utajiri wetu ndani ya Kristo. Anatuacha kuonja mbele utukufu utakaokuja. Lakini namna gani tunaweza kujua kabisa ya kwamba tutapokea uriti mzima siku nyingine? Roho Mtakatifu mwenyewe ni **arabuni** yenye we.

Kama mhuri, ye ye ni arabuni kwamba sisi wenye we totalindwa kwa uriti. Kama amana, ye ye ni arabuni kwamba **uriti** totalindwa kwa sisi.

Roho ni **arabuni kufika ukombozi wa mali yake mwenyewe.** Arabuni inatazamia **ukombozi** mzima, kama malimbuko yanavyotazamia mavuno mazima. Kazi ya Roho kama arabuni itakwisha wakati **mali iliyonunuliwa** itakapokwisha kukombolewa. Lakini Paulo alifikiri maana ya **mali iliyonunuliwa** ni nini?

1. Labda alifikiri ni **uriti wetu.** Mali yote ya Mungu ni yetu kwa njia ya Bwana Yesu Kristo: sisi ni wariti wa Mungu na wariti pamoja na Yesu Kristo (Rom. 8:17; 1 Kor. 3:21-23). Ulimwe-

ngu mzima umechafuwa kwa sababu ya zambi, na unahitaji kupatanishwa na kusafishwa (Kol. 1:20; Ebr. 9:23). Wakati Kristo atakaporudi duniani kutawala, viumbe vyote vinavyouguvitafunguliwa toka utumwa wa kuhabibika, viingie uhuru wa utukufu wa wato-to wa Mungu (Rom. 8:19-22).

2. Labda maana ya **mali yake mwenyewe** ni mwili wa mwamini. Roho zetu na nafsi zetu zilikombolewa wakati tulipoamini, lakini miili yetu itakombolewa kwa wakati wa kuja. Maumivu yetu, na kugeuka wazee na kufa kunahakikisha kwamba miili yetu hajjakombolewa bado. Wakati Kristo atakaporudi kwa sisi (1 Tes. 4:13-18), miili yetu itabdalishwa ili iweze kufanana na mwili wake wa utukufu (Flp. 3:21). Halafu ukombozi wa miili yetu utatimizwa kabisa kwa milele (Rom. 8:23).

3. Mwishoni, labda **mali yake mwenyewe** inasema juu ya kanisa (1 Pet. 2:9: “watu walio mali ya Mungu mwenyewe”). Kama ni hivi, ukombozi unatazamia vilevile saa Kristo atakaporudi tena, na atajilettea mwenyewe kanisa la utukufu, pasipo alama wala kikunjo wala kitu cho chote kama hivi (Efe. 5:27). Watu wengine wanafikiri kwamba labda **mali** ya Mungu ni watakatifu wa Agano la Kale vilevile.

Si neno kama **mali** iliyonunuliwa ikisema juu ya nini, mwisho wake ni sawasawa – ni kwa **sifa ya utukufu wake**. Halafu shauri la ajabu la Mungu kwa watu wake litatimizwa naye atopokea sifa daima. Paulo alitukumbusha mara tatu ndani ya sura hii ya kwamba kusudi na mwisho wa maneno yote Mungu aliyofanya yalikuwa aweze kutukuzwa.

Kwa sifa ya utukufu wa neema yake
(sh. 6)

Ili sisi tupate kuwa sifa ya utukufu
wake (sh. 12)

Kuwa sifa ya utukufu wake (sh. 14)

C. Mashukuru na maombi ya Paulo kwa watakatifu (1:15-23)

1:15 Ndani ya shairi 3 kufika shairi 14 ya sura 1 mtume alipasha habari za makusudi ya kushangaza ya Mungu tangu zamani kufika milele ya kuja. Alitaka kushiriki sasa na wasomaji wake mzigo wa maombi rohoni mwake ili waweze kufahamu habari hizi za ajabu vilevile. Alitaka wafahamu baraka za utukufu ambazo walikuwa nazo ndani ya Kristo. Na alitaka wafahamu uwezo mkubwa ambaa ulihitajiwa kwa Kristo kutolewa kuwa Kichwa cha muumbo wote.

Kwa sababu hii: Paulo alikumbuka tena maneno yote Mungu anayokwisha kufanya na atakayofanya kwa viungo vyote vya mwili wa Kristo tuliyosoma ndani ya mashairi 3-14.

Nikikwisha kusikia habari za imani katika Bwana Yesu iliyo katikati yenu, na munayoonyeshea watakatifu wote. Wakati Paulo alipokwisha kusikia habari hizi juu yao, aliamini kabisa ya kwamba walikuwa wamepokea baraka hizi za roho, na aliwaombea. Kwa njia ya **imani yao ndani ya Bwana Yesu** walipokea ajabu ya wokovu. **Mapendo yao kwa watakatifu wote** yalionyesha kwamba walikuwa wameokolewa kweli.

Walimu wengine wa Biblia wanafikiri shairi hili linaonyesha kwamba barua hii haikuandikwa kwa Waefeso peke yao. Paulo alisema hapa juu ya imani ya wasomaji wake, sawasawa hakukutana nao mbele. Lakini alikuwa ameshinda miaka mitatu au zaidi katika Efeso (Mdo. 20:31). Hivi wanafikiri kwamba barua hii ilitumwa kwa makanisa mengine vilevile.

Hata kama hatujui jibu la ulizo hili kabisa, shairi hili linatufundisha maneno mengine. Neno moja tunaloona ni kwamba inatupasa kutia **imani ndani ya Bwana Yesu**. Hatuagizwi kwamba tunapaswa kuamini kanuni ya imani fu-

lani, ndani ya kanisa, au ndani ya Wakristo. Lazima imani yetu ya wokovu iwe ndani ya Kristo tu aliyefufuliwa, na kutukuzwa kwa mkono wa kuume wa Mungu.

Neno lingine ambalo inatupasa kuji-funza ndani ya shairi hili ni juu ya **mapendo yenu munayoonyeshea watakatifu wote**. Haifai tupende watakatifu wa kanisa letu tu, lakini wote wanaokwisha kusafishwa na damu ya Kristo, ndio wote walio wa jamaa ya imani.

Neno la tatu ni juu ya **imani na mapendo** pamoja. Watu wengine wanasema wana imani, lakini ni nguvu kuona mapendo ndani ya maisha yao. Watu wengine wanasema wana mapendo makubwa, lakini hawaweki roho juu ya hitaji la kuamini Kristo. Ndani ya maisha ya Wakristo wa kweli mafundisho mazuri na mwenendo mzuri yanafungana pamoja.

1:16 Imani na mapendo ya waamini yalisukuma Paulo kusifu Bwana na kuwaombea bila kuacha.

1:17 Ni baraka kubwa kwa sisi kuweza kusoma kidogo juu ya maisha ya maombi ya mtu huyu wa Mungu, hapa, na kwa 3:14-21. Ombi lake hapa kwa shairi 17 ni wapewe hekima na ufunuo wa roho, ombi la pili, kwa 3:14-21, ni waweze kupewa nguvu kwa Roho. Ombi la kwanza ni kwa **Mungu**; ombi la pili ni kwa Baba. Kila mara Paulo aliomba bila kuacha, na juu ya mahitaji ya watu kwa wakati ule. Hapa ndani ya shairi 17 aliomba kwa **Mungu wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba ya utukufu**.

Labda maana ya **Baba ya utukufu** ni ya kwamba Mungu ni:

1. Mwanzo wa utukufu,
2. au Mwenye utukufu wote,
3. au Baba wa Bwana Yesu Kristo, aliye ufunuo wa utukufu wa Mungu.

Aliendelea kuomba Mungu **awape**

ninyi roho ya hekima na ya ufunuo katika kumjua yeye. Roho Mtakatifu ni **Roho ya akili** (Isa. 11:2), na **ufunuo** (1 Kor. 2:10). Lakini kwa sababu kila mwamini anakaliwa naye, Paulo haombi hapa wasomaji wake wapokee Roho Mtakatifu, lakini waweze kupewa mwanagaza toka kwake.

Ufunuo ndio kuleta elimu; **hekima** ni juu ya namna gani kutumika na ufunuo huu ndani ya maisha yetu. Paulo hakufikiri hapa juu ya kujua maneno yo yote, lakini juu ya **kumjua yeye** (Kiyunani *epignosis*). Alitaka waamini **kujuana na Mungu karibu karibu** rohoni mwao. Neno hili haliwezekani kwa njia ya elimu tu, lakini kwa utumishi wa neema ya Roho Mtakatifu.

1:18 Tumeona ya kwamba mwanga-za ya roho inatoka kwa Mungu; inatufikia kwa njia ya Roho Mtakatifu; na kusudi lake ni tuweze kujua Mungu sana. Sasa tunasoma juu ya viungo vya mwili vinavyotiwa nuru: **macho ya miyo yenu yatiwe nuru**.

Mfano huu unatufahamisha kwamba kwa kufahamu maneno ya Mungu tunahitaji **miyo** ya upole na huruma, hata kupita akili kubwa. Mungu anafunua kweli zake kwa wale ambao wanampenda. Asante kwa sababu baraka hizi si kwa wenye akili nyangi tu, lakini kwa sisi sote, kwa sababu sisi sote tunaweza kuwa na **miyo** ya mapendo.

Halafu Paulo alitaja maneno matatu anayotaka kwa watakatifu:

1. **tumaini la kuita kwake**
2. **wingi wa utukufu wa uriti wake katika watakatifu**
3. na ukubwa kupita wa uwezo wake kwetu tunaoamini.

Tumaini la kuita kwake linatazamia wakati wa kuja; ni maneno aliyokusudi kwa sisi wakati alipotuita, na ya kwamba tutakuwa pamoja na Kristo na sawasawa naye kwa milele. Tutaonye-

shwa kwa ulimwengu kama wana wa Mungu, na kutawala pamoja naye kama bibi arusi yake bila kipako. Hili ni tumaini letu. Si kusema ya kwamba tuna shaka juu yake. Tunajua ni sehemu ya wokovu wetu usiotimizwa bado na tunayotazamia.

Wingi wa utukufu wa uriti wake katika watakatifu ni maneno makubwa sana inayopasa waamini kutafutia. Ona namna Paulo alivyooingeza maneno kuonyesha ukubwa na utukufu:

Uriti wake

Uriti wake katika watakatifu
Utukufu wa uriti wake katika watakatifu

Wingi wa utukufu wa uriti wake katika watakatifu

Kuna njia mbili kwa sisi kufahamu maneno haya. Njia hizi mbili zote zina maana kubwa kwa sisi, hata tutazionyesha mbili zote. Njia ya kwanza inatuonyesha kwamba **watakatifu** ni **uriti wake**, naye anafikiri juu yao kama hazina ya faida isiyoweza kufananishwa. Ndani ya Tito 2:14 na 1 Petro 2:9, waamini wanaitwa “mali ya Mungu mwenyewe.” Habari hizi zinaonyesha neema kubwa sana iliyowezesha Mungu kupokea moyoni mwake wenye zambi wasiostahili hata kidogo, wapotovu, waliookolewa kwa njia ya Kristo, na kuwaita **uriti wake**.

Elezoo la pili ni ya kwamba **uriti** ndio mambo yote ambayo *sisi* tutariti. Ni ulimwengu mzima unaotawaliwa na Kristo, na sisi, bibi arusi yake, tukiutawala pamoja naye. Kama tukifahamu kweli utajiri wa utukufu wa vyote ambayo ametutayarisha, mambo ya kuendeza na furaha za dunia hii zitakuwa kitu bure kwasi.

1:19 Ombi la tatu la Paulo kwa watakatifu lilikuwa waweze kufahamu sana na kutambua **uwezo** amba Mungu alitumia ili maneno haya yote yafanyikane: **ukubwa wa kupita wa**

uwezo wake kwetu tunaoamini.

F. B. Meyer alisema, “Ni *uwezo*. Ni *uwezo wake*. Ni *uwezo mkubwa*. Uwezo wa kipimo kidogo kupita hiki haukutoshia. Ni *uwezo mkubwa kupita* mafikiri yetu.”⁴

Huu ndio uwezo Mungu aliotumia kwa ukombozi wetu, anaotumia kwa kuttulinda, na atakaotumia kwa wakati wa kuja kwa kutukuzwa kwetu. Lewis Sperry Chafer aliandika:

Paulo alitaka mwamini kushangazwa na ukubwa wa uwezo uliofanya kazi ili yeye aweze kufanyizwa kila kitu ambacho Mungu alikusudi kwa njia ya mchaguzi, na kuwekwa kama mwana.⁵

1:20 Kwa kuonyesha kupita ukubwa wa uwezo huu, mtume aliendelea kusema juu ya onyesho kubwa zaidi la **uwezo** wa Mungu duniani tangu zamani. Ulikuwa uwezo **uliofufua** Kristo **toka wafu** na kumkalisha juu ya kiti cha kifalme kwa **mkono wa kuume** wa Mungu. Labda sisi tungefikiri kuumbwa kwa ulimwengu kungeonyesha uwezo wa Mungu zaidi. Au ajabu la kuponyesha watu wake saa ya kuwatambusha Bahari Nyekundu. Sivyo! Agano Jipyainafundisha kwamba **ufufuko wa Kristo** na kwenda kwake mbinguni kulihiataji uwezo mkubwa kupita wote wa Mungu!

Ilikuwa hivi kwa sababu gani? Ni kama majeshi yote ya gehena yalifungana pamoja kuzuiza makusudi ya Mungu kwa njia ya kuchunga Kristo kaburini, au kumzuiza asipande mbinguni nyuma ya kufufuliwa. Lakini Mungu alishinda mazuizo yote. Shetani na majeshi yake walishindwa kabisa wakati Kristo alipofufuka na kupanda mbinguni, na kushinda kwa Mungu na utukufu kulionekana wazi.

Hakuna mtu anayeweza kueleza uwezo mkubwa namna hii, “**ukubwa wa kupita wa uwezo wake kwetu tu-**

naoamini, kwa kadiri ya utendaji wa nguvu wa uwezo wake aliotenda katika Kristo, wakati alipomfufua toka wafu.” Tushangae juu ya ukubwa wa kupita wa uwezo huu, na kuabudu Mungu kwa enzi yake!

Ufufuko wa Kristo ulikuwa ufufuko wa kwanza namna hii duniani tunao-soma juu yake ndani ya Biblia (1 Kor. 15:23). Kulikuwa na watu wengine waliofulufiwa toka wafu, lakini walikufa tena. Bwana Yesu alikuwa wa kwanza asiyekufa tena nyuma ya kufufuliwa. Nyuma ya ufufuko wa Kristo na kwenda kwake mbinguni, Mungu **alimkalisha kwa mkono wake wa kuume katika pahali pa mbingu. Mkono wa kuume** wa Mungu ni pahali pa mapendeleo (Ebr. 1:13), uwezo (Mt. 26:64), heshima (Ebr. 1:3), furaha (Zab. 16:11), na mamlaka (1 Pet. 3:22).

Mungu alimkalisha **katika pahali pa mbingu.** Maneno haya yanaonyesha pahali hapa ni kao la Mungu. Bwana Yesu ni pale leo vilevile, mwenye mwili wa nyama na mifupa, mwili unaokwisha kutukuzwa, mwili usioweza kufa tena. Nyuma kidogo sisi vilevile tutakuwa pahali alipo sasa.

1:21 Mwokozi wetu ametukuzwa hata kupita, na tunasoma kwamba ye ye ni **juu sana kuliko utawala wote na mamlaka na nguvu na usultani, na kila jina linalotajwa, si katika ulimwengu huu tu, lakini vilevile katika ule utakaokuja.** Bwana Yesu ni juu kupita kila mtawala au mwenye amri, mtu au malaika, sasa na kwa milele.

Katika pahali pa mbingu kuna madaraja mbalimbali ya malaika, malaika wabaya na wema. Wana kipimo mbalimbali cha uwezo, kufanana na watawala na serikali ya dunia. Si neno kama wakiwa na **uwezo na mamlaka** nyingi, Kristo ni **juu sana** kuliko wote.

Na neno hili si **kweli katika ulimwengu huu wa sasa tu, lakini vilevile kwa wakati wa kuja,** ndio wakati wa uta-

wala wa Kristo kwa miaka elfu moja duniani. Kwa wakati ule atakuwa Mfalme wa wafalme wote na Bwana wa wabwana wote. Atatukuzwa kupita vi-umbe vyote pia.

1:22 Zaidi ya ile, Mungu **ameweka vitu vyote** vilivyoumbwa **chini ya miguu yake.** Hana amri juu ya watu na malaika tu, lakini juu ya viumbe vyote vingine vilevile, vyenye uzima au vina-vyokosa uzima. Mwandishi wa kitabu cha Waebrania anatukumbusha kwamba hatuoni bado vitu vyote chini yake sasa (Ebr. 2:8). Hata Kristo akiwa na mamlaka yote sasa, hatumiki na mamlaka hii kwanza sasa. Watu wanakaa kumwasi na kumkana au kushindana naye. Lakini Mungu ameamuru ya kwamba kwa wakati wa kuja Mwana wake atakuwa na mamlaka juu ya ulimwengu mzima.

Maneno tutakayosoma sasa ni karibu kutushinda kuamini. Huyu mwenye alama za misumari ndani ya mikono yake atakuwa mwenye mamlaka juu ya ulimwengu mzima. Paulo alikuwa amefunua siri sehemu sehemu, habari za ufufuko, kutukuzwa, na utawala wa Kristo. Mungu ameleta Huyu mwenye utukufu **kwa kanisa!** Ni ufunuo wa kutushangaza. Tungali tunastaajabu juu ya neno hili, Paulo alisema kwamba Mungu ameweke Kristo, aliye **juu ya vitu vyote, kwa kanisa.**

Kama tukisoma shairi hili mbiombio bila kuwaza sana, labda tungefikiri linasema Kristo ni Kichwa **cha kanisa.** Neno hili ni kweli, lakini zaidi ya ile linasema kwamba **kanisa** linaunganishwa karibu sana na Kristo aliye na mamlaka kutawala ulimwengu mzima.

Ndani ya shairi 21 tulijifunza kwamba Kristo ni juu kupita kila kiumbe mbinguni na duniani, kwa wakati wa sasa, na wakati wa kuja. Kwa mwanzo wa shairi 22 tulijifunza ya kwamba **vitu vyote** na viumbe vyote vilivyoumbwa ni **chini ya miguu yake.** Sasa tunajifunza

ya kwamba **kanisa** linaitwa kuunganishwa naye katika utawala wake usio na mpaka. **Kanisa** litashiriki ndani ya utawala wake. Viumbe vyote vingine vitatawaliwa naye.

1:23 Ndani ya shairi hili la mwisho la sura 1, tunajifunza juu ya ukaribu wa ufungu wa Kristo na kanisa. Tunaona kwamba kanisa ni **mwili wake**; vilevile ni **utimilifu wake anayetimiza vyote katika vyote**.

Hakuna ushirika unaoweza kuwa karibu kupita kichwa na **mwili**. Wao ni mwungano hai mmoja na wanakaliwa na Roho mmoja. Kanisa ni kundi la watu wanaoitwa toka mbalimbali duniani, tangu Pentekote kufika wakati Kristo atakapokuja kwa kanisa. Ni watu wa-naokolewa kwa neema ya ajabu ya Mungu na kupewa mapendeleo ya kuwa **mwili** wa Kristo. Hakuna jamii nyingine ya waamini tangu zamani, na kwa wakati wa kuja watakaokuwa na heshima hii.

Neno la pili tunalosoma juu ya kanisa ni ya kwamba ni **utimilifu wake anayetimiza vyote katika vyote**. Maana yake ndiyo kwamba kanisa ni kitimizo cha Kristo, aliye pahali po pote kwa kila saa. Kama mwili ni kitimizo cha kichwa, vivyo hivyo kanisa ni kitimizo cha Kristo.

Lakini haifai watu kufikiri kwamba Kristo hakutimia kwa njia yo yote, hivi Paulo anaongeza mara moja, **utimilifu wake anayetimiza vyote katika vyote**. Bwana Yesu hahitaji kitu, lakini ni ye ye **anayetimiza vyote** na kutimiza mahitaji yote ya ulimwengu.

Ndiyo, inatoshinda sisi watu kufahamu maneno haya. Tunaweza kushangaa tu juu ya nia na shauri la ajabu la Mungu, pamoja na kukubali kwamba hatuwezi kulifahamu.

D. Wokovu wa Mataifa na Wayuda unaonyesha uwezo wa Mungu (2:1-10)

2:1 Kwa mwisho wa sura 1 tulisoma

juu ya uwezo mkubwa wa Mungu uki-fufua Kristo toka kaburi na kumtia taji ya utukufu na heshima. Kwa mwanzo wa sura 2 tunaona namna uwezo ule umetumika ndani ya maisha yetu vilevile, ukitupandisha toka mauti ya roho na kutukalisha ndani ya Kristo katika pahali pa mbingu.

Mashairi haya yanafanana na sura ya kwanza ya Mwanzo. Yanaonyesha kwanza ukiwa, machafuko, na uharibifu (Mwa. 1:2a; Efe. 2:1-3). Nyuma yake tunaona uwezo wa Mungu (Mwa. 1:2b; Efe. 2:4); kisha muumbo wa uzima mpya (Mwa. 1:3-31; Efe. 2:5-22).

Kwa mwanzo wa Waefeso 2 sisi ni maiti kwa maneno ya roho. Kwa mwisho wa sura hii tunakalishwa ndani ya Kristo katika pahali pa mbingu, na zaidi ya ile sisi ni kao la Mungu kwa njia ya Roho. Nyuma ya mwanzo na mbele ya mwisho wa sura hii, ajabu ya uwezo mkubwa ilitugeuza kabisa.

Mashairi 1-10 yanapasha habari za wokovu wa Mataifa na Wayuda, toka umasikini wao kupewa utajiri tele, kwa uwezo wa Mungu.

Ndani ya mashairi 1 na 2 Paulo alikumbusha wasomaji wake Mataifa kwamba mbele ya kuokolewa kwa walikuwa **wafu** kwa sababu ya **Makosa na zambi** zao. Hawakuwa na uzima wa roho, wala mwungano na Mungu, na waliishi bila kufikiri kuna Mungu. **Makosa na zambi** zilizaa mauti. **Zambi** ni matendo mabaya namna yo yote mtu anayotenda na kujua, au bila kujua, na mawazo, masemo, au matendo yasi-yopendeza Mungu. **Makosa** ni zambi ambazo mtu anatenda kuvunja sheria watu wanayojuwa.

2:2 Waefeso walikuwa wapotovu na wafu mbele. **Walitembea kufuata desturi za dunia** hii na kuzama ndani ya matendo ya udanganyifu, uasherati, jeuri na uasi.

Zaidi ya ile, mwenendo wao ulikuwa mwovu sana. Waliiga Shetani, **mfalme**

wa uwezo wa anga. Waliongozwa na mkubwa wa pepo wabaya katika anga. Walikubali kutii mungu wa muda huu. Neno hili linaleza kwa sababu gani mara nyingi mwenendo wa wasioamini ni mwovu sana, hata mbaya kupita matendo ya nyama.

Mwishoni walikuwa waasi, na walitembea sawasawa na **roho yule anayetenda kazi sasa ndani ya wana wa kuasi.** Wasioamini wote ni **wana wa kuasi** wanaoasi Mungu. Shetani anawapa nguvu, na hivi wanashindana na Mungu, wanamwasi na kutokumhe-shimu.

2:3 Ndani ya shairi hili Paulo aligeuka, na kwa pahali pa kusema *ninyi* ananza kusema *sisi*. Neno hili linaonyesha kwamba kuanza saa ile alisema zaidi kwa waamini Wayuda (lakini maneno aliyosema ni kweli vilevile kwa kila mtu asiyeokolewa bado.) Maneno matatu yanaonyesha hali yao. Wao ni wenye tamaa ya mwili, wapotovu, na wahukumiwa.

Katikati yao sisi sote tulishi vile-vile, katika tamaa za mwili wetu. Paulo na ndugu zake Wakristo walitembea vilevile katikati ya wana wa kuasi mbele ya kuzaliwa tena. Waliishi katika *tamaa za mwili*, wakiweka roho juu ya kupendeza mwili tu. Paulo aliishi maisha mema mbele ya watu, lakini sasa alifahamu kwamba alikuwa akijipe-ndeza mwenyewe tu. Na hali ya roho yake ilikuwa mbaya kupita matendo yake.

Wayuda wasiookolewa bado walikuwa *wapotovu* vilevile, **wakifanya mapenzi ya mwili na ya nia. Mapenzi ya mwili na ya roho** yanaweza kuwa maneno mazuri au maovu. Hapa ni zaidi zambi za mwili. Na ona ya kwamba Paulo alisema juu ya zambi za mawazo na ya matendo vilevile.

Masemo ya mwisho ya Paulo juu ya Wayuda wasiookolewa bado ni ya kwamba walikuwa **kwa tabia wana wa**

kasirani, kama wale wengine. Wali-elekea kuwa na kasirani, uovu, uchungu, na kasirani kama watu wote wengine. Nao ni chini ya **gazabu** ya Mungu vilevile na wanahukumiwa kufa. Ona ya kwamba tunasoma juu ya adui tatu za watu ndani ya mashairi 2 na 3: dunia (sh. 2), Shetani (sh. 2), na mwili (sh. 3).

2:4 Lakini Mungu – maneno haya mawili ni maneno yenye maana kubwa zaidi ndani ya maandiko yote ya dunia. Yanatuondosha katika maangamizi na ukosefu wa tumaini ya bonde la mauti, na kutufikisha kwa furaha kubwa tele ya ufalme wa Mwana mpendwa wa Mungu.

Mungu mwenyewe alileta mabadi-lisho haya. Yeye peke yake *aliweza kufanya hivi*, na hakuna mwingine *angalifanya hivi*.

Mungu huyu mbarikiwa ni **mwenye rehema nyingi.** Anatuonyeshea **rehema** kwa njia ya kutotutendea namna tunavyostahili (Zaburi 103:10). Hata kama ametendea watu na rehema kwa miaka elfu sita, rehema yake haipunguki.

Mungu alifanya hivi **kwa mapendo yake makubwa ambayo alitupenda sisi.** Mapendo yake ni makubwa kwa sababu yeye mwenyewe ni mkubwa. Kupendwa na mwenye enzi wa uwezo wa ulimwengu ni vizuri kupita ku-pendwa na mtu. Mapendo ya Mungu ni makubwa kwa sababu ya bei aliyolipa. Ni mapendo yaliyotuma Bwana Yesu, Mwana wa pekee wa Mungu, kufa na maumivu makubwa kwa ajili yetu kwa Kalvari. Mapendo ya Mungu ni makubwa kwa sababu yanatumwangia utajiri usiotafutikana.⁶

2:5 Na mapendo ya Mungu ni makubwa kwa sababu wenye kuyapokea hawastahili hata kidogo. **Tulikuwa wa-fu kwa sababu ya makosa yetu.** Tulikuwa adui za Mungu. Tulikuwa masikini na bila heshima. Alitupenda hata hivi.

Kwa sababu ya mapendo ya Mungu kwasi, na kwa sababu ya kazi ya uko-

mbozi ya Kristo, (1) **alitupatiza uzima pamoja na Kristo**; (2) alitufufua pamoja naye; na (3) kutukalisha ndani yake.

Maneno haya yanaonyesha hali yetu ya roho kwa sababu ya umoja wetu naye. Alitenda hivi kama badala yetu – si *kwa ajli* yetu tu, lakin *kama* sisi. Hivi wakati alipokufa, sisi tulikufa. Wakati alipozikwa, sisi tulizikwa.

Wakati *Yeye alipopatizwa uzima*, alifufuliwa, kunyanyuliwa, na kukalishwa kwa pahali pa mbinguni, *sisi* vivyo hivyo. Tunafurahishwa na kubarikiwa na faida yote ya zabihu yake kwa sababu ya umoja wetu naye. Maana ya **kupatizwa uzima pamoja naye** ni ya kwamba waamini Wayuda na Mataifa wanaunganishwa naye katika uzima mpya. Uwezo ambao ulimfufua *Yeye* na kumpa uzima, ulifanya vivyo hivyo na sisi.

Mawazo haya yалишангаzа Paulo sana sana hata alisema kwa sauti kubwa, **Mumeokolewa kwa neema**. Ali-shindwa kabisa na mawazo ya **neema** kubwa ya Mungu kwa watu wasiostahili hata kidogo!

Tumesema mbele ya kwamba maana ya rehema ni kwamba hatupokei azabu tunayostahili kupokea. Maana ya **neema** ni kwamba *tunapokea* wokovu tusio-stahili kupokea. Tunaupokea kama zawi, si kama mshahara. Na tunaupokea toka Mungu asiyelazimishwa kuutoa. Ni mapendo ya Mungu bila kipimo kwa wamasikini wenye zambi.

2:6 Hatukupewa uzima tu pamoja na Kristo. **Tumefufuliwa** pamoja naye vilevile. Hatakufa na kuhukumiwa tena, na maneno haya hayatatupata sisi tena vilevile. Tunasimama kwa mahali ya ufufuko ngambo ya kaburi kwa sababu tumefungana naye. Na kwa sababu hii ingetupasa sisi kuishi namna inavyofaa kwa watu waliokuwa wafu mbele, na wanaokwisha kupata uzima.

Neno lingine juu ya mahali petu ni ya kwamba tunakalishwa pamoja naye

katika pahali pa mbingu katika Kristo. Kwa njia ya kufungana naye ni kama tunakwisha kuponyeshwa toka dunia hii bovu na tunaketishwa **katika Kristo** katika utukufu hata sasa. Mungu anatuona hivi. Kama tukijitwalia hali hii kwa imani, neno hili litageuze maisha yetu. Hatutafungwa tena na maneno ya dunia yasiyo na faida na yaliyo kwa wakati tu. Tutatafuta maneno yaliyo juu, pahali Kristo anapoketi kwa mkono wa kuume wa Mungu (Kol. 3:1).

Maneno makubwa ndani ya mashairi 5 na 6 ni, **katika Kristo Yesu**. Ni ndani yake tumepewa uzima, kufufuliwa, na kukalishwa katika pahali pa mbingu. Yeye anasimama badala yetu, hivi kushinda kwake na hali yake ni yetu. George Williams alisema, “Ni mshangao kufikiri kwamba watu namna ya Maria Magdalene, na mwizi aliyesulibishwa watakuwa pamoja na Mwana wa Mungu katika utukufu.”

2:7 Ajabu hili la neema litakaa kufunuliwa kwa milele. Kwa muda bila mwisho Mungu atakaa kufunua kwa makutano ya mbingu bei kubwa aliylipa kutuma Mwana wake kwa dunia hii mbovu ya zambi, na bei kubwa Bwana Yesu aliylipa kwa zambi zetu msalabani. Ufunuo huu hautakwisha kamwe. Paulo alipanga masemo juu ya masemo kuonyesha ukubwa wake:

**Wema wake kwetu
Neema yake kwa wema wake kwetu
Kupita kiasi wa neema yake kwa
wema wake kwetu
Wingi wa kupita kiasi wa neema
yake kwa wema wake kwetu**

Hivi kama Mungu atakaa kufunua maneno haya kwa milele, sisi tutakaa kuyajifunza kwa milele na milele. Mbingu zitakuwa chuo chetu. Mungu atakuwa mwalimu wetu. Atatufundisha juu ya **neema** yake. Sisi tutakuwa wanafunzi wake. Muda wa chuo utaendelea kwa milele.

Habari hizi zinatuzuiza tuiswaze kwa-mba tutakwisha kujua maneno yote wakati tutakapofika mbinguni. Mungu tu anajua maneno yote, nasi hatutakuwa kamwe sawasawa naye.

Basi tutajua maneno gani wakati tutakapofika mbinguni? Labda tutaweza kujitayarisha kwa université ya mbingu kwa njia ya kuweka saa nydingi sasa kujifunza Biblia.

2:8 Mashairi 8-10 yanaeleza njia ya wokovu wazi kupita mashairi yote mengine ndani ya Biblia. Elezo hili linaanza na **neema** ya Mungu. Ni yeze anayeeleza habari hizi. Watu wasiostahili hata kidogo wanapewa wokovu, kwa njia ya Bwana Yesu Kristo na kazi yake.

Wanapewa wokovu sasa. Watu wanaweza kujua kwamba wamepokea wokovu. Paulo aliandika kwa Waefeso, **Mumeokolewa**. Alijua kwamba waliokolewa, nao walijua neno hili vilevile.

Tunapokea zawadi ya uzima wa milele **kwa njia ya imani**. Maana ya **imani** ni ya kwamba mtu anakubali kwamba yeze ni mwenye zambi, mpotevu, na anapokea Bwana Yesu kama tumaini lake la pekee kupokea wokovu. Imani yenye kuokoaa inapatana na ahadi ya mtu kufungana na Mtu, ndiye Yesu.

Neno hili halikutoka ndani yenu wenyewe. Maneno haya yanaonyesha wazi kwamba mtu hawezi kamwe kustahili kupokea wokovu kwa njia ya kazi yake mwenyewe. Wafu hawawezi *kufanya* kitu, na wenye zambi *wanastahili azabu* tu.

Wokovu ni zawadi ya Mungu. Zawadi ni bila bei na bila masharti. Mungu anatolea watu wokovu kwa njia hii tu. **Zawadi ya Mungu ni wokovu kwa neema, na kwa njia ya imani.** Anataka watu wote pahali pote kuupokea.

2:9 Si kwa matendo, maana si kitu

mtu anachowenza kupata kwa njia ya kazi yake. Hawezi kuupokea kwa njia ya:

1. Kupokewa kanisani
2. Ubatizo
3. Kuwa mtu wa kanisa
4. Kufikia kanisa
5. Meza ya Bwana
6. Kujaribu kutii amri kumi.
7. Kutii mafundisho ya Yesu mlimani
8. Kutoa zawadi kusaidia wenye mahitaji
9. Kuwa jirani mzuri
10. Kuishi maisha safi na ya heshima

Watu hawaokolewi kwa njia ya **kazi** zao. Na *hawaokolewi* kwa njia ya imani *pamoja na kazi*. **Wanaokolewa kwa njia ya imani peke yake**. Ukiongeza kazi yo yote, na kipimo cho chote cha kazi, kwa kupokea uzima wa milele, wokovu huu si kwa neema tena (Rom. 11:6). **Kazi** zinakatazwa kabisa ili watu wasiwe na njia ya kujisifu. Mtu akiweza kuokolewa kwa njia ya **kazi** yake, ana-pata njia **kujivuna** mbele ya Mungu. Neno hili haliwezekani (Rom. 3:27).

Kama mtu angaliweza kuokolewa na kazi zake njema, mauti ya Kristo yasingalihitajiwa (Gal. 2:21). Lakini tunajua alikuwa kwa sababu njia nydingine hai-kuwa kwa wenye zambi kuokolewa.

Kama mtu angaliweza kuokolewa na kazi zake njema, angalikuwa mwokozi wake mwenyewe, na angaliweza kuji-abudu mwenyewe. Kufanya hivi kunga-likuwa ibada ya sanamu, ndilo neno linalokatazwa na Mungu (Kut. 20:3).

Kama ingaliwezekana kwa mtu kuokolewa kwa njia ya kuamini Kristo *pamoja* na kazi zake njema, mtu huyu angalikuwa na waokozi wawili – Yesu na mwenye zambi. Neno hili hali-wezekani. Ingalipasa Kristo kushiriki na mtu utukufu wa kuwa Mwokozi, na hatafanya hivi (Isa. 42:8).

Mwishoni, kama mtu angaliweza ku-saidia kupokea wokovu kwa njia ya kazi

zake, Mungu angalikuwa na deni kwake. Neno hili vilevile haliwezekani. Mungu hawezu kuwa na deni karibu na mtu ye yote (Rom. 11:35).

Imani ni namna nyingine na kujisifu (Rom. 3:27) kwa sababu imani haina ustahili. Hakuna sababu kwa mtu kujisifu kwa sababu aliamini Bwana. Kuamini Bwana ni kitu cha akili zaidi mtu anachowenza kufanya. Kwa mtu kuamini Mwumba na Mkombozi wake ni neno la peke la akili. Kama tuisipeweza kumwamini yeye, basi tutamini nani?

2:10 Kwa sababu ya wokovu **sisi ni kazi yake**. Tuliumbwa na Mungu. Hatukujiumba wenyewe. Mwamini aliyezaliwa tena ni kazi bora ya Mungu. Ni muumbo mpya kwa njia ya kufungana na Kristo, kwani “kama mtu akiwa ndani ya Kristo, yeye ni kiumbe kipyta; maneno ya zamani yamepita; tazama, maneno yote yamekuwa mapya” (2 Kor. 5:17).

Kusudi la muumbo huu ni tutende **matendo mema**. Ndiyo, hatukuokolewa *kwa njia ya matendo mema*, lakini tunaoolewa *kusudi tutende matendo mema*. **Matendo mema** si *msingi* lakini *matunda*. Hatufanyi kazi njema *kusudi tuweze kuokolewa*, lakini *kwa sababu tumeokolewa*.

Tunaona kweli hii katika Yakobo 2:14-26. Yakobo alisema “imani, isipo-kuwa na matendo imekufa.” Hakutaka kusema kwamba tunaokolewa kwa njia ya imani pamoja na matendo, lakini ya kwamba kwa njia ya imani inayozaa maisha ya **matendo mema**. **Matendo mema** yanahakikisha kwamba imani yetu ni imani ya kweli. Paulo alipatana na mafundisho haya na alisema: **sisi ni kazi yake, tuliumbwu katika Kristo Yesu ili tutende matendo mema**.

Hivi utaratibu wa Mungu ni hivi:

Imani – Wokovu – Matendo Memu –
Zawabu.

Imani ni njia ya kupata wokovu. Matunda ya wokovu ni **matendo mema**. Mungu ataleta zawabu kwa matendo mema.

Tunaweza kuuliza: Inatupasa kutenda matendo mema ya namna gani? Paulo alijibu, **Matendo mema Mungu aliyo-tengeneza mbele ili tutembee ndani yao**. Ni kusema, Mungu ana ramani kwa maisha ya kila mtu. Hata mbele ya wokovu wetu alifanya shauri namna gani tutamtumikia. Ni kazi yetu kutambua kama mapenzi yake kwa maisha yetu ni nini, na kuyatii. Hatuhitaji kufanya shauri sisi wenyewe kwa maisha yetu, lakini kufahamu tu kama kusudi lake kwa maisha yetu ni nini. Kwa njia hii hatutakaa kufazaika na kusumbuka, lakini maisha yetu yatamtukuza zaidi, yatakuwa baraka kwa watu wengine, na sisi tutapokea zawabu kubwa zaidi.

Kwa kufahamu kama Mungu alikusudi **matendo mema** gani kwa sisi mmoja mmoja kufanya, sharti:

- (1) tukiri na kuacha kila zambi mara moja wakati tunapokwisha kufahamu tumekosa;
- (2) tujitoe saa zote na bila kizuizo kwa yeye;
- (3) tujifunze Neno la Mungu tuweze kutambua mapenzi yake, na kuyatii;
- (4) kushinda katika maombi kila siku;
- (5) kumtumikia kila mara tunapopata njia;
- (6) kuwa na ushirika, na kushauriana na Wakristo wengine.

Mungu anatutayarisha kwa kufanya **matendo mema**. Anatayarisha **matendo mema** kwa sisi kufanya. Kisha anatupa zawabu wakati tunapoyafanya. Hii ndiyo neema yake kubwa!

E. Umoja wa waamini Wayuda na Mataifa ndani ya Kristo (2:11-22)

Ndani ya mwanzo wa sura 2 Paulo alipasha namna gani watu mmoja mmoja wa Mataifa na Wayuda wana-

okolewa. Sasa anaendelea kusema juu ya ondoleo la tofauti ya makabila yao, na juu ya kufungana kwao ndani ya Kristo, na kufungamizwa kwao kuwa kanisa, hekalu takatifu katika Bwana.

2:11 Ndani ya mashairi 11 na 12 mtume anakumbusha wasomaji wake ya kwamba mbele ya kuokolewa walikuwa **Mataifa** kwa njia ya kuzaliwa, na kwa sababu hii walikataliwa na Wayuda. Walizarauliwa na Wayuda na kuitwa **Wasiotahiriwa**. Maana yake ni ya kwamba hawakukatwa mwilini na alama iliyoonyesha ya kuwa Waisraeli walikuwa watu wa agano wa Mungu. Jina hili “wasiotahiriwa” lilikuwa jina la kuzarau, namna watu wanavyoita watu wa kabilia zarauliwa lingine mara nyingine kwa wakati wa sasa. Tunaweza kusikia kuzarau namna hii ndani ya sauti ya Daudi wakati aliposema juu ya Goliata aliye kuwa mtaifa, “Mfilistini huyu asiyetahiriwa ni nani, hata atukane jeshi la Mungu wa uzima?” (1 Sam. 17:26).

Lakini Wayuda walijiita **Waliotahiriwa**. Walijisifu juu ya jina hili. Lilionyesha kwamba walikuwa watu wa chaguliwa wa Mungu hapa duniani, mbali na mataifa yote mengine. Ni kama Paulo hakufurahi juu ya kujisifu kwao, akasema tohara yao **ilifanyika kwa mikono**, maana ilikuwa kwa mwili tu. Hata kama walikuwa na alama iliyonekana kwa watu kwamba walikuwa watu wa agano la Mungu, hawakuwa na imani na kweli rohoni ndani ya Bwana. “Maana yeye si Myuda aliye Myuda kwa inje tu, wala tohara si ile ya inje tu katika mwili; lakini yeye ni Myuda aliye Myuda kwa ndani, na tohara ni ya moyo, katika roho, si katika maandiko, na sifa yake haitoki kwa watu, lakini kwa Mungu” (Rom. 2:28, 29).

Lakini hata kama Wayuda walitahiriwa rohoni au sivyo, tunaona ndani ya shairi 11 ya kwamba walifikiri wao

walikuwa watu wazuri zaidi, na Mataifa walizarauliwa. Uadui huu wa Wayuda na Mataifa ulikuwa tofauti kubwa zaidi kwa maneno ya taifa na dini duniani tangu zamani. Myuda alikuwa na mapendeleo makubwa mbele ya Mungu (Rom. 9:4, 5). Mataifa alikuwa mgeni. Akitaka kuabudu Mungu wa kweli kwa njia iliyofaa, ilimpasa kushika dini ya Wayuda (kama Rahaba na Ruta). Hekalu la Wayuda kwa Yerusalem lilikuwa pa-hali pa pekee duniani Mungu alipoweza jina lake, na pahali watu walipoweza kumkaribia. Azabu kwa Mataifa walio-ingia viwanja vyta ndani vyta hekalu ilikuwa mauti.

Wakati Bwana Yesu aliposema na mwanamke wa mahali ya Tiro na Sidoni, Bwana Yesu alipima imani yake kwa njia ya kusawanisha Wayuda na watoto wa nyumba, na Mataifa na mbwa wadogo chini ya meza. Mwanamke alikubali kwamba alikuwa imbwa mdogo tu, lakini aliomba kupewa vipande vidogo vyta chakula tu ambavyo watoto waliweza kuacha kuanguka chini. Alipewa zawabu kwa sababu ya imani yake (Mk. 7:24-30). Hapa ndani ya Waefeso 2:11 mtume alikumbusha wasomaji ya kwamba walikuwa Mataifa mbele, na kwa sababu hii walizarauliwa.

2:12 Mataifa walikuwa **mbali na Kristo**: hawakuwa na Masiya. Mungu aliahidi Masiya kwa taifa la Israeli. Mataifa watabarikiwa kwa njia ya Masiya (Isa. 11:10; 60:3), lakini atazaliwa Myuda atumikie zaidi “kondoo wapotevu za nyumba ya Israeli” (Mt. 15:24). Mataifa hawakuwa bila Masiya tu, lakini **walitengwa mbali na jamaa ya Israeli** vilevile. Walikuwa wageni, watu wa inchi nyingine, na bila mapendeleo ya Wayuda. Walikuwa **inje ya jamaa ya Israeli**. Na walikuwa **wageni kwa maagano ya ahadi**. Mungu alikuwa amefanya **maagano na taifa la Israeli** kwa njia ya watu kama Abra-

hamu, Isaka, Yakobo, Musa, Daudi na Solomono. **Maagano** haya yalikuwa ahadi za baraka kwa Wayuda. Haya-kuwa kwa Mataifa. Hayakuwa na **tu-mainini**, wala kwa watu mmoja mmoja, wala kwa taifa lao. Mataifa hawakuwa na matumaini ya kwamba inchi yao, serikali yao, na watu wao watapona. Hawakuwa na tumaini kwa muda una-yofuata kaburi. **Hawakuwa na Mungu duniani.** Si ku-sema kwamba walifikiri hakuna Mungu. Waliabudu miungu yao ambayo walifanya toka miti na mawe. Lakini hawakuja Mungu wa pekee wa kweli. Walikuwa bila Mungu katika dunia hii ya uadui isiyojua Mungu.

2:13 Lakini sasa. Maneno yaligeuka gafula tena (ona 2:4). Mataifa wa Waefeso walikuwa wameponyeshwa toka umbali na uadui na walinyanyuliwa kwa pahali pa ukaribu wa Mungu. Neno hili lilitokea wakati walipookolewa. Wakati walipoamini Mwokozi, Mungu ali-waweka ndani ya **Kristo Yesu** na ali-wapokea ndani ya mpendwa wake. Kuanza wakati ule walikuwa **karibu** na Mungu kwa kipimo Kristo alivyo karibu naye, kwa sababu walikuwa **ndani ya Kristo Yesu**. Bei ya neno hili kuweza kufanyikana ilikuwa **damu ya Kristo**. Mbele ya Mataifa hawa wenye zambi kuweza kufurahi kukaa karibu na Mungu iliwapasa kusafishwa toka zambi zao. **Damu ya Kristo** tu iliyomwangwa kwa Kalvari iliweza kufanya hivi. Wakati walipopokea Bwana Yesu na imani, damu yake ya damani iliwasafisha.

Yesu hakuwfakisha **karibu** tu, lakini alianza jamii mpya ya watu. Ndani ya jamii ile uadui wa zamani uliotenga Wayuda na Mataifa uliondoshwa kwa milele. Kufika mwanzo wa Agano Jipyu dunia nzima ilitengwa kwa jamii mbili – Wayuda na Mataifa. Mwokozi wetu alianza jamii ya tatu – kanisa la Mungu (1 Kor. 10:32). Ndani ya mashairi yana-yofuata, tunaona namna waamini Wayuda na waamini Mataifa wanakuta-

nishwa kuwa moja ndani ya Kristo, na kuingizwa ndani ya jamii hii mpya isiyokuwa na Wayuda wala Mataifa.

2:14 Kwa maana yeze ni salama yetu. Ona ya kuwa hatusomi “alifanya salama,” lakini “yeze ni salama.” Ndani ya shairi 15 tutaona kwamba neno hili ni kweli vilevile, lakini hapa tunasoma kwamba **yeze ni salama yetu**. Basi namna gani mtu anaweza *kuwa* salama?

Wakati Myuda anapoamini Bwana Yesu, anaacha kuwa Myuda; kuanza sasa yeze ni “ndani ya Kristo.” Vivyo hivyo wakati Mataifa anapopokea Mwokozi, yeze si Mataifa tena; yeze ni “ndani ya Kristo.” Waamini Wayuda na waamini Mataifa waliokuwa adui mbele, sasa **wao ni mmoja** ndani ya Kristo. Umoja wao na Kristo unawa-fanyiza kuwa moja vilevile. Hivi Mtu **ni salama**, kama nabii Mika alivyotabiri (Mika 5:5).

Ndani ya mashairi 14-18 tunasoma juu ya kazi yake kama **salama yetu**.

Kazi ya kwanza ilikuwa, kama tulivoona sasa tu, kufanyiza waamini Wayuda na Mataifa kuwa **mmoja**. Si taratibu kabisa kusema juu yao kama Wayuda Wakristo na Mataifa Wakristo. Matofauti yote ya mwili, kama taifa, yalifungwa kwa msalaba na misumari.

Sehemu ya pili ya kazi ya Kristo ilikuwa kazi ya kubomoa: **alibomoa ki-ambaza cha kati ambacho kiliwataenga**. Hakikuwa kiambaza kabisa kili-choonekana kwa macho, lakini kiambaza kisichoonekana kilichosimamishwa na sheria ya Musa, ndiyo amri na maagizo yaliyotenga Waisraeli na Mataifa. Mfano wa neno hili ni kiambaza kilichoruhusu watu wasiokuwa Wayuda kuingia kiwanja cha Mataifa, lakini kili-wakataza kuingia Pahali Patakatifu. Mataifa akipatikana akiingia pahali pale alikufa.

2:15 Sehemu ya tatu ya kazi ya Kristo ilikuwa kubomoa **uadui** kati ya Wayuda na Mataifa, na kati ya watu na

Mungu. Paulo alitambua sheria kama mwanzo wa uadui huu, ndiyo **sheria ya amri zilizo katika maagizo**. Sheria ya Musa ilikuwa mpango wa kanuni moja, lakini ndani yake kulikuwa na maagizo kwa maneno mbalimbali mengi ya maisha ya watu. Sheria yenye we ili-kuwa takatifu, haki, na njema (Rom. 7:12), lakini watu wenye zambi walitumika nayo kwa machukio. Kwa sababu sheria iliweka Israeli kuwa watu wa-chaguliwa wa Mungu, Wayuda wengi waligeuka wenye kiburi na walizarau Mataifa. Neno hili lilizaa uadui ndani ya roho za Mataifa, nao walichukia Wayuda. Basi namna gani Kristo ali-ondosha sheria iliyokuwa sababu ya **uadui** huu? Kwanza, alikufa kulipa azabu ya sheria iliyokwisha kuvunjwa. Halafu hakuna neno lililobaki kwa Mungu kuhukumu. Sheria haina hukumu kwa wale walio “katika Kristo”; azabu nzima kwa zambi zao imelipwa pia. Waamini si chini ya sheria, lakini chini ya neema. Maana yake haiko ya kwamba sasa wanaweza kufanya neno lo lote wanilotaka. Sasa wao ni chini ya amri ya Kristo na inawapasa kuishi kumpendeza Yeye.

Kwa sababu ya kuondosha uadui wa sheria, Bwana ameweza kuanza mu-umbo mpya. Amefanya ndani yake mwenyewe **toka wawili**, ndio waamini Wayuda na waamini Mataifa, **mtu mpya mmoja** – kanisa. Kwa sababu waamini wanafunganishwa na Bwana, watu hawa waliokuwa adui mbele wanafungana pamoja ndani ya ushirika **mpya**. Kanisa ni **jipy** kwa sababu ushirika namna hii haukuwa mbele tangu zamani. Vizuri tu-fahamu neno hili. Kanisa la Agano Jipy si mwendeleo wa Israeli la Agano la Kale. Ni namna nyngine kabisa na jambo lo lote lililotangulia au litakalotokea nyuma. Maneno yanayofuata yanaonyesha neno hili wazi:

1. Ni **jipy** kwa sababu ndani yake mwamini Mataifa na mwamini Myuda

wana mapendeleo sawasawa.

2. Ni **jipy** kwa sababu waamini hatatujlikana kama Wayuda na Mataifa tena kwa sababu sasa wao ni Wakristo.
3. Ni **jipy** kwa sababu sasa waamini Wayuda na Mataifa ni viungo pamoja ndani ya mwili wa Kristo.
4. Ni **jipy** kwa sababu sasa mwamini Myuda si mtu anayetawaliwa katika ufalme wa Kristo tu, lakini ana tumaini ya kwamba atatawala pamoja naye.
5. Ni **jipy** kwa sababu mwamini Myuda si chini ya sheria tena.

Ni wazi ya kwamba kanisa ni mu-umbo **mpya**, na lina pahali pa namna ya pekee ndani ya mashauri ya Mungu. Lakini neno hili halikumaliza kazi ya Kristo. Aliondoa vilevile uadui kati ya Wayuda na Mataifa na kuukomboa na **salama**. Alifanya hivi kwa njia ya kuondosha shina la uadui na kuwapa tabia mpya na umoja mpya. Msalaba ndio jibu la Mungu kwa uadui na magomvi yo yote ya watu.

2:16 Na hakupatanisha Wayuda na Mataifa tu, lakini zaidi ya ile **aliwapatanisha na Mungu**. Hata kama Israeli na mataifa walishindana na uchungu sana, walipatana ndani ya neno moja, ndilo uadui wao na Mungu. Sababu ya uadui huu ilikuwa zambi. Bwana Yesu aliondosha **sababu ya uadui huu** kwa njia ya kufa kwake msalabani. Wale ambao wanampokea kuwa Mwokozi wao wanahesabiwa haki, wanasmehewa, wanakobolewa, na wanafunguliwa toka uwezo wa zambi. Hakuna uadui tena; sasa wana salama na **Mungu**. Bwana Yesu anafunganisha mwamini Myuda na mwamini Mataifa kuwa **mwili mmoja**, ndilo kanisa, na anatoa Mwili huu kwa **Mungu**, bila uadui wo wote pia.

Mungu hakuhitaji kupatanishwa nasi kamwe; hakutuchukia kamwe. Lakini sisi tulihitaji kupatanishwa naye. Kazi ya Bwana wetu msalabani ni njia ya haki

ambayo inatuwezesha kufikishwa mbele ya Mungu kama rafiki, si kama adui.

2:17 Ndani ya shairi 14 Kristo *ni salama yetu*. Ndani ya shairi 15 *alifanya salama*. Sasa tunaona kwamba **aliuja na kuhubiri salama**. Alikuja wakati gani na namna gani? Alikuja kwanza yeye mwenyewe kwa njia ya ufufuko wake. Na vilevile alikuja kwa njia ya Roho Mtakatifu. **Alihubiri salama** katika ufufuko; ndiyo **salama** ilikuwa moja la maneno ya kwanza alilosema nyuma ya kufufuka toka wafu (Lk. 24:36; Yn. 20:19, 21, 26). Kisha alituma mitume kwa uwezo wa Roho Mtakatifu na **alihubiri salama** kwa njia yao (Mdo. 10:36). Habari Njema ya **salama** ilihubiriwa **kwenu muliokuwa mbali** (Mataifa), na **kwao waliokuwa karibu** (Wayuda), na kutimiza ahadi ya neema ya Mungu katika Isaya 57:19.

2:18 Neno linalohakikisha kwamba kuna salama sasa katika viungo vya Mwili ule mmoja na Mungu ni ya kwamba wanaweza **kukaribia** Mungu saa yo yote wanayotaka. Neno hili halikuwezekana hata kidogo kwa wakati wa Agano la Kale. Kwa wakati ule kuhani mkubwa tu aliweza kuingia pahali patakatifu, pahali Mungu alipokaa. Na aliweza kuingia siku moja tu kwa mwaka mmoja.

Kwa njia ya maombi mwamini ye yote anaweza kuingia mbingu na kupiga magoti mbele ya Mwenye Enzi wa ulimwengu, na kumwita **Baba**.

Tunaona hapa kawaida ambayo inapasa kufuata kwa maombi. Kwanza, ni **kwa Yeye** (Bwana Yesu). Yeye ni Mpatanishi wa pekee wa Mungu na watu. Mauti yake, kuzikwa kwake, na ufufuko wake zilindosha kila kizuizo kilichoweza kufunga njia kwa sisi kufika karibu na Mungu. Sasa kama Mpatanishi yeye ni hai na anatulinda tuweze kuwa na ushirika na Baba. Tunakaribia Mungu kwa jina lake; sisi wenyewe hatustahili hata kidogo, hivi

tunategemea ustahili wake. Wenye kuomba ndio **sisi sote** – waamini Wayuda na Mataifa, na mapendeleo yetu ni kwamba **tumepata njia kukaribia**. Roho Mtakatifu anatusaidia ndani ya maombi yetu – **katika Roho mmoja**. “Roho Mtakatifu anasaidia uzaifu wetu; kwa maana hatujui kuomba kitu namna inavyotupasa, lakini Roho mwenyewe anatuombea kwa kuugua kusikoweza kusemwa” (Rom. 8:26).

Yule ambaye tunakaribia ni **Baba**. Hakuna mtu katika Agano la Kale aliyejuana na Mungu kama Baba. Mbele ya ufufuko wa Kristo, watu walismama mbele ya Mungu kama viumbi mbele ya Mwumba. Nyuma ya ufufuko wake alisema, “Kwenda kwa ndugu zangu, ukiwaambia: ‘Ninapanda kwa Baba yangu na Baba yenu; na kwa Mungu wangu na Mungu wenu’” (Yn. 20:17). Halafu kwa sababu ya kazi yake ya ukombozi waamini waliweza mara ya kwanza kuita Mungu **Baba**. Ndani ya shairi 18 tunaona Mungu Baba, Bwana Yesu Kristo, na Roho Mtakatifu, wote watatu, wakishiriki ndani ya maombi ya mwamini. Anaomba kwa Mungu **Baba**, akimkaribia **kwa njia ya** Bwana Yesu Kristo, na kwa uwezo wa **Roho** Mtakatifu.

2:19 Ndani ya mashairi mane ya mwisho ya sura hii mtume Paulo alitaja mengine ya mapendeleo mapya ya kushangaza sana ya waamini Mataifa. Wao **si wageni na wasafiri tena**. Hawatakuwa tena kamwe wageni, imbwa, wasiotahiriwa, watu wasio wa jamaa. Sasa wao ni **wenyeji pamoja na watakatifu** wote wa muda wa Agano Jipy. Waamini waliozaliwa Wayuda hawakubarikiwa kupita waamini Mataifa. Wakristo wote ni wenyeji sawasawa wa mbingu (Flp. 3:20, 21). Wao ni **watu wa nyumba ya Mungu** vilevile. Hawakuingizwa ndani ya *ufalme* wa Mungu tu; wameingizwa ndani ya *jamaa* ya Mungu vilevile.

2:20 Mwishoni, wamepokewa ndani

ya kanisa. Kwa mfano Paulo aliwaita mawe yanayotumiwa kujenga hekalu takatifu. Mtume alitaja maneno mengi juu ya hekalu hili – **msingi** wake, **jiwe kubwa la pembedni**, kuunganishwa kwake, umoja wake, kukua kwake, na maneno yake mengine.

Hekalu hili *linajengwa juu ya msingi wa mitume na manabii, ndio mitume na manabii wa wakati wa Agano Jipy* (si manabii wa Agano la Kale wasiojua habari za kanisa). Si kusema kwamba **mitume na manabii walikuwa msingi** wa kanisa. Kristo ndiye **msingi** wake (1 Kor. 3:11). Lakini waliweka msingi kwa njia ya mafundisho yao juu ya Bwana Yesu na kazi yake. Kanisa linasi-mamishwa juu ya Kristo na habari zili-zofunuliwa na ushuhuda na mafundisho ya mitume na manabii. Wakati Petro alipokiri kwamba ye ye ni Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai, Yesu ali-tangaza kwamba kanisa lake litajengwa juu ya mwamba ule, ndio, kweli imara ya kwamba ye ye ni mpakaliwa wa Mungu na Mwana wa pekee wa Mungu (Mt. 16:18). Katika Ufunuo 21:14 mitume wanachangamana na misingi kumi na miwili ya Yerusalem mtakatifu. Wao si msingi lakini wanaungana nao, kwa sababu walikuwa watu wa kwanza waliwfundisha kweli kubwa juu ya Kristo na kanisa. **Msingi** wa jengo unahitaji kuwekwa mara moja tu. **Mitume na manabii** walifanya kazi hii mara moja tu. **Msingi** waliweka umelindwa kwa sisi ndani ya maandiko ya Agano Jipy, hata kama wao wenyewe si pamoja nasi tena. Lakini kwa kila wakati kuna watu wenye kazi iliyo sawasawa na ile ya mitume au manabii. Wao ndio wahubiri na wenye kuanza makanisa, na wale wanaohubiri Neno la Mungu kujenga wamini ni manabii. Lakini wao si kama mitume na manabii wa kwanza.

Yesu Kristo si msingi tu wa hekalu; ye ye ni **jiwe kubwa la pembedni** vilevile. Hakuna mfano unaoweza ku-

onyesha utukufu wake wote au utumishi wake namna mbalimbali. Kuna njia tatu au zaidi kueleza **jiwe kubwa la pembedni**, nazo zote zinaonyesha Bwana Yesu Kristo kama Kichwa cha kanisa asiye na kifani, mwenye sifa zaidi, na wa lazima.

Ni desturi yetu kufikiri kwamba **jiwe la pembedni** ndilo jiwe linalolala kwa pembe ya chini ya mbele ya jengo. Ni kama baki la jengo linalitegemea, hivi jiwe hili ni lenye kazi kubwa sana, na ni mfano mzuri wa Bwana Yesu. Jiwe hili linafunganisha kuta mbili pamoja na linatifikirisha kufungamana kwa wa-amini Wayuda na Mataifa kanisani kwa njia yake.

Walimu wengine wanafikiri kwamba **jiwe kubwa la pembedni** ni jiwe lililo juu zaidi la jengo. Vivyo hivyo Kristo ni Kichwa cha kanisa. Hakuna mwingine kama ye ye, na utumishi wake ni msingi wa mawe mengine. Ni mfano wa Kristo aliye mkubwa zaidi kanisani. Anahitajiwa kabisa vilevile; bila ye ye jengo lingueangamia.

2:21 Kristo ni **msingi** wa kanisa na asili na uzima wake, na ndani yake kanisa linakua.

Katika ye ye **jengo zima linaunganishwa**. Ni umoja wa viungo vingi. Kila mtu ana pahali fulani ndani ya **jengo** panapofaa kabisa kwa ye ye, na wanalingana vizuri. Lakini jengo hili ni namna nyininge. Ni nyumba **inayokua**. Halikui kwa njia ya kuongeza matofali na ciment. Tunaweza kulisawanisha na mwili wa mtu. Kanisa si jengo linalokosa uzima. Si chama vilevile. Kanisa lina uzima, na Kristo ni kichwa chake. Waamini wote ni mwili wake. Lilizaliwa siku ya Pentekote na linakaa kukua na kuongezeka kufika siku Mwokozi ataka-polipeleka mbinguni.

Jengo hili lenye uzima linaitwa **hekalu takatifu katika Bwana**. Neno ambalo Paulo alitumia hapa kwa **hekalu** (*naos* kwa Kiyunani) halikutumiwa kwa

viwanja vilivyozunguka hekalu, lakini kwa pahali patakatifu pa patakatifu. Mungu alikaa pale na alijionyesha ndani ya wingu la kungaa la utukufu.

Tunajifunza maneno mengine hapa: (1) Mungu anakaa ndani ya kanisa. Waamini Wayuda na Mataifa ni pahali patakatifu hai ambapo anakaa ndani yake na kufunua utukufu wake. (2) **Hekalu** hili ni **takatifu**. Ni mbali na dunia na linawekwa kwa Mungu kwa makusudi matakatifu. (3) Kama **hekalu takatifu**, sifa na kuabudu kunapanda kwa Mungu toka kanisa kwa njia ya Bwana Yesu Kristo.

Halafu Paulo alisema **hekalu takatifu** hili ni **katika Bwana**. Ni kusema, utakatifu unatoka kwa Bwana Yesu. Vingoo vyake ni **vitakatifu** kwa sababu vinafungamana naye, na ingepasa wawe **watakatifu** katika matendo yao kwa sababu wanampenda sana.

2:22 Ndani ya hekalu hili la ajabu, waamini Mataifa wana cheo sawasawa na waamini Wayuda. Ingepasa kutufurahisha sisi sana kusoma neno hili, kama bila shaka ilivyofurahisha Waefeso na watu wengine vilevile wakati waliposikia habari hizi mara ya kwanza. Ni heshima kubwa sana kwa waamini kuwa **kao la Mungu katika Roho**. Hili ndilo kusudi la hekalu – kuwa pahali Mungu anapoweza kukaa na upatano mwema na watu wake. Kanisa ndipo pahali pale. Sawanisha habari hizi na hali ya Mataifa katika Agano la Kale. Kwa wakati ule hawakuweza kukaribia kao la Mungu. Sasa wao wenyewe *ni sehemu* kubwa ya kao hili!

Na waza vilevile juu ya kazi ya Kristo, Mungu, na Roho ndani ya kanisa. (1) **Katika yeye**, ndiye Kristo. Kwa sababu tunafungamana na Kristo tunajengwa kuwa hekalu. (2) **Kao la Mungu**. Hekalu hili ni kao la Mungu Baba duniani. (3) **Katika Roho**. Ni Mungu **Roho** Mtakatifu anayekaa ndani ya kanisa (1 Kor. 3:16).

Hivi kwa mwanzo wa sura 2 tuliona Mataifa kama wafu, waovu, watu wa Shetani, na waasi, lakini kwa mwisho wa sura hii Mataifa hawa walikuwa wamesafishwa toka hatia ya zambi na uchafu, na wamegeuka kuwa **kao la Mungu katika Roho!**

F. Habari nyininge juu ya siri (3:1-13)

3:1 Paulo alianza kusema juu ya neno fulani ndani ya shairi 1, lakini alilazimishwa kuacha kusema juu yake ndani ya shairi 2 mpaka shairi 14. Habari zili zoingizwa katikati ni juu ya siri ile kubwa – ndiyo Kristo na kanisa.

Na habari hizi za muda wa sasa wa kanisa zinaingizwa vilevile ndani ya habari za mashauri ya Mungu. Tunaweza kueleza neno hili hivi: Kwa wakati wa muda tunaosoma juu yake katika Agano la Kale, Mungu alikuwa akitumika zaidi na Wayuda. Kuanza na Mwanzo 12 na kufika Malaki 4 tunasoma zaidi juu ya Abrahamu na wazao wake. Wakati Bwana Yesu alipofika duniani, alikataliwa na Israeli. Kwa sababu hii Mungu hakutumika na taifa hili tena kwa wakati kama watu wake wachaguliwa wa dunia. Hivi sasa tunaishi katika muda wa Kanisa, na Wayuda na Mataifa ni sawasawa mbele ya Mungu. Wakati kanisa litakapotimizwa na kipelekwa mbinguni, Mungu atatumika na taifa la Israeli tena. Hivi muda huu wa sasa wa kanisa umeingizwa katikati ya shauri la Mungu kwa muda wa mbele na wakati wa kuja wa Israeli. Ni utawala mpya kabisa wa Mungu, namna nyininge kabisa na makusudi yake ya mbele, na ya wakati wa kuja.

Ndani ya mashairi 2-13 Paulo alieleza maneno mengi kidogo juu ya muda huu.

Alianza na kusema, **Kwa sababu hii mimi Paulo, mfungwa wa Kristo Yesu kwa ajili yenu ninyi Mataifa**. Alikumbusha wasikiaji wake maneno aliyosema sasa tu juu ya mapendeleo ya

waamini Mataifa kwa sababu ya kufungamana kwao na Kristo.

Watu wanafikiri kwamba barua hii ili-andikwa wakati Paulo alipofungwa mara ya kwanza na Waroma. Lakini Paulo hakusema juu yake mwenyewe kama mfungwa wa Roma. Hakutaka watu wafikiri kwamba alikuwa ameshindwa, na alijihurumia mwenyewe, na alitaka watu wengine kumhurumia vilevile. Paulo alijiita **mfungwa wa Kristo Yesu**; neno hili lilionyesha roho ya ukubali na adabu na kushinda.

Bila shaka Paulo alifungwa kwa ajili ya **Mataifa**. Kwa muda mzima wa utumishi wake watu walishindana naye na uchungu kwa sababu alihubiri kwamba waamini Mataifa walibarikiwa na mapendeleo yote sawasawa na waamini Wayuda ndani ya kanisa la Wakristo. Mwishoni walimfunga na kumshitaki mbele ya Kaisari juu ya neno lisilokuwa kweli. Walisema Paulo alikuwa amepeleka Trofimo, mtu wa Efeso, kwa upande wa hekalu uliokatazwa kwa Mataifa kuingia (Mdo. 21:29). Lakini shina la shitaki hili lilikuwa uadui mkali sana wa viongozi vya dini ya Wayuda.

3:2 Halafu sasa Paulo aligeuka na kusema tena juu ya siri aliyokwisha kusema juu yake mbele. Labda wasomaji wake wengine hawakusikia juu ya ujumbe wake kwa Mataifa, na walifikiri hakujuwa watu ambao aliwaandikia barua hii walikuwa Waefeso. Paulo aliita ujumbe huu **uwakili wa neema ya Mungu**. Kazi ya mwakili ni kuchunga na kusimamia maneno ya mtu mwagine. Paulo alikuwa mwakili wa Mungu, na alikuwa na kazi ya kufundisha kweli kubwa ya kanisa la Agano Jipy. Ulikuwa uwakili wa **neema** ya Mungu kwa njia tatu:

1. Ulikuwa upendeleo ambao Paulo hakustahili, ndio kuchaguliwa kwa kazi hii ya heshima kubwa.
2. Ulikuwa habari za wema wa Mungu

tusiostahili.

3. Mataifa hawakustahili kubarikiwa hivi.

Basi Paulo alipewa uwakili huu wa **neema** ili aweze kuupitisha kwa Mataifa.

3:3 Hakujifunza **siri** hii toka mtu mwagine, na hakuitambua kwa njia ya akili yake mwenyewe. **Ilifunuliwa kwa-ke na Mungu mwenyewe**. Hatujulishwi kama neno hili lilitokea namna gani. Tunajua tu kwamba kwa njia ya ajabu Mungu alionyeshea Paulo shauri lake kwa kanisa lenye waamini Wayuda na waamini Mataifa. Tumekwisha kusema mbele ya kwamba **siri** ni habari takatifu watu wasiyoweza kujua mbele, lakini sasa ilifunuliwa na Mungu. Paulo alitaja nusu nusu tu juu ya **siri** hii ndani ya 1:9-14, 22, 23; 2:11-22.

3:4 Habari Paulo alizoandika mbele juu ya siri hii zilitosha kufahamisha wasomaji wake kwamba Mungu alimpa ufahamu wa **siri ya Kristo**.

“Siri ya Kristo” hapa inasema juu ya Kichwa *na* Mwili. (Pahali pengine tunaposoma juu ya jina la **Kristo** lenye maana ya Bwana Yesu na watu wake pamoja ni kwa 1 Kor. 12:12.)

3:5 Ndani ya mashairi 5 na 6 Paulo alieleza maana ya siri wazi zaidi, kisha alieleza kama siri ya Kristo ni nini.

Kwanza, ni kweli **isiyojulishwa kwa wana wa watu katika vizazi vingine**. Hivi si faida kujaribu kuiona ndani ya maandiko ya Agano la Kale. Labda kuluiwa na mifano ya kweli hii, lakini kweli yenye kwanza haikujulikana kwa wakati ule.

Neno la pili, **ni kweli inayofunuliwa sasa na Roho** Mtakatifu kwa **mitume na manabii watakatifu** wa Mungu. Mungu alifunua kweli hii, na **mitume na manabii** walichaguliwa kupokea ufunuo huu; **Roho** Mtakatifu alikuwa mfereji kwa njia yake ufunuo huu uliwafikia.

Sharti tufahamu kwamba **mitume na**

manabii hawa walikuwa watu wa Agano Jipy, si wa Agano la Kale. Kweli kubwa hii ya Kristo na kanisa ilifunuliwa kwa watu wa muda wa kanisa waliochaguliwa, kama Paulo, na Bwana mfuliwa alimwezesha kuwa mnenaji wake. (Paulo hakusema kamwe kwamba siri hii takatifu ilifunuliwa kwa ye ye *peke yake*. Ilifunuliwa kwa watu wengi wengine vilevile. Lakini Paulo, kupita wengine, alijulisha kwa Mataifa kwa wakati wake, na kwa vizazi nya umu kwa njia ya barua zake.)

Wakristo wengi wanatafsiri mashairi haya namna nyingine. Wanasema kanisa lilikuwa hata ndani ya Agano la Kale; ya kwamba taifa la Israeli lilikuwa kanisa kwa wakati ule; lakini kwamba *kweli ya kanisa imefunuliwa wazi kupita sasa*. Wanasema, “Siri haikufunuliwa *kwa kipimo inayofunuliwa sasa*, lakini tungali sasa Israeli ya Mungu, ndio watu wa Mungu.” Kusimamisha mabishano yao wanataja Matendo 7:38, pahali taifa la Israeli linapoitwa “kanisa jangwani,” lakini neno hili halionyeshi kwamba wana mwunganisho na kanisa la *Wakristo*. Neno linalotafsiriwa kanisa ni *ekklesia* kwa Kiyunani na linatumia kwa makusanyiko namna namna vilevile (kama kwa makutano ya wapagano kwa Matendo 19:32, 41).

Lakini watu wengine wanasema shairi 5 linaonyesha kwamba kanisa lilikuwa katika Agano la Kale, lakini haliku-funuliwa wazi kufika sasa. Neno hili si kweli. Tunasoma waziwazi ndani ya Kol. 1:26 kwamba siri hii “ilifichwa tangu nyakati na vizazi vyote; lakini sasa imefunuliwa kwa watakatifu wake.” Neno kubwa si kama sehemu yake ilifunuliwa, lakini kwamba siri yenyewe ilifunuliwa.

3:6 Sasa tunafikia kweli kubwa ya siri hii, ndiyo ya kwamba ndani ya kanisa la Bwana Yesu Kristo waamini **Mataifa ni wariti pamoja, na washiriki pamoja wa ahadi hii katika**

Kristo Yesu kwa njia ya Habari Njema. Ni kusema waamini **Mataifa** wanabarikiwa na mapendeleo yote sawasawa na waamini Wayuda.

Kwanza, wao ni **wariti pamoja**. Wanashiriki sawasawa na waamini Wayuda. Wao ni wariti wa Mungu, wariti pamoja na Yesu Kristo, na **wariti pamoja** na wakombolewa wote.

Na vilevile wao ni viungo **vya mwili mmoja**. Wana hali moja na waamini Wayuda ndani ya kanisa.

Mwishoni, wao ni **washiriki** pamoja wa **ahadi katika Kristo kwa njia ya Habari Njema**. Laba maana ya **ahadi** hapa ni Roho Mtakatifu (Mdo. 15:8; Gal. 3:14). Au ni maneno yote ambayo yanaahidiwa ndani ya **Habari Njema** kwa wale walio **ndani ya Kristo** Yesu. **Mataifa** na Wayuda wanashiriki ndani ya maneno haya yote.

Habari hizi zote hazikuwa kweli kwa wakati wa Agano la Kale, na hazitakuwa kweli kwa wakati wa ufalme wa kuja wa Kristo.

Katika Agano la Kale Israeli lilikuwa na pahali pa mapendeleo mbele ya Mungu. Myuda angalicheka wazo kwamba Mtaifa angalishiriki naye sawasawa ndani ya ahadi za Mungu. Haikuwa hivi hata kidogo. Manabii wa Israeli walitabiri kwamba Mataifa wataitwa (Isa. 49:6; 56:6, 7), lakini hawakusema neno lo lote kwamba Mataifa watakuwa viungo ndani ya jamii pahali Wayuda hawataheshimiwa kuliko wengine.

Ndani ya ufalme wa kuja wa Bwana wetu, Israeli litakuwa mkubwa wa mataifa. Mataifa watabarikiwa, lakini baraka hii itawafikia kwa njia ya Israeli (Isa. 60:3; 61:6; Zek. 8:23).

Israeli liliitwa kupokea zaidi baraka zilizokuwa kwa wakati tu kwa pahali mbalimbali duniani (Tor. 28; Amo. 9:13-15). Kanisa liliitwa kupokea zaidi baraka za roho kwa pahali pa mbingu (Efe. 1:3). Israeli liliitwa kuwa watu wachaguliwa wa Mungu duniani. Ka-

nisa linaitwa kuwa Bibi Arusi ya Kristo mbinguni (Ufu. 21:2,9). Israeli watabarikiwa wakati wa utawala wa Kristo wa miaka elfu moja (Hos. 3:5); kanisa litatawala pamoja naye juu ya ulimwengu mzima, na kushiriki katika utukufu wake (Efe. 1:22, 23).

Hivi ni wazi ya kwamba kanisa si Israeli wala ufalme. Ni chama mpya, ushirika wa waamini wenye mapendeleo usio na kifani, ambao tunasoma habari zao ndani ya Biblia. Kanisa lilianzwa nyuma ya kupanda kwa Kristo mbinguni na kupewa kwa Roho Mtakatifu (Mdo. 2). Lilianzwa na ubatizo wa Roho Mtakatifu (1 Kor. 12:13). Litamalizwa wakati waamini wote watakopolekwa mbinguni (1 Tes. 4:13-18; 1 Kor. 15:23, 51-58).

3:7 Nyuma ya kufundisha kwamba waamini Mataifa na waamini Wayuda wanashiriki sawasawa ndani ya kanisa, Paulo aliendelea kusema juu ya utumishi wake mwenyewe (mash. 7-9).

Alifanya mhubiri wa Habari Njema, na alitumikia Bwana kwa maneno ya siri iliyofunuliwa sasa.

Utumishi huu ulikuwa zawadi: **kwa kadiri ya zawadi ya neema ile ya Mungu niliyopewa**. Zawadi hii haikonyesha **neema** ya Mungu tu. Ilionyesha **uwezo** wa Mungu vilevile uliogeuza Mfarisayo yule mwenye kiburi, na kumwokoa. Ulimweka kuwa mtume na kumwezesha kupokea funuo toka Mungu, na kumpatisha nguvu kufanya kazi yenye. Hivi Paulo alisema alipewa **zawadi** hii kwa kadiri ya **utendaji wa uwezo wa Mungu**.

3:8 Mtume alisema vilevile kwamba alikuwa **mdogo kuliko** kupita **watakatifu wote**. Hakusema hivi kwa kuonyesha unyenyekevu usiokuwa kweli. Ndiyo, kila mtu anayejazwa na Roho Mtakatifu anaweza kusema hivi. Kila mtu anayeona Kristo katika utukufu wake anafahamu yeye mwenyewe ni mwenye zambi kabisa asiye na faida. Na

zaidi ya ile, bila shaka Paulo alikumbuka kwamba alikuwa ametesa Bwana Yesu (Mdo. 9:4) kwa njia ya kutesa kanisa la Mungu (Gal. 1:13; Flp. 3:6). Lakini hata hivi Bwana alimwamuru kupeleka Habari Njema kwa **Mataifa** (Mdo. 9:15; 13:47; 22:21; Gal. 2:2, 8). Paulo alikuwa mtume kwa **Mataifa** kama Petro alivyokuwa mtume kwa Wayuda. Utumishi wake ulikuwa na sehemu mbili: kuhubiri Habari Njema, na kusaidia kanisa. Kwanza alijulisha watu namna gani wanaweza kuokolewa, kisha aliwfundisha kweli ya kanisa la Agano Jipy. Paulo hakufikiri utumishi wake ulikuwa kuhubiri Habari Njema tu, lakini kwamba ulikuwa mwanzo wa kusimamisha makanisa ya Agano Jipy na kuyapatisha nguvu.

Sehemu ya kwanza ya utumishi wake ilikuwa **kuhubiri** kwa **Mataifa utajiri wa Kristo usiotafutikana**.

Wakati mtu anapoamini Bwana Yesu, anageuka mara moja mtajiri mwenye mamilioni za roho. Ndani ya Kristo ana hazina isiyomalizika.

3:9 Sehemu ya pili ya utumishi wa Paulo ilikuwa **kuangazia** **watu wote** wajue habari za madaraka ya **siri** iliyofichwa. Shauri la Mungu kwa muda huu wa sasa ni kuita katika Mataifa watu kwa jina lake (Mdo. 15:14), bibi arusi kwa Mwana wake. **Watu wote** hapa ndio **waamini wote**. Wasioamini hawawezi kufahamu kweli hizi za ndani ndani za **siri** (1 Kor. 2:14). Hivi wakati Paulo aliposema juu ya watu **wote** hapa anasema juu ya waamini **wote** namna namna – Wayuda na Mataifa, watumwa na walio huru.

Siri hii ilikuwa **imefichwa tangu zanmani** **ndani ya Mungu**. Lilikuwa shauri la Mungu tangu milele, lakini ni kama alilificha kwa eoni za watu walioishi duniani mbele. Tunaona tena kwamba Roho Mtakatifu alituonyeshea wazi ya kwamba kanisa ni kusanyiko jipy, lisilokuwa mbele. Mungu peke yake ali-

juu habari hizi. Siri hii **ilifichwa ndani ya Mungu aliyeumba vitu vyote. Aliumba** ulimwengu, **aliumba** nyakati, na **aliumba** kanisa – lakini kwa hekima yake alichagua kuficha habari za mwumbo mpya huu kufika wakati Kristo alipofika duniani mara ya kwanza.

3:10 Moja la makusudi ya siri ya Mungu kwa wakati wa sasa ni kufunua **hekima yake ya namna nyingi** kwa majeshi ya malaika mbinguni. Paulo alitumika tena na mfano wa chuo. Mungu ndiye mwalimu wa chuo hiki. Ulimwengu ni chumba cha darasa. Malaika ndio wanafunzi. Somo ndilo “**Hekima ya namna nyingi ya Mungu.**” Mfano wa mafundisho ni **kanisa**. Toka mbingu malaika wanalazimishwa kushangaa juu ya hukumu za Mungu na njia zake zisizotafutikana. Wanaona namna gani Mungu alishinda zambi kwa utukufu wake mwenyewe. Wanaona namna gani alilipa bei kubwa sana kukomboa adui zake, aliwashinda na mapendo, na kuwatayarisha kuwa bibi-arusi kwa Mwana wake. Wanaona namna alivyo-wabari na baraka zote za roho mbinguni. Na wanaona kwamba kwa njia ya kazi ya Bwana Yesu msalabani, Mungu alitukuzwa zaidi, na waamini Wayuda na waamini Mataifa walibarikiwa sana, kupita wangalibarikiwa kama zambi zisipopata njia kuingia dunia. Mungu alithibitishwa; Kristo alitukuzwa; Shetani alishindwa; na kanisa limeketishwa katika Kristo kushiriki utukufu wake.

3:11 Siri yenye, namna ilivyo-fichwa, na namna ilivyofunuliwa nyuma ya wakati, inaonyesha hekima ya Mungu na ni **kwa kadiri ya kusudi la milele alilokusudi katika Kristo Yesu Bwana wetu.** Mbele ya kuumbwa kwa dunia, Mungu alijua Shetani ataanguka na watu watamuata na kutenda zambi. Na aliquwa ametayarisha njia kuteengeneza neno hili. Shauri hili zima lilitimizwa kwa njia ya Kristo kutwaa utu, mauti yake, kufufuka, kupanda mbi-

nguni, na kutukuzwa. Sasa Mungu anaweza kuokoa Wayuda na Mataifa wazalimu, kuwafanya viungo vya mwili wa Kristo, kuwageuzea kufanana na sura ya Mwana wake, na kuwaheshimu kama bibi-arusi wa Mwana-Kondoo kwa milele.

3:12 Kwa sababu ya kazi ya Kristo na kwa sababu tunafungamana naye, ni baraka kubwa kwasi kuweza kutokeea mbele yake saa yo yote tunayotaka, na bila woga kwamba tutahamakiwa (Yak. 1:5). Tuna **uhodari** kumkaribia na heshima na adabu kama watoto wakisema na baba yao na maombi. Na tuna **tu-maini** kwamba atatukaribisha vizuri, atatusikiliza, na kutujibu na mapendo. Ni yote kwa njia ya **imani** yetu **ndani** ya Bwana Yesu Kristo.

3:13 Kwa sababu ya heshima ya utumishi wake na matunda ya ajabu ya utumishi huu, Paulo alisema na waamini kwamba haifai wahuzunishwe wakati walipofikiri juu ya mateso yake. Alifurahi kupata **mateso** kwa njia ya kazi yake kwa Mataifa. Ingewapasa kujisifu kwa sababu alihesabiwa kustahili kuteswa kwa Bwana Yesu Kristo. Alisema nao kufurahishwa wakati walipofikiri juu ya faida waliyopata pamoja na Mataifa wengine kwa njia ya **mateso** yake. Wafahamu kwamba haikuwa haya kwaye kufungwa gerezani, lakini **utukufu**.

G. Maombi ya Paulo kwa watakatifu (3:14-19)

3:14 Sasa Paulo aliendelea na masemo aliyoanza ndani ya shairi 1, lakini asiyomaliza ili kutoa mafundisho juu ya siri. Kwa sababu hii shairi 14 linaanza na maneno haya, **Kwa sababu ya neno hili**, kutukumbusha habari za sura 2. Sura ile ilitujulisha hali ya Mataifa mbele ya wokovu wao, na namna walivyogeuka kwa njia ya kufungamana na Kristo. Walikuwa wametoka umasikini na mauti, na kupata utajiri wa roho

na utukufu. Maneno haya ya kushangaza yalisukuma Paulo kuwaombea waweze kuishi daima katika hali yao bora.

Paulo alipiga magoti wakati alipomboa. Si kusema ya kwamba inapasa watu kupiga magoti kila mara wana-poomba, lakini ingepasa kupiga magoti kuwa mfano wa hali yetu ya roho. Tunaweza kuomba saa tunapotembea njiani, au kuketi, au kulala chini, pamoja na kuwa na roho ya unyenyekevu na adabu.

Aliomba mbele ya Baba. Kwa kawaida, Mungu ni Baba wa wanadamu wote, maana yeye ni Mwumba wao (Mdo. 17:28, 29). Lakini zaidi yeye ni Baba wa waamini wote na amewazaa ndani ya jamaa yake ya roho (Gal. 4:6). Na kwa njia isiyo na kifani **yeye ni Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo.** Ni kusema wao ni sawasawa (Yn. 5:18).

3:15 Paulo alifikiri juu ya Baba kama yule **katika yeye jamaa zote mbinguni na duniani wanaitwa.** Labda maana yake ni:

1. Wakombolewa wote mbinguni na duniani wanamtazamia kama Kichwa cha jamaa.

2. Viumbe vyote, malaika na watu, si mmoja mmoja tu, lakini jamaa vilevile, wanaishi kwa sababu yake. Jamaa mbinguni ni daraja mbalimbali za malaika. Jamaa duniani ni mataifa mbalimbali duniani yaliyoanzwa na Noa.

3:16 Tunashangazwa sana na ukubwa wa ombi la Paulo: **awape ninyi, kwa kadiri ya utajiri wa utukufu wake.** Aliomba waamini waweze **kupatishwa nguvu rohon.**

Kwa kipimo gani? Si kwa udogo wa miyo yetu, lakini kwa kadiri ya **utajiri wa utukufu wake** (Jamieson, Fausset, and Brown).⁷ Mtajiri anaweza kutoa mali nusu, sehemu ndogo ya mali yake, lakini **si kwa kadiri ya utajiri wake!** Paulo aliomba Mungu aweze kuleta nguvu **kwa kadiri ya utajiri wa ukamilifu wake!** Bwana akiwa na utajiri mkubwa sana katika

utukufu, waamini wakae tayari kupokea garika! Kwa nini tutaomba maneno nusu nusu toka mfalme huyu mkubwa? Wakati mtu mmoja alipofikia mfalme Napoleon na ombi kubwa sana, Napoleon alikubali mara moja kufanya kitu alichoomba, akisema, "Mtu huyu alin-heshimu kwa njia ya ukubwa wa ombi lake."

Unafikia Mfalme mkubwa,
Umfikie na maombi makubwa;
Neema na uwezo wake ni kubwa sana,
Ombi lako haliwezi kuwa kubwa
kupita kipimo. — John Newton

Sasa tunafikia maombi kwa maneno fulani moja moja ya Paulo. Tufikiri juu yao kama jengo lenye msingi wa mawe, na madaraja ya maombi yanayojengwa juu yao.

Ombi la kwanza lilikuwa waweze **kupata nguvu na uwezo kwa njia ya Roho yake katika mtu wa ndani.** Ni ombi kwa *uwezo wa roho*. Si uwezo kufanya maajabu kushangaza watu, lakini ni kuwa na akili, kukomea na kusimama imara. **Roho** Mtakatifu anatoa uwezo huu. Lakini anaweza kutupa sisi nguvu tu kama tukilisha roho zetu na Neno la Mungu, kama tukiomba, na kukaa kutumikia Bwana kila siku.

Tunaweza kuwa na uwezo huu katika **mtu wa ndani.** Ni **mtu wa ndani** anayefurahia sheria ya Mungu (Rom. 7:22). Ni **mtu wa ndani** anayefanywa mpya kila siku, hata kama mtu wetu wa inje anapooza (2 Kor. 4:16). Hata kama **mtu wa ndani** akiwa wa Mungu, anahitaji nguvu na kukomea.

3:17 Ombi la pili la Paulo ni **Kristo akae ndani ya miyo yenu kwa imani.** Ni Roho ambaye anatupatisha nguvu ili **Kristo akae ndani ya miyo** yetu. Bwana Yesu anakuja kukaa ndani ya kila mwamini saa anapookolewa (Yn. 14:23; Ufu. 3:20), lakini hapa ombi la Paulo lilikuwa kwa Bwana *kupanga* ndani ya kila mwamini, ndani ya kila sehemu ya maisha yake; asihuzunishwe na ma-

semo, mawazo, makusudi na matendo mabaya; lakini yeze na mwamini wawe na ushirika mtamu. Hivi moyo wa mwamini unageuka kao la Kristo, pahali anapopenda kushinda – kama nyumba ya Maria, Marata, na Lazaro katika Be-tania. Moyo wetu unatawala maneno yote tunayofanya. Mtume anaomba Kristo aweze kutawala maneno yote ya maisha yetu, vitabu tunavyosoma, kazi tunayofanya, vyakula tunavyokula, namna tunavyotumika na mali yetu, maneno tunayosema – ndiyo, hata maneno madogo sana ya maisha yetu.

Tutafanana kupita na Bwana Yesu mwenyewe kwa kipimo tunapopatishwa nguvu na Roho Mtakatifu. Na kwa kipimo tunachofanana naye, Bwana atafurahi kukaa miyoni mwetu.

Kwa njia ya imani sisi tunafurahi vilevile kwa yeze kukaa ndani yetu. Tunamtegemea yeze wakati wote, tukijitoa na kumnyenyekea saa zote, na kumbuka saa zote kwamba anapanga ndani yetu.

Kufika saa hii Paulo alitaja Mungu Baba, Kristo, na Roho Mtakatifu ndani ya ombi lake. Aliomba Baba (sh. 14) kupatisha waamini nguvu kwa njia ya Roho yake (sh. 16) **ili Kristo** akae ndani ya **moyo** yao (sh. 17). Ni heshima na mapendeleo makubwa kwa sisi kuweza kufikia Mungu Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu kutusaidia sisi na watu wengine.

Kwa sababu Kristo anaweza kukaa ndani ya Mkristo bila kizuizo, Mkristo anapata **shina na msingi katika mapendo**. Hapa Paulo anatumika na mapando na jengo kama mfano. Shina la pando linalisha pando na kulipatisha nguvu. Jengo linasimama juu ya msingi. Scroggie alisema, “Sharti mashina ya uzima wetu yawe ndani ya udongo wa mapendo; na lazima imani yetu ikae juu ya mwamba wa mapendo daima.”⁸ **Kuwa na shina na msingi katika mapendo** ni kuwa na desturi ya kuishi

katika **mapendo**. Mwenye maisha ya mapendo anatenda mema, hajifikiri mwenyewe, ni mwenye roho ya kuvunjika, na mpole. Ni maisha ya Kristo yakionekana ndani ya mwamini (ona 1 Kor. 13:4-7).

3:18 Maneno haya Paulo aliyoomba yanasaadia mtoto wa Mungu kupata nguvu na kukomea aweze kufahamu **pamoja na watakatifu wote upana na urefu na urefu juu na urefu chini**.

Mbele ya kufikiri juu ya vipimo hivi, tuwaze kwanza juu ya maneno haya matatu, **na watakatifu wote**. Habari hizi ni kubwa sana, na hakuna mwamini peke yake anayeweza kufahamu hata nusu yao. Hivi inafaa kwa waamini pamoja kuwaza, kujifunza, na kuzungumuza juu yao. Roho Mtakatifu anaweza kuwaongoza na kuwanyeshea mashairi mengine vilevile kuongeza ufahamu wao.

Ni kama vipimo hivi vinasema juu ya mapendo ya Kristo. (Mapendo ya Kristo yanatajwa nyuma vilevile.) Kama ni hivi, tunaweza kuvieleza hivi:

Upana – dunia (Yn. 3:16)

Urefu – Kwa milele (1 Kor. 13:8)

Urefu chini – Hata mauti msalabani (Flp. 2:8)

Urefu juu – Mbinguni (1 Yn. 3:1-2)

Lakini vipimo hivi vinaweza kusema vilevile juu ya siri ambayo tunasoma habari zake tena na tena ndani ya Waefeso.

1. Tunasoma juu ya **upana** wake katika 2:11-18. Unasema juu ya upana wa neema ya Mungu inayookoa Wayuda na Mataifa, na kuwaingiza ndani ya kanisa. Siri ni juu ya Wayuda na Mataifa vilevile.

2. **Urefu** unanyosha muda toka milele hata milele. Waamini walichaguliwa zamaani ndani ya Kristo, mbele ya kuwekwa misingi ya ulimwengu (1:4). Kwa milele ya kuja, utajiri wa neema yake utafunuliwa kupita na kupita kwa njia ya wema wake kwetu katika Kristo

Yesu (2:7).

3. **Urefu chini** unaonekana wazi ndani ya 2:1-3. Tulizama ndani ya shimo kubwa sana la zambi, na aibu. Kristo alifikia uchafu na ubovu huu mkubwa, na alikufa kwa ajili yetu.

4. Tunaona **urefu juu** katika 2:6. Pale tulifufuliwa pamoja na Kristo, na kukalishwa katika pahali pa mbingu katika Kristo kushiriki ndani ya utukufu wake. Vipimo hivi ni vikubwa sana kupita ufa-hamu wetu.

3:19 Halafu mtume aliomba wataka-tifu waweze **kujuana na mapendo ya Kristo** ndani ya maisha yao yanayopita ufahamu yao. Hawataweza kuyajua yote kamwe, kwa sababu ni makubwa sana, kama bahari isiyo na ukingo, lakini Paulo aliomba waweze kujifunza kupita na kupita juu yake kila siku. Anaomba waweze kujuana na kufurahia kupita na kupita **mapendo** ya ajabu ya Bwana wetu wa ajabu.

Kumaliza ombi hili zuri sana Paulo aliomba wapate **kutimizwa kwa utimilifu wote wa Mungu**. Utimilifu wote wa uungu unakaa ndani ya Bwana Yesu (Kol. 2:9). Kwa kipimo anachokaa ndani ya miyo yetu kwa imani, kwa kipimo hiki **tunajazwa** kwa **utimilifu wa Mungu**. Haiwezekani kamwe kwa sisi kujazwa *na* utimilifu wa Mungu, lakini hili ndilo kusudi letu.

Lakini hata nyuma ya kueleza maneno haya, inatupasa kusema kwamba kuna maana ya ndani ndani tusiyofahamu. Wakati tunaposoma Maandiko tunaona kwamba tunasoma kweli ambazo zinatushinda kufahamu na kueleza. Siri tuliyosoma juu yake mbele ndani ya Efeso ingali siri, na tunaweza kushangaa tu juu ya ajabu bila mwisho la Neno la Mungu.

H. Wimbo wa sifa ya Paulo kwa Mungu (3:20, 21)

3:20 Paulo alimaliza ombi hili na wimbo unaojaza roho zetu na sifa. Alikuwa ameomba maneno makubwa,

na ukaramisu, maneno tusiyofikiri yan-gewezekana. Lakini Mungu **anaweza** kufanya mambo kuliko yote **tunayo-ombu au kufikiri**. Ona namna Paulo alivyovimbisha baraka hizi kubwa saba:

Anaweza

Anaweza kufanya

Anaweza kufanya tunayoomba

Anaweza kufanya tunayofikiri

Anaweza kufanya tunayoomba au kufikiri

Anaweza kufanya yote tunayoomba au kufikiri

Anaweza kufanya kuliko yote tunayoomba au kufikiri

Anaweza kufanya mambo kuliko yote tunayoomba au kufikiri

Anaweza kufanya sana kuliko yote tunayoomba au kufikiri

Mungu anajibu maombi kwa **kadiri ya uwezo unaotenda kazi ndani yetu**. Uwezo huu ni Roho Mtakatifu anayetu-mika siku zote ndani ya maisha yetu, akijaribu kutufananisha na Kristo, akihamakia zambi zetu, akiongoza maombi na kuabudu kwetu, na utumishi wetu. Kwa kipimo tunachojitoa kwake, kwa kipimo hiki ataweba kutufananisha na Kristo.

3:21 Kwake uwe utukufu katika kanisa na katika Kristo Yesu hata vizazi vyote kwa milele na milele. **Amina.** Mungu anastahili kupokea sifa kwa milele. Tunaona hekima na uwezo wake ndani ya majeshi ya malaika; ndani ya jua, mwezi, na nyota; ndani ya nyama, ndege, na samaki; ndani ya moto, mvua za mawe, theluji na ukungu; ndani ya upepo, milima, vilima, na miti; ndani ya wafalme na watu; wazee na vi-jana; katika Israeli na mataifa. Kusudi la vitu hivi vyote ni kusifu jina la Bwana (Zab. 148).

Lakini kuna jamii nyingine watakao-tolea Mungu **utukufu** bila mwisho, **ndilo kanisa** – Kristo aliye Kichwa chake na waamini, Mwili wake. Jamii hii ya wakombolewa itashuhudia kwa milele neema yake ya ajabu isiyo na ki-

fani. Williams aliandika:

Utukufu wa milele wa Mungu, kama Mungu na Baba utaonekana kwa eoni zote ndani ya Kanisa na ndani ya Kristo Yesu. Ajabu hili kubwa litaonekana kwa milele kwa njia ya Kristo na Kanisa kama Mwili mmoja.⁹

Hata kwa wakati wa sasa ingepasa kanisa kutukuza jina lake “kwa njia ya makusanyiko ya sifa, na kwa njia ya maisha safi ya watu wa kanisa, kwa njia ya kutangaza Habari Njema duniani pote, na kwa njia ya utumishi wa kusaidia wenye hitaji” (Erdman).

Sifa hii ni **kwa vizazi vyote, kwa milele na milele**. Paulo aliita watu kutolea Mungu sifa kwa milele ndani ya kanisa na ndani ya Kristo Yesu, na jibu la mioyo yetu ni **Amina!**

2. UTENDAJI WA MWAMINI KATIKA BWANA (Sura 4 – 6)

A. Maonyo kwa Wakristo kushiriki katika umoja (4:1-6)

4:1 Fungu lingine la barua kwa Waefeso linaanza hapa. Sura za mbele zilifundisha juu ya mwito wa Mkristo. Ndani ya sura tatu za mwisho kuna maonyo aweze **kutembea kama inavyostahili mwito alioitwa**. Kufika sasa tulisoma zaidi juu ya mahali pa heshima, pahali neema ya Mungu ilipotunyanya. Kuanza sasa sharti mwenendo wetu upatane na mahali hapa pa heshima. Ndani ya Waefeso 1–3 tulisoma juu ya pahali pa mbingu, lakini ndani ya sura 4-6 mafundisho ni zaidi juu ya maneno duniani, juu ya kanisa pahali tunapopanga, nyumba zetu, na watu wa dunia ambao wanatuzunguka. Stott alionyesha kwamba sura hizi za mwisho za Waefeso zinafundisha kwamba “inatupasa kuweka roho kuwa na umoja ndani ya kanisa, kuishi maisha matakifu, kuwa na salama na jamaa nyumbani mwetu, na kusimama imara ndani ya vita yetu

na majeshi ya pepo wabaya.”

Hii ni mara ya pili ambayo Paulo alijiita **mfungwa** – mara hii alijiita **mfungwa katika Bwana**. Theodoret alisema kwamba “Watu wa dunia walifikiri ilikuwa aibu, lakini Paulo alifikiri ni heshima kubwa sana kuwa mfungwa kwa Kristo, na alijisifu ndani ya vifungo vyake kupita mfalme ndani ya taji yake.”

Paulo alikuwa mfungwa kwa sababu ya kutii Bwana na uaminifu, na alionya wasomaji wake kutembea **kama inavyostahili mwito walioitwa**. Hakuwa-agiza au kuwaongoza, lakini anawasihi na upole na masemo ya neema.

Tunaona neno hili, **tembea**, mara saba ndani ya barua hii (2:2, 10; 4:1, 17; 5:2, 8, 15). Linaonyesha namna ya mwenendo mzima wa mtu. Mwendo **unao-stahili** ni mwendo unaofaa kwa Mkristo mwenye heshima kuwa kiungo cha mwili wa Kristo.

4:2 Sharti tuonyeshe roho ya Kristo ndani ya mambo yote ya maisha yetu. Inatupasa kuwa na:

Unyenyekevu – unyenyekevu wa kweli kwa sababu ya ushirika wetu na Bwana Yesu. **Unyenyekevu** unatufahamisha kwamba sisi wenyeWE si kitu, na unatuwezesha kufahamu kwamba watu wengine ni wenye heshima kupita sisi. Unyenyekevu ni mbalimbali na kiburi.

Upole – ni kunyenyekea maneno Mungu anayofanya, bila kunungunika wala kuasi, na kupokea mabaya ambayo watu wanatutendea bila kulipiza kisasi. Tunaona upole namna hii vizuri zaidi ndani ya maisha ya Bwana Yesu aliyesema, “Mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo” (Mt. 11:29).

Uvumilivu – roho ya saburi hata kwa wakati wa kukasirishwa kwa muda mrefu.

Mukichukuliana katika mapendo – maana ni kuvumilia kuanguka kwa watu wengine, au desturi zao zilizo mbali na desturi zetu, tabia zao, na uwezo wao

kwa kazi namna namna. Ni kupenda na mapendo ya kweli wale ambao wana-tukasirisha, kutusumbua, au kutuha-yarisha.

4:3 Mukiangalia sana kuchunga umoja wa Roho katika kifungo cha salama. Kwa njia ya kusimamisha kanisa, Mungu aliondosha kitu kikubwa zaidi kilichotenga watu tangu zamani, mtengo katikati ya Wayuda na Mataifa. Maneno ambayo yaliwatenga yaliondoshwa ndani ya Kristo Yesu. Lakini namna gani neno hili litawezekana ndani ya ushirika wao wa kila siku? Watakaa na ushindani ro-honi? Watawaza juu ya kusimamisha “Kanisa la Kristo kwa Wayuda” na “Kanisa kwa Mataifa?” Kuzuiza neno hili lisitokee Paulo alisihii Wakristo sasa kukaa na umoja.

Aliwaonya **kuchunga umoja wa Roho.** **Roho Mtakatifu** amefanyiza wa-amini wote wa kweli kuwa moja ndani ya Kristo; **Roho** mmoja anakaa ndani ya Mwili. Hakuna kitu kinachoweza ku-haribu **umoja** namna ule. Lakini kwa njia ya kugombana na kubishana inawe-zezeka kwa waamini kukana kweli hii. Maana ya **kuchunga umoja wa Roho** ni kukaa pamoja na salama. Ni **salama** inayofunganisha viungo vya mwili pa-moja hata kama wao ni namna mbalimbali kabisa. Wakati wa magawa-nyiko, ni nyepesi kwa watu kutaka kuanza jamii nyingine. Lakini waki-ongozwa na Roho, watafahamu kwamba kwa maneno yaliyo lazima, sharti wawe na umoja. Kwa maneno walio na shaka juu yao, wanaweza kuchagua. Kwa ma-neno yote, sharti wawe na mapendo. Sisi sote tungali na tabia ya zamani ndani yetu inayoweza kuharibu kanisa, au kazi lo lote lingine la Mungu. Hivi inatupasa kuzamisha maneno sisi wenyewe tunayotaka, na kutumika pamoja na wengine na **salama** kwa utukufu wa Mungu na baraka ya watu wote.

4:4 Kwa pahali pa kuweka roho juu ya maneno ambayo yanatutenga, tuweke

roho zaidi juu ya maneno saba yaliyo msingi kwa umoja wa kweli wa Wakristo.

Mwili mmoja. Waamini wote wa kweli tangu Pentekote kufika siku wata-kapopelekwa mbinguni ni ndani ya **mwili mmoja**. Si neno kama ni watu wa taifa au rangi gani, au wakisema lugha gani. Waamini wakifungana ndani ya aina na jamii mbalimbali wanazuiza kweli hii. Matengo yote yanayosi-mamishwa na watu yataondoshwa wa-ki Mwokozi atakaporudi.

Roho mmoja. Roho Mtakatifu ana-yekaa ndani ya kila mwamini mmoja mmoja (1 Kor. 6:19) anakaa ndani ya Mwili wa Kristo vilevile (1 Kor. 3:16).

Tumaini moja. Kila mwamini kani-sani anaitwa kuwa pamoja na Kristo, ku-fanana naye, na kushiriki katika utukufu wake bila mwisho. **Tumaini hili moja** ni kwa maneno yote yanayongojea watakatifu saa ya kurudi kwa Bwana Yesu, na nyuma ya kurudi kwake.

4:5 Bwana mmoja. “Kwa maana hata wakiwa walioitwa miungu, au katika mbingu au katika dunia, kama ni miungu mingi na bwana wengi; lakini kwetu kuna Mungu mmoja ... na kuna Bwana mmoja, Yesu Kristo, kwa ye ye vitu vyote vimekuwa, na sisi kwa ye ye” (1 Kor. 8:5,6; ona vilevile 1 Kor. 1:2).

Imani moja. Ni **imani** ya Wakristo, “imani waliyopewa watakatifu mara moja tu” (Yuda 3), na kulindwa kwasi ndani ya Agano Jipyta.

Ubatizo mmoja. Neno hili ni kweli kwa njia mbili. Kwanza kuna **ubatizo mmoja** kwa Roho. Kwa njia ya ubatizo huu wote wanaoamini Kristo wanaingi-zwa katika mwili mmoja (1 Kor. 12:13). Na vilevile kuna **ubatizo** mwininge kwa njia yake waamini wanakiri kwamba wao ni mamoja na Kristo kwa mauti yake, kuzikwa kwake, na ufufuko wake. Hata kama kwa wakati wa sasa watu wanabatizwa kwa njia mbalimbali, kuna ubatizo mmoja tu wa waamini unao-

kubaliwa ndani ya Agano Jipy, ndio ubatizo kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu. Kwa njia ya kubatizwa hivi, waamini wanakiri kwamba wao ni wafuata wa Kristo sasa, ya kwamba wamezika tabia yao ya zamani, na wanakusudi kufuata Bwana tu katika maisha yao mapya.

4:6 Mungu mmoja. Kila mtoto wa Mungu anatambua **Mungu mmoja na Baba ya** wakombolewa **wote**, aliye:

Juu ya yote – mwenye enzi wa ulimwengu.

Katika yote – Anatumika kwa njia ya yote, akitumia kila kitu kutimiza makusudi yake.

Ndani yenu yote – anapanga ndani ya waamini wote, na ni pahali pote kwa saa moja.

B. Utaratibu kwa matumizi mazuri ya viungo vya mwili (4:7-16)

4:7 Kuna kweli nyininge pamoja na ile ya umoja wa mwili wa Kristo, ndiyo kweli ya tofauti ya viungo vya mwili wake. Kila kiungo kinapewa kazi fulani. Hakuna viungo viwili vilivyo sawasawa kabisa, na hawapewi kazi sawasawa. Kila mtu katikati yetu anapewa neema kwa **kadiri ya kipimo cha zawadi ya Kristo**. Ni kusema kwa namna Kristo anavyowaza ni vizuri. Kama **zawadi ya Kristo** hapa ni Roho Mtakatifu (Yn. 14:16, 17; Mdo. 2:38, 39), halafu tunawaza ni Roho Mtakatifu ambaye anagawia kila mwamini zawadi fulani, pamoja na uwezo ambaa anahitaji kutumika na zawadi yenyewe. Kila mtu aki-fanya kazi aliyopewa, Mwili wa Kristo unapata nguvu kwa roho, na hesabu ya viungo vyake inaongezeka vilevile.

4:8 Kwa kusaidia kila mtoto wa Mungu kutambua na kufanya kazi yake, Bwana ametoa **zawadi** nyininge za utumishi, kwa kazi ya kanisa. Zawadi hizi ni mbali na zile ambazo tuliona ndani ya shairi 7. Kila mwamini ana zawadi (sh. 7), lakini si kila mwamini ni moja ya **za-**

wadi zinazotajwa ndani ya shairi 11. Kusudi la **zawadi** hizi za shairi 11 ni ili mwili uweze kupata nguvu.

Kwanza tunaona ya kuwa mwenye kutoa **zawadi** hizi nyininge ni Bwana Yesu Kristo aliyefufufuliwa, aliyepanda mbinguni, na kutukuzwa. Paulo alitaja Zaburi 68:18 kama unabii ya kuwa Masiya atapanda mbinguni, atashinda adui zake na kuwafunga, na, kama zywabu kwa kushinda kwake, atapokea **zawadi** kwa **watu**.

4:9 Lakini namna gani Masiya aliweza kupanda mbinguni? Aliishi mbinguni pamoja na Mungu Baba tangu milele! Ni wazi ya kwamba kwa kuweza kupanda mbinguni, ilimpasa kushuka toka mbingu kwanza. Hivi tunaweza kufafanua shairi 18 la Zaburi 68 hivi “**‘Alipanda,’ – maana yake ni kusema kwamba ye ye alishuka vilevile mpaka pande za chini za inchi.**” Tunajua kwamba hili ndilo neno lililotokea. Bwana Yesu **alishuka** kwanza hata sanduku ya kulisha nyama kwa Betelehemu, mauti kwa msalaba, na kaburi. Walimu wengine wanafikiri maana ya **pande za chini za inchi** ni hadeze au gehena, lakini hii si maana ya kweli. Ndiyo, kwa kupanda mbinguni ilimpasa kushuka kwanza kwa dunia lakini si kwa hadeze. Na vilevile Maandiko yanaonyesha kwamba roho ya Kristo alikwenda mbinguni, si kwa hadeze, wakati alipokufa (Lk. 23:43, 46).

4:10 Unabii wa Zaburi 68:18 kwa-mba atashuka chini ultimizwa kabisa kwa njia ya Bwana Yesu kutwaa utu, kufa na kuzikwa. Yule **aliyeshuka** toka mbingu ndiye aliyeshinda zambi, She-tani, pepo wachafu na mauti, na **aliyepanda** vilevile **juu sana** kupita mbingu (za nyota) **ili ajaze vitu vyote**.

Anajaza vitu vyote, maana ye ye ni mwanzo wa baraka zote, mwenye njema zote, na mwenye enzi yote.

Neno kubwa ndani ya mashairi 8-10 ni ya kwamba mwenye kutoa zawadi

hizi ni Kristo nyuma ya kupanda kwake mbinguni. Zawadi namna hii hazikuwa mbele ya kurudi kwake mbinguni. Linaonyesha vilevile ya kwamba kanisa halikuwa katika Agano la Kale; kama kungalikuwa na kanisa, kanisa hili lingalikosa kuwa na zawadi.

4:11 Tunaona sasa majina ya zawadi hizi na tunashangaa kwa sababu si akili au uwezo kufanya kazi fulani, lakini ni watu. **Naye alitoa wengine kuwa mitume; na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wahubiri wa Habari Njema; na wengine kuwa wachungaji na walimu.**

Mitume walikuwa watu waliotumwa na Bwana kuhubiri neno na kusimamisha makanisa. Walikuwa watu waliorna Kristo nyuma ya ufufuko wake (Mdo. 1:22). Walikuwa na uwezo kufanya maajabu (2 Kor. 12:12) kwa kuhakikisha habari walizohubiri (Ebr. 2:4). Pamoja na manabii wa Agano Jipya, kazi yao ilikuwa zaidi kuweka msingi wa kanisa (Efe. 2:20). Mitume ambao tunasoma juu yao hapa ni wale tu waliokuwa mitume *nyuma* ya kupanda kwa Kristo mbinguni.

Manabii ndio wale waliosema kwa ajili ya Mungu. Walipokea funuo toka Bwana na walizijulisha kwa kanisa. Maneno waliyosema wakiongozwa na Roho Mtakatifu yalikuwa maneno ya Mungu.

Hatuna mitume na manabii namna hii kwa wakati wa sasa. Utumishi wao ulikwisha wakati msingi wa kanisa ulipowekwa na kanuni la Agano Jipya lilipomalizwa. Tulisema mbele ya kumba **manabii** hawa walipewa na Kristo nyuma ya kwenda kwake mbinguni.

Wahubiri wa Habari Njema wana-tangaza habari njema za wokovu. Wametayarishwa na Mungu na akili ya kuleta wapotevu kwa Kristo. Wanajua namna gani kutambua hali ya roho ya mwenye zambi, kupima zamiri yake, kujibu maulizo yake, na kuamsha hamu

ndani ya roho yake kupokea Kristo. Na wakati anapokwisha kugeuka mwamini, mhubiri anapatisha imani yake nguvu na Neno la Mungu. Kisha anafikisha mwamini huyu wa sasa kwa kanisa pahali Wakristo watakapolishia na Neno la Mungu na kumsaidia kukomea katika imani.

Wachungaji wanasaidia kuchunga kondoo za Kristo, aliye Mchungaji Mku-bwa. Wanaongoza na kulisha kundi. Utumishi wao ni kushauri, kuonyesha makosa, kutia moyo, na kufariji kondoo.

Utumishi wa **wachungaji** unafungana karibu-karibu na kazi ya wazee. “Mchungaji” unaonyesha wazi zawadi ya mtu. “Mzee” unaonyesha madaraka yenye. Ndani ya Agano Jipya tunaona wachungaji wachache katika kanisa moja (Mdo. 20:17, 28; 1 Pet. 5:1, 2), si mchungaji mmoja au mzee mkuu.

Walimu ni watu wanaowezeshwa na Mungu kueleza maneno ya Biblia, kutafsiri maana yake, na kuonyesha kama ingepasa kufanya kazi gani ndani ya miyo na zamiri za waamini.

Kwa sababu **wachungaji na walimu** wanaungana ndani ya shairi hili, watu wengine wanafikiri hii ni zawadi moja tu na ingetupasa kuandika “mchungaji-mwalimu.” Si hivi kila mara. Mtu ana-weza kuwa mwalimu bila kuwa na roho ya mchungaji. Na mchungaji anaweza kutumika na Neno la Mungu bila kuperwa zawadi ya kufundisha. Kama **wachungaji na walimu** ni mtu mmoja ndani ya shairi 11, halafu ndani ya 2:20 mitume na manabii ni mtu mmoja vilevile.

Lazima tufahamu neno moja lingine, ndilo ya kwamba zawadi zilizopewa na Mungu ni mbalimbali na akili ya asili. Hakuna msiyeamini, hata akiwa na akili nyingi, anayeweza kuwa mhubiri, mchungaji au mwalimu namna tunavyoona ndani ya Agano Jipya. Neno hili ni kweli kwa Mkristo vilevile, kama asipopokea zawadi ile. Zawadi za Roho si za uli-

mwengu. Zinawezesha mtu kufanya maneno asiyoweza kufanya kama mtu.

4:12 Sasa tutaona kazi au kusudi la zawadi. Ni kwa **kukamilisha watakatifu kwa kazi ya utumishi, hata mwili wa Kristo ujengwe**. Maneno haya yanafuatana hivi:

1. Zawadi zinatayarisha **watakatifu**.
2. Halafu **watakatifu** wanatumikia.
3. Kisha **Mwili** unapatishwa nguvu.

Utumishi huu si kazi fulani watu wanayojifunza chuoni. Ni *utumishi* au kazi namna namna kwa Mungu. Shairi hili linatufundisha kwamba ingepasa kila mtu kuwa mtumishi.

Zawadi hizi ni kukamilisha au kutayarisha Wakristo wote kufanya kazi ya Bwana, na kupatisha **mwili wa Kristo** nguvu kwa njia hii. Vance Havner alisema:

Kila Mkristo amepewa kazi ya kuhubiri Habari Njema. Haifai afikie kanisa kusikiliza mhubiri tu, lakini atoke kanisa vilevile na kuitangaza maneno aliyosikia. Ingepasa kila Mkristo kutumikia Bwana na nguvu yake yote. ... Ndiyo, wengine wamepewa kazi ya mchungaji, au mwalimu, au mhubiri wa Habari Njema. Walipewa kazi hii kwa sababu gani? Kwa kukamilisha watakatifu kwa kazi ya utumishi.¹⁰

Haifai kwa watu fulani tu kufanya kazi ya Mungu. Neno hili linazuiza watu wa Mungu wasipate nguvu. Linazuiza vilevile kazi ya kuhubiri Habari Njema kwa dunia nzima, na linazuiza kanisa kupata nguvu. Hakuna mafundisho ndani ya Biblia yanayoruhusu tofauti katikati ya maaskofu na watu wengine wa kanisa. Labda tofauti hii ni neno linazuiza kuenea kwa Habari Njema.

4:13 Shairi hili linajibu ulizo kama kanisa litakaa kupata nguvu kufika wakati gani. Hili ndilo jibu lenyewe: **Kufika wakati sisi sote tutakapofika umoja** wa imani na kukomea na ku-

patana.

Umoja. Wakati Bwana atakapokuja kupeleka kanisa lake mbinguni, sisi sote tutafikia **umoja wa imani**. "Sasa tumaona kama katika kioo," nusu nusu (2 Kor. 3:18). Tuna mafikiri mbalimbali juu ya maneno mengi, lakini kwa wakati ule sisi sote tutapatana kabisa. Na tutafikia **umoja wa ... kujuwa sana Mwana wa Mungu**. Hapa duniani tuna mawazo namna mbalimbali juu ya Bwana, kama akionekana namna gani, maana ya mafundisho yake. Lakini kwa wakati ule tutamwona namna alivyo, na tutajua namna tunavyojuliwa (1 Kor. 13:12).

Kukomea. Saa tutakapolekwa mbinguni, tutakomea kabisa vilevile. Waamini mmoja mmoja, na kama Mwili wa Kristo, tutafikia ukamilifu katika kukomea kwa roho.

Kufanana. Na sisi sote tutafananishwa naye. Sisi sote tutakuwa wema sawasawa na **Kristo**. Na kanisa la dunia nzima litakuwa mwili unaokomea, na unaofaa kabisa kwa Kichwa chake kikamilifu. "Utimilifu wa Kristo ni kanisa, utimilifu wake anayetimiza vyote katika vyote" (FWG). Maana ya **kipimo cha urefu** wa kanisa ni kutimia kwa kukomea kwake na shauri la Mungu kwa kuongezeka na kupata nguvu kwake.

4:14 Wakati zawadi hawa wanapofanya kazi yao namna walivyoongozwa na Mungu, na waamini wakitumikia Bwana, wanaepuka hatari namna tatu – kutokukomea, kutokusimama imara, na kudanganywa.

Kutokukomea. Waamini ambao hawajitoi kabisa kwa kazi ya Kristo watakaa **watoto** tu kwa imani. Mwandishi kwa Waebrania alisema na watu namna hii, "Kwa wakati uliopita imewapasa ninyi kuwa walimu, lakini munahitaji mtu kuwafundisha ninyi tena – (Ebr. 5:12).

Kutokusimama imara. Hatari nyinegine kwa Wakristo wasiokomea ni

kugeukageuka **huko na huko** na kumpima na kudanganywa na maneno ya dini mbalimbali.

Kudanganywa. Kudanganywa ni hatari kubwa zaidi. Waamini walio kwanza watoto kwa imani hawajuani na neno la haki na hawatambui maneno yaliyo mema na mabaya (Ebr. 5:13, 14). Wanakutana na mtu wa dini ya uwongo mwenye bidii sana. Mtu huyu anatumika na masemo ya dini, na kwa sababu hii waamini wanafikiri bila shaka mtu huyu ni mwamini wa kweli. Kama wangalijifunza Biblia wao wenyewe, kama wanagetambua udanganyifu wa masemo ya mtu huyu. Lakini sasa **wanatupwa huko na huko** kwa kila upepo wa elimu, kwa hila ya watu, na kuingizwa ndani ya mafundisho ya uwongo.

4:15 Mashairi 15 na 16 yanaonyesha njia nzuri kwa Mwili wa Kristo kupata nguvu. Kwanza inapasa viungo vya mwili kushika mafundisho ya kweli: **lakini, tukisema kweli** ... Haifai hata kidogo kuruhusu maneno yasiyopatana na kweli hii. Na vilevile inapasa kutangaza kweli hii na roho nzuri: **lakini tukisema kweli katika mapendo.** Isipokuwa hivi, usuhuhuda wetu si sawa.

Kristo alitoa watu wenyewe zawadi kuytarisha watakatifu kwa kazi yake. Wakati wanapojoitoo kwa utumishi wao, **wanapata kukua katika maneno yote ndani ya Kristo.** Ndani ya **maneno yao yote** na sehemu zote za maisha yao wanageuka kufanana kupita na kupita **naye.** Wakati Kristo aliye Kichwa ana-poweza kufanya mapenzi yake ndani ya kanisa, Mwili wake utakuwa mfano mzuri zaidi kwa ulimwengu.

4:16 Ni kusudi la Bwana Yesu kwa kanisa kupata nguvu, na ni yeye vilevile ambaye analifanyiza kupata nguvu. **Toka kwake viungo vya mwili vinaunganishwa na kushikanishwa** kwa njia ya ajabu. Kila kiungo kinata-yarishwa kwa pahali na kazi yake katika Mwili, na **kufunganishwa** vizuri na

kila kiungo kingine. Kila kiungo kinahitajiwa kabisa, **na kushikanishwa kwa kusaidia kwa kila kiungo kingine.** Mwili wa mtu ni zaidi mi-fupa, moyo, mishipa ya damu, tumbo, vivi hivi. Mifupa na vipande vingine vinafungwa pamoja na viungo na mishipa. Kila kiungo na kila mshipa una kazi kusaidia mwili kupata nguvu na kuwa na faida. Ni vivyo hivyo katika **mwili** wa Kristo. Kila kiungo, hata mwamini asiyekuwa na heshima hapa duniani, anahitajiwa.

Wakati kila mwamini anapofanya kazi yake kwa pahali pake, **mwili** unapata nguvu vizuri. Ni kama mwili wenyewe unafanyiza mwili kupata nguvu. Ni kusema kwamba mwili unakaa kupata nguvu kwa kipimo viungo wanavyokulisha roho zao na Neno la Mungu na maombi na kuabudu na kushuhudia Kristo. Na zaidi ya ile unajijenga wenyewe **katika mapendo.** Ni kusema viungo wanachungana na kupendana. Wakristo wakikaa ndani ya Kristo na kufanya kazi yao kanisani watacaa karibu kupita waamini wengine **katika mape-ndo** na umoja.

C. Maonyo kwa waamini kuwa na mwenendo mpya (4:17 – 5:21)

4:17 Hapa mtume alianza kuonya waamini kutembea katika mwenendo mpya. Maonyo haya yanaendelea kufika 5:21. Maana ya kushuhudu **katika Bwana** ni kushuhudu na amri ya **Bwana.** Akiongozwa na Mungu, ana-onya Wakristo kuachana na maneno mabaya yote ya maisha yao ya zamani, kama vazi chafu, na kuvaajnjema zote na ubora wa Bwana Yesu Kristo. **Musitembee tena namna Mataifa wanavyotembea.** Hawakuwa Mataifa tena; walikuwa Wakristo. Hivi ingepasa wageuze mwenendo wao kupatana na neno hili. Paulo aliona dunia hii bila Kristo kama mataifa yaliyozama ndani ya ujinga na hali mbaya. Alitaja maneno

mabaya sana saba, ndiyo:

Bila kusudi. Walitembea **katika ubatili wa nia zao.** Maisha yao yalikuwa bure, bila kuzaa matunda ya faida. Walikaa kufanya maneno mengi, lakini hawakupata nguvu katika imani, lililo neno la faida zaidi.

4:18 Wapofu. Ufahamu wao **ulitiwa giza.** Wakiwa watu, hawakuweza kufahamu kweli za roho. Na kwa sababu walikataa kujua Mungu wa kweli, aliwahukumu na upofu.

Bila utawa. Walitengwa mbali na uzima wa Mungu, ndilo tunda la ujinga wao wa kusudi, na kwa sababu ya ugumu wa mioyo yao. Walikuwa wamekataa nuru ya Mungu ndani ya muumbo wa dunia na ndani ya damiri zao, na waligeuka kuabudu sanamu. Kisha walikuwa wameanguka na kwendwa mbali zaidi na Mungu.

4:19 Bila haya. Damiri zao hazikuwashitaki tena.

Unyonge. Walijitoa **wenyewe kutenda uasherati**, ndiyo matendo maovu. Uasherati ulikuwa zambi kubwa zaidi ya Mataifa. Ni vivyo hivyo katika Mataifa hata sasa.

Bila adabu. Walijitoa wenyewe kutenda **kila namna ya uchafu.**

Kwa choyo. Hawakushiba kamwe. Hamu yao kwa zambi hii ilikaa kuongezeka.

4:20 Maneno haya yalikuwa namna nyingine kabisa na **Kristo** ambaye Waefeso walikuwa wamejua na kupenda! Alikuwa mwenye usafi na utakatifu. Hakujua zambi, hakufanya zambi, zambi haikuwa ndani yake.

4:21 Ndiyo, **mulimsikia na kufundishwa naye**, maana yake wote waliokuwa **wamesikia** Kristo na **waliokuwa wamefundishwa naye** walikuwa wamemjua kama mwenye utakatifu na utawa. Maana ya **mulimsikia** ni kumsikia na imani – kumpokea kama Bwana na Mwokozi. **Walifundishwa naye** ni mafundisho Waefeso waliyo-

pokea wakati walipotembea pamoja na Bwana nyuma ya kuokolewa kwao. **Kama kweli ilivyo katika Yesu.** Yesu hafundishi tu kweli; yeche mwenyewe ni kweli katika mwili (Yn. 14:6). Jina hili **Yesu** linaludisha mawazo yetu kwa maisha yake hapa duniani, kwani hili ni jina lake wakati alipotwaa utu. Maisha yake safi na bila kipaku alioishi kama mtu duniani ni mbalimbali kabisa na mwenendo wa Mataifa ambaao Paulo aliandika juu yake sasa tu.

4:22 Kwa wakati tunapookolewa tunajifunza kwamba tunaondosha **yule mtu wa zamani, anayeharibika kwa kufuata tamaa za udanganyifu.** Maana ya **mtu wa zamani** ni namna mtu alivyokuwa mbele ya kuokolewa, namna alivyokuwa kama mtoto wa Adamu. Alikuwa mwovu, **mdanganyifu** na mwenye tamaa kwa zambi ambazo zinaonekana kuwa tamu lakini zinazozaa uchungu tu. Mahali ya mwamini ni ndani ya Kristo sasa, na **mtu wa zamani** alisulibishwa na kuzikwa pamoja na Kristo. Inafaa kwa mwamini kumhesabu kuwa mfu. Paulo alionyesha hapa kweli ya kwamba tumendonsha **mtu wa zamani** kabisa.

4:23 Kweli nyininge Waefeso walijojifunza ilikuwa kwamba walikuwa **wakifanywa wapya katika roho ya nia zao.** Mawazo yao yaligeuka kabisa. Mafikiri yao ya zambi na uchafu yali kombolewa na mawazo matakatifu. Hawaongozwi sasa na mawazo ya wasioamini, lakini na Roho ya Mungu.

4:24 Neno la tatu walilojifunza lilikuwa kwamba walikuwa **wamevaa mtu mpya.** **Mtu mpya** ni mwamini ndani ya Kristo. Ni kiumbe kipyta; maneno ya zamani yamepita; tazama maneno yote yamekuwa mapya (2 Kor. 5:17). Namna hii **mpya** ya mtu **aliumbwa** kwa namna ya Mungu, maana kufanana naye. Neno hili linaonekana katika **haki na utakatifu wa kweli.** Maana ya **haki** ni kutendea watu

wengine na haki. **Utakatifu** ni heshima na utawa kwa Mungu.

4:25 Halafu Paulo aliwakumbusha kwamba walikuwa wameondosha mtu wa zamani na wamevaa mtu mpya kwa njia ya kufunganishwa na Kristo. Sharti neno hili lioneokane ndani ya kugeuka kabisa kwa mwenendo wao wa kila siku.

Wanaweza kufanya hivi kwa njia ya **kuondosha uwongo** na kuukomboa na kweli. Kuna namna mbalimbali za **uwongo**, ndizo kusema maneno yasiyo kweli kabisa, udanganyifu, kutokutimiza ahadi, ubembelezi, kutokutenda haki kwa maneno ya kulipa kodi kwa serikali. Ni lazima kwa Mkristo kusema haki tu. Maisha ya Mkristo asiyesema na kutenda kweli ni ushuhuda mbaya.

Sharti tuseme kweli kwa watu wote. Lakini wakati Paulo aliposema juu ya **jirani** hapa, alifikiri zaidi juu ya waamini wenzetu, kwani **sisi ni viungo, kila mmoja kiungo cha mwenzake** (ona Rom. 12:5; 1 Kor. 12:12-27). Kwa Mkristo kusema uwongo kwa Mkristo mwagine ni kama kiungo kimoja cha mwili kikiumiza kiungo kingine na kusudi, au kwa jicho kudanganya mwili wakati hatari inapokaribia.

4:26 Neno lingine ambalo linatupasa kufahamu ndani ya maisha yetu mapya ni **gazabu** ya zambi na kasirani ya haki. Mara nyininge inapasa mwamini kuwa na **kasirani** ya haki, kwa mfano wakati watu wanaposema maneno mabaya juu ya Mungu. Saa ile mwamini anaagizwa **kukasirika**. Kasirani kwa wakati wa namna hii inaweza kuwa haki. Lakini mara nyininge ni zambi kukasirika. Tunakatazwa kukasirika kwa sababu ya uovu, wivu, na machukio ambayo watu wanatutendea. Aristote alisema, “Ni nyepesi kukasirika, lakini ni nguvu kujua kama ikitupasa kukasirikia nani, kwa kipimo gani, na kwa namna inavyofaa.”

Kama mwamini akishindwa na **gazabu** isiyo haki, sharti akiri neno hili

mara moja na kuliacha. Inapasa alikiri kwa Mungu na kwa mtu ambaye alimkasirikia. Haifai akae kuficha uchungu rohoni mwake. **Jua lisishuke na uchungu wenu haujawkwisha bado.** Lazima tutengeneze mara moja neno lo lote linaloharibu upatano wetu na Mungu na ndugu zetu.

4:27 Kama tusipokiri zambi ya kasirani, tunafungulia Shetani njia kutu angusha ndani ya zambi nydingine vilevile. Hivi haifai kwetu kutoa uzuru kwa nia ya kuzuru wengine, gazabu, wivu, na machukio ndani ya roho zetu. Maneno haya yanaharibu ushuhuda wetu kwa Kristo, yanakwaza wasioamini, yanachukiza waamini wengine, na yanajiumiza sisi wenyewe kwa njia ya roho na mwili.

4:28 Sasa Paulo alionyesha kwamba kuiba ni mbalimbali na kushiriki. Mtu wa zamani anaiba; mtu mpya anashiriki na wenyе mahitaji. Sharti tuondoshe mtu wa zamani na kuva mtu mpya! Agizo la Paulo, “**Yeye aliyeiba asiibe tena**” linaonyesha wazi kwamba Wakristo wangali wenyе zambi. Wangali na tabia yao ovu ya zamani ambayo inajifikiri yenyewe tu. Lazima tuihesabu kama kitu kinachokwisha kufa ndani ya mwenendo wetu wa kila siku. Unyanganyi ni namna namna. Labda ni kuiba maneno makubwa makubwa, au kutokulipa deni, au kuiba saa ya bwana wa kazi kwa njia ya kushuhudia Kristo kwa saa ile, vivi hivi. Watu walikatazwa kuiba tangu zamani. Sheria ya Musa ilikataza watu kuiba (Kut. 20:15). Lakini maneno yanayofuata yanaonyesha kwamba maagizo haya ni kwa Wakristo vilevile. Haifai kuacha kuiba tu, lakini inatupasa **kufanya kazi** njema, ili tuweze kuwa na mali kusaidia watu wengine wenyе mahitaji. Neema ya Mungu tu, si sheria, inatuwezesha kufanya hivi.

Agizo hili ni neno kubwa kabisa. Ni desturi ya watu kutumika kazi kwa kuji-

patia vitu wanavyohitaji na kutamani. Wakati mshahara wao unapoongezeka, wanaongeza vilevile hesabu ya mali wanayotumia kwa maisha yao wenyewe. Zaidi watu wanajifikiri wenyewe tu. Lakini shairi hili linatuonyesha kwamba njia nzuri kupita kuwaza juu ya mshahara wetu ni kuchunga sehemu yake tu kwa mahitaji yetu na ya jamaa yetu, na kutumika na mali inayobaki kusaidia wenyе **mahitaji**, katika inchi yetu, na kwa inchi nyingine vilevile. **Mahitaji** haya ni makubwa kabisa!

4:29 Mtume alisema vilevile juu ya masemo. Masemo mengine yana faida na yanajenga wasikiaji; mengine ni bure. Masemo **maovu** yanatufikirisha juu ya maneno machafu, matukano, habari chafu, vivi hivi. Lakini tunafikiri hapa mwandishi aliwaza zaidi juu ya mazungumuzo bure, yasiyo na faida. Paulo aliandika juu ya masemo machafu na mapotovu ndani ya 5:4; hapa katika sura 4 alisema nasi kuachana na masemo bure, na kuyakomboa na masemo ya faida. Inapasa masemo ya Mkristo kuwa:

Masemo ya **kujenga** wasikiaji.

Masemo ya **kufaa** kwa wakati ule.

Masemo ya **neema**, na **kuwapa neema wale wanaosikia**.

4:30 Wala musihuzunishe Roho Mtakatifu ya Mungu, ndani yake mulitiwa mhuri hata siku ya ukombozi. Tukiwaza juu ya shairi lililotangulia, tunafahamu kwamba masemo bure ya-nahuzunisha Roho Mtakatifu. Na mash. 25-28 yanatukumbusha kwamba wongo, kasirani isiyo ya haki, na wizi zinamwumiza vilevile. Sharti tuepuke kila kitu na maneno yo yote ambayo yanamhuzu-nisha. Kwa sababu gani?

1. Kwa sababu yeche ni Roho *Mtakatifu*. Anachukizwa na kitu cho chote kisi-cho takatifu.

2. Yeye ni Roho Mtakatifu ya **Mungu**, mmoja wa Utatu Mtakatifu, ndio Mungu Baba, Mungu Mwana, na Roho

Mtakatifu.

3. Tulitiwa mhuri naye hata siku ya ukombozi. Kama tulivyosoma mbele, mhuri unaonyesha kwamba kitu chenye mhuri ni mali ya nani. Roho Mtakatifu ni mhuri kuhakikisha ya kwamba tutalindwa kufika wakati Kristo atakapokuja kutupeleka kwake, na wokovu wetu utakapotimia. Ona hapa namna Paulo alitumia haki ya amani ya mwamini kwa milele kama sababu kuwba zaidi kwa sisi *tusitende* zambi.

Tunaona kwamba Roho Mtakatifu anaweza kuhuzunishwa, hivi tunafahamu kwamba yeche si uwezo fulani tu. Anatupenda vilevile. Kazi anayopenda kufanya zaidi ni kutukuza Kristo na kugeuza mwamini kufanana naye (2 Kor. 3:18). Wakati Mkristo anapofanya zambi, inapasa Roho Mtakatifu kuacha kazi yake ya kutukuza Kristo, na kutumika kurudisha mwenye kutenda zambi kutubu na kukiri zambi yake.

4:31 Sharti zambi zote za tabia na ulimi ziondoshwe. Paulo alitaja mengine ya maneno haya hapa:

Uchungu – chuki, kukataa kusamehe, na kukaa na uchungu rohoni.

Hasira – kuwa na gazabu ya gafula.

Kasirani – uadui, uchungu wa roho.

Kelele – makelele ya kasirani kujaribu kushinda mabishano ya adui.

Matukano – kuzarau watu wengine.

Ubaya – Kila namna ya ubaya.

4:32 Sharti zambi zile za tabia, za dunia ziondoshwe, na kukombolewa na matendo ya kikristo:

Mema – kuwaza juu ya hali ya watu wengine, na kuwasaidia bila kujifikiri mwenyewe, hata kama ikitupasa kujinyima wenyewe kufanya hivi.

Wenye huruma – kwa watu wengine na kuwahurumia na kushiriki kubeba mizigo yao.

Usamehe – Kuwa tayari kusamehe zambi za wengine, hata kama walitukosea sisi, na bila kutaka kulipa kisasi.

Mungu mwenyewe ndiye mfano mku-

bwa zaidi wa usamehe. Msingi wa usamehe wake ni kazi ya Kristo kwa Kalvari. Na sisi tusiostahili hata kidogo ni wenye kupokea usamehe huu. Lakini haiwezekani kwa Mungu kusamehe zambi na haki bila mwingine kubeba azabu ile. **Ndani ya Kristo** na kazi yake Mungu alipata njia ya haki kutusamehe.

Alitusamehe deni kubwa sana, hivi inatupasa sisi kusamehe deni ndogo za watu (ona Mt. 18:23-28). Lenski ali-fundisha:

Mara moja wakati mtu anaponite-ndea mabaya inanipasa kumsamehe. Halafu roho *yangu* ina salama. Kama nikishika uchungu rohoni mwangu kwa sababu ya ubaya ambao alinitendea, nina-mkosea, na ninakosea Mungu na kuhatarisha usamehe wake kwa mimi. Si neno kama mtu mwenyewe akitubu, akiniomba kumsamehe au akijaribu kutengeneza neno alilofanya. Nilikwisha kumsamehe mara moja. Itampasa kujibu Mungu juu ya ubaya ambao alifanya. Ni kazi yangu kujaribu kusaidia roho yake, kama Matayo 18:15 linavyotufundisha, lakini la-zima nimsamehe kwanza.¹¹

5:1 Ndani ya 4:32 tulisoma juu ya usamehe wa Mungu. Mungu ametuse-mehe ndani ya Kristo. Sasa Paulo ali-tuonya kwamba inatupasa **kuiga Mungu**, na kusameheana. Aliongeza maneno haya, **kama watoto wanao-pendwa**. Hapa duniani sura ya watoto inaonyesha kama wao ni wazao wa jamaa gani, na ni kazi yao kuthibitisha jina la jamaa. Kwa uzima wa roho inatupasa kufunua Mungu Baba wetu kwa dunia, na kutembea kama inavyofaa kwa **watoto** wake wapendwa.

5:2 Inatupasa kufanana na Bwana wetu vilevile kwa njia ya kutembea **katika mapendo**. Baki la shairi hili linaleze ya kwamba **kutembea katika mapendo** ni kujitoa kusaidia watu

wengine. Hili ndilo neno Kristo, mfano wetu mkamilifu, alilofanya. Ni ajabu kabisa! Alitupenda. Alihakikisha ma-pendo yake kwa njia ya kujitoa mwenyewe kufa kwa ajili yetu kwa Kalvari.

Zawadi yake inaitwa **oleo na zabihu kwa Mungu**. **Oleo** ndilo kitu cho chote kinacholetwa kwa Mungu. **Zabihu** hapa ni pamoja na kufa vilevile. Kristo alikuwa kweli **zabihu** ya kuteketezwa. Alijitoa pia kufanya mapenzi ya Mungu, hata kufa msalabani.

Bwana Yesu alipendeza Baba yake kwa njia ya kujitoa kwa wengine. Nasi vilevile tunaweza kufurahisha Mungu kwa njia ya kujitoa kusaidia watu wengine.

5:3 Ndani ya mashairi 3 na 4 mtume alirudi tena kufundisha juu ya zambi za tamaa ya mwili, na anaita waamini ku-jitenga kabisa na maneno haya.

Anataja kwanza **uasherati**. **Uasherati** ni tendo la mume na mke *wasiooa* wanaolala pamoja. Lakini tunafikiri kwamba hapa uasherati ni zambi yo yote ya kulalana.

Uchafu unaweza kusema juu ya zambi za tamaa ya mwili, pamoja na vitabu vyta maandiko machafu, picha chafu, na maneno mengine ambayo yanaamsha tamaa ndani yetu na kutongoza kuishi maisha ya zambi.

Kutamani. Tunafikiri kutamani ni zaidi kutaka mali, lakini hapa neno hili linasema juu ya tamaa ya mwili vilevile inje ya ndoa. (Ona Kut. 20:17, “Usita-mani . . . mke wa jirani yako . . . ”)

Haifai Wakristo **hata kusema juu ya maneno** namna hii, wala *kuyatenda*. Ni hatari kuzungumuza juu yao kwa njia inayopunguza haya na ubaya wao, na kutoa uzuru. Hivi Paulo aliwakum-busha kwamba maneno haya **hayastahili kwa watakatifu**. Waamini wa-metengwa na ubovu wa dunia; inafaa sasa wajitenge vilevile na tamaa mbaya ndani ya masemo na matendo yao.

5:4 Haifai masemo yao kuwa:

Masemo machafu juu ya namna zote za uovu na ukosefu wa adabu;

Masemo yasiyo na maana yanayofaa kwa mpumbavu tu;

Maneno ya kuchekesha yasiyofaa. Kukaa kusema na kuchekesha juu ya maneno haya kunayaingiza ndani ya nia yako na kuamsha hamu kuyafanya.

Ni hatari kila mara kuzihaki zambi. Kwa pahali pa kutumika na ulimi wake juu ya maneno haya yasiyofaa, inapasa Mkristo kuweka roho na bidii kutolea Mungu **mashukuru** kwa baraka na vitu vyote anavyopokea kwa maisha yake. Neno hili linapendeza Bwana, ni mfano mzuri kwa watu wengine, na ni faida kwa roho ya Mkristo mwenyewe.

5:5 Mafikiri ya Mungu juu ya waasherati ni wazi: hawana **uriti katika ufalme wa Kristo na Mungu**. Mafikiri haya ni namna nyingine kabisa na mafikiri ya watu wa dunia. Watu wanasema waasherati ni wagonjwa wanaohitaji mganga. Wanasema uzini ni ugonjwa; Mungu anasema ni zambi. Watu wanaukubali; Mungu anauhukumu. Wanganga wa dunia wanafikiri wanaweza kusaidia wenyewe uzaifu namna hii; Mungu anasema lazima wazaliwe tena.

Ndani ya shairi 3 tuliona wenyewe zambi namna tatu: **mwasherati, mchafu**, na **mwenye kutamani**. Ndani ya shairi 5 tunaona kwamba **mwenye kutamani** ni **mwabudu sanamu** vilevile. Yeye ni **mwabudu sanamu** kwa sababu hafahamu kama Mungu ni namna gani, na anaweka roho juu ya kutaka kwake mwenyewe mbele ya kutaka kwa Mungu. Mwisho wa kutamani ni kuabudu kiumbe, si Mwumba (Rom. 1:25).

Maneno Paulo aliyo sema ni kweli kabisa: Watu namna hii hawana **uriti katika ufalme**. Watu wanaotenda zambi namna hii wamepotea. Wao wanafungwa na zambi zao ambazo zitawafikisha kwa gehena. Wao si ndani ya **ufalme** usioonekana kwa macho kwa

wakati wa sasa; hawatakuwa ndani ya **ufalme** wakati Kristo atakaporudi kutawala; na hawatakuwa kamwe ndani ya **ufalme** wa milele mbinguni. Mtume hasemi hapa juu ya watu walio ndani ya **ufalme** watakaopata hasara kwa kiti cha hukumu cha Kristo. Alisema hapa juu ya wokovu, si juu ya zawabu. Labda wanakiri kwamba wao ni Wakristo, lakini matendo yao yanahakikisha kwamba hawakuokolewa kamwe. *Wanaweza* kuokolewa kama wakitubu na kuamini Bwana Yesu. Lakini kama wa-kiockolewa kweli, hawatatenda maneno haya mabaya tena.

Ona ya kwamba maneno haya **ufalme wa Kristo na Mungu** yanaonyesha kwamba **Kristo** ni Mungu, na sawasawa na **Mungu** Baba kama Mtawala ndani ya **ufalme**.

5:6 Watu wengi duniani hawafikiri kwamba zambi kama uzini na uasherati ni mbaya sana. Wanasema ni desturi za inchi yao na kwamba zinasaidia watu. Wanakubali kupita na kupita kwa watu kulala pamoja mbele ya kuoa, au hata wakati mmoja wao akiwa na mume au mke mwengine, au kwa wanaume wawili kuoana, na kwa wanawake kufanya vivyo. (Neno la Mungu linahukumu matendo haya na kuyaita uasherati, uzini, na upotovu.) Ni shangao kwa sababu hata viongozi vya makanisa mengine wanakubali zambi hizi za mwili sasa, na wanakubali kwa watu wa makanisa yao kuyafanya, hata kama mbele watu hawa waliamini matendo namna hii hayafai.

Wakristo wakae na ange wasidanganywe na masemo namna hii. **Kwa sababu ya maneno haya kasirani ya Mungu inakuja juu ya wana wa kuasi**. Mawazo ya Bwana juu ya zambi za uzini na uasherati yanaonekana wazi ndani ya Hesabu 25:1-9 saa Waisraeli elfu makumi mbili na ine walipouawa kwa sababu walizini na wanawake wa Moabu. Na vivyo mawazo yake juu ya wanaume wawili, au wanawake wawili

wakioana (homosexualité) yalifunuliwa wazi wakati miji ya Sodomo na Gomora ilipoharibiwa na kiberiti na moto toka mbinguni (Mwa. 19:24, 28).

Lakini **gazabu** ya Mungu haionekani kwa njia ya maajabu namna hii tu. Wale wanaotenda zambi za mwili kama uasherati na uzini wanaazibowi kwa njia ya gonjwa za mwili na za roho. Wale walio na tabia ya kike watageuka hata kupita kuwa kama mwanamke (Rom. 1:27). Na mwishoni hukumu ya milele ya Mungu itakuwa juu ya waasherati na wazini (Ebr. 13:4). Mungu hatarehemu **wana wa kuasi** – ndio wazao wa mwasi Adamu, wanaochagua kumwasi (Ufu. 21:8).

5:7 Waamini wanaagizwa na nguvu wasishiriki ndani ya matendo mabaya namna hii. Kama wakishiriki ndani yao wanahayarisha jina la Kristo, wanangusha watu wengine, wanaharibu ushuhuda wao wenyewe, na kuazibowi sana.

5:8 Mtume aliendelea kuongeza ma-fundisho ya nguvu juu ya **giza** na **nuru** (mash. 8-14). Waefeso **walikuwa giza zamani, lakini sasa wamekuwa nuru katika Bwana.** Paulo hakusema walikuwa *katika* giza, lakini ya kwamba wao wenyewe **walikuwa giza.** Sasa, kwa sababu walikuwa wamefunganishwa na Bwana, wamegeuka **nuru**. Yeye ni nuru; wao ni ndani yake; hivi **sasa** wao ni **nuru katika Bwana.** Ingewapasa **kutembea kama watoto wa nuru.**

5:9 Mashairi yanayofuata yanaeleza kama wale wanaotembea ndani ya nuru wanazaa **matunda** ya namna gani.

Tunda la Roho ni namna **zote** za **wema, haki, na kweli.** **Wema** hapa unasema juu ya mema namna zote. **Haki** ni kutenda Mungu na watu na haki. **Kweli** ni kutenda kwa haki, bila udanganyifu. Mtu akiwa na maneno haya yote atakuwa mwenye maisha yanayo-jaa na nuru ya Kristo ndani ya dunia hii ya giza.

5:10 Wale wanaotembea katika nuru

wanazaa matunda yanayotajwa ndani ya shairi 9. Zaidi ya ile wanafahamu **nini inayopendeza Bwana.** Wanajaribu kila wazo, kila neno na tendo, na kuuliza kama **Bwana** akifikiri nini juu yake. Wanapima maneno yote ya maisha yao hivi – mazungumuzo yao, vyakula vyao, mavazi, vitabu, urafiki, vivi hivi.

5:11 Haifai waamini **kushirikiana na matendo ya giza.** Haifai washiriki ndani yao, au kwa njia ya kuonyesha ukubali na wale ambao wanayatenda. **Matendo** haya **ya giza** hayazai matunda kwa Mungu wala kwa watu. Ni neno hili ambalo lilisukuma Paulo kuuliza Wakristo wa Roma, “Basi faida gani muli-yopata kwa maneno yale munayoona haya juu yao sasa?” (Rom. 6:21). Na vilevile matendo haya ni **matendo ya giza**. Yanaonyesha kwamba tabia ya watu inapenda **giza**, na inachukia nuru wakati matendo yao ni maovu (Yn. 3:19). Inapasa mwamini kuepukana na matendo ya giza yasiyozaa matunda mema, na zaidi ya ile anaitwa **kuya-funua.** Anafanya hivi kwa njia mbili: kwanza kwa njia ya kutembea katika utakatifu, na ya pili, akiongozwa na Roho Mtakatifu, kuonya wenye matendo ya giza.

5:12 Sasa mtume anaeleza kwa sababu gani haifai Mkristo kuwa na ushirika na ubovu huu, lakini anapaswa kuuhamakia. Zambi mbaya sana watu wanazotenda katika giza ni **haya kabisa.** Ni aibu hata kusema juu yao, au kuzitenda. Hata kuzungumuza juu yao kungechafua nia ya wasikiaji. Hivi haifai Mkristo kuzungumuza juu yao.

5:13 Nuru inaonyesha kitu cho chote kilicho katika giza. Hivi mwenendo mtakatifu wa Mkristo unaonyesha uovu wa wale wasiozaliwa tena. Na makemeo yanayofaa yanafunua ubaya wa zambi vilevile. Blaikie alileta mfano huu:

Kwa mfano, wakati Bwana wetu

alipohamakia unafiki wa Wafarisayo – kwa macho ya wanafunzi matendo yao hayakuonekana mavu sana mbele, lakini wakati Kristo alipoyaangazia nuru safi ya kweli, uovu wao ulionekana wazi, na hata sasa ni machukizo.¹²

Sehemu ya mwisho ya shairi 13 inasema: **kila kitu kinachoonyeshwa ni nuru.**¹³ Maana yake ni ya kwamba wakati utumishi wa Wakristo ni nuru, watu wengine wanakokotwa karibu na nuru. Watu waovu wanageuzwa kuwa watoto wa nuru kwa njia ya makemeo ya utumishi wa **nuru**.

Si hivi kila mara. Si kila mtu anayekutana na nuru anageuka Mkristo. Lakini kwa maneno ya roho, nuru inazaa nuru. Tunaona mfano wa neno hili ndani ya 1 Petro 3:1. Shairi hili linafundisha wake walio waamini kusaidia waume wao wasioamini waweze kuamini Kristo kwa njia ya mfano wa mwenendo wao: “Ninyi wanawake, mutii waume wenu wenyewe; kusudi ikiwa wengine hawatii Neno, wavutwe kwa mwenendo wa wake wao pasipo neno.” Hivi nuru ya wake Wakristo inashinda giza la waume wao wapagano, na waume wao wanageuka nuru.

5:14 Ingepasa mwenendo wa mwa-minni kuwa mahubiri, na kufunua giza ambalo linatuzunguka, na kuita wasio-amin:

**“Amka, wewe unayelala,
Na ufuluke katika wafu,
Na Kristo atakuangaza.”**

Hii ni sauti ya nuru ikisema na wale wanaolala katika giza na mauti ya roho. Nuru inawaita kupata uzima na mwanagaza. Kama wakitii mwito huu, **Kristo** atawaangaza na **kuwapa nuru**.

5:15 Ndani ya mashairi saba yanayofuata Paulo alisawanisha mwenendo wa wapumbavu na mwenendo wa wenyе hekima. Kwanza alisihi wasomaji wake **wasitembee kama watu wasio na hekima**, lakini **kama watu wenyе**

hekima. Tuliona mbele kwamba **mwendendo** ni neno linaloonekana sana ndani ya barua hii. Linatajwa mara saba kusema juu ya matendo yote ya mtu. **Kutembea na hekima** ni kuishi kama inavyofaa kwa watoto wa Mungu. **Kutembea kama watu wasio na hekima** ni kushuka toka heshima ile na kute-mbea kama watu wa dunia.

5:16 Tukitembea na hekima tunaagi-zwa kukomboa **wakati**, maana yake kutumikia na kushuhudia Kristo kila mara tunapopata njia. Tunakuta kila siku mi-lango iliyo wazi kwa kazi ya Bwana. **Kukomboa wakati** ni kuishi maisha matakatifu, kutenda na rehema, na kusema maneno yatakayosaidia watu. Ni neno linalohitaji haraka kwa sababu **siku za sasa** ni za **uovu**. Zinatukumbu-sha ya kwamba Mungu hatashindana na watu kwa milele, muda wa neema uta-kwisha nyuma kidogo, na njia kuabudu, kutoa ushuhuda, na kutumikia Bwana duniani itakwisha kwa milele.

5:17 Hivi haifai tuwe **wajinga, la-kini wenyе kufahamu mapenzi ya Bwana**. Hili ni neno kubwa. Kwa sababu ya uovu ambao unatuzunguka, na ufupi wa wakati, ni nyepesi kwa sisi ku-jaribiwa kutumika na nguvu, tukifanya kazi ambayo sisi wenyewe tunachagua. Lakini kazi hii ingepoteza nguvu bure. Sharti tuombe Mungu kutuonyesha **mapenzi** yake kwa kila siku na kuyafanya. Hii ndiyo njia ya pekee kwa maisha yetu kuwa na faida. Ingewezekana kwa Wakristo kufanya kazi ya Bwana namna wao wenyewe wanafikiri ni vizuri, na kwa nguvu yao wenyewe, lakini utu-mishi huu haupatani hata kidogo na **mapenzi ya Bwana**. Njia ya hekima ni kwa sisi kutambua **mapenzi** ya Mungu kwa maisha yetu, kisha kuyatii kwa kila neno.

5:18 **Wala musilewe kwa mvinyo, ndani yake ni makelele**. Wakristo we-nji katika Amérique hawakunywi mvinyo kamwe. Lakini tukumbuke ya

kwamba Biblia iliandikwa kwa waamini ndani ya inchi zote, na ndani ya inchi nyingine mvinyo inakubaliwa. Maandiko hayahukumu kunywa mvinyo, lakini haifai kunywa kupita kipimo. Mara nyingine watu waliongozwa kunywa mvinyo kama dawa (Mez. 31:6; 1 Tim. 5:23). Bwana Yesu alifanya mvinyo kwa watu kunywa kwa karamu ya ndoa kwa Kana katika Galilaya (Yn. 2:1-11).

Lakini kunywa mvinyo ni vibaya na kunakatazwa kwa jambo fulani:

1. Kama watu wanapokunywa kupita kipimo (Mez. 23:29-35).
2. Wakati kunywa mvinyo kunapo-geuka desturi ya lazima kwa mku-nywaji (1 Kor. 6:12b).
3. Wakati kunapoumiza damiri zaifu ya mwamini mwingine (Rom. 14:13; 1 Kor. 8:9).
4. Wakati kunapopunguza uwezo wa ushuhuda wa Mkristo pahali ana-pokaa, na hivi si kwa utukufu wa Mungu (1 Kor. 10:31).
5. Wakati Mkristo mwenyewe akiwa na shaka rohoni juu ya kunywa mvinyo (Rom. 14:23).

Paulo alisema kwamba kwa pahali pa **kulewa kwa mvinyo** inapasa **kujazwa na Roho**. Labda onyo hili lina-tushangaza, lakini wakati tunaposawanisha na kulinganisha hali hizi mbili, tunaona kwa sababu gani Paulo alisema hivi juu yao.

Kwanza tuone kwa njia gani hali hizi zinafanana:

1. Ndani ya hali hizi mbili, mtu anatawaliwa na uwezo ulio inje yake: au uwezo wa malofu, au uwezo wa **Roho**.
2. Ndani ya hali mbili mtu mwenyewe ana bidii. Siku ya Pentekote, wali-jazwa na bidii ya **Roho**, lakini watu walifikiri walilewa na mvinyo mpya (Mdo. 2:13).
3. Mwenendo wa mtu anayelewa na mvinyo ni namna nyingine na mwenendo safi wa mtu anayejazwa na

Roho.

Lakini kwa njia nyingine hali ya watu wale ni namna mbalimbali kabisa:

1. Kulewa kunazaa uasherati na m-kelele. Roho akijaza mtu, hazai ma-neno haya kamwe ndani yake.
2. Mtu anayelewa hawesi kutawala mwili wake. Lakini tunda la **Roho** ni ujizua (Gal. 5:23). Mwamini ana-yejazwa na Roho anaweza kutawala matendo yake saa zote. Roho ya nabii anatii nabii kila mara (1 Kor. 14:32).

Ni kama ndani ya Biblia tunasoma mara nyingine kwamba **kujazwa na Roho** ni zawadi toka Mungu. Kwa mfano, Yoane Mbatizaji **alijazwa na Roho** Mtakatifu toka tumbo la mama yake (Lk. 1:15). Hakufanya kitu kumstahilisha kupokea Roho. Hakuomba wala kutumika kazi kwa kumpokea. Bwana anamtoa kama ikimpendeza. Hapa ndani ya Waefeso 5:18 mwamini *anaagizwa kujazwa na Roho*. Kuna maneno mengine ambayo inampasa ku-fanya kwa kujazwa na Roho. Anajazwa na Roho kwa sababu ya kutii.

Kwa sababu hii inatupasa kufahamu kwamba kujaza kwa Roho ni mbali na utumishi wake mwingine. *Si* sawasawa na maneno haya:

1. *Kubatizwa na Roho* Mtakatifu. Kwa njia ya tendo hili la Roho, mwamini anaingizwa ndani ya mwili wa Kristo (1 Kor. 12:13).
2. *Kukaliwa naye* kwa utumishi kama Mfariji, Kwa njia hii Roho Mtakatifu anakaa ndani ya mwili wa Mkristo na kumpa uwezo kwa mwenendo mtakatifu, kuabudu, na utumishi (Yn. 14:16).
3. *Kupakaliwa mafuta*. **Roho** mwenyewe ni mafuta yale yanayofundisha mtoto wa Mungu maneno ya Bwana (1 Yn. 2:27).
4. *Arabuni na mhuri*. Tumeona mbele ya kwamba Roho Mtakatifu, kama

arabuni, anahakikisha ya kwamba Mkristo atapokea uriti, na kama mhuri anahakikisha Mkristo kwa uriti (Efe. 1:13, 14).

Hizi ndizo kazi nyingine Roho anazofanya ndani ya mtu mara moja wakati anapookolewa. Kila mtu aliye ndani ya Kristo anabatizwa na Roho, anakaliwa naye, anapakaliwa mafuta, ana arabuni, na mhuri.

Lakini kujazwa na Roho ni namna nyingine. Si neno linalotokea mara moja tu ndani ya mwanafunzi, lakini linalokaa kutokea kila siku. Kujazwa na Roho leo hakutoshi kwa kesho. Hali nzuri zaidi kwa mwamini hapa duniani ni kujazwa na Roho. Inaonesha kwamba Roho Mtakatifu anaweza kufanya kazi yake bila kizuizo ndani ya maisha ya mwamini. Hivi mwamini yule anatimiza kazi ambayo Mungu anakusudi kwa ye ye kufanya kwa wakati ule.

Basi mwamini anaweza **kujazwa na-mna gani na Roho?** Mtume Paulo hakutuambia neno hili hapa ndani ya Waefeso; alituagiza tu **kujazwa**. Lakini kwa njia ya mashairi mengine ya Mandiko tunajua ya kwamba **kujazwa na Roho** inatupasa:

1. Kukiri na kuondosha zambi zote ndani ya maisha yetu (1 Yn. 1:5-9). Si nguvu kwa sisi kufahamu kwamba Roho aliye Mtakatifu hivi hawesi kutumika vizuri ndani ya mtu anayebaki na zambi ndani ya maisha yake.
2. Kujitoa kabisa kwa Roho aweze kututawala (Rom. 12:1, 2). Lazima tumtolee kabisa kutaka kwetu, akili yetu, mwili wetu, saa yetu, zawadi zetu, na mali yetu. Sharti tumpe njia kutawala kabisa kila sehemu ya maisha yetu.
3. Kuacha neno la Kristo kukaa kwa wingi ndani yetu (Kol. 3:16). Inatupasa kusoma na kujifunza Neno la Mungu na kulitii. Wakati Neno la Kristo linapokaa ndani yetu kwa

wingi (Kol. 3:16), mwisho wake ni sawasawa na kujazwa kwa **Roho** (Efe. 5:19).

4. Mwishoni, lazima tujinyenyeyekeze kabisa, na kufika mbele ya Bwana kama chupa wazi na safi, tayari **kujazwa na Roho** (Gal. 2:20). Kwa **kujazwa na Roho**, lazima roho yetu ya “*mimi kwanza*” iondoshwe kabisa.

Mwandishi tusiyejua jina lake ali-andika:

Uliacha mzigo mzima wa zambi yako, na umetegemea kazi ambayo Kristo alitimiza. Vivyo hivyo sasa acha mzigo mzima wa maisha yako na utumishi wako, na tegemea kazi Roho Mtakatifu anayofanya ndani yako. Ujitee kila asubui, uweze kuongozwa na Roho Mtakatifu, na kwenda yako ukisifu na kustarehe, ukimwacha ye ye kuongoza maneno yako siku ile. Pata desturi kugeuka kwake tena na tena siku ile, kumtegemea na furaha na kumtii, ukiamini kwamba atakuongoza, kukuhamakia na kukufundisha, kutumika nawe, na ndani yako, kitu cho chote anachotaka. Amini kwamba atafanya hivi, hata kama huoni au kusikia kitu rohoni mwako. Tuamini tu na kutii Roho Mtakatifu aliye mtawala wa maisha yetu. Tuache kujaribu kuongoza maneno yetu sisi wenyewe; halafu tunda la Roho litaonekana ndani yetu na pmna Yeye anavyotaka kwa utukufu wa Mungu.

Mtu anafahamu wakati **anapojazwa na Roho?** Kwa kipimo tunachotembea karibu na Bwana, tunafahamu kupita ukubwa wa zambi zetu na ya kwamba hatustahili hata kidogo (Isa. 6:1-5). Wakati tunaposimama mbele yake, hatuna kitu ndani yetu ambacho tunaweza kujisifu juu yake (Lk. 5:8). Hatufikiri tunapita watu wengine kwa maneno ya

roho. **Mwamini anayejazwa na Roho** anafikiri juu ya Kristo, si juu yake mwenyewe.

Lakini hata hivi anafahamu mara nyingine kwamba Mungu anafanya kazi ndani yake na kwa njia yake. Anaona maneno mengine yakinkeza yasiyo kwa desturi ya dunia hii, kama kwa ajabu. Watu wanageuka kwa Mungu. Maneno yanatokeza yakifuata orodha ya saa ya Mungu. Hata upepo na jua na mvua zinamsaidia. Mwamini anaona maneno haya yote, na anafahamu ya kuwa Mungu anatumika na anafanya kazi kwa njia yake, lakini anafahamu kwamba yeze mwenyewe hastahili kupokea sifa kwa matokeo haya, ni yote kazi ya Bwana.

5:19 Sasa mtume alitaja matunda namna ine ya kujazwa na Roho. Kwanza, Wakristo wanaojazwa na Roho **wanasemezana kwa zaburi na tenzi na nyimbo za roho**. Kujazwa na Roho kunafunga vinywa vyetu kusemezana na watu wengine juu ya maneno ya Bwana. Tunafahamu kwamba **zaburi** ndizo maandiko ya Daudi, Asafu, na wengine walioongozwa na Mungu. **Tenzi** ni nyimbo za kuabudu na sifa kwa Mungu lakini zisizoongozwa naye. **Nyimbo** za roho ni nyimbo zisizotaja Mungu waziwazi kila mara.

Neno la pili linaloonyesha kwamba mwamini anajazwa kwa Roho ni furaha na sifa rohoni mwake kwa Mungu: **mukiimba na kushangilia Bwana mio-yoni mwenu**. Mwamini anayejazwa na Roho Mtakatifu ni kama kisima kinachofurika na furaha (Mdo. 13:52). Zakaria ni mfano wa neno hili: wakati alipojazwa na Roho Mtakatifu aliimba na roho yake yote kwa Bwana (Lk. 1:67-79).

5:20 Tunda la tatu ni mashukuru: **mukishukuru Mungu ndiye Baba siku zote kwa mambo yote, katika jina la Bwana wetu Yesu Kristo**. Watu wanotawaliwa na Roho ni wenye shukrani kwa **Mungu** inayoonekana wazi. Si

roho ya asante wakati mmoja mmoja tu, lakini saa zote. Si kwa maneno ya kufurahisha tu, lakini kwa maneno yote. Mtu ye yote anaweza kuwa na roho ya asante wakati wa salama na baraka; lakini tunahitaji uwezo wa Roho kutujaza na asante wakati mambo magumu yanapotupata.

Njia nzuri na fupi zaidi kwa kukaa na furaha ni hii:

Iwe desturi yako kushukuru na kusifu Mungu kwa kila kitu ambacho kinakupata. Bila shaka kama neno ambalo linakupata likionekana kama msiba mkubwa, kama ukishukuru na kusifu Mungu kwa neno hili, unaligeuza kuwa baraka. Hata ungaliweza kufanya maajabu, huwezi kujisaidia kupita kwa njia yo yote kama kwa njia ya kuwa na roho ya asante. Kuwa na roho ya namna hii, hata bila kuhitaji kusema neno, kunageuza kila kitu kuwa baraka. (*Sehemu chaguliwa*)

5:21 Neno la ine linalohakikisha kwamba tunajazwa na Roho ni **kunyenyekeana katika woga wa Mungu**. Haya ndiyo maonyo ya Erdman:

Mara nyingi zaidi Wakristo hawaweki roho juu ya agizo hili ... Watu wengi wanafikiri kwamba kulalamika haleluya na kuimba nyimbo za sifa hata ndani ya “Iugha watu wasizouja” kunahakikisha kwamba “wanajazwa na Roho.” Labda mambo haya yote ni matendo ya uwongo bila maana ya kweli. Alama zinazoonyesha bila shaka uwezo wa Roho ukitumika ndani ya Wakristo ni unyenyevu, kuwa na adabu, kukataa kubishana, uvumilivu, na upole ... Inapasa Wakristo kunyenyekeana “katika woga wa Kristo,” maana yake wakifahamu kwamba yeze ni Bwana ya yote.¹⁴

Haya ndiyo matunda mane ya kujazwa na Roho – masemo, nyimbo,

mashukuru, na kunyenyekanea. Lakini kuna matunda mane mengine:

1. Uhodari kukemea zambi (Mdo. 13:9–12), na kushuhudia Bwana (Mdo. 4:8–12, 31; 13:52–14:3).
2. Uwezo kutumikia Bwana (Mdo. 1:8; 6:3, 8; 11:24).
3. Ukarimu, si choyo (Mdo. 4:31, 32).
4. Kutukuza Kristo (Mdo. 9:17, 20) na Mungu (Mdo. 2:4, 11; 10:44, 46).

Ni vizuri kwa sisi kuwa na hamu kujazwa na Roho, lakini kwa utukufu wa Mungu tu, si kwa utukufu wetu wenyewe.

D. Maonyo kwa watu nyumbani mwa Wakristo kuwa na utawa (5:22 – 6:9)

5:22 Sehemu hii mpya ya Waefeso inafungana na shairi 21. Pale Paulo alisema kwamba kunyenyeka ni moja la matunda ya kujazwa na Roho. Ndani 5:22 – 6:9, alitaja kwamba ni mapenzi ya Mungu kwa watu namna tatu ndani ya nyumba ya Wakristo kuwa na roho ya kutii:

Inapasa **wake kutii waume** wao **wenyewe**.

Inapasa **watoto** kutii **wazazi** wao.

Inapasa **watumwa** kutii **bwana** zao.

Waamini ni moja ndani ya Kristo Yesu, lakini hata hivi inatupasa kuheshimu utaratibu wa amri na utawala, ambao Mungu alisimamisha. Kila kundi la watu wenyewe shauri moja linategemea nguzo mbili – amri na utii. Lazima watu wengine ni wenyewe amri, na watu wengine wanatii amri zao. Tunasoma hata juu ya Mungu: “Lakini ninataka mujue ya kwamba ... kichwa cha Kristo ni Mungu” (1 Kor. 11:3). Mungu aliamuru watu wengine kuwa serikali duniani. Hata serikali ikiwa ovu kabisa, kwa mafikiri ya Mungu kuwa na serikali ovu ni vizuri kupita kuwa bila serikali. Inatupasa kutii watawala wetu kwa maneno yote yasiyokana Bwana. Bila serikali kuna machafuko inchini.

Ni vivyo hivyo katika jamaa nyumbani. Ni lazima kuwa na kichwa, ndiye kiongozi, na watu wengine nyumbani kuwa wenyewe kutii kichwa hiki. Mungu aliamuru kwa mwanamume kupewa kazi ya kiongozi. Alionyesha neno hili kwa njia ya kuumba mwanamume kwanza, kisha aliumba mwanamke kusaidia mwanamume. Hivi kwa njia ya kuumba, aliweka mwanamume kwa pahali pa amri, na mwanamke kwa pahali pa kutii.

Maana ya utii haiko ya kwamba mwenye kutii ni chini kupita kamwe. Bwana Yesu anatii Mungu Baba, lakini yeze si chini kupita Baba kwa njia yo yote. Wala mwanamke si chini kupita mwanamume. Labda anapita mwana-mume kwa njia nyingi – kwa njia ya bidii, huruma, utendaji, na uvumilivu hodari. Lakini **wake** wanaagizwa **kutii waume wao wenyewe, kama kutii Bwana**. Wakati mke anapotii amri ya mume wake, anatii amri ya Bwana. Aki-fahamu neno hili, hautakuwa uchungu au uasi kwake kutii mume wake.

Ndani ya miaka inayopita tunaona tena na tena machafuko yaliyo tunda la wake wakiasi agizo hili la Mungu. Kwa njia ya kujitwalia ruhusa ya kuongoza kwa pahali pa mume wake, Hawa aliingiza zambi katika taifa la waadamu na kuleta msiba na maangamizi makubwa. Kwa siku hizi, dini za uwongo zilianzwa na wanawake ambao walijitwalia amri ambayo Mungu hakukusudi kuwapa. Wanawake wanaokataa mahali wali-yopewa na Mungu wanaweza kuharibu kanisa pahali wanapokaa, na kuvunja ndoa na nyumba yao.

Lakini ni neno la kupendeza kabisa kuona mwanamke anayetimiza kazi ali-yopewa na Mungu. Tunasoma juu ya mwanamke namna hii ndani ya Mezali 31 – ukumbusho wa daima wa mke na mama anayependeza Bwana.

5:23 Inpasa mke kutii kwa sababu **mume** wake ni **kichwa** chake. Yeye ni

kwake namna Kristo ni kwa kanisa. **Kristo ni kichwa cha kanisa; naye ni Mwokozi wa mwili.** (Neno hili Mwo-kozi linaweza kutafsiriwa Mlinzi hapa.) Hivi **mume ni kichwa cha mke**, naye ni mlinzi wake vilevile. Kama **kichwa** anampenda na kumwongoza; kama mlinzi anampatia mahitaji yake na anamchunga.

Watu wengi kwa wakati wa sasa wanachukia mafundisho haya. Wanashitaki Paulo wakisema alikuwa mkaidi asiye-oa, na kwamba alichukia wanawake. Au wanasema mafundisho yake yanapatana na desturi za wakati alipoishi, lakini hayana maana kwa wakati wa sasa. Masemo namna hii yanakana Maandiko haya yaliyoongozwa na Mungu. Maneno haya si maneno ya Paulo tu; ni maneno ya Mungu. Kuyakataa ni kukataa Mungu, na kuleta matata na msiba.

5:24 Ni heshima kubwa sana kwa daraka la mwanamke kusawanishwa na daraka la **kanisa** kama **bibi-arusi** ya **Kristo**. Inapasa mke kuiga namna kanisa linavyotii Kristo. Sharti **atti katika kila kitu** – maana **kila kitu** kinachopatana na mapenzi ya Mungu. Haifai mke kutii mume wake kama mume akitaka afanye kitu kitakachokana kwamba Kristo ni Bwana wake. Lakini ndani ya maneno yote mengine ya maisha ya kila siku inampasa kutii mume wake, hata kama mume huyu ni msyeamini.

5:25 Si **wake** tu wanaopewa maagizo namna hii. Kuna mafundisho yanayofanana nayo kwa **waume** vilevile. **Waume** hawaagizwi kutiisha wake wao na nguvu; wanaagizwa **kupenda wake wao; kama vile Kristo alivyopenda kanisa**. Hakuna mke atakayekataa kutii mume ambaye anampenda kwa kipimo **Kristo** anachopenda **kanisa**. Mtu mmoja aliuliza mtumishi wa Mungu kama ikiwezekana kwaye kupenda mke wake kupita kipimo. Mkristo alimwuliza kama alimpenda kupita mapendo ya

Kristo kwa kanisa. Alijibu hapana. Mtumishi wa Mungu alisema naye, “Kama ukipenda mke wako kupita mapendo ya Kristo kwa kanisa, unampenda kupita kipimo.”

Tunasoma maneno makubwa matatu juu ya mapendo ya Kristo kwa **kanisa** tangu zamani kufika wakati wa kuja. Zamani alionyesha mapendo yake kwa kanisa kwa njia ya **kujitoa mwenyewe kwa ajili yake** kwa njia ya kufa kama zabihu juu ya msalaba. Alilipa pale bei kubwa zaidi kwa kujinunulia bibi arusi. Kama Hawa aliviyotolewa toka mbavu ya Adamu, ni kama **kanisa** lilumbwa toka kuumiwa kwa mbavu ya Mwo-kozi.

5:26 Kwa wakati wa sasa mapendo yake kwa kanisa yanaonekana kwa njia ya utakaso: **apate kulitakasa, akiwa amelisafisha kwa maji katika neno**. Maana ya **kutakasa** ni kuweka mbali. Kanisa limekwisha kutakaswa; lakini linatakaswa kila siku vilevile kulitayarisha kwa roho na mwenendo vilevile. Linatakaswa kwa njia ya **kusafishwa kwa maji katika neno**. Ni kusema, maisha ya waamini yanafishwa wakati wanaposikia maneno ya Kristo na kuyatii. Hivi Yesu alisema na wanafunzi, “Ninyi mumekwisha kuwa safi kwa sababu ya neno ambalo niliwaambia ninyi” (Yn. 15:3). Ndani ya ombi lake kama kuhani mkubwa alisema juu ya kutakaswa kwa neno lake vilevile: “Uwatakase kwa kweli; neno lako ni kweli” (Yn. 17:17). Kama damu ya Kristo inavyosafisha mara moja toka hatia na azabu ya zambi, vivyo hivyo neno la Mungu linakaa kusafisha toka uchafu wa zambi. Mashairi haya yanafundisha kwamba kwa wakati wa sasa kanisa halisafishwi kwa maji, lakini kwa neno la Mungu.

5:27 Zamani mapendo ya Kristo ya lionyesha ndani ya **ukombozi** wetu. Kwa wakati wa sasa yanaonyeshwa

ndani ya *utakaso* wetu. Kwa wakati wa kuja yataonekana ndani ya *kutukuzwa* kwetu. Yeye **atajiletea mwenyewe kanya la utukufu, pasipo alama wala kikunjo wala kitu cho chote kama hivi; lakini liwe takatifu na pasipo kilema.** Kwa wakati ule litafikia ukamili fu wa roho.

5:28 Nyuma ya masemo haya ya kushangaza juu ya mapendo ya Kristo kwa kanisa, Paulo alikumbusha waume tena kwamba huu ndio mfano ambao inawapasa kuiga: **Hivi vilevile inafaa waume kupenda wake wao wenyewe kama miili yao wenyewe.** Wakiiga mapendo ya Kristo, ingewapasa **kupenda wake wao wenyewe kama miili yao wenyewe.**

Kwa Kiyunani, neno hili “mwenyewe” linaonekana mara sita ndani ya mashairi 22–33. Linatukumbusha kwamba ni kutaka kwa Mungu kwa mume kuwa na mke mmoja tu. Hata kama aliacha wanaume kuwa na mke kupita mmoja kwa wakati wa Agano la Kale, hakupendezwa na neno hili kamwe.

Ona vilevile namna Paulo alivyo-andika juu ya ukaribu na ufungu wa mume na mke wake. Anasema kwamba kwa njia ya kupenda mke wake, mwana-mume anapenda mwili wake mwenyewe (sh. 28a); anajipenda **mwenyewe** (sh. 28b, 33), na “mwili wake mwenyewe” (sh. 29). Ndoa inafunganisha watu wawili kuwa moja, nao wawili wanageuka mwili mmoja, hivi ni kweli ya kwamba mwanaamume **anayependa mke wake**, anajipenda **mwenyewe**.

5:29 Mtu anazaliwa na akili kuchunga mwili wake. Anaukulisha, kuvatalisha na kuuogesha; anaulinda usipatwe na maumivu. Anaishi kwa sababu ya kuchunga mwili wake vizuri. Huu ni mfano zaifu wa namna **Bwana** anavyo-linda **kanisa**.

5:30 Kwa kuwa sisi ni viungo vya mwili wake. Neema ya Mungu ina-

tushangaza! Haituokoi tu toka zambi na gehena, lakini inatuunganisha na Kristo kama **viungo** ndani ya **mwili wake usioelezeka.** Neno hili linaonyesha mapendo yake makubwa kwa sisi. Anatulinda kama mwili wake mwenyewe. Anatalisha, kututakasa, na kutufundisha. Anatuchunga na salama bila woga. Hatakuwa mbinguni bila **viungo** vyake. Yeye na sisi tunashiriki uzima pamoja. Neno lo lote linalogusa viungo vyake linagusa Kichwa vilevile.

5:31 Halafu mtume alitaja Mwanzo 2:24, pahali tunapoona Mungu akisimamisha ndoa. Kwanza, mwanaamume anakomboa uaminifu wake kwa wazazi wake na uaminifu kwa mke wake. Kwa kusimamisha ndoa yake, anaacha wazazzi wake na **anafungana na mke wake.** Neno la pili ndilo ya kwamba mume na mke **wanakuwa mwili mmoja:** watu wawili wanafungamana. Kama watu wangalikumbuka maneno haya mawili, kama hakuna magomvi ya mume na mke wake nyumbani, wala matatizo kati ya jamaa na watoto wao linaoana.

5:32 Siri hii ni kubwa; lakini ni-nasema habari za Kristo na kanisa. Halafu Paulo alitimiza mafundisho yake juu ya ndoa kwa njia ya kutangaza kweli hii ya ajabu watu wasiyojua mbele, kwamba mke ni kwa mume wake namna kanisa ni kwa Kristo.

Wakati Paulo aliposema **siri hii ni kubwa**, ni kusema hii ndiyo kweli kubwa sana. **Siri** yenyewe ndiyo kusudi la ajabu Mungu aliloficha kwa nyakati za kale, lakini linalofunuliwa sasa. Kusudi la siri hii lilikuwa kuita toka mataifa watu watakaokuwa Mwili na Bibi Arusi ya Mwana wake mtukufu. Hivi ndoa ni mfano mkamilifu wa **Kristo na kanisa.**

5:33 Shairi hili la mwisho linajumlisha maneno mtume aliyokwisha kusema na waume na wake. Agizo la mwisho kwa waume ndilo: kila mwana-mume **apende mke wake** kama **nafsi**

yake mwenyewe, akikumbuka kwa-mba yeche ni mmoja naye. Onyo kwa wake ni mke **akae kuheshimu** na kutii **mume** wake siku zote. Fikiri kwanza kama nini itatokea kama zaidi ya Wakristo wakinii maagizo haya ya Mungu wakati wa sasa. Tusingalikuwa na magomvi na kuachana. Nyumba zetu zingekuwa kama malimbuko ya mbingu, si pahali pa vita.

6:1 Ndani ya sura 5 tulijifunza kwa-mba tunda moja la kujazwa na Roho ni kunyenyekeana. Kwa mfano, tuliona kwamba mke anayejazwa na Roho, ananyenyekeea mume wake. Sasa tunaji-funza kwamba watoto wanaojazwa na Roho ni wenye roho tayari kunyenyekeea amri ya wazazi wao. Inapasa watoto wote **kutii wazazi** wao **katika Bwana**. Si neno kama watoto wenyewe, au wazazi wao ni Wakristo. Agizo hili kwa watoto na wazazi wao ni kwa watu wote duniani, si kwa waamini tu. Maana ya agizo **kutii ... katika Bwana** ni ya kuwa inapasa watoto **kutii** wakijua kwamba kwa njia ya kufanya hivi **wanatti Bwana**. Inawapasa **kutii** vilevile maagizo yote yanayopatana na mapenzi ya Mungu. Kama wazazi wao wakiwaa-giza kufanya zambi, haifai kutii agizo hili. Wakatae na adabu, na wakae tayari kuvumilia azabu na unyenyekevu bila kujilipiza kisasi. Lakini watii maagizo yao mengine yote.

Inawapasa kutii kwa sababu ine: Kwanza, kwa sababu **ni haki**. Ni msingi mwema kwa hali ya jamaa kama wana wasiokomea bado, wanaopenda kufanya maneno gafula, bila ufahamu, waki-nyenyekeea amri ya wazazi, ambao wanawapita na miaka na hekima.

6:2 Sababu ya pili ni ya kama ni agizo la Neno la Mungu. Hapa Paulo alitaja Kutoka 20:12: **Heshimu baba yako na mama yako** (ona vilevile Tor. 5:16). Amri hii **kuheshimu** wazazi ni agizo la kwanza la amri kumi lililo na ahadi vilevile kwa wenye kulitii. Ni agizo kwa

watoto kuheshimu, kupenda, na kutii wazazi wao.

6:3 Sababu ya tatu ni ya kwamba ni faida zaidi kwa watoto: **upate heri**. Waza kwanza juu ya hali ya mtoto asiyefundishwa au kuazibowi na wazazi wake! Mtoto huyu hatakaa na furaha, na hatapatana na watu wengine.

Sababu ya ine ni ya kwamba mara nyingi wenye kutii wanakuwa na maisha marefa: **uishi siku nyingi katika dunia**. Ndani ya Agano la Kale mtoto aliyetii wazazi wake aliihi miaka minge. Si hivi kila mara kwa muda huu wa Habari Njema. Mara nyingine mwana wa kutii anakufa angali yeche ni kijana. Lakini zaidi wenye kutii na kujitawala wenyewe wanakaa na afya njema na wanaishi kwa miaka minge. Mara nyingine wale wasiofanya hivi lakini wanaishi maisha ya uasi na upotovu wanakufa wangali vijana.

6:4 Maonyo **kwa baba** yanafuata maagizo kwa watoto. Haifai baba **wachokoze watoto** wao, na kuwaagiza maneno magumu kupita kipimo, na kuwattendea na ukali na kuwakemea saa zote. Inapasa kulea watoto **katika azabu na maonyo ya Bwana**. Ona ya kwamba azabu na maonyo haya ni “katika ... **Bwana**,” maana yake kupatana na mapenzi yake, kama yanavyofunuliwa ndani ya Biblia.

6:5 Mwishoni watumishi wa **bwana** wa nyumba wanaagizwa kumtii. Paulo aliwaita **watumwa**, lakini mafundisho haya ni kwa watumishi wote.

Neno la kwanza wanaloagizwa ni kutii **wale walio bwana wao kwa maneno ya mwili**. Semo hili **bwana wao kwa maneno ya mwili** linatukumbusha kwamba bwana wa kazi ana mamlaka juu ya kazi ya mwili au akili ya mtumishi wake, lakini hana amri juu ya roho na damiri yake.

Neno la pili inalofaa kwa watumishi ni kuwa na adabu. **Woga na kutete-meka** si kuogopa sana namna watumwa

wa zamani walivyoogopa na kutete-meka. Ni kuwa na adabu, na kuogopa kuchukiza Bwana na bwana wa kazi.

Neno la tatu ndilo kutumikia bwana wa kazi **kwa roho moja**. Kwa kupokea mshahara kwa saa moja, ni lazima vilevile kufanya kazi kwa saa moja nzima.

Na vile inatupasa kufanya kazi yetu **kama kutii Kristo**. Maneno haya ya-naonyesha kwamba haifai kuwa na to-fauti kati ya kazi ya dunia na kazi ya Mungu. Ingetupasa kufanya kwa Bwana maneno yote tunayofanya. Neno hili litapendeza na kuheshimu Bwana, na litakokota watu wengine karibu naye. Kazi ya chini zaidi inaweza kufanywa kwa utukufu wa Mungu, hata kusukula sahani au kuvua mavazi!

6:6 Lazima tutumike na bidii saa zote, si wakati bwana wa kazi ni karibu tu. Sharti tukumbuke kwamba Bwana wetu mbinguni anaangalia saa zote. Ni majoribu kwa sisi kulegea wakati bwana wa kazi si karibu, lakini kufanya hivi ni udanganyifu. Mnunuzi mmoja alisukuma mtumishi wa duka kumpa kitu kupita mali aliyolipa, akisema mwenye duka hataona. Mtumishi wa duka ali-jibu, “Bwana wangu anatazama wakati wote!” Kama watumishi wa Kristo, inatupasa **kufanya mapenzi ya Mungu kwa moyo**, maana na hamu ya kweli kumpendeza.

6:7 Inatupasa kutumika vilevile **kwa nia njema**. Si na onyesho la ukubali usoni na uchungu rohoni, lakini na furaha kwa nia. Si neno kama bwana wa kazi ni mkali, mtukanaji, na mwenye kuagiza maneno yanayokosa akili; hata hivi tunaweza kufanya kazi yetu **kama kutumikia Bwana, wala si watu**. Huu ndio ushuhuda wa uwezo zaidi ndani ya dunia yetu ya sasa.

6:8 Sababu moja ambayo inatuletea sisi hamu kufanya kila kazi kama kwa Kristo ni kujua kwamba atatua zawabu kwa kila kazi njema. **Si neno** kama mtu

wa kazi ni **mtumwa** au kama ni **huru**. Bwana anaona kila kazi inayofanywa kwa yeye, kazi za kupendeza au zenye chuki, na atampa kila mtumishi zawabu.

Mbele ya kuacha mafundisho haya juu ya watumwa, inapasa kuongeza maneno mengine:

1. Agano Jipyä halikatazi utumwa kabisa. Ndiyo, linasawanisha mwamini wa kweli na mtumwa wa Kristo (sh. 6). Lakini matumizi mabaya ya utumwa yamekwisha kila pahali Habari Njema ilipohubiriwa, zaidi kwa njia ya kugeuka kwa roho za bwana za kazi.

2. Agano Jipyä lina mafundisho kwa watumwa kupita mafundisho kwa wafalme. Labda ni kwa sababu si watu wakubwa wengi wananaoitwa (1 Kor. 1:26). Ni kama zaidi ya Wakristo si wenyewe mali nydingi au watu wa kujulikana. Baraka nzuri zaidi ya ukristo ni kwa watumishi wenyewe kazi ya chini zaidi.

3. Mafundisho haya kwa watumwa yalizaa matunda. Kwa wakati wa mwanzo wa ukristo, pahali watumwa wali-pouzwa kwa soko, mara nydingi bei ya watumwa Wakristo ilipita bei ya watumwa wapagano. Vivyo hivyo kwa wakati wa sasa ingepasa watu wa kazi walio waamini kuwa na faida kwa bwana zao kupita watumishi wasio-aminis wasioguswa bado na neema ya Mungu.

6:9 Maagizo kwa **bwana wa kazi ni vivyo hivyo** na yale kwa watumishi. Sharti wawe bila kupendelea, wema na wenyewe haki. Waepuke masemo ya **kuogopesha** na matukano. Kama wakijitawala kwa maneno haya, hawatahitaji kamwe kuazibu mtumishi kwa njia ya kumwumiza mwilini. Inapasa bwana wa kazi kukumbuka kwamba wao wana **Bwana vilevile, Bwana aliye mbinguni aliye Bwana wa mtumwa vilevile**. Hata kama bwana na mtumishi hapa duniani wanakaa mbalimbali, mbele ya Bwana wao ni sawasawa. Siku nyiningine bwana

na mtumishi vilevile watatoa habari zao wenyewe mbele ya Mungu.

E. Maonyo juu ya vita inayopasa Wakristo kupiga (6:10-20)

6:10 Paulo alifikia mwisho wa barua yake sasa. Akisema na jamaa nzima ya Mungu, anawasihi sana kama askari za Kristo. Kila mtoto wa kweli wa Mungu anafahamu mbio kwamba maisha ya Ukristo ni vita. Majeshi ya Shetani yana bidii kushindana na kuzuiza kazi ya Kristo, na kuachisha kila askari kupiga vita. Kama mwamini akiwa na faida kwa kazi ya Bwana, atakutana na vita kali ya adui. Shetani hapotezi saa na nguvu yake kushindana na watu wasio Wakristo wa kweli. Sisi wenyewe hatuna nguvu ya kutosha kupigana na Shetani, hivi agizo la kwanza kwa sisi ni kuwa hodari katika **Bwana, na katika uwezo wake** usio na kipimo. Askari wenye faida zaidi kwa Mungu ndio wale wanaofahamu uzaifu wao, na ya kwamba kazi yao yenye we haina faida, na wanaotegemea Mungu peke yake. “Mungu alichagua vitu zaifu vya dunia kupatiza vitu nguvu haya” (1 Kor. 1:27b). Uzaifu wetu unatufungulia njia kuwa hodari **katika uwezo wake**.

6:11 Agizo la pili ni juu ya hitaji letu kwa **silaha** ya Mungu. Sharti mwamini **avae silaha zote za Mungu ili aweze kusimama juu ya hila ya Shetani**. Lazima avae silaha zote. Kuvaal kipande kimoja au viwili tu ni bure. Silaha zote tu ambazo Mungu anatuletea zinatosha kutuchunga tusiumie. **Shetani** anajua uzaifu wetu na anatumika kwa njia mbalimbali kutuangusha – maneno ya kushusha moyo, mazuizo, zambi na mafundisho ya uwongo. Kama ikimshinda kutushinda kwa njia moja, atajaribu kufanya hivi kwa njia nydingine.

6:12 Ndani ya vita hii hatushindani na wenye elimu wasio na mungu, makuhani wenye hila, wenye dini wanaokataa Kristo, au watawala wa-

sioamini Mungu. Ni vita na pepo wabaya, majeshi ya malaika walioanguka, roho waovu walio na uwezo mkubwa sana. Hatuwezi kuziona na macho, lakini zinatzunguka wakati wote. Ni kweli ya kwamba haziwezi kumpanga ndani ya mwamini wa kweli, lakini zinaweza kumwonea na kumtaabisha. Haifai Mkristo kukaa kufikiri juu ya pepo mbaya, wala kuishi akiwogopa. Anapata ndani ya silaha za Mungu vyote anavyohitaji kumwezesha kushinda vita namna zote. Mtume anaita malaika haya yaliyoanguka **falme** na **mamlaka**, na **watawala wa ulimwengu wa giza hili**, na **majeshi ya pepo wabaya katika pahali pa mbingu**. Hatuna elimu kutuwezesha kutambua tofauti ya pepo hawa; labda wengine ni wenye amri ya kipimo mbalimbali, kama watawala wetu kwa wakati wa sasa.

6:13 Tunafikiri wakati Paulo alipolandika maneno haya, alilindwa na askari akivala silaha yake. Kama ilivyokuwa desturi yake, aliona ndani ya neno hili mafundisho kwa roho zetu, kwamba tunazungushwa na adui za kuogofya. Anatuonya **kutwaa silaha zote za Mungu, mupate kuweza kushindana** wakati vita ni kali zaidi, na **mukikwisha kutimiza yote, kusimama**. Tunafikiri **siku ya uovu** inasema juu ya wakati vita ya Shetani ni kama maji ya garika. yanayoongezeka na kupunguka. Hata wakati Bwana wetu alipojaribiwa jangwani, Shetani alimwondokea kwa wakati (Lk. 4:13).

6:14 Kipande cha kwanza kinachota-jwa ni mkaba wa **kweli**. Lazima tuwe waaminifu na kushika kweli ya Neno la Mungu, lakini inapasa **kweli** kutushika sisi vilevile. Sharti tutumie kweli ndani ya maisha yetu ya kila siku. Wakati tunapojaribu kila kitu na **kweli**, tunalindwa na kupata nguvu wakati wa vita.

Kipande cha pili ni **silaha ya haki**

kwa kifua. Kila mwamini anavikwa na haki ya Mungu (2 Kor. 5:21), lakini sharti aonyeshe uaminifu na haki ndani ya maisha yake ya kila siku vilevile. Mtu mmoja alisema ya kwamba “Wakati mtu anapovikwa na mwenendo wa haki, hawezekani kumshinda. Hawezi kushindwa na mashitaki ya watu.” Mishale ya Shetani haiwezi kutuumiza kama tukiwa na damiri safi mbele ya Mungu na watu. Daudi alivaa **silaha ya haki** katika Zaburi 7:3-5. Bwana Yesu aliivaa wakati wote (Isa. 59:17).

6:15 Lazima askari afungiwe **miguu yake na utayari wa Habari Njema ya salama.** Inapasa akae tayari kutoka nyumba yake, na kupeleka Habari Njema ya salama, na kuingia hata inchi ya adui. Ni hatari kubwa kupumzika tu nyumbani. Lakini ni salama kufuata miguu mizuri ya Mwokozi na kuhubiri habari za furaha na kutangaza salama (Isa. 52:7; Rom. 10:15).

6:16 Zaidi ya yote, inafaa askari kuttwaan **ngabo ya imani ili mishale yenye moto ya yule mwovu** inayotumwa kumwumiza, ipige ngabo yake na kuananga chini bila kumwumiza. Maana ya **imani** hapa ni kutegemea Bwana na Neno lake. Wakati wa majaribu makali, na tukiwa na matata mengi yanayoamsha mashaka rohoni mwetu, tunananya macho na **imani** na kusema, “Ninaamini Mungu.”

6:17 Mwishoni, **kofia** ya Mungu ni wokovu (Isa. 59:17). Si neno kama vita ni kali, Mkristo haogopi kwa sababu anajua kwamba bila shaka itakwisha naye atashinda. Kujua neno hili kabisa kutamzuiza asirudi nyuma au kushindwa na adui. “Kama Mungu akiwa upande wetu, ni nani aliye juu yetu?” (Rom. 8:31).

Mwishoni, askari anashika **upanga wa Roho, ndio Neno la Mungu.** Hata Bwana wetu alitumika na **upanga** huu wakati alipokutana na Shetani. Alitaja mashairi toka Neno la Mungu mara tatu,

– si mashairi yo yote, lakini mashairi ya kufaa kwa wakati ule aliyopewa na Roho Mtakatifu (Luka 4:1-13). Maana ya **neno la Mungu** hapa si Biblia nzima, lakini mashairi fulani yanayofaa vizuri zaidi kwa wakati wenyewe.

David Watson anasema:

Mungu anatalinda kwa kila njia. Sharti mwenendo wetu uwe na kweli pamoja na Bwana, na ya kwamba maisha yetu ni haki na Mungu na wenzetu. Sharti tujaribu kuleta salama pahali po pote tunapokwenda, na kunyanya ngabo ile ya imani pamoja kuzima mishale ya kuwaka kwa moto ya yule mwovu. Lazima tulinde nia zetu tusishindwe na woga na mashaka, na tutumike na Neno la Mungu vizuri kwa uwemo wa Roho. Kumbuka kwamba Yesu alishinda adui yake jangwani kwa njia ya kumpiga mara tatu na neno la Mungu.¹⁵

6:18 Maombi hayatajwi kama sehemu ya silaha, lakini ni neno kubwa sana kwa askari, na inafaa aishi na roho ya maombi. Sharti ajivike na silaha yake pamoja na maombi na kupiga vita na adui. Sharti tukae na **maombi saa zote**, si wakati mmoja mmoja tu. Inapasa kuwa desturi kwa sisi kuomba, si neno tunalofanya mara moja moja tu. Na inapasa **maombi** kuwa namna namna. Inapasa askari kuomba pamoja na watu wengine, na wakati yeeye ni peke yake vilevile. Anaweza kuomba na kusudi juu ya neno fulani, na vilevile kwa wakati wa hitaji la gafula. Anaweza kuombea watu wengine, na anaweza kuomba pamoja na kukiri zambi zake mwe nyewe na kujinyenyekeza mbele ya Bwana, na anaweza kutoa sifa na mashukuru.

Na sharti **maombi** yawe **katika Roho**, maana yake kuongozwa na Roho. Kuomba maombi tuliojifunza kwa nia

ni faida gani kwa kushindana na majeshi ya gehena? Sharti tuwe na uangalifu katika **maombi**. Haifai kuacha mafikiri yetu kuhangaika na kupata hamu ya usingizi kwa wakati wa maombi, au kuwaza juu ya maneno mengine. Na sharti **tudumu** katika maombi. Inapasa kukaa kuomba, kutafuta, kupiga hodi (Luka 11:9). Inafaa **kuombea watakatifu wote**. Wao wanapiga vita vilevile, na wanahitaji kusaidiwa na **maombi** ya askari wenza.

6:19 Paulo aliongeza, **na kwa ajili yangu**. Yeye mwenyewe alihitaji maombi ya Waefeso.

Paulo alikuwa gerezani wakati alipandika maneno haya, lakini hakuomba aweze kufunguliwa mbio. Aliomba apewe **usemi** kwa kufungua **kinywa** chake na **uhodari** kuhubiri **siri ya Habari Njema**. Hii ni mara ya mwisho Paulo aliyoitaja **siri** ndani ya barua yake kwa Waefeso. Ni kwa sababu ya siri hii alikuwa gerezani. Hakuwa na uchungu juu ya neno hili lakini alitaka kuitangaza na uhodari na bidii kupita.

6:20 Ni desturi kwa mjumbe wa inchi fulani anayetumwa kwa inchi nyngine kutokuhukumiwa au kufungwa gerezani ndani ya inchi ile. Lakini ni kama watu wanavumilia karibu maneno yote kupita kusikia Habari Njema. Inaamsha uadui ndani ya roho zao na kuwasukuma kutesa wahubiri. Hivi **mjumbe** huyu wa Kristo, ndiye Paulo, alikuwa **katika mi nyororo**.

Neno la mahubiri la Paulo lililoamsha uadui zaidi ndani ya roho za Wayuda lilikuwa tangazo lake kwamba waamini Wayuda na wa Mataifa ni sasa jamii mpya moja wanaoshiriki ndani ya mapendeleo sawasawa, na kukiri kwa mba Kristo ni Kichwa chao.

F. Salamu ya Paulo (6:21-24)

6:21, 22 Paulo alikuwa akituma **Tikiko** toka Roma kwenda Efeso kujulisha watakatifu habari zake. Alisifu

Tikiko akisema yeye ni **ndugu mpendwa na mtumishi mwaminifu katika Bwana**. Tunasoma juu ya Tikiko mara tano tu ndani ya Agano Jipy. Alikuwa mmoja wa watu waliosafiri pamoja na Paulo toka Yunani kwenda Asia (Mdo. 20:4). Alikuwa mjumbe wa Paulo kwa Wakristo katika Kolosayi (Kol. 4:7); kwa Efeso (ona 6:21 pamoja na 2 Tim. 4:12), na labda kwa Tito katika Krete (Tito 3:12). Hapa, pamoja na kupeleka barua ya Paulo kwa Waefeso, kazi ya Tikiko ilikuwa kujulisha watakatifu hali ya Paulo gerezani, na kufariji **mioyo** yao wasiogope bure.

6:23 Ndani ya mashairi ya mwisho ya barua hii tunaona salamu Paulo ali-yotumia mara nyngi – *salama* na *neema*. Maneno haya mawili yanajumlisha baraka zote alizotuma kwa wasomaji wake. Kwa njia ya kutumika na maneno haya ya Wayuda na Mataifa pamoja, labda alifikiri tena kwa maficho juu ya siri ya Habari Njema – ya kwamba waamini Wayuda na wa Mataifa ni moja sasa ndani ya Kristo. Ndani ya shairi 23 alitaka wasomaji wake kuwa na **salama na mapendo** pamoja na **imani**. **Salama** itasaidia mioyo yao kuwa na nguvu katika maneno yo yote yatakyotokea. **Mapendo** yatawasaidia kuabudu Mungu na kutumika pamoja na watu wengine. **Imani** itawapa uwezo kupiga vita kwa Kristo. Baraka hizi zote zinatoka kwa **Mungu Baba na Bwana Yesu Kristo**. Neno hili liliwezekana tu kwa sababu Baba na Mwana ni sawasawa.

6:24 Mwishoni, mtume mpPENDWA aliomba **neema** iwe pamoja na **wote wanaopenda Bwana wetu Yesu Kristo** katika mapendo yasiyokoma. Mapendo ya kweli ya Wakristo yanaweza kupunguka mara nyngine, lakini hayazimiki kamwe.

Mfungwa huyu wa heshima ameondokea gereza ile ya Waroma zamani. Mtume Paulo amepokea zawabu yake na kuona uso wa Bwana wake mpe-

ndwa. Lakini sisi tungali na barua hii – haikugeuka tangu siku Paulo alipoiandika. Hata kwa wakati wa sasa inatufundisha, kututia bidii, kuonyesha zambi zetu, na kutuonya.

Vizuri kitabu hiki ... na mafundisho yake juu ya utakatifu kitusaidie kuishi maisha ya faida kupita mbele, kwa utukufu wa Mungu. (H. W. Webb-Peploe)¹⁶

NOTES

- ¹ (1:3) Lewis Sperry Chafer, *The Ephesian Letter*; p. 74.
- ² (Excursus) W. G. Blaikie, "Ephesians," *Pulpit Commentary*, XLVI:3.
- ³ (1:10) John G. Bellett, *Brief Notes on the Epistle to the Ephesians*, pp. 6, 7.
- ⁴ (1:19) F. B. Meyer, *Key Words of the Inner Life*, p. 92.
- ⁵ (1:19) Chafer, *Ephesian Letter*; p. 57.
- ⁶ (2:4) John Eadie, *Commentary on the Epistle to the Ephesians*, p. 141.
- ⁷ (3:16) Jamieson, Fausset, and Brown, *Commentary Practical and Explanatory on the whole Bible*, VI:408.
- ⁸ (3:17) Graham Scroggie, "Paul's Prison Prayers," *The Ministry of Keswick*, Second Series, p. 49.
- ⁹ (3:21) George Williams, *The Student's Commentary on the Holy Scriptures*, p. 925.
- ¹⁰ (4:12) Vance Havner, *Why Not Just Be Christians*, p. 63.
- ¹¹ (4:32) R. C. H. Lenski, *The Interpretation of the Epistles to the Galatians, to the Ephesians, and to the Philippians*, p. 588.
- ¹² (5:13) Blaikie, "Ephesians," XLVI: 209.
- ¹³ (5:13) Bishop Ellicott and Dean Alford preferred this translation.
- ¹⁴ (5:21) Charles Erdman, *Ephesians*, p.
- 106.

¹⁵ (6:17) David Watson, *Discipleship*, p. 183.

¹⁶ (6:24) H. W. Webb-Peploe, "Grace and Peace in Four Pauline Epistles," *The Ministry of Keswick, First Series*, p. 69.

BIBLIOGRAPHIE

Bellet, John G. *Brief Notes on the Epistle to the Ephesians*. London: G. Morrish, n.d.

Blaikie, W. G. "Ephesians," *Pulpit Commentary*, Vol. XLVI. New York: Funk & Wagnalls, n.d.

Chafer, Lewis Sperry. *The Ephesian Letter*. Findlay, Ohio: Dunham Publishing Company, 1935.

Dale, R. W., *The Epistle to the Ephesians: Its Doctrine and Ethics*. London: Hodder and Stoughton, 1893.

Eadie, John. *Commentary on the Epistle to the Ephesians*. Grand Rapids: Zondervan Publishing House, 1957.

Erdman, Charles R. *The Epistle of Paul to the Ephesians*. Philadelphia: Westminster Press, 1931.

Flint, V. Paul. *Epistle to the Ephesians: To the Praise of His Glory*. Oak Park, IL Emmaus Bible School, n. d.

Meyer, Frederick Brotherton. *Key Words of the Inner Life: Studies in the Epistle to the Ephesians*. Fleming H. Revell Company, 1893.

_____. *The Heavenlies*. Westchester, IL Good News Publishers, n. d.

Paxson, Ruth. *The Wealth, Walk, and Warfare of the Christian*. New York: Fleming H. Revell Co., 1930.

Wright, Walter C. *Ephesians*. Chicago: Moody Press, 1954.

BARUA KWA WAFILIPI

Utangulizi

“Kitabu kidogo chenye mafundisho ya neema ndani ya vifuniko vya neema.”

— J. H. Jowett

I. Nafasi ya pekee katika Kanuni

Watu wanahehimu sana nyumba ya kwanza kwa kuabudu Mungu, ndilo kanisa, linalosimamishwa ndani ya mji fulani. Wangeheshimu sana sana kanisa la kwanza lililosimamishwa ndani ya sehemu kubwa ya dunia, ndiyo Europe! Kanisa hili la kwanza katika Europe lisimamishwa kwa inchi ya Makedonia, (iliyo sehemu ya kaskazini ya Yunani kwa wakati wa sasa). Ingepasa Wakristo (na hata wasioamini) kufurahi sana kama tungefahamu baraka zote za Mungu tulizopokea kwa sababu Paulo alitii mwito wa Mungu kwenda kwa mangaribi kwa inchi ya Makedonia kuhubiri Habari Njema.

Waamini wa kanisa kwa Filipi walikuwa wenyewe ukarimu na walituma mali tena na tena kusaidia mahitaji ya Paulo. Ni kwa sababu hii Paulo aliwaandikia barua hii ya asante.

Lakini barua kwa Wafilipi si barua ya asante tu. Ni barua ya furaha – tunaona maneno kama “furaha” na “furahi” zaidi ya mara kumi na mbili ndani ya sura inezza barua hii. Paulo alijuana na kufurahi kwa saa ya baraka na saa ya taabu (4:11). Na vilevile kulikuwa na mabishano na maonyo nusu tu ndani ya barua hii.

Wakristo wanaweza kufurahi zaidi kwa sababu Mwana wa Mungu alikubali kuja duniani kama Mtu – si kama mtu tu, lakini kama Mtumwa! Na hakuponyesha wagonjwa tu na kufundisha watu, lakini alifuata njia ambayo ilimfikisha hata mauti – mauti juu ya msalaba. Wafilipi 2:5-11 yanapasha juu ya kweli hii kubwa. Watu wengine wanafikiri Wakristo wa kwanza waliimba mashairi haya kama wimbo ulioandikwa na Paulo au mtu mwingine. Hata mashairi haya yanafundisha umoja kwa njia ya unyenyekevu. Mafundisho ya dini yanafungana pamoja na mafundisho juu ya mwenendo kila mara ndani ya Agano Jipya.

Barua hii kwa Wafilipi ni kimoja cha vitabu vya furaha na utamu zaidi ndani ya Biblia nzima.

II. Mwandishi

Zaidi ya walimu wanafikiri kwamba bila shaka barua hii iliandikwa na Paulo. Wengine wanafikiri ilikuwa barua mbili pamoja au kwamba mashairi juu ya Mtumwa (2:5-11) yaliongezwa nyuma. Hakuna andiko linalohakikisha mawazo haya.

Watu waliotaja mashairi ya barua hii zamani walisema mara nyingi kwamba iliandikwa na Paulo. Majina ya wengine

yalikuwa Ignatius, Clément ya Roma, Polycarp, Irenaeus, Clément ya Alexandrie, na Tertullian. “Canon” ya Marcion na ile ya Muratorian zinataja kwamba kitabu hiki kiliandikwa na Paulo.

Ndani ya 1:1 jina la Paulo linatajwa waziwazi, na zaidi ya ile, namna ya maandiko ya barua hii inatufikirisha maandiko mengine ya Paulo.

III. Tarehe

Paulo aliandika Wafilipi wakati alipokuwa gerezani, kama vilevile Waefeso, Wakolosayi, na Filemono. Kwa sababu hii barua hizi zinaitwa “Barua za Kifungo.” Ni kama Waefeso, Wakolosayi, na Filemono zi-liandikwa karibu na 60 A.D., lakini maneno mengine yanaonyesha kwamba barua kwa Wafilipi iliandikwa nyuma kidogo. Marcion alisema wazi kwamba Paulo aliandika toka Roma. Masemo yake yanapatana na 1:13 na 4:22 ambayo yanatufikirisha kwamba barua hii iliandikwa kwa Roma. Paulo alishinda miaka miwili katika kifungo kwa Roma, na maneno mengine yana-tufikirisha kwamba aliandika barua hii karibu na mwisho wa muda huu. Kwa mfano, 1:12-18 yanaonyesha ya kuwa alihubiri katika Roma kwa muda mrefu kidogo. Ni kama 1:12, 13, 19, 23-26 yanaonyesha kwamba aliamini atafunguliwa nyuma kidogo.

Maneno haya, pamoja na habari za kufika kwa wageni, na barua na zawiadi za mali zilizotumwa zinaonyesha tarehe karibu na mwisho wa 61 A.D.

IV. Msingi na Jambo Kubwa

Ilikuwa siku kubwa na yenyewe maana sana wakati Paulo alipofikia Troa kwa safari yake ya pili ya kuhubiri Habari Njema. Troa ulikuwa mji kwa pwani wa kaskazini-mangaribi wa Asia Ndogo kwa Bahari ya Kati. Ngambo ya bahari hii ilikuwa Yunani. Usiku mmoja, mtu

toka Makedonia alitokea mtume katika ono, akisema: “Vuka, uje Makedonia kutusaidia” (Mdo 16:9). Mara moja Paulo aliondokea Troa na chombo kwenda kwa Makedonia, pamoja na Timoteo na Luka na Sila. Walifikia *Europe* kwanza kwa Neapoli na walisafiri toka pale kwenda Filipi. Mji huu ulikuwa sehemu ya ufalme wa Roma. Ulitawaliwa na serikali waliokuwa Waroma na walitolea wenyeji wa mji ruhusa kugeuka Waroma.

Siku ya sabato wahubiri wa Habari Njema walikwenda kwa mto pahali ilipokuwa desturi ya wanawake kuku-sanyika kwa maombi (Mdo. 16:13). Ludia wa Tuatera alikuwa mmoja wao, mwenye kazi ya kuuza rangi nyekundu. Tunafikiri wakati alipopokea Habari Njema, ali-geuka mtu wa kwanza kwa Europe aliyegeuka Mkristo.

Lakini Paulo hakukaa na salama tu katika Filipi. Msichana mmoja mwenye pepo ya kuagua (maana yake kupasha mbele habari za maneno yatakayotokea kwa wakati wa kuja), alikutana na watumishi wa Bwana, akawafuata kwa wakati akipaza sauti, na kulia: “Watu hawa ni watumishi wa Mungu aliye juu, wenyewe kutuhubiri njia ya wokovu” (Mdo. 16:17). Mtume Paulo hakukubali kupokea ushuhuda wa mwenye roho ovu, akaagiza pepo kumtoka. Bwana za kazi za kijakazi walipata faida nyingi kwa njia ya kuagua kwake. Wakati walipoona neno lilokwisha kutokea, walikasirikia Paulo sana. Walikokota Paulo na Sila kwa soko kukutana na serikali ya Roma. Watu hawa waliagiza wapigwe kwa fimbo na kutupwa gerezani.

Tumejua maneno yaliyotokea ndani ya gereza ile. Katikati ya usiku Paulo na Sila walikuwa wakiomba na kusifu Mungu na nyimbo. Gafula kulikuwa na tetemeko kubwa la inchi lililofungua milango ya kifungo na kulegeza minyororo

ya wafungwa wote. Mlinzi wa kifungo alifikiri wafungwa wote walikimbia na alikuwa karibu kujiuwa mwenyewe, lakini Paulo alimjulisha kwamba wafungwa hawakukimbia. Halafu mlinzi wa kifungo aliwauliza, "Bwana zangu, nifanye nini nipate kuokolewa?" Hatutasahau kamwe jibu la Paulo: "Amini Bwana Yesu Kristo nawe utaokolewa" (Mdo. 16:31). Kwa neema ya Mungu mtu mwingine aliokolewa kwa Filipi! Asubui watawala wa mji walisukuma Paulo nao waliokuwa pamoja naye kuondokea mji mbio. Paulo alikataa kufanya hivi. Aliwakumbusha kwamba hata kama akiwa Mroma, walikuwa wame-mpiga na simbo, na walimfunga gerezani bila kumhukumu. Watawala wa mji walikaa kumsihii kuondoka mji. Mwishoni Paulo nao waliosafiri pamoja naye walifikia nyumba ya Ludia

na kulagana nao, kisha walikwenda zao (Mdo. 16:40).

Nyuma ya karibu miaka 10 Paulo aliandikia Wafilipi barua. Alikuwa gerezani tena. Wafilipi walikuwa wamesikia habari hizi, na walimtumia zawadi ya mali. Epafroditu aliagizwa kupelekeea Paulo zawadi hii. Nyuma ya kufanya hivi alikaa pamoja na Paulo kwa wakati kumsaidia. Halafu Epafroditu mwenyewe alipata ugonjwa vilevile na alikuwa karibu kufa, lakini Mungu alimrehemu na kumponyesha. Alikuwa tayari kurdia Filipi sasa, kwa kanisa lake, hivi Paulo alimpa barua hii ya asante kupelekeea waamini wa pale.

Barua hii kwa Wafilipi inaonyesha kwamba Paulo alipenda sana kanisa hili aliloanza, na alikuwa na ushirika mtamu na waamini wale.

HABARI YALIYOMO

1. Salamu ya Paulo, sifa na maombi (1:1-11)
2. Paulo gerezani, mambo aliyotazamia, na maombi kwa uvumilivu (1:12-30)
3. Maonyo kwa umoja, kufuatana na mfano wa unyenyekevu na zabihu ya Kristo (2:1-16)
4. Paulo, Timoteo na Epafroditu, ndio mifano ya Kristo (2:17-30)
5. Maonyo juu ya walimu wa uwongo (3:1-3)
6. Paulo alihesabu uriti na utendaji wake bora wa mbele kuwa hasara kwa ajili ya Kristo (3:4-14)
7. Maonyo ya kuiga mwenendo mtakatifu wa Paulo (3:15-21)
8. Kusihii Wakristo kuwa na umoja, wasaidiane, wawe na furaha, maombi, kuvumiliana, na mawazo mema (4:1-9)
9. Asante ya Paulo kwa zawadi ya mali ya waamini (4:10-20)
10. Salamu ya mwisho (4:21-23)

Maelezo

1. Salamu ya Paulo, sifa na maombi (1:1-11)

1:1 Paulo na Timoteo wanatajwa pamoja kwa mwanzo wa barua hii, lakini Timoteo na Paulo hawakuandika barua hii pamoja. Timoteo alikuwa pamoja na Paulo wakati alipofikia Filipi mara ya kwanza, hivi waamini wa Filipi walimjua. **Timoteo** alikuwa pamoja na **Paulo** sasa wakati mtume alipoanza kuandika barua hii.

Paulo alikuwa mzee sasa (Flm. 9), na Timoteo alikuwa kwanza kijana. Hivi mzee na kijana walifungana pamoja ndani ya utumishi wao kwa Bwana aliye bora kuliko bwana wo wote.

Wao wawili waliitwa **watumwa wa Kristo Yesu**. Wao wawili walipenda Bwana wao, na zabihu yake kwa Kalvari iliwafunga kutumikia Mwokozi wao daima.¹

Barua hii iliandikwa **kwa watakatifu wote katika Kristo Yesu walio katika Filipi, pamoja na waangalizi na watumishi**. Neno hili *wote* linaonekana mara nyingi kidogo ndani ya barua hii. Paulo alipenda watu **wote** wa Bwana.

Watakatifu katika Kristo Yesu walio katika Filipi. Kwa maneno ya roho, Mungu aliweka waamini hawa mbali **ndani ya Kristo Yesu**. Kwa maneno ya dunia walikuwa kwa **Filipi**. Walikuwa kwa pahali hapa pawili pamoja kwa saa moja!

Halafu mtume alitaja **waangalizi na watumishi**. **Waangalizi** walikuwa wazee au wasimamizi walioangalia maneno ya kanisa, na waliolinda kundi la Mungu kwa njia ya mfano wa mwenendo wao mtakatifu. Kazi ya **watumishi** ilikuwa kuangalia mahitaji ya kanisa, kama nyumba yenye, kulinda mali yake, vivi hivi.

Kulikuwa na watu namna tatu tu ndani ya kanisa – **watakatifu, waangalizi, na**

watumishi. Kama askofu angalikuwa juu ya watu hawa wote, Paulo angalimtaja vilevile. Lakini alisema juu ya **waangalizi** (kupita mmoja) na **watumishi** (kupita mmoja vilevile.)

Tunaona hapa kwamba kanisa la wakati wa mwanzo halikuwa na maneno na mapambo mengi. **Watakatifu** walitajwa kwanza, nyuma yao *viongozi vyao kwa maneno ya roho*, na mwishoni *watumishi* walioangalia mahitaji ya kanisa. Hakuna wakubwa na viongozi wengine!

1:2 Kama ilivyokuwa desturi yake, Paulo alisalimu watakatifu na **neema** ... na **salama**. Neema hii haikuwa zaidi neema mwenye zambi aliyopokea wakati alipookolewa. Ilikuwa **neema** ambayo mwamini anahitaji na kupokea kwa kiti cha neema kumsaidia kwa wakati wa mahitaji (Ebr. 4:16). Na vilevile Paulo hakufikiri zaidi juu ya **salama** ya waamini na Mungu, kwani walikuwa wamepokea salama hii. Alitaka wawe na **salama ya** Mungu inayopatikana kwa njia ya maombi na mashukuru (4:6, 7).

Baraka hizi mbili zote zinatoka kwa **Mungu Baba yetu na Bwana Yesu Kristo**. Mtume aliheshimu Mwana kwa kipimo alichoheshimu Baba (Yn. 5:23). Ni wazi kabisa ya kwamba Paulo alijuwa Yesu Kristo ni Mungu.

1:3 Sasa Paulo alianza wimbo wa mashukuru. Alifanya hivi mbele vilevile wakati alipokuwa katika kifungo pamoja na Sila saa alipokuwa kwa Filipi mara ya kwanza. Labda wakati alipoandika maneno haya alikuwa gerezani kwa Roma, lakini hakuacha kutoa wimbo wa sifa. Magumu hayakumshinda! **Ukumbusho wa Wafilipi** uliamsha sifa rohoni mwake kila mara. Waamini wa Filipi walikuwa watoto wake kwa imani, na zaidi ya neno hili kanisa lao lilikuwa mfano mwema kwa makanisa mengine.

1:4 Aliwaombea kila mara **pamoja na furaha**. Halikuwa neno gumu kwa ye ye kuwaombea. Shairi hili na mashairi mengine yanaonyesha kwamba Paulo alikuwa mtu wa maombi. Neno hili linatufahamisha kwa nini Mungu aliweza kufanya kazi ya ajabu kwa njia ya Paulo. Wakati tunapokumbuka kwamba alifanya safari nyingi, na alijuan na na watu wengi, tunashangaa kuona kwamba aliwakumbuka wote mmoja mmoja.

1:5 Aliwashukuru kwa **ushirika** wao katika kuendesha **Habari Njema toka siku ya kwanza hata sasa**. Labda walishiriki naye kwa njia ya zawadi ya mali, lakini kwa njia ya maombi yao vilevile, na kwa njia ya kujitoo kabisa kwa kazi ya kuhubiri Habari Njema. Wakati tunaposoma juu ya **siku ya kwanza**, tunafikiri labda mlinzi wa kifungo alikuwa kwanza hai wakati barua hii iliposomwa kwa waamini kanisani. Kama ni hivi, habari hizi zingejaza roho yake na furaha.

1:6 Wakati mtume alipowaza juu ya mwanzo mwema wa waamini katika maisha yao kwa Kristo **alijua kabisa** kwamba Mungu atatimiza **kazi njema aliyoanza** ndani yao.

Labda **kazi njema** hii ilikuwa wokovu wao, au mali yao kusaidia kazi ya kuendesha Habari Njema. **Siku ya Yesu Kristo** ni wakati Bwana atakapokuja tena kupeleka watu wake mbinguni. Labda ni wakati wa kiti cha hukumu cha Kristo vilevile, saa atakapoangalia utumishi wa waamini na kuwapa zawabu.

1:7 Paulo alifikiri ni haki kwa ye ye kuwa na asante kwa Wafilipi **moyoni** mwake. Alikumbuka namna walivymsimamia na roho moja wakati alipohukumiwa na waamuzi, katika gereza, au wakati aliposafiri pahali mbalimbali **kulinda na kusimamia Habari Njema**. Maana ya **kulinda Habari Njema** ni zaidi kujibu maulizo ya wajuzi, lakini **kusimamia Habari Njema** ni zaidi

kuimarisha Habari Njema rohoni mwa wale amba wanakwisha kuiamini.

W. E. Vine alisema, “Habari Njema inashinda adui zake na inapatisha rafiki zake nguvu.”² **Neema** ndani ya shairi hili inasema juu ya nguvu tusiyostahili kupokea toka Mungu kuendelea na kazi ya Bwana hata wakati wa ushindani wa nguvu wa adui.

1:8 Ukumbusho wa namna walivymsimamia na uaminifu uliamsha **hamu** ndani ya roho ya mtume kuwa pamoja nao tena. Aliomba **Mungu** kumshuhudia kwamba **alikuwa na hamu kubwa** kwa ajili yao **katika moyo wa Yesu Kristo**. Masemo ya mapendo ya Paulo ni ajabu zaidi wakati tunapokumbuka ya kwamba ye ye aliyekuwa Myuda alikuwa akiandika barua hii kwa watu wa Mataifa. Neema ya Mungu ilikuwa imebomoa machukio ya zamani, na sasa waliikuwa wote moja ndani ya Kristo.

1:9 Mashukuru ya Paulo yalikombolewa na maombi sasa. Paulo atanomba wapewe mali, kuburudishwa na kuweza kukaa bila masumbuko? Sivyo. Aliomba **mapendo** yao yaweze kukaa kuongezeka sana **katika hekima na ufahamu wote**. Kusudi la kwanza la maisha ya Mkristo ni **kupenda** Mungu na **kupenda** watu wenzake. Lakini pamoja na ile inampasa kutumika na hekima na **ufahamu**. Bila kufanya hivi inawezekana kwa kazi yetu kuwa bure. Hivi Paulo aliombea Wafilipi waweze kuendelea kuonyesha mapendo ya Kristo, lakini **mapendo** yao yaongozwe na **hekima na ufahamu wote**.

1:10 Mapendo yao yakiongozwa hivi na hekima na ufahamu wataweza kufahamu maneno gani ni **mema zaidi**. Tena na tena ndani ya maisha yetu maneno mengine ni mema lakini mengine ni mema zaidi. Ni kama mara nyine mambo mema ni adui za yale yaliyo mema zaidi. Kwa kutumikia Bwana vizuri, inatupasa kuchagua mambo yaliyo na faida zaidi.

Mapendo yao yakiongozwa na ufa-hamu, neno hili litawawezesha kuepuka maneno mabaya. Paulo alitaka wawe na moyo safi, pasipo kosa, mpaka **siku ya Kristo**. Sisi sote tunafanya zambi, lakini hapa mtu pasipo kosa ni mtu anayekiri zambi zake na kuziacha, pamoja na kuomba watu ambaو alikosea wa-msamehe, na kuwalipa ukombozi kama ikiwezekana.

Siku ya Kristo, kama ndani ya shairi 6, ni wakati Kristo atakapokuja kupeleka waamini mbinguni, na kisha kupima kazi yao.

1:11 Mwishoni mtume aliomba Wakristo wawewe **kujazwa na matunda ya haki**, maana **matunda** yanayozaliwa na mwenye maisha ya **haki**, yaliyo **kwa njia ya Yesu Kristo, na kwa utukufu na sifa ya Mungu**. Ombi hili la Paulo linafanana na maneno katika Isaya 61:3, “wapate kuitwa miti ya haki (**kujazwa na matunda ya haki**), iliyopandwa na BWANA (**yaliyo kwa njia ya Yesu Kristo**) ili atukuzwe (**kwa utukufu na sifa ya Mungu**).”

Lehman Strauss aliandika, “Neno hili ‘tunda’ linatukumbusha ukaribu wetu na Kristo, na maneno anayotaka kuona ndani ya maisha yetu. Kusudi la matawi ya mzabibu ni kuzaa matunda.”³

2. Paulo gerezani, mambo aliyotazamia, na maombi kwa uvumilivu (1:12-30)

1:12 Ombi la Paulo lilikwisha. Sasa alitaja baraka zake zote, ndizo matunda ya kufungwa kwake gerezani. Jowett alii mashairi haya “Baraka ya taabu.”

Mtume alitaka **ndugu kujua ya kumba mambo ambayo yalimpata**, ndiyo hukumu na kufungwa kwake gerezani, hayaku zuiza Habari Njema, kama watu waliweza kufikiri, lakini yalitokea **kuendelesha** Habari Njema. Ni mfano mwagine namna Mungu ana-vyogeuza mashauri maovu ya pepo wachafu na watu, na analeta kushinda

toka msiba. “Mtu anafungana na uovu wake, lakini Mungu anatimiza shauri lake.”

1:13 Neno la kwanza lilikuwa kumba watu nyumbani mwa askari **waliona wazi** ya kuwa **vifungo** vyake vimekuwa **katika Kristo**; maana yake alifungwa kwa sababu ya ushuhuda wake kwa Kristo, si kwa sababu alitenda mabaya.

Watu walijua sababu ya **minyororo** yake katika **nyumba nzima ya askari**, ndipo pahali pa askari waliolinda kao la mfalme, na pahali pote pengine vilevile. Paulo alikuwa akisema kwamba kufungwa kwake kulikuwa ushuhuda kwa watawala Waroma pahali alipokuwa.

1:14 Tunda zuri la pili la kufungwa kwake lilikuwa kuongezeka kwa uhdari wa waamini wengine kushuhudia Bwana Yesu bila woga. Mara nyingi mateso yanageuza waamini wapole na wenyre woga kuwa washuhuda wahodari.

1:15 Wengine walihubiri **Kristo** pamoja na **hasidi** na fitina rohoni.

Wengine, wakiwa na makusudi safi, walihubiri Kristo **kwa nia njema** kwa sababu walitaka kusaidia Paulo.

1:16 Wahubiri wenyre vivu walifikiri ya kwamba neno hili litaongeza uchungu wa kufungwa kwa Paulo. Habari walizohubiri ziliikuwa njema, lakini roho yao ilikuwa mbaya. Ni huzuni kufikiri kwamba inawezezana kutumikia Kristo kwa nguvu ya mwili, na choyo, vita, kiburi, na hasidi. Ni lazima kwa sisi kukaa kuangalia kama tukitumikia Bwana na kusudi gani. Haifai tuhubiri na kusudi la kukokota macho ya watu juu yetu, kwa kusimamia dini fulani, au kushinda Wakristo wengine. Njia nzuri kwa sisi ni kuwa wenyre mapendo pamoja na elimu na ufahamu.

1:17 Wengine walikuwa wakihubiri Habari Njema **na roho na mapendo safi**, wakijua kwamba Paulo aliweka roho sana juu ya kusimamia Habari

Njema. Walijua kwamba Paulo alikuwa gerezani kwa sababu ya kuhubiri **Habari Njema** na uhodari. Hivi walikusudi kuendelea na kazi yake wakati alipo-kuwa katika kifungo.

1:18 Paulo alikataa kuacha makusudi mabaya ya watu wengine kumhuzunisha. Watu wale wote **walihubiri** Habari Njema ya **Kristo**, na neno hili lilimfurahisha sana.

Ni ajabu ya kama hata kwa wakati wa hali ngumu namna hii Paulo hakujihurumia mwenyewe wala kuomba huruma karibu na watu wengine. Aliazwa na furaha ya Bwana, na alionya wasomaji wake kufurahi vilevile.

1:19 Paulo alitazamia na tumaini maneno yatakayotokea. Alijua kwamba ataponyeshwa toka kifungo. Mungu atatumika kwa njia ya maombi ya Wafilipi na kwa kusaidia kwa **Roho ya Yesu Kristo**. Kwa mafikiri yake maombi ya waamini wale wachache yalikuwa na uwezo wa kutosha kushinda uwezo mkubwa wa Roma. Ndiyo, ni kweli. Kwa njia ya maombi Wakristo wanawenza kushawishi hali ya mataifa na kugeuza maneno yatakayotokea.

Maana ya **kusaidia kwa Roho ya Yesu Kristo** ni uwezo wa Roho Mtakatifu ukitumika kwa ajili yake na kumpa nguvu. Ni uwezo usio na mpaka wa Roho kusaidia na kuwezesha waamini kusimama imara katika hali na magumu yo yote.

1:20 Wakati alipofikiri juu ya maombi ya Wakristo na kusaidia kwa Roho Mtakatifu, alisema juu ya hamu yake kubwa na **tumaini** lake ya kwamba hatakuwa na **haya** kamwe, lakini atashuhudia Kristo bila woga daima.

Si neno kama atafunguliwa, au kuhukumiwa **kufa**; tumaini lake lilikuwa kwa Kristo **kutukuzwa** ndani ya **mwili** wake, ili watu wengine waweze kumtukuza vilevile. Guy King alionyesha namna gani Kristo anaweza **kutukuzwa** ndani ya miili na **maisha** yetu:

... kumtukuza na midomo yetu ikimshuhudia na furaha; na mikono ambayo inamtumikia na furaha; na miguu inayofurahi kutumwa naye; kwa njia ya kupiga magoti na maombi kwa ufalme wake; kwa njia ya mabega yanayofurahi kubeba mizigo ya watu wengine.⁴

Kristo anaweza **kutukuzwa** ndani ya miili yetu kwa njia ya **mauti** vilevile – miili inayochakaa kwa njia ya kutumikia Bwana sana, inayoumizwa na adui, au kuvunjwa kwa sababu ya kutupiwa mawe au kuteketezwa.

1:21 Shairi hili linatuonyesha kusudi la maisha ya Paulo. Hakuishi kwa kupata mali mingi, wala kwa kusifiwa na watu, au kwa anasa. Kusudi kubwa la maisha yake lilikuwa kupenda, kuabudu, na kutumikia Bwana Yesu. Alitaka mai-sha yake kufanana na maisha ya **Kristo**. Alitaka Mwokozi kuishi maisha yake ndani ya maisha yake mwenyewe.

Na kufa ni faida. **Kufa** ni kuwa pamoja na Kristo na kuwa sawasawa naye kwa milele. Ni kumtumikia bila zambi moyoni, na miguu isiyoshika njia mbaya kamwe. Si desturi ya watu kufikiri kwamba mauti ni faida. Ni huzuni kwa sababu kwa wakati wa sasa zaidi ya watu wanafikiri “kuishi duniani ni faida, na ya kwamba hii itakwisha wakati wa kufa.” Lakini Jowett alisema: “Kwa mtume Paulo, mauti haikuwa njia ya giza pahali hazina zetu zote zinapooza upesi. Sivyo, ni njia ya neema, ambayo inatulinda na kutufishwa kwa nuru.⁵

1:22 **Kama** ni mapenzi ya Mungu kwa Paulo **kuishi** kwa muda mwингine **katika mwili**, halafu **utumishi** wa Paulo utakaa kuzaa matunda kwa yeye. Atawea kukaa kusaidia watu wa Bwana. Lakini ilikuwa nguvu kwa Paulo kuchagua – au kufikia Mwokozi ambaye alimpenda, au kubaki duniani kwa utumishi wa Bwana ambao alipenda sana vilevile. Hakujua kama **attachagua** nini.

1:23 Maana ya **kusongwa katika mambo mawili** ni kuchagua katika mambo **mawili** – kwenda mbinguni au kubaki duniani kama mtume wa Yesu Kristo.

Alikuwa na hamu sana **kwenda na kukaa pamoja na Kristo, maana ni vizuri zaidi sana**. Kama angalijifikiri mwenyewe tu, kama bila shaka angalichagua neno hili.

Ona ya kwamba Paulo hakuamini mafundisho ya watu wengine kwamba nafsi ya mtu inalala saa ya mauti. Aliamini kwamba Mkristo anakwenda kukaa **pamoja na Kristo** saa ya kufa kwake, na ya kwamba kwa saa ile anafurahi sana kuwa pamoja na Bwana. Ingekuwa neno la kuchekesha kwa yeze kusema kama watu wengine kwa wakati wa sasa: “Kuishi ni Kristo; kulala ni faida.” Au “Kuondoka na kulala ni vizuri zaidi.” Agano Jipyä linasema juu ya kulala kwa *mwili* wa mwamini kwa wakati wa kufa (1 Tes. 4:14), si juu ya kulala kwa nafsi yake. Usingizi wa nafsi ni hadizi.

Ona vilevile kwamba mauti ni mbali na kuja kwa Mwokozi. Kwa wakati wa kufa kwetu, sisi tunakwenda **kukaa pamoja naye**. Kwa wakati Kristo atakapokuja tena, yeze atafika kwetu.

1:24 **Kwa ajili** ya Wafilipi **ilihitajiwa zaidi** kwa Paulo kubaki duniani kwa wakati. Kweli hakujifikiri mwenyewe, na maneno gani yangaliweza kumsaidia kukaa vizuri. Aliweka roho tu juu ya maneno gani yaliyoweza kuendesha kazi ya Kristo vizuri zaidi, na nini itasaidia watu wake.

1:25 **Nikitumaini neno hili** – ya kwamba alihitajiwa kwanza duniani kufundisha, kufariji, na kusaidia roho za watakatifu – Paulo alijua kwamba hatauawa kwa wakati huu. Alijua neno hili namna gani? Tunaamini ya kwamba aliihi karibu sana na Bwana hata Roho Mtakatifu aliweza kumjulisha neno hili. “Siri ya Bwana ni pamoja na wale

ambao wanamwogopa” (Zab. 25:14). Watu wanaokaa karibu sana na Mungu, na mawazo kimya mbele yake, wanasiakia siri zinazozimwa na makelele na haraka haraka ya dunia yetu ya sasa. Ni lazima kukaa karibu sana na Mungu kwa kusikia siri zake. Paulo alikaa karibu.

Kwa njia ya kuishi kwanza duniani, Paulo atawenza kuwasaidia **kupata nguvu** katika imani, na kuongeza **furaha** ambayo walikuwa nayo kwa sababu ya kuamini Bwana.

1:26 Kama akiishi miaka mingine duniani, Wafilipi wataweza **kufurahi** hata kupita katika Kristo Yesu wakati Paulo atakapokuja kuwaona tena. Bila shaka wangemwambata na kumbusu, na kusifu Bwana na furaha kubwa wakati atakapofikia Filipi. Labda wangesema, “Hatukufikiri tutakuona tena. Tunasifu Bwana sana kwa sababu alikurudisha tena kwetu!”

1:27 Halafu Paulo aliongeza manonyo: “**Lakini mwenendo wenu uwe kama inavyopasa Habari Njema ya Kristo.**” Inafaa Wakristo kufanana na Kristo. Sharti wenyeji wa mbingu wataende kama inavyofaa kwa watu kutenda mbinguni.

Zaidi ya ile, hata akifikasi kuwaona yeze mwenyewe, au akipata tu habari zao, **anataka** kujua kwamba walikaa **imara** katika **roho** moja, na walishindana **kwa imani ya Habari Njema**. Wakristo wote wanashindana na adui mmoja; haifai wawe na magomvi, lakini wafungane pamoja kupigana na adui huyu.

1:28 Wala haifai **waogopeshwe** sana na adui za Habari Njema. Wakristo wakiwa bila woga kwa wakati wa mateso, ni alama wazi ya kupotea kwa adui zao wanaoshindana na Mungu. Ni alama ya **wokovu** vilevile kwa wenye kushindana na adui na uhodari. Labda **wokovu** unasema hapa juu ya wakati wa kuja saa Mkristo anapoponyeshwa toka

mateso, na juu ya ukombozi wa mwili wake, na wa roho na nafsi yake vilevile.

1:29 Ingepasa Wafilipi kukumbuka kwamba ni heshima **kuamini Kristo**, na **kuteswa** kwa ajili yake vilevile.

Dr. Griffith John aliandika ya kwamba siku moja wakati alipozungukwa na wapagano, na kupigwa, aliweka mkono wake kwa uso wake. Wakati alipondonsha mkono tena, aliona kwamba uliogeshwa na damu. “Neno hili lilijaza roho yake na shangwe kubwa kwa sababu alistahilishwa kupata mateso kwa jina la Kristo.” Ni ajabu kwa sababu hata mateso yanatukuzwa na ukristo!

1:30 Wafilipi vilevile walikuwa na **mashindano** namna Paulo aliyokuwa nayo mbele, na hata kwa saa ile.

3. Maonyo kwa umoja, kufuatana na mfano wa unyenyekevu na zabihu ya Kristo (2:1-16)

Kanisa katika Filipi lilikuwa kanisa zuri sana, na Paulo aliweza kusifu waamini juu ya maneno mengi. Hata hivi kwa siri kulikuwa na magomvi katikati yao. Wanawake wawili, Ewodia na Sintike, hawakupatana vizuri (4:2). Ni vizuri kukumbuka neno hili, kwa sababu ndani ya sura 2 mtume alifundisha wazi juu ya sababu ya magomvi katikati ya watu wa Mungu, na namna gani kuyamaliza.

2:1 Shairi hili linatujua maneno mane ambayo ingepasa kusaidia waamini kupatana vizuri na kushirikiana. Paulo alisema ya kwamba ikiwa faraja yo yote **katika Kristo**, na matulizo yo yote ya **mapendo** yake, na **Roho Mtakatifu** akitukutanisha ndani ya **ushirika** mzuri sana, na Wakristo wakiwa na **mapendo na rehema** nyingi, ingetuweza kukaa pamoja na upatano mzuri.

Ni wazi ya kwamba Paulo alionya waamini kuwa na umoja kwa sababu wao wote walipenda Kristo, nao wote

walikuwa na Roho Mtakatifu. Na mambo mema yote yaliyo **ndani ya Kristo**, ingepasa viungo vyta mwili wa Kristo kuwa na shauri moja, mapendo, upatano, na huruma.

2:2 Kwa sababu ya mafundisho haya, Paulo aliwasihii waweze **kujaliza furaha** yake. Wafilipi walikuwa wamemfurahisha mbele vilevile, na Paulo hakukana neno hili. Lakini sasa aliwaomba kujaza kikombe chake cha furaha tele na hata kufurika. Wanaweza kufanya hivi kwa njia ya kuwa na **nia moja, wenye mapendo mamoja, na wenye roho na nia moja**.

Shairi hili linatufundisha kwamba inapasa Wakristo kufikiri na kutenda sawasawa ndani ya maneno yote? Sivyo. Haya si mafundisho ya Neno la Mungu. Ndiyo, inapasa tuwe na nia moja juu ya misingi ya imani ya Wakristo. Ni wazi vilevile kwamba watu wana mafikiri mbalimbali juu ya maneno madogo. Kuwa *mfano wa mmoja* ni mbali na *umoja*. Hata kama hatupatani juu ya maneno madogo, tunaweza kuficha mawazo yetu wenye kusaidia watu wengine.

Maana ya kuwa na **nia moja** ni kuwa na nia ya Kristo, kuwaza juu ya maneno kama yeye angewaza, kuitika kama yeye. Kuwa na **mapendo mamoja** ni kuwa na **mapendo** kwa watu wengine namna ya **mapendo** ambayo Bwana alikuwa nayo kwa sisi, mapendo ya bei kubwa sana. Maana ya kuwa na **roho moja** ni kutumika pamoja na upatano wema kutimiza kusudi fulani. Mwishoni, kuwa **na nia moja** ni kutumika pamoja na umoja kuonyesha kwamba nia ya Kristo inangoza matendo yetu.

2:3 Haifai tutende neno lo lote kwa **kushindana wala kwa majivuno**, kwani maneno haya ni mawili ya adui kubwa zaidi zinazoharibu umoja wa

watu wa Mungu. Kwa sisi **kushindana** ni kutaka kuwa mkubwa zaidi, kwa garama yo yote. Kuwa na **majivuno** ni kujionyesha kuwa watu wema, kusudi watu wengine watufuate. Majivuno namna hii ni mbegu itakayozaa kushindana na ugomvi. Kwa mwisho wa shairi hili tunaona njia ya kuepuka hatari hii. **Kwa unyenyekevu kila mtu ahesabu mwenzake mzuri kuliko yeze mwenyewe.** Si kusema kwamba inatupasa kufikiri wavunja sheria wana roho safi kupita sisi, lakini inatupasa kuishi kwa watu wengine, bila kujifikiri wenyewe, na kuweka roho juu ya mahitaji yao kupita juu ya mahitaji yetu. Ni nyepesi kusoma maonyo namna hii ndani ya Biblia, bila kufikiri sana juu ya maana yao, lakini ni nguvu kupita kuyatii. Sisi watu hatujuani hata kidogo na **kuhesabu wenzetu wazuri kuliko sisi wenyewe**, na hatuwezi kufanya hivi na nguvu yetu wenyewe. Inawezekana tu kwa uwemo wa Roho Mtakatifu anayekaa ndani yetu.

2:4 Njia kutengeneza kiburi na mashindano na ugomvi katikati ya watu wa Mungu ni kwa kila mtu kuangalia kupita **maneno ya watu wengine**, si maneno ya maisha yake mwenyewe. Neno lililo ufunguo kutufahamisha mafundisho ya sura hii ni **wengine**. Kwa njia ya kujitoo kutumikia wengine na bidii tunaweza kushinda ugomvi na choyo ya watu.

*Wengine, Bwana, ndio, wengine
Hili live kusudi langu
Unisaide kuishi kwa wengine,
Niishi kama Wewe.*

— Charles D. Meigs (traduit)

2:5 Muwe na nia hii ndani yenu iliyokuwa ndani ya Kristo Yesu vilevile. Sasa Paulo alikokota macho ya Wafilipi juu ya mfano wa Bwana Yesu Kristo. Bwana Yesu alitendea wengine namna gani? Guy King aliandika kwamba Bwana Yesu:

(1) hakujifikiri mwenyewe;

- (2) alijitoa kama zabihu kwa wengine;
- (3) alitumikia wengine. Bwana Yesu aliwaza juu ya watu wengine saa zote.⁶

2:6 Wakati tunaposoma kwamba Kristo Yesu alikuwa na **namna ya Mungu**, tunafahamu kwamba tangu milele alikuwa kama **Mungu**. Si kusema kwamba alifanana tu na Mungu, lakini ya kwamba yeze *ni Mungu*.

Hata hivi **hakuona kuwa sawa na Mungu kuwa kitu kushikamana nacho**. Lazima tuone hapa tofauti ya kuwa sawa na Mungu kwa njia ya nafsi yake, na kwa njia ya mahali. Kwa njia ya nafsi Kristo ni mamoja na Mungu *tangu milele, sasa*, na atakuwa mamoja naye *kwa milele*. Isingaliwezekana kwa yeze kuacha kuwa hivi kamwe. Lakini ili-kuwa namna nyingine kwa maneno ya mahali pake. Tangu milele Kristo alikuwa mamoja na Baba yake, akifurahishe na utukufu wa mbingu. Lakini **hakuona** mahali hapa kuwa kitu cha kushikamana nacho na nguvu. Akiona dunia hii iliyojaa na watu wenye hitaji la ukombozi, alikuwa tayari kuacha mahali pake pamoja na **Mungu** — hali njema na furaha za mbingu. **Hakuona** maneno yale kuwa kitu cha kushikamana nacho na nguvu na kwa milele.

Hivi alikuwa tayari kufikia dunia hii na kuvumilia mabishano makubwa ya wenye zambi juu yake (Ebr.12:3). Mungu Baba hakutemewa mate wala kupigwa wala kusulibishwa. Kwa maneno haya Baba alikuwa mkubwa kupita Mwana. Yesu alisema neno hili wazi ndani ya Yoane 14:28: “Kama mungalinipenda, mungalifurahi, kwa sababu ninakwenda kwa Baba; kwa maana Baba yangu ni mkubwa kuliko mimi.” Ingalipasa wanafunzi kufurahi kusikia kwamba alikuwa akikwenda kwake mbinguni. Wakati alipokuwa duniani alitendewa jeuri na kukataliwa. Kwa maneno haya alikuwa chini kupita Baba

yake, na Baba yake alikuwa mkubwa kupita yeye. Lakini wakati aliporudi mbinguni, alikuwa tena sawasawa na Baba katika *hali zake* pamoja na *nafsi yake*.

2:7 Hivi alijifanya mwenyewe kuwa hana utukufu. Inawezekana kutafsiri neno hili: “Alijifanya kuwa tupu.” Basi tunauliza, “Alijifanya kuwa tupu kwa njia ya kuondosha nini?”

Inapasa kujibu ulizo hili na ange sana. Watu wengine wamesema kwamba ali-ondosha tabia yake ya uungu. Kwa mfano, wengine wanasema, wakati Bwana Yesu alipokuwa duniani hakujuu tena maneno yote, na hakuwa na uwezo wote. Wanasema hakuwa tena pahali pote kwa saa moja. Wanasema kwamba na kutaka kwake mwenyewe aliachaa kuwa na tabia hii ya uungu wakati alipofika duniani kama mtu. Wanasema alikuwa na vizuizo kama watu wote, aliweza kuanguka kwa mawazo, na alikubali mawazo na hadizi za watu walioishi kwa wakati alipokuwa duniani.

Mawazo haya yote tunakataa kabisa. Bwana Yesu hakuacha tabia yake ya Mungu hata kidogo wakati alipofika duniani.

Alikaa kujua maneno yote, na alikuwa pahali pote kwa saa moja, na alikuwa na uwezo wote.

Alijifanya tupu toka mahali pake pa umoja na Mungu na alifunika utukufu wake wa uungu ndani ya mwili wa mtu. Alibaki na utukufu wake wote, kwa maficho. Utukufu huu ulionekana mara moja moja, kama wakati alipogeuzwa sura mlimani. Alikuwa na tabia ya Mungu kwa kila dakika alipokuwa duniani.

Njia nzuri sana kueleza “Alijifanya tupu” ni maneno yanayofuata, ya kama **alitwaa namna ya mtumwa, akakuwa na mfano wa mtu.** Ni kusema alijifanya tupu kwa njia ya kujikamatia kitu asi-chokuwa nacho mbele kamwe, ndio utu. Hakuondosha uungu wake, lakini ali-

acha pahali pake mbinguni tu, kwa muda mfupi.

Kama angalikuwa mtu tu, neno hili lisengalikuwa kujifanya tupu. Hatujifanyi tupu kwa njia ya kuzaliwa duniani. Lakini kwa Mungu kugeuka Mtu ni kweli kujifanya tupu. Mungu tu aliweza kufanya hivi.

Akitwaa namna ya mtumwa. Tunaweza kujumlisha maneno ya kutwaa utu na maisha ya Mwokozi na masemo haya matamu ya Yoane 13:4: “Yesu akaweka mavazi yake kando; akatwaa kitambaa, akafunga kiuno chake.” Kitambaa hiki ni alama ya utumishi. Watumwa walitumika na kitambaa. Na Bwana Yesu, Mbarikiwa, alitumika na-cho kwa sababu hakuja kutumikiwa, lakini kutumikia, na kutoa uzima wake uwe ukombozi kwa watu wengi” (Mt. 20:28). Ni vizuri kwa sisi kukumbuka kwamba kulikuwa na ugomvi katikati ya waamini wa Filipi. Paulo aliwaonya kuwa na nia ya Kristo. Wakristo hawatakuwa na magomvi kama wakikubali kujinyenyekeza na kutumikia wengine, na kuishi maisha yao kama zabihu. *Si desturi kwa watu wale walio tayari kufa kwa pahali pa watu wengine kugombana nao.*

Kristo alikuwa tangu milele, lakini alifika duniani **kwa mfano wa mtu**, maana yake kama mtu kabisa. Yeye ni Mungu na Mtu vilevile. Ni siri kubwa kabisa. Hakuna mtu atakayeweza kuifahamu.

2:8 Kila sehemu ya shairi hili linaonyesha kuongezeka kwa aibu ya Mwana mpendwa wa Mungu. Alikuwa tayari kuacha utukufu wa mbingu! Alijifanya tupu! Alitwaa mfano wa mtumwa! Aligeuka Mtu! Lakini sasa tunasoma kwamba **alijinyenyekeza mwenyewe!** Alikuwa tayari kujinyenyekeza chini sana kuokoa nafsi zetu zenye hatia. Jina lake lenye utukufu libarikiwe kwa milele!

Alijinyenyekeza mwenyewe, aka-

kuwa mwenye kutii hata mauti. Ni neno la kutushangaza sana! Alitii, hata kama bei ya kutii ilikuwa mauti. Maana ya **mwenye kutii hata mauti** ni alitii hata mwisho. Kweli alikuwa mfanya biashara, aliyekwenda na kuuza yote aliyokuwa nayo, na kununua lulu moja ya bei ya damani (Matayo 13:46).

Ndiyo mauti ya msalaba. Mauti kwa njia ya kusulibishwa ilikuwa kufa kwa haya kubwa zaidi. Ingeweza kusawanishwa na kunyongwa, au kufishwa kwa nguvu ya umeme, vivyo hivyo – namna wauaji tu walivyouawa. Hii ndiyo namna ya **mauti** iliyowekwa kwa Mwenyeji mwema zaidi wa mbingu wakati alipofika hapa duniani. Hakuweza kufa kitandani, au kwa njia ya tukio mbaya. Ilikuwa lazima kwaye kufa na haya zaidi, ndiyo **mauti ya msalaba**.

2:9 Habari zinageuka kabisa ndani ya shairi hili. Ndani ya shairi 8 tulisoma juu ya maneno Bwana Yesu aliyofanya. Alichagua kujinyima mwenyewe. Hakujitafutia ukubwa na heshima. Alijinyeyekeza.

Lakini sasa tutawaza juu ya maneno *Mungu* aliyofanya. Mwokozi alijinyeyekeza, lakini **Mungu alimtukuza sana**. Hakujitafutia jina la heshima, lakini **Mungu amempa jina lililo juu ya kila jina**. Alipiga magoti yake kutumikia watu, na Mungu ameamuru kwa **kila goti kupigwa** mbele yake.

Mafundisho kwa Wafilipi – na kwa sisi, ni nini? Haifai kwa sisi kujitokuza wenyewe, lakini kuwa watumishi wa watu wengine, ili Mungu aweze kutukuza kwa wakati wa kuja.

Mungu alitokuza Kristo kwa njia ya kumfufua toka wafu, na kufungua mbingu kumpokea kwa mkono wake wa kuume mwenyewe. Na zaidi ya ile, **Mungu amempa jina lililo juu ya kila jina**.

Walimu wa Neno la Mungu wana mawazo mbalimbali juu ya **jina** hili.

Wengine wanasema ni *Yesu*, lililo na jina la *Yehova* ndani yake. Ndani ya Isaya 45:22, 23, kuna amri ya kwamba kila goti litapigwa mbele ya jina la Mungu (*Yehova*).

Wengine wanafikiri **jina lililo juu ya kila jina** linasema kwa mfano juu ya pahali palipo juu zaidi ulimwenguni, pahali pa enzi kubwa. Maelezo haya mawili yanakubaliwa.

2:10 Mungu alipendezwa kabisa na kazi ya ukombozi wa Kristo hata aliamuru kwamba **kila goti litapigwa** mbele yake – la vitu vya **mbinguni, na vya duniani, na chini ya dunia**. Si kusema ya kwamba viumbe hivi vyote wataokolewa. Wale *wasiokubali* kupiga magoti yao sasa *watalazimishwa* kufanya hivi siku nytingine. Wale wasiopatanishwa na Mungu kwa wakati wa muda wa neema yake watatiishwa kwa wakati wa hukumu.

2:11 Kwa neema isiyo na kifani, Bwana Yesu alisafiri toka utukufu wa mbingu hata Betelehemu, Getesemané, na Kalvari. Mungu, badala yake, atamheshimu na heshima kubwa toka watu wote, na ukubali wao kwamba ye ye ni Bwana. Wale amba waliokataa kwamba ye ye ni Bwana, watakubali upumbavu wao siku nytingine, ya kwamba walianguka kabisa, na ya kwamba Yesu wa Nazareti ni kweli Bwana wa utukufu.

Mbele ya kuacha mashairi haya mazuri sana juu ya Bwana Yesu na kazi yake, vizuri tuseme tena ya kwamba habari hizi ziliandikwa kwa sababu ya neno gumu dogo ndani ya kanisa kwa Filipi. Paulo hakukusudi kuandika juu ya Bwana Yesu, lakini kujaribu kuonya waamini juu ya roho yao kujitafutia wenyewe faida, na juu ya roho ya wafuasi kanisani. Walihitaji kuwa na nia ya Kristo kwa kutengeneza maneno haya. Paulo aliingiza Bwana ndani ya kila neno, kila tukio.

2:12 Nyuma ya kuandika juu ya mfano wa Kristo na maneno mazuri

sana, Paulo alikuwa tayari sasa kuonyesha maana ya mafundisho haya kwa wamini. Waamini **walikuwa wametii** Paulo **siku zote** wakati alipokuwa pamoja nao. Iliwapasa **kukaa kufanya hivi** sasa vilevile wakati asipokuwa pamoja nao, na **kutimiza wokovu wao kwa kuogopa na kutetemeka**.

Hili ni shairi lingine lililo ngumu kufahamu, na maelezo mbalimbali ya watu si sawa. Neno la kwanza ambalo inatupasa kufahamu ni kwamba watu hawawesi kujipatia wokovu kwa njia ya kutenda kazi njema. Paulo alifundisha tena na tena ndani ya maandiko yake ya kwamba hatupati wokovu kwa njia ya matendo mema, lakini kwa njia ya kuamini Bwana Yesu Kristo. Maana yake nini?

1. Labda maana yake ni ya kwamba inatupasa **kutimiza** wokovu amba Mungu anakwisha kuweka ndani yetu. Mungu ametupa sisi uzima wa milele kama zawadi. Sasa inatupasa sisi kutumika na zawadi hii kwa njia ya kuishi maisha matakatifu.

2. Labda **wokovu** hapa ni njia kuteengeneza neno lao gumu. Walikuwa na magomvi na mashindano. Mtume amewaonyeshea namna gani kutengeneza maneno haya. Sasa iliwapasa kuteengeneza magumu haya kwa njia ya kuwa na nia ya Kristo, **na kutimiza wokovu wao**.

Wokovu amba tunasoma juu yake hapa si wokovu wa nafsi, lakini ni kuponyeshwa toka mitego ambayo inataka kuzuiza Mkristo asifanye mapenzi ya Mungu. Vine anasema ni kuponyeshwa toka maovu yote ya wakati wa sasa.

Wokovu una maana mbalimbali ndani ya Agano Jipy. Tuliona mbele ya kwamba maana yake kwa 1:19 ni kuponyeshwa toka gereza. Ndani ya 1:28 ni wokovu wetu kwa mwisho wa maisha yetu ya miili, toka pahali hapa pa zambi. Tunaweza kufahamu maana ya neno hili kwa pahali fulani, kwa njia ya kusoma

mashairi ambayo yanalitangulia na kulfuata. Tunaamini ya kwamba katika shairi hili maana ya **wokovu** ni kuteengeneza maneno yaliyochokoza Wafilipi, ndiyo magomvi yao.

2:13 Paulo aliwakumbusha kwamba wanaweza kutimiza wokovu wao kwa sababu **ni Mungu anayetenda kazi ndani** yao **kutaka na kutenda**, kwa **kutimiza kusudi lake njema**. Ni kusema kwamba **ni Mungu** anayetia ndani yetu hamu au kutaka, kufanya mapenzi yake. Kisha **anatumika ndani** yetu na uwezo kutimiza hamu hii.

Hapa tena tunaona kuungana kwa yale yaliyo ya Mungu na ya mwanaadamu. Ndiyo, tunaitwa kutimiza wokovu wetu, lakini ni Mungu tu ambaye anatuwezesha kufanya hivi. Sharti sisi tufanye kazi ambayo inatupasa kufanya, na Mungu atafanya kazi yake. (Lakini maneno haya si juu ya usamehe wa zambi, wala juu ya kuzaliwa tena. Ukombozi ni kazi ya Mungu peke yake. Sisi tunaamini tu, na kupata faida yake.)

2:14 Wakati tunapofanya maneno ambayo yanapendenza Mungu, sharti tufanye hivi bila kunungunika wala kuuliza kwa sababu gani inatupasa kuyafanya, lakini tuyafanye na roho ya kushinda. Mara nyingi **manunguniko na mashindano** yanatangulia mambo mabaya kupita.

2:15 Kwa njia ya kuepuka manunguniko na mabishano, tunaweza kuwa **bila laumu wala udanganyifu**. Haiwezekani kushitaki mtu asiyie na laumu (ona Dan. 6:4). Inawezekana kwa mtu asiyie na **laumu** kufanya zambi, lakini anaomba usamehe kwa neno alilofanya, na roho safi, **bila udanganyifu**.

Ingepasa **wana wa Mungu** kuwa **bila kipaku katika kizazi cha jeuri na ubishi**. Wakiishi maisha bila kipaku, wana wa Mungu wataonekana wazi sana katika dunia hii ya giza. Paulo aliwasawanisha na **taa** katika giza la usiku. Ni kama taa inangaa kupita kwa kwa

kipimo cha giza la usiku. Wakristo ni **taa** au wenyewe kubeba taa. Hawawezi kufanya nuru, lakini wanaweza kurudisha nuru ya utukufu wa Bwana ili watu wengine waweze kuona Yesu ndani yao.

2:16 Mukishika neno la uzima. Kama taa tunangaa, lakini pamoja na ushuhuda wa maisha yetu inatupasa kushuhudia Kristo na sauti zetu vilevile.

Kama Wafilipi wakitimiza maneno haya, mtume anajua kwamba atawezeku kujisifu katika **siku ya Kristo**. Paulo hakutaka kwa watu kuokolewa tu, lakini alitaka kuleta kila mtu mtimilifu katika Kristo Yesu (Kol. 1:28).

Siku ya Kristo ni wakati wa kurudi kwa Kristo na wa hukumu ya utumishi wa kila mwamini (1:6, 10). Kama Wafilipi wakitumikia Bwana na uaminifu, neno hili litaonyesha wazi siku ile kwamba utumishi wa Paulo **haukuwa bure**.

4. Paulo, Timoteo na Epafroditon mifano Kristo (2:17-30)

Ndani ya mashairi yaliyotangulia, Paulo alionyesha Bwana Yesu kama mfano mzuri zaidi wa unyenyekevu. Lakini labda watu wengine wangejarihiwa kusema, "Lakini ye ye ni Mungu na sisi ni wanadamu tu." Hivi Paulo alitaja mifano ya watu watatu walioonesha nia ya Kristo – ye ye mwenyewe, Timoteo, na Epafroditon. Kama Kristo ni jua, halafu watu hawa watatu ni miezi, wakirudisha utukufu wa jua. Wao ni taa ndani ya dunia ya giza.

2:17 Mtume alitumika na mfano mzuri sana kueleza utumishi wa Wafilipi na wa utumishi wake mwenyewe. Alikopa mfano wa desturi ya Wayuda na ya wapagano vilevile waliomwanga **toleo la kinyweo** juu ya **zabihu** iliyotolewa kwa Mungu.

Alisema juu ya Wafilipi kama wenyewe kutoa zabihu. **Imani** yao ndiyo **zabihu**. Paulo mwenyewe ni **toleo la kinyweo**. Angefurahi **kumimiwa**, maana kuuawa, juu ya **zabihu na utumishi** wa **imani**

yao. **Atafurahi** kama neno hili likimpata.

2:18 Inapasa Wafilipi **kufurahi vivyo hivyo pamoja na** Paulo. Haifai wafikiri ingekuwa msiba mkubwa kama akiuawa, lakini wamtakie heri kwa sababu ya kuweza kwenda mbinguni na heshima kubwa.

2:19 Kufika saa ile Paulo alikuwa ameleta mifano ya wawili ambao walijitoa na mapendo kama zabihu – Bwana Yesu, na ye ye mwenyewe. Wao wawili walikuwa tayari kumimia maisha yao hata mauti. Kulikuwa na mifano ya watu wawili wengine ambao hawakujifikiri wenyewe – **Timoteo na Epafroditon**.

Mtume alikusudi **kutuma Timoteo** kwa Filipi nyuma kidogo ili **aweze kufarijiwa** na habari za hali toka kwao.

2:20 Katikati ya rafiki za Paulo, Timoteo alijitoa kupita wao wote kulinda hali ya roho ya Wafilipi. Paulo hakuwa na **mtu mwingine** mwenyeye nia moja naye, ambaye aliweza kutuma na salama rohoni kuwasaidia. Ilikuwa sifa kubwa kwa Timoteo aliyekuwa kijana tu!

2:21 Rafiki zake wengine walizama ndani ya **maneno yao wenyewe**. Walisumbushwa zaidi na mahitaji ya maisha yao hata hawakuwa na saa tena kwa **maneno ya Kristo Yesu**. Kuna mafundisho kwa sisi tunaoweka roho sana juu ya vitu vya dunia: nyumba, na frigo na motakaa, na television, na *vitu vingine?* (ona Luka 8:14.)

2:22 Timoteo alikuwa mwana wa mtume kwa njia ya imani, na alikuwa mwana mwaminifu sana kwa Paulo. **Walijua roho yake na sifa yake**, ya kwamba **kama mwana** alivyotumika pamoja na **baba yake**, vivyo hivyo Timoteo **alitumika pamoja na** Paulo ndani ya kazi ya kuhubiri **Habari Njema**.

2:23, 24 Kwa sababu uaminifu wa Timoteo ulikuwa umeonekana wazi, Paulo alitaraji **kumtuma** kwa Wafilipi

mara moja nyuma ya kusikia mwisho wa ombi lake kwa Kaisari, na kujuu nini itampata. Alitumaini ya kwamba ombi lake litakubaliwa, na ya kwamba atafunguliwa ili aweze kufikia Wafilipi tena.

2:25 Halafu tunaona nia ya Kristo ndani ya **Epafradito**. Hatujui kabisa kwamba ni mtu aliyeitwa Epafra ndani ya Wakolosayi 4:12. Epafroditu alikuwa mtu wa Filipi na alikuwa mjambe wa kanisa pale.

Paulo alisema kwamba yeye ni: (1) **ndugu yangu**; (2) **mtenda kazi pamoja** nami; (3) **askari pamoja** nami. Majina haya yanasema juu ya mapendo, kazi ya nguvu, na vita. Epafroditu alikuwa mtu aliyeweza kutumika pamoja na watu wengine vizuri. Hili ni neno linalohitajiwa kabisa kwa maisha na utumishi wa Wakristo. Kuna watu wengine wanaotumika peke yao na kufanya maneno yote namna wao wanavyotaka. Ni nguvu kupita kutumika pamoja na watu wengine, na kukubali namna watu hawa wanavyotaka kufanya maneno, na kuyenyekaa kutaka kwao. Tuwe **watenda kazi pamoja** na **askari pamoja** na waamini wengine!

Zaidi ya maneno haya, Paulo alisema juu ya Epafroditu kama **mtume wenu na mtumishi wa mahitaji yangu**. Maneno haya yanatuonyesha kwamba alikuwa tayari kufanya kazi ya mtumishi. Kwa wakati wa sasa watu wengine wanataka kutumika tu kazi ya kupendeza na inayoonekana mbele ya watu. Ingetupasa kuleta asante kwa watu walio tayari kufanya kazi ya kila siku na roho ya kimya na bila kuonekana! Kwa njia ya kutumika na nguvu, Epafroditu alijinyenyekeza. Lakini Mungu alimtukiza kwa njia ya kutaja kazi yake aminifu ndani ya sura 2 ya barua hii kwa Wafilipi, pahali watu wote watakapo-weza kusoma juu yake kwa vizazi vya kuja.

2:26 Watakatifu walikuwa wame-

tuma Epafroditu kusaidia Paulo – safari ndefu sana ya karibu 1200 km. Mjumbe wao mwaminifu alipata **ugonjwa** kwa sababu ya safari ile, na alikuwa karibu kufa. Neno hili lilimsumbusha sana – si ugonjwa wenyewe, lakini aliogopa waamini watasikia habari hizi. Kama wakizisikia, watajilaumu kwa sababu walikuwa wamemtuma kwa safari ile na kumhatarisha. Kweli Epafroditu hakuwa mtu ambaye alijifikiri mwenyewe.

Wakristo wengi wanafungwa na desturi ya kupasha habari zote za ugonjwa wao, au kama mganga aliwapasua. Mara nyingi hii ni alama ya zambi ya kujifikiri na kujihurumia na kujionyesha wenyewe kwa watu.

2:27 Ndiyo, Epafroditu alikuwa na ugonjwa kweli **karibu na kufa, lakini Mungu alimhurumia**. Mashairi haya yanaleta mafundisho juu ya namna Mungu anavyoponyesha watu.

1. Kwanza, ugonjwa si tunda la zambi kila mara. Epafroditu alipata ugonjwa kwa sababu ya kutimiza kazi yake na uaminifu (ona sh. 30), “... **kwa ajili ya kazi ya Kristo alikuwa karibu na kufa.**”

2. Neno la pili tunaloona ni ya kwamba si kila mara kutaka kwa Mungu kuponyesha mgonjwa mara moja, na kwa njia ya ajabu. Ni kwamba Epafroditu alikuwa mgonjwa kwa muda mrefu, na aliponyeshwa polepole (ona vilevile 2 Tim. 4:20; 3 Yn. 2).

3. Neno la tatu tunalojifunza ni ya kwamba tunaponyeshwa kwa rehema ya Mungu tu; si neno lililo haki yetu tunayoweza kuomba kwake kwa nguvu.

Paulo aliongeza kwamba **Mungu hakuhurumia** Epafroditu tu, lakini alimhurumia yeye vilevile, asiwe **na huzuni juu ya huzuni**. Paulo alikuwa na huzuni kwa sababu ya kufungwa kwake, na kama Epafroditu angalikufa, Paulo angalipata huzuni nyingi kupita.

2:28 Lakini Epafroditu alikuwa ame-

pona vizuri sasa, hivi Paulo **alimtuma** tena kwao **na bidii**. Wafilipi **watafurahi** kwa ndugu yao mpenzi kuwa pamoja nao tena, na neno hili litapunguza huzuni ya Paulo vilevile.

2:29 Pamoja na **kupokea** Epafrodito na furaha, iliwapasa **kuheshimu** mtu huyu wa Mungu. Ni heshima na mapeendeleo makubwa **kutumikia Bwana**. Ingepasa waamini kutambua neno hili, hata kama ndugu mwenyewe ni mtu ambaye wanajua sana.

2:30 Kama Paulo alivyoandika mbele, ugonjwa wa Epafrodito ulikuwa tunda la kutumikia **Kristo** bila kuchoka. Neno hili ni faida kubwa kwa macho ya Bwana. Kutumikia Yesu hata kufa ni faida kupita kufa kwa sababu ya ugonjwa au tukio baya.

Maana ya “**ili atimize yaliyokosa katika utumishi wenu kwangu**” haiko kwamba Wafilipi hawakutunza Paulo vizuri, na ya kwamba Epafrodito alifanya kazi ambayo ilipasa Wafilipi kufanya. Wao wenyewe walikuwa wametuma Epafrodito karibu na Paulo kufanya kazi wasiyoweza kufanya kwa sababu mji wao ulikuwa mbali sana na Roma. Hakuwahamakia, lakini alisema tu kwamba Epafrodito, kama mjumbe wao, alifanya kazi Wafilipi wasiyoweza kufanya.

5. Maonyo juu ya walimu wa uwongo (3:1-3)

3:1 Paulo hakuwa karibu kumaliza barua yake wakati aliposema: “**Basi kwa kumaliza, ndugu zangu.**” Maana ya semo hili ni “Maneno yanayobaki ...” Alitumia semo hili tena ndani ya 4:8.

Aliwaonya **kufurahi katika Bwana**. Mkristo anaweza kuwa na furaha ya kweli katika **Bwana**, si neno kama hali yake ni nzuri au akiwa na taabu yo yote. Anaweza kuimba hata hivi kwa sababu yule ambaye anamsifu kwa nyimbo zake ni mbinguni. Hakuna neno linaloweza kupunguza furaha yake isipokuwa lina-

iba kwanza Mwokozi wake, ndilo neno lisilowezekana. Maumivu, huzuni, ugonjwa, umasikini, na msiba zinapunguza furaha yetu duniani. Lakini furaha ndani ya Kristo inashinda taabu hii yote ya maisha yetu ya sasa. Kwa sababu hii Paulo aliweza kutoa maonyo haya hata wakati alipokuwa gerezani. Vizuri tupokee na kutii maonyo ya mtu huyu wa Mungu!

Kuandika maneno haya tena kwa Wafilipi hakutaabisha Paulo kwa sababu alijua ilikuwa faida kwao. Lakini aliandika juu ya neno hili tena namna gani? Aliwaza juu ya wakati alipowaonya mbele **kufurahi katika Bwana**? Au juu ya mashairi yanayofuata pahali alipowaonya juu ya walimu wabaya? Tunafikiri sasa alifikiri juu ya walimu hawa wabaya. Mara tatu ndani ya shairi 2 alisema nao **kujiangalia**. Kufanya hivi **hakumtaabisha**, lakini kwao ilikuwa faida na kuwalinda.

3:2 Aliwaagiza kujiangalia **kwa imbwaa**, ... kwa wale **wanaotenda mabaya**, na kwa wale ambao **wanajikata wenyewe**. Tunawaza watu hawa namna tatu ni wanaume wa jamii moja – walimu wa uwongo waliojaribu kuingiza Wakristo chini ya sheria za dini ya Wayuda, na kufundisha kwamba haki inapatikana kwa njia ya kushika sheria na kawaida za dini.

Kwanza, walikuwa **imbwa**. Ndani ya maandiko ya Biblia **imbwa** zilikuwa nyama wachafu. Wayuda waliita Mataifa imbwaa. Katika inchi za mashariki imbwaa zilikuwa nyama zilizokosa kao, zisizofugwa na zilizokimbia pahali po pote zikijitafutia vyakula. Hapa Paulo alitumika na neno hili kwa walimu hawa wa uwongo waliojaribu kuchafua kanisa. Walikaa inje ya kanisa, wakijaribu kuisi kwa sheria na kawaida za dini. “Walikokota makombo wakati wangalipeweza kushiriki ndani ya karamu.”

Neno la pili, walikuwa **watenda mabaya**. Kwa njia ya kukiri kwamba

wao ni waamini wa kweli, walipata njia kuingia ndani ya ushirika wa Wakristo kueneza mafundisho yao maovu. Matunda ya kazi yao yalikuwa maovu tu.

Kisha Paulo aliwaita vilevile **wanao-jikata wenyewe**. Ni jina la kuzarau kuonyesha mawazo yao juu ya tohara. Bila shaka walifundisha na nguvu kwamba inapasa mtu kutahiriwa kwa kuweza kuokolewa. Lakini walisema juu ya kutahiriwa kwa mwili tu. Hawakuwaza juu ya maana ya roho. Tohara inasema juu ya mauti ya mwili. Maana yake ni ya kwamba haifai tukubali matendo maovu ya mwili. Lakini hata kama watu wale walisema na nguvu kwamba lazima watu watahiriwe, walifaruhusu kufanya matendo ya mwili. Hawakukubali miyoni mwao kwamba mwili wa zambi uliuawa wakati Kristo alipokufa msalabani. Paulo alikuwa akisema kwamba walikuwa wenyewe kukan mwili tu bila kufahamu tofauti ya kawaida hii ya dini na maana yake ya roho.

3:3 Lakini kuonyesha tofauti na watu wale, Paulo anasema kwamba **sisi** (waamini wa kweli) ni **wale wa tohara**, si wale waliozaliwa na wazazi Wayuda au waliotahiriwa mwilini. Sisi ni watu tynaofahamu kwamba mwili hauna faida, na mtu hawesi kufanya kitu kwa nguvu yake mwenyewe kupendeza Mungu. Halafu Paulo alionyesha alama tatu za wale wenyewe tohara ya kweli:

1. Wanaabudu Mungu kwa Roho. Ni kusema wanaabudu na roho ya kweli, si kwa njia ya ibada kwa dini tu. Mtu anayeabudu na roho ya kweli anaingia mbele ya Mungu kwa imani, na kumwanga mbele yake mapendo, sifa, kuabudu na ibada yake. Lakini kuabudu kwa nafsi tu ni kuwaza juu ya mapambo ya majengo na ya vitu ndani yao, kawaida za ibada, mavazi ya mapambo ya makuhani, na maneno yo yote yanayosaidia furaha ya nafsi.

2. Wenyewe tohara ya kweli wanafurahi

ndani ya Kristo Yesu peke yake. Hawajisifu ndani ya kazi ambazo waliweza kufanya wao wenyewe, malezi yao, au kwa sababu wanashiriki na uaminifu ndani ya ushirika mtakatifu.

3. Hawatumaini mwili. Hawafikiri wanaweza kuokolewa kwa njia ya kazi zao za mwili, wala kwamba wanaweza kulindwa na nguvu yao wenyewe nyuma ya kupata wokovu. Wanafahamu kwamba tabia waliyopokea toka Adamu ni ovu tu.

6. Paulo alihesabu uriti na utendaji wake bora wa mbele kuwa hasara kwa ajili ya Kristo (3:4-14)

3:4 Bila shaka Paulo alicheka kidogo rohoni mwake wakati alipowaza juu ya kujisifu kwa watu wale juu ya mapeendeleo na kazi zao za mwili. Kama wao waliweza kujisifu, yeye aliweza kujisifu **zaidi**. Ndani ya mashairi 4 na 5 alionyesha kwamba alibarikiwa zaidi na maendeleo ambayo watu walijisifu juu yao.

Ona ya kwamba alisema juu ya kujisifu juu ya wazazi (sh. 5a); juu ya usafi wa dini (sh. 5b); juu ya kazi yake (sh. 6a); na juu ya kushika sheria (sh. 6b).

3:5 Tunaona hapa maendeleo ya Paulo kwa njia ya mwili:

Alitahiriwa siku ya nane – alizaliwa mtu wa Israeli, hakuwa Mwisimaeli, na hakugeuka Myuda nyuma ya kuzaliwa.

wa kabila la Benyamina – ndilo kabila lililoheshimiwa kuwa kiongozi kwa utawala (Amu. 5:14); mfalme wa kwanza wa Israeli alikuwa mtu wa kabila hili.

Mwebrania wa Waebriani – alikuwa mmoja wa sehemu ya taifa waliokaa kusema na lugha yao ya asili na kushika desturi zao za zamani.

kwa maneno ya sheria, Mfarisayo – Wafarisayo walishika sheria sana, lakini Wasadukayo walikuwa wameacha mafundisho juu ya ufufuko.

3:6 kwa maneno ya bidii, nikitesa kanisa – Paulo aliamini kabisa ya

kwamba alikuwa akitumikia Mungu wakati alipojaribu kuharibu “jamii” ya Wakristo. Alifikiri wao ni adui za dini yake mwenyewe, na ya kwamba kwa sababu hii ilimpasa kuwaharibu.

kwa maneno ya haki iliyo katika sheria, pasipo kosa – maana ya semo hili haiko kwamba alitimiza kila agizo la sheria bila kuanguka. Yeye mwenyewe alikiri katika Waroma 7:9, 10 kwamba alikuwa na zambi. Wakati aliposema alikuwa pasipo kosa, maana yake ilikuwa kwamba hakuwa na **hatia**, si kwamba alikuwa bila zambi. Tunawaza ya kuwa wakati Paulo alipoasi sehemu yo yote ya sheria, alitoa vilevile sadaka iliyohitajiwa kwa usamehe wa zambi ile. Aliweka roho sana kutii magizo yote ya dini ya Wayuda.

Hivi, kwa maneno ya kuzaliwa kwake, majina ya wazazi wake, usafi wa mafundisho wake, bidii, na haki ya maisha yake, Saulo wa Tarso alikuwa mtu wa kujulikana sana.

3:7 Lakini sasa mtume alikataa maneno haya yote. Alikuwa ametaja maneno yaliyokuwa **faida** kwake mbele, lakini wakati alipoyasawanisha sasa na hazina aliopata ndani ya **Kristo**, alifahamu kwamba yalikuwa bure tu. **Aliyahesabu kuwa hasara kwa ajili ya Kristo.**

Kama Paulo angalitegemea maneno yale, asingaliweza kuokolewa. Lakini nyuma ya kuokolewa kwake, maneno haya yote yalikuwa bure kwake, kwa sababu alikuwa ameona utukufu wa Bwana, na maneno mazuri mengine yote yalikuwa kama si kitu wakati yaliposawanishwa naye.

3:8 Wakati Paulo alipofikia Kristo kupokea wokovu, alihesabu **maneno yote** kuwa hasara wakati yaliposawanishwa na **uzuri wa kujua Kristo Yesu, Bwana** wake.

Hakujisifu tena juu ya uzazi wake, taifa lake, elimu yake, sifa kwa maarifa yake, dini yake, maneno yo yote ambayo

ye ye alikwisha kufanya. Aliacha **maneno haya yote na kuyahesabu kama mavi ili apate Kristo.**

Shairi hili na lile linalofuata yanandiwa sawasawa maneno haya yalikuwa yaktikea kwa saa ile ile. Sivyo. Paulo alikuwa akiandika juu ya maneno yaliyotokea mbele kwa wakati alipo-okolewa. Kwa **kupata Kristo** alilazimishwa kuacha maneno yale ambayo alifundishwa kupenda sana. Kwa kupata Kristo, ilimpasa kuachana na dini ya mama yake, uriti wa baba yake, na maarifa yake yenyewe.

Na alifanya hivi! Alijitenga na dini ya Wayuda kabisa akijua watu hawawezi kupata wokovu kwa njia yake. Kwa sababu alifanya hivi, ndugu zake walimwondoshea uriti wake, alikataliwa na rafiki zake, na kuteswa na watu wa inchi yake. **Alipata hasara ya maneno yote** wakati alipogeuka Mkristo.

Kwa sababu ya namna shairi hili lili-voandikwa, tungeweza kufikiri kwamba Paulo alijaribu **kupata Kristo** hata kwa wakati ule. Lakini alikwisha kupata Kristo mbele saa alipokiri ya kuwa yeye ni Bwana na Mwokozi wake. Na mawazo yake juu ya Kristo hayakugeuka – hata saa ile alihesabu maneno yote **kama mavi** wakati yaliposawanishwa na faida ya kujua Bwana Yesu Kristo. Hamu kubwa ya roho ya Paulo ilikuwa aweze kupata Kristo, si zahabu, wala feza, wala heshima kwa njia ya kufuata dini.

3:9 Na nioneokane ndani yake. Aliangalia nyuma tena kwa siku ile wakati asipokuwa Mkristo bado na ilipompasa kuchagua kama atafanya nini. Alikuwa tayari kuacha kujaribu kujiooka mwenyewe kwa njia ya matendo yake, na kuamini Kristo tu? Ndiyo, alikuwa amechagua kuacha maneno yote ili aweze kuonekana ndani ya Kristo. Dakika alipoamini Bwana Yesu, alisimama na hali mpya mbele ya Mungu. Hakuonekana tena kama mwana wa

Adamu, mwenye zambi, lakini alionekana *ndani ya Kristo*, akifurahi ndani ya kibali chote cha Bwana Yesu mbele ya Mungu Baba.

Alikuwa amekataa haki yake mwenyewe inayopatikana kwa njia ya kushika sheria, na alikuwa amechagua **haki ya Mungu** ambayo inaletwa kwa kila mtu anayepokea Mwokozi. Tunasoma juu ya **haki** hapa kama vazi au kifuniko. Mtu anahitaji haki ili Mungu aweze kukubali kwaye kusimama mbele yake. Lakini mtu hawesi kuzaa haki ile. Hivi Mungu, mwenye neema, anatoa *haki yake mwenyewe* kwa wale wanapokea Mwana wake kuwa Bwana na Mwokozi. “(Mungu) alifanya (Kristo) asiyejua zambi *kuwa* zambi kwa ajili yetu ili sisi tuwe haki ya Mungu katika yeye” (2 Kor. 5:21).

Tukumbushwe tena ya kwamba mashairi 8 na 9 hayafundishi kwamba Paulo hakupokea kwanza haki ya Mungu. Sivyo. Alipokea wakati alipozaliwa tena kwa njia inayokwenda Damasiki. Mashairi haya yanaonyesha kwamba matunda ya tukio hili yaliendelea kufika hata wakati Paulo alipokuwa akiandika barua hii. Alikaa kuhesabu Kristo kuwa na faida nyingi kupita maneno yo yote ambayo aliacha kwa ajili yake.

3:10 Watu wengi wanasema kwamba **mateso, kufa, na ufufuko** ndani ya shairi hili ni mifano ya maneno tunayosikia rohoni, kama maumivu rohoni, kujaribu kujikana mwenyewe, na kuishi uzima wa ufufuko, vivi hivi. Lakini sisi tunafikiri maneno haya si mifano. Ni maneno ya hakika. Paulo alisema kwamba anataka kuishi namna Kristo alivyoishi. Yesu aliteswa? Paulo alitaka kuteswa vilevile. Yesu alikufa? Halafu Paulo alitaka kuuawa ndani ya utumishi wake kwa Kristo. Yesu alifufuliwa toka wafu? Paulo alitaka kufufuliwa vilevile. Alifahamu kwamba mtumishi si juu kupita Bwana wake. Hivi alitaka kufuata Kristo ndani ya

mateso, mauti, na ufufuko wake. Hasemi kwamba inapasa watu wote kufikiri kama yeye, lakini kwa yeye njia hii ilikuwa njia ya lazima.

Ili nimjue yeye. Maana ya **kumjua yeye** ni kujuana naye karibu karibu ndani ya matukio madogo ya kila siku ili mtume mwenyewe ageuke kufanana na Kristo kupita. Alitaka uzima wa Kristo kuonekana ndani yake.

Na uwezo wa ufufuko wake. Uwezo uliofufua Bwana Yesu toka wafu ni uwezo mkubwa zaidi ulioonekana ulimwenguni (Efe. 1:19, 20). Ni kama majeshi maovu yote ya mbingu yalifungana pamoja kuzuiza mwili wake usitoke kaburi. Uwezo mkubwa sana wa Mungu ulishinda jeshi lile la Shetani kwa njia ya kufufua Bwana Yesu toka wafu siku ya tatu. **Uwezo** ule ule ni tayari kwa waamini wote (Efe. 1:19), watumike nao kwa imani. Paulo alitaka sana kwa uwezo huu kuonekana ndani ya maisha na ushuhuda wake.

Na ushirika wa mateso yake. Mtu anahitaji uwezo toka Mungu kumwezesha kuvumilia mateso kwa Kristo. Kwa sababu hii tunasoma juu ya **uwezo wa ufufuko wake** mbele ya **ushirika wa mateso yake**.

Ndani ya maisha ya Bwana, mateso yalitangulia ufufuko. Lazima iwe vivyo hivyo ndani ya maisha ya Paulo. Sharti ashiriki ndani ya mateso ya Kristo. Alifahamu kwamba hakuna upatanisho kwa watu ndani ya mateso yake yenye, lakini alijua vilevile kwamba haikuwa taratibu kwa yeye kuishi na anasa ndani ya dunia pahali Bwana wake alipokataliwa, alipopigwa mijeledi, na kusulibishwa.

Nikifananishwa na kufa kwake. Kama tulivyosema mbele, watu wengi wanasema maana ya maneno haya ni ya kwamba Paulo alitaka kuishi maisha yanayosulibishwa, kujihesabu mfu kwa zambi, mambo ambayo yalimpendeza mwenyewe, na maneno ya dunia. Elezo

hili ni zuri lakini ni zaifu. Maneno haya yana maana kubwa zaidi. Paulo alitaka na roho yake yote kuwa mfuata wa Yule aliyekufa juu ya msalaba wa Kalvari. Zaidi ya ile, aliona na macho yake kufa kwa mkristo wa kwanza wa kanisa kwa sababu ya imani yake, na yeze mwenyewe alisaidia ndani ya kuuawa kwake! Tunaamini ya kwamba Paulo alitaka sana kutoa maisha yake vivyo hivyo. Labda angalipata haya kukutana na Stefano mbinguni kama angalifika pale kwa njia nyininge bila kuuawa kwa imani yake. Jowett alifikiri vivyo hivyo:

Wakristo wengi wanakubali kutoa kwa Kristo vitu ambavyo hawahitaji wao wenyewe, na kama wakiweza kufanya hivi bila kutoa uzima wao. Lakini wanajificha kama ikiwapasa kujitoa wenyewe.

Lakini mtume Paulo alitazamia na furaha kuweza kufanya hivi. Alikuwa na haya juu ya kazi yake ndogo ndani ya ufalme. Alikuwa na hamu kumwanga damu yake, kama ikihitajiwa!⁷ *Adapté*

Hudson Taylor aliandika maneno namna hii vilevile:

Inatupasa sisi kujitoa *wenyewe* kwa uzima wa dunia. ... Kwa kuweza kuzaa matunda tunahitaji kubeba msalaba. "Kama punza ya ngano isipoanguka kwa udongo na kufa, inakaa peke yake." Tunajua namna gani Bwana Yesu aligeuka kuwa mwenye kuzaa matunda – si kwa njia ya kubeba tu msalaba wake, lakini kwa njia ya kufa juu yake. Sisi tunashiriki naye ndani ya neno hili? Hakuna Wakristo wawili – Kristo mmoja mpole ambaye hajisumbushi, kwa Wakristo wanaoishi namna hii, na Kristo mwininge anayeteswa na kujisumbusha sana, kwa waamini wenyewe roho ya namna nyininge. Kuna Kristo mmoja tu. Sisi ni tayari kukaa ndani yake na kuzaa matunda?⁸

3:11 Hapa tena watu wana maelezo

mbalimbali. Tuone mengine ya maelezo haya:

1. Paulo hakujua kabisa kama atafufuliwa toka wafu, hivi alisumbuka sana aweze kushiriki ndani ya ufufuko. Elezo hili haliwezekani! Paulo alifundisha tena na tena ya kwamba ufufuko ni kwa njia ya neema, si kwa njia ya matendo ya watu. Zaidi ya ile, alisema wazi ya kwamba yeze mwenyewe atashiriki ndani ya ufufuko (2 Kor. 5:1-8).

2. Paulo hakusema juu ya ufufuko wa mwili, lakini juu ya hamu yake kuishi maisha ya ufufuko wakati yeze ni kwanza duniani. Labda hili ni elezo la zaidi ya walimu.

3. Paulo alisema juu ya ufufuko wa mwili, lakini hakuwa na shaka ya kwamba atashiriki ndani yake. Alisema hakusumbuka kwamba labda atapata mateso mbele ya kufikia ufufuko. Alikuwa tayari kuvumilia taabu na mateso makubwa, kama neno hili likihitajiwa ndani ya muda wa sasa kufika saa ya ufufuko. Maana ya "**kwa njia yo yote**" haiko kwamba alikuwa na shaka (ona Mdo. 27:12; Rom. 1:10; 11:14), lakini kwamba lilikuwa neno alilotaka sana, au kwamba alifikiri itampasa kulipa bei kubwa kwa kulipata.

Tunakubali elezo hili la tatu. Mtume alitaka kufananishwa na Kristo. Kristo alikuwa ameteswa, kufa, na kufufuliwa toka wafu, na haya yalikuwa maneno Paulo aliyotaka kwa maisha yake mwenyewe. Tunaogopa ya kwamba mapeendo yetu kwa maisha ya anasa yanatufichia mara nyininge ukali wa magizo ya Mungu ndani ya mashairi haya. Ingepasa kuyapokea namna yanavyo-andikwa – isipokuwa baki la Biblia linayakana.

Mbele ya kuacha shairi hili, sharti tuone ya kwamba Paulo alisema juu ya **ufufuko toka wafu**. Si ufufuko wa wafu wote. Watu wengine watafufuliwa kwa **ufufuko** huu, lakini wengine watabaki ndani ya makaburi. Kwa njia ya 1 Tesa-

lonika 4:13-18 na 1 Wakorinto 15:51-57 tunajua kwamba waamini watafufuliwa wakati Kristo atakapokuja (wengine watafufuliwa kwa wakati atakapo-wapeleka mbingini, na wengine kwa mwisho wa mateso makubwa), lakini wafu wote wengine hawatafufuliwa kufika nyuma ya utawala wa Kristo duni-ani kwa miaka elfu moja; ona Ufu. 20:5.

3:12 Mtume hakufikiri kwamba alikuwa **amekwisha kukamilishwa**. **Ukamilisho** huu si ufufuko amba tulisoma juu yake ndani ya shairi 11, lakini ni kufananishwa na Kristo. Paulo hakufikiri iliwezekana kufikia hali ya kutokuwa na zambi, na bila kuhitaji kuendelea mbele.

Hivi alikaza mwendo ili kusudi la Bwana Yesu kwa wokovu wake liweze kutimizwa ndani ya maisha yake. **Kristo Yesu** alikuwa ameshika Paulo kwa njia ya Damasiki. Walikutana kwa sababu gani siku ile yenye maana sana? Ili kuanza siku ile Paulo aweze kuwa mfano mwema wa Mkristo kwa njia yake Mungu aliweza kuonyesha kazi Kristo anayoweza kufanya ndani ya maisha ya mtu. Paulo hakufananishwa bado kabisa na Kristo, na aliweka roho sana ili kazi hii ya neema ya Mungu iweze kuendelea na kuongezeka ndani ya maisha yake.

3:13 Mtu huyu (ndiye Paulo) aliye-kwisha kujifunza kufurahi na vitu vyo vyote vya dunia alivyokuwa navyo (4:11) hakuweza kamwe kufurahi na kipimo cha hali ya roho yake. Basi alifanya nini?

Ninafanya neno moja. Alikuwa mtu mwenye kusudi moja tu. Aliweka roho juu ya neno moja tu. Kwa njia hii alifanana na Daudi, aliyesema, "Kitu ki-moja niliomba na Bwana..."

Nikisahau maneno yaliyo nyuma hayakuwa zambi na makosa yake tu, lakini vilevile maneno mazuri aliye-weza kufanya mbele, na hata kushinda kwake kwa maneno ya roho ambayo aliandika juu yao mbele.

Na nikijinyosha kwa maneno yaliyo mbele, ndiyo mapendeleo na kazi ya Mkristo, kama kuabudu, utumishi, na kukua kupita kufananishwa na Kristo.

3:14 Paulo alijisawanisha na mshindani ndani ya shindano la mbio, anaye-kaza mwendo hata **afikie mwisho wa zawabu ya mwito mkubwa wa Mungu katika Kristo Yesu**.

Mwisho ni kamba inayoonyesha mwisho wa shindalo. Mshindaji anapewa **zawabu**. Ndani ya shairi hili mwisho ni mwisho wa uzima, au labda ni kiti cha hukumu cha Kristo. **Zawabu** ndiyo taji ya haki Paulo aliyosawanisha pahali pengine na zawabu kwa wale walioshindana kuonekana vizuri (2 Tim. 4:7, 8).

Mwito mkubwa wa Mungu katika Kristo Yesu ni maneno yote Mungu aliyokusudi wakati alipotuokoa. Ni wokovu wetu, kufananishwa na Kristo, kuwa wariti pamoja naye, kao mbinguni, na baraka nyingi nyingine za roho.

7. Maonyo kuiga mwenendo mta-katifu wa Paulo (3:15-21)

3:15 Ingepasa wale walio **watimilifu** kuwa tayari, kama Paulo, kuteswa na kufa kwa Kristo, na kujaribu sana kufananishwa na Bwana Yesu. Watu wengine wanafikiri mawazo namna hii ni nguvu sana, na yanapita kadiri na kiasi. Lakini mtume alisema kwamba wale walio watimilifu watakubali kwamba hii ni njia ya pekee kuishi kwa Yule aliye-mwanga damu yake kwa Kalvari kwa ajili yao.

Kama mukifikiri maneno mengine katika neno lo lote, Mungu atawa-funulia ninyi hili vilevile. Paulo alifa-hamu kwamba si watu wote watakubali mawazo haya magumu. Lakini aliamini kwamba mtu akiwa tayari kujuu kweli ya neno hili, **Mungu atafunua** kwake. Hatuna uwezo katika ukristo wetu kwa wakati wa sasa kwa sababu hatutaki kujuu kweli, na hatuko tayari kutii maagizo magumu ya Kristo.

Mungu ni tayari kuonyesha kweli kwa wale walio tayari kuipokea na kuitii.

3:16 Halafu Paulo aliongeza ya kwamba kufika wakati ule, inatupasa kuishi tukitii nuru ambayo Bwana ametupa sisi. Haifai tukae bure tu kufika wakati tunapojuishwa nini inapasa sisi Wakristo kufanya. Wakati tunapongojea Bwana kutufunulia maana ya msalaba kwa maisha yetu, inatupasa kutii **kipimo** gani cha kweli tunayokwisha kupokea.

3:17 Halafu Paulo alionya Wafilipi kumfuata au kumwiga. Ni sifa kwa yeze kuweza kusema maneno namna hii juu ya maisha yake mwenyewe ambayo yalikuwa mfano mzuri kwa waamini. Mara nyingine tunasikia watu wakisema kama kwa michezo, “Fanya maneno ninayosema, si maneno ninayofanya.” Mtume hakusema hivi! Aliweza kusema juu ya maisha yake mwenyewe kama mfano mwema wa kujitoa na roho yote kwa Kristo na kwa kazi yake.

Lehman Strauss alisema:

Paulo alifikiri juu yake mwenyewe kama mtu aliyeokea rehema ya Mungu ili aweze kuwa “mfano.” Hivi kusudi la maisha yake yote, tangu alipookolewa, lilikuwa kuonyesha mfano wa namna Mkristo anavyofaa kutenda na kuishi. Mungu aliokoa Paulo ili aweze kuonyesha kwa njia ya mfano wa wokovu wake ya kwamba kazi ambayo Kristo aliyea kwa yeze anaweza, na anataka kufanya kwa wengine vilevile. Na Bwana aliturehemu sisi kwa kusudi hili vilevile. Ninaamini alituokoa tuwe mfano kwa waamini wote kwa wakati wa kuja. Basi, tuko kweli mifano mizuri ya watu waliokwisha kuokolewa kwa njia ya neema yake? Tunaomba iwe hivi!⁹

Na muwatazame wao wanaotembea kwa kufuata mfano ambao tuliwapa ninyi. Alisema hapa juu ya wengine walioishi kama yeze.

3:18 Ndani ya shairi 17 alionyesha kama ikipasa waamini kufuata watu *gani*, lakini shairi 18 linaonyesha kama kuna watu wengine ambao *haifai* wafuate. Hataji kama walikuwa watu *gani*. Labda walikuwa walimu wa uwongo wa dini ya Wayuda walijotajwa ndani ya shairi 2. Au labda walikuwa walimu waliookiri wao ni Wakristo, na waliosema neema ya Mungu iliwapa ruhusa kufanya zambi.

Paulo alionya watakatifu mbele juu ya watu hawa, na alifanya hivi tena sasa, pamoja na **machozi**. Kwa sababu gani alitoa machozi pamoja na mashitaki haya ya nguvu? Kwa sababu ya uhari-bifu watu hawa walioleta kwa makanisa ya Mungu. Kwa sababu ya maisha ya watu waliyoharibu. Kwa sababu wali-laumu jina la Kristo. Kwa sababu walikuwa wakificha maana ya kweli ya msalaba. Ndiyo, lakini alitoa machozi vilevile kwa sababu mwenye mapendo ya kweli anatoa machozi hata wakati anaposhitaki **adui za msalaba wa Kristo**, namna Bwana Yesu alivyotoa machozi juu ya Yerusalem, mji wa kiuaji.

3:19 Mwisho wa watu hawa utakuwa uhari-bifu. Si kusema wataangamizwa kabisa, lakini kwamba watahukumiwa kwa milele katika ziwa la moto.

Mungu wao ulikuwa **tumbo lao**. Matendo yao yote, hata kwa utumishi wa dini, yalikuwa kununua vyakula (na labda vinyweo vilevile) kupendeza njaa ya miili yao.

Utukufu wao ulikuwa **haya yao**. Walijisifu juu ya maneno ambayo ingaliwapasa kuwa na haya juu yao – utupu wao na matendo yao maovu.

Walifikiri **maneno ya dunia**. Walikeka roho zaidi juu ya vyakula, mavazi, heshima, raha na anasa. Mawazo juu ya milele na mbingu hayakuwazuiza wasijipendeze na uchafu wa dunia hii. Ni kama walifikiri watacaa duniani kwa milele.

3:20 Halafu mtume alisawanisha maisha yao na nia ya mwamini wa kweli, mwenye nia ya mbingu.

Wakati barua hii ilipoandikwa, Filipi ultawaliwa na ufalme wa Roma (Mdo. 16:12). Wafilipi walikuwa wenyeji wa Roma, na walibarikiwa na ulinzi na mapendeleo yake. Lakini walikuwa wenyeji wa mji na serikali yao vilevile. Akikumbuka maneno haya, mtume alikumbusha waamini kwamba wao ni **wenyeji wa mbingu**.

Lakini Wakristo ni wenyeji wa inchi za dunia vilevile. Mashairi mengine ndani ya Biblia yanafundisha wazi kwamba inatupasa kutii serikali za inchi yetu kwani zimewekwa na Mungu (Rom. 13:1-7). Lazima waamini watii serikali ndani ya maneno yote ila yale yanayokatazwa wazi na Mungu. Hivi ili-pasa waamini kutii serikali ya mji pahali walipokaa, na mfalme wa Roma vilevile. Waamini wanapaswa kutii serikali za dunia, lakini zaidi utii wao ni kwa Bwana mbinguni.

Pamoja na kuwa wenyeji wa mbingu, **tunangojea Mwokozi kutoka pale na hamu kubwa**.

3:21 Wakati Bwana Yesu atakapokuja toka mbingu, atageuza miili yetu. Mwili wa mtu hauna haya. Unageuka na kupata haya wakati tunapoutumia kwa kazi mbaya.

Lakini ni mwili wa unyenyekevu. Unapata vikunjo vya ngozi, alama za vilonda, za maumivu, ugonjwa, uzee, na mauti. Unaweka mpaka kwa maneno tunayoweza kufanya!

Bwana **ataubadilisha** kuwa mwili wa utukufu. Hatujui maana nzima ya neno hili. Mwili ule hautaoza wala kufa, wala kutiwa mpaka kwa njia ya saa au maneno mengine ya dunia. Utakuwa mwili unaofaa kabisa kwa kuweza kukaa mbinguni. Utakuwa sawasawa na **mwili** wa ufufuko wa Bwana Yesu.

Si kusema kwamba sisi sote tuta-

onekana sawasawa! Watu waliweza kuitambua Bwana Yesu nyuma ya ufufuko wake, na bila shaka kila mtu atakuwa na sura yake mwenyewe na kuonekana namna nyingine na watu wengine kwa milele.

Vilevile shairi hili halifundishi kwa-momba tutakuwa sawasawa na Bwana Yesu kwa maneno mengine. Hatutajua kamwe maneno yote kama yeye, hatutakuwa na uwezo wote, wala hatutaweza kuwa pa-hali pote kwa saa moja kama yeye.

Lakini kwa maneno ya roho tutakuwa sawasawa na Bwana Yesu. Hatutakuwa na zambi kamwe. Mashairi haya haya-tujulishi maneno yote ambayo tunge-penda kujua, lakini yanatusariji na ku-tupa tumaini.

Kwa uwezo ule anaoweza kutiisha vitu vyote viwe chini yake. Miili yetu itabadiishwa na uwezo wa Bwana ambaio atatumia kwa wakati wa kuja **kutiisha vitu vyote chini yake**. “Anaweza kuoko” (Ebr. 7:25). “Anaweza ku-saidia” (Ebr. 2:18). “Anaweza kulinda” (Yuda 24). Sasa tunajifunza ya kwamba **anaweza kutiisha**. “Huyu ni ... Mungu wetu milele na milele: Atakuwa kiongozi chetu hata kufa” (Zab. 48:14).

8. Kusihi Wakristo kuwa na umoja, wasaidiane, wawe na furaha, maombi, kuvumiliana, na mawazo mema (4:1-9)

4:1 Nyuma ya kupasha waamini juu ya tumaini la ajabu katika shairi la mwisho wa sura 3 mtume aliwaonya **kusimama imara katika Bwana**. Kuna majina mengi ya mapendo kwa waamini ndani ya shairi hili. Kwanza Paulo ali-waita **ndugu** zake. Lakini hakuwaita ndugu tu – lakini **ndugu** zake **wapendwa**. Halafu aliwapasha kwamba alikuwa na hamu sana kuwa pamoja nao tena. Halafu alisema wao ni **furaha na taji** yake. Bila shaka alifikiri kwamba walikuwa **furaha** yake wakati ule, na watakuwa **taji** yake kwa kititicha

hukumu cha Kristo. Mwishoni, kwa mwisho wa shairi hili aliwaita **wa-pendwa**. Mtume alipenda watu na mapendo ya kweli. Bila shaka neno hili lilimsaidia sana ndani ya kazi yake kwa Bwana.

4:2 Ewodia na **Sintike** walikuwa wanawake wa kanisa kwa Filipi wa-siopatana vizuri. Hatuambiwi sababu ya ugomvi wao.

Mtume alitumia neno hili **kusihii** mara mbili kuonyesha kwamba maonyo yake yalikuwa kwa wanawake hawa wawili. Aliwaonya wawe na **nia moja katika Bwana**. Haiwezekani kwa sisi kuwa na nia moja ndani ya maisha yetu ya kila siku. Hata hivi, kwa sababu ya **Bwana**, inawezekana kwa sisi kuacha kusimamia na nguvu maneno sisi tunayotaka, kusudi Bwana atukuzwe, na kazi yake iendeleshwe mbele.

4:3 Watu wana mawazo mbalimbali kama **mtumishi** mwenzangu **wa kweli** ambaye Paulo alisema naye ndani ya shairi hili alikuwa nani. Wengine wamefikiri alikuwa Timoteo, au Luka, lakini tunafikiri alikuwa Epafroditu. Aliagizwa **kusaidia wanawake hawa walijitaabisha** pamoja na Paulo **kwa Habari Njema**. Tunafahamu kwamba wanawake wenyewe walikuwa Ewodia na Sintike, na ya kwamba Paulo aliwatolea shauri njema. Mara nyingi njia nzuri zaidi kutengeneza magomvi ya watu wawili ni kuyapasha kwa mtu mwininge kabisa – mtu wa kukomea kwa maneno ya Mungu. Kazi ya mtu huyu wa tatu si kuhukumu magomvi yao, lakini ni kuru-disha mafikiri yao kwa Biblia na kuwaonyesha namna gani Neno la Mungu linawafundisha kutengeneza magomvi yao.

Maana ya “**walijitaabisha** pamoja na Paulo **kwa Habari Njema**” haiko ya kwamba wanawake hawa walihubiri Habari Njema pamoja na mtume Paulo. Wanawake wanaweza kujitaabisha kwa

njia nyingi katika kazi ya Habari Njema. Wanaweza kupokea watumishi wa Kristo nyumbani mwao na kuwalisha; wanaweza kufikia wasioamini, au wa-amini wengine nyumbani mwao; wanaweza kufundisha wanawake vijana na watoto Neno la Mungu, bila kufanya kazi ya kufundisha Neno la Mungu, na kuhubiri mbele ya watu wote.

Mtu mwininge aliyetumika pamoja na Paulo alitajwa, jina lake **Klementi**. Hatujui maneno mengine juu yake. Halafu Paulo alitaja **wale wengine waliotenda kazi** pamoja naye, **walio na majina yao katika kitabu cha uzima**. Ni njia nzuri sana kuandika juu ya baraka kubwa sasa na ya milele ya wale wanaoamini Kristo na kumtumikia.

4:4 Halafu Paulo alionya kanisa zima tena kufurahi katika Bwana. Maneno makubwa mawili ya onyo hili ni **katika Bwana**. Hata mambo magumu sana yakipata Wakristo, inawezekana kwao **kufurahi katika Bwana**. Neno hili linawezekana namna gani? Jowett aliandika juu ya furaha ya Mkristo:

Furaha ya Mkristo haitegemei maneno ambayo yanatuzunguka na kutupata, na yanayogeukageuka Siku moja inanipa kufikia ndoa; kesho yake ninasimama karibu na kaburi. Siku moja ndani ya utumishi wangu ninaweza kupata watu kumi kwa Bwana, na halafu kwa siku nyingi sipati hata mtu mmoja. Ndiyo, siku za maisha yetu zinageukageuka, lakini inawezekana kwa furaha ya Mkristo kuendelea bila kubadilika. Siri yake nini?

Ni hii: “Sitakupungukia kabisa, wala sitakuacha hata kidogo.” Ndani ya mambo ya kugeukageuka ya mai-sha yangu Bwana hageuki, wala hachoki. Yeye ni pamoja nami siku za furaha, na hajifichi wakati ni-napata taabu. ... “Siku zote.” Siku ya uhai – siku ya kufa – siku ya hukumu.¹⁰

4:5 Halafu Paulo aliwaonya kuacha **upole wao ujulikane na watu wote.** Maana ya upole hapa ni kuwa tayari kuacha kufanya mapenzi yetu wenyewe. Maneno makubwa ndani ya shairi hili ni ambayo yanatupasa kutii ni “**na watu wote.**”

Labda maana ya “**Bwana ni karibu**” ni ya kuwa Bwana ni pamoja nasi sasa, au kwamba kuja kwake ni karibu. Maana mbili zote ni kweli lakini sisi tunapenda zaidi maana ya pili.

4:6 Inawezekana kwa Mkristo kukaa bila **kujisumbusha kwa neno lo lote?** Baki la shairi hili linaonyesha namna gani tunaweza kuishi bila zambi ya kujisumbusha. Inatupasa **kuomba** Bwana juu ya kila neno. Maana ya **kila neno** ni *kila neno*. Hakuna neno lililo dogo zaidi au kubwa zaidi – anaweka roho na mapendo juu yao yote!

Maombi ni tendo, na hali ya roho vilevile. Tunafikia Bwana kwa wakati fulani na kumwomba juu ya maneno fulani. Lakini inawezekana kwa sisi kuishi ndani ya *roho* ya maombi. Labda *kuomba* ndani ya shairi hili kunatufikirisha zaidi juu ya kuishi maisha ya maombi, lakini **kusihni** ni kuomba Bwana juu ya maneno fulani.

Tuone vilevile ya kwamba sharti tuombe Mungu **pamoja na kushukuru.** Mtu mmoja alijumlisha shairi hili na kusema kwamba “haifai tusumbuke juu ya neno lo lote, tuombe juu ya kila neno, na kuwa na asante kwa kitu cho chote.”

4:7 Maneno haya yakionekana ndani ya maisha yetu, **salama ya Mungu, inayopita akili zote, italinda miyo** yetu **na nia zetu katika Kristo Yesu.** **Salama ya Mungu** ni raha na imani zinazojaza roho ya mwamini wakati anapotegemea Mungu.

Salama hii inapita akili zote. Watu wa dunia hawawezi kuifahamu hata kidozo, na ni siri hata kwa Wakristo

wenye salama hii. Wanashangala kwa sababu hawasumbushwi kwa wakati wa msiba au taabu kubwa.

Salama hii inalinda roho na mafikiri yetu. Tunaihitaji kabisa sasa kwa wakati watu wengi wanapoteswa na ugonjwa wa nia, wakitangatanga rohoni, na kumeza dawa ya kila aina wakitafuta salama.

4:8 Mtume alileta maonyo mengine sasa kumaliza mafundisho juu ya mawazo yetu. Biblia inafundisha tena na tena kwamba tunaweza kutawala mawazo yetu. Ni bure kwa sisi kusema hatuwezi kufanya neno lo lote kuzuiza mawazo mabaya yasijaze nia zetu. Neno hili si kweli. Haiwezekani kwa mtu kuwa na mawazo maovu pamoja na mawazo juu ya Bwana Yesu vilevile. Hivi wakati wazo baya linapotaka kuingia nia yake ingepasa mara moja kulfikuza kwa njia ya kuwaza juu ya Kristo na kazi yake. Wanganga wa nia kwa wakati wa sasa wamepatana na mafundisho ya mtume Paulo. Wanafundisha kwamba ni hatari kwa mtu kukaa kuwaza juu ya maneno mabaya.

Si nguvu kuona Bwana Yesu Kristo ndani ya shairi 8. Maneno yote yaliyo ya **kweli**, maneno yote yaliyo ya **heshima**, maneno yo yote yaliyo **haki**, maneno yo yote yaliyo **safi**, maneno yote ya **kupendeza**, maneno yote yenye **sifa njema**; ukiwa **wema** wo wote na ikiwa **sifa** yo yote, maneno haya yote yanokane na ndani ya Bwana Yesu.

Ndani ya shairi 7 Paulo aliwaambia watakati fu kwamba Mungu atalinda miyo na nia zao katika Kristo Yesu. Lakini sasa aliwakumbusha kwamba Mungu atalinda nia na mawazo ya mtu yule tu *anayetaka* Mungu kumlinda na nia safi.

4:9 Hapa tena Paulo alitaja maisha yake mwenyewe kama mfano kwa waamini. Alitaka wafanye **maneno waliyofundisha kwake na kuona** ndani ya maisha yake.

Mafundisho haya yakifuata yale ya shairi 8 yanaonyesha kwamba maisha safi ni tunda la mawazo safi. Mawazo ya mtu yakiwa safi, maisha yake yatakuwa safi vilevile. Lakini mafikiri ya mtu yakiwa maovu, tunajua kwamba bila shaka matendo yake yatakuwa maovu vilevile. Na tuisisahau kamwe kwamba mtu akikaa kuwa na wazo ovu kwa muda mrefu, mwishoni atafanya neno lenyewe.

Kuna ahadi hapa kwamba **Mungu wa salama atakuwa pamoja** na watu wale wanaoiga mfano wa Paulo na uaminifu. Ndani ya shairi 7 wenye maombi watakuwa na salama ya Mungu rohoni. Hapa ndani ya shairi 9 **Mungu wa salama** ni pamoja na wenye maisha matakatifu. Watu wanaoonyesha kweli ya Mungu ndani ya maisha yao wanajuana na Mungu na mapendo yake karibu sana.

9. Asante ya Paulo kwa zawadi ya mali ya waamini (4:10-20)

4:10 Ndani ya mashairi 10-19, Paulo alisema juu ya namna kanisa la Filipi walimsaidia na mali. Bila shaka mashairi haya yamesaidia watumishi wengi wa Mungu kwa wakati wa ukosefu wa mali ya kutosha kwa mahitaji yao!

Paulo alifurahi kwa sababu **sasa**, nyuma ya siku nyingi, Wafilipi walituma mali kumsaidia ndani ya kazi ya Bwana. Hakushitaki Wafilipi juu ya muda uliopita wakati asipopokea mali toka kwao; alisema kwamba bila shaka walitaka kutuma zawadi kwake, lakini **walikosa nafasi** kufanya hivi.

4:11 Ni vizuri kuona adabu ya Paulo wakati alipoandika juu ya maneno ya mali. Hakutaka waamini wafikiri kwamba alinungunika juu ya ukosefu wa mali. Alitaka wajue kwamba hakutegemea maneno ya dunia namna hii. **Amejifundisha ... kufurahi** katika hali yo yote, si neno kama akikosa kuwa na mali au akiwa na mali ya kutosha. “Kuwa na furaha ni neno kubwa kupita

kuwa na mali.” Hata kama furaha haizai mali, faida yake ni hata kubwa kupita mali, kwa sababu inaondosha hamu yetu kuwa na mali.

“Ni baraka sana wakati mwamini anapojo funza kutokuonyesha huzuni wakati anaposikia njaa, wakati mifuko yake inapokosa mali, wakati anapoweza kuka na furaha rohoni hata wakati asi-popewa mshahara wake, na wakati anapoweza kufurahia Mungu wakati watu wasipomtendea kwa uaminifu.”

(Sehemu chaguliwa)

4:12 Paulo alijua namna gani **ku-nyenyekezwa**, maana kukosa vitu watu wanavyohitaji kwa maisha ya kila siku, na alijua **namna gani kuzidi**, maana kuwa na mali kupita ile aliyo hitaji kwa wakati ule. **Katika hali yo yote**, na **katika maneno yo yote** alikuwa amejifunza **kushiba na kuona njaa, kuwa na vitu vingi na kupungukiwa**. Mtume **ali-jifunza** maneno haya namna gani? Kwa sababu aliamini kabisa kwamba alikuwa akifanya mapenzi ya Mungu. Alijua ya kwamba alikuwa Mungu ambaye alimchagulia hali yake. Kama alikuwa na **njaa**, ilikuwa kwa sababu Mungu alitaka awe na njaa. Kama **akishiba**, lili kuwa shauri la Mungu. Akikaa kutumikia Mfalme wake na uaminifu, aliweza kusema, “Ndiyo, Baba, kwa maana hivi ilikupendeza.”

4:13 Maneno Paulo aliyosema ndani ya shairi hili linafazaisha watu wengi: “**Ninaweza kufanya maneno yote katika Kristo ambaye ananitia nguvu.**” Alifikiri kweli kwamba hakuna neno asiloweza kufanya? Sivyo. Maana ya kwamba aliweza **kufanya maneno yote**, ni **maneno yote** yaliyo mapenzi ya Mungu kwa yeche kufanya. Alikuwa amejifunza kwamba Mungu akimwagiza kufanya neno fulani, atamwezesha kulifanya. Alijua kwamba Mungu hata-mwagiza kamwe kufanya neno fulani bila kumpa neema ambayo atahitaji kwa

kuweza kulifanya. Tunafikiri **maneno yote** hayakuwa matendo ya uwezo na ajabu, lakini kuvumilia ukosefu na njaa.

4:14 Hata nyuma ya kusema maneno haya, Paulo alitaka Wafilipi kujuua kwamba walikuwa **wamefanya vema kushiriki** naye katika **taabu yake**. Tunafikiri alikuwa akisema juu ya mali waliyotuma kumsaidia wakati alipokuwa gerezani.

4:15 Hata mbele, **Wafilipi** walikuwa wenyewe ukarimu sana. Kwa wakati wa mwanzo wa utumishi wa Paulo, **saa alipoondokea Makedonia, hakuna kenis lingine liloshiriki** naye kwa njia ya mali ila Wafilipi.

Ni ajabu kuona kwamba habari hizi zisizoonekana kama maneno makubwa machoni mwa watu, yameandikwa kwa milele ndani ya Neno la damani la Mungu. Neno hili linatufundisha kwamba kitu cho chote kinacholetwa kwa watumishi wa Bwana kinaletwa kwa Bwana. Anaweka roho juu ya kila kitu kama zawadi inayotolewa kwa yeye, na kuitolea zawabu.

4:16 Hata wakati alipokuwa **katika Tesalonika**, walituma mali wakati na wakati kumsaidia. Roho Mtakatifu alitia mzigo ndani ya roho zao waweze kusaidia mtume Paulo, nao walituma mali kumsaidia **wakati na wakati**. Hili ni neno la kutushangaza zaidi wakati tunapokumbuka kwamba alikuwa kwa Tesalonika kwa muda mfupi tu.

4:17 Shairi hili linaonyesha kwamba Paulo hakujifikiri mwenyewe hata kidogo. Alifurahishwa zaidi kwa sababu wao walipata faida kwa njia ya **zawadi** yao. Hamu yake waweze kuzaa **matunda** mengi na kuzidi ilipita hamu yake kusaidiwa nao na mali. Hili ndilo neno linalotokea wakati Bwana anapotolewa zawadi. Zawadi zote zinaandikwa, na zitapokea zawabu mara mia moja kwa wakati wa kuja.

Mali yote tuliyo nayo ni mali ya Bwana, na wakati tunapomtolea zawadi,

tunampa tu mali yake mwenyewe. Wakristo wanaobishana kama ingepasa watoolee Mungu sehemu moja ya kumi ya mali yao hawafahamu neno hili hata kidogo. Zamani Waisraeli waliagizwa kutolea Mungu zawadi ya sehemu moja ya kumi, au kupita, wakati walipokuwa chini ya sheria. Kwa wakati wa sasa, ndio muda wa neema, haifai tuulize kama ikipasa kutolea Bwana mali ngapi, lakini kama “ningekuwa na ruhusa kuchunga sehemu gani ya mali yangu kwa mimi mwenyewe.” Ingepasa kuwa hamu ya Mkristo kuwa mwenye kiasi katika kutumia feza au mali, ili aweze kutumika na sehemu kubwa kupita ya mali anayopokea kwa kazi ya Mungu, kusudi watu wasipotee kwa milele kwa sababu hawakusikia Habari Njema ya Kristo.

4:18 Wakati Paulo aliposema, **nina vitu vyote**, maana yake ilikuwa **nina vitu vyote ninavyohitaji, na kuzidi**. Kwa wakati wa sasa watumishi wa Mungu wengi wanaomba kusaidiwa na mali, na wachache tu wanakubali kwamba wana mali ya kutosha. Kuomba mali hivi bila kizuizo ni chukizo kwa macho ya Mungu, na laumu kwa jina la Kristo. Neno hili halihitajiwi hata kidogo. Hudson Taylor alisema zamani, “Wakati kazi ya Mungu inapofanywa kwa namna Mungu anavyotaka, kazi hii haitakosa mali toka Mungu.” Inawezekana kufanya kazi watu wanayoita utumishi kwa Bwana, isiyo mapenzi ya Mungu hata kidogo. Ni hatari kwa Wakristo walio na mali nyingi kujabiriwa kuanza kazi kubwa bila ukubali wa Mungu. Hudson Taylor alisema vilevile, “Neno tunalohitaji kuogopa si ukosefu wa mali, lakini kuwa na mali nyingi isiyotolewa kweli kwa Mungu.”

Zawadi ya mapendo ya Wafilipi ambayo **Epafroditu** alipelekea Paulo, inaitwa **harufu ya manukato, zabihu ya kukubaliwa inayopendeza Mungu**. Tunasoma maneno namna hii mara moja

nyingine tu ndani ya Biblia. Ni katika Waefeso 5:2, juu ya Kristo mwenyewe. Paulo aliheshimu zawadi ya Wafilipi kwa njia ya kuonyesha kwamba ilipanda kwa Mungu kama **zabihu** ya manukato. **Ilikubaliwa** naye na **kumpendeza**.

4:19 Labda watu wanajua na kupenda shairi hili kupita mashairi yote mengine ya sura hii. Tuone kwamba ndani yake Paulo anaongeza ahadi inayofuata habari za zawadi ya Wafilipi. **Mungu atajaza mahitaji yao** yote kwa sababu ya uaminifu wao kutolea Mungu ya mali yao, na kuhatarisha hata mali waliyohitaji kwa mahitaji yao wenyewe. Ahadi hii si kwa Wakristo wanaopoteza mali yao bure kwa maneno wao wenyewe wanayotamani, bila kukumbuka kazi ya Mungu!

Ni kweli ya kwamba **Mungu anajaza** mahitaji ya watu wake, lakini ahadi hii ni zaidi kwa wale wanaotolea Kristo mali na uaminifu na mapendo. Watu hawa hawatakuwa na mahitaji.

Watu wengi wamesema Mungu hajazi mahitaji ya watu wake *toka utajiri* wake, lakini **kwa kadiri ya utajiri wake katika utukufu, ndani ya Kristo Yesu**.

4:20 Mawazo haya ya Paulo juu ya ukarimu wa Mungu kwa watoto wake yanamjaza na sifa. Ingepasa kila mtoto wa Mungu kumtolea sifa namna hii kwa namna anavyomlinda kila siku na neema yake kwa kumwongoza, kumsaidia kushinda majaribu, na kuwakisha roho yake wakati inapopoa kwa maneno ya Mungu.

10. Salamu ya mwisho (4:21-23)

4:21 Akifikiri juu ya waamini wakati walipokusanyika na kusikiliza barua ambayo aliwaandikia, Paulo alisalimu **kila mtakatifu katika Kristo Yesu**, na alituma salama toka **ndugu waliokuwa pamoja** naye.

4:22 Tunapenda shairi hili zaidi kwa sababu ya wale waliokuwa **nyumbani mwa Kaisari**.

Walikuwa watu wa nyumba ya Néron? Walikuwa askari walioagizwa kulinda mtume Paulo, na waliookolewa kwa sababu ya ushuhuda wake? Walikuwa watumwa au watu huru waliofanya kazi ndani ya nyumba ya Kaisari? Au walikuwa watu wa serikali ya Waroma? Hatuwezi kujua kabisa, lakini habari hizi ni mfano mzuri wa namna Wakristo, kama buibui (au mjis), wanavyopata njia kuingia nyumba za mfalme (Mez. 30:28)! Hakuna mipaka inayoweza kuzuiza Habari Njema. Inaweza kupita katika viambaza vya nguvu sana. Inaweza kufanya kazi yake hata katikati ya wale amba wanajaribu kuiharibu. Kweli milango ya Hadeze haitashinda kanisa la Yesu Kristo!

4:23 Halafu Paulo alimaliza barua hii na salama yake ya neema ambayo alitumia ndani ya zaidi ya barua zake. Tuliona **neema ya** Mungu kwa mwanzo wa barua yake, na tena sasa kwa mwisho wake. Roho ya Paulo ilijaa na kufurika na habari hizi kubwa zaidi za nyakati zote – **neema ya** Mungu kwa njia ya **Kristo** – hatushangai kwa sababu kweli hii ya damani iligusa kila sehemu ya maisha yake.

Paul Rees alisema maneno haya kumaliza barua hii:

Mtu wa kujulikana zaidi duniani ameandika barua yake ya mapeンド mengi. Kazi hii ilikuwa sasa. Ilikuwa mangaribi. Mnyororo ulibaki kwa kifundo cha mkono wa mtume. Askari angali akisimama akimlinda. Si neno! Roho ya Paulo ilikuwa huru! Nia yake ilikuwa bila shida! Moyo wake uliwaka!

Kesho yake Epafroditu alishika njia kwenda Filipi!¹¹

NOTES

¹ (1:1) J. H. Jowett, *The High Calling*, p. 2.

² (1:7) W. E. Vine, *The Epistles to the*

- Philippians and Colossians*, p. 23.
- ³ (1:11) Lehman Strauss, *Devotional Studies in Philippians*, p. 63.
- ⁴ (1:20) Guy King, *Joy Way*, p. 33.
- ⁵ (1:21) Jowett, *Calling*, p. 34.
- ⁶ (2:5) King, *Joy Way*, p. 51.
- ⁷ (3:10) Jowett, *Calling*, p. 217.
- ⁸ (3:10) Hudson Taylor, quoted by Mrs Howard Taylor in *Behind the Ranges*, p. 170.
- ⁹ (3:17) Strauss, *Philippians*, p. 202,
- ¹⁰ (4:4) Jowett, *Day by Day*, pp. 169-171.
- ¹¹ (4:23) Paul Rees, *The Adequate Man*, p. 127.

BIBLIOGRAPHIE

Erdman, C. R. *The Epistle of Paul to the Philippians*. Philadelphia: Westminster Press, 1928.

Gifford, E. H. *The Incarnation: A Study of Philippians*. London: Hodder & Stoughton, 1897.

Jowett, J. H. *The High Calling*. London: Andrew Melrose, 1909.

Kelly, William, *Lectures on Philippians and Colossians*. London: G. Morristh, n.d.

Kennedy, H. A. A. "Philippians," *The Expositor's Greek New Testament, Vol. III*. Grand Rapids: Wm. B. Eerdmans Publishing Co., 1961.

King, Guy H. *Joy Way*. London: Marshall, Morgan & Scott, Ltd., 1954.

Meyer, F. B. *Devotional Commentary on Philippians*. Grand Rapids: Kregel Publications, 1979.

Rees, Paul. *The Adequate Man*. Westwood, N. J.: Fleming, H. Revell Co., 1959.

Strauss, Lehman. *Devotional Studies in Philippians*. Neptune, N. J.: Loizeaux Bros. Publishers, 1959.

Vine, W. E, *The Epistles to the Philippians and Colossians*, London: Oliphants, 1955.

BARUA KWA WAKOLOSAYI

Utangulizi

“Ni faida kubwa kwa sasa na kwa milele kwa roho zetu kuwaza juu ya mafundisho ya Mungu [katika Wakolosayi] na kuyaacha kugusa na kutengeneza maisha yetu.

— R. C. H. Lenski

I. Nafasi ya pekee katika Kanuni

Zaidi ya barua za Paulo ziliandikwa kwa makusanyiko ya watu ndani ya miji mikubwa au ya kujulikana: Roma, Ko-rinto, Efeso na Filipi. Kolosayi ulikuwa mji mdogo kupita katika miaka iliypota. Hata kanisa la pale halikujulikana sana ndani ya historia ya mwanzo wa makanisa. Kwa wakati wa sasa wenye kujifunza maneno ya historia ya zamani tu wangejuana na jina la Kolosayi.

Hata kama mji huu haukulikana, barua ambayo Paulo alituma pale ilikuwa na maana kubwa sana. Pamoja na mafundisho ndani ya Yoane 1 na Waebrania 1, Wakolosayi 1 ni mafundisho ya ajabu zaidi juu ya uungu kamili wa Bwana wetu Yesu Kristo. Mafundisho haya ni msingi wa kweli nzima ya kikristo.

II. Mwandishi

Kufika wakati wa miaka 1.800 nyuma ya wakati wa makanisa ya kwanza, hakuna mtu aliyeshindana kwamba Paulo alikuwa mwandishi wa barua hii. Wallimu wa zamani waliotaja sehemu za barua hii pamoja na jina la Paulo kama mwandishi wake walikuwa Ignatius, Justin Martyr, Théophilus wa Antiochia, Irénaeus, Clément ya Alesandria, Tertullian. na Origen. Canon ya Marcion na ile

ya Muratori zinakubali kwamba barua hii iliandikwa na Paulo.

Mara tatu mwandishi alisema kwamba ye ye ni Paulo (1:1, 23; 4:18), na maneno yaliyoandikwa ndani ya mashairi haya yanahakikisha kwamba yaliandikwa na Paulo. Kama ilivyokuwa desturi ya Paulo ndani ya barua zake nyingine, barua hii inaleta kwanza mafundisho ya dini mbele ya maagizo kwa mwenendo. Neno linalohakikisha zaidi kwamba barua hii iliandikwa na Paulo ni kuungana kwa barua hii na barua yake kwa Filemono. Watu watano wanatajwa ndani ya barua ile ndogo wanaotajwa ndani ya Wakolosayi vilevile. Neno hili liliaminisha hata mwenye kupima ukweli kama Renan, naye alishangaa juu ya neno hili, hata kama *alikuwa na shaka juu ya Wakolosayi*.

Maneno mengine watu wanayotaja kuonyesha kwamba barua hii haiku-andikwa na Paulo ni masemo ambayo Paulo alitumia ndani ya barua hii, mafundisho yake juu ya Kristo, na masemo mengine juu ya Gnosticisme. Ndani ya Wakolosayi Paulo alitumika na masemo asiyotumia mbele, lakini alikuwa na ruhusa kufanya hivi. Mafundisho yake juu ya Kristo ndani ya barua hii yanapatana na mafundisho juu ya Kristo ndani ya Wafilip na Yoane. Watu wale

tu wanaotaka kugeuza mafundisho haya wangeshindana nayo. Mwalimu mmoja, jina lake Moffatt, la inchi ya Ecosse, alifikiri ingewezekana kwa kosa la Gnosticisme kuanza baada ya miaka michache nyuma ya mwanzo wa wakati wa kikristo.

III. Tarehe

Wakolosayi ilikuwa moja ya “Barua za Kifungo,” hivi labda iliandikwa na Paulo wakati alipofungwa kwa miaka miwili kwa Kaisaria (Mdo. 23:23; 24:27). Lakini alipokewa na mhubiri Filipo nyumbani mwake wakati alipokuwa pale. Bila shaka Paulo, akiwa mtu wa adabu sana, angalitaja habari hizi ndani ya barua yake. Ni kama Paulo aliandika barua hii wakati alipofungwa kwa Roma, karibu na A.D. 60 (Mdo. 28:30, 31).

Ni asante kwa sababu tunaweza kufahamu mafundisho ya barua hii hata kama hatujui kabisa kama iliandikwa pahali na mwaka gani.

IV. Msingi na Jambo Kubwa

Kolosayi ulikuwa mji wa wilaya ya Furigia, kwa inchi inayoitwa Asia Ndogo kwa wakati wa sasa. Ulikuwa kilomètres 16 toka Laodikia kwa upande wa mashariki na kilomètres 21 toka Hierapoli kwa upande wa kusini-mashariki (ona 4:13). Ulikuwa karibu kilomètres 160 toka Efeso kwa upande wa mashariki.

Hatujui kama Habari Njema ilifikia Kolosayi namna gani. Kwa wakati Paulo alipoandika barua hii, hakukutana bado na waamini wa pale (2:1). Walimu wanafikiri Epafra ndiye aliyefikisha Habari Njema kwa mji huu kwanza (1:7). Watu wengi wanafikiri wakati Paulo alipokuwa kwa Efeso kwa miaka mitatu, ushuhuda wake uliaminisha Epafra Habari Njema, naye aliokolewa. Paulo alikuwa kwa Furigia (Mdo. 16:6; 18:23), lakini hakuwa kwa Kolosayi (2:1).

Lakini tunajua kwa njia ya Paulo kwamba kulikuwa na hatari kwa mafundisho ya uwongo ulioitwa Gnosticisme kwa wakati wa nyuma, kuharibu kanisa kwa Kolosayi. Watu wa dini hii, ndio Wagnostiques, walijisifu juu ya elimu yao. Walisema walijua kupita mitume na walijaribu kufikirisha watu kwamba haiwezekani kwa watu kuwa na furaha ya kweli bila kupokewa na kuingizwa ndani ya siri za dini yao.

Wengine wa Wagnostiques hawakumini utu wa Kristo. Walifundisha kwamba “Kristo” alikuwa *uvutu* toka Mungu uliokaa juu ya Mtu, Yesu, wakati wa ubatizo wake. Walifundisha vilevile kwamba Kristo aliondokea Yesu wakati alipokuwa karibu na kusulibishwa. Hivi walifundisha kwamba Yesu alikufa, lakini Kristo hakufa.

Wengine wa Wagnostiques waliamini kwamba mwili ni mwovu, hivi walijinyima vitu na mambo ya kujifurahisha. Walijitesa wenyewe kwa kupima kufikia hali juu kupita ya roho. Lakini wengine waliishi katika anasa. Walisema mwili si neno, wala kitu kwa hali ya roho ya mtu!

Wongo za Gnosticisme na za dini nyingine za uwongo kwa Kolosayi ni duniani hata kwa wakati wa sasa. Zinaonekana ndani ya kawaida mbalimbali nyingi za dini zinazofundisha kwamba mtu anaweza kukubaliwa na Mungu kwa njia ya vitendo vyake. Zinafundisha watu vilevile kuona bure, au kukataa kwamba wao ni wenye zambi wanaohitaji wokovu toka Mungu peke yake.

Ndani ya barua yake kwa Wakolosayi, mtume Paulo alionyesha ubaya wa mafundisho haya yote ya uwongo kwa njia ya kuonyesha utukufu wa Bwana Yesu Kristo na kazi yake.

Barua hii inafanana kwa njia nyingine na barua ya Paulo kwa Waefeso, lakini kwa njia nyingine barua hizi ni mbalimbali vilevile. Ndani ya Waefeso tonaona waamini wakikalishwa pamoja na

Kristo kwa pahali pa mbingu. Katika Wakolosayi tunawaona duniani, lakin tunaona Kristo, aliye Kichwa chao mtukzwa, mbinguni. Ndani ya *Waefeso* tunasoma zaidi juu ya *mwamini ndani ya Kristo*. Ndani ya *Wakolosayi* tunaona *Kristo ndani ya mwamini*, tumaini la utukufu. Ndani ya Waefeso tunasoma zaidi juu ya kanisa kama “mwili” wa Kristo, “utimilifu wake anayetimiza

vyote katika vyote” (Efe. 1:23). Hivi kuna mafundisho juu ya umoja wa mwili wa Kristo. Mafundisho ndani ya sura 1 ya Wakolosayi ni juu ya ukubwa wa Kristo kama Kichwa, na kwamba inatupasa “kushika Kichwa” (Kol. 2:18, 19), na kumnyenyeka. Barua kwa Waefeso ina mashairi 155. Mashairi 54 ya mashairi haya yanafanana na mashairi ndani ya Wakolosayi.

HABARI YALIYOMO

1. MAFUNDISHO JUU YA UKUU MNO WA KRISTO (Sura 1, 2)
 - A. Salamu 1:1, 2)
 - B. Mashukuru na maombi ya Paulo kwa waamini (1:3-14)
 - C. Utukufu wa Kristo, aliye Kichwa cha Kanisa (1:15-23)
 - D. Utumishi Paulo aliopewa (1:24-29)
 - E. Kristo anatosha kuonyesha hatari ya mafundisho ya uwongo juu ya elimu, kushika sheria, mafundisho ya siri, na kujinyima vitu kwa ajili ya damiri (2:1-23)
2. WAJIBU WA MWAMINI KWA KRISTO MWENYE SIFA (Sura 3, 4)
 - A. Uzima mpya wa mwamini: Kuondosha mtu wa zamani na kuvalaa mtu mpya (3:1-17)
 - B. Mwendo wa kufaa kwa watu nyumbani mwa Wakristo (3:18– 4:1)
 - C. Maisha ya maombi ya mwamini, na ushuhuda wake kwa njia ya mwenendo na masemo (4:2-6)
 - D. Habari za wengine wa washirika wa Paulo (4:7-14)
 - E. Salamu na mafundisho (4:15-18)

Maelezo

1. MAFUNDISHO JUU YA UKUU MNO WA KRISTO (Sura 1, 2)

A. Salamu (1:1, 2)

1:1 Kwa wakati Agano Jipya kilipoandikwa, ilikuwa desturi kuanza barua na jina la mwandishi. Hivi **Paulo** alianza barua hii akijiita **mtume wa Kristo Yesu kwa mapenzi ya Mungu**. **Mtume** alikuwa mtu aliyetumwa na Bwana Yesu kama mjumbe. Kwa kuhakikisha habari za mafundisho yao, mi-

tume walipewa uwezo kufanya maajabu (2 Kor. 12:12). Zaidi ya ile, tunasoma kwamba mara nyingine wakati mitume walipowekea waamini wengine mikono, Roho Mtakatifu alitolewa (Mdo. 8:15-20; 19:6). Hakuna mitume kama hawa duniani kwa wakati wa sasa, na ni upumbavu kwa watu kujitaja wafuataji wa mitume kumi na wawili wa kwanza. Walimu wengi wanatafsiri Waefeso 2:20 kusema kazi ya wale wenye zawadi ya mitume na manabii ilikuwa zaidi kwa

mwanzo wa kanisa, lakini kazi ya wahubiri wa Habari Njema, na wachungaji na walimu (Efe. 4:11) inaendelea kwa madaraka ya sasa.

Paulo alisema alipewa kazi ya mtume **kwa mapenzi ya Mungu** (ona vilevile Mdo. 9:15; Gal. 1:1). Haikuwa kazi aliyochagua yeze mwenyewe, wala kufundishwa na watu wengine. Wala hakupewa utumishi huu kwa kutiwa mikono na askofu. Alitimiza utumishi wake mzima akifahamu kwamba Mungu mwenyewe alimchagua kuwa mtume.

Pamoja na Paulo saa alipoandika barua hii alikuwa **Timoteo ndugu yetu**. Ni vizuri kuona kwamba Paulo haku-jionyesha kuwa mkubwa wa Timoteo. Wao wawili walikuwa ndugu pamoja na ndugu wengine kanisani, na hatusomi neno juu ya majina ya heshima au mavazi ya kuonyesha cheo fulani.

1:2 Barua yenyele iliandikwa kwa **watakatifu na ndugu waaminifu katika Kristo walio katika Kolosayi**. Hapa tunaona majina matamu mawili ambayo Wakristo wote ndani ya Agano Jipyä walipewa. Maana ya **watakatifu** ni ya kwamba walitengwa kwa Mungu toka dunia, na ya kwamba kwa sababu hii ilipasa maisha yao kuwa matakatifu. **Ndugu waaminifu** ni jina linaloonyesha kwamba wao wote ni watoto wa Baba mmoja kwa njia ya kuamini Bwana Yesu. Wao ni ndugu waamini waume na wake. Ndani ya sehemu nyingine za Agano Jipyä Wakristo wanaitwa vilevile wanafunzi na waamini.

Katika Kristo inaonyesha mahali yao kwa maneno ya *roho*. Wakati walipookolewa, Mungu aliwaweka katika Kristo, “katika huyu mpendwa” (Efe. 1:6.) Sasa walikuwa na uzima na tabia yake. Toka saa hii Mungu hakuwaona tena kama watoto wa Adamu au watu wasiozaliwa, lakini kwa macho yake walikubaliwa kwa kipimo ambacho Mwana wake mwenyewe anakubaliwa.

Sisi wana wa Adamu tunashindwa kufahamu maana tamu ya maneno haya **katika Kristo**, yanayosema juu ya ukaribu, kupokewa, na salama. Duniani waamini hawa **walikuwa katika Kolosayi**. Labda tusingalisikia kamwe habari za kijiji hiki isipokuwa Habari Njema ilihubiriwa pale, na watu wengine waliokolewa.

Halafu Paulo alisalimu watakatifu na masemo haya matamu: **Neema iwe kwenu na salama toka Mungu Baba yetu na Bwana Yesu Kristo**. Maneno haya mawili, **neema na salama**, yanayonyesha vizuri kupita maneno yote mengine baraka za waamini. **Neema** ndiyo salamu ya Wayunani. Wayuda walilalimiana na **salama**. Watu walitumia masemo haya saa ya kukutana au kuagana. Paulo aliyataja pamoja, na kwa njia hii aliongeza maana yao. **Neema** inaonyesha Mungu akiinama na mapendo na huruma kwa wapotevu. **Salama** inaonyesha tunda ndani ya maisha ya mtu wakati anapopokea neema ya Mungu kama zawadi. Haifai turuhusu Shetani ktuondolea salama hii kamwe. Ona ya kwamba tunasoma kwanza juu ya **neema**, mbele ya **salama**. Kama Mungu asipotutendea kwanza na mapendo na rehema, tungalikuwa wapotevu. Lakini kwa sababu yeze alitenda kwanza na neema na kutuma Mwana wake kutukufia, tunaweza kuwa na salama sasa, salama na Mungu na watu, na salama *ya* Mungu ndani ya roho zetu. Lakini hata nyuma ya kusema maneno haya yote tunajua hatutaweza kamwe kueleza na kufahamu maneno makubwa mno kama haya.

B. Mashukuru na maombi ya Paulo kwa waamini (1:3-14)

1:3 Nyuma ya kusalimu watakatifu hawa na salamu ya maneno yaliyogeuka desturi ya salamu ya Wakristo, mtume alifanya neno lingine alilofanya wakati na wakati. Alipiga magoti yake na

mashukuru na maombi. Ni kama ilikuwa desturi yake kuanza maombi yake na sifa kwa Bwana. Ni vizuri kwa sisi kufanya vivyo hivyo. Aliomba kwa **Mungu, Baba ya Bwana wetu Yesu Kristo.** Maombi ndiyo mapendeleo ya ajabu sana kwa mtu kusikiwa na Mwenye Enzi wa ulimwengu. Watu wanaweza kuuliza: "Namna gani mtu ana ukaramisu kusimama mbele ya Mungu mjuu sana?" Tunaona jibu la ulizo hili ndani ya mashairi yetu. Mungu mwenye enzi na utukufu wa ulimwengu ni **Baba ya Bwana wetu Yesu Kristo.** Yule aliye mjuu sana amegeuka karibu sana. Kwa sababu sisi waamini wa Kristo tunashiriki uzima wake, Mungu ni Baba yetu vilevile (Yn. 20:17). Tunaweza kumkaribia kwa njia ya Kristo. **Tukiwaombea ninyi siku zote.** Maneno haya si semo la kutushangaza sana, lakini lina maana sana wakati tunapokumbuka linatuonyesha namna Paulo alivyofikiri watu hawa ambao hakukutana nao kamwe. Mara nydingine ni nguvu kwa sisi kukumbuka kuombea hata watu wa jamaa yetu wenyewe na rafiki zetu. Paulo aliombea watu wengi sana. Hakuombea wale ambao aliwajua tu, lakini Wakristo kwa pahali pengine alioambiwa majina yao, na watu wengine. Kuwaza juu ya maisha ya maombi ya Paulo kunatusaidia kufahamu roho yake.

1:4 Alikuwa amesikia habari za **imani** yao **katika Kristo Yesu** na za **mapendo** yao **kwa watakatifu wote.** Alitaja kwanza **imani** yao **katika Kristo Yesu.** Ni lazima kwa sisi kuwaza juu ya imani ya watu kwanza. Kuna watu wengi wenye dini duniani kwa wakati wa sasa wanaokaa kusema juu ya mapendo yao kwa watu wengine. Lakini ukiulizana nao, utaona kwamba wana-kosa **imani katika Bwana Yesu.** Mapendo yao ni bure na hayana maana. Na kuna watu wengine wanaokiri kuwa na **imani katika Kristo**, lakini **mapendo**

hayaonekani ndani ya maisha yao. Paulo angekuwa na shaka juu ya imani ya watu hawa. Ni sharti kwa mtu kuwa na **imani** ya kweli katika Mwokozi, na lazima imani hii ionekane ndani ya maisha ya **mapendo** kwa Mungu na kwa wenzake.

Paulo alisema kwamba **imani** ni **katika Kristo Yesu.** Ni lazima kwa sisi kuona neno hili. Ndani ya Maandiko tunaona kila mara kwamba inapasa imani yetu kuwa katika Bwana Yesu Kristo. Mtu akiweka imani yake ndani ya banki anafikiri mwizi hawezи kuiba mali iliyo pale, lakini imani yake ni bure kama banki hii hailindwi vizuri. Ni vivyo hivyo na uzima wa roho. Imani peke yake haitoshi. Lazima imani iwe katika Bwana Yesu Kristo. Haiwezekani kwa ye ye kupunguka kamwe, hivi kila mtu anaweza kumwamini na kumtegemea kabisa.

Paulo alikuwa amesikia habari za **imani** na **mapendo** yao. Neno hili linaonyesha kwamba hawakuficha imani yao. Hakuna mafundisho ndani ya Agano Jipyä kuruhusu mtu kuficha imani yake. Neno la Mungu linafundisha ya kwamba mtu aliyeamini Mwokozi kweli kweli atamshuhudia wazi mbele ya watu.

Wakolosayi walikuwa na mapendo kwa **watakatifu wote.** Hawakupenda waamini wa kanisa lao tu, lakini waamini wa kweli pahali po pote walipokutana nao. Neno hili ni mfano mzuri kwa sisi. Pamoja na kupenda waamini wa makanisa yetu ingetupasa kutambua na kupenda kondoo za Kristo pahali po pote tunapoweza.

1:5 Si wazi kabisa kama shairi hili linafungana na shairi 3: Tunashukuru ... **kwa sababu ya tumaini mulilowekewa akiba mbinguni?** Au linafungana na sehemu ya nyuma ya shairi 4: mapendo muliyo nayo kwa watakatifu wote, **kwa sababu ya tumaini mulilowekewa akiba mbinguni?** Tafsiri zote mbili zinakubaliwa. Labda mtume ali-

leta asante kwa imani na mapendo yao, na vilevile kwa uriti wao kwa wakati wa kuja. Na ni kweli vilevile kwamba shairi hili ni juu ya kuwa na imani katika Kristo Yesu na mapendo kwa watakatifu wote, tukijua mambo ambayo ni mbele yetu. Tunaona hapa maneno makubwa matatu ambayo Paulo anataja yaliyo sharti kwa maisha ya Mkristo: imani, mapendo, na **tumaini**. Maneno haya yanatajwa vilevile katika 1 Wakorinto 13:13 na 1 Watesalonika 1:3; 5:8. Light-foot anasema: “Imani inategemea muda unaopita; mapendo yanafanya kazi kwa wakati wa sasa; tumaini linatazamia muda wa kuja.”¹

Maana ya **tumaini** ndani ya shairi hili si kungojea na kutazamia kitu fulani. Ni kitu ambacho mtu anatumainia. Maana yake hapa ni utimilizo wa wokovu wetu wakati tutakapoolekwa mbinguni na tutakapoingia uriti wetu wa milele. Wakolosayi walikuwa wamesikia juu ya **tumaini** hili mbele, labda kwa wakati waliposikia mahubiri ya Epafra. Maneno waliyosikia kwa wakati ule yaliitia **neno la kweli ya Habari Njema**. Hapa **Habari Njema** inaitwa neno la *kweli*. Labda Paulo alikuwa akifikiri juu ya ma-fundisho ya *uwongo* ya walimu wa Gnosticisme wakati alipoandika maneno haya. Mtu mmoja alieleza kwamba “*kweli*” ni neno Mungu analogesema juu ya neno fulani (Yn. 17:17). **Habari Njema** ni kweli kwa sababu ni neno la Mungu.

1:6 Kweli ya Habari Njema **iliikuwa imefikia** Wakolosayi, kama **ni vile katika ulimwengu wote**, ndiyo sehemu ya ulimwengu watu waliyofua kwa wakati ule. Maana yake haiko ya kwamba *kila mwanamume na mwanamke* duniani alikuwa amesikia Habari Njema. Labda maana yake ni ya kwamba watu toka *kila kabilo* walikuwa wamesikia Habari Njema (Mdo. 2). Au labda

maana yake ni ya kwamba Habari Njema ni kwa watu wote, na ilikuwa ikiinezwa pahali mbalimbali bila kuzuizwa na kusudi. Paulo aliandika vilevile juu ya matunda yake. Katika Kolosayi na **kwa kila** pahali pengine **duniani** ilipohubiriwa, Habari Njema ilizaa **matunda na kukua**. Habari hizi zinaonyesha kwamba Habari Njema si ya dunia. Si desturi kwa pando kuzaa matunda pamoja na kuongezeka. Mara nyingi inapasa kupunguzia matawi yake ili pando liweze kuzaa matunda. Likiota bila kupunguziwa matawi, nguvu yote ya pando hili litaingia ndani ya majani na matawi, si ndani ya matunda. Lakini Habari Njema inafanya maneno haya mbili kwa saa moja. Inazaa **matunda**, ndiyo kuokoa watu, na kujenga watakatifu, na zaidi ya ile inaenea toka mji mmoja kwendea miji mingine, na toka taifa moja kwendea taifa lingine.

Hili ndilo neno lililotokea ndani ya maisha ya Wakolosayi wakati Habari Njema ilipohubiriwa kwao **tangu siku waliposikia na kujua neema ya Mungu katika kweli**. Hesabu ya wa-amini ndani ya kanisa kwa Kolosayi iliongezeka, na zaidi ya ile, waamini walipata nguvu katika imani.

Ni kama Habari Njema ilienea mbali sana ndani ya miaka mia moja ya kwanza nyuma ya kuzaliwa kwa Kristo, na kufikia Europe, Asie, na Afrique, na zaidi. Hata hivi haikuhubiriwa ndani ya dunia nzima. **Neema ya Mungu** ni elezo tamu sana la Habari Njema. Linajumlisha kweli ya ajabu ya neema ya Mungu waliyopewa watu wenye hatia waliostahili gazabu ya Mungu tu!

1:7 Mtume alisema wazi kwamba waamini walisikia Habari Njema toka **Epafra**, waliamini na kuipokea ndani ya maisha yao. Paulo alisifu Epafra akisema yeye ni **mjoli mpenzi**, na **mtumishi mwaminifu wa Kristo kwa ajili** yao. Hakuwa na uchungu wala wivu wakati mhubiri mwingine alipopata sifa.

Alikuwa mtu wa kwanza aliyesifu watumishi wengine wa Bwana.

1:8 Alikuwa Epafra aliyepasha Paulo habari za **mapendo katika Roho** ya Wakolosayi. Hayakuwa mapendo ya umtu tu, lakini **mapendo** ya kweli kwa Bwana na kwa watu wake, yaliyo tunda la **Roho** Mtakatifu wa Mungu aliyekaa ndani yao. Hii ni mara ya pekee tunayosoma juu ya Roho Mtakatifu ndani ya barua hii.

1:9 Nyuma ya kumaliza mashukuru haya, Paulo alianza kuombea watakatifu. Tumetaja mbele kwamba aliombea watu wengi. Sasa tunaongeza kwamba maombi yake yalipatana na mahitaji ya watu wa Mungu kwa pahali fulani. Ni kama hapa aliombea Wakolosayi kwa maneno fulani mane: (1) ufhamu wa roho; (2) mwenendo mzuri; (3) uwezo wengi; (4) roho ya asante.

Hakuwa na choyo wakati alipoomba maneno haya, kama tunavyoona ndani ya mashairi 9-11 pahali alipotumia maneno kama *yote, kabisa, kila, na wote*. (1) **Hekima yote na ufhamu wa roho** (sh. 9). (2) “kumpendeza kabisa” (sh. 10). (3) “Kila kazi njema” (sh. 10). (4) “Uwezo wote” (sh. 11). (5) “Saburi yote na uvumilivu” (sh. 11).

Maneno haya **kwa sababu hii** yanaturudisha kwa *habari Epafra alizoleta* (mash. 4, 5, 8). Tangu mara ya kwanza Paulo **aliyosikia** habari za watakatifu wapendwa hawa kwa Kolosayi na imani, mapendo, na tumaini yao, mtume alianza desturi ya kuwaombea. Kwanza, alionba **wajazwe na kujua mapenzi** ya Mungu **katika hekima yote na ufhamu wa roho**. Hakuomba washibishwe na kujua elimu ya walimu wa Gnosticisme. Alitaka waweze kujua kabisa **ufhamu wa mapenzi** ya Mungu kwa maisha yao, namna yanavyofunuliwa ndani ya neno lake. Hekima hii si namna ya dunia, na si ya tamaa za mwili. Ni **hekima yote na ufhamu wa roho**. Inatupasa kutumika na elimu

kujuua namna gani kutumika, na **ufahamu** wa roho kutambua maneno gani yanapatana na mapenzi ya Mungu, na yale ambayo hayampendezi.

1:10 Mafundisho ya mashairi 9 na 10 yanafungana pamoja. Kwa sababu gani mtume Paulo alitaka Wakolosayi kujazwa na kujua kwa mapenzi ya Mungu? Alitaka waweze kugeuka walimu wa uwezo? Alitaka wapate wafuata wengi, kama walimu wa Gnosticisme walivyojaribu kufanya? Sivyo. Kusudi la elimu na ufhamu lilikuwa kusaidia Wakristo **kutembea kama inavyostahili na Bwana kwa kumpendeza kabisa**. Hafunui mapenzi yake kusaidia kiburi yetu. Bwana anatufunulia mapenzi yake kwa maisha yetu ili tuweze kumpendeza ndani ya maneno yote.

Mukizaa matunda katika kila kazi njema. Hapa tunakumbushwa kwamba mtu haokolewi *kwa njia ya kazi njema zake*, lakini bila shaka anaokolewa ili aweze *kutenda kazi njema*. Labda mara nyingine wakati tunapofundisha watu kwamba hawawezi kuokolewa kwa njia ya kutenda kazi njema, tunafikirisha watu kwamba Wakristo hawaweki roho juu ya kutenda kazi njema. Neno hili si kweli hata kidogo. Ndani ya Waefeso 2:10 tunajifunza kwamba “tuliumbwu katika Kristo Yesu ili tutende matendo mema.” Na Paulo aliandikia Tito: “Neno hili ni aminifu, nami ninataka useme maneno haya kwa nguvu, hata watu walioamini Mungu wakumbuke kudumu katika kazi nzuri” (Tit. 3:8).

Pamoja na kuzaa matunda **katika kila kazi njema**, Paulo alitaka **wazidi kujua Mungu**. Wataweza kufanya hivi namna gani? Neno la kwanza ni kujifunza Neno la Mungu na bidii. Halafu inapasa kutti mafundisho ya Mungu na kumtumikia na uaminifu. Wakati tunapofanya hivi, tutaongezeka katika **kujua** Bwana. “Kisha tutajua kama tukiendelea kujua BWANA” (Hos. 6:3).

Ona ya kwamba ndani ya sura 1 ya

Wakolosayi tunaona tena na tena maneno juu ya *kujua* na kuongezeka kwa kujua. Ndani ya shairi 6, “*walijua* neema ya Mungu.” Ndani ya shairi 9, wali-jazwa na “*kujua* kwa mapenzi yake.” Ndani ya shairi 10, “*walizidi katika kujua* Mungu.” Tungeweza kusema kwamba shairi 6 ni juu ya wokovu, shairi 9 linasema juu ya kujifunza Maandiko, na shairi 10 ni juu ya kuongezeka katika utumishi na kuishi namna inavyopasa Mkristo kuishi.

Mafundisho mema yanatuongoza kuishi na kutenda yaliyo mema, nayo yanaonekana ndani ya utii katika utumishi wetu.

1:11 Neno la tatu mtume aliloomba ni kwa watakatifu **kuwezeshwa kwa uwezo wote, kwa kadiri ya nguvu ya utukufu wake.** (Ona kuendelea kwa maneno haya: *walijazwa*, sh. 9; *walizaa matunda*, sh. 10; *waliwezeshwa*, sh. 11.) Mkristo hawezi kuishi maisha namna inavyofaa kwa nguvu yake ya umtu. Inawezekana kwa nguvu ya Mungu tu. Kwa sababu hii Paulo alitaka waamini kujua uwezo wa Mwana wa Mungu aliyefufuliwa, na zaidi ya ile waweze kuuja **kwa kadiri ya nguvu ya utukufu wake.** Ona maneno haya: kwa kadiri ya **nguvu ya utukufu wake** haina mpaka, na hii ndiyo kipimo cha maombi yake.

Paulo alitaka Wakristo kuwa na uwezo huu kwa sababu gani? Ili waweze kufanya matendo ya ajabu? Ili waweze kufufua wafu, kuondosha pepo wachafu? Sivyo! Uwezo huu ulihitajiwa ili mtoto wa Mungu aweze kuwa na **saburi yote na uvumilivu pamoja na furaha.** Tu-fikiri sana juu ya neno hili! Kwa wakati wa sasa Wakristo wengine wanaweka roho sana juu ya maajabu, kama kusema kwa lugha, kuponyesha wagonjwa, na matendo mengine ya namna hii. Lakini kuna ajabu lingine lililo kubwa kupita maajabu haya yote kwa wakati wa sasa: Ni mtoto wa Mungu akivumilia taabu na

saburi na akishukuru Mungu hata kwa wakati wa taabu hii!

Ndani ya 1 Wakorinto 13:4 tunasoma juu ya uvumilivu pamoja na **upole**; hapa kwa Wakolosayi uvumilivu ni pamoja na **furaha.** Kwa Mkristo kuwa mshinda-ji anahitaji uwezo wa Mungu kumweze-sha kukaa na **furaha** rohoni na kutendea watu wengine mema. Watu wengine wanasema kwamba **saburi** ni kubeba maumivu bila kunungunika, na **uvu-milivu** ni kuyabeba bila kujilipiza kisasi. Neema ya Mungu imetimiza moja la makusudi yake makubwa zaidi ndani ya maisha ya mwamini anayeweza kubeba taabu na saburi, na kusifu Mungu ndani ya mateso makubwa.

1:12 Mukishukuru Baba: Paulo alionbea Wakolosayi ili pamoja na kuwezeshwa kwa uwezo wote, wawe na roho ya asante vilevile. Hakutaka wakose kamwe kushukuru **Baba** ambaye **aliwastahilisha kupokea sehemu ya uriti wa watakatifu katika nuru.** Sisi wana wa Adamu, hatukustahili kufurahi na utukufu wa mbingu. Kama wasioamini wangalipelekwa mbinguni, wasingalifurahi hata kidogo pale, lakini wangalitaabishwa sana. Watu wanaostahilishwa tu wanaweza kufurahi mbinguni. Hata sisi tulioamini Bwana Yesu, hatustahili kukaa mbinguni. Tunaweza kukaa katika utukufu wa mbingu kwa sababu tulipewa ruhusa kuwa ndani ya Bwana Yesu Kristo.

Wakati Mungu anapookoa mtu, ana-mstahilisha mara moja kwa mbingu kwa njia ya Kristo. Hakuna kitu ambacho kinamstahilisha kupita. Hata kuishi mai-sha marefu ya utii na utumishi duniani hakuwezi kumstahilisha kwa mbingu kupita kustahilishwa kwake siku alipo-okolewa. Ni kwa sababu ya damu ya Kristo tu tutaweza kufika mbinguni. Hata kama uriti ni **katika nuru** na “unatungojea mbinguni,” sisi waamini duniani tuna Roho Mtakatifu kama “arabuni ya uriti wetu.” Hivi tunaweza

kufurahi ndani ya maneno ya kuja, tungali tunafurahi hata sasa ndani ya “mamlimbuko ya Roho.”

1:13 Kwa njia ya “kutustahilisha kupokea ... uriti wa watakatifu katika nuru,” Mungu **alitutoa katika uwezo wa giza, akatuhamisha na kutuingiza katika ufalme wa Mwana wa mapendo yake** (ona vile 1 Yn. 2:11). Mambo yaliyopata wana wa Israeli na kuandikwa katika Kutoka ni mfano wa maneno haya. Walikuwa wakiishi katika Misri, wakiteswa na mapigo ya bwana zao za kazi. Kwa njia ya ajabu Mungu aliwaondosha toka woga wa utumwa ule, akawaongoza kusafiri jangwani, na kuwafikisha kwa inchi ya ahadi. Vivyo hivyo sisi wenyewe zambi tulikuwa watumwa wa Shetani, lakini kwa njia ya Kristo **tumefunguliwa toka** utumwa huu, na sasa sisi ni watu wa **ufalme** wa Kristo. Ufalme wa Shetani ni ufalme wa **giza** – unakosa nuru, moto, na furaha. Ufalme wa Kristo ni **ufalme** wa **mapendo**, na una maneno yale matatu yanayokosa ndani ya ufalme wa Shetani.

Tunaona **ufalme** wa Kristo kwa njia mbalimbali ndani ya Maandiko. Wakati Kristo alipofikia dunia mara ya kwanza, alitaka kuwapa taifa la Israeli ufalme. Wayuda walitaka kufunguliwa toka mateso ya Waroma, lakini hawakutaka kukiri zambi zao. Kristo aliweza kutawala watu wenyewe hali taratibu ya roho tu. Wakati walipofahamishwa neno hili, walikataa Mfalme wao na kumsulibi. Nyuma yake, Bwana Yesu alirudia mbingu, na sasa tuna ufalme kwa siri (Mt. 13). Ni kusema kwamba hatuwezi kuuona na macho. Mfalme si hapa. Lakini wote wanaopokea Bwana Yesu Kristo kwa muda huu wa sasa, wanamkulabi kuwa Mtawala wao, nao ni watu wa ufalme wake. Kwa wakati wa kuja Bwana Yesu atarudia dunia tena, atasi-mamisha ufalme wake na kuweka Yerusalem kuwa mji wake mkubwa, na atatawala kwa miaka elfu moja. Kwa

mwisho wa muda ule, Kristo atashinda adui zake zote na kuwaweka chini ya miguu yake, kisha atatoa ufalme kwa Mungu Baba. Huu utakuwa mwanzo wa ufalme utakaoendelea kwa milele.

1:14 Nyuma ya kutaja ufalme wa Mwana mpendwa wa Mungu, Paulo alianza kuandika moja ya maandiko ya thamani zaidi la Neno la Mungu juu ya Nafsi na kazi ya Bwana Yesu . Ni nguvu kwa sisi kujuu kama amemaliza maombi yake, au kama aliendelea nayo ndani ya mashairi tunayoanza kusoma sasa. Si neno, kwani hata kama si maombi, ni ibada takatifu.

Sturz ameonyesha kwamba “Ndani ya mashairi haya yanayotukuza Yesu Kristo kupita mashairi mengine yote, jina lake halitajwi hata mara moja.” Ndiyo, neno hili lingweza kutushangaza, lakini hakuna mwingine ila Mwokozi wetu mbarikiwa anayeweza kutimiza ndani ya maisha yake maneno yote tunayosoma hapa. Mashairi haya yanatukumbusha ulizo la Maria kwa mlinzi shamba: “Bwana, kama umemchukua, uniambie pahali ulipomweka, nami nitamwondo” (Yn. 20:15). Hakutaja jina lake. Alifikiri juu ya Mmoja tu, ndiye Bwana Yesu.

Neno la kwanza tunaloona juu ya Kristo ni ya kwamba **ndani yake tuna ukombozi wetu ...² usamehe wa zambi**. Kwa njia ya **ukombozi** tulinunuliwa toka soko la watumwa wa zambi. Ni kama Bwana Yesu aliweka bei juu yetu. Kipimo cha bei hii kilikuwa nini? Ni kama alisema, “Wao ni thamani kubwa sana kwangu hata mimi ni tayari kumwanga damu yangu kuwanunua.” Hivi tukinunuliwa kwa bei kubwa sana, ingetupasa kufahamu kwamba sisi si mali yetu wenyewe tena. Tulinunuliwa kwa bei, hivi haifai tuishi namna sisi tunavyochagua kuishi. Borden ya Yale alionyesha kwamba tukiishi maisha yetu namna sisi tunayotaka, na kufanya maneno sisi tunavyochagua, tunatumika na kitu kisicho mali yetu, nasi ni wizi!

Bwana Yesu hakutukomboa tu, lakini alitupa vilevile **usamehe wa zambi**. Maana ya neno hili ni ya kwamba Mungu amezima deni yetu ya zambi. Bwana Yesu Kristo alilipa azabu kwa zambi hizi msalabani; haifai kuilipa tena kamwe. Mungu ametusamehe, na zaidi ya ile amehamisha makosa yetu mbali, kama mashariki ilivyo mbali na mangaribi (Zaburi 103:12).

C. Utukufu wa Kristo, aliye Kichwa cha kanisa
(1:15-23)

1:15 Ndani ya mashairi 15-18 tunasoma juu ya (1) Bwana Yesu na Mungu (sh. 15); (2) Bwana Yesu na viumbe vyote (mash. 16, 17); na (3) Bwana Yesu na kanisa (sh. 18).

Bwana Yesu ni **mfano wa Mungu asiyonekana**. Mfano unatufikirisha juu ya maneno mawili. Kwanza, Bwana Yesu anatuwezesha kuona kama Mungu ni namna gani. Mungu ni Roho, hivi hatuwezi kumwona na macho. Lakini kwa njia ya Kristo, Mungu amejionyesha kwa macho ya watu. Kwa njia hii Bwana Yesu ni **mfano wa Mungu asiyonekana**. Mtu ye yote ambaye alimwona yeye ameona Baba (ona Yn. 14:9). Lakini neno hili **mfano** lina maana ya "wakili" vilevile. Kwa mwanzo Mungu aliweka Adamu duniani kusimamia maneno yake, lakini Adamu alishindwa. Halafu, Mungu alituma Mwana wake wa pekee duniani kama wakili wake, kutunza maneno yake, na kufunua mapendo ya moyo wake kwa watu. Kwa njia hii yeye ni mfano wa Mungu. Neno hili **mfano** linatumia kwa 3:10, pahali tunaposoma kwamba waamini ni mfano wa Kristo.

Kristo ni **mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote**. Maana yake nini? Walimu wa uwongo wengine wanasema Bwana Yesu aliumbwa mwenyewe, ya kwamba yeye ni kiumbe cha kwanza Mungu alichoumba. Wengine wanakubali kwa-

mba yeye ni kiumbe kikubwa zaidi Mungu alichoumba. Mawazo haya yote ni mbalimbali kabisa na mafundisho ya neno la Mungu.

Maneno haya "mzaliwa wa kwanza" yana maana tatu au zaidi ndani ya Maandiko. Ndani ya Luka 2:7, yana-sema juu ya neno lililotukia kweli, ndilo Maria akizaa Mwana wake wa kwanza. Ndani ya Kutoka 4:22 tunaona maneno haya na maana ya *mfano*, "Israel ni mwana wangu, mzaliwa wangu wa kwanza." Shairi lile si juu ya kuzaa, lakini Bwana anatumia maneno haya kuonyesha pahali na makusudi yake ya pekee kwa taifa la Israeli. Mwishoni, ndani ya Zaburi 89:27, maneno haya "mzaliwa wa kwanza" yanaonyesha *pahali pa juu zaidi*, pa ukubwa, na pa namna ya peke yake. Pale Mungu anasema kwamba atafanyiza Daudi mzaliwa wake wa kwanza, juu kupita wafalme wa dunia. Kwa njia ya mwili, Daudi alikuwa mwana wa mwisho wa Yese. Lakini Mungu alimpa pahali palipo juu zaidi, pahali pa enzi.

Haya ndiyo maneno tunayoona ndani ya Wakolosayi 1:15, pahali tunaposoma yeye ni **mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote**. Bwana Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu asiyenya na kifani. Kwa njia nydingine waamini wote ni wana wa Mungu, lakini Bwana Yesu ni Mwana wa Mungu kwa njia isiyo kweli kwa mtu ye yote. Alikuwa mbele ya kuumbwa kwa viumbe vyote, naye ni mkubwa kupita vyao vyote, na mtawala wa wote. Hapa maneno haya **mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote** hayasemi juu ya kuzaliwa kwa njia yo yote. Maana yao ni kwamba Yeye ni Mwana wa milele wa Mungu. Yanasema juu ya *daraja* lake, si juu ya maneno ya wakati tu.

1:16 Walimu wa uwongo wanataja shairi 15 kufundisha kwamba Bwana Yesu aliumbwa. Mara nyingi inaweze-kana kuonyesha uwongo wao kwa njia

ya kutumika na shairi lile lile ambalo walimu wale walitumika nalo kufundisha uwongo wao. Ni hivi hapa. Shairi 16 linaonyesha wazi kwamba Bwana Yesu si kiumbe, lakini ye ye mwenyewe ni Mwumba. Ndani ya shairi hili tunajifunza kwamba **vitu vyote** – ulimwengu mzima wa vitu – **viliumbwa naye**, na **kwa njia yake** na **kwa ajili yake**. Tunaona kwamba **vitu vyote viliumbwa naye**. Ni kusema kwamba uwezo wa kuumba ulikuwa ndani yake. Nyuma yake tunaona ndani ya shairi hili kwamba **vitu vyote viliumbwa kwa njia yake**. Ni kusema alikuwa mtendaji wa kuumba. Ni Mungu Mwana aliyeumbwa vyote. Na vilevile, vitu vyote viliumbwa **kwa ajili yake**. Vitu vyote viliumbwa **kwa yeye**, ndilo kusudi la muumbo.

Paulo aliweka roho sana kuonyesha kwa nguvu ya kwamba **vitu vyote viliumbwa kwa njia ya** Kristo, ndivyo vitu vilivyo **mbinguni**, na **duniani**. Hakuacha njia kwa mtu ye yote kusema kwamba Kristo aliumba kwanza, hata kama aliumba vitu vingine ye ye mwenyewe.

Halafu mtume aliendelea kusema kwamba vingine vya vitu Bwana aliyeoumba **vinaonekana** kwa macho, na vingine **havionekani**. Hatuhitaji kueleza maana ya **vinaonekana**, lakini bila shaka alijua kwamba tutafazaika juu ya maana ya vitu visivyoonekana. Hivi alianza kueleza maana ya vitu **visivyoonekana**. Ni **vitu vya wafalme** au **usuliani** au **falme** au **mamlaka**. Tunafikiri maneno haya yanasema juu ya malaika mbalimbali, lakini hatuwezi kufahamu tofauti za viumbe hivi.

Wagnostiques walifundisha kwamba kuna madaraja mbalimbali amba yo yagawa Mungu na viumbe, na ya kwamba Kristo alikuwa ndani ya moja la madaraja haya. Washuhuda wa Yehova wanafundisha kwamba mbele ya kufika duniani, Bwana wetu alikuwa malaika

mkubwa aliyeumbwa, ndiye Mikaeli! Paulo alibisha na nguvu mafundisho mapumbavu namna hii kwa njia ya kusema wazi kabisa ya kwamba Bwana Yesu Kristo ni Mwumba wa malaika, na wa vitu vyote, **vilivyoonekana**, au **visivyoonekana**.

1:17 Naye ni mbele ya vitu vyote na ndani yake vitu vyote vinashikamana. Paulo alisema, “Naye ni mbele ya vitu vyote.” Hakusema, “*Alikuwa mbele ya vitu vyote.*” Mara nyingi maneno yanayosema juu ya wakati wa sasa yanatumiwa ndani ya Biblia kuonyesha kwamba Mungu ni bila saa, na bila mwisho. Kwa mfano, Bwana Yesu alisema: “Mbele Abrahamu hajazaliwa, Mimi NIKO” (Yn. 8:58).

Hivi Bwana Yesu alikuwa mbele ya kuumbwa kwa vitu vyo vyote. Zaidi ya ile, ndani yake **vitu vyote vinashikamana**. Ni kusema ye ye ni mwenye kutegemeza ulimwengu, na mwenye kutezembeza saa zote. Anaongoza nyota na jua na mwezi. Hata wakati alipokuwa hapa duniani, alitembeza ulimwengu wetu na utaratibu.

1:18 Bwana Yesu hatawali ulimwengu tu, lakini maneno ya roho vilevile. **Yeye ni kichwa cha mwili, ulio kanisa.** Waamini wote wa Bwana Yesu kwa madaraka ya sasa wanafungwa pamoja na kujulikana kama **mwili** wa Kristo, unaoitwa **kanisa** vilevile. Mtu anaonyesha mafikiri ya roho yake kwa njia ya mwili wake. Vivyo hivyo mwili huu wa Kristo ni chombo cha Bwana ambacho alichagua kujionyesha duniani, na ye ye ni **kichwa cha mwili** huu. Kichwa kinatufikirisha maongozi, maagizo, na utawala. Yeye anashika pahali **pa kwanza** kanisani.

Yeye ni **mwanzo**, maana yake **mwanzo** wa muumbo mpya (ona Ufu. 3:14), mwanzo wa uzima wa roho. Naye ni **nzaliwa wa kwanza kutoka katika wafu**. Sharti tueleze wazi ya kuwa maana ya maneno haya si ya kwamba

Bwana Yesu alikuwa wa kwanza aliye-fufuka toka wafu. Kuna wengine walio-fufuliwa katika Agano la Kale na Agano Jipyi vilevile. Lakini Bwana Yesu ni wa kwanza aliye-fufuliwa toka wafu *asiye-kufa tena*. Alikuwa wa kwanza aliye-fufuliwa na mwili wa utukufu, na alifufuliwa kama Kichwa cha muumbo mpya. Ufufuko wake ni namna ya peke yake, na ni ahadi ya kwamba wote ambao wanamwamini watafufuliwa vilevile. Ni tangazo kwamba yeche ni mwenye enzi wa muumbo wa roho.

Alfred Mace alieleza neno hili vizuri:

Haiwezekani kwa Kristo kuwa wa pili pahali po pote. Yeye ni “mzaliwa wa kwanza wa kila kiumbe” kwa sababu aliumba kila kitu (Kol. 1:15, 16). Yeye ni mzaliwa wa kwanza vilevile toka wafu walio-kombolewa na walio jamaa ya mbingu. Hivi kwa maneno ya muumbo na ukombozi, Kristo anaheshimiwa na mamlaka juu ya kila kitu kwa sababu yeche ni Mwana wa Mungu, na kwa sababu ya kazi yake; “ili apate kuwa wa kwanza katika yote.” Yeye ni kwanza pahali po pote.³

Hivi Bwana Yesu ana sifa zaidi kwa njia mbili – kwanza katika muumbo, na halafu katika kanisa. Mungu ameamuru ya kwamba ***katika vyote apate kuwa wa kwanza***. Ni jibu la uwezo kabisa kwa watu wa wakati wa Paulo (na kwa wakati wa sasa vilevile) wanaajaribu kufundisha kwamba Kristo si Mungu, na wanaosema yeche ni kiumbe tu, kiumbe chenye heshima sana!

Wakati tunaposoma ili ***katika vyote apate kuwa wa kwanza***, ingefaa tuji-ulate, “Ana pahali pa kwanza ndani ya maisha yangu?”

1:19 Utimilifu wote wa Mungu una-kaa ndani ya Kristo. Walimu wa Gnosticisme walifundisha kwamba Kristo si Mungu kabisa, na ya kwamba “nyuma ya kumjua yeche inapasa watu kuendelea

mbele na kufikia utimilifu!” Lakini Paulo alijibu, “Sivyo, hata kidogo. Kristo mwenyewe ni utimilifu ukamilifu!”

Utimilifu wote *unakaa* ndani ya Kristo. Maana ya **kukaa** hapa ni kupanga daima, si kwa muda mfupi tu.

1:20 Ona namna shairi 19 linafungana na shairi 20. Sh. 19: “Kwa kuwa **katikia yeche** (Kristo) ilipendeza **Baba** ili utimilifu wote ukae, (sh. 20); **na kwa yeche** (Kristo) **kupatanisha vitu vyote kwake, akiwa amefanya salama kwa njia ya damu ya msalaba wake; ...” Ni kusema ilipendeza Mungu kwa utimilifu wote kukaa ndani ya Kristo (sh. 19), na vilevile kwa Kristo **kupatanisha vitu vyote kwa yeche** (sh. 20).**

Kuna upatanisho namna mbili ndani ya sura hii: (1) Upatanisho wa vitu (sh. 20), na (2) upatanisho wa watu (sh. 21). Upatanisho wa kwanza haujatokea bado, lakini upatanisho wa pili umekwisha kutukia kwa watu wote walioamini Kristo.

MAFUNDISHO JUU YA UPATANISHO

Kupatanisha ni kutengeneza maneno na kukomboa uadui wa mbele na salama. Hatusomi kamwe ndani ya Biblia juu ya Mungu akitajiri kupatanishwa na mtu, lakini tunasoma kwamba mtu anahitaji kupatanishwa na Mungu. Nia ya mwili ni uadui juu ya Mungu (Rom. 8:7), na kwa sababu hii, mtu anahitaji kupatanishwa.

Wakati zambi ilipoingia dunia, mtu alitengwa mbali na Mungu, na alishika roho ya uadui kwa Mungu. Kwa sababu hii alihitaji kupatanishwa.

Lakini zambi imegusa viumbe vyote, si watu tu.

1. Wengine wa malaika wamefanya zambi zamani. (Lakini hatusomi ndani ya Neno la Mungu ya kwamba malaika hawa watapanishwa wakati wo wote. Wamewekwa “*katika vifungo* vya milele chini ya giza kwa hukumu ya siku ile

kubwa," (Yud. 6.) Katika Yobu 4:18, Elifasi alisema kwamba Mungu alishitaki malaika zake na upumbavu.

2. Zambi zilizoingia dunia ziligusa nyama: "Kwa maana viumbe vyote vinangojea kwa hamu sana ufunuo wa wana wa Mungu. Kwa maana viumbe vyote viliwekwa chini ya ubatili ... Kwa maana tunajua ya kuwa viumbe vyote pia vinaugua, na vina uchungu pamoja hata sasa" (Rom. 8:19-22). Maumivu na na gonjwa na mauti ya nyama yanaonyesha wazi kwamba zinalaaniwa vilevile kwa sababu ya zambi.

3. Udongo ulilaaniwa na Mungu wakati Adamu alipokwisha kufanya zambi (Mwa. 3:17). Majani bure, miiba, na mibaruti zinahakikisha neno hili.

4. Ndani ya kitabu cha Yobu, Bildadi alituambia kwamba hata nyota si safi machoni mwa Mungu (Yob. 25:5).

5. Kwa Waebrania 9:23 tunasoma kwamba mifano ya mambo yaliyo mbinguni yalipaswa kusafishwa. Hatujui maana ya maneno haya yote, lakini labda mambo mbinguni yamechafuwa kwa njia ya Shetani, anayeweza kukaribia Mungu kama mshitaki wa ndugu (Yob. 1:6, 7; Ufu. 12:10). Watu wengine wanafikiri mashairi haya yanasema juu ya pahali Mungu anapokaa; watu wengine wanawaza juu ya mbingu za nyota. Watu wale wanafikiri ni katika mbingu za nyota Shetani anapoweza kukaribia Mungu. Lakini watu wote wanakubali kwamba kiti cha ufalme wa Mungu hakichafuwi na zambi kamwe.

Kusudi moja la kufa kwa Kristo lilikuwa kuwezesha kupatanishwa kwa watu na vitu kwa Mungu. Kwa kufanya hivi ilimpasa kuondosha kitu kile kili-chokuwa sababu ya uadui na ufarakisho. Alifanya hivi kwa njia ya kubeba hukumu ya zambi msalabani, na kutuliza Mungu kabisa.

Ndani ya Wakolosayi 1, tunaona eneo la upatanisho. (1) Wote wanaoamini Bwana Yesu Kristo wamekwisha ku-

patanishwa na Mungu (sh. 21). Hata kama kazi ya upatanisho ya Kristo inatosha kwa watu wote, inafaa kwa watu wale tu ambaa wanaopokea faida yake wao wenyewe. (2) Mwishoni vitu vyote vitapananishwa, vitu duniani au mbinguni (sh. 20). Shairi hili linasema juu ya nyama, na vitu visivyo na uzima vilivyochofuwa na zambi. Lakini halisemi juu ya Shetani, wala malaika waliofanya zambi, wala watu wasio-amin. Maandiko Matakatifu yanaonyesha wazi maangamizi ya milele.

Hatusomi juu ya upatanisho wa "vitu vilivyo chini ya dunia." Upatanisho ni mbalimbali na kutiishwa. Tunasoma juu ya kutiishwa ndani ya Wafilipi 2:10: "hata kwa jina la Yesu kila goti lipigwe, la vitu vya mbinguni na vya duniani, na chini ya dunia." Mwishoni viumbe vyote, hata malaika walioanguka, watalazimishwa kuinama mbele ya Bwana Yesu, lakini maana ya neno hili si kwamba watapananishwa. Wakolosayi 1:20 inasema juu ya upatanisho wa vitu duniani na mbinguni tu, si juu ya vitu "chini ya dunia." ♦

1:21 Paulo alikumbusha Wakolosayi kwamba walikwisha kupatanishwa. Mbele ya kuokolewa kwao, Wakolosayi walikuwa Mataifa na wenye zambi, **waliotengwa mbali** na Mungu, na **adui** zake katika nia zao kwa sababu ya **ubatili** wa nia zao (Efe. 4:17, 18). Walihitaji sana kupatanishwa, na Bwana Yesu Kristo, mwenye neema isiyo na kifani, alifungua njia kwa upatanisho wao.

1:22 Aliwapatanisha **katika mwili wa nyama yake, kwa kufa**. Hakufanya hivi kwa njia ya maisha yake, lakini kwa njia ya **kufa** kwake. Maana ya **mwili wa nyama yake** ni ya kwamba Bwana Yesu aliwapatanisha kwa njia ya kufa juu ya msalaba ndani ya **mwili** wa mtu (hakuwa roho, kama walimu wa Gnosticisme walivyosema). Soma Waebrania 2:14-16, pahali tunapoona kwamba

ilikuwa lazima kwa Kristo kutwaa utu ili aweze kukomboa watu. Walimu wa Gnosticisme walikataa kweli hii.

Mwisho wa ajabu wa upatanisho huu ndio **ili awalete ninyi mbele yake, watakatifu na pasipo kilema, wala laumu.** Ni neema ya ajabu kabisa kwa wenye zambi kuponyeshwa toka maisha yao maovu ya mbele na kupokewa katika hali ya baraka kubwa namna hii!

C. R. Erdman alisema vizuri: "Ndani ya Kristo tunakuta Mungu aliye karibu, anayeangalia, anayesikia, anayehurumia na anayeokoa."⁴

Kazi nzima ya upatanisho wa Kristo kwa maneno ya watu wake itaonekana kwa wakati wa kuja saa tutakaposimama mbele ya Mungu Baba, bila zambi, kipaku, au laumu, na wakati, kama wabudaji, tutakopokiri na furaha kwamba Kristo ni mwenye kustahili (Ufu. 5).

1:23 Sasa mtume Paulo aliongeza moja ya mashairi yale yanayoanza na **kama** ambayo yamefazaisha watoto wengi wa Mungu. Ni kwamba shairi hili linafundisha ya kuwa kwa kuendelea kuwa na wokovu, ni lazima kwa sisi kuendelea **katika imani.** Kama ni hivi, namna gani shairi hili linapatana na mashairi mengine ya neno la Mungu, kama Yoane 10:28, 29, yanayofundisha kwamba hakuna kondoo ya Mungu atakayeweza kupotea kamwe?

Mbele ya kujaribu kujibu ulizo hili, tunataka kusema kwamba kweli hii nzuri sana ya kuwa mwamini hawezikupotea kamwe imefundishwa wazi kabisa ndani ya Agano Jipy. Lakini pamoja na kweli hii Maandiko Matakatifu yanafundisha kila mara, kama ndani ya shairi hili, ya kama imani ya kweli ni imani inayodumu. Yanafundisha kwamba wale waliozaliwa kweli na Mungu, wataendelea na imani kufika mwisho. Ndiyo,

mara nyingine mwamini anarudi nyuma, lakini Mkristo akianguka atasimama tena (Mez. 24:16). Hataacha imani yake kabisa.

Ilipendeza Roho ya Mungu kuweka mengi ya "**kama**" mashairi namna hii ndani ya neno la Mungu, kusukuma watu wote amba wanajiita Wakristo kupima imani yao na kujiuliza kama wao ni waamini wa kweli.

Bila shaka Paulo alikumbuka walimu wa Gnosticisme wakati alipoonya Wakolosayi **wasigeuzwe mbali na tumaini la Habari Njema.** Iliwapasa **kudumu katika imani** waliyofundishwa na Epafra, na **kusimama imara juu ya msingi.**

Paulo alisema tena juu ya Habari Njema **iliyohubiriwa katika viumbe vyote chini ya mbingu.** Ndiyo, Habari Njema inatangazwa kwa viumbe vyote, lakini haijafikia kila mtu mmoja mmoja. Paulo alisema kutangazwa kwa Habari Njema katika dunia nzima ni ushuhuda kwamba ni habari za kweli zinazofaa kwa mahitaji ya watu pahali po pote. Maana ya shairi hili haiko kwamba kila mtu aliyeishi kwa wakati ule aliquwa amesikia Habari Njema. Kazi ya kuhubiri Habari Njema inaendelea hata sasa bila kwisha bado. Lakini ilikuwa imefikia inchi zote kwa upande wa Bahari ya Kati, pahali Neno la Mungu lilipokwisha kufika.

Paulo anajiita **mtumishi**, si mwalimu mkubwa, lakini mwenye kazi ya unynekevuu.

D. Utumishi Paulo aliopewa (1:24-29)

1:24 Mashairi 6 ya mwisho ya sura hii ni habari za utumishi wa Paulo. Tuniona kwanza kwamba ulikuwa utumishi pamoja na maumivu. Alikuwa gerezani wakati ule, lakini aliweza kusema kwamba anafurahi **sasa** katika

mateso yake **kwa** watakatifu, maana yake kwa ajili yao. Akiwa mtumishi wa Bwana Yesu Kristo, ilimpasa kuvumilia taabu kubwa, mateso na **maumivu**. Alifikiri maneno haya ni mapendeleo – mapendeleo ya kutimiza mateso yaliyokosa ya **mateso ya Kristo**. Maana ya masemo haya ya Paulo ni nini? Kwanza tunafahamu kwamba hasemi juu ya maumivu ya *upatanisho* ya Kristo msalabani. Maumivu haya yanakwisha kabisa, na hakuna mtu aliyeweza kushiriki ndani yao kamwe. Lakini kwa njia nyingine Bwana Yesu anateswa hata sasa. Wakati Saulo wa Tarso alipotupwa chini hata udongo, kwa njia inayokwenda Damasiki, alisikia sauti toka mbingu akisema, “Saulo, Saulo, kwa sababu gani unanitesa?” Saulo hakujuua mbele kwamba alikuwa akitesa Bwana – alikuwa akitesa Wakristo tu. Lakini alijifunza kwamba kwa njia ya kutesa waamini, alikuwa akitesa Mwokozi wao. Kichwa mbinguni anashiriki ndani ya maumivu ya Mwili wake duniani.

Hivi, Paulo aliwaza juu ya mateso yote ambayo Wakristo wanalazimishwa kuvumilia kwa ajili ya Bwana Yesu kama sehemu ya mateso ya Kristo yasiyokwisha kwanza. Ni mateso kwa ajili ya haki, mateso kwa ajili ya Bwana wao, (na kubeba laumu yake), na kwa ajili ya Habari Njema.

Lakini **mateso ya Kristo** si mateso *kwa ajili ya Kristo* tu, lakini *namna ya* mateso Mwokozi aliyovumilia wakati alipokuwa hapa duniani, lakini si kwa kipimo kikubwa kama mateso yake.

Mateso mtume Paulo aliyovumilia **katika mwili** wake yalikuwa **kwa ajili ya mwili** wa Kristo, ndilo **kanisa**. Ni kama mateso ya wasioamini hayana faida wala kusudi. Ni kama kionjo cha mbele tu cha maumivu makali sana ya Gehena ambayo watalazimishwa ku-

vumilia kwa milele. Lakini si hivi kwa Wakristo. Wakati wao wanapoteswa kwa Kristo, Kristo anateswa pamoja nao.

1:25 Nami nimefanywa mtumishi wake. Paulo alisema maneno haya ndani ya shairi 23 vilevile. Lakini sasa yana maana nyingine. Mtume alikuwa na utumishi wa namna mbili: kwanza aliagizwa kuhubiri Habari Njema (sh. 23), na neno la pili, alitumwa ku-fundisha siri ya ajabu kubwa ya kanisa (sh. 25). Haya ni mafundisho ya faida sana kwa kila mtumishi wa kweli wa Kristo. Hatuagizwi kuleta watu kwa Kristo kwa njia ya Habari Njema tu, na kuwaacha peke yao kujaribu kupata nguvu katika imani. Sivyo. Inatupasa kuwafundisha Neno la Mungu, na kuwaongoza kusimamisha makanisa namna tunavyoona ndani ya Agano Jipy, pahali waamini wa sasa wanapoweza kujengwa katika imani yao takatifu, pamoja na kujifunza juu ya kweli ya kanisa. Bwana anataka watoto wa imani kufikishwa kwa pahali wanapokulishwa na Neno la Mungu, na pahali wanapoweza kupata nguvu.

Hivi ndani ya Wakolosayi 1 tumeona kwamba (1) Kristo ana *utimilifu* namna mbili; (2) ana *upatanisho* wa namna mbili, na (3) Paulo ana *utumishi* namna mbili. Hapa ndani ya shairi 25, wakati Paulo aliposema, “**nami nimefanywa mtumishi wake**,” alisema juu ya utumishi wake kwa kanisa, si juu ya kuhubiri Habari Njema. Maneno yanayofuata yanaonyesha neno hili wazi: **Sawasawa na uwakili wa Mungu niliopewa kwa faida yenu**. Wakili ni mtu anayelinda mali au maneno ya mtu mwингine. Paulo alikuwa wakili kwa sababu alifunuliwa kweli kubwa ya kanisa. Kweli hii ilifunuliwa kwa watu wengine vilevile, lakini Paulo alichaguliwa kujulisha kweli hii ya damani kwa Mataifa.

Ilikuwa kweli ya mahali ya ukaribu wa kanisa na Kristo na maongozi ya Mungu, kanuni yake, tumaini na maisha yake, na kweli nyingi nyingine juu ya uzima na utaratibu wake ambazo Mungu alijulisha Paulo na mitume wengine.

Wakati aliposema, **niliopewa kwa faida yenu**, alifikiri juu ya Wakolosayi kama waamini Mataifa. Mtume Petro alitumwa kuhubiri kwa Wayuda, na Paulo alitumwa kwa Mataifa.

Maneno yaliyo nguvu zaidi kufahamu ndani ya sura hii ni **nitimize Neno la Mungu**. Paulo alitaka kusema nini? Hakutaka kusema kwamba alitimiza Neno la Mungu kwa njia ya kuongeza kitabu chake cha mwisho. Kitabu cha Ufunuo kiliandikwa na Yoane, ndicho kitabu cha mwisho cha Agano Jipy. Basi, kwa njia gani Paulo **alitimiza neno la Mungu?**

Inatupasa kufahamu kwamba maana nyingine ya **kutimiza** ni kutangaza na kujulisha pia. Hivi Paulo alikuwa ametangaza makusudi yote ya Mungu (Mdo. 20:27). Na alitimiza mafundisho ya neno la Mungu. Kweli kubwa ya siri ndio ufununo kubwa zaidi wa Agano Jipy. Vitabu vingine viliandikwa nyuma ya vitabu vya Paulo, lakini siri kubwa za imani ndani ya vitabu hivi vilikuwa vyote ndani ya maandiko ya Paulo vilevile. Funuo juu ya siri ya kanisa zilitimiza neno la Mungu. Hakuna kweli nyingine zilizoongezwa nyuma.

1:26 Shairi hili linaonyesha kwamba ndani ya shairi 25 Paulo alikuwa akitimiza neno la Mungu juu ya siri, ndiyo **siri iliyofichwa tangu nyakati na vizazi vyote; lakini sasa imefunuliwa kwa watakatifu wake**. Ndani ya Agano Jipy siri ni kweli isiyofunuliwa mbele, lakini sasa imejulishwa kwa watu kwa njia ya mitume na manabii wa Agano Jipy. Ni kweli ambayo watu wasiyo-weza kujua kamwe na akili yao wenye, lakini Mungu, kwa neema yake,

alikubali kuwajulisha.

Hili ni moja la mashairi mengi katika Agano Jipy linalofundisha kwamba kwa muda wa Agano la Kale watu hawakujua kweli ya Kanisa. **Ilifichwa tangu nyakati na vizazi vyote** (Efe. 3:2-13; Rom. 16:25-27). Hivi haifai kusema kanisa lilianzwa na Adamu au Abrahamu. Kanisa lilianza siku ya Pentekote, na kweli ya Kanisa ilifunuliwa na mitume. Kanisa katika Agano Jipy si Israeli katika Agano la Kale. Halikuwa kamwe mbele.

Taifa la Israeli lilianza wakati Mungu alipoita Abrahamu kutoka Uri wa Wakkaldea, na aliacha baki la mataifa kukaa kutenda zambi na kuabudu sanamu. Alianza taifa toka mzaao wa Abrahamu. Taifa hili lilikuwa namna nyingine na mataifa yote mengine, na lilikuwa mbali nao. Lakini kanisa si hivi hata kidogo. Ni kufungamana kwa waamini toka mataifa yote kuwa mwili mmoja, kwa njia ya roho na mwendo safi, mbali na watu wote wengine.

Inaonekana kwa njia mbalimbali kwamba kanisa si endeleo la Israeli. Njia moja ni mfano Paulo alilotumia wa “mzeituni” ndani ya Waroma 11 kuongesha kwamba taifa la Israeli halikugeuka, hata kama Myuda mmoja mmoja anayeamini Kristo anageuka sehemu ya kanisa (Kol. 3:10, 11).

1:27 Inawezekana kwa kweli ya **siri hii** kujumlishwa hivi: (1) Kanisa ni Mwili wa Kristo. Waamini wote wa kweli ni viungo vya Mwili, na watashiriki utukufu wa Kristo kwa milele. (2) Bwana Yesu ni Kichwa cha Mwili, na anauletea uzima, vyakula, na anauongoza. (3) Wayuda na Mataifa wanapokewa sawasawa kanisani. Wayuda na Mataifa vilevile wanageuka viungo vya Mwili kwa njia ya imani, na kufanywa mtu mpya mmoja (Efe. 2:15; 3:6). Ya kwamba Mataifa wataweza kuokolewa, haikuwa kweli iliyofichwa ndani ya Agano la Kale, lakini ya

kwamba Mataifa walioamini watakuwa viungo ndani ya Mwili wa Kristo, kuwa pamoja naye katika utukufu, na kutawala pamoja naye, ni kweli isiyofunuliwa mbele kamwe.

Neno moja la siri hii ambalo Paulo alitaka kusema juu yake zaidi ndani ya shairi 27 ni ya kwamba Bwana Yesu anakubali kupanga ndani ya moyo wa Mtaifa. **Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu.** Maneno haya yalisemwa na Wakolosayi waliokuwa Mataifa. F. B. Meyer aliandika: “Kwa Kristo kukaa ndani ya moyo wa mtoto wa Abrahamu lilikuwa tendo la wema wa ajabu. Lakini kwa Kristo kukaa ndani ya moyo wa Mtaifa ni tendo ambalo linatushinda kuamini.” Lakini hii ndiyo kweli ya siri – “ya kwamba Mataifa ni wariti pamoja nasi wa uriti mmoja, na wa mwili mmoja, na washiriki pamoja nasi wa ahadi hii katika Kristo Yesu kwa njia ya Habari Njema” (Efe. 3:6). Kuonyesha ukubwa wa kweli hii mtume hakusema tu, “siri hii” au “utukufu wa siri hii,” lakini **utajiri wa utukufu wa siri hii.** Alivimbisha masemo yake haya ili wasomaji wake waweze kufahamu na kuweka roho sana juu ya kweli hii ya utukufu.

Iliyo Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu, Kristo akikaa ndani ya mwanmini ni tumaini lake la utukufu. Yeye peke yake ni ruhusa yetu kuingia mbingu. Kristo akikaa ndani yetu anahakikisha neno hili sawasawa tunakwisha kufika mbinguni hata sasa.

1:28 Maneno haya, **ambaye tuna-mhubiri,** yana maana kubwa. Ni Bwana Yesu Kristo, kama tulivoona ndani ya shairi 27. Paulo hakupoteza saa na kuhubiri juu ya serikali na maneno mengine ya dunia. Aliweka roho juu ya kuhubiri juu ya Bwana Yesu Mwenyewe tu kwa sababu alifahamu kwamba ukristo ndio Kristo. **Tukionya kila mtu na kufundisha kila mtu na akili yote, ili tuplicate kuleta kila mtu mtimilifu katika**

Kristo. Aliweka roho juu ya kufundisha mtu mmoja mmoja. Alionya wasioamini juu ya gazabu ya kuogopesha ambayo itawapata, na alifundisha watakatifu kweli kubwa za imani ya Wakristo.

Tunaona vilevile kwamba aliweka roho sana juu ya kufundisha watu amba walikwisha kuamini kwa sababu ya mahubiri yake. Hakufurahi kwa watu kuokolewa tu, na kuwaacha kuendelea peke yao bila mwongozi. Alitaka **kuleta kila mtu mtimilifu katika Kristo.** Paulo aliwaza juu yake mwenyewe kama kuhani akitolea Mungu zabihu. Zabihu zake ni wanaume na wanawake. Aliwatolea kwa Bwana na hali gani? Wazaifu, au watoto wachanga? Sivyo, anataka wawe Wakristo wanaokwisha kupata nguvu na kukomea. Anataka waweze kusimama imara katika kweli. Sisi tuna mzigo namna hii rohoni kwa watu tuliofikisha kwa Mwokozi?

1:29 Ni kwa kusudi hili alijitaabisha, na mitume wengine vilevile. Lakini alifahamu kwamba hakufanya hivi kwa nguvu yake mwenyewe, lakini **kwa kadiri ya kutenda kazi kwake anayetenda kazi ndani yake kwa nguvu.** Alifahamu kwamba aliweza kutumikia Bwana tu kama akiwezeshwa naye. Alifahamu kwamba Bwana alikuwa **aktienda kazi ndani yake kwa nguvu** wakati aliposafiri pahali mbalimbali akisimamisha makanisa na kufundisha watakatifu wa Mungu.

E. Kristo anatosha kuonyesha

hatari ya mafundisho ya uwongo juu ya elimu, kushika sheria, mafundisho ya siri, na kujinyima vitu kwa ajili ya damiri (2:1-23)

2:1 Shairi hili linafungana na mshairi mawili ya mwisho ya sura 1. Pale alionyesha kwamba alijaribu sana, kwa njia ya kufundisha na kuhubiri, kuleta kila mtu mtimilifu katika Kristo. Hapa ndani ya 2:1 **alishindana sana** vilevile,

na maombi, lakini juu ya neno lingine. **Alishindana sana** kwa ajili ya wale ambao hakukutana nao kamwe. Tangu siku ya kwanza aliposikia habari za Wakolosayi aliwaombea, pamoja na **wale katika Laodikia**, mji uliokuwa karibu na Kolosayi, na kwa Wakristo wengine asiokutana nao bado (ona Ufu. 3:14-19 juu ya hali ya huzuni ya kanisa lile kwa wakati wa nyuma).

Shairi 1 linafariji Wakristo wale wasiobarikiwa na zawadi ya kufundisha neno la Mungu kwa makutano ya watu. Linatufundisha kwamba tunaweza kutumikia Bwana peke yetu, tukipiga magotia maombi ndani ya vyumba vyetu. Na kama tukipata njia kutumikia Bwana mbele ya watu, mahubiri yetu yatakuwa na uwezo kwa kipimo tulichoabudu na kusifu na kuomba Bwana peke yetu.

2:2 Ndani ya shairi hili tunaona maneno Paulo aliyoomba. Aliomba kwanza **mioyo yao ifarijiwe**. Wakolosayi walikuwa katika hatari ya kudanganywa na walimu wa uwongo wa Gnosticisme. Hapa maana ya **kufarijiwa** ni kusimamishwa imara au kupatishwa nguvu.

Sehemu ya pili ya ombi hili ni **wanganishwe pamoja katika mapendo**. Waamini wakishirikiana pamoja na mapendo, wanaweza kufungana pamoja kushindana na nguvu na adui. Na wakiwa na mapendo mioyoni mwao kwa Kristo, atawafunulia kweli za ndani ya imani ya Wakristo. Tunaona tena na tena ndani ya maandiko ya kwamba Bwana anafunua siri zake kwa wale wanaokaa karibu naye. Kwa mfano Yoane alikaa kwa kifua cha Yesu, na hatushangai kuona ya kwamba alipewa vilevile ufunuo mkubwa wa Yesu Kristo.

Halafu Paulo aliomba vilevile wapate **utajiri wote wa kufahamu kwa hakika**. Kwa kipimo walichoendelea katika ufahamu wa imani ya Wakristo, kwa kipimo hiki wataaminishwa kwamba ni imani ya kweli. Na wakisimama imara

katika imani, hawatakuwa katika hatari ya kudanganywa na mafundisho ya walimu wa uwongo wa wakati ule.

Mwishi wa ombi la Paulo ni wapate kujuia siri ya Mungu, ndiye Baba na Kristo.

Maana ya masemo haya ya Paulo, **siri ya Mungu ... ndiye Kristo** ni nini? Aliendelea kusema juu ya kweli ya kanisa – Kristo, Kichwa cha Mwili, na waamini wote, viungo vya Mwili. Lakini sehemu ya siri hii anayowaza juu yake zaidi ni ukubwa wa Kristo kama Kichwa. Anataka sana waamini wakubali kweli hii. Anajua kama wakifa-hamu ukubwa wa Kichwa chao, havatadanganywa na kukokotwa mbali na Bwana na walimu wa Gnosticisme, na walimu wa wongo nyingine.

Paulo alitaka watakatifu kujipatia faida toka Kristo, na kusaidiwa naye katika kila hatari ya gafula.

2:3 Ndani ya Kristo **hazina zote za hekima na kujuia zinafichwa**. Walimu wa Gnosticisme walijisifu juu ya kufahamu maneno mengi mengine kupita yale yanayoandikwa ndani ya ufunuo wa Mungu. Hekima yao ilipita ile inayopatikana ndani ya Kristo au ukristo. Lakini hapa Paulo alisema kwamba **hazina zote za hekima na kujuia zinafichwa** ndani ya Kristo, ndiye Kichwa. Hivi waamini hawahitaji kutafuta pahali pengine maneno yasiyoandikwa ndani ya Maandiko Matakatifu. **Hazina** ndani ya Kristo zinafichwa kwa wasioamini, na inapasa hata mwamini kujuana na Kristo karibu karibu ili aweze kuziingia.

Kuna maneno mengine ndani ya shairi hili vilevile. Hazina ya **kujuia** inapatikana ndani ya Kristo. Yeye ni kweli katika mwili. Alisema: “Mimi ni njia, na kweli, na uzima.” Hakuna kitu kilicho kweli kitakachoshindana kamwe na masemo na kazi zake. Watu wameonyesha tofauti ya **kujuia** na hekima. Kujuia ni kufahamu **kweli**, lakini **hekima** ni uwezo wa kutumika na kweli tunayo-

kwisha kujifunza.

2:4 Kwa sababu hekima zote na kujua ni ndani ya Kristo, haifai Wakristo kudanganywa na **maneno ya kushawishi** ya walimu wa uwongo. Mtu anayekosa kweli anahitaji kujaribu kupata wafuata kwa njia ya masemo ya hila na udanganyifu wake. Hii ndiyo desturi ya wazushi kila mara. Wanasi mamisha mafundisho yao juu ya mambo yanayonekana kuwa kweli. Lakini kama mtu akihubiri kweli ya Mungu, hahitaji kutegemea usemajji au masemo ya akili yake mwenyewe. Kweli haihitaji neno kujisimamia. Ni kama simba imbayo inajipigania yenyewe.

2:5 Shairi hili linaonyesha kwamba mtume Paulo alitambua kabisa magumu na hatari za Wakolosayi. Alijisawanisha na mkubwa wa askari akiangalia jeshi waliosimama mbele yake. Alifurahi sana kuona (katika **roho**, hata kama alikuwa mbali katika mwili) utaratibu na uaminifu wa imani yao kwa neno la Mungu.

2:6 Sasa aliwaonya wakae kuendelea katika imani, namna walivyoanza. **Kama mulivyopokea Kristo Yesu Bwana, mutembee vivyo hivyo ndani yake.** Ni kama mkazo hapa ni neno hili **Bwana**. Ni kusema ya kwamba waliikuwa wamekiri kwamba ndani ya Kristo walipata mambo yote ya kutosha. Hakutosha kwa kuwaokoa tu, lakini kwa maisha yao mazima. Sasa Paulo alionya Wakristo kuendelea kukiri ya kwamba Kristo ni Bwana. Haifai waende mbali naye kwa njia ya kukubali mafundisho ya watu, hata kama yakioneckana kuwa mazuri. Mara nyingi watu wanasema juu ya **mwendo** wa Wakristo. Mwendo unasema juu ya kuendelea mbele. Huwezi kuendelea mbele pamoja na kubaki nafasi unapokuwa. Ni vivyo hivyo kwa maisha ya Wakristo; au tunienda mbele, au tunarudi nyuma.

2:7 Paulo alitumia kwanza mfano wa kilimo, kisha wa ujenzi. Tuliwekewa

mashina wakati tulipookolewa. Ni kama Bwana Yesu ni udongo, na sisi tunaingiza mashina yetu ndani yake na kukulishwa naye. Neno hili linaonyesha vilevile kwamba sharti tuingizwe mashina yetu ndani kabisa, ili wakati wa tufani hatutatikiswa (Mt. 13:5, 20, 21).

Halafu Paulo aligeuka na kusema juu ya mjengo. **Kujengwa ndani yake.** Hapa tunaona Bwana Yesu kama msingi, na sisi tunajengwa juu yake (Lk. 6:47-49). Tumepewa mashina mara moja tu kwa wakati tulipookolewa, lakini tunakaa **kujengwa**.

Na kusimamishwa katika imani yenu. Neno hili **kusimamishwa** lina-weza kutafsiriwa “kuimariswa” vilevile. Ni kama neno hili linakaa kuendelea katika maisha mazima ya Mkristo. Epafra alikuwa amefundisha Wakolosayi misingi ya imani. Wakati walipoendelea ndani ya imani, kweli hizi za damani zitaingizwa kupita na kupita ndani ya roho na maisha yao. Lakini katika 2 Petro 1:9 tunaona kwamba tukikosa kuendelea na kupata nguvu katika imani tutaanza kuwa na mashaka na kupungukiwa furaha na baraka ya Habari Njema.

Paulo alimaliza maonyo haya na **musikizidi kutoa kushukuru**. Hakutaka Wakristo kuwa na miyo baridi kwa sababu ya mafundisho ya dini, lakini roho zao ziweze kufurika na sifa na mashukuru kwa Bwana kwa kweli za ajabu za Habari Njema. **Mashukuru** kwa baraka za ukristo ni dawa nzuri inayoharibu sumu ya mafundisho ya uwongo.

2:8 Sasa Paulo alikuwa tayari kutoa maonyo juu ya mafundisho ya uwongo yaliyokuwa yakihatarisha waamini wa Kolosayi. **Angalieni hata mtu asiwatege ninyi kwa elimu yake ya bure na madanganyifu yake matupu.** Mafundisho ya uwongo yanajaribu kuiba yaliyo faida kwa watu, bila kuleta maneno ya hakika kuyakomboa. **Elimu** si mbaya, lakini imageuka kuwa mbaya

wakati watu wanapajaribu kupata elimu isiyotoka kwa Bwana Yesu Kristo. Hapa elimu inasema juu ya watu wanaojaribu na akili yao wenyewe kutafuta na kufahamu maneno yale yanayofunuliwa na Mungu tu (1 Kor. 2:14). Ni mbaya kwa sababu inatukuza akili ya mtu kupita Mungu, na kuabudu kiumbe kupita Mwumba. Ni alama ya watu wa wakati wa sasa wanaojisifu kuwa wenye akili ya binadamu. **Madanganyifu matupu** ni mafundisho ya uwongo bila faida ya watu ambayo wanapitisha kwa watu fulani tu wanaojisifu juu ya kugeuka “wafuata wao wachaguliwa.”

Elimu ya bure na madanganyifu matupu ambayo Paulo alishindana nayo ni **desturi ya watu, kwa maneno ya ulimwengu, wala si kwa Kristo.** Maana ya **desturi ya watu** ni mafundisho watu waliyosimamisha bila kuwa na msingi wa kweli ndani ya Maandiko. **Maneno ya ulimwengu** ndiyo utaratibu wa dini kwa njia yao watu walitaraji kupendeza Mungu.

Paulo alitaka Wakolosayi kupima mafundisho yote kuona kama yalipatana na mafundisho ya **Kristo**.

2:9 Ni ajabu kuona namna Paulo alivyokaa kurudisha wasomaji wake kuwaza juu ya Kristo. Shairi hili ni moja la mashairi bora zaidi ndani ya Biblia yanayoonyesha bila shaka ya kwamba Bwana Yesu Kristo ni Mungu. **Maana katika yeye unakaa utimilifu wote wa Mungu kwa mwili.** Ona namna alivyovimbisha masemo kuhakikisha ya kwamba Kristo ni Mungu. Kwanza alisema juu ya uungu wake: “Maana katika yeye unakaa ... **Mungu kwa mwili.**” Neno la pili, alisema, “Maana katika yeye unakaa *utimilifu* ... wa Mungu kwa mwili.” Mwishoni, alisema juu ya ukamilisho wa uungu: Kwa maana ndani yake unakaa **utimilifu wote wa Mungu kwa mwili.**” (Hii ni njia nzuri kujibu namna nyingi za mafundisho ya uwongo wa wakati wa sasa.)

Vincent alisema: “Shairi hili linaonyesha maneno makubwa mawili: (1) Uungu wa kutimia unakaa ndani ya Kristo kwa milele ... ; (2) Uungu wa kutimia unakaa ndani yake ... akiwa na mwili wa mtu.”⁵ Nyingi za dini za uwongo zinakubali kwamba nusu ya uungu unakaa ndani ya Yesu. Shairi hili linaonyesha wazi kwamba **utimilifu wote wa Mungu** unakaa naye, ndani ya utu wake. Hivi ni wazi kabisa – kama mambo yote yakipatikana ndani ya Bwana Yesu Kristo, kwa nini tunakubali kushibishwa na mafundisho ambayo yanamzarau au kumwona bure?

2:10 Mtume alikaa kujaribu sana kuingiza ndani ya ufahamu wa wasomaji wake kwamba Bwana Yesu Kristo anatosha kabisa kwa mahitaji yao yote, na kwamba wametimilika **ndani yake.** Kwa shairi 10 kufuata shairi 9 ni alama ya neema ya ajabu ya Mungu. Utimilifu wote wa Mungu unakaa ndani ya utu wa Kristo, na mwamini **anatimilika ndani yake.** Si kusema kwamba utimilifu wote wa Mungu unakaa ndani ya mwamini. Neno hili lilikuwa kweli na litakuwa kweli kwa milele, kwa Mmoja tu, ndiye Bwana Yesu Kristo. Lakini shairi hili linafundisha kwamba ndani ya Kristo mwamini anapata maneno yote anayohitaji kwa maisha mema na ya utawa.

Sisi tumetimilika ndani ya huyu aliye **kichwa cha falme zote na mamlaka.** Walimu wa Gnosticisme walifikiri sana juu ya malaika. Tutasoma tena nyuma juu ya neno hili ndani ya sura hii. Lakini Kristo ni juu kupita malaika zote, na si faida hata kidogo kwa sisi kuweka roho juu ya malaika wakati tunapoweza kuabudu na kufurahia Mwumba wa malaika.

2:11 Tohara ni kawaida ya Wayuda. Ni kupasula kidogo na kisu mwili wa mtoto mwanamume. Ni mfano wa mauti ya tabia ovu na ya kuoza kwa mwili wa mtu asiyezaliwa tena bado. Lakini ni

huzuni kwa sababu Wayuda waliweka roho juu ya tendo la tohara bila kumkumbuka maana yake. Walijaribu ku-pendeza Mungu kwa njia ya kawaida ya dini na matendo mema, lakini kwa njia hii walisema kwamba kuna neno ndani ya tabia ya mtu linaloweza ku-pendeza Mungu. Neno hili si kweli hata kidogo.

Ndani ya shairi hili hatusomi juu ya tohara ya mwili, lakini juu ya **tohara** ya roho ya kila mtu aliyeamini Bwana Yesu. Maneno haya **tohara isiyofanyika kwa mikono** yanaonyesha neno hili wazi. Shairi hili linafundisha kwamba kila mwamini anatahiriwa **kwa tohara ya Kristo. Tohara ya Kristo** inasema juu ya mauti yake juu ya msalaba wa Kalvari. Wakati Bwana Yesu alipokufa, mwamini alikuifa vilevile. Alikufa kwa zambi (Rom. 6:11), kwa sheria, kwa kutaka kwake mwenyewe (Gal. 2:20), na kwa dunia (Gal. 6:14). (Tohara hii haikufanywa “kwa mikono,” maana yake mikono ya mtu haikuweza kushiriki ndani yake kwa njia ya kufanya neno la ustahili. Mtu hawezi kufanya kitu kustahili kuipata. Ni kazi ya Mungu.) Hivi anakwisha **kuondosha mwili wa zambi za nyama**. Hivi wakati mtu anapookolewa anaunganishwa na Kristo katika kufa kwake, na anaacha kutumaini kujipatia wokovu kwa njia ya kazi za nyama.

2:12 Halafu Paulo aliachaka kusema juu ya tohara na alianza kusema juu ya **ubatizo**. Tohara inasema juu ya mauti ya mwili, na **ubatizo** unasema juu ya kuzikwa kwa mtu wa zamani. Hivi tunasoma: **Mukizikwa pamoja naye katika ubatizo, na katika huu mulifufiliwa pamoja naye kwa kuamini nguvu za Mungu, ambaye alimfufua toka wafu**. Shairi hili linafundisha kwamba hatukufa tu pamoja na Kristo, lakini **tulizikwa pamoja naye** vilevile. Ubatizo wetu ni mfano wa neno hili. Neno hili lilitokea wakati tulipooko-

lewa, lakini tulilikiri mbele ya watu wakati tulipoingia ndani ya maji na kubatizwa. Ubatizo ni maziko, maziko ya hali yetu kama watoto wa Adamu. Kwa njia ya ubatizo tunakiri kwamba ndani yetu hakuna kitu kinachowezu ku-pendeza Mungu kamwe, na hivi tunandonsha mwili wetu wa zambi toka macho ya Mungu kwa milele. Lakini maziko si mwisho wa neno hili. Zaidi ya kusulibishwa na Kristo, na kuzikwa pamoja naye, tumefufuliwa pamoja naye vilevile ili tuweze kutembea katika uzima mpya. Maneno haya yote yanatukia saa tunapookolewa. Ni kwa njia ya **kuamini nguvu za Mungu, ambaye alifufua Kristo toka wafu**.

2:13 Sasa Paulo alionyesha maana ya maneno haya yote kwa Wakolosayi. Mbele ya kuokolewa kwao walikuwa **wafu** kwa sababu ya **makosa** yao. Walikuwa kama wafu kwa Mungu rohoni sababu ya zambi zao. Si kusema ya kwamba roho zao hazikuwa na uzima, lakini ya kwamba hawakuwa na hamu kwa Mungu, na hawakuweza kufanya neno lo lote kumpendeza. Hawakuwa **wafu katika** zambi tu, lakini Paulo alisema vilevile juu ya **kutokutahiriwa** kwa **mwili wao**. Mara nyingi ndani ya Agano Jipyta Mataifa waliitwa **wasiotahiriwa**. Wakolosayi walikuwa Mataifa mbele. Hawakuwa ndani ya jamaa ya dunia ya Mungu, ndio Wayuda. Hivi walikuwa mbali na Mungu, na walijitoa kwa tamaa na matendo yao ya mwili. Lakini wakati waliposikia Habari Njema na kuamini Bwana Yesu Kristo, walikuwa **wamefanywa hai pamoja** na Kristo, na **makosa** yao yote **yalisamehewa**. Namna ya mwenendo wa Wakolosayi ilikuwa imegeuka kabisa. Maisha yao ya mbele kama wenye zambi yalikwisha, nao walikuwa vi-umbe vipyta ndani ya Kristo Yesu. Walikuwa wamefufuliwa, na iliwapasa kuachana na maneno yote ya zambi yaliyokuwa desturi zao mbele kama

watu wa mwili.

2:14 Halafu Paulo aliendelea kusema juu ya neno lingine lililokuwa sehemu ya kazi ya Kristo. **Akikwisha kuzima hati ile iliyoandikwa ya kuttushitaki kwa hukumu zake, iliyo-kuwa na uadui kwetu, akaiondoshana kuifunga kwa msalaba na misumari. Hati ile iliyoandikwa ya kuttushitaki** inasema juu ya sheria. Ndiyo, Amri Kumi zilituhukumu kwa sababu hatukuzitii kabisa. Lakini mtume Paulo hakuwaza juu ya Amri Kumi tu, lakini juu ya kawaida za matendo ya kuabudu ambayo taifa la Israeli walipewa. Kuiliwa na maagizo juu ya kushika siku takatifu, vyakula, na maagizo mengine ya dini. Maagizo haya yote yalikuwa sehemu ya dini ya Wayuda. Yalitazamia mbele kwa wakati wa kuja kwa Bwana Yesu. Yalikuwa kivuli cha Bwana Yesu na kazi yake. Wakati alipokufa msalabani, **aliondosh**a maneno haya yote na kuyafunga **kwa msalaba** wake na misumari, na kuyazima namna deni inavyozimwa saa inapokwisha kulipwa. Kama Meyer alivyosema, “Kwa njia ya kufa kwa Kristo msalabani, sheria ili-yohukumu wapotevu haikuwa na amri tena kuwaazibu, kwani kwa njia ya kufa kwake msalabani Kristo alibeba laana ya sheria kwa pahali pa watu, na alitimiza sheria.”⁶ Kelly alijumlisha maneno haya hivi: “Sheria haikufa, lakini sisi tume-kufa kwa sheria.”

Tunawaza Paulo alikumbuka desturi ya zamani ya watu, ndiyo kufunga karatasi ya deni iliyo hakikisha kwamba deni fulani ilikwisha kulipwa, kwa pahali watu wote walipoweza kuiona.

2:15 Kwa njia ya kufa kwake msalabani na ufufuko wake na kupanda kwake mbinguni, Bwana Yesu alishinda vilevile **mamlaka** maovu, **akazionyesha waziwazi** na **kuzishangilia**. Tunafikiri habari za kushinda huku zili-andikwa vilevile kwa Waefeso 4:7 pahali tunaposoma juu ya Bwana Yesu

akifunga kifungo. Kwa njia ya mauti, kuzikwa, ufufuko, na kupanda mbinguni alishinda kabisa majeshi yote ya Gehena na ya Shetani. Wakati alipopita hewa kwendea mbingu, alipita kwa pahali mfalme wa uwezo wa anga anapotawala sasa (Efe. 2:2).

Labda habari hizi zilifarji zaidi wale waliotawaliwa na pepo wabaya mbele ya kuokolewa, na waliokaa kuogopa pepo wabaya. Hatuhitaji kuwa na woga tukiwa Wakristo, kwa sababu Kristo anakwisha **kuondosh**a **falme na mamlaka**.

2:16 Mtume Paulo alisema tena maneno aliyo sema sasa tu. Tunaweza kujumlisha maneno haya hivi: Wakolosayi walikuwa wamekufa kwa njia zote walizajaribu kupendeza Mungu na kazi za mwili. Hawakufa tu, lakini walikuwa wamezikwa pamoja na Kristo na kufufuliwa kwa namna mpya ya uzima. Hivi haifai wawe na maneno tena kwa milele na walimu wa sheria na Gnosticisme ambao walijaribu kuwarudisha kwa maneno waliyokufia. **Basi mtu asiwahukumu ninyi katika vyakula na vinywaji, au kwa sababu ya siku kubwa, au mwezi mwanadamo au siku ya sabato.** Dini zote za dunia zinaingiza watu ndani ya utumwa na kuwalazimisha kutii maagizo na amri na siku kubwa fulani, kama siku takatifu kila mwaka, siku ya sabato kila juma, na mwezi mpya. Maana ya semo “**Basi mtu asiwahukumu ninyi**” ni ya kwa-mba haiwezekani kwa Mkristo kuhukumiwa na haki kwa sababu ya maneno mengine, kama kula nyama ya nguruwe, au kushika siku takatifu fulani. Dini nyingine za uwongo zinakataza wafuata wao kula nyama. Kwa mia za miaka Wakatoliki walikatazwa kula nyama siku ya kazi tano ya juma. Makanisa mengi yanakataza waabudaji wao kula vyakula fulani kwa muda unaotangulia sikuu ya ufufuko wa Yesu Kristo. Wengine, kama Wamor-

mon, wanakataza wafuata wao kunywa chai au kahawa. Wengine, kama wafuata wa dini ya Sabato, wanaagiza wafuata wao kushika sabato kwa kupendeza Mungu. Mkristo halazimishwi kutii magizo namna hii. Kwa kuona maelezo mengine juu ya Sheria, na Sabato, ona mafundisho kwa Matayo 5:18; 12:8; ndani ya kitabu cha kwanza, na Wagalatia 6:18 ndani ya kitabu hiki.

2:17 Maagizo ya dini ya Wayuda yaliikuwa **kivuli cha maneno ya kuja, lakini mwili ni** wa Kristo. Yalisi-mamishwa ndani ya Agano la Kale kama mfano. Sabato ilisimamishwa kama mfano wa raha ambayo waamini wote wa Bwana Yesu Kristo watakuwa nayo. Bwana Yesu amekuja sasa, hivi haifai watu kufikiri juu ya vivuli hivi.

2:18 Ni nguvu kujua maana ya shairi hili kwa sababu hatujui maneno yote ya mafundisho ya walimu wa Gnosticisme. Labda maana yake ni ya kwamba wali-jaribu kusadikisha watu kwamba yaliikuwa wanyenyekevu sana, na kwa sababu hii walikosa ukaramisu kukaribia Mungu wao wenyewe na maombi. Labda walimu wa Gnosticisme wali-fundisha kwamba inapasa kukaribia Mungu kwa njia ya malaika, na hivi kwa njia ya kujionyesha kuwa na **unyenyekevu** walikuwa wakiabudu **malaika**, si Bwana. Habari hizi zinatufikirisha Wakatoliki wengine wa wakati wa sasa. Wakatoliki hawa wanafikiri haifai wao wenyewe kuomba Mungu au Bwana Yesu, na wanaamini ni sharti kwao “kukaribia Yesu kwa njia ya Maria.” Mawazo haya yanaonekana kama **unyenyekevu usio wa kweli**, na yanaongoza watu kuabudu kiumbe. Haifai Wakristo kuruhusu mtu ye yote kuiba zawabu yao kwa njia ya kuwasukuma kutii mafundisho namna hii yasiyopatana na maandiko matakatifu. Neno la Mungu linafundisha wazi ya kwamba “mpatanishi katikati ya Mungu na watu ni mmoja, yule mtu Kristo

Yesu” (1 Tim. 2:5).

Mtume Paulo aliendelea na semo hili lisiloonekana wazi: **akijitia katika maono yake na kujivuna bure kwa akili zake za mwili**. Walimu wa Gnosticisme walisema walijua siri za ndani ndani, na kwa mtu kujifunza siri hizi, ni lazima aingizwe ndani ya chama chao. Labda nyingine za siri hizi zilikuwa maono mengi. Ndani ya dini nyingine za uwongo za wakati wa sasa watu wana-weka roho sana juu ya maono. Watu wa chama hiki walijivuna juu ya siri hizi walizojua, hivi Paulo alisema juu yao: **Kwa akili zake za mwili**. Walitenda kama wenye ukubwa kupita watu wengine, na ya kama watu hawa-wezi kuwa na furaha bila kuingia siri hizi za ndani. Kwa wakati wa sasa desturi zao zinafanana na desturi za vyama nyingine za siri. Mkristo mwenye ushirika wa karibu na Bwana yake hana saa wala huruma kwa vyama namna hii.

Neno kubwa kuona ndani ya shairi hili ni kwamba watu wale walichagua wao wenyewe desturi zao za dini. Desturi hizi hazikupatana na mafundisho ya Neno la Mungu. Hawakunyenyekeea Kristo. **Walijivuna bure kwa akili** zao za mwili kwa sababu walifanya maneno wao wenyewe waliyotaka bila ushirika na Bwana; hata hivi walionekana kama wanyenyekevu na wenyewe kushika dini.

2:19 Asiyeshika kichwa. Bwana Yesu anaitwa hapa **Kichwa** cha mwili. Maana ya “kushika Kichwa” ni kufahamu kwamba Kristo ni **Kichwa**, na kupata toka kwake vyote tunavyohitaji toka hazina yake kubwa sana, na kufanya maneno yote kwa utukufu wake. Ni kuzamia Bwana katika utukufu kutuletea vyakula vyetu, kwa kuongozwa naye, na kuwa na upatano naye. Maneno yana-yofuata yanaongeza maelezo mengine: **kwa ye ye mwili wote ukisaidiwa na kuuganishwa pamoja kwa viungo na mishipa, unakua kwa maongezo ya Mungu**. Vipande vya mwili wa mtu vi-

nafungwa pamoja na **viungo na mishipa**. Halafu mwili unafungwa na kichwa. Mwili unatazamia kichwa ku-uongoza. Hili ndilo neno ambalo mtume Paulo alisema juu yake hapa na nguvu. Inapasa viungo vya Kristo hapa duniani kupata kushibishwa na kutulizwa ndani yake; haifai waache mabishano ya walimu hawa wa uwongo kuwavuta kwao.

Kushika Kichwa kunaonyesha wazi kwamba tunahitaji kutegemea Bwana kila dakika. Maneno aliyofanya jana kutusaidia hayatoshi kwa leo. Lakini Wakristo wakishika Kichwa, matendo yao yatapatanishwa vilevile na matendo ya viungo vingine vya mwili.

2:20 Maneno ya ulimwengu ndani ya shairi hili yanasema juu ya kawaida na amri za dini. Kwa mfano, kawaida za Agano la Kale zilikuwa kama mwanzo wa **mafundisho** ya dini duniani (Gal. 4:9-11). Labda Paulo alifikiri vilevile juu ya kawaida na amri za Gnosticisme na dini nyingine, na watu wengine ambao walijinyima hata vitu vya halali. Basi Wakolosayi walikuwa **wamekuufa pamoja na Kristo**, hivi Paulo ali-wauliza kwa sababu gani walitaka **kujittia chini ya amri** namna hii. Wakifanya hivi, wangeonyesha kwamba walikuwa wamesahau ya kuwa hawakufungani-shwa na dunia tena. Labda wengine wangeuliza: “Mkristo akiwa mfu kwa kawaida zile, kwa sababu gani anati amri za ubatizo na karamu ya ukumbusho wa Bwana?” Jibu wazi kwa ulizo hili ni: Amri hizi mbili za kanisa la Wakristo zinafundishwa ndani ya Agano Jipy. Lakini kazi yao si kutusaidia kustahili kupita kuweza kufika mbinguni, au kwa kupata ukubali mbele ya Mungu. Ni matendo ya kutii Bwana kuonyesha uthibitisho wao na Kristo, na kukumbuka mauti yake. Si maagizo ambayo tunalazimishwa kutii, lakini mapendeleo ambayo tunaweza kufurahia.

2:21 Paulo aliuliza ndani ya shairi 20 kwa sababu gani, hata kama wakiishi

duniani, walikaa kunyenyeka maagizo namna yale katika sh. 21, **Musishike, musionje, musiguse?** Ni shangao kwa sababu watu wengine walifundisha kwamba Paulo *alikataza* Wakolosayi kushika, kuonja au kugusa! Sivyo. Hii si maana ya shairi hili hata kidogo.

2:22 Shairi hili linaendelea kuonyesha kwamba haya yalikuwa **maagizo na mafundisho ya watu**. Dini ya hakika si kuweka roho juu ya vyakula na vinyweo, lakini juu ya Kristo mwenye uzima.

2:23 Matendo haya ya dini za watu **yanaonekana ya kwamba yana hekima katika kuabudu kwa mapenzi yao wenye**, na katika **unyenyekevu**, na katika kutawala **mwili** kwa ukali. Maana ya **kuabudu kwa mapenzi yao wenye** ni ya kwamba watu wale wana utaratibu wao wa kuabudu usiopatana na Neno la Mungu. Wanaonekana kama watu wa dini, lakini si wenye ibada ya Wakristo. **Unyenyekevu usio kweli** umeelezwa mbele. Walitenda sa-wasawa hawakustahili kukaribia Mungu wao wenye, hivi walimfikia kwa njia ya malaika. Walitesa **mwili** na kujinyima maneno mengine wakifiki kwamba kwa njia hii waliweza kuwa watakatifu kupita. Hii ni desturi ya Hindouisme na ya dini nyingine za inchi za mashariki.

Maneno haya yana faida gani? Jibu zuri zaidi ni lile tunaloona ndani ya sehemu ya mwisho ya shairi hili: **Hayafai kitu kwa kuzuiza tamaa za mwili**. Maneno haya yote yanaonekana vizuri kwa macho, lakini hayawezi kuzuiza **tamaa za mwili**. Hakuna kawaida ya uwongo ya kuabudu inayoweza kugeuza watu kuwa wema kupita. Zinafikirisha watu kwamba kuna mambo wao wenye wanayoweza kufanya kustahili ukubali wa Mungu, lakini hawawezi kuzuiza tamaa za mwili. Nia ya Wakristo ni ya kwamba tumekufa kwa tamaa zote za mwili, na ya kwamba kuanza sasa tu-

naishi kwa utukufu wa Mungu. Hatufanyi hivi kwa sababu tunaogopa azabu, lakini kwa sababu ya mapendo kwa Mwokozi ambaye alijitoa kufa kwa ajili yetu. A. T. Robertson alisema vizuri: "Kwa sababu ya mapendo tuko huru kuteenda yaliyo haki. Mapendo yanatusaidia kuchagua vizuri. Ni mapendo yanayogeuzza kazi ya bidii kuwa kitu cha kupendeza."

2. WAJIBU WA MWAMINI KWA KRISTO MWENYE SIFA (Sura 3, 4)

A. Uzima mpya wa mwamini: Kuondosha mtu wa zamani na kuvaa mtu mpya (3:1-17)

3:1 Basi mukiwa mumefufuliwa pamoja na Kristo, tafuteni maneno yaliyo juu, pahali Kristo yuko, akiketi mkono wa kuume wa Mungu. Ndani ya sura 2 tuliona kwamba mwamini alikuwa amekufa pamoja na Kristo, amezikwa pamoja naye, na amefufuliwa pamoja naye toka wafu. Maana kwa roho zetu ya maneno haya ni ya kwamba tumeagana na desturi za maisha yetu ya mbele, na tumeanza maisha namna mpya kabisa, maisha ya Bwana Yesu Kristo. Kwa sababu **tumefufuliwa pamoja na Kristo**, ingetupasa **kutafuta maneno yaliyo juu**. Tungali duniani, lakini ingetupasa kujuana na maneno ya mbingu.

3:2 Haifai kwa Mkristo kuwaza juu ya maneno ya dunia tu. Haifai aone maneno namna yanavyoonekana kwa macho yake ya mwili tu, lakini kwa maana yao kubwa kwa Mungu na kwa milele. A.T. Robertson aliandika: "Mtu anayekwisha kubatizwa sasa ni Mkristo anayetazamia mbingu na kuwaza juu ya mbingu. Miguu yake inasimama duniani, na anaishi duniani kama mwenyeji wa mbingu."⁷

Kwa wakati wa Vita ya Pili ya Dunia Mkristo wa sasa alijulisha Mkristo wa kukomea, "Ni kama bombardiers zi-

likuwa juu ya miji ya adui tena jana usiku." Mwamini wa kukomea alijibu, "Sikujua kwamba kanisa la Mungu lilikuwa na bombardiers." Ni wazi kwamba mwamini huyu alifikiri neno hili na mawazo ya Mungu, na hakufurahia uharibifu wa wanawake na watoto.

F. B. Hole alieleza wazi:

Mfano wa umaja wetu na Kristo, ndani ya kufa kwake, ni umaja wetu naye ndani ya ufufuko wake vilevile. Tukio la kufa kwake linatutenga na maneno ya dunia ya watu, na dini za watu, na hekima ya watu. Ufufuko wake unatukutanisha na Mungu na maneno yake yote. Mashairi mane ya kwanza ya sura 3 yanatufunulia hali ya baraka hii.⁸

3:3 Wakati Paulo aliposema mwamini **amekuifa**, anasema juu ya pahali pake, si juu ya mazoeo yake. Kwa sababu tumefunganishwa na Kristo ndani ya mauti yake, Mungu anataka tujihesabu kuwa **wafu** pamoja naye. Miyo yetu ni tayari saa zote kushindana na neno hili, kwa sababu roho zetu ni hai na zinajaribiwa mbio na zambi. Lakini ni ajabu ya kuwa wakati kwa imani tunapoijihesabu kuwa wafu pamoja na Kristo, neno hili linageuka neno la hakika ndani ya maisha yetu. Tukiishi kama watu waliokwisha kufa, maisha yetu yatakananishwa kupita na kupita na maisha ya Bwana Yesu Kristo. Ndiyo, hatutafikia ukamilifu kamwe tungali na uzima duniani, lakini ingepasa kila mwamini kuendelea na kufanana na Bwana Yesu kupita na kupita.

Tumekufa pamoja na Kristo, lakini zaidi ya neno hili **maisha yetu yamefichwa pamoja na Kristo katika Mungu**. Maneno ambayo watu wa dunia wanaweka roho juu yao, yanapatikana ndani ya ulimwengu pahali tunapoishi. Lakini maneno yaliyo na maana zaidi kwa mwamini yanafungana

na Bwana Yesu Kristo. Hakuna neno ambalo litatutenga naye kwa milele. Wazo la Paulo ni kwa sababu **maisha yetu yamefichwa pamoja na Kristo katika Mungu**, haifai tuweke roho na saa juu ya maneno hafifu ya dunia hii, na zaidi juu ya dini za watu.

Lakini maneno haya **maisha yenu yamefichwa pamoja na Kristo katika Mungu** yanatufahamisha neno lingine vilevile. Watu wa dunia hawawezi kuona uzima wetu wa roho. Hawatufahamu. Wanafazaika kwa sababu gani hatuishi namna wao wanavyoishi. Hawafahamu mawazo yetu, makusudi yetu, wala desturi zetu. Tunasoma juu ya Roho Mtakatifu ya kwamba dunia “haimwoni, wala kumjui.” Ni vivyo hivyo na maisha yetu ya roho; **yamefichwa pamoja na Kristo katika Mungu**. Ndani ya 1 Yoane 3:1 imemandikwa: “Kwa sababu hii dunia haitutambui, kwa sababu haikumtambua ye.” Tunatengwa na dunia kwa sababu dunia inakosa kufahamu mwamini.

3:4 Mtume alitimiza habari zake juu ya sehemu ya mwamini ndani ya Kristo kwa njia ya kusema juu ya kurudi kwa Kristo. **Wakati Kristo, aliye uzima wetu atakapofunuliwa, ninyi vilevile mutafunuliwa pamoja naye katika utukufu.** Kwa wakati wa sasa tumefufuliwa pamoja naye, na tunafurahi na maisha watu wasiyoona wala kufahamu. Lakini kwa wakati wa kuja Bwana Yesu atarudi kwa watakatifu wake. Kwa wakati ule tutaonekana **pamoja naye katika utukufu**. Halafu watu watatufahamu, na sababu ya mwenendo wetu.

3:5 Ndani ya shairi 3 tuliamiwa kwamba tumekufa. Hapa ndani ya shairi 5 tunaagizwa **kuua viungo** vyetu **vilivyo duniani**. Ndani ya mashairi haya tunaona wazi mfano wa tofauti ya mahali ya mwamini na maisha yake. Mahali yake ndiyo ya kwamba amekufa. Kwa maisha yake ingempasa kujihesabu kuwa mfu kwa zambi kwa njia

ya **kuua viungo** vyake **vilivyo duniani**. Mahali yetu ni namna tulivyo ndani ya Kristo. Maisha yetu ndiyo namna sisi tulivyo wenyewe. Mahali yetu ni zawadi ya Mungu kwa njia ya imani ndani ya Bwana Yesu Kristo. Maisha yetu yanonyesha jibu letu kwa neema ya Mungu.

Hapa ingetupasa kuona tofauti ya sheria na neema. Mungu hasemi, “Kama ukiishi maisha bila zambi, halafu nitakupa mahali ya mauti pamoja na Kristo.” Neno hili lingekuwa sheria kwa sababu tungepokea mahali ile kwa sababu ya bidii yetu wenyewe, na tunajua hakuna mtu angaliweza kufikia mahali ile. Lakini Mungu anasema, “Ninawapa wote wanaoamini Bwana Yesu mahali ya pendeleo, bila bei, kwa macho yangu. Sasa waende na kuishi maisha yanayopatana na mwito wa heshima namna hii.” Hii ndiyo neema!

Mtume alisema ingetupasa **kuua viungo** vyetu **vilivyo duniani**, lakin **maana** ya maneno haya **haiko** kwamba inatupasa kuharibu vingine vya viungo vya mwili wetu! Alisema hivi kwa mfano, na alitumia neno hili **viungo** kusema juu ya tamaa na kuchukia namna mbalimbali ya mwili yanayotajwa hapa.

Uasherati ni zaidi tendo la mume na mke wanaolala pamoja bila sheria, zaidi watu wasiooa bado (Mt. 15:19; Mk. 7:21). **Uchafu** unasema juu ya mawazo, masemo, au matendo yasiyo safi. **Tamaa mbaya** ni tamaa ya nguvu isiyotishwa wala kuzuizwa. **Kutamani** ni kuwa na hamu kwa vitu kupita vile tulivyo navyo, labda hamu kwa kula-lana, **ndiyo kuabudu sanamu**.

Nyuma ya kusoma juu ya matendo, tunaaendelea kusoma juu ya mwanzo na sababu ya matendo haya ya zambi. Yanaanza kwa tamaa ya moyo wa mtu. Neno la Mungu linafundisha wazi kwamba hali ya kuwa kiume au kike si mbaya. Mungu aliumba watu na uwezo wa kuzaa. Lakini ni zambi wakati watu

wanapotumia maneno haya ambayo Mungu kwa neema yake aliwatoolea, kutenda upotovu na uovu uliokatazwa. Kwa wakati Paulo alipoishi, watu walitenda zambi hizi za mwili kupita zambi zote nyingine, na bila shaka ni vivyo hivyo kwa wakati wa sasa. Waamini wasiojitoa kutawaliwa na Roho Mtakatifu wanaangushwa mara nyingi kwa njia ya zambi za mwili kama uasherati.

3:6 Watu wanafikiri wanaweza kufanya zambi hizi mbaya sana bila kuazibiwa. Ni kama Mungu mbinguni ni kimya, na ukaramisu wa watu kutenda zambi unakaa kuongezeka. Lakini Mungu hazihakiwi. **Gazabu ya Mungu** inakuja **juu ya watu wa kuasi** kwa sababu ya maneno haya. Watu wanapata maumivu na ugonjwa miilini mwao wangali hai. Zaidi ya ile humkuu kali ya Mungu itawapata kwa wakati wa kuja.

3:7 Paulo alikumbusha Wakolosayi kwamba walitenda zambi hizi wakati wasipookolewa bado. Lakini kwa neema ya Mungu walisafishwa toka uchafu huu. Muda huu wa sasa wa maisha yao ulifunikwa na damu ya Kristo. Walikuwa na uzima mpya sasa umbao uliwawezesha kuishi kwa Mungu. Ona Wagalatia 5:25: “Tukiishi kwa Roho, twende kwa Roho.”

3:8 Kwa sababu walikuwa wamekombolewa kwa bei hii kubwa sana, ingewapasa **kuondosha** maneno haya yote kama vazi chafu. Zaidi ya namna chafu zote za tamaa alizotaja ndani ya shairi 5 mtume aliendelea sasa kusema juu ya machukio maovu namna namna.

Hasira ni kasirani ya nguvu. **Uovu** ni kutendea mtu mwingine mabaya au kuharibu sifa yake njema. Ni kufurahi kuona watu wengine wakiteswa. Maana ya **matukano** hapa ni masemo mabaya sana juu ya mtu mwingine. Ni kumke-meaa na masemo makali na ya jeuri. **Masemo ya haya** ni masemo machafu na mapotovu. Uchungu unaanza ndani

ya moyo wa mtu na unaonekana kwa njia hizi zilizotajwa.

3:9 Ndani ya shairi hili mtume ali-sema: “**Mumeondosha kabisa mtu wa zamani na matendo yake.**” Hivi haifai waseme wongo tena. Kusema wongo ni moja la matendo ya **mtu wa zamani**, na halifai kwa mtoto wa Mungu. Tunajaribiwa kila siku kusema au kutenda wongo, kwa njia ya udanganyifu namna namna, kama hesabu ya kulipa kodi, kujibu maulizo ya mtihani, au kupasha habari, na ni vibaya zaidi kama kwa njia ya uwongo wetu tunaumiza mtu mwininge.

3:10 Hatukuondosha tu mtu wa zamani, lakini tumeava **mtu mpya anayefanywa mpya apate ufahamu sawasawa na mfano wake ye ye ambaye ali-mwumba.** Maneno haya *mtu wa zamani* yanasema juu ya namna tulivyokuwa kama wana wa Adamu, na tabia isiyoza-liwa tena. Maneno haya **mtu mpya** yanasema juu ya mahali yetu mpya kama watoto wa Mungu. Kulikuwa na muumbo mpya, nasi ni viumbe vipyta. Kusudi la Mungu ni kwa mtu huyu mpya kukaa kufanana kupita na kupita na Bwana Yesu Kristo. Haifai tuwaze kamwe kwamba tumefikia kipimo cha kutosha, lakini tukae kukaza mwenendo kuongezeka kwa kufanana na Mwokozi kupita na kupita. Yeye ni mfano wetu, na sharti tumwige ndani ya maisha yetu. Kwa wakati wa kuja, saa tutakaposi-mama mbele ya Kiti cha Hukumu cha Kristo, hatutahukumiwa juu ya kipimo maisha yetu yalikuwa mazuri kupita ya maisha ya watu wengine, lakini kwa kipimo gani maisha yetu yalifanana na Bwana Yesu mwenyewe.

Sura ya Mungu haionekani kwa njia ya mwili wetu, lakini kwa njia ya nia na moyo iliyofanyizwa mpya. Inaonekana ndani ya maisha yetu kwa njia ya utakatifu, mappendo, unyenyekevu, upole, wema, na usamehe. (*Notes de la Ligue*

pour la Lecture de la Bible)

3:11 Ndani ya muumbo mpya ambao mtume alisema juu yake, **hapana Myunani wala Myuda, kutahiriwa wala kutokutahiriwa, mgeni wala mshenzi, mtumwa wala aliye huru; lakini Kristo ni yote na katika yote.** Tofauti ya taifa, dini, mazoea, na cheo si kitu. Kwa macho ya Mungu, waamini wote ni sawasawa, na ingepasa kuwa vivyo vivyo kanisani.

Lakini haifai tufikiri shairi hili linafundisha kwamba hakuna tofauti kanisani. Wengine wamepewa zawadi ya kuhubiri Habari Njema. Wengine ni wachungaji, na wengine walimu. Wanajume wengine kanisani ni wazee, na wengine ni watumishi.

Na vilevile haifai tufikiri tofauti zilitotajwa mbele haziko duniani kwa wakati wa sasa. Hata sasa kuna **Wayunani na Wayuda. Wayunani** ndio Mataifa yote. Na kuna **watahiriwa na wasiotahiriwa.** Maneno haya mawili yanatumiwa ndani ya Agano Jipyä kwa Wayuda na Mataifa. Labda yanasema vilevile juu ya kawaida ya tohara ya Wayuda, lakini isiyokuwa kwa Mataifa.

Hata sasa kuna **wageni** (wasio na malezi mema) na **washenzi** waliokuwa wageni wabaya zaidi. Mwishoni tuniona **mtumwa** wala aliye **huru. Huru** ndio watu wasiokuwa watumwa kamwe, lakini waliokuwa huru tangu kuzaliwa kwao. Kwa mwamini tofauti hizi si neno kubwa tena, lakini Kristo ni yote kwa mwamini, na katika yote, na kuongoza na kutawala maneno yake yote.

Askofu Ryle alisema na uhodari juu ya kweli hii:

Kristo ni yote – maneno haya matatu ni maneno makubwa zaidi ya Ukristo. Kama tukiyakubali kabisa miyoni mwetu, nafsi zetu ni safi mbele ya Mungu. ... Watu wengi wanagawia Kristo nafasi nusu ndani ya dini yao, lakini si

nafasi ambayo Mungu alikusudi kwaye kuwa nayo. Kristo peke yake si “yote na katika yote” ndani ya nafsi zao. Sivyo! Ndani ya maisha yao ni Kristo pamoja na kanisa – au Kristo pamoja na sakaramenti – au Kristo na wahubiri walioitiwa mikono – au Kristo na toba yao wenyewe – au Kristo na wema wao wenyewe – au Kristo na maombi yao wenyewe, au Kristo na weupe na wema wao, ambayo roho zao zinategemea.⁹

3:12 Ndani ya shairi 10, Paulo alisema kwamba tumevaa mtu mpya. Sasa alionyesha namna gani tunaweza kufanya hivi ndani ya maisha yetu ya kila siku. Alianza na kuita Wakolosayi **wachaguliwa wa Mungu.** Maneno haya ni juu ya kuchaguliwa kwao na Mungu ndani ya Kristo mbele ya kuwekwa msingi wa ulimwengu. Neema ya uchaguzi wa Mungu ni moja ya siri za ufuno wake. Tunaamini kwamba Maandiko yanafundisha wazi ya kuwa mwenye enzi amechagua watu fulani kuwa watu wa Kristo. Hatuamini kwamba Mungu amechagua kamwe mtu ye yote kulaaniwa kwa milele. Mafundisho namna hii yangalikana Maandiko kabisa. Pamoja na kuamini uchaguzi wa neema ya Mungu, tunaamini vilevile kwamba ni lazima kwa mtu kuchukua madaraka yake mwenyewe mbele yake. Mungu haokoi watu wasiotaka kuokolewa. Biblia inayosema “kama vile Mungu Baba aliviyotangulia kuwajua ninyi” (1 Pet. 1:2), inasema vilevile “kila mtu anayeita jina la Bwana ataokolewa” (Mdo. 2:21).

Halafu Paulo aliita Wakolosayi **watakatifu na wapendwa.** Maana ya **watakatifu** ni kwamba waliwekwa kwa Mungu, mbali na dunia, na sharti mwenendo wao uwe mtakatifu vilevile. Mapendo ya Mungu kwa sisi yanaamsha hamu ndani yetu kumpendeza ndani ya maneno yote.

Halafu Paulo alitaja maneno mengine ya roho ambayo inapasa Mkristo **kuva** kama vazi. **Moyo wa rehema** ndio roho ya huruma. **Wema** ndio roho ya mapendo kusaidia watu wengine bila ku-jifikiri mwenyewe. **Unyenyekevu** ni kuwa tayari kunyenyekezwa, na kuhesabu watu wengine kuwa wazuri kupita kujihesabu mwenyewe. **Upole** si uzaifu. Ni kuwa na roho ya nguvu kujikana mwenyewe, na kuwa na neema kwa watu wote. Vine alisema:

Watu wanazania kama mtu ni mpole, ni kwa sababu hawezি kujsaidia mwenyewe. Lakini Bwana Yesu alikuwa “mpole” kwa sababu msaada wote wa Mungu ulikuwa wake vilevile. Mpole si mtu anayetaka watu wawaze yeye ni mtu mkubwa kwa faida yake mwenyewe. Ni mwenye roho ya utulivu. Hafurahi sana siku moja, na kusumbushwa na huzuni kubwa kesho yake, kwani hajifikiri mwenyewe hata kidogo.¹⁰

Kama mwenye **unyenyekevu** “aki-kosa kiburi,” **mpole** anakosa hasira. **Uvumilivu** ni kuwa na saburi wakati wa kuumizwa na watu kwa muda mrefu. Mwenye uvumilivu ana furaha vilevile na roho nzuri kwa watu, pamoja na kudumu ndani ya mteso.

3:13 Kuchukuliana ni kuwa na saburi ambayo inatupasa kuwa nayo na desturi za namna nyininge na kuanguka kwa ndugu zetu. Wakati tunapokaa na kutumika pamoja na watu wengine, hatuwezi kuepuka kujua kuanguka kwao vilevile. Tunahitaji neema ya Mungu kuntuwezesha kuvumilia desturi za watu wengine, na vivyo hivyo ni nguvu kwa watu wengine kuvumilia desturi zetu. Lakini ni lazima kwa sisi kuchukuliana. **Kusameheana kama mtu akiwa na sababu ya kushitaki mwenzake.** Zaidi ya magomvi ya watu wa Mungu yan galitengenezwa kama wangalitii manyo haya. Tukiumizwa na mtu mwini-

ngine inatupasa kumsamehe. Lakini mara nyininge mtu aliyeumizwa atanungunika: “Lakini ni yeye ambaye alinumiza mimi ...” Ni matukio namna hii ambayo tunapaswa kusamehe. Kama mtu mwingine asingalituumiza, tusingalihitaji kumsamehe. Kama mimi ningaliumiza mtu mwingine, ingalinipasa mimi kumfikia na kuomba kusamehewa. Kuchukuliana ni kutokuuacha desturi za namna nyininge za watu kutuchokoza; usamehe ni kutokuchunga maumivu ya maneno haya rohoni. Onyo kubwa sana ndani ya shairi hili ni kwa sisi kusamehe **kama vile Bwana alivyowasamehe ninyi, ninyi mufanye vivyo hivyo.** **Kristo** alitusamehe namna gani? Alitusamehe bila sababu. Ingetupasa kufanya vivyo hivyo. Alisamehe na kusahau neno ambalo alisamehe. Ingetupasa sisi kufanya vivyo. Inafaa sisi kuiga Bwana wetu mbarikiwa kwa njia hizi mbili nzuri sana.

3:14 Hapa tunasoma juu ya **mapendo** kama vazi la inje, au mkaba, unaofunga pamoja maneno haya yote ambayo yanahitajiwa kwa mwenendo **mtimilifu** wa mwamini. Inawezekana kwa mkristo kuonyesha nyininge za njema hizi bila kuwa na mapendo ya kweli moyoni. Hivi Paulo alisema tena kwamba ni lazima kwetu kutenda lo lote kwa ndugu zetu na roho ya **mapendo**. Walimu wa Gnosticisme walifikiri elimu ni **kifungo cha utimilifu**, lakini Paulo alisema na nguvu kwamba ni **mapendo**.

3:15 Salama ya Mungu ingepasa kutusaidia kufahamu mapenzi ya Mungu **moyoni** mwetu. Tukifazaika rohoni kama ikitupasa kufanya neno fulani, tujiulize: “Nitakuwa na salama moyoni kama nikifanya neno hili?”

Shairi hili linawenza kutusaidia sana wakati tunapotaka kujua mapenzi ya Mungu juu ya neno fulani. Kama Bwana akitaka kweli ufanye neno fulani, bila shaka atakupa **salama** juu yake moyoni. Haifai uendelee na neno lenyewe

kama ukikosa salama.

Kristo alituita kufurahishwa na salama yake, watu mmoja mmoja, na kanisani vilevile. Usikose kuona maneno makubwa ya sehemu ya pili ya shairi hili: **kwa sababu yake muliitwa katika mwili mmoja**. Ingewezekana kwa sisi kuishi peke yetu mbali na Wakristo wote wengine, lakini neno hili si kusudi la Mungu. “Anaweka nyumbani walio peke yao” (Zab. 68:6). Ni shauri la Mungu kwa sisi kukutana ndani ya makanisa katika mijii au vijiji tunapokaa. Hata kama mara nyingine tunahitaji saburi kukaa pamoja na Wakristo wengine, hii ni njia ya pekee kwa Mungu kuongeza njema hizi ndani ya maisha ya Mkristo. Hivi haifai kwa sisi kuepuka madaraka yetu ndani ya kanisa letu, au kuyaacha wakati tunaposumbushwa au kukasirishwa. Inafaa kwa sisi kupatana na waamini wenzetu, na kuwasaidia ndani ya maneno yote tunayofanya na kusema.

Tena muwe watu wa kushukuru. Tunaona masemo haya tena na tena ndani ya maandiko ya Paulo. Kwa sababu gani? Ni kama Roho Mtakatifu anafikiri kuwa na roho ya **kushukuru** ni neno kubwa sana. Nasi tunaamini ni vivyo! – Si neno kubwa kwa maisha ya roho ya mtu tu, lakini kwa afya ya mwili wake vilevile. Wanganga wanafahamu sasa kweli ambayo Maandiko yamefundisha kwa miaka mingi – ya kwamba kuwa na nia ya furaha na **mashukuru** kunasaidia mwili, na kwamba masumbuko, huzuni, na roho ya kunungunika zinapunguza afya yetu. Mara nyingi tunafikiri mashukuru ni tunda la usitawi na hali yetu njema, lakini Paulo anonyesha hapa kwamba inatupasa sisi **kuchagua** kuwa na roho ya **mashukuru**. Sisi tuna sababu kupita watu wote duni-ani kuleta asante (sawanisha na Tor. 33:29). Tusipokuwa na roho ya asante, si kwa sababu tunakosa sababu kwa mashukuru, lakini kwa sababu ya roho

zetu ambazo zinajifikiri wenyewe tu.

3:16 Neno la Kristo likae kwa wingi ndani yenu kwa hekima yote, mukifundishana na kuonyana kwa zaburi na nyimbo na tenzi za roho, mukimbia Mungu kwa neema miyoni mwenu.

Shairi hili lina sehemu tatu. Kwanza, inatupasa **kuacha neno la Kristo kuka kwa wingi** ndani yetu. **Neno la Kristo** ndilo mafundisho ya Kristo ndani ya Biblia. Wakati tunapoja za miyo na nia zetu na neno lake takatifu, na kulitii ndani ya mwenendo wetu, **neno la Kristo** litakaa kabisa ndani ya miyo yetu.

Sehemu ya pili ni ya kwamba **kwa hekima yote** inatupasa **kufundishana na kuonyana**. Haya ndiyo maonyo kwa kila Mkristo juu ya namna gani kuteendea ndugu zake waume na wake Wakristo. Tuna deni karibu na ndugu zetu ya kushiriki nao elimu yetu ya Maandiko, na kuwasaidia na maonyo toka Mungu. Wakati **tunapofundishana na kuonyana** hivi, pamoja na **elimu** na mapendo, watakubali kupita kupokea masemo yetu.

Neno la tatu ni kwamba pamoja na **zaburi na nyimbo na tenzi za roho**, ingetupasa **kuimbia Mungu** kwa **neema miyoni** mwetu. **Zaburi** ndiyo maandiko ndani ya kitabu cha Zaburi. Waisraeli walizimba wakati wa kubabdu kwao. **Nyimbo** za kuabudu ziliandikwa na watu kusifu Mungu Baba au Bwana Yesu Kristo. Kwa mfano:

Kukufikiri wewe, Yesu,
Iko kutamu kwangu;
Zaidi kukuona wewe,
Na kupumzika kwako.

Nyimbo za Mungu 63

Nyimbo hizi hazikuongozwa na Mungu namna **zaburi** zilivyoongozwa. **Tenzi za roho** ziliandikwa na watu kuonyesha maneno Wakristo wanayosikia rohoni mwao. Huu ndiyo mfano wa nyimbo namna hii:

Yesu ni Rafiki yetu
anayetupenda kweli,
Tunaweza kumwambia
mahitaji yetu yote.
Nyimbo za Mungu 288

Tukitumia nyimbo hizi namna namna ingetupasa **kuimbia Bwana kwa neema** au mashukuru **mioyoni** mwetu. Vizuri tufahamu kwamba nyingi ya muziki ambayo watu wanafikiri ni nyimbo za Wakristo haipatani hata kidogo na Maandiko na zinaaibisha jina la Kristo.

Shairi 16 linafanana sana na Waefeso 5:18, 19, pahali tunaposoma: "Wala muisilwe kwa mvinyo, ndani yake ni makelele, lakini mujazwe Roho, mukisemezana ninyi kwa ninyi kwa zaburi na tenzi na nyimbo za roho, mukiimba na kushangilia Bwana mioyoni mwenu." Kwa pahali pa kusema "mujazwe Roho" Paulo alisema kwa Wakolosayi 3:16: "**Neno la Kristo likae kwa wingi ndani yenu.**" Hivi tunaona ya kwamba tunapaswa kujazwa na Roho na kujazwa na neno la Mungu ili tuweze kuishi maisha ya furaha, ya faida, na ya kuzaa matunda. Hatutajazwa na Roho kama tusipojazwi na neno la Mungu, na kujifunza neno la Mungu hakutakuwa na faida kama tusipotoa roho zetu nzima zitawaliwe na Roho Mtakatifu. Hivi tunafahamu kwamba maana ya kujazwa na Roho ni kujazwa na neno la Mungu. Ni kila siku kulisha roho zetu na Maandiko, kuwaza juu yao, na kuyatii ndani ya mwenendo wetu.

3:17 Shairi 17 linafundisha nini inapasa Wakristo kujiliza juu ya kila neno wanaloofanya. Zaidi vijana wanafazaika kama mambo gani ni mema au mabaya. Kujifunza shairi hili kwa nia kunaweza kutusaidia sana kujibu maulizo namna hii: Ninaweza kufanya neno hili **kwa jina la Bwana Yesu Kristo?** Neno hili lingemtukuza? Atawenza kubariki neno hili? Ningetaka Bwana kunikuta niki-fanya hivi wakati atakapokuja tena?

Vizuri tukumbuke kwamba inatupasa kupima matendo, na masemo yetu vile-vile na maulizo haya. Ni vizuri sana kwa Mkristo kujifunza kufanya maneno yote kwa Bwana na kwa utukufu wake. Na mtume anaongeza tena, "**Mukishukuru Mungu Baba kwa yeye.**" Kuleta asante! **Kuleta asante!** Inapasa wale waliookolewa kwa neema ya Mungu, na watakaofikia mbingu, kuwa na mashukuru daima.

B. Mwenendo wa kufaa kwa watu nyumbani mwa Wakristo (3:18 – 4:1)

Sasa, na kufika 4:1, Paulo alitoa maonyo kwa watu nyumbani mwa Wakristo. Ana maonyo kwa wake na waume, kwa watoto na wazazi, na kwa watumishi na mabwana.

MAFUNDISHO JUU YA NYUMBA YA WAKRISTO

Mungu anaweka roho sana juu ya nyumba ya Wakristo. Alikusudia jamaa kusimamia na kulinda mambo ya uzima mema. Kwa kipimo watu wanachokosa kulinda hali ya jamaa, maneno mengi ya utaratibu wa dunia yetu yanaharibika mbio. Ndani ya barua yake ya kwanza kwa Timoteo Paulo alitoa mafundisho mengi juu ya kusudi la Mungu kwa utaratibu wa nyumba ya jamaa. Kusudi lake lilikuwa kutayarisha watu kuwa viongozi kanisani sawasawa waliongoza nyumba zao vizuri.

Ndani ya mashairi yanayofuata kuna maagizo juu ya mambo yaliyo lazima kusimamisha nyumba ya jamaa walio Wakristo.

1. Sharti watu wa nyumba wakutane kwa saa fulani kila siku kusoma Maandiko matakatifu na kuomba pamoja.

2. Inapasa baba kuwa mwenye amri nyumbani, na kutumika na amri hii na hekima na mapendo.

3. Ingepasa mke wake na mama ya

watoto kufahamu kwamba kazi yake ya kwanza kwa Mungu na kwa jamaa yake ni nyumbani mwao. Si vizuri kwa mwanamke kuwa na kazi ya mshahara inje ya nyumba yao, lakini mara moja moja ni neno la lazima.

4. Sharti mume na mke wawe mfano unaotokuza Mungu kwa watoto wao. Vizuri wapatane ndani ya maneno yote, na ndani ya namna gani kufundisha watoto, na kuwaazibu wakati inapohitajiwa.

5. Ingepasa watu wa jamaa wafungane pamoja na mapendo. Inawezekana kwa wazazi kutawaliwa na kazi yao, au kuvutwa na rafiki zao wenyewe, na hata kujitoa kwa kazi ya Mungu; lakini watoto wao wanakosa mapendo, urafiki, mafundisho, na azabu. Wazee wengi wenyewe mwana au binti aliyeacha kufuata Bwana wamekiri na huzuni nyingi: “Wakati mtumwa wako alipokuwa akitenda hapa na kule, yule aka-kwenda zake” (1 Waf. 20:40).

6. Kwa maneno ya kuazibu watoto, inapasa kukumbuka maneno matatu:

- 1) Usiwaazibu kamwe saa wewe mwenyewe unapokasirika.
- 2) Usiwaazibu kamwe bila haki.
- 3) Usiwaazibu kamwe bila kueleza sababu ya azabu yenyewe.

7. Ni vizuri kwa watoto kujifunza “kuchukua nira wakati wa ujana wao” (Omb. 3:27), ndiyo kujuana na kutumika kazi, madaraka ya kazi, na thamani ya feza.

8. Zaidi ya yote, wazazi Wakristo wanahitaji kujizuiza wasisukume watoto wao katika njia ya kazi yenyewe kufurahisha mwili, sawa na watu wa dunia. Vizuri wakae kuwaonyeshea saa zote ya kwamba kutumikia Bwana ni faida kubwa kuliko kwa maisha yao. Wanawea kufanya hivi kwa njia ya kuhubiri Habari Njema kwa pahali au inchi yiningine, au kwa pahali pa kazi yao ya mshahara. Hata wakiwa pahali gani, ni lazima kuweka kazi ya Bwana kwanza,

na kukumbuka ya kuwa tunasimamia Mwokozi wetu. Sharti tumheshimu na kuongozwa naye ndani ya kila semo na tendo. ♦

3:18 Mtume alionya **wanawake** kwanza. Inawapasa **kutii waume wao kama inavyopendeza** katika **Bwana**. Ni kusudi la Mungu kwa mume kuwa mkubwa wa nyumba, na Paulo aliagiza mwanamke kunyenyeka mume wake. Haifai atawale au kuongoza, lakini afuate mwongozi wake, kama akiweza kufanya hivi bila kuasi Kristo. Ndiyo, mara nyingine haiwezekani kwa mwanamke Mkristo kutii mume wake bila kuasi Kristo. Kama ni hivi, inampasa kutii Bwana Yesu kwanza.

Kama mwanamke Mkristo akiwa na mume wa kusitasita kwa maneno ya Mungu, shairi hili linafundisha kwamba inapasa mwanamke kumsaidia ndani ya kazi yake kama mwongozi nyumbani. Haifai amtawale, hata kama labda akiwa na akili kupita mume wake.

3:19 Mtume aliendelea na kuonyesha kwamba kuna maonyo kwa **waume** vilevile ndani ya Neno la Mungu. Inawapasa **kupenda wake** wao, na **wana-katazwa kuwa na uchungu nao**. Kama wake na waume wangetii maonyo haya, kama wangekaa na salama na furaha kupita katika Bwana nyumbani mwao. Isingekuwa nguvu kwa mke kunyenyeka bwana ambaye anampenda. Hakuna agizo ndani ya Maandiko kwa mume kulazimisha mke wake kumtii. Mke akikataa kutii bwana wake, ingepasa mume kuomba Bwana juu ya neno hili. Ingepasa mke kuchagua kunyenyeka mume wake “kama inavyopendeza katika Bwana.”

3:20 **Watoto** wanaagizwa **kutii wazazi** wao **katika maneno yote, maana neno hili linapendeza** katika **Bwana**. Kwa wakati zo zote kuna maneno mwili ambayo yanafunganisha watu wa jamaa pamoja – amri na utii. Hapa tuna-

soma juu ya utii. Wanaagizwa kutii **katika maneno yote**, si maneno amba-yo yanawapendeza tu.

Ni nguvu mara nyingine kwa watoto Wakristo wenye wazazi wasio waamini kujua nini inawapasa kufanya. Wanataka kutii Bwana, lakini inawapasa kutii wazazi wao vilevile. Ni kama waki-heshimu na kutii wazazi wao, wao wenye we wataheshimiwa na Mungu. Wakati wanapokaa kwanza nyumbani mwa wazazi wao, inawapasa kuwanye-nyekea. Hata hivi haifai wafanye neno lo lote linaloasi mafundisho ya Kristo. Mara nyingi itawapasa kufanya maneno wasiyopenda kufanya, lakini kama maneno haya si mabaya au zambi, ni vizuri wayafanye kama kwa Bwana. Kwa njia hii watakuwa na ushuhuda mwema kwa wazazi wao, na kujaribu kuwaongoza kuamini Bwana.

3:21 Haifai baba wachokoze watoto wao, wasichoke katika roho zao. Ona kwamba agizo hili ni kwa **baba**, si kwa mama. Ni kama baba wanaanguka kwa neno hili kupita mama. Labda mama wanajaribiwa kuendekeza watoto kupita kipimo.

3:22 Toka shairi hili kufika mwisho wa sura tatu, Roho Mtakatifu anasema kwa watumwa. Kuna mafundisho mengi ndani ya Agano Jipyä juu ya watumwa. Neno hili linaonyesha kwamba hata kwa macho ya watu Mkristo anakosa heshima, anaweza kuendelea sana ndani ya maisha yake kwa Bwana, kwa njia ya kutii neno la Mungu na uaminifu. Labda inaonyesha vilevile kwamba Mungu alijua mbele ya kuwa zaidi ya Wakristo watakuwa watumishi, si watu wenye amri. Kuna mafundisho nusu tu ndani ya Agano Jipyä kwa watawala wa mataifa, lakini kuna maonyo mengi kwa watu wale wanaoishi kutumikia watu wengine. Kwa wakati wa Paulo watu hawakuweka roho juu ya watumwa, na bila shaka Wakristo wa kwanza walishangaa kwa sababu aliandika maneno

mengi juu yao ndani ya barua zake. Neno hili linaonyesha kwamba neema ya Mungu inagusa watu wote, si neno kama wakiwa watumishi wenye kazi ya chini sana. C. H. Mackintosh aliandika: “Mtumwa hazuizwi asitumikie Mungu. Kwa njia ya kufanya kazi yake kwa Mungu anaweza kupamba mafundisho na kutukuza Mungu” (Tit. 2:9, 10).

Watumwa wanaagizwa kutii walio bwana wao kwa maneno ya mwili katika maneno yote. Ona ya kwamba wanaagizwa kutii bwana wao **kwa maneno ya mwili** tu. Wana Bwana mwiningine aliye juu ya yote na anayeona kila neno ambalo watoto wake wanyonge zaidi wanatendewa. Haifai watumwa kufanya kazi yao na **utumwa wa macho kwa kupendeza watu, lakini na roho moja, wakiogopa Bwana.** (Kuna mfano mzuri wa neno hili ndani ya Agano la Kale, ona Mwanzo 24:33.) Wakati mtu anaposumbushwa, ni nyepesi kwa yeze kulegea kwa kazi yake wakati bwana wake si karibu. Lakini mtumishi Mkristo atafahamu kwamba Bwana wake anaangalia saa zote, hivi hata kazi yake ikiwa chungu, atafanya kazi hii kama kwa ku-pendeza Bwana tu.

Hakuna agizo wazi ndani ya Agano Jipyä kukataza utumwa. Lakini kila pahali Habari Njema ilipohubiriwa, utumwa umeondoshwa. Hata hivi maagizo haya yana maana kwa watumishi na bwana wa kazi kwa wakati wa sasa vilevile.

3:23 Inapasa kufanya kila kitu kwa moyo (ndiyo kwa roho) kama kwa Bwana, wala si kwa watu. Ndani ya kila utumishi wa Wakristo kwa Bwana, na ndani ya maisha yo yote mengine, kuna kazi namna nyingine watu wanazochukia kufanya. Tunajaribu kuepuka kazi za namna hii. Lakini shairi hili linafundisha kwamba hata kazi ya chini zaidi inaweza kutukuzwa na kuheshimiwa kwa njia ya kuifanya kwa Bwana. Hakuna tofauti kwa kazi takatifu kwa Mungu na kazi yo yote nyingine. Zote ni takatifu. Zawabu mbi-

nguni hazitakuwa kwa kazi zinazonekana sana au kusitawi, wala kwa zawadi kwa kazi fulani, lakini kwa uaminifu. Watu wale wasioonekana sana sasa watapokea zawabu kubwa siku ile kama walifanya kazi yao na uaminifu kwa Bwana. Wakristo wengine wameweka andiko hili nyumbani mwao kwa pahali pa kusukula sahani: "Kazi kwa Bwana inafanywa hapa mara tatu kila siku na furaha, bila manunguniko."

3:24 Bwana anaona kila kazi inayofanywa kwa ye ye na hatasahau hata moja. Watu wenye uriti mdogo tu duni-an **watapokea kwa Bwana zawabu ya uriti** mbinguni. Tukumbuke neno hili wakati inapotupasa kufanya neno ambalo hatupendi, kanisani, nyumbani mwetu, au kwa pahali pa kazi. Ni ushuhuda mwema kwa Kristo kama tukifanya neno lenyewe vizuri sana, bila kunungunika.

3:25 Paulo hakusema wazi kama alifikiri juu ya mtu gani ndani ya shairi hili. Labda alifikiri juu ya bwana wa kazi asiyetenda kwa haki, lakini aliyetesa watumishi wake. Labda mtumishi Mkristo amechoka na maagizo yasiyo haki ya bwana mwenyewe. Paulo alisema, "Si neno, Bwana anajua yote, naye atatengeneza vilevile mabaya uliyotendewa."

Lakini shairi hili ni zaidi kwa watumishi, hata kama ni kwa bwana za kazi vilevile. Bwana ataona vilevile kazi isiyofanywa vizuri, udanganyifu, mtumishi akikaa bure saa ya kazi, vivi hivi. Mungu hana upendeleo. Yeye ni Bwana wa wote, na tofauti katikati ya watu ni bure kwake. Watumishi wanaoiba mali ya bwana zao (ni kama Onesimo alifanya hivi), watalazimishwa kutoa hesabu kwa Bwana vilevile.

4:1 Shairi hili linaendelea na mafundisho ya shairi la mwisho la sura 3. Inapasa **bwana za kazi wawape watumwa wao yaliyo haki na sawa** kwa kazi waliyofanya. Agizo hili ni kwa bwana Wakristo. Mungu anachukia kwa

wamasikini kuteswa, na hakubali kupokea zawadi za mtu aliyegeuka tajiri kwa njia ya kunyimia watumishi wake mshahara waliostahili kupokea. Ni kama anasema: "Bakia na mali yako; sifurahi juu ya namna gani ulipata." (Ona Yak. 5:1-4). Haifai bwana wa kazi kuwa wenyewe kiburi, lakini wakae na woga. **Wao vilevile wana Bwana mbinguni**, aliye haki kwa njia zake zote.

Mbele ya kuacha sehemu hii ya mwisho ya sura 3, mtume Paulo alitukumbusha tena na tena kwamba lazima tutii Bwana Yesu Kristo ndani ya maneno haya ya kila siku: (1) Wake – kama inavyopendeza katika Bwana (sh. 18). (2) Watoto – neno hili linapendeza katika Bwana (sh. 20). (3) Watumwa – mukiogopa Bwana (sh. 22). Watumishi – kama kwa Bwana (sh. 23).

C. Maisha ya maombi ya mwamini, na ushuhuda wake kwa njia ya mwenendo na masemo (4:2-6)

4:2 Paulo hakuchoka kamwe kuonya waamini kudumu katika maombi. Bila shaka sisi sote tutahuzunishwa wakati tutakopofika mbinguni kwa sababu tulishinda saa nusu tu kwa maombi, zaidi wakati tunapoona majibu kwa maombi yetu. Kuna maneno mengi juu ya maombi yaliyo siri kwetu, maulizo mengi bila jibu. Haifai kwa sisi kujaribu kufahamu na kueleza siri kubwa za maombi. Ni vizuri zaidi kukaa kuomba na imani, bila roho ya mashaka.

Pamoja na **kudumu sana katika maombi**, inatupasa **kuangalia ndani yao**. Agizo hili linatukumbusha mara moja ombi la Bwana Yesu kwa wanafunzi katika shamba la Getesemanie: "Angalieni na kuomba ili musiingie majoribuni" (Mk. 14:38). Hawakuangalia, hivi walishindwa na usingizi. Sharti tuangalie tusishindwe na usingizi, na vilevile haifai tuache mafikiri yetu kuhangainka. Na haifai tuache maneno mengine kunyanganya saa yetu ya maombi (Efe. 6:18). Na sharti

tuombe **pamoja na mashukuru**. Inatupasa kuleta asante kwa majibu ya maombi yetu, na vilevile kwa imani tunaweza kushukuru Bwana kwa maombi asiyojibу bado. Guy King alijumlisha mawazo haya vizuri: “Mapendo ya Mungu yanataka yaliyo mema zaidi kwa sisi; hekima yake inajua yaliyo mazuri zaidi kwa sisi; na uwezo wake unatupatia yaliyo mema zaidi kwa sisi.”¹¹

4:3 Paulo aliomba Wakolosayi kumwombea yeye vilevile, pamoja na watumishi wa Bwana ambaо walikuwa pamoja naye. Ni vizuri kuona kwamba hakuomba aweze kufunguliwa toka gereza, lakini **Mungu awaze kumfungulia mlango** kwa kuhubiri **neno** lake. Mtume alitaka Mungu kumfungulia milango. Ombi hili lina mafundisho makubwa kwa sisi! Ni nyepesi kwa sisi kujifungulia milango sisi wenyewe ndani ya kazi yetu kwa Kristo. Kufanya hivi ni hatari ambayo inatupasa kuepuka. Kama Bwana akitufungulia milango, tunaweza kuingia milango hii bila woga, tukijua kwamba ni Yeye ambaye anatuongoza. Lakini tukijifungulia milango sisi wenyewe, hatuwezi kujua kabisa kwamba tunafanya mapenzi ya Mungu, na labda nyuma kidogo tunanza kufanya ‘kazi ya Bwana’ na uwezo wa mwili. Paulo aliomba aweze kufunguliwa **mlango kwa neno** aweze **kusema siri ya Kristo, kwa ajili yake alifungwa**. **Siri ya Kristo** ndani ya shairi hili ni kweli ya kanisa, na zaidi kweli ya “Kristo kwa Mataifa.” Haya yalikuwa habari ambazo Paulo aliagizwa kuhubiri. Kwa sababu ya uhodari wake kusema kwamba Mataifa wanaweza kuokolewa namna Wayuda walivyoокolewa, viongozi vya Wayuda walipata njia kumtuma kwa Roma kama mfungwa.

Kuna water wengine wanaofundisha kwamba siri kubwa ya kanisa ilifunuliwa kwa Paulo wakati alipokuwa gerezani. Hivi wanaweka roho sana juu ya barua alizoandika wakati alipokuwa gerezani (Wagalatia, Waefeso, Wafilipi na Wako-

losayi), kupita juu ya mafundisho ya vitabu vya Habari Njema na vitabu vingine vya Agano Jipy. Lakini shairi hili linaonyesha kwamba alifungwa *kwa sababu ya mahubiri yake juu ya siri hii, hivi bila shaka ilifunuliwa kwake mbele ya kufungwa*.

4:4 Alitaka sana **kuionyesha**, maana kuitangaza na masemo ambayo watu wanaweza kufahamu vizuri. Ingepasa kila Mkristo mwenye hamu kusambaza habari za Kristo, kufanya vivyo hivyo. Si faida kutumika na masemo yaliyo nguvu kufahamu. Tukitaka kugusa elfu elfu za watu wa dunia hii na Habari Njema, lazima tutiangaze na masemo yaliyo mepesi kufahamu.

4:5 Inapasa Wakristo **kutembea kwa hekima mbele yao walio injе**. Sharti wafahamu kwamba wasioamini wanaangalia matendo yao karibu karibu. Watu wa dunia wanaweka roho juu ya matendo yetu kupita juu ya masemo yetu. Sharti tushuhudie Kristo na midomo yetu vilevile, lakini sharti matendo na masemo yetu yapatane.

Maana ya **kukomboa wakati** ni kushuhudia uwezo wa kuokoa wa Bwana Yesu Kristo kila mara tunapopata njia. Neno hili “komboa” linatufahamisha kwamba mara nyingi inatupasa kulipa bei kwa kufanya hivi. Hata kama kipimo cha bei hii ni nini, ingetupasa kuwa tayari kushiriki habari za Mwokozi wetu wa damani na wale ambaо hawamjui bado.

4:6 Sharti **masemo** yetu **yawe na neema siku zote, yakinengenezwa na chumvi, ili tujue namna inavyotupasa kujibu kila mtu**. Kwa masemo yetu kuwa **na neema** saa zote, lazima yawe na adabu, unyenyekevu, na kufanana na masemo ya Kristo. Hayafai kuwa mazungumuzo hafifu, masemo ya uchafu na uchungu. Labda maana ya **kutengenezwa na chumvi** ni ya kwamba masemo yetu yawe na neema, haki, na bila unafiki. Walimu wengine wanakumbuka kwamba **chumvi** inaongeza uta-

mu wa chakula, hivi Bwana Yesu alisema kwa mwanamke aliyetenda uzini, “Wala mimi sikuhukumu; kwenda na usifanye zambi tena.” Hapa tunaona kwanza neema, “wala mimi sikuhukumu”; kisha chumvi, “kwenda, na usifanye zambi tena.” Na halafu Bwana Yesu alisema na mwanamke kwa kisima cha Yakobo, “Unipe maji ya kunywa. ... Kwenda kuita mume wako.” Maneno yake ya kwanza yanatufikirisha neema, na maneno aliyosema nyuma yanatukumbusha zaidi chumvi.

Mupate kujuua namna inavyowapasa ninyi kujibu kila mtu. Labda Paulo alifikiri hapa zaidi walimu wa Gnosticisme waliofikia Wakolosayi na mafundisho yao yaliyoonekana kwamba ni kweli. Ilipasa Wakolosayi kuwa tayari **kujibu** walimu hawa wa uwongo na masemo ya hekima na uaminifu.

D. Habari za wengine wa washirika wa Paulo (4:7-14)

4:7 Ni kama mtume Paulo alichagua **Tikiko** kupeleka barua hii toka Roma kwa Kolosayi. Maclarens alikumbuka kwamba bila shaka Tikiko angalishangaa sana kama angaliambiwa ya kwamba “barua ya karatasi namna hii ya zamani itadumu muda mrefu kupita mapambo yote ya Roma. Angalishangaa vilevile kujuua kwamba watu watasoma jina lake pahali pote duniani kwa sababu liliandikwa ndani ya barua ile.”

Paulo aliwaambia watakatifu kwamba wakati Tikiko atakapofika, atawajulisha **maneno yote** ya mtume. Ni tamu kusoma vilevile majina yote ya heshima ya Paulo kwa ndugu huyu. Alimwita **ndugu mpendwa, mtumishi mwa-minifu, na mjoli wake katika Bwana.** Tungepasa kutamani majina haya kupita majina ya kiburi viongozi vyta kanisa wanavyopewa kwa wakati wa sasa!

4:8 Tikiko alisafiri kwa Kolose na sababu mbili. Kwanza atawezeku julisha watakatifu habari za hali ya Paulo na

wale waliokuwa pamoja naye kwa Roma, na vilevile **atafariji miyo** ya Wakolosayi. Mafundisho yake atawasadia kusimama imara na kushindana na mafundisho ya uwongo yaliyoenea kwa wakati ule.

4:9 Jina la **Onesimo** linatufikirisha habari tamu Paulo alizoandika ndani ya barua yake kwa Filemono. Onesimo alikuwa mtumwa mkimbizi aliyeckimbia kwa Roma kuepuka azabu. Pale alikutana na Paulo, naye alimwongoza kuamini Kristo. Sasa Onesimo atarudi karibu na bwana wake wa mbele, ndiye Filemono, kwa Kolosayi. Atafikisha barua ya Paulo kwa Filemono, wakati Tikiko atakapofikisha barua yake kwa kanisa kwa Kolosayi. Bila shaka waamini wa Kolosayi walifurahi sana wakati ndugu hawa wawili walipofika kwao na barua hizi za Paulo! Bila shaka walikaa pamoja nao kufika hata katikati ya usiku na maulizo juu ya Roma, na kusikia habari za utumishi wa uhodari wa Paulo kwa Mwokozi wake.

4:10 Hatujui habari nyingi juu ya **Aristarko** ila ya kwamba alifungwa mbele kwa sababu ya utumishi wake kwa Bwana, ona Matendo 19:29. Sasa **ali-fungwa pamoja** na Paulo katika Roma.

Marko aliiwta **mjomba wa Barnaba** hapa. Kijana huyu alianza kutumikia Bwana pamoja na Paulo na Barnaba. Kwa sababu Marko hakudumu ndani ya kazi, Paulo alisema vizuri abaki kwake, lakini Barnaba alitaka kwa nguvu kupeleka Marko pamoja nao. Kwa sababu hii watumishi hawa wawili walitengana na hawakusafiri pamoja tena. Ni vizuri kuona kwamba nyuma ya wakati Marko alirudi kwa utumishi wa Bwana, na alikubaliwa tena na Paulo, mpendwa.

Hivi kama Marko **akifikia Kolosayi**, ilipasa watakatifu **kumpokea**.

4:11 Mtumishi mwininge aliyetu-mika pamoja na Paulo alikuwa **Yesu, anayeiwa Yusto.** Watu wengi waliiwta

Yesu kwa wakati ule. Ni vivyo hivyo ndani ya inchi nyingine hata sasa. Kwa Kiebrania Yesu ni “Yosua.” Bila shaka mtu huyu aliiwa **Yusto** kwa sababu Wakristo wengine wangefikiri haifai kuita mtu na jina lililo vilevile jina la Mwana wa Mungu.

Watuhawa watatu walikuwa wote Wayuda waliookolewa. Walikuwa watu **wa pekee** waliokuwa Wayuda mbele na **waliotenda kazi pamoja** na Paulo **kwa ajili ya ufalme wa Mungu**, na watu **ambao walimfariji**.

4:12 Wakati Paulo alipokuwa aki-maliza barua yake, **Epafra** alimku-mbusa kutuma salamu yake mwenye-we kwa watakatifu wapendwa katika Kolosayi. Epafra alikuwa mtu wa Kolosayi, na alikuwa **akiombea wa-amini** siku zote, ili **wasimame wenye kutimia na kujua sana mapenzi yote ya Mungu**.

4:13 Paulo alitoa **ushuhuda** vilevile ya kwamba Epafra hakudumu sana na maombi kwa Wakristo kwa Kolosayi tu, lakini kwa wale **kwa Laodikia na Hierapoli vilevile**. Aliweka roho sana juu ya watu wa Mungu ambao alijuana nao. Tusingeshangaa kama angewaombea wote, mmoja mmoja, kila siku.

4:14 Sasa Paulo alituma salamu kwa **Luka, mganga mpendwa, na Dema**. Watuhawa wawili walikuwa namna mbalimbali kwa roho. **Luka** alisafiri pamoja na Paulo mara nyingi, na tunafikiri alimsaidia vilevile kwa wakati wa mahitaji ya mwili na roho wakati wa ugonjwa, mateso, na gerezani.

Dema alisafiri pamoja na Paulo kwa wakati, lakini mwishoni ilipasa mtume kusema juu yake: “Dema aliniacha, akiwa amependa dunia hii ya sasa, na alikwenda hata Tesalonika” (2 Tim. 4:10).

E. Salamu na mafundisho

(4:15-18)

4:15 Halafu salamu zilitumwa kwa

ndugu waliokuwa katika Laodikia, na kwa Nimfa, na kanisa lililo katika nyumba yake. Tunasoma tena juu ya kanisa kwa Laodikia katika Ufunuo 3:14-22. Kanisa la pahali pale halikuwaka tena kwa maneno ya Mungu. Wakristo waliweka roho kwa maneno ya dunia. Waliwaza maneno yao yalitembea vizuri, lakini hawakutambua kwamba walikuwa wichi. Maandiko hayaonyeshi wazi kama barua hii iliandikwa kwa mwanaume (Nimfo) au mwanamuke (Nimfa). Inatosha kwa sisi kujua kwa-mba kulikuwa na kanisa ndani ya nyumba ile kwa Kolosayi. Kwa wakati ule Wakristo hawakukutana ndani ya jumba kubwa za mapambo mengi, kama kwa wakati wa sasa. Lakini sisi tunafikiri neno kubwa ni kwa uwezo wa Mungu kuonekana ndani ya kanisa la pahali fulani kupita kuwa na nyumba yenye mapambo kwa makusanyiko yao. Mara nyingi jumba za mapambo zinazuiza uwezo wa Mungu.

4:16 Nyuma ya kusoma barua hii kwa Kolosayi, ilipasa kuituma kwa **kanisa la Laodikia** vilevile. Bila shaka neno hili lilifanywa, lakini kwa Ufunuo 3 tunaona kwamba waamini wa Laodikia hawakutii mafundisho yake kwa wakati ule.

Paulo aliagiza vilevile **barua toka Laodikia** isomwe kwa Kolosayi. Hatuwezi kujua kwamba ilikuwa barua gani.

4:17 Arkipo aliagizwa **kuangalia sana kwa utumishi aliopewa na Bwana, ili kuutimiza**. Hatujulishwi wazi kama ulikuwa **utumishi** gani. Watuhengi wanafikiri **Arkipo** alikuwa mwana wa **Filemono**, na ya kwamba alikuwa na kazi ndani ya kanisa kwa Kolosayi. Shairi hili litakuwa na maana kubwa kupita kwa sisi kama tukikomboa jina la Arkipo na jina letu, na kama tukisikia Roho ya Mungu akisema nasi: **“Angalia sana utumishi uliopewa na Bwana, na kuutimiza.”** Bwana ametupa sisi sote, kila mtu, utumishi fu-

lani, na siku nyingine itatupasa kueleza kama tuliutimiza.

4:18 Halafu mtume alikamata kalamu ya karani **kwa mkono wake** mwenyewe na kuandika **salamu** yake na jina lake la Mtaifa, ndilo **Paulo**. Bila shaka **vifungo** kwa mikono yake vili-msumbusha wakati alipoandika, lakini vilimkumbusha kusema na Wakolosayi: **Kumbukeni vifungo vyangu**. “Sauti ya kalamu na vifungo pamoja ni alama ya mwisho kwamba haiwezekani kwa vifungo kufunga Neno la Mungu.”¹² Kisha alimaliza barua yenyewe na maneno haya: **Neema iwe pamoja nanyi. Amina.**

A. T. Robertson aliandika: “Neno hili ‘neema’ ni neno tajiri kupita maneno yote mengine, kwani linaonyesha mapendo yote ya Mungu yanayofunuliwa ndani ya zawadi ya Mwana wake kwa sisi.”¹³

NOTES

¹ (1:5) J. B. Lightfoot, *Saint Paul's Epistles to the Colossians and to Philemon*, p. 134.

² (1:14) The words “through His blood” definitely occur in the parallel passage in Ephesians 1:7.

³ (1:18) Alfred Mace, further documentation unavailable.

⁴ (1:22) Charles R. Erdman, *Epistle of Paul to the Colossians and Philemon*, p. 46.

⁵ (2:9) Marvin Vincent, *Word Studies in the New Testament*, II:906.

⁶ (2:14) F. B. Meyer, further documentation unavailable.

⁷ (3:2) Robertson, *Intellectuals*, page 149.

⁸ (3:2) F. B. Hole, *Paul's Epistles*, Volume 2, p. 105.

⁹ (3:11) J. C. Ryle, *Holiness*, pp. 436, 455.

¹⁰ (3:12) W. E. Vine, *Expository Dictionary of New Testament Words*, p. 56.

¹¹ (4:2) Guy King, *Crossing the Border*, p. 111.

¹² (4:18) *New Bible Commentary*, p. 1051.

¹³ (4:18) Robertson, *Intellectuals*, p. 211.

BIBLIOGRAPHIE

(Wakolosayi, na Filemono, Vol. 3)

Carson, Herbert M. *The Epistles of Paul to the Colossians and to Philemon*. Grand Rapids: Wm. B. Eerdmans Publishing Co., 1960.

English, E. Schuyler, *Studies in the Epistle to the Colossians*. New York: Our Hope Press, 1944.

Erdman, Charles R. *Epistles of Paul to the Colossians and Philemon*. Philadelphia: Westminster Press, 1933.

King, Guy. *Crossing the Border*. London: Marshall, Morgan and Scott, Ltd., 1957.

Lightfoot, J. B. *Saint Paul's Epistle to the Colossians and to Philemon*. Grand Rapids: Zondervan Publishing House, reprint of 1879 edition by MacMillan.

Maclaren, Alexander. “Colossians and Philemon.” *The Expositor's Bible*. London: Hodder and Stoughton, 1888.

Nicholson, W. R. *Popular Studies in Colossians: Oneness with Christ*. Grand Rapids: Kregel Publications, 1903.

Peake, Arthur S. “Colossians,” *The Expositor's Greek New Testament*. Vol. 3. Grand Rapids: Wm. B. Eerdmans Publishing Co., 1961.

Robertson, A. T. *Paul and the Intellectuals*. Nashville: Sunday School Board of the Southern Baptist Convention, 1928.

Rutherford, John. *St. Paul's Epistles to Colossae and Laodicea*. Edinburgh: T. & T. Clark, 1908.

Sturz, Richard. *Studies in Colossians*. Chicago: Moody Press, 1955.

Thomas, W. H. Griffith. *Studies in Colossians and Philemon*. Grand Rapids: Baker Book House, 1973.

Vine, W. E. *The Epistle to the Philippians and Colossians*. London: Oliphants, 1955.

